Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 1 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

## TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tarehe 22 Juni, 2011 Bunge hili lilipitisha Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2011 (*The Finance Bill Act, 2012*). Baada ya hatua ya Uchapishaji kukamilika, Muswada huo ulipelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ajili ya kibali chake kwa mujibu wa Kanuni ya 92.

Kwa taarifa hii, nafurahi kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa, Mheshimiwa Rais ameishasaini Muswada huo tangu tarehe 28 Juni, 2011 na sasa ni Sheria ya nchi inayoitwa *The Finance Act, 2011*, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2011. Kwa hiyo, sasa inaweza kutumika kufanyakazi zilizokusidiwa. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, pamoja na Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):**

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 155

### Mradi Mpya wa Maji wa Namtumbo

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Mradi wa maji katika mji wa Namtumbo unaendelea vyema ambapo Mhandisi Mshauri wa mradi huo umeishakamilisha *report* ya usanifu na kuwasilisha Serikalini.

Je, utekelezaji wa mradi huo umefikia wapi na lini utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa utekelezaji wa mradi wa maji Mjini Namtumbo umefikia hatua ya usanifu ambapo Mhandisi Mshauri wa Kampuni ya *Don Consult in Venture with Consulting Engineers Centre*, *Saidi &* Partners ya Jordan, amewasilisha taarifa ya awali (*Draft report*) ya usanifu na Makadirio ya gharama za mradi Serikalini. Mamlaka ya Majisafi Songea ilipita taarifa hiyo na kumrejeshea Mhandisi Mshauri ili afanye marekebisho yaliyostahili kabla ya kutoa taarifa ya mwisho (*Final Report*). Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Benki ya Dunaia kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo itatoa dola za Kimarekani milioni 9.4 sawa na shilingi bilioni 14.1 za Kitanzania kwa ajili ya mradi wa maji katika Mji wa Namtumbo. Mradi huu utaanza kutekelezwa baada ya kupata kibali *(No Objection)* kutoka Benki ya Dunia. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imepanga kutumia shilingi milioni 861.5 kwa ajili ya shughuli za maji katika vijiji vya Njalamatata, Mwangaza, Mkongo-Nakawale na Ulamboni. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Wananchi wanaotumia mtandao huu wa maji wa Luwegu, Suluti, Mtwara Pachani, Namtumbo, Lwinga na Libango hawana uhakika wa maji, Matepwende na Migeregere hawana maji kabisa.

Je Serikali inaweza kuwaambia Benki ya Dunia nia ya kutusadia wanapochelewa namna hii wananchi wa maeneo hayo wanazidi kuteseka?

(ii)Kwa kuwa mtandao huu wa maji wa Namtumbo ulijengwa miaka 30 iliyopita wakati Namtumbo ikiwa ni kijiji na sasa hivi ni mji na ni Makao Makuu ya Wilaya na hivyo mahitaji yake ni makubwa.

Je, Serikali wakati tunasubiri mchakato huu wa Benki ya Dunia ukamilike inaweza kutukarabatia bomba eneo chakavu lililopo katika maeneo ya Mgambo katika Kijiji cha Libango, ili wananchi wa wilaya ya Namtumbo waweze kufaidika na maji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vita R. Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Vita R. Kawawa, kwa jitihada zake. Mimi nimekwenda mpaka pale Namtumbo nimeona kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge ameifanya pale kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji. Katika Bajeti hii ambayo tunamaliza sasa hivi walikuwa na shilingi bilioni 1.4 zilizokuwa zimepelekwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anachozungumza Mheshimiwa Mbunge ni habari ya *World Bank* na matatizo ya urasimu ambayo yako pale. Ninavyojua mimi ni kwamba katika Wizara ya Maji pameanzishwa Kurugenzi maalum kwa ajili ya kuratibu mambo yote haya yanayohusiana na hela hizi zinazotoka kwa Wahisani. Kwa hiyo, ninaamini kwamba utaratibu ambao umewekwa na Wizara ya Maji kwa ajili ya kushughulikia hizi anazozungumza Mheshimiwa Kawawa, utaratibu ule utasaidia katika kuhakikisha kwamba inakwenda haraka zaidi. Tumezungumza na Mhandisi wa Mkoa na Mhandisi wa Wilaya pia na wamesema kwamba watafuatalia kwa karibu, tunachohitaji sasa ni hiyo *no objection.*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza kwamba wakati tunapokuwa tunasubiri sasa hiyo *no objection*. Je, wananchi hawa tunawasaidiaje? Nimezungumza na UWASA, hii ni kama unavyosema DUWASA, DAWASA na nini, ya kule kwao. Wanasema katika ukarabati wameweka shilingi milioni 6 kwa ajili ya kusaidia haya maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia na katika kuelekeza katika haya maeneo mapya anayoyazungumzia wameweka milioni nyingine 6. Mimi namwomba Mheshimiwa Vita Kawawa aamini kwamba hizi pia ni jitahada za Serikali zinazoonesha jinsi ambavyo tunajali kwamba wananchi wa Namtumbo hawana maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho niliwaelekeza pale nikawaambia kwamba wahakikishe wanavuna maji kwa sababu kuna tatizo la maji pale. Ukiwa na tatizo unakaa mkao unaofanana na tatizo ulilonalo. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuhamasisha watu wake wavune maji ili yaweze kusaidia wananchi pale katika eneo hilo. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa swali la msingi mradi huu unatekelezwa na Benki ya Dunia, na kwa kuwa uzoefu unaonesha miradi mingi inayotekelezwa na Benki ya Dunia hutekelezwa kwa kusuasua ukiwemo mradi wa Maji unaotekelezwa Singida Mjini kwa kushirikiana na *BADEA.*

Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu sasa ya kukaa na wenzetu wa Benki ya Dunia, ili kuwaeleza adha inayowapata wananchi mpaka wanafikia hatua ya kukata tamaa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa Benki ya Dunia, Wizara imeliona hilo na ndiyo maana tumeanzisha Kurugenzi ambayo itashughulikia kuratibu mradi huu na kuweza kufuatilia hatua kwa hatua. Kilichokuwa kimecheleweshwa ilikuwa ni ile *procurement* wakati wa manunuzi mwanzoni tulitumia hizi taratibu za kawaida, lakini Benki ya Dunia wana taratibu zao, sasa baada ya kurudisha tena nyuma kuanza upya ndiyo maana ikaonekana halmashauri nyingi zikawa zimechelewa.

Mheshimiwa Spika, niongezee pia kwamba katika maeneo yale ambayo kwa mfano Namtumbo, yale maeneo ambayo mradi huu uko sasa hivi wa Benki ya Dunia ambao haujafikia maeneo mengi, tunataka tuboreshe katika awamu ya pili ya programu inayoanza Julai, mwaka 2012 kwamba maeneo yale ambayo hayajafikiwa yote tutayaweka kwenye programu awamu ya pili ya. *(Makofi)*

Na. 156

**Posho ya Kufundishia na Posho ya Nyumba kwa Walimu**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA (K.n.y. PUDENCIANA KIKWEMBE)** aliuliza:-

Serikali imejielekeza kuboresha zaidi huduma za kijamii kama Elimu kwa kuajiri walimu wengi zaidi na kuchukua hatua ya kuboresha maslahi na mazingira ya kufanyia kazi ya walimu:-

(a)Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kurudisha posho ya kufundishia na posho ya nyumba kwa Walimu ili kujikimu na mazingira magumu ya kazi yao?

(b)Je, ni lini mpango kabambe wa kujenga nyumba za walimu kote nchi utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU**, **TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imekuwa inaongeza ajira ya walimu ili kuweza kumudu mahitaji kutokana na ongezeko la shule nchini. Kwa mwaka 2010/2011 Serikali iliajiri Walimu wa kufundisha katika shule za msingi 12,482 na Walimu wa shule za Sekondari 9,226 wakiwemo walimu wa Shahada 4,920 na Stashahada 4306.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ukubwa wa kazi ya Mwalimu pamoja na mchango mkubwa anaoutoa kwa jamii pamoja na changamoto zinazomzunguka katika kutoa elimu nchini. Kwa kutambua ukweli huu, Serikali imeendelea kuboresha maslahi, mishahara na stahili za Walimu ili kuwapa ari ya kufanya kazi.

Katika maboresho hayo posho ya kufundishia na ya nyumba zilijumuishwa katika mishahara yao ili wanufaike, kwani inakuwa sehemu ya mafao yao wanapostaafu. Aidha, ni azma ya Serikali kuendelea kuboresha maslahi, posho na mishahara ya Walimu na Watumishi wengine kadri uwezo wa Serikali unavyoongezeka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na mazingira bora ya kazi kwa Walimu ikiwemo uwepo wa nyumba za Walimu. Kwa kutambua hilo katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi wamu ya pili (MMEM II) kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo, inakamilisha ujenzi wa nyumba za Walimu 87,744.

Wakati huohuo Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 285 za Walimu wa shule ya Msingi. Aidha, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari awamu ya pili (MMES II) mwaka 2010/2011, imetoa jumla ya shilingi bilioni 3.8 kujenga nyumba za Walimu 274 na shilingi bilioni 4.3 zimetengwa kwa mwaka 2011/2012 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu 224 zikiwa na samani zote muhimu (*basic furniture*).

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga nyumba za Walimu kadri fedha zinavyopatikana na kuhakikisha kila Mwalimu anapata nyumba ya kuishi akiwa shuleni.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i)Kwa kuwa, mishahara ya Walimu pamoja na ongezeko alilolisema Mheshimiwa Waziri bado ni midogo na Walimu wanaishi maisha dhalili.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda mwafaka kuongeza posho hizo ili Walimu waishi maisha sawa na Watumishi wengine mahali popote walipo?

(ii)Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina Walimu wachache ambao wanafanya uwiano wa Walimu kuwa 1: 58 tofauti na uwiaano wa kitaifa wa Mwalimu 1: 54.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza Walimu katika maeneo ambayo yana upungufu mkubwa kama Wilaya ya Nkasi? (*Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Desderius Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la kwanza Serikali inatambua maslahi yasiyotosha kwa Walimu wetu na tutaendelea kuweka juhudi ya kuhakikisha kwamba tunayaboresha ili Walimu hawa wawe na mazingira mazuri zaidi ya kufundishia.

Hivi sasa tuko katika mchakato wa kuyatambua maeneo magumu katika nchi yetu, maeneo yale ambayo Walimu wengi wanapata mitihani mikubwa sana kuweza ku - *settle in* ili tuweze kuwapa posho maalum ya kuweza kujikimu katika maeneo hayo. Mara tu tutakapomaliza kuanisha maeneo magumu katika nchi yetu tutahakikisha kwamba tunatenga pesa kwa ajili ya kulipa posho maalum kwa ajili ya Walimu wanao kwenda kwenye maeneo hayo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kuongeza Walimu, tunatambua upungufu huo na tunalifanya hivi sasa. Katika baadhi ya maeneo kuna Wilaya ambazo tayari zina ziada ya Walimu, ni chache lakini zipo jambo kubwa sasa ni Halmashauri kuhakikisha kwamba wanawasambaza wale Walimu vizuri katika shule zao ili mapungufu haya yanayojitokeza shule kwa shule yasiwepo kwa sababu kwa ujumla ndani ya Wilaya halmashauri ina uwezo wa kuwatawanya Walimu vizuri na kuwa na mgawanyo mzuri wa Walimu katika shule hizi. Tunafundisha Walimu wengi kila mwaka na tunatarajia katika mwaka huu tutapata wahitimu wengi ambao tutawagawanya kufuatana na upungufu katika shule kwenye wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA**: Ahsante, majibu yalikuwa marefu. Tunaendelea na swali linalofuata kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa January Y. Makamba, sijui kwa niaba yake nani atamuulizia, Mheshimiwa Mwigulu L. M. Madelu.

Na.157

## Motisha kwa Walimu walioko kwenye Mazingira Magumu

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU (K.n.y. JANUARY Y. MAKAMBA)** aliuliza:-

Upungufu mkubwa wa Walimu katika jimbo la Bumbuli unatokana na mazingira magumu?

Je, Serikali haioni kwamba haja ya kutoa motisha kwa Walimu wanaopangwa katika mazingira magumu kama Bumbuli?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa January Y. Makamba, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto yenye jimbo la uchaguzi Bumbuli ina shule za Sekondari za Serikali 79 na Walimu 485. Jimbo la uchaguzi Bumbuli lina shule za Sekondari 26 za Serikali na idadi ya Walimu katika shule hizo ni 142. Mahitaji ya Walimu wa Shule za Sekondari katika Halmashauri ya Lushoto ni 1,095 wakati mahitaji ya walimu wa shule za Sekondari katika jimbo la Bumbuli ni 390. Kwa hiyo, ni kweli kwamba Jimbo la Bumbuli lina upungufu wa Walimu wa shule za Sekondari unaotokana na changamoto nyingi ikiwemo ugumu wa maeneo hayo kufikika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kutoa motisha kwa walimu waliopangwa kwenda kufanya kazi katika maeneo hayo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwapanga walimu wapya katika Halmashauri ya Lushoto kulingana na upatikanaji wa walimu na hatimaye Halmashauri ya Lushoto kuwapanga walimu hao jimboni Bumbuli. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ya Lushoto ilipangiwa jumla ya walimu 115 wakiwemo 40 wa Shahada ya 75 wa Stashahada. Aidha, katika mwaka wa fedha 201/2012, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI itaendelea kupanga Walimu katika Halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Halmashuri ya Lushoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaboresha mazingira ya shule ili kuwavutia walimu kubaki katika shule walizopangwa hususan katika maeneo magumu kwa kujenga nyumba za walimu na kutoa posho maalum kwa walimu wa maeneo hayo. Awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES II) imeainisha kuwa Serikali itajenga nyumba 264 ambapo nyumba 2 zitajengwa kwa kila Halmashauri na nyumba moja itajengwa kwa kuwa na uwezo wa kuishi familia mbili yaani (*two in one).* Ujenzi huo utaendelea hadi kufikia nyumba 1,200 kabla ya mwaka 2015. Aidha, posho maalum itatolewa kuwawezesha walimu wanaopangwa kuanza kazi katika shule zitakazoainishwa kuwa katika maeneo magumu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kutatua changamoto zinazokabili shule zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu, Halmashauri zinashauriwa kubuni mikakati ya kuvutia walimu wanaopangwa katika shule hizo. Kwa mfano, mkoa wa Rukwa umefanikiwa katika hali hii kwa kuanzisha mfuko unaochangiwa na Halmashauri za Wilaya za mkoa huo, wafanyabiashara na wadau wengine kwa ajili ya kuwawezesha walimu wapya kuanza maisha katika mazingira stahiki kwa kuwapatia nyumba, vitanda, magodoro, chakula na fedha za kujikimu. Ili kuhakikisha kuwa walimu wanaoripoti wanabaki katika shule walizopangiwa, wanalazimika kusaini mkataba wa kisheria kabla ya kupewa motisha hiyo. Nachukua nafasi hii kuupongeza mkoa wa Rukwa na nashauri mikoa mingine nchini kuiga mfano huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya vijijini kwa kusambaza huduma muhimu kama umeme, maji, mawasiliano na barabara hatua ambayo itaondoa vikwazo vinavyofanya maeneo mbalimbali nchini kuwa magumu kufikika.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule zilizopo Kidaru, Tulya, Mgongo, Mtekente, Urugu na Kaselya zina mazingira magumu sana ambayo hata mwalimu akipewa posho inawezekana ikawa vigumu kuyazoea. Je, Serikali haioni vyema sasa kuwachukua vijana waliozaliwa maeneo hayo ambayo wana sifa za kwenda kusomea ualimu na kufundisha lakini hawajapata nafasi iwafundishe na iwarudishe kuwafundisha wadogo zao katika maeneo hayo ambayo wameyazoea?

Swali la pili, kwa kuwa walimu wanapopangiwa mazingira kama haya niliyoyataja na maeneo mengine yaliyoko Iramba hawaripoti. Je, Serikali itachukua hatua sasa kuwapeleka wengine kwa sababu wengi waliopangiwa hawakuripoti?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwigulu amejaribu kuorodhesha vijiji katika jimbo lake ambavyo vina mazingira magumu. Akasema kwamba Serikali ingependelea kuwachukua vijana hao wanaokuwa kwenye jimbo lake kuwapeleka Vyuo vya Walimu na wakishahitimu baadaye warudi kufundisha katika shule hizo. Serikali haina tatizo kwa hili na huwa tunafanya pale Mbunge anapoweza kuomba kuhudumiwa katika hali hiyo.

Kwa hiyo namwomba tu Mheshimiwa Mbunge akihitaji hivyo aje atuone Ofisi tunawezatukamsaidia kama kweli walimu wanaopangiwa kwenye jimbo hilo huwa hawaripoti, lakini kuna walimu ambao wapo katika jimbo lake wanaomba wakafundishe katika mazingira huko kwao basi tuko tayari kumsaidia kwa hilo.

**MHE. SUSAN L. B. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa swali hilo linaambatana na matatizo ya walimu naomba kuuliza. Je, Serikali ina mpango gani wa walimu ambao waliajiriwa tangu mwezi Januari na kuna taarifa zao katika mkoa wa Kilimanjaro, Tanga na Wilaya ya Singida hawajapewa stahili zao mpaka sasa na wanahangaika kila kukicha hawafundishi wanafuatilia stahili zao kwa Wakurugenzi wao?

**SPIKA:** Pamoja na kwamba ni swali jipya lakini Waziri naomba ujibu pia kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, wakati walimu hawa tunawapeleka kwenye shule tulitenga pesa pia za kulipa stahili zao pamoja na nauli na posho za kujikimu wao pamoja na wale wanaomtegemea. Lakini tumepata taarifa hizo.

Naomba katika maeneo yale ambayo hili halijakamilishwa kama inavyohitajika basi wahusika waweze kuwasilisha kama haiwezekani katika Halmashauri hata moja kwa moja kwa Waziri wa Elimu, mimi na Waziri wa Nchi TAMISEMI tutashirikiana kuhakikisha kwamba hili tunaliondosha. *(Makofi)*

Na. 158

**Maslahi Duni Kwa Walimu Nchini**

**MHE. RASHID ALI OMAR** aliuliza:-

Serikali imejitahidi kuboresha sekta ya elimu nchini kwa kuongeza shule za Sekondari zikiwemo za Kata lakini kuna kasoro nyingi katika sekta hii ikiwemo maslahi duni kwa walimu na watendaji wengine katika sekta hii:-

(a) Je, Serikali inaziangaliaje kasoro hizi?

(b) Kwa kuwa, walimu ndio mhimili mkuu katika Wizara hii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaboreshea mazingira ya kazi na maslahi yao kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mbunge wa Kojani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kasoro zilizopo katika Sekta ya Elimu zikiwemo za mazingira duni ya kufundishia na kujifunzia, upungufu wa nyumba za walimu, maji, umeme, mawasiliano pamoja na maslahi duni kwa walimu na watumishi wengine katika sekta hii. Kasoro hizi ni changamoto ambazo Serikali inazifanyia kazi ili kuinua ubora wa elimu inayotolewa nchini katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira ya kazi ya walimu na maslahi yao ikiwa ni pamoja na:-

(i)Kuimaisha miundombinu ya shule ambayo haikukamilika wakati wa MMES I ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu, madarasa, maabara, vyoo, maji, umeme na barabara.

(ii)Kuhuisha Muundo wa Utumishi wa kada ya walimu kwa lengo la kuboresha maslahi yao. Mapendekezo ya kuboresha muundo huo yamewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi;

(iii)Kulipa mishahara ya walimu na stahili nyingine za walimu kwa wakati; na

(iv)Kuwajengea uwezo walimu kwa kuwapatia mafunzo kazini ili waweze kumudu kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mikakati hii, ni matarajio ya Serikali kuwa utekelezaji wa mikakati hiyo utapunguza kama si kumaliza kabisa kasoro zinazoikabili Sekta ya Elimu.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua kwamba elimu ndio Dira ya Maendeleo ya Taifa lolote duniani. Je, Serikali kupitia Wizara hii husika inaweza kuwahakikishia na kuwapa ahadi wadau hawa kutokana na kuchoshwa na masuala haya ya siku nyingi?

**SPIKA:**Vipi mbona mnaongea kwani kimetokea nini? (*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri anayeshughulikia TAMISEMI ametoka hapa ameelezea mikakati mingi sana ya maboresho ya walimu na mimi nimefika hapa yaliyoandikwa nimesoma kwa ufasaha na nikajibu na majibu ya nyongeza na Mheshimiwa Waziri wangu amejibu kwa ufasaha namna tutakavyoboresha mambo yote ya maslahi duni ya walimu pamoja na posho zao.

Lakini Mheshimiwa Mbunge alikuwa anataka apate uhakika kwamba tunatekeleza. Namjibu kwamba ndio tutatekeleza na Serikali iko makini kweli kuyafuatilia matatizo ya walimu nchini.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua hali duni inayowapata walimu kwenye maeneo wanayofanyia kazi. Na kwa kuwa wametaja vipaumbele mbalimbali watakavyovifanya ili kuboresha hali hizo. Na kwa kuwa walimu hao hupata adha ya usafiri kutoka maeneo wanayofundishia mpaka kwenda kufuata mishahara yao hutumia zaidi ya robo tatu ya mshahara wao. Je, ni lini Serikali itatoa mkopo wa pikipiki kwa walimu hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, hatujawa na mpango mahsusi wa Kiserikali wa kuwakopesha walimu pikipiki. Lakini niseme tu kwamba mchango wa Mheshimiwa Vulu tumeusikia, tutaufanyia kazi aidha kwa kupitia Serikali Kuu moja kwa moja au kupitia Vyama vyao vya Walimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 159

**Uhamishaji wa Kambi za Silaha Kutoka Kwenye Sehemu za Makazi ya Watu**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA (K.n.y. MHE. ABBAS Z. MTEMVU)** aliuliza:-

Katika Kambi la Gongo la Mboto, mabomu yalilipuka tarehe 16 Februari, 2011 kama ilivyotokea katika Kambi ya Mbagala, hali iliyosababisha uharibifu wa mali za Serikali na wananchi pamoja na vifo:-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kuhamisha Kambi zote zenye mabomu na silaha kali karibu na makazi ya watu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi zote za JWTZ ziliwekwa pale zilipo kwa kuzingatia mahitajio ya Ulinzi wa Taifa kwa ujumla, kwa maana ya mahitajio ya Stratejia na Mbinu za Ulinzi wa Taifa. Aidha, ikumbukwe kwamba wakati Kambi nyingi za JWTZ zilipokuwa zinajengwa, zikiwemo Kambi za Gongo la Mboto na Mbagala, makazi ya watu yalikuwa mbali kabisa. Mipango inafanywa ili kuhakikisha kuwa Kambi za Mbagala na Gongo la Mboto zinakuwa za maghala yasiyo ya milipuko.

Hata hivyo, mipango ya muda mfupi itajumuisha kujenga matuta makubwa kati ya maghala na mipango ya muda mrefu itajumuisha kujenga upya maghala yetu ili milipuko itunzwe kwenye maghala yaliyoko chini ya ardhi. Mipango hiyo inahitaji fedha nyingi na itaweza kukamilika kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

**MHE EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa waathirika wa Gongo la Mboto bado wanaishi katika mahema waliopewa na Serikali na kwa kuwa wamepata adha kubwa sana hasa wakati wa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza sasa kujenga nyumba ambazo waliwaahidi waathirika hawa.

Kwa kuwa wapo watoto waliopoteza wazazi wao, lakini pia wapo wazazi waliopoteza viungo na kwa sababu hiyo wameshindwa kuendelea na shughuli zao za kiuchumi. Je, Serikali inasemaje kuhusu kulea familia hizi ili waweze kuendelea kupata masomo na maisha mengine ya kawaida?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Spika, baada ya tukio lile la milipuko ya Mbagala na Gongo la Mboto, Kitengo cha Maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu walifanya uthamini wa mali zote ambazo zilipotea pamoja na kuangalia jinsi wahusika mbalimbali walivyoathirika. Kama mnavyotambua wale ambao walifiwa au walipoteza maisha kuna kifuta machozi ambacho walipewa pamoja na kusaidiwa katika gharama za mazishi.

Lakini wale ambao nyumba zao zilibomoka kwa viwango mbalimbali kuna ambao walipewa tu fedha za kukarabati na sasa hivi Shirika la Suma la Jeshi la Kujenga Taifa limepewa kazi ya kujenga upya zile nyumba ambazo zimebomoka kabisa. Kazi hiyo imeanza, viwanja vimeshapatikana na sasa hivi ujenzi unakaribia kuanza kwa sababu matofali yameendelea kufyatuliwa ili ujenzi uweze kuanza wa nyumba hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kusaidiwa kwa waathirika. Kama nilivyosema ni kwamba inategemea ni kiwango gani waathirika walipata matatizo. Kama nilivyosema wapo ambao walilipwa kifuta machozi na wapo ambao wamepewa fedha kwa ajili ya kuwasaidia baada ya kupata ulemavu kwa viwango mbalimbali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ushahidi wa kihistoria unaonyesha kwamba Kanisa Katoliki Parokia ya Pugu ilianza kujenga Pugu mwaka 1889 kwa Missionari wa kwanza kuingia pale na Wajerumani walijenga Stesheni ya Reli ya Kati ya Pugu mwaka 1905 na baadaye Kanisa likajenga Shule ya Sekondari ya Pugu mwaka 1948.

Je, Serikali iko tayari kurekebisha historia yake kwamba sio wananchi waliovamia pale Jeshini ila ni Jeshi liliwafuata wananchi? Kwa kuwa Jeshi liliingia pale Gongo la Mboto mwaka 1975?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ambacho nimesema ni kwamba maeneo ya Jeshi au Kambi za Jeshi kisheria zinatakiwa ziwe umbali wa angalau kilomita moja kutoka makazi ya watu.

Kwa hivyo hatubishi kwamba ambao wamejenga Pugu wako umbali huo, ni kweli. Tatizo letu ni wale ambao wako karibu wanaingia ndani ya Kambi wamekaribia mno. Sasa lazima tukubali kwamba lipo tatizo la mipango miji.

Wananchi hawakupaswa kuwa karibu kiasi kile lakini kwa sababu imetokea kwamba wapo basi Serikali inachukua jukumu la kuhakikisha kwamba katika mipango yetu ya muda mrefu kama nitakavyoeleza wakati wa Bajeti yangu ni kwamba

tutahakikisha kwamba tathmini inafanyika ili angalau wale ambao wako karibu mno, wale watu ambao wako ndani ya kilomita moja kutoka kwenye makambi haya yanayohifadhi milipuko basi wanaweza kuhamishwa kwa kulipwa fidia ili matokeo kama haya yanapotokea yasiweze kuathiri wananchi waliokuwa karibu.

Kwa maana hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Pugu na Gongo la Mboto sio sehemu ambayo iko ndani ya kilomita 1, kwa hiyo hatuna ugomvi katika hilo. *(Makofi)*

Na. 160

**Kukomesha Vitendo Vya Unyanyasaji Watoto**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Vitendo vya unyanyasaji wa watoto vimekithiri hususan ukeketaji katika Mikoa ya Mara, Singida, Arusha na kwingineko ambapo vitendo hivyo hufanyika bila ridhaa ya wahusika na kupelekea watoto hao kuathirika kisaikolojia:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukomesha vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu Na. 169 (A) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu *(Penal Code)* Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania kama kilivyorekebishwa mwaka 2002, kinatamka wazi kwamba mtu yoyote ambaye mtoto yuko chini ya usimamizi wake akamtendea vibaya au kumkeketa au kumwacha au mtu huyo kusababisha mtoto huyo kukeketwa au yeye mwenyewe kumkeketa, atakuwa ametenda kosa la ukatili dhidi ya watoto na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 5 na atawajibika kumlipa fidia mtoto aliyetendewa ukatili huo. Aidha, Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 inatamka wazi kwa kufanya kitendo cha ukeketaji adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi 5,000,000 au kifungo kisichozidi miezi 6 au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba sheria peke yake si suluhisho la kutokomeza ukeketaji hapa nchini kwani suala hili limejikita zaidi ndani ya mila na tamaduni za baadhi ya jamii. Hivyo Serikali itaendelea kushirikiana na wadau

mbalimbali zikiwemo Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini na Vyombo vya Habari ili kuunganisha nguvu za mapambano dhidi ya ukeketaji.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali haya yafuatayo:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amikiri kwamba wanashikiana ama wataendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za dini, *NGO's* na vyombo vya habari katika kutokomeza janga hili dhidi ya watoto na hasa vyombo vya habari vinafanya kazi nzuri sana katika kuibua matatizo mbalimbali yakiwemo matatizo haya ili kuelemisha jamii.

Mimi kwa macho yangu nimeona kwenye Taarifa ya Habari moja kule Mara inafanywa sherehe kubwa sana kwa kuwakeketa watoto ni sherehe kubwa sana na watu mbalimbali wamealikwa.

Je, Serikali hivi kule hakuna ulinzi au kule hakuna Ma-*DC* au RC, kweli kule hakuna viongozi wa kuwakamata hawa watu wanaokeketa watoto na kuathiri maisha yao?

Je, ni kwa kiwango gani Sheria hii inafanyiwa kazi? Kwa sababu kila kukicha matatizo haya yanaongezeka badala ya kupungua?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kuna changamoto kubwa ya kuwakamata wahusika wa vitendo hivi vya ukeketaji kwa sababu kunakuwa na ushirikiano mkubwa kati ya jamii husika.

Lakini nataka kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali kadri inavyowezekana inawakamata na kuwatia wale wote anaoendeleza vitendo hivi, tuna ushahidi wa kesi ambazo zimeshafikishwa Mahakamani. Kwa mfano Disemba 2010, Mahakama ya Wilaya ya Tarime ilimhukumu ngariba kifungo cha miaka kumi jela.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuiomba jamii zinazoendeleza vitendo hivi wakae chini na wawatathimini kuna uhalali wowote wa kuendelea kuwakeketa watoto wa kike. Kwa sababu hakiwaongezei kitu chochote na sana sana kina wapunguzia baadhi ya vitu na kuwaletea matatizo ya kisaikolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni mapema mno kusema kwamba tunaweza kutoa tathmini ni kwa kiasi gani Sheria ya Mtoto imeanza kufanya kazi kama unavyoelewa Sheria hii ilipitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 4/9/2009 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais 20/9/2009.

Lakini kama nilivyosema, tumeshapata matokeo mazuri na tutaendelea kuhamasisha jamii na vyombo vya habari, mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha tunatokomeza kwa sababu inachafua taswira nzuri ya Tanzania linapokuja suala la haki za watoto na wanawake.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize Naibu Waziri wa Jinsia swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna watu wazima wenye akili zao timamu wanawafanyia watoto wadogo vitendo vya ukatili na visivyokuwa na maana na huwa wanafikishwa katika vyombo vya Sheria na watu hawa hatujui kesi hizi huwa zinamalizika vipi na watoto hao wanakuwa tayari wameharibikiwa kimaisha. Je, Naibu Waziri atanihakikishiaje kuwa watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili nao wanatendewa haki?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na bahati mbaya taarifa za mambo ya ndani ukitizama inaonekana hali bado inaongezeka badala ya kupungua. Nitashindwa kumpa takwimu sasa hivi Mheshimiwa Mbunge lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi sisi kama Wizara tutaendelea kujenga mwamko, hamasa na ari kwa jamii kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukapunguza tatizo la ukatili dhidi ya watoto na tuna *champion* wa suala hili ambaye ni Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, alishazindua kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, mwaka 2008. Pia tumezindua filamu kwa ajili ya kuonyesha matatizo ya kuonyesha matatizo mbalimbali ya ukatili dhidi ya watoto, tutaendelea kuionyesha katika vituo vya televisheni, redio na vijarida mbalimbali.

Na. 161

**Serikali Kufanya Utafiti wa Madini ya Shaba –Tunduru Kusini**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Kuna dalili zote za kupatikana madini ya shaba eneo la Kata ya Mbesa Jimbo la Tunduru Kusini na itakuwa tija zaidi kuuza madini hayo ya shaba yakiwa yamesafirishwa ambapo umeme mkubwa utahitajika:-

(a) Je, ni lini Serikali kupitia Shirika la *STAMICO* litafanya utafiti haraka kujua ujazo wa shaba katika eneo hilo?

(b) Je, Serikali imejipangaje kupeleka umeme mkubwa kijiji cha Mbesa ili utumike kusafisha shaba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti wa awali wa kijiolojia katika eneo la Kata ya Mbesa Jimbo la Tunduru Kusini ulifanywa na Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* mwaka 1988 na kuonyesha kuwepo kwa madini aina ya shaba. Ili kujua kiasi na ubora wa mashapo ya shaba katika eneo hilo, utafutaji wa kina unahitajika kufanyika.

Lengo kubwa la utafutaji wa kina *(detailed geological exploration)* ni kubaini kama madini husika yanaweza kuchimbwa kwa faida kabla ya kufikia uamuzi wa kuanza kuyachimba. Hatua hii ya utafutaji madini inahitaji utaalam, vifaa vya kisasa na fedha nyingi. Aidha Serikali inaendelea kuimarisha STAMICO ili iweze kuwa na uwezo wa kufanya shughuli hizo za utafutaji na uchimbaji madini kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Kwa sasa Serikali kupitia *STAMICO* haina mpango wa kufanya utafiti wa haraka ili kujua wingi wa shaba katika eneo hilo kwa kuwa *STAMICO* haina leseni ya utafutaji madini katika eneo hilo. Eneo hilo lina leseni za utafutaji madini wa awali *PLR 6090/2009* inayomilikiwa na kampuni ya *Zari Exploration Limited na PLR 6056/2009* ya kampuni ya *JAM Minerals and Mining Limited*. Aidha katika eneo hilo kuna leseni nne za wachimbaji wadogo (*Primary Mining Licences*) kwa ajili ya uchimbaji wa shaba.

(b) Mheshimiwa Spika, mahitaji ya chini ya umeme ya mgodi wa wastani wa shaba ni MW 2.5 wakati umeme unaozalishwa Tunduru Mjini kwa sasa ni MW 1 hivyo kuanzisha mgodi wa shaba kijiji cha Mbesa Tunduru lazima kuambatane na upatikanaji wa umeme wa kutosha katika eneo hilo.

Serikali inaendelea kuhakikisha maeneo yote ya vijiji yanapatiwa umeme kupitia *REA* na vyanzo vingine na kwa upande wa Tunduru, maombi yametufikia ya kuongeza upatikanaji wa umeme kutokea Mtwara baada ya mradi uliokusudiwa na Masasi – Mangaka (Nanyumbu) kukamilika. *(Makofi)*

Mwekezaji atakayejitokeza kuchimba madini ya shaba huko Mbesa Tunduru atalazimika kufua umeme wake mwenyewe kwa kutumia *Generator* za mafuta kama ilivyo katika baadhi ya migodi mingine ya madini hapa nchini.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwe mkweli, jibu la swali hili namba (a) kwa kweli halileti matumaini si kwa wananchi wa Tunduru peke yake ila hata kwa wananchi wa nchi hii ya Tanzania.

Katika Mkutuno wa Tatu Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atawatuma wataalam Tunduru kwenda kufanya utafuti. Naomba kujua kutoka kwake. Je, wataalam hao wamefikia hadi sasa?

Swali la pili, nchi hii kabla hujafanya shughuli zozote za kibiashara hasa uchimbaji wa madini ni lazia ufanyike tathmini ya kimazingira, Je, hao wachimbaji walioko Tunduru sasa hivi tathimni yoyote ya kimazingira imefanyika mpaka wakaruhusiwa kuanza kuchimba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia wa Tanzania ndiyo wenye mamlaka ya kufanya tafiti kwa kila eneo na daadhi ya maeneo ya Tanzania yameshafanyiwa utafiti juu ya ule ulikwishafanywa miaka ya 50 na kazi hiyo inaendelea sasa hvi katika baadhi ya maeneo. Sasa hatuwezi kufanya utafiti kwa Tanzania nzima KM 940,000 zote kwa wakati mmoja. Sasa hivi tumefanya na tuna maeneo ya QDS kama 30 ambayo yanafanyika hivi sasa, kulingana na upatikanaji wa fedha tutakwenda kwenye maeneo mengine.

Sasa nimhakikishe tu kwamba Wataalam watakwenda tu Tunduru. Tunduru kuna upatikanaji wa madini ya vito yamejitokeza kwa wingi. Lakini kwa sasa pana watu wenye leseni zao.

Sasa wale wenye leseni wanapochukua kwetu leseni wakienda pale ndiyo maana inaitwa *PL* kwa maana ya kwamba wanaanza katika hatua za awali za kufanya utafiti na watakapobaini kwamba wanahitaji kutengeneza mgodi watakuja kuomba leseni nyingine.

Wakati huo watakuja na maelezo pamoja na *Environmental and Social Impact Assessment* ambayo itapitishwa na watu wa *NEMC* na kadhalika na kadhali. Sisi tunaipokea tunaipeleka kwa wenzetu wenye ujuzi wa mazingira.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba utafika Tunduru kwa sababu ni eneo ambalo limeshajulikana lina madini lakini yako maeneo ya Tanzania mengine ambayo yanafanyiwa *QDS assessment* sasa hivi.

La pili ni kwamba kama mtu amepata leseni hawezi kuanza kuchimba kwa kiwango cha mgodi bila kufanya *Environmental and Social Impact Assessment.*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza nafasi ya nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Ruvuma ni ukweli usiopingika kwamba katika huo utafiti wa miaka 50 unaosemwa na Mheshimiwa Naibu Waziri imegundulika Mkoa ule una madini ya aina mbalimbali na yako mengi kwa kiasi cha kutosha sana; na kwa kuwa wenzetu wa *NDC* wana mkakati maalum wa mpango wa kuendeleza Ukanda wa Mtwara katika uwekezaji wa aina mbalimbali.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kushirikiana na wachimbaji wadogo wadogo kuwamilikisha leseni hizo kabla ya wachimbaji wakubwa hawajaja kuchukua leseni na kufanya uharibifu mkubwa wa kuondoa madini kwa kuwafaidisha Wawekezaji wakubwa na si wananchi wenyewe wa Tanzania na hasa wale wa Mkoa wa Ruvuma.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimesema hivi, utafiti ulianza zaidi ya miaka 50 uliopita, baada ya hapo Wakala wa Jiolojia wameboresha utafiti ule na wameanza kazi hiyo kama miaka miwili iliyopita kupitia baadhi ya maeneo lakini lengo ni kupitia Tanzania nzima. Sio kwamba utafiti

umekuwa unafanywa kwa miaka 50. Hili la wachimbaji wadogo ndiyo sera ambayo tumekuja nayo tangu mwaka 2009 na mwaka jana imehimizwa ndani ya Sheria ya Madini.

Lakini lazima tukubaliane, kuna maeneo ambayo yana uwezo na maslahi ya kuchimbwa na wachimbaji wadogo na kuna maeneo ambayo kwa namna yake. Kwa fano yale mashapo yapo mita 500 chini wachimbaji wadogo watachimba.

Kwa hiyo, tunafanya *balance,* kitu cha kwanza tunachoangalia ni maslahi ya taifa na maslahi ya wananchi wake. Kama maeneo yanakidhi kuchimbwa na wachimbaji wadogo wao watapata *priority* na kama maeneo ambayo hawawezi kuyachimba kwa maslahi na wachimbaji wakubwa wamejitokeza kwa uwekezaji wenye maslahi ya taifa watapewa kazi hiyo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, nifafanue kwamba tusiwatizame wawekezaji wakubwa kama wezi wa rasilimali zetu. Wote tunafahamu ni sera ya taifa kushirikisha sekta binafsi katika kusaidiana na juhudi za Serikali kuendeleza rasilimali tulizonazo kwa manufaa yetu lakini pia na washirika ambao tunashirikiana kuvuna hizi rasilimali. Yanayofanyika yote ni kwa mujibu wa sera na sheria zetu lakini pia tutambue ya kwamba sisi kama taifa hatuna rasilimali za kutosha kuweza kuvuna rasilimali zetu kwa manufaa ya leo. Mataifa makubwa yaliyofanikiwa, nchi zote ambazo zina maendeleo makubwa kiuchumi, zimeshirikiana na sekta binafsi kuvuna rasilimali zao.

Lakini mwisho ni kwamba tunapoongelea wawekezaji wakubwa hatumaanishi wageni peke yao. Mazingira ya Sheria zetu na Sera zetu zinaelekeza ushiriki wa sekta binafsi ikiwemo Watanzania wenyewe. Mazingira tunayoyajenga ni kwa ajili ya Watanzania na ukiangalia takwimu za leseni ambazo zimetolewa na Wizara ya Nishati na Madini nyingi ziko mikononi mwa Watanzania. Imani yetu ni kwamba pamoja na kwamba sekta ya madini inaonekana imetawaliwa na wawekezaji wachache wageni huko tuendako watawala wa sekta hii watakuwa ni Watanzania wenyewe. Ndiyo mazingira ambayo tunawajengea. *(Makofi)*

Na. 162

**Gawio la Misaada ya Kibajeti kwa Tanzania Zanzibar**

**MHE. WARIDE BAKARI JABU** aliuliza:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata misaada ya kibajeti *(General Budget Support)* kutoka Jumuiya wahiriki wa maendeleo.

(a) Je, ni kiwango au asilimia gani ya misaada hiyo hupelekwa kusaidia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar?

(b) Je, tangu misaada hiyo ianze kutolewa ni kiasi gani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata na kiasi gani kimepelekwa Tanzania Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Waride Bakari Jabu, wa Jimbo la Kiembesamaki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kulingana na makubaliano yaliyopo kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, misaada na mikopo ya kibajeti inayopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kusaidia utekelezaji wa Bajeti ni asilimia 4.5.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipokea misaada ya mikopo ya kibajeti tangu mwaka 2001/2002 kutoka kwa Washiriki wa Maendeleo. Tangu misaada ya mikopo ya kibajeti ianze kutolewa mwaka 2001/2002 hadi 2009/2010, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea jumla ya shilingi trilioni 5.5. Kati ya hizo, jumla ya shilingi bilioni 196.127 zilipelekwa Zanzibar kwa ajili ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2001/2002 hadi 2008/2009 asilimia 4.5 ya fedha zilizopelekwa SMZ zilihusisha misaada pekee yaani *grants* ambapo shilingi bilioni 144.9 kati ya shilingi trilioni 2.74 ambazo ni misaada zilipelekwa Zanzibar katika kipindi hicho.

Kuanzia mwaka 2009/2010 fedha zinapelekwa SMZ asilimia 4.5 zinahusisha misaada na mikopo yaani *grants and loans* ambapo shilingi bilioni 51.2 kati ya shilingi trilioni 1.14 zilipelekwa huko.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, asante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kiwango cha asilimia 4.5 kipo sasa kwa muda mrefu na kwa kuwa kimetokea kwa muda mrefu na kwa kuwa kumetokea mabadiliko mengi ya kijamii na kiuchumi.

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haioni sasa ni muda wa kuongeza kiwango hiki?

Lakini pili je, Washirika wa Maendeleo wameridhia kiwango hiki cha asilimia 4.5?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA**: Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kwamba asilimia 4.5 kwamba ni suala la zamani nakubaliana naye moja kwa moja kwamba maamuzi haya yalifanywa mwaka 1994 na kweli kumetokea mabadiliko ya Idadi ya watu na masuala mengine ya kijamii na

kwa kulitambua hilo Serikali mbili zilianza mchakato wa kufanyia kazi na kufanya marejeo ya makubaliano hayo ili tuone kwamba hali hii inaweza kuendelea au kufanyiwa marekebisho yanayofaa.

Mheshimiwa Spika Pili, mariadhiano yaliyofanywa ya asilimia 4.5 ni maridhiano kati ya Serikali mbili, na kwa mujibu uasili wa GBS ni kwamba lengo ni kupata *policy space* kwa ajili ya nchi ambayo inasaidiwa.

Kwa hiyo, maridhiano haya siyo lazima yakubaliwe au yaridhiwe na wahisani wa nchi za nje ambao wanatupatia misaada.

**SPIKA**: Kwa ajili ya muda naomba tuendelee na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Mnyika atauliza swali hilo.

Na. 163

**Ripoti ya Kamati Iliyochunguza Maeneo ya Wazi**

**MHE. JOHN J. MNYIKA** aliuliza:-

Serikali ilieleza kuwa taarifa ya Kamati iliyoundwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2010 ni siri baada ya kudokeza baadhi ya mambo machache yaliyokamilishwa ndani ya taarifa hiyo:-

(a) Je, Serikali itatoa taarifa hiyo kwa umma lini?

(b) Je, kwa nini Serikali isitoe nakala za taarifa hiyo kwa wawakilishi wa wananchi Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa ili kurahisisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo?

(c) Serikali inachukua hatua gani mpaka sasa ikiwa pamoja na kurejesha viwanja vya umma vilivyochukuliwa na kubadilishwa matumizi yake?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja na kufuatana na uwiano wa vipengele vya swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2010 aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge, aliunda Kamati Maalum ili kuchunguza hali ya uvamizi wa maeneo ya wazi katika Jiji la Dar es Salaam. Kamati hiyo ilikamilisha kazi yake mwezi Julai, 2010 na kuwasilisha mapendekezo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yameainisha masuala ya kisheria na kiutawala yaliyokiukwa. Serikali imekwishaanza kuyafanyia kazi na kuwajulisha

watendaji juu ya maudhui ya taarifa hiyo na mapendekezo yake. Aidha, utekelezaji wa mapendekezo yaliyoainishwa kwenye taarifa hiyo unaendelea katika ngazi mbalimbali. Mathelani, Halmashauri za Manispaa ndani ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na Wizara yangu zimeanza kuyalinda maeneo hayo kwa kuyatangaza kwenye gazeti la Serikali. Hadi sasa maeneo takriban themanini (80) yameshawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuyatangaza katika Gazeti la Serikali. Aidha hatua nyingine madhubuti za kuyalinda zinaendelea kuchukuliwa, kwa mfano, maeneo manne (4) katika Manispaa ya Temeke. *(Makofi)*

Mwisho, yameshazungushiwa uzio wa waya kwa ajili ya kuyalinda dhidi ya uvamizi na matumizi mengine yasiyofaa au yanayoleta kero kwa majirani katika maeneo hayo kwa mfano shughuli zenye kelele.

Mheshimiwa Spika, Vile vile Serikali, kwa kuzingatia Sheria za Ardhi na nyingine husika, inaendelea kusitisha na kuondoa maendelezo yaliyofanyika kwenye baadhi ya viwanja hivyo, mfano, Serikali ilivunja ukuta katika kiwanja Na. 1006 Upanga kilichokuwa karibu na Hoteli ya *Palm Beach* na Kiwanja Na. 59 *Ocean Road* kilichokuwa karibu na Hospitali ya Aghakhan na kwenye ufukwe ulio kati ya viwanja Na. 934 na 615-616 *Mbezi beach.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda miji kabla haijaharibika, Serikali, katika jiji la Dar es Salaam tayari imeajiri Askari Ardhi (*Land Rangers*) wenye jukumu la kufanya ukaguzi kwa lengo la kuzuia maendelezo kinyume na utaratibu wa Sheria ya Mipango miji namba 8 ya mwaka 2007. Vitendo vya kuvamia maeneo au kukiuka taratibu sasa vitaweza kudhibitiwa mara moja. Naomba wananchi watoe ushirikiano kwa askari hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikishirikiana na vyombo husika vya dola tayari imekwisha chukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wake katika ngazi mbalimbali wanaokiuka maadili ya utumishi na kujihusisha na vitendo vya kuvamia maeneo ya umma na kuvunja Sheria ya Mipango Miji. Moja ya hatua hizo ni wahusika kufikishwa Mahakamani hivi majuzi tarehe 28 Juni, 2011.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali haitavumilia wala kumwonea haya mtu yeyote atakayebainika amejimilikisha maeneo hayo kinyume cha taratibu kwa kushirikiana na maofisa wasio waaminifu. Hatua za ujumla zinazochukuliwa nchini kote ni kama ifuatavyo:-

(i) Maeneo yaliyoporwa na hayajaendelezwa yatarejeshwa mara moja kuendelea kuwa maeneo ya wazi;

(ii) Maeneo yaliyomilikishwa na kutolewa Hati, mchakato wa kuzifuta hati hizo unaendelea ili yarejeshwe kuwa ya wazi kwa manufaa ya umma; na

(iii) Maeneo yaliyomegwa na kujengwa kinyume na taratibu, Halmashauri za Miji na Wilaya zimeagizwa zifuatilie na kuyarudisha maeneo hayo kuwa ya wazi kwa kufuata Sheria.

Kwa mfano tayari Wizara yangu imeamuru eneo la Shule ya Sekondari ya Welwei Karatu, lililokuwa limemegwa kurudishwa kuwa eneo la shule chini ya Sheria Na. 8 ya Mipango Mji ya 2007, kifungu 37, na Sheria Namba 4 ya Ardhi ya 1999 kifungu cha 18(1), zinazompa Waziri wa Ardhi mamlaka ya kutengua mabadiliko ya matumizi ya ardhi kinyume cha Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo ya Kamati ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na mara yakikamilika taarifa zaidi itatolewa kwa viongozi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri pamoja na hatua ambzo zimeanza kuchukuliwa, lakini izingatiwe kwamba ripoti hii imekamilika mwaka mmoja uliopita na miezi sita toka Wizara ianze kufanya kazi. Nina maswali ya nyongeza yafuatayo.

(a)Kwa kuwa sehemu ya (a) na (b) ya swali langu haijajibiwa kiukamilifu kwa kuwa taarifa hii ambayo mpaka sasa ni ya siri itolewe kwa Wabunge, Madiwani, viongozi wa mitaa na itolewe kwa umma. Je, Waziri yupo tayari kuitoa taarifa hii kwa wahusika ili tuunganishe nguvu kwa pamoja kuhakikisha kwamba suala hili linashughulikiwa ipasavyo, kwa sababu mimi binafsi ninayo ripoti hiyo kwa ukamilifu wake nimeipata kwa njia zangu. Kwenye Kata ya Makurumla Magomeni peke yake kuna maelezo ya kugushi nyaraka na kadhalika; nataka kujua hatua zitakazochukuliwa kwa hawa waliotajwa moja kwa moja.

(b)Sehemu ya pili ya swali naomba Waziri anijibu kama yupo tayari sasa kwa kuwa askari wa *Range Rovers* wapo na mwezi Disemba tulipokuwa kwenye ziara aliahidi kwamba atatembelea vile vile viwanja vya Jimbo la Ubungo.

Je, yupo tayari sasa kutumia rungu lake kwenda hususani kwenye Kata ya Sinza ambako kuna viwanja takribani ishirini vimeuzwa na kuvamiwa kinyemela?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**Mheshimiwa Spika, kama nilisikika kwa makini nilijibu kwamba mchakato wa kutoa taarifa inavyofaa na kuzingatia hadidu rejea za Kamati hiyo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutembelea Jiji la Dar es Salaam, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tulitembea wote katika safari yetu ya kwanza tukitekeleza matokeo ya Kamati ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, na sasa hivi kwa sababu tuna *Land Rangers* sasa nina *mechanism* ya *intervention*, kwa sababu kabla ya kuwa na *Land Rangers* ilikuwa ni juhudi bila maarifa alivyosema Mwalimu Nyerere, kwa sababu huwezi kulinda Miji kama huna Mechanism ya *Intervention*, lakini kwa sasa hivi ukitupigia simu tutakupa na *hotline*. Kama mtu

anavamia eneo sasa tuna *mechanism* ya *intervention* kabla ya hapo kwa kweli ilikuwa haiwezekani. Nashukuru tutakuwa wote Dar es Salaam. *(Makofi)*

Na. 164

**Kuimarisha Ulinzi na Usalama ziwa Tanganyika**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Ukosefu wa ulinzina usalama katika mipaka ya Ziwa Tanganyika unasababisha wizi uliokithiri wa mazao ya uvuvi na kupoteza maisha kwa wavuvi wa Kitanzania. Pia hali hii imetoa mwanya kwa wafanyabiashara kutoka *DRC,* Zambia na kadhalika kufanya biashara haramu ya mazao huko huko majini.

(a)Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuimarisha usalama katika ziwa hilo?

(b)Je, Serikali inazieleza nini Halmashauri za Wilaya ambazo zimepoteza mapato yake kutokana na uvuvi kwa sababu ya biashara zinazofanyika majini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa muda mrefu hali ya usalama kwenye ziwa Tanganyika imekuwa sio ya kuridhisha. Hali hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kuzorota kwa usalama katika nchi jirani hasa Burundi na Kongo. Aidha, ni kweli kwamba zipo taarifa za watu kutoka nchi za nje kujihusisha na biashara ya mazao ya uvuvi majini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya juhudi za kuimarisha usalama katika ziwa Tanganyika kwa kuongeza doria zinazofanywa kwa kutumia boti za Polisi na pale inapojitokeza dharura boti za JWTZ hutumika. Aidha, wavuvi nao wameanzisha vikundi vyao vya ulinzi na wanashirikiana na Polisi katika doria hizo kupitia mkakati wa Polisi Jamii. Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi katika ziwa Tanganyika, maziwa mengine pamoja na maeneo mengine ya mipakani kadri hali itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upotevu wa mapato ya Halmashauri yatokanayo na uvuvi kwa sababu ya biashara zinazofanyika majini nazishauri Halmashauri husika kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, pamoja na wananchi ili kuunganisha nguvu na kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usalama katika ziwa hilo ili biashara ziweze kufanyika kwa amani na kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza;

(a)Mheshimiwa Spika, kama Waziri alivyojibu kweli suala hili ni la muda mrefu, nimewahi kulichangia mwaka 2007 na nimewahi kuuliza swali, nikaiomba Serikali ifanye mazungumzo na Serikali ya Kongo na Burundi ili kuhakikisha kwamba tunashirikiana katika ulinzi wa mipaka yetu.

Je, suala hilo limefikia wapi? Mazungumzo yalifanyika au hayakufanyika?

(b)Mara nyingi hizo *speed boat* ambazo zimetolewa huwa hazina mafuta kutokana na kwamba Serikali inatoa Bajeti kidogo. Je Serikali inatuambia nini kwa Bajeti ya mwaka huu ili ulinzi uweze kufanyika kama ilivyopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kweli nitakuwa na majibu mafupi lakini ieleweke kwamba tunapozungumzia ziwa Tanganyika tunazungumzia Ziwa ambalo katika kina chake ni ziwa la pili ulimwenguni lakini pia katika ukubwa wa maji *fresh water lake* ni ziwa la pili ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, ziwa hili linamilikiwa na nchi Nne na Tanzania ikiwemo na umiliki wa Tanzania ni asilimia 41 ya maji ya Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, tuna neema ambayo tumeipata inatufungulia pia changamoto ambazo ni kubwa sana.

Tumekuwa na mazungumzo na wenzetu wa Congo na Burundi lakini ifahamike hizi ni nchi ambazo zimekuwa katika matatizo ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, mbali na matatizo ambayo yamo katika nchi hizo bado tunakabiliwa na matatizo ya wakimbizi kutoka katika nchi hizo, ambazo bado tupo katika mazungumzo ya kuwarejesha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mbunge kwamba matatizo ni makubwa lakini tunajitahidi kadri tuwezavyo kukabiliana nayo na mazungumzo yanaendelea yakiwemo hayo ya kuwarejesha hao wakimbizi lakini pia ya kupatikana amani katika Ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Speed Boat*, zimepatikana na mwisho wa Mwezi Julai Marekani watatupatia boti nne na katika boti hizo tumo katika utaratibu wa kuona Ziwa Tanganyika watapata ngapi. Upande wa mafuta hili ni tatizo kwa kweli tumekuwa nalo, lakini kwa mujibu wa Bajeti ambayo tunakwenda nayo tunajitahidi kulikabili kwa sababu usalama wa nchi yetu tunaupa kipaumbele. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umepita sana. Wageni waliopo hapa Bungeni leo, kwanza ni wanafunzi 20 waliofanya vizuri katika mitihani yao ya Kidato cha Sita mwaka 2011. Hawa wataletwa kwa utaratibu maalum. Lakini pia pamoja nao kuna

Wakuu wa shule 20 wasimame huko walipo, ahsanteni sana kwa kuwalea watoto hawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wazazi wa Wanafunzi hawa 20 mahali walipo tunaomba wasimame. Karibuni sana na tunawashukuru sana kwa malezi kati yenu na walimu, kuna viongozi na Maafisa toka Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, wasimame karibuni ahsante sana. Wengine wanatoka Wizara ya Elimu Mafunzo na Ufundi (WEMU) wasimame mahali walipo, Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wanafunzi sabini na walimu kumi wa shule ya msingi Mirambo ya Dar es Salaam wasimame walipo, poleni na safari, karibuni sana. Tunao wanafunzi 39 na walimu watatu wa shule ya Msingi Kikombo, Mpwapwa wapo wapi, ahsanteni sana karibuni sana.

Wageni wengine wote mnakaribishwa na mnafahamu katika *Gallery* ya *Speaker* ni Wakuu wa Mikoa wanaofuatilia Wizara yao ya TAMISEMI.

Naomba pia niwatangazie Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwamba kutakuwa na semina, siku ya Jumapili tarehe 3 Julai, 2011 kuanzia saa tano asubuhi. Aidha Mawaziri wafuatao pia wanaomba wahudhurie semina hiyo. Hawa ni Waziri wa Fedha na Uchumi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Waziri wa Kazi na Ajira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Kwa hiyo, hawa watakuwa na semina yao siku ya Jumapili katika Ukumbi wa Msekwa, naomba mhudhurie. *(Makofi)*

## BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUWATAMBUA, KUWAENZI NA KUWAPONGEZA WANAFUNZI WALIOFANYA VIZURI KATIKA MITIHANI YAO YA KIDATO CHA SITA MWAKA 2011

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge napenda kuwajulisha kuwa ni utamaduni wetu tuliojiwekea wa kuwatambua na kuwaenzi vijana wetu Watanzania pale wanapofanya vema katika jambo lolote ambalo lina maslahi kwa nchi yetu.

Leo tunawatambua Vijana wanafunzi ambao wamefanya vizuri sana katika mitihani yao ya Kidato cha Sita ngazi ya kitaifa kwa mwaka 2011.

Waheshimiwa Wabunge huu ni utamaduni wa Bunge letu kuzitambua juhudi mbalimbali za Watanzania katika fani mbalimbali kama vile Sanaa, Elimu, Uvumbuzi, Michezo na kadhalika. Aidha baada ya utangulizi huo wa awali sasa namwomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, awatambulishe kwetu wanafunzi hao ambao anayo orodha yao, naona kuna Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri naomba wanafunzi hao wangeingia kwanza, maana utawatambulisha hatutawaona, Tafadhali, waingie kwanza.

*(Hapa Wanafunzi waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge wakisindikizwa na Mpambe wa Bunge)*

**WAZIRI WA ELIMU, MAFUNZO NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Walimu, Wazazi na Wanafunzi, Mabibi na Mabwana:

Mwaka 2011, Wanafunzi 44,720 kutoka shule mbalimbali walifanya Mtihani wa Kidato cha Sita. Kati ya Wanafunzi hao wa shule, asilimia 92 walifaulu mtihani huo kwa kupata Daraja la Kwanza hadi la Nne. Katika ufaulu huo mzuri, Wanafunzi kumi walioongoza walikuwa wavulana; katika hao kumi, Wanafunzi wanane walisoma masomo ya sayansi. Aidha, Wanafunzi sita katika hao walitoka Shule za Serikali na wanne shule zisizokuwa za Serikali. Katika kundi la Wanafunzi wasichana waliofanya vizuri zaidi, Wanafunzi sita walifanya masomo ya sayansi. Pia Wanafunzi sita katika hao walitoka Shule za Serikali na wanne kutoka shule zisizokuwa za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuwazawadia Wanafunzi hawa 20; wavulana kumi na wasichana kumi kwa ufaulu wao mzuri sana. Wanafunzi hawa, kwanza, wanapewa heshima ya kuingia Bungeni leo na kufanyiwa utambulisho hapo. Watapata pia cheti na zawadi ya fedha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na Wanafunzi hawa, Serikali imeamua kuwatambua Walimu 31 waliowafundisha katika ngazi hiyo, pamoja na kuzitambua shule 13 ambazo Wanafunzi hawa walimaliza elimu yao ya Kidato cha Sita. Aidha, Serikali imefuatilia walikosoma elimu yao ya *O-level* na kugundua kuwa Wanafunzi saba kati ya wahitimu hawa 20, elimu yao ya *O- level* waliifanya katika shule saba zilizojengwa kwa nguvu ya Wananchi ama Shule za Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuzipa Shule hizo za Kata vyeti na zawadi za fedha. Ninafuraha kuwatambulisha kwako, Wanafunzi 20 waliofanya vizuri sana katika Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2011, kuwatambulisha kwako Wakuu wa Shule za *A- Level* walikosoma Wanafunzi hao, Wazazi na Wanafunzi hao na Wakuu wa Shule saba za Sekondari zilizojengwa na Wananchi, ambazo Wanafunzi saba kati ya hao 20 walisoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi 20 waliofanya vizuri katika Mtihani wa Kidato cha Sita, ambao tunawapongeza hapa watatambulishwa kwa majina na shule walizotoka na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninaomba nichukue nafasi hii, kuwatambulisha Wakuu wa Shule ambazo Wanafunzi hao wamesoma na wazazi wao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Shule za *A- Level* ambapo Wanafunzi hao wanatoka, ninaomba niwambulishe kama ifuatavyo: Abdul Wahid Zachariah, Shule ya Sekondari Al-Muntazil Seminari.

**SPIKA:** Atasimama huko huko aliko.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mwingine ni Sekundi Kayenza, Shule ya Sekondari Kibaha; Mwalimu Richard Maina, Shule ya Sekondari *Feza Boys*, Mwalimu Flora Hinju, *Marian Girls,* hii ipo katika Jimbo la Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Jimbo la Bagamoyo; Mwalimu Dismas Njawa, Mzumbe Sekondari; Mwalimu Tabitha Tusekelege, Kilakala Sekondari.

**SPIKA:** Hiyo shule alisoma Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mwalimu Sister Lillian Mdoapsu, *Kifungilo Girls Secondary*; Mwalimu Julieth Matoo, Shule ya Benjamin William Mkapa; Mwalimu Esther Nhosha, *Tabora Boys*; Mwalimu Elizabeth Abdallah, *Ashira Secondary;* Mwalimu Martin Kija, *Tarakea Secondary*; Mwalimu Dismas Njawa, *Mzumbe Secondary* na Mwalimu Anderson Mwaihabi, *Usongwe Secondary*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii pia kuwatambulisha kwako Wakuu wa Shule saba za Sekondari za Kata, walikosoma Wanafunzi saba, kati ya Wanafunzi hawa 20 waliofanya vizuri sana. Wakuu wa Shule hawa ni kama ifuatavyo: Mwalimu Jason Rwegasira, *Uhuru Secondary,* Manispaa ya Shinyanga; Mwalimu Magige Mhagachi, *Bukandwe Secondary,* Magu; Mwalimu Anderson Mwaihabi, *Usongwe Secondary,* Mbeya; Mwalimu Zaituni Mkoi, *Kikuyu Secondary,* Dodoma; Mwalimu Martin Kija, *Tarakea Secondary,* Rombo; Mwalimu Peter Lyimo, *Majengo Secondary,* Moshi; na Mwalimu Gervas Mase, *Nchugu Secondary,* Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi watakaozawadiwa leo, wameongozana pia na wazazi, ninaomba kuwatambulisha wazazi ambao walipata fursa kufika hapa Bungeni kama ifuatavyo: Fatma Sharrif kutoka Shinyanga; Zaynab Hashim kutoka Dar es Salaam; Julius Mhondela kutoka Mwanza; Mrs. Jennies Kipato Dar es Salaam; Mrs. Mwangamba kutoka Mbeya; Christina Matovolwa Dodoma; Restuta Rwezaura kutoka Dar es Salaam; Lucy Moshi kutoka Mbeya; Mrs. Naide Mvile kutoka Dar es Salaam; Mrs. Janet Kabuche Dar es Salaam; Bwana Peter Chacha Dar es Salaam; Garson Kigeza kutoka Mwanza na Rashid Mfaume Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambulisha Wakuu wa Shule na Wazazi, ninaomba kwa heshima, nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kuwatambulisha Wanafunzi waliofanya vizuri katika Mtihani wa Kidato cha Sita na kuwakabidhi zawadi alizowaandalia. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana:

Awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii, kuwashukuru waandaji wa hafla hii, kwa kunipa fursa ya kuzungumza katika tukio hili la kuwapongeza Wanafunzi waliofanya vizuri katika Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Sita Mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa kukubali vijana wetu 20 kuingia ndani ya Ukumbi huu wa Bunge ili wapongezwe na wakati wa tukio hilo likifanyika, waweze pia kushuhudiwa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Wananchi kote nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kukubali kwako kuruhusu watoto hawa waingie hapa Bungeni, ninaamini kutawatia pia moyo vijana hawa siku za usoni, watamani vilevile kuwa ni sehemu ya Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mhehsimiwa Spika, katika matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita, uliofanyika nchi nzima mwezi Februari mwaka 2011, mambo ya kutia moyo ni kuwa Wanafunzi walifanya vizuri katika masomo ya sayansi, ikilinganishwa na miaka ya nyuma hasa mwaka 2010. Masomo hayo ni *advanced mathematics, physics, chemistry* na *basic mathematics*. Hii ni hatua nzuri katika maendeleo ya sayansi hapa nchini, ikizingatiwa kuwa masomo ya sayansi yamekuwa na ufaulu usioridhisha kwa muda mrefu. Ninapenda kutoa pongezi kwa wadau wote waliohusika katika kuleta mafanikio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona matokeo na hasa viwango vya ufaulu, Serikali kwa kushirikiana na Bunge, tuliona ni vyema kuonesha kuridhishwa kwetu na juhudi za Wanafunzi hawa. Tuliona ni vyema kuwepo na jambo litakalooonesha kuridhishwa kwetu na mafanikio yao na kuamsha ari na ushindani kwa Wanafunzi ambao bado wako mashuleni ili nao waweze kuyafikia mafanikio haya na ikiwezekana kufanya vizuri zaidi. Tukaamua waje Bungeni ili tuwapongeze mbele ya Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi tuliowaalika ni 20 na majina yao ni kama ifuatavyo: Nitaomba nikitaja jina itabidi utokee mbele kidogo wakuone kisha urudi. Wa kwanza ni Mhaga Chacha kutoka Kibaha Mkoa wa Pwani; wa pili, ni Samuel Katwale kutoka Mzumbe, Morogoro; wa tatu ni Amir Abdallah kutoka *Feza Boys,* Dar es Salaam; wa nne Aaron Geshon kutoka *Tabora Boys,* Tabora. Wa Tano, ni Shaaban Omar kutoka *Tabora Boys,* Tabora; wa sita ni Kudra Baruti kutoka *Feza Boys,* Dar es Salaam; anayefuatia ni George Asenga kutoka Majengo, Kilimanjaro; anayefuatia ni Komo Nduru, kutoka *Feza Boys,* Dar es Salaam; anafuatiwa na Bwana Francis Joseph huyu anatoka *Tabora Boys,* Tabora; na Bwana George Felix kutoka Mzumbe Morogoro. *(Makofi)*

Tuingie kwenye kundi sasa lingine la akina mama wakiwezeshwa wanaweza. Bi Dourine Kabuche kutoka Benjamin Mkapa Dar es Salaam; Rahab Mwang'amba,

Kilakala Morogoro; Mary Moshi, *Kifungilo Girls* Tanga; Nuru Kipato, *Marian College,* Pwani; Zaynab Hassan, Al-*Muntaz Islamic,* Dar es Salaam; Catherine Temu, *Ashira Girls,* Kilimanjaro; Antonia Lugomo, Usongwe Mbeya; Cecilia Mvile, *Kifungilo Girls*, Tanga; Marian Matovolwa, Kilakala Morogoro; na Suzan Makoi, Tarakea, Kilimanjaro. Ahsanteni sana, ninaomba msimame kama mlivyokuwa mmesimama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtaona kuwa tumealika wasichana kumi waliofaulu vizuri miongoni mwa wasichana wote waliofanya mtihani huo wa Kidato cha Sita mwaka 2011. Uchambuzi unaonesha kuwa, wasichana hawa walifaulu kutoka Shule za Sekondari za Benjamin William Mkapa (1), Kilakala (2), Kifungilo (2), *Marian College* (1), *Al-Mutazir Islamic* (1), *Ashira Girls* (1), Usongwe (1) na Tarakea (1). Aidha, tumealika wavulana kumi waliofanya vizuri kuliko wavulana wote waliofanya mtihani huo. Wavulana hawa wamefaulu kutoka Shule za Kibaha (1), Mzumbe (2), *Feza Boys* (3), *Tabora Boys* (3) na Majengo (1). Hapa tunachokiona ni kwamba, Shule za *Tabora Boys* na *Feza* Boys ndiyo zenye idadi kubwa ya Wanafunzi kati ya 20 walioongoza katika mitihani ya Kidato cha Sita mwaka huu. Shule hizi mbili, kwa kweli zinastahili pongezi nyingi kutoka kwetu kama Waheshimiwa Wabunge na wapenzi wa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la kutia moyo kwenye matokeo haya ni kuwa, miongoni mwa Wanafunzi hawa 20 Wanafunzi saba walijiunga na Kidato cha Tano baada ya kumaliza Kidato cha Nne katika Shule za Kata. Wanafunzi hao ni Samuel Katwale kutoka Sekondari ya Bukwande Magu, Francis Josephat kutoka Sekondari ya Nchungu Tarime, Rahab Mwang'amba kutoka Sekondari ya Vwawa Mbeya, Zaynab Hassan kutoka Sekondari ya Uhuru Shinyanga, Marian Matovolwa kutoka Sekondari ya Kikuyu Dodoma, Suzan Makoi kutoka Sekondari ya Tarakea Rombo na Antonia Logomo kutoka Sekondari ya Usongwe Mbozi. Kati ya Wanafunzi hao saba, watano ni wasichana na wawili ni wavulana. (*Makofi*)

Ninapenda nitumie nafasi hii, niwapongeze Wanafunzi hawa saba kwa dhati kabisa, kwa kuwa wamethibitisha kuwa uamuzi wa Serikali wa kujenga Shule za Kata ulikuwa na utakuwa uamuzi sahihi. (*Makofi*)

Kama shule hizi zisingekuwepo, huenda vijana hawa wasingeweza kuonesha uwezo wao kitaaluma kama walivyofanya hususan wasichana hao. Kwa mara nyingine, niwaombe Viongozi na Wananchi, ambao wakati mwingine hubeza shule hizi, wakubali kuwa ni heri kuwa na shule hizo kuliko kutokuwa nazo kabisa. (*Makofi*)

Jukumu la Serikali, Wabunge na Wananchi kwa ujumla ni kuendelea kuziboresha shule hizo na kuwatia moyo Walimu na Wanafunzi wao ili waendelee kufundisha na kujifunza kwa bidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wanafunzi hawa hawakufikia mafanikio haya bila ya malezi na msaada kutoka Wazazi na Walimu wao. Kwa hiyo, tulifanya makusudi kualika mzazi mmoja kwa kila Mwanafunzi ili ashuhudie mwanae anavyopongezwa siku ya leo. Ninawaomba wazazi hawa na wale waliobaki nyumbani, wapokee pongezi zangu kwa malezi na miongozi yao kwa Wanafunzi hawa iliyochangia mafanikio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inathamini kazi zinazofanywa na Walimu nchini; ni kwa mtazamo huo, tumewaalika Walimu waliowafundisha Wanafunzi hawa. Kufaulu kwa Wanafunzi kumechangiwa na juhudi za Walimu wao. Nao tumetaka washuhudie matokeo ya kazi zao siku ya leo. Vilevile hii itakuwa ni fursa ya kutoa ujumbe kwa Walimu wengine, kuongeza bidii katika kuwawezesha Wanafunzi wao kufikia malengo yao. Ninaomba Walimu waliochangia mafanikio ya Wanafunzi hawa, wapokee shukrani zangu binafsi pamoja na Serikali kwa kazi kubwa na heshima waliyoifanya.

Kwa pamoja ninawapongeza Wazazi na Walimu wote, kwa kutimiza wajibu wenu vizuri, wajibu wa kuwalea watoto hawa katika maadili mema na kuwaongoza kwenye njia nzuri zilizowawezesha kukaribishwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwaalika Bungeni Wanafunzi hawa, pamoja na Walimu na Wazazi wao, tumeona tusiishie hapo, kwa hiyo, tumepanga kutoa zawadi ndogo kwa Wanafunzi bora ishirini, Walimu wao na Shule zao, ikiwa ni ishara ya kuthamini kazi kubwa iliyofanywa. Zawadi hizo ni kama ifuatavyo: Kompyuta ndogo *(laptops)* na shilingi laki moja na hamsini elfu, pamoja na cheti cha ubora kwa kila Mwanafunzi aliyealikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shilingi laki tano pamoja na cheti kwa Walimu wale thelatini na moja wa *A-Level* waliowafundisha Wanafunzi hao. Shilingi milioni moja pamoja na cheti kwa kila shule walikosoma Wanafunzi hao. Vilevile tumeamua kutoa meza ya maabara yenye thamani ya shilingi milioni tano pamoja na cheti kwa kila Shule ya Kata, ambapo walisoma Wanafunzi saba kati ya ishirini waliofanya vizuri Kidato cha Sita. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zawadi nitakazozitoa hapa Bungeni ni kwa Wanafunzi wale ishirini ni cheti tu ili nisikuchukulie muda wako mwingi, zawadi nyingine zitatolewa kwenye hafla nyingine ambayo imeandaliwa hapo baadae jioni kwa ajili ya Walimu na makundi mengine yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina imani kuwa, utaratibu huu wa kutambua na kutoa motisha kwa Wanafunzi Bora, utaongeza ari ya Wanafunzi na Walimu kujifunza na kufundisha kwa bidii na hivyo kuinua kiwango cha ubora wa elimu nchini; ni vyema ukawepo sasa utaratibu bora na endelevu wa utoaji wa motisha kwa Wanafunzi na Walimu wao. Nimeagiza Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, walifanyie kazi suala hili ili kuwezesha utaratibu huu kuwa wa kudumu na watazame vilevile uwezekano wa kuongeza katika utaratibu huu, hata wale wanaofanya vizuri katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Lengo langu ni kuona kama tunaweza tukawa na Mfuko Maalum utakaowezesha Wanafunzi wa aina hii, kupata fursa ya kuendelezwa katika Vyuo Vikuu nje ya nchi, ambavyo vinafanya vizuri zaidi hasa katika fani zile ambazo tunadhani zitatujengea uwezo kama Taifa letu kwa siku zijazo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa wanangu hawa ni kuwa, bila shaka Mwenyezi Mungu atawajalia, mpate nafasi ya kuendelea mbele zaidi kuliko hapa mlipofika. Huko mnakokwenda, mtaona kuna uhuru zaidi kuliko mlikotoka, uhuru huo si tatizo bali tatizo ni jinsi utakavyotumia uhuru huo. Ninaomba niwashauri wanangu; msijiingize kwenye mambo yasiyo na tija na elimu yenu, someni na msipoteze muda mwingi na migomo isiyo na tija wala maandamano ambayo hayatawasaidieni katika uhai wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru Wanafunzi, Walimu na Wazazi, kwa kukubali mwaliko wetu. Niwaombe Wanafunzi waongeze bidii kwenye masomo yao kwa siku zijazo, vilevile wadumishe nidhamu kwa Walimu na Wazazi ili waweze kupata mafanikio zaidi. Ninawashukuru pia Walimu kwa juhudi zao na niwaombe waongeze bidii katika kazi zao ili yapatikane mafanikio makubwa zaidi hasa katika masomo ya sayansi. Ninawashukuru wazazi kwa malezi yao na kuwaomba kuendelea kuwaongoza vijana waliobaki na hawa ambao mmewalea hadi hapa, endeleeni kuwalea ili waweze kuwa ni Watanzania wema zaidi. Mwisho, ninawatakia hafla njema jioni ya leo, safari njema kurudi nyumbani na maisha mema ya hapo baadae kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, ninaomba basi mniruhusu niwakabidhi vyeti Wanafunzi hawa na kama nilivyosema, hizo zawadi nyingine watakabidhiwa katika hafla itakayofanyika leo jioni.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante. Sasa Waheshimiwa wakati Waziri Mkuu anatoa vyeti, atampa mkono huyo mtoto, atanipa mimi mkono, atakwenda kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, halafu anachukua nafasi yake.

(*Hapa Mwanafunzi Husika Alikabidhiwa Cheti na Kupewa Mkono wa Pongezi na Waziri Mkuu, Spika na Kiongozi wa Upinzani Bungeni)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa zoezi lianze, tunaanza na Mwanafunzi Susan J. Makoi, Mariam Matovolwa, Celilia A. Mvine, Antonia J. Lugomo, Catherine E. Temu, Zainab Hassan, Nuru N. Kipato, Mary C. Moshi, Rahabu Mwangamba na Dorine Kabuche. Sasa ni wavulana; George M. Felix, Francis Joseph, Coman Duru, George V. Yasenga, Kudra H. Baruti, Shabani Omary, Aron Gason, Amiri Abdallah, Samuel Katwale na Muhagachi P. Chacha. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, vijana ambao walikuwa wameandaliwa, wamekabidhiwa wote.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu pia ninaomba niwapongeze sana watoto wetu wazuri, niwapongeze Walimu na Wazazi. Kama alivyosema Waziri Mkuu; na sisi Wabunge tuendelee kutengeneza mfumo mzuri sana, ambao utawezesha nchi yetu kuwa na watoto namna hii wengi zaidi. Kwa hiyo, sisi tunawaonea fahari kama alivyosema, huko mnakokwenda, safari bado mbichi kabisa, unachokifanya wewe ndiyo

utakuwa wewe, wanachofanya wenzako siyo chako. Kwa hiyo, ninadhani mtatumia nafasi hiyo kufanya yale makubwa. *Sergeant-at-Arms* warudishe watoto. *(Makofi)*

*(Hapa Wanafunzi Husika Walitoka Ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, katika siku tulizoongeza, leo imefikia tamati. Kwa hiyo, inabidi Waziri Mkuu aanze kujibu, kufafanua ama kuelezea yale yote mliyokuwa mmejadiliana katika siku hizi zote. Sasa tuna wachache ambao hawakupata nafasi, lakini hatuna namna kwa sababu kama nilivyoeleza siku ile, tunaongeza siku mbili, Ofisi ya Waziri Mkuu ni sawasawa na Wizara kama nne; sasa kwa sababu hiyo, asubuhi hii muda nilionao unatosha kuwapa Naibu Mawaziri wawili wa TAMISEMI kuchangia. Halafu na Waziri wa TAMISEMI mwenyewe, kwa sababu ile ni Wizara kabisa, Waziri Mkuchika atapewa dakika thelathini, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Uwekezaji, atapewa dakika thelathini na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera naye atapewa dakika thelathini. Hii itatufikisha mpaka saa saba, halafu jioni tutampa Mheshimiwa Waziri Mkuu kipindi cha muda wa saa moja, aweze kuhitimisha. Sina sababu ya kumpa muda, lakini kwa safari hii itabidi nimpe, kwa sababu kuna kazi bado itaendelea ya kuingia kwenye vifungu, tusipofanya hivyo hatutamaliza. Kwa hiyo, huo ndiyo mpangilio utakaokuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, ambao hawakufanikiwa kufikiwa kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 60(11) - (15), wanaweza kuandika, halafu wakiandika maandiko yao yanaingia kwenye rekodi halisi ya Bunge. Usipoandika ndiyo basi, uliomba kuchangia haukupata nafasi wala mawazo yako hayakuingia kwenye *Hansard* yetu. Kwa hiyo, ninawashawishi wale waliobakia, wapo kama kumi na mbili, waandike kusudi rekodi za mchango wao ziweze kuingia kwenye *Hansard*.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata wasaa huu ili niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda. Ninampongeza kwa Hotuba yake, lakini pia ninaipongeza Hotuba iliyotolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe, ambayo kama Serikali itaitumia japo kwa kiasi fulani, itaweza kuliendeleza Taifa letu, kwa faida yetu wote na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia juu ya mambo yafuatayo; Elimu, Kilimo, Ajira na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, katika suala la elimu, nitazungumzia juu ya shule na walimu. Kazi iliyofanywa na Serikali ya ujenzi wa shule za kata kwa kila kata imeonekana, lakini shule hizi zinakabiliwa na changamoto kubwa sana; shule hizi nyingi hazina madawati, wanafunzi katika baadhi ya shule wanakaa chini. Ninaiomba Serikali kama ilivyosimamia ujenzi wa shule hizi, basi ihakikishe pia madawati yanapatikana, kwani watoto wetu wanakuwa na miandiko mibaya kwa kutokuwa na madawati.

Mheshimiwa Spika, shule hizi za kata pia zina upungufu mkubwa wa walimu na vitendea kazi. Kwa upande wa walimu, wapewe stahili zao, wapandishwe madaraja kwa muda unaostahili; hii itafanya wale wanaopangwa shule hizo kuzikubali. Nyingi ya shule hizi, zimekosa walimu kwa sababu ya historia ya manyanyaso wanayoyapata walimu, hivyo hata wale wapya kuikimbia kazi hii. Serikali isikilize kilio cha walimu wote nchini.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha mpaka sasa bado wanawake wanapokwenda kujifungua, wanadaiwa vifaa kama vile pamba, *gloves* na pesa kidogo. Vilevile Dawa ya Mseto ya Malaria imeonesha kutokuwa na matokeo makubwa hususan kwa watoto, wanaharisha sana wanapoitumia. Ninaiomba Serikali iichunguze dawa hii ina matatizo gani.

Wauguzi wengi wamekuwa na vitendo visivyo vizuri, vya kudhalilisha wagonjwa hususan wajawazito, kwa kutumia lugha chafu. Ninaiomba Wizara husika ilitupie jicho jambo hili.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo ni jambo muhimu sana na asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo. Ninaiomba Serikali ihakikishe vocha za kilimo zinawafikia walengwa ili kuwa na kilimo chenye tija. Matrekta yapatikane, ufanyike utaratibu wa kuwakopesha Wananchi ili Kilimo Kwanza kifanikiwe. Mazao yanayohimili ukame, tuyasambaze nchi nzima baada ya kuyafanyia utafiti ili kuondokana au kupunguza njaa. Mfano wa mazao haya ni kama vile Zao la Mtama na Uyoga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira; viwanda vyetu vifufuliwe ili vijana wetu waweze kuajiriwa. Wawekezaji wanapokuja hapa nchini, pamoja na sheria zilizopo, zisimamiwe kikamilifu kuhakikisha kwamba, Wananchi wetu wanaajiriwa katika Miradi hiyo. Pia vijana na akina mama wakopeshwe kupitia SACCOS au katika mabenki kwa masharti nafuu. Ninaamini Serikali ikilitilia maanani suala hili, watu wengi wataweza kujiajiri, lakini pia Serikali itengeneze ajira ambazo Watanzania wanaweza kuajiriwa nazo.

Mheshimiwa Spika, suala la Utawala Bora ndiyo kioo cha kila kitu. Kiongozi anategemewa na Wananchi wake awaelekeze wafanye nini au waende vipi. Pamoja na nia njema aliyonayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bado Watendaji wake Serikalini wameendelea kumwangusha sana katika maeneo mbalimbali. Tumeshuhudia huduma mbalimbali zikidhoofika kutokana na udhaifu wa Viongozi kutoa maamuzi. Mawaziri wamekuwa ni wengi mno na hata baadhi ya majibu yao ni ya kisiasa

zaidi, kitu ambacho wanakwenda kinyume na matarajio na maagizo ya Rais. Watendaji wanasababisha Wananchi wamchukie Rais, kwa kuwa hata Mawaziri hawatekelezi maagizo anayoyatoa Rais katika ziara na hotuba mbalimbali. Tunaomba Watendaji watekeleze maagizo ya Rais na siyo ya kwao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuchaguliwa kwa mara ya pili kuwa Waziri Mkuu. Pia ninampongeza kwa maandalizi mazuri yaliyofanywa na Ofisi yake, kwa kuandaa Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu, ninaomba nianze kuchangia juu ya shughuli nzima za utendaji katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia, utendaji kwa ujumla unaanza kugusa katika Halmashauri za Vijiji. Vijiji vyetu kwa hivi sasa vimekuwa vikipanga shughuli za maendeleo na kusimamia utekelezaji ili kuleta maendeleo ya vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kupanga mipango mizuri ya kuunga mkono jitihada za Wananchi kwa kutoa ruzuku katika Halmashauri zetu ili kusaidia Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Serikali ilikuwa na mpango wa kutoa ruzuku katika vijiji, fedha ambazo zilikuwa chachu katika kusaidia maendeleo ya vijiji. Kwa maana hiyo, vijiji vyetu vilikuwa vinapokea fedha nyingi na Wasimamizi Wakuu ni Mwenyekiti wa Kijiji na Halmashauri yake, lakini inasikitisha sana kuona Mwenyekiti huyu huyu anayesimamia shughuli za maendeleo na kudhibiti fedha za umma zitumike ipasavyo, hana mshahara, hana posho wala motisha yoyote. Je, Serikali haioni kuwa haitendi haki? Kwa kutenda hivyo, hatuoni inawapa kishawishi cha kutumia fedha hizi kinyume na mipango iliyopo; hivyo, kuzorotesha maendeleo au viongozi kuishia jela kwa ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Mheshimiwa Diwani ndiye Msimamizi Mkuu wa maendeleo katika kata; anawajibika kusimamia mapato na matumizi ya halmashauri; lakini Waheshimiwa Madiwani wamekuwa wakipata posho ndogo sana, ambayo haikidhi hata kumwezesha kuzunguka katika Kata yake. Serikali haioni kuwa haiwatendei haki Waheshimiwa Madiwani hawa?

Kwa kuwa mara zote Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukiomba sana Waheshimiwa Madiwani walipwe mishahara na marupurupu mengine; kwa nini Serikali haitaki kusikiliza maombi yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi ya Wabunge ni pamoja na kuishauri Serikali, ninaomba nichukue nafasi hii, kuishauri Serikali kwa mara nyingine kama ifuatavyo: Waheshimiwa Madiwani walipwe shilingi 500,000 kwa mwezi, ikiendana na kuboresha viwango vya posho na marupurupu mengine; Wenyeviti wa Vijiji walipwe shilingi

200,000 kwa mwezi; na Wenyeviti wa Vitongoji walipwe posho ya shilingi 100,000 kila baada ya miezi mitatu.

Ninatarajia kama Serikali itatekeleza ombi na pendekezo hili, usimamizi wa shughuli za maendeleo zitaboreka na tutapunguza ubadhirifu mkubwa katika Miradi ya Maendeleo. Ninaamini Serikali ni sikivu na itasikiliza kilio changu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa matarajio ya utekelezaji wa hoja hii.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na muda wangu wa kuchangia kwisha, kabla sijamaliza hoja zangu zote, nimeona nimalizie kwa maandishi.

Tatizo kubwa la Daraja la Mto Momba, kiunganishi cha Wilaya ya Sumbawanga na Wilaya ya Mbozi kwa Vijiji vya Kilyamatu na Kamsamba, Ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa, ambalo ni muhimu sana kiuchumi, kijamii na kisiasa ni kama ifuatavyo:-

Kiuchumi: Daraja hilo likijengwa litatumika kwa jamii kusafirisha mazao yao yanayolimwa kwa wingi katika maeneo haya kama vile Mpunga, Mtama, Ulezi, Ufuta, Mbaazi na Samaki toka Ziwa Rukwa, ambayo soko lao kubwa lipo Mkoa wa Mbeya, Tunduma na nchi jirani za Zambia na *DRC*.

Kijamii: Katika maeneo hayo, hakuna Hospitali wala Kituo cha Afya. Hivyo, Wananchi wa maeneo ya Vijiji vyote vya Tarafa ya Kipeta, hutegemea huduma hiyo Wilaya ya Mbozi au Hospitali ya Rufaa Mbeya, jambo ambalo kukosekana kwa Daraja hilo, wagonjwa hulazimika kupita kwenye kivuko cha mguu kilichotengenezwa na Wamissionari wa Dhehebu la *RC*, ambalo huwatoza Wananchi shilingi 50 kila anapovuka.

Mara nyingine Mwananchi akikosa fedha hulazimika kuvuka Mto huo kwa mguu, jambo ambalo ni hatari na mara nyingine Wananchi hubebwa na Mto huo na kufa na pia hukamatwa na Mamba. Hivyo, tunaomba Daraja hilo lijengwe kunusuru maisha ya watu.

Maji: Kutegemea ufadhili wa Benki ya Dunia tu hakuwezi kukidhi tatizo kubwa la maji tulilonalo. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga iliteua vijiji kumi kupitia ufadhali wa Benki ya Dunia; mpaka sasa hakuna hata kijiji kimoja kilichopatiwa maji hadi sasa. Hivyo, Serikali itenge fedha za kutosha ili kutatua tatizo hilo.

Uvuvi: Tunayo Maziwa mengi katika Nchi yetu ya Tanzania, yenye kila aina ya samaki, lakini hayajatumiwa vizuri ili kuleta kipato kwa nchi yetu wala kupunguza umaskini kwa wavuvi wadogo wadogo. Mfano, Ziwa Rukwa linatoa ajira kubwa kwa wavuvi wadogo wadogo, kila mwaka takriban Wavuvi wa Ziwa Rukwa huvua samaki si chini ya tani 42 kwa zana hafifu na duni. Wavuvi hao wangekuwa na zana za kisasa, wangevua samaki wengi, wangepata kipato kikubwa zaidi; hivyo, uchumi wao ungekua. Ninaishauri Serikali itoe vifaa vya uvuvi kwa mkopo katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Rukwa lina mamba wengi, tunaomba Serikali iwapunguze.

Ninaiomba Serikali iwezeshe kuwepo kwa mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata ya Milepa, Vijiji vya Milepa, Kisa, na Msui; Kata ya Kaoze, Vijiji vya Chombe, Tululu na Kianda Igonde; Kata ya Mfinga, Vijiji vya Mfinga, Kasekela, Mtapenda na Nkwilo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikumbushie ahadi za Serikali ili zitekelezwe: Mheshimiwa Mwandosya, Waziri wa Maji, alitoa ahadi mwaka 2008, kuwapelekea maji Wananchi wa Kijiji cha Sakalilo; Mheshimiwa Rais Kikwete wakati wa Uchaguzi Mkuu, alitoa ahadi zifuatazo; kupeleka maji Mji Mdogo wa Laela; kupeleka umeme Mji Mdogo wa Laela; kuweka lami Km.12 Barabara ya Kalambanzite – Ilemba; na kuweka lami Barabara ya Miangalua – Chombe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ninautoa kwenye Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo ndiyo Sekta pekee inayoajiri Watanzania wengi na tafiti zimeonesha kwamba, ukuaji wa uchumi unaotokana na ukuaji wa Sekta ya Kilimo unapunguza umaskini kwa zaidi ya mara mbili kuliko ukuaji unaotokana na Sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele hiki ni muhimu sana na kitatekelezeka tu, iwapo nyenzo kwa maana ya pembejeo, zinazokamilisha kilimo hicho, zinapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu na kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuishauri Serikali iwarahisishie wakulima kupata pembejeo zote husika kwa wakati na kwa bei nafuu. Uwepo utaratibu mzuri wa kuwakopesha wakulima matrekta kwa gharama nafuu na kwa utaratibu wa vijiji au vyama vya wakulima au vikundi vya wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itengeneze utaratibu wa kuwafanya wakulima hawa sasa kukopesheka na hasa wakulima wadogo wadogo, ambao sasa hivi hawapati mikopo kwa madai kwamba, hawakopesheki.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la pembejeo kutopatikana kwa wakati mwafaka, suala hili ni vyema litiliwe mkazo, Wananchi wana mwamko mkubwa sasa wa Kilimo Kwanza, lakini pembejeo hazipatikani kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Liwale ni moja ya Wilaya ambazo zinalima Zao la Korosho kwa wingi sana. Jambo la kusikitisha, hadi sasa Wilaya hii imekosa pembejeo

aina ya *Sulphur* (Salfa), ambayo hutumika kunyunyizia mikorosho ili kutibu Ugonjwa wa Ukungu wa Mikorosho. Kipindi hiki ndiyo kipindi mwafaka cha kunyunyizia dawa hiyo katika mashamba yao. Wakulima wa wilaya hii wamekosa *Sulphur,* haipatikani kabisa, bei ya mfuko mmoja ilikuwa shilingi 18,000; hivi sasa imepanda hadi shilingi 30,000 kutokana na kutopatikana kwa pembejeo hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, wakulima wa Wilaya hii iwapo hawatapata *Sulphur* hiyo kwa wakati mwafaka, kwa vyovyote vile watapata madhara makubwa na tutegemee kabisa kupata zao hili pungufu na kwa hiyo, kuathiri Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumwomba Wakala wa kupeleka *Sulphur* Mtwara, ajitahidi kufanya hivyo kabla wakulima hawa hawajaathirika. Vilevile nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, anisaidie kufuatilia suala hili ili wakulima hawa wapate pembejeo hiyo muhimu sana kwa Zao hili la Korosho.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuzungumzia suala la Wakimbizi kama ifuatavyo:-

Kwanza, wakimbizi kuwepo nchini ni mzigo kwa Serikali na sasa wapo wapatao 162,256 na Serikali imeridhia kuwapatia uraia na ndiyo ubinadamu kusaidiana, lakini Serikali kwa nia yake nzuri pia iangalie kwa kuchukua tahadhari kubwa juu ya kutokuwa na athari yoyote ya baadae katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiusalama.

Mheshimiwa Spika, maelezo yangu ni kutoa angalizo kabla ya utekelezaji.

Pili, baadhi ya Halmashauri bado zinaendelea kutoza ushuru wa “Geti” na ambayo tayari agizo hilo limefutwa kwa Tangazo la Serikali Namba 230 la Mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ifuatilie tatizo hilo ambalo tayari ni chanzo cha migogoro katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria Na. 25 ya 1972 na Marekebisho yake, inayowataka wafanyabiashara wafanye biashara zao mahali panaporuhusiwa tu, lakini kama tunavyoona, Sekta Isiyo Rasmi inakua kwa kasi na wahusika wa biashara hizi wanajikita mahali popote, mradi tu waweze kuuza bidhaa zao. Mfano ni Dar es Salaam, Mwanza na maeneo mengine mengi. Ninashauri Halmashauri zetu na Manispaa, zihimize vijana hawa kuhamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Hii itasaidia kuwatambua na pia kuwawezesha kujiunga na Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kwani mingi

ipo tayari sasa kuwaundia mafao yao na hivyo kupanua wigo wa Watanzania wanaofaidika na Hifadhi za Jamii kutoka asilimia tatu ya sasa hadi angalau asilimia 75.

Kama tunavyoelewa, Sekta Isiyo Rasmi ndiyo yenye wajasiriamali wengi na wanaolizalishia Taifa uchumi mkubwa, lakini wengi wao hawalipi kodi husika na kulikosesha Taifa pato zaidi. Hivyo, ninazisihi Halmashauri na Manispaa, zisimamie kikamilifu katika kuwaweka mahali na sehemu zilizotengwa kwa ajili hiyo ili Sekta nyingine zinazohusika na wajasiriamali hawa, nazo ziweze kufanya yanayohitajika ili kuwawezesha zaidi na wao waweze kuchangia zaidi katika *GDP* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, ninawasihi sana Wakurugenzi na wahusika wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, yaani Ilala, Temeke na Kinondoni, waonee huruma pesa ya wafanyakazi iliyomwagwa pale *Machinga Complex Ilala.* Jengo hili halitumiki kama ilivyokusudiwa, vizimba vimehodhiwa na kufungwa bila kutumiwa na kuna haja ya Manispaa zote kushirikiana ili kuona ni jinsi gani jengo litatumika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ninarudia kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), kwa kuteuliwa tena kushika wadhifa huo na uteuzi wake kuridhiwa na Bunge kwa kura nyingi sana. Vilevile ninawapongeza Mawaziri; Mheshimiwa William Lukuvi (Mb), Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Mary Nagu (Mb), Waziri wa Nchi – Uwezeshaji na Uwekezaji; Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Aggrey Mwanri (Mb) na Mheshimiwa Kassim Majaliwa (Mb), Makatibu Wakuu; Bw. Peniel Lyimo na Hussein Katanga; na Naibu Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa jitihada walizofanya kuandaa, kuongoza na kuratibu shughuli za Ofisi hiyo na Mikoa yote nchini. Hongereni sana na ninawahakikishia kuwa, ninaunga mkono hoja.

Baada ya pongezi, ninaomba niwasilishe mchango wangu kwa Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utawala unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Changamoto zitokanazo na ukubwa wa Wilaya – Wilaya ya Arumeru ni moja ya Wilaya kubwa sana nchini; ukubwa wa eneo pamoja na wingi wa watu na miundombinu duni, hukwaza utoaji wa huduma kwa Wananchi. Uongozi wa Wilaya (Chama cha Mapinduzi na Halmashauri ya Wilaya), walikwishapendekeza kuwa, Wilaya hiyo igawanywe kuwa wilaya mbili. Ninaomba Serikali ipokee ombi hilo na kulifanyia kazi ili kusogeza huduma karibu na Wananchi.

(b) Wapo watumishi kwenye ngazi za Wilaya ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu sana. Hiyo huwafanya utendaji wao kushuka na zaidi sana huwa chanzo cha

kero zinazowakabili Wananchi katika wilaya. Mojawapo ya kero hizo, miradi na majukumu mbalimbali kutotekelezwa ingawa fedha zinatengwa na taarifa ya matumizi kutolewa. Ninashauri watumishi waliokaa kituo kimoja muda mrefu na wale ambao utumishi wao hauridhishi wahamishwe.

Sehemu kubwa ya Wilaya ya Arumeru hususan Arumeru Magharibi ilikumbwa na ukame kwa takriban miaka minne hadi sasa. Tunaishukuru Serikali kwa msaada wa chakula walichopewa Wananchi wanaokabiliwa na ukame na njaa kwenye Wilaya hiyo. Ninapenda kuwasilisha ombi kuwa tupatiwe chakula cha kutosha, kwani hali inaendelea kuwa mbaya kwenye Kata za Bwawani, Oljoro, Mateves, Kisongo, Musa, Mwandet, Olkokola, Oldonyosambu, Nduruma, Mlangalini na maeneo mengine ya Jimbo hilo. Ninaomba Idara zinazoshughulika na ugawaji wa chakula cha njaa, ziache kutumia takwimu za mezani zinazotolewa na Ofisi ya Mkoa, badala yake wachukue takwimu Wilayani ama waende Vijijini kuhakiki na kuandika taarifa ya hali halisi.

Mwaka 2009 kufuatia ukame wa muda mrefu, wafugaji wengi walipoteza mifugo katika Jimbo la Arumeru Magharibi. Serikali ilifanya tathmini ya hasara iliyopatikana na kuahidi kulipa fidia. Hadi sasa hakuna fidia iliyolipwa na hivyo ilichangia kupungua kwa kura za Wagombea wa CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2010. Ninaomba Serikali iwajulishe Wafugaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kiasi cha fidia iliyopangwa kulipwa na tarehe iliyopangwa kutekelezwa ahadi hiyo.

Asilimia tisini ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha haina maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alipofanya mkutano wa hadhara kwa ajili ya Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, aliagiza kuwa, Uongozi wa Wilaya uandae *Master Plan* ya maji kwa Wilaya nzima na kuwasilisha Serikalini ili fedha zitengwe na kutatua kero hiyo kabla ya 2015. Mheshimiwa Rais, alihimiza kuwa utekelezaji wa agizo hilo uanze mara moja. Hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa kutekeleza agizo hilo na jambo hili ni la haraka, kwa sababu hadi tunapoadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika, Wananchi bado hawajui kuwa watapataje maji ya kunywa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aingilie kati ili agizo hilo la Mkuu wa Taifa letu, litekelezwe bila kuchelewa zaidi.

Tarafa za Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Kata zilizo nyingi hazina majengo ya ofisi. Watendaji hufanyia kazi maeneo ambayo hayaabirishi hadhi ya Serikali na Taifa letu kwa ujumla. Ninaomba Wilaya hiyo itengewe fedha ili iweze kujenga Ofisi za Tarafa na Kata; hivyo, kuwafanya Watendaji kutekeleza wajibu wao kwenye mazingira mazuri.

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha haina barabara. Hakuna hata kilometa moja ya barabara ya lami na zile za udongo ni mifereji ya maji ya mvua na njia za ng'ombe. Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa, barabara hizo zitatengenezwa ili zipitike mwaka mzima. Hata hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), haijumuishi hata barabara moja ya Wilaya hiyo. Hii ina maana kuwa, ahadi hiyo haitatekelezwa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015. Ili kujenga imani ya Wananchi kwa Chama cha

Mapinduzi, ninashauri kuwa fedha zitengwe ili kujenga barabara hizo, ikiwemo barabara moja ya lami aliyoahidi Mheshimiwa Rais.

Ninaipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kuendeleza kilimo kupitia Mpango wa Kilimo Kwanza. Hata hivyo, ninaona kuwa mikakati iliyowekwa ya utekelezaji ina upungufu. Upungufu mkubwa ni kutokuwepo kwa mkakati wa kuwezesha vijana kupata mafunzo na nyenzo ili waanzishe ushirika na kushirikiana na wawekezaji kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi, pamoja na ujenzi na uendeshaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Ninashauri kuwa uandaliwe Mpango Maalum wa kuwezesha vijana wetu kushiriki kwa vitendo katika Mpango huo. Aidha, Idara ya Vijana iwakilishwe kwenye Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ili kuwakilisha maslahi ya vijana.

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ni Wilaya ya Vijijini *(Rural District);* robo tatu ya Vijiji vya Wilaya hiyo havina umeme, bado wanatumia koroboi. Ninaishukuru Serikali kwani kupitia Wakala wa Umeme Vijijini, fedha za kupeleka kwenye sehemu *(part of)* Kata za Oldonyosambu, Mlagarini, Oljoro na Musa zimetengwa mwaka 2010/11. Hata hivyo, utekelezaji bado haujaanza. Ninaiomba sana Serikali kuwa ituongezee fedha ili kusambaza umeme kwenye Kata zilizobaki tupunguze kero kwa Wananchi na kuvutia wawekezaji, kwani Wilaya hiyo haina hata kiwanda kimoja hadi sasa. Hali hiyo husababisha umaskini kwani Wananchi wengi hutegemea kilimo cha mbogamboga, ambacho mapato yake hayakidhi mahitaji halisi ya kujikimu kwa familia.

Wilaya ya Arumeru (Halmashauri ya Wilaya ya Arusha) ni moja kati ya zile zilizo nyuma kielimu. Baadhi ya Kata hazina Sekondari; mfano, Sambasha na Kiranyi. Shule zilizoko zina upungufu mkubwa sana; hazina nyumba za walimu, vyumba vya madarasa, maabara, vyoo na samani. Hali hii hufanya mazingira ya kufundishia kuwa magumu kwa walimu na wanafunzi. Matokeo yake, shule nyingi hazina walimu na zimekuwa zikifanya vibaya kwenye mitihani. Mheshimiwa Rais alipoitembelea Wilaya hiyo, tarehe 17 Septemba, 2010, aliwajulisha Wananchi kuwa, Serikali imetenga shilingi bilioni 230 kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu. Ninaomba fedha hizo pamoja na fedha za MMEM II, zigawanywe kwa uwiano ili Wilaya yangu nayo ipate mgawo wake.

Ninaomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukiendeleza Kituo cha Afya Olturumet kuwa Hospitali ya Wilaya ili kupunguza kero ya ukosefu wa huduma za kitaalam *(Specialist Services)* kwenye Wilaya yetu. Sambamba na hilo, Vijiji vingi Wilayani kwangu, zaidi ya asilimia 80, havina zahanati wala kliniki za afya ya uzazi na mtoto. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010, imeweka lengo la kupeleka huduma karibu na Wananchi. Ninaomba tupatiwe rasilimali fedha na wataalam ili tutekeleze malengo hayo. Kwenye Kata ya Olkokola kimejengwa Kituo cha Afya. Hata hivyo, Kituo hicho hakina wataalam wala nyumba za watumishi. Ninaomba Serikali ituwezeshe kituo hicho kitoe huduma, kwani hadi sasa hakitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo mawili makuu ya kiusalama yanayowakabili Wananchi kwenye Wilaya ya Arumeru kama ifuatavyo:-

(a) Wananchi katika Wilaya ya Arumeru wamekuwa wanakumbana na kero nyingi sana zinazotokana na kukosekana kwa Vituo vya Polisi karibu na Wananchi. Makao Makuu ya Wilaya yako Usa River. Mwananchi aliyeko kata ya Bwawani, Oljoro au Kisongo na nyinginezo zilizoko Arumeru Magharibi, hulazimika kusafiri takriban kilomita 50 kufuata huduma za Polisi wanapopatwa na tatizo. Hii huhatarisha usalama wa raia na mali zao kwani hawana ulinzi.

(b) Inaelekea kuwa askari wengi kwenye Wilaya ya Arumeru kuanzia Kamanda wa Wilaya na wengine, wamekaa kwenye Wilaya hiyo kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu; wamezoweana na wahalifu na wengine wamekuwa sehemu ya kero zinazowakabili Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuzikabili kero zote mbili, ninapendekeza yafuatayo:-

(i) Wilaya ya Arumeru igawanywe kuwa mbili kiusalama (Polisi na Idara nyingine) na hivyo Ofisi ya Wilaya na Kituo kikubwa kijengwe kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi; na

(ii) Askari na Maafisa wa Polisi waliokaa muda mrefu (zaidi ya miaka mitatu) kwenye kituo kimoja, wahamishwe. Askari kwenye Vituo vya Ngaramtoni, Oldonyosambu na Longido, wasikae muda mrefu kwa sababu njia hiyo ndiyo lango la biashara haramu kati ya Arusha na Namanga.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kuchukua nafasi hii adimu, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuchaguliwa kushika wadhifa wake. Hii ni imani tosha kwa Waheshimiwa Wabunge, uwezo wako kiutendaji na imani yako kwa nchi (uzalendo).

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, ningependa kuchangia hoja iliyo mbele yetu, ambayo imesheheni nia na dhamira nzuri sana kwa ustawi wa Wananchi wa Nchi hii ya Tanzania. Imani yangu ni kwamba, maelezo yote yaliyojitokeza kwenye Hotuba hii ni hatua ya kwanza katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu mwaka 2010 – 2015.

Pamoja na uhuru wa kutoa maoni katika jengo hili, kwa hali yoyote ninaiomba ofisi yako tukufu ihakikishe kwa hali yoyote, ninarudia suala la Muungano lilindwe kwa nguvu zote na kusiwe na namna ya kudhihaki jitihada zilizooneshwa na Viongozi wetu wa asili; Mzee Karume na Mwalimu Nyerere; historia itatuadhibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeelewa wazi kabisa kwamba, kuna wenzetu hawana nia njema, lazima utaratibu uwekwe wa kutangulia kuona njama zao zikiwemo za kuandaa maandamano, kurubuni vijana vyuoni na kudanganya watu kupitia mikutano yao mbalimbali. Aidha, nitahadharishe kwamba; ni vyema Vikao vya Kero za Muungano vifanye maamuzi ya haraka na utekelezaji wake uelezwe kwa umma, kwani ni miongoni

mwa mwanya unaotumiwa kutaka kuvunja muungano. Hakuna namna yoyote ya kuwa na mbadala wa maisha bora, usalama na utulivu katika nchi hii kama Muungano utavunjwa.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu suala hili litaguswa katika majumuisho na kuwapa moyo Watanzania wenye imani na Muungano kuwa ndiyo usalama na mhimili pekee wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote, mimi na Wananchi wa Jimbo la Amani Zanzibar, tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri, iliyogusa maeneo mengi muhimu na yenye kuleta matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo muhimu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyagusa ni Kilimo Kwanza, ikiwa ni pamoja na Kilimo cha Mazao, Ufugaji na Uvuvi. Aidha, amegusia ukuzaji wa viwanda vidogovidogo, maliasili na kadhalika ili maeneo haya yaweze kuwa na mchango wa tija na endelevu ni vizuri utafiti upewe kipaumbele. Kwa bahati mbaya, utafiti hautajwi kabisa katika hotuba ya Waziri Mkuu. Je, utafiti una nafasi gani katika maendeleo yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa miaka kadhaa sasa kumekuwa na ongezeko la migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji hususan kutokana na ongezeko kubwa la watu na mifugo wakati eneo la ardhi linazidi kupungua.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza au kupunguza ukubwa wa tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuunga mkono hoja asilimia kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri, yenye mantiki, sambamba na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia eneo la Muungano. Muungano wetu ni muhimu sana katika nchi zetu kwa sababu wahenga walisema "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu." Katika Muungano huu kuna mambo machache ambayo yanaitwa Kero za Muungano. Ninaishauri Serikali yetu ifuatilie kwa kina na udhati ili iweze kuweka sawa kero hizi na kuzitafutia ufumbuzi ili Wananchi wetu wasiwe na wasiwasi na Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, anayekataa Muungano hajaelewa maana yake, kwa hiyo, ninaiomba Serikali itoe elimu juu ya Muungano wetu ili Wananchi wauelewe uzidi kunawiri siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, bila ya Muungano sisi Wananchi wa Zanzibar tusingeweza kuwa na amani na utulivu tulionao. Serikali ya Muungano ndiyo imetupa nguvu ya ulinzi katika kuijenga Zanzibar, tofauti na wanachokiongelea wengine kwamba, Muungano unaimeza Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kitu muhimu kinachotakiwa ni ufuatiliaji na utekelezaji wa maamuzi muhimu.

Mheshimiwa Spika, ninaupongeza Muungano wetu na ninauombea udumu milele na milele.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia Hotuba Waziri Mkuu kuhusu Muundo wa kupeleka madaraka yote ya Kiserikali kwa Wakurugenzi wa Wilaya, ambapo kazi zimekuwa nyingi sana kwenye Halmashauri, yaani Miradi ya Maendeleo mingine haifanyiki na kuwa viporo kwa mwaka wa fedha mwingine, jambo ambalo halileti tija thabiti ya maendeleo kwa kuzingatia muda wa utekelezaji wa Mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mbeya kuna baadhi ya fedha zimerudi na hazijatumika hasa kwenye Idara ya Kilimo na Miradi yake. Hali hii siyo sahihi, hatuwatendei haki Wananchi wetu kwa kuwa na visingizio vingi kwa Watendaji.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Ofisi ya Waziri Mkuu igawanywe kwa baadhi ya Watendaji, wawe kazi yao ni kufuatilia utekelezaji wa Miradi iliyopo kwenye Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni pana sana na inabidi igawanywe kuwa Wilaya mbili; na kwa kuwa mchakato wa kupata Wilaya mpya ulishaanza pale Mji wa Mkwajuni ambapo ndiyo Makao Makuu ya Jimbo langu la Songwe; tunaomba basi tupatiwe hadhi ya Mji Mdogo pale Mkwajuni ili kurahisisha utekelezaji kazi za Serikali na kurahisisha utoaji huduma mbalimbali kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI, inatoa fedha kidogo sana kwa Mradi wa Barabara zinazoshughulikiwa na Halmashauri ya Chunya, ambapo mpaka sasa zilitengwa shilingi 60,000,000, kwa matengenezo ya Barabara za Kapalala – Udinde – Rukwa Km.10 na Kapalala – Gua Km. 35, pia Vijiji vya Kapalala – Ngwala Km. 46, jumla ni kilomita 91; je, fedha hizo zinatosha?

Ninaiomba Serikali iongeze mgao wa fedha za matengenezo ya barabara kwenye Halmashauri ya Chunya kwenye Vijiji hivi.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zipo mpaka sasa ila hakuna Mkandarasi anayekubali kutoa vifaa vyake toka Mjini Mbeya mpaka Vijiji hivyo vya Kapalala,

Kininga, Gua, Udinde na Ngwala, kwa kutengeneza barabara Km. 91 kwa milioni sitini. Ninaomba bajeti iongezwe Wilaya ya Chunya kwenye Miradi ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake kwa kiasi fulani lakini kuna jambo moja muhimu ambalo ninapenda kwa njia hii ya maandishi liangaliwe vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kama mimi ningekuwa na mamlaka ya uamuzi, ningeweka kipaumbele kwenye mambo yafuatayo:-

Kwanza, viwanda: Viwanda vinatoa ajira kubwa kwa kutumia malighafi ambazo zinazalishwa na Wananchi, kwa maana hiyo kiwanda kitakuwa ni soko la kununua mazao ya wakulima kwa bei nzuri vilevile ajira zitaongezeka na biashara zitaimarika.

Pili, uvuvi: Kinachohitajika katika uvuvi ni zana tu za mvuvi na kutafuta soko, hii italeta tija kubwa sana kwa Taifa na hivyo kukuza uchumi wetu.

Tatu, Usafiri wa Anga: Kuanza na kusimamia usafiri wa anga ni muhimu sana. Hii ni Sekta inayoingiza mapato makubwa katika Taifa letu na ni rahisi kujenga uhusiano na Mataifa mengine ulimwenguni. Uchumi utapanda kwa kasi.

Nne, Bandari: Bandari kazi yake ni ndogo sana; ni kuweka miundombinu mizuri tu na kutoa huduma nzuri. Ninaomba Taifa liweke mbele vipaumbele vinne na kuwa makini sana katika kipindi chote cha miaka minne.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Timu yake yote, kwa kuandaa Hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora ni kati ya Mikoa mitatu hapa Tanzania ambayo bado iko nyuma sana katika huduma za Afya. Tabora ya leo bado akina mama wengi wajawazito na watoto, wanapoteza maisha kila leo kwa idadi kubwa. Sababu kubwa ya vifo hivyo ni kukosekana kwa huduma muhimu kwenye hospitali zilizopo, uchache wa vituo vya afya, kukosekana kwa wahudumu wa afya wa kutosha kwenye vituo vichache vilivyopo na kukosekana kwa usafiri wa magari ya wagonjwa wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya za Mkoa wa Tabora, vituo vya huduma kwa mama na mtoto ni vichache sana vijijini na maeneo mengine kuna *Mobile Clinics.* Hizi *Mobile Clinics* zinakuwepo tu pale usafiri unapopatikana. Kutokana na shida ya usafiri,

inaweza kupita miezi mitano hadi sita, hawajapata huduma hiyo kwenye maeneo yao. Wajawazito wanafika kujifungua hawajapimwa hata kama wana tatizo halitajulikana.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Urambo haina gari la wagonjwa, wanategemea gari moja linaloharibika mara kwa mara na halina uhakika. Mgonjwa akilazimika kutumia gari hilo analipishwa pesa ya mafuta ndipo achukuliwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali itueleze imeandaa mkakati gani wa dhati wa kusaidia Sekta ya Afya kwa Mkoa wa Tabora na Wilaya zake ili kuokoa maisha ya Wananchi yanayoangamia kila leo.

Mheshimiwa Spika, mifugo ni rasilimali kubwa sana na inayoweza kuchangia Pato la Taifa kama ikitumiwa vizuri. Katika Taarifa ya Kikundi Kazi *(Task Force),* iliyoundwa kuangalia suala la wafugaji wanaoambiwa wapo katika hifadhi maeneo mbalimbali Mkoani Tabora, mwaka 2009 waligundua kwamba, zaidi ya moja ya tatu ya Vijiji vya Wilaya za Urambo, Nzega, Uyui na Igalula wameishi kwenye maeneo ya hifadhi zaidi ya miaka 20 - 30 na vimesajiliwa na Serikali imepeleka huduma zote za jamii ikiwepo shule, vituo vya afya, maji na kadhalika. Ilikubaliwa kwenye kikao cha pamoja hapa Dodoma, Viongozi wote wa Mkoa wa Tabora, Wabunge na Waziri wa Maliasili kwamba, Serikali iandae utaratibu mzuri wa kuainisha mipaka ya hifadhi na kuandaa maeneo ya kuwahamishia Wananchi waliohifadhi na kuweka miundombinu kwanza, kwenye maeneo mapya.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa alitamka kwenye kikao kwamba, hakuna Operesheni ya Kuhamisha Wafugaji itakayoendeshwa bila maandalizi yote ya msingi kukamilika Aprili mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba, Mkuu wa Wilaya ya Urambo, anaagiza Polisi, Afisa Wanyamapori na Mgambo wa Urambo kwenda maeneo ya vijiji vya wafugaji kukusanya ng’ombe bila utaratibu, kukusanya eneo moja kwa siku tano tangu 24 Mei, 2011 – 29 Mei, 2011 bila kula wala kunywa. Askari Polisi wa Kituo cha Urambo wamewaua ng’ombe saba kwa risasi wakati wa kuwaswaga. Siku walipowafungua, baada ya haki za binadamu kufuatilia na Viongozi wa CUF kufuatilia, kwa sababu ya kiu na njaa ya muda mrefu, zaidi ya ng’ombe 15 wamekufa wakinywa maji. Je, huu ni uchumi tunaoutafuta?

Huyu *DC* ni Kiongozi tunayeweza kumtegemea kuleta maendeleo ya Wilaya. Mkuu wa Wilaya anawafanya wafugaji ni vitega uchumi vyake. Anatumia nafasi yake kwenda kwenye mazizi ya wafugaji na kufanya lolote, ikiwemo kuchukua hata mbuzi wa wafugaji kwamba, anakwenda kula. Serikali iangalie sana Watendaji wa Wilaya ya Urambo na suala zima la mifugo, kwani linaweza kuvuruga amani. Wananchi wamechoka.

Mheshimiwa Spika, suala la Watendaji wa Halmashauri zetu kutokuwajibika ni tatizo kubwa linalotufanya kupiga *mark-time* kwenye maendeleo yetu. Miradi ya Maendeleo haipigi hatua kwa sababu Viongozi hawawajibiki, hakuna uzalendo, ubinafsi

umezidi. Watendaji wanaangalia maslahi yao na siyo ya Taifa. Fedha nyingi zinatafunwa Wilayani, zinafanya vikao, semina, makongamano na kujaza mafuta kwenye magari, kinachokwenda kwenye Mradi ni kidogo sana. Hakuna ufuatiliaji wa karibu kwa wakandarasi, Viongozi/Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mbalimbali wanakaa maofisini hawaendi *field* kuangalia kazi zinazofanyika. Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali iandae utaratibu wa kuhakikisha Watendaji wanawajibika, kuwepo tathmini ya Miradi ndani ya Wilaya zetu na thamani ya Mradi *(value for money).*

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi wa Taifa (Ukurasa wa159), unaeleza kwamba, mwaka 2010, Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo ilitoa mikopo 30 ya matrekta madogo ya mikono ikilinganishwa na mikopo 57 mwaka 2009. Aidha, mikopo 89 ya matrekta makubwa ilitolewa mwaka 2010, ikilinganishwa na mikopo 165 mwaka 2010. Kupungua kwa mikopo hiyo kulitokana na ufinyu wa bajeti. Je, huu ndiyo utekelezaji wa Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Spika, Vocha za Pembejeo za Kilimo zinavyotolewa kwa wakulima vijijini nyingi zinauzwa na wale wanaozisimamia wakiwemo Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji. Wamefanya hii ni biashara yao na wakulima wanabaki wanalalamika huku malengo ya kilimo yakiwa yanarudi nyuma. Lazima hatua kali zichukuliwe dhidi ya Watendaji hawa wanaodumaza kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kutowalipa Wastaafu wa Afrika Mashariki, stahili zao kwa muda wote huu ni kuendelea kuwatesa watu ambao wametumika kujenga Taifa hili. Katika nchi za wenzetu, wazee wanathaminiwa kwa michango yao ndani ya Taifa/Mataifa yao wakati wa utumishi wao, ndiyo maana wanapewa kila kitu bure kuanzia nyumba za kuishi, huduma za afya na huduma nyingine.

Tunaonesha taswira gani kwa wazee hawa kulala barabarani na kumwagiwa maji machafu na kupigwa na polisi? Hatuoni hii ni aibu katika nchi ya amani lakini haijali wastaafu? Serikali iondoe aibu hii.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali iamue kwa dhati kuachana na madai ya wastaafu wa muda mrefu kwa kutenga fedha ndani ya Bajeti ya mwaka huu. Neno hili "madai ya wastaafu" tuachane nalo tuangalie masuala mengine.

Mheshimiwa Spika, kujenga ujuzi wa vijana wetu ni suala la kuangalia kwa umakini mkubwa sana *(this is a timing bom)*, tunapambana na madawa ya kulevya, wizi, wazururaji uporaji na kadhalika. Haya yote yanasababishwa na vijana wengi kutokuwa na kazi za kufanya, wanajikuta kwenye matendo yasiyostahili kwa jamii. Lazima Serikali iandae utaratibu wa kuhakikisha Vijana wa Tanzania popote walipo, wanajulikana wanafanya nini. Taifa lisiloangalia vijana ambao ndiyo asilimia kubwa ni Taifa ambalo haliwezi kwenda haraka kwenye maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeagiza Vyuo vya *VETA* kutochukua vijana wasiokuwa na Elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita kupata mafunzo. Miaka ya nyuma, wale vijana waliomaliza Darasa la Saba na hawakupata fursa ya kupata Elimu ya Sekondari waliweza kupata staid za kazi kwenye Vyuo vya *VETA.* Tunaomba Waziri Mkuu atueleze ameandaa utaratibu gani kwa vijana waliomaliza darasa la saba *(Std.VII)* na hawakupata fursa za kufika sekondari na hawapokelewi *VETA?* Huku siyo kuwanyima fursa za maisha watoto wa maskini waliokosa kwenda sekondari?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuandaa na kuwasilisha hoja kwa umahiri. Pongezi hizi ziwaendee pia Maafisa Waandamizi na Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ya kuandaa hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri mengi ambayo Serikali yetu imemudu kuyatekeleza katika Jimbo langu la Bagamoyo, chini ya usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kuna changamoto kadhaa ambazo bado zinatukabili. Awali ni tatizo la uhaba wa huduma ya afya; bado vijiji kadhaa havina Zahanati. Mfano, Vijiji vya Kitupeni, Kitonga, Buma, Pande, Matimbwa, Chasimba, Kondo na Buyuni. Wananchi katika maeneo hayo, wanaendelea kuteseka sana. Pia katika Vijiji vyenye Zahanati, vingi vinakabiliwa na upungufu wa madawa na vitendea kazi. Zahanati ya Kerege iko mita kama kumi toka nguzo ya umeme; ajabu ni kuwa, Halmashauri kwa miaka kadhaa sasa imeshindwa kuifungia umeme hata baada ya Msukumo wa Mbunge. Tunaomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, itusaidie.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 31 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametaja umuhimu wa eneo la *SEZ* la Bagamoyo, lakini changamoto kubwa ya Wananchi wanaohusika na maeneo hayo ni fidia ya ardhi, mazao na mali zao. Sasa ni muda mrefu Wananchi wamezuiliwa maendelezo yoyote katika maeneo hayo na wala wasiuze ardhi zao hizo, lakini fidia hawapati. Serikali itenge fedha za kuwalipa fidia Wananchi hawa ambao wanapata hisia za kuonewa.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, tulipata bahati ya kuwekewa nguzo kuu za umeme katika Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Bagamoyo. Umeme huu unapita katika Vijiji vingi vya Kata za Kerege, Zinga na Kiromo, lakini Wananchi wanaofaidika ni wale wa njiani tu. Mita chache toka njiani, gharama yake kuvuta umeme haishikiki. *TANESCO* waongeze usambazaji angalau laini moja moja kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima sana, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri Mkuu na Waziri wa TAMISEMI, kwa Hotuba zao nzuri.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo tofauti kisekta:-

Kwanza, utendaji kazi wa Halmashauri za Wilaya:-

(a) Halmashauri za Wilaya nyingi tenda zinachukuliwa na Madiwani kwa kubadilisha majina ya Makampuni ya marafiki. Ninaomba Serikali ilichunguze hili kwa makini. Kazi nyingi zinazofanywa na Madiwani hawa (Miradi ya Serikali), haikamiliki vizuri na Watendaji wa Vijiji na Kata hawathubutu kusema.

(b) Tenda za kukusanya mapato katika minada zinachukuliwa pia na Wakurugenzi wa majina ya ndugu (Halmashauri ya Wilaya nyingine siyo zote). Muhimu Serikali izichunguze pia hizi.

(c) *CAG* ametaja Halmashauri za Wilaya 60 ambazo hawafuati Kanuni na Taratibu za Manunuzi. Ninashauri *Procurement Officers* wa Halmashauri ya Wilaya wapewe elimu ya kazi hiyo. Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 irekebishwe ili Mkurugenzi wa Bodi apewe mamlaka ya kufanya ukaguzi wa *Supplies* kama anavyofanya *CAG* ili kujua mali iliyonunuliwa, iliyotumika na iliyobaki.

(d) *CAG* awe pia mwangalifu na makini kwa sababu vipo vitendo vya rushwa vinavyofanywa na Wakurugenzi kuwapa Wakaguzi wa nje walioko mikoani fedha ili kuepusha Hati Chafu. Ikiwezekana, *Auditors* wawe wanatoka Mikoa tofauti na Halmashauri zao.

(e) Mheshimiwa Spika, inaelekea Serikali itaweka mkazo juu ya kilimo katika Nyanda za Juu Kusini, kwa Mpango wa *SAGCOT*. Mkoa wa Kilimanjaro una sehemu za umwagiliaji za Lower Moshi, Kaloleni na maeneo ya Miwaleni; ni Mkoa unaokumbwa sana na mabadiliko ya tabia nchi na janga la njaa.

- Ukanda wa juu una watu wengi, unahitaji maji ya kumwagilia mazao na kuosha kahawa.

- Ukanda wa chini kuna kilimo cha mahindi, mpunga na miwa.

- Kuongeza nguvu katika kilimo Mkoani Kilimanjaro kutaongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya bustani; mfano, mboga, matunda, maua, viungo na kahawa, ambayo inaleta fedha za nje *(Foreign Exchange*) nchini.

- Mradi wa Lower Moshi unaojumisha Vijiji vya Mandaka, Mneno na Kaloleni ni vyema utiliwe mkazo (hekta 2300), kuondoa tatizo la upungufu wa maji.

- Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo; hekta milioni 10.4 tu ndiyo zinalimwa.

- Kuna umuhimu Serikali iwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza ajira, lakini pia kuondoa tatizo la ukame linalosababisha upungufu wa chakula.

Pili, Vyama vya Ushirika:-

Mheshimiwa Spika, yapo mashamba makubwa ya kahawa 41 yanayomilikiwa na Vyama vya Ushirika katika Wilaya ya Moshi Vijijini 16; Wilaya ya Hai 18; na wilaya ya Siha 7. Yapo pia mashamba mawili ya Serikali (NAFCO – West Kilimanjaro na TALIRO); mashamba 14 yana uwekezaji mbovu usiokuwa na maslahi kwa Vyama vya Ushirika; mashamba 12 mikataba yake ya uwekezaji ni mibovu. Kuna haja Serikali kuingilia migogoro hiyo ili pato la kahawa liendelee kuwa zuri na Wananchi wafaidike. Kamati ya Ushauri ya Mkoa iliyokaa 3 Desemba, 2008 na kutolewa mapendekezo 2009 na 21 Januari 2010, haijazaa matunda. Pato la kahawa linazidi kudidimia na matumizi ya Kiwanda cha *Coffee Curing* yanazidi kuwa madogo *(Under Utilized).* Vyama vya Ushirika ni vingi na wafanyakazi wachache.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mkoa wa Kilimanjaro unakabiliwa na tatizo kubwa la mabadiliko ya Tabia nchi. Profesa mmoja wa Chuo cha Ohio Marekani alitafiti na kusema, mpaka 2015 barafu kileleni mwa Mlima Kilimanjaro itakuwa imeyeyuka. Watafiti wengine wanasema ni 2025. Mwaka 2009, maporomoko ya ardhi yaliua watu 24 Wilaya ya Same. Maeneo ambayo yanaweza kutokea maporomoko mengine yapo mengi Mkoani Kilimanjaro, kwa sababu ya asili *(nature)* ya milima ya mkoa. Mfano, Wilaya ya Mwanga, Wilaya ya Moshi Vijijini maeneo ya Kilema, Wilaya ya Rombo na Hai. Ipo haja ya Serikali kulichukulia jambo hili kwa umuhimu, ielimishe Wananchi wawe na tahadhari.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mkomazi na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni vivutio vikubwa vya utalii. Ninashauri Serikali iwekeze katika Kiwanja cha Ndege cha KIA ili kiendane na wimbi la watalii wanaokuja nchini na hasa Ukanda wa Kaskazini. Ipo haja pia ya kununua ndege/kukarabati ndege zetu ili ziweze kusafirisha watalii hata kama safari za ndani. Nchi ya jirani Kenya inajenga Uwanja wa Ndege Holili mpakani na Mkoa wa Kilimanjaro. Baada ya ufunguzi wa Soko la Afrika Mashariki, watalii wngi watapitia Nairobi washuke Holili na hatimaye kupanda Mlima Kilimanjaro na kutembelea Hifadhi ya Mkomazi na nyinginezo. Ninashauri Serikali ilitilie hili umuhimu.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya Magunia, Ngozi na *Machine Tools* Mkoani Kilimanjaro, havifanyi kazi. Viwanda vya Magunia na Ngozi vilibinafsishwa, wawekezaji hawavitumii ipasavyo na Wananchi hawafahamu Mikataba inasema nini. Ninaishauri Serikali ihimize *Consolidated Holding Corporation (CHC),* ambao walichukua jukumu la *PSRC* kupitia Mikataba ya Ubinafsishaji wa Viwanda hivi na kuchukua hatua muhimu. Aidha, warudishe Serikalini au wavifungue ili Watanzania wapate ajira na kipato kwa Serikali.

Ninaishauri Serikali kupitia *NDC,* wakifungue Kiwanda cha *Machine Tools* ili kisaidie pia ajira na nyenzo kwa viwanda vingine nchini.

Mheshimiwa Spika, Walimu wengi wa Shule za Msingi na Sekondari Mkoani Kilimanjaro wamestaafu. Ninaishauri Serikali itoe Waraka, Walimu hawa warudishwe kwenye *system* hata kama kwa fedha kidogo ili wasaidie nguvu kazi katika shule hizo.

Shule za Ashira, Weruweru na Machame ambazo ni kongwe, zimelengwa kama Shule za Sayansi za Wasichana. Ninaishauri Serikali ipeleke Walimu wa Sayansi ili azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM), kuweka asilimia 50 kwa 50 Serikalini na Bungeni itimie. Serikali/Taifa la Tanzania linahitaji Wataalamu Wanawake. Ninaipongeza Serikali kwa Sera yake ya kujenga Sekondari za Kata. Shule hivi ni za msaada mkubwa. Ninaishauri Serikali iwekeze sasa katika kupeleka wanafunzi wengi Vyuo vya Ualimu. Serikali ilichukulie hili kwa umuhimu, kila mwanafunzi anayeingia chuoni awe na *Bond* na Serikali kuwa ataifanyia kazi kwa muda wa miaka mitatu kabla hajatafuta kazi mahali popote pengine nchini na nje ya nchi. Mfumo huu uta-*stabilize* ajira za Walimu, Madaktari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maadili ya watoto wetu yameporomoka sana; ni wepesi kudanganyika; na ni wepesi kufuata mkumbo. Hata Bungeni (Bunge la Kumi); ni mfano halisi wa Wabunge wengine vijana; hata kuchagua lugha za kuongea mbele ya Bunge au kadamnasi ni vigumu; ninaishauri Serikali iharakishe mchakato wa kuweka Sheria, Jeshi la Kujenga Taifa lianze.

Mheshimiwa Spika, Soko la Afrika Mashariki limeanza wakati bado elimu haijatolewa kwa Wananchi kuhusu fursa na changamoto za soko hili. Nilishuhudia wafanyabiashara toka Kenya wakiingia Vijijini Mkoani Kilimanjaro, kuangua maparachichi kwa bei ya shilingi elfu ishirini kwa gunia lenye maparachichi zaidi ya 300. Wafanyabiashara hawa wananunua kwa bei ya mkulima siyo ya soko. Yapo maeneo mengine, wageni wamefunga ndoa za kigezo kwa kupata ardhi tu. Ninaishauri Serikali itoe elimu na hasa katika mikoa iliyoko majirani na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari Dar es Salaam litapunguza kukua kwa uchumi nchini. Jambo la kufanywa kwa saa mbili, lazima linafanywa kwa saa nne kwa sababu ya foleni. Serikali ilifanyie kazi tatizo la foleni lililoko Dar es Salaam. Huu ni Mji Mkuu wa Biashara, ambapo pato takriban, asilimia 85 linapatikana hapa.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya KCMC ni ya Rufaa kwa Watanzania wote. Hospitali hii ipo Mkoani Kilimanjaro. Kuna haja Serikali isaidie kuiboresha ili iwe *Super Hospital*, itakayotibu magonjwa mengi kutokana na wataalamu waliobobea. Ni vyema basi Hospitali ya Mkoa, yaani Hospitali ya Mawenzi, ikarabatiwe vizuri iweze kupokea wagonjwa wote wanaotoka katika Wilaya zote saba za Mkoa. Hospitali hii ukarabati wake uwe ni pamoja na Wodi ya Wazazi na *Theatre* za *Operations.*

Zipo Hospitali za Wilaya mfano, Moshi Vijijini (Himo), ambayo haina mashine za *X-ray.* Hospital hii inahudumia zaidi ya wakazi elfu tano.

Vibali vya kuajiri wafanyakazi takriban 68 vyote vime-expire bila wafanyakazi kupatikana. Katika Hospitali ya Mkoa na hata za Wilaya, hakuna *Specialists.* Serikali ipunguze msongamano katika Hospitali za Rufaa kama *KCMC* na Muhimbili, kwa kuajiri wataalam katika Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya. Msongamano ukipungua, ufanisi utakuwa wa kiwango kizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM); imefanya mengi mazuri. Kazi kubwa, tusimamie utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, ambako Serikali inapeleka fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walio chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuwajengea Ofisi Majimboni, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, lakini hadi sasa hali inaonekana ni tofauti kabisa, kwani haieleweki kama azma hii ya Serikali bado ipo katika mipango yake. Katika Kisiwa cha Pemba, Serikali iliweza kujenga baadhi ya Ofisi katika Majimbo, ambapo nyingine zimeonesha kukamilika na baadhi bado kabisa. La kusikitisha zaidi ni kwamba, hakuna *activities* zozote zinazoendelea. Vilevile hakuna ishara yoyote ya dhati au dhamira ya kuonesha kwamba, mpango huu bado upo.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri Mkuu, haikuonesha kabisa dhamira ya ujenzi au umaliziaji wa Ofisi hizi Majimboni, kwani hata katika Vitabu vya Bajeti vinaonesha ya kwamba, hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge Majimboni.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri Mkuu, alieleze Bunge hili ni nini kinachosababisha au kukwamisha ujenzi huo, pia kuhamiwa kwa baadhi ya Ofisi ambazo zimekamilika kama vile Mkoani na Chake Chake katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri Mkuu, afahamu ya kwamba, unapompatia Mbunge Ofisi ya kufanyia kazi, basi utakuwa umelipa heshima Bunge na Mbunge mwenyewe. Ieleweke ya kwamba, Wabunge na wao wanalipa kodi kila mwezi kutoka katika mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wengi Serikalini wana mawazo mabaya kwa kuona ajira ya Serikali ni kitu cha kawaida tu, hawajali muda wa kuingia/kutoka kazini na wala hawaheshimu maadili ya kazi zao. Ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kufanya ziara za makusudi katika Wizara zote na kukumbusha majukumu kwa Watendaji. Hali kadhalika, Waziri Mkuu kwa Semina Elekezi kwa Wakuu wa Mikoa. Vilevile Katibu Mkuu Kiongozi alipokuwa anafungua Maonesho ya Utumishi, alitoa nasaha zenye mwelekeo wa kuwaeleza Watendaji ni nini Watanzania wanachohitaji kukiona.

Ninamwomba Waziri Mkuu, aipe makali zaidi Kamati ya Maadili, mbali ya kuangalia mali tu za Viongozi, lakini wawe na tabia ya kupita katika Ofisi za Serikali na kuangalia utendaji na uwajibikaji katika maeneo ya kazi, kwa kuanzia kwa Mawaziri hadi Watendaji/Waajiriwa wa chini kabisa. Hii ni pamoja na kuangalia muda wa kila mwajiriwa na kazi anayoifanyia Taifa hili na ni tija gani anayochangia Taifa hili kutokana na ajira yake.

Mheshimiwa Spika, sasa muda umefika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, kusimamia na kutoa kauli juu ya ujangiri ambao unalitafuna Taifa letu. Wimbi hili la ujangiri ni lile la baadhi ya watu wazima kuwalawiti vijana wadogo, watoto wetu, ambao ndiyo nguvu kazi yetu ya kesho. Kuna baadhi ya nchi tayari zimeingia katika matatizo makubwa, baada ya baadhi ya Wananchi ambao wanadai kutungwa Sheria ya Kuwaruhusu Watu wa Jinsia Moja Kuoana. Hili haliji tu kwa bahati mbaya, bali chanzo chake ni vitendo vibaya ambavyo hufanyiwa watoto wetu na hususan watoto wa mitaani, ambao hurubuniwa kwa pipi na senti kidogo tu. Baya zaidi ni kwamba, hata pale kesi zinapofikishwa katika Vyombo vya Sheria, hatua za dhati za kimahakama hucheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, kesi za aina hii zimekuwa ni nyingi na hazipatiwi ufumbuzi kwa muda mrefu. Ripoti inayotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuhusu vitendo ambavyo wanafanyiwa watoto inatisha. Matendo haya yamewaathiri sana watoto wetu na kuwatia katika Janga la Ukimwi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe karipio kali kwa wale wote ambao wanawafanyia watoto wetu vitendo hivi vibaya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zaidi ya miaka minne sasa, nchi yetu imekumbwa na mauaji makubwa ya albino, tena ya aibu, ambayo yameliletea Taifa letu aibu. Pamoja na juhudi za Serikali kuwapeleka mahakamani wahusika wachache wa mauaji hayo; ni vyema Serikali ichukue hatua za makusudi na haraka, kuitisha Vyombo vya Kimataifa kama Scortland Yard au Inter Pool, kuchunguza mauaji hayo ili kama Taifa lijiridhishe.

Tunaamini kuna baadhi ya wahusika walioshiriki mauaji hayo, hawakuhusishwa katika kesi zilizopo mahakamani, yaani ni wale ambao walikuwa wanawatuma hao walioko mahakamani kukamilisha azma yao ya ukatili huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi katika Taifa letu, juu ya vigezo vinavyotumiwa katika kugawana rasilimali kwa maendeleo ya Taifa letu. Lindi ni kati ya mikoa ambayo ina mchango mkubwa katika maendeleo, lakini ni mkoa ambao uko nyuma kimaendeleo na hakuna juhudi za makusudi kuleta msukumo wa maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Spika, bajeti zaidi ya vipindi vitatu haioneshi dhamira ya kuukwamua Mkoa huu ambao ni wa mwisho katika bajeti ya kila mwaka wa fedha. Ushauri wangu ni kwamba, kuwe na upendeleo wa makusudi, kuongezewa bajeti yake kama ilivyoelezwa katika kauli za Viongozi kuwa, tutatoa upendeleo wa makusudi kwa maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, stakabadhi ghalani ni mfumo ambao ninafikiri ulikuwa ni dharura ili kumuwezesha mkulima kupata bei bora ya mazao yao, lakini leo imekuwa kinyume kwa matarajio ya Wananchi na Watendaji Wakuu, waliopewa dhamana, wanatumia fursa ya mpango huu kujitajirisha kupitia fursa hii ambayo ipo kisheria. Muhimu hapa Serikali ikutane na Wadau, kuangalia upya matatizo yanayotokana na malalamiko ya wakulima wa ufuta/korosho, kuna mambo kadhaa yanahitaji kuangaliwa upya; mfano, makato kwa mkulima ni makubwa; kuingiliwa kwa Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika; Wanachama wa Vyama vya Ushirika vya Msingi kutokuhusishwa katika maamuzi yanayohusu mambo yao; na mnada wa mazao katika *Warehouse Receipt* unaofanywa kwa siri na mzabuni anayeshinda hulalamikiwa na wazabuni wengine.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa wakulima wakawa huru katika kutafuta bei za mazao yao kwa njia ya amani kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Rais hazijatekelezwa kwa asilimia kubwa katika awamu zote. Hali hii inakatisha tamaa na kupoteza matumaini. Rais wa Awamu ya Nne, ametoa ahadi nyingi kwa Wananchi wa Lindi kama vile ujenzi wa Bandari, Soko Kuu, Mradi wa Maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa imeonekana nafasi za ajira katika majeshi yetu ni za upendeleo mkubwa, kiasi Majeshi ya Polisi, Magereza na JWTZ, yanaathiriwa na familia zile zile, kwani kama Askari wa juu anaposimamia dhamana ya ajira, kinachofanyika pale ni namna gani atawaajiri aidha watu wa karibu yake au wakubwa walio juu yake. Hatari iliyopo mbele yetu ni kwamba, itafikia mahali majeshi haya yatakosa sura ya kitaifa; ni hatari kwa usalama na amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, turudie utaratibu wa awali ambao tulisajili vijana wetu kujiunga na majeshi yetu kupitia Serikali za Vijiji/Mitaa, huko ndiko tunaweza kupata vijana wazuri na wazalendo na siyo utaratibu wa sasa kupata vijana wa kutoka mijini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake iliyo wazi, ina mambo kadhaa yaliyo mazuri, ingawa sikubaliani na baadhi ya mambo yanayosemwa. Ninampongeza Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa CHADEMA na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa Hotuba yake, yenye mwelekeo sahihi wa kisiasa na

kimaendeleo, unaozingatia utatuzi wa changamoto zinazotukabili. Ninawapongeza Wabunge wa CCM, ambao hawana ushabiki wa Chama na ambao badala ya kukaa tukishangilia maendeleo tuliyoyapata katika miaka 50, wanaelekeza umakini wao kwenye changamoto zinazolikabili Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuanza kuchangia kwa kuzungumzia kidogo fikra iliyoenea humu Bungeni kwamba, wapo Wapinzani ambao wanadai kwamba, hakuna lolote ambalo limefanyika toka tupate Uhuru. Ninapingana na fikra hii, hakuna ukweli wowote katika jambo hili. Kwa ufahamu wangu, si *CHADEMA, TLP, UDP, NCCR* wala *CUF* wamesema kuwa, hakuna lolote lililofanyika toka tupate Uhuru. Nitadondoa mafungu machache kutoka kwenye Ilani ya CHADEMA ili kuweka wazi kuwa CHADEMA haibezi maendeleo yaliyopatikana hapa nchini toka tupate Uhuru.

Dondoo 1: "Tukiamua kwa dhati…tuna uwezo wa kubadili hali tuliyonayo kutoka Taifa linaloendelea taratibu na kuwa Taifa linaloendelea kwa kasi."

Dondoo 2: "Mafanikio mbalimbali yaliyopatikana tangu nchi yetu ipate Uhuru katika Sekta mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya, Miundombinu na Uchumi, bado hayaendani kabisa na hali halisi ya umri wetu kama nchi na rasilimali ambazo nchi imejaliwa…"
(Ukurasa wa 2, Ilani ya Uchaguzi Mkuu 2010).

Ni wazi kuwa kinachosemwa ni kuwa, maendeleo yamepatikana lakini si kwa kasi tuliyotarajia.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, nitajielekeza kwenye maeneo matatu: Elimu, maslahi ya Watumishi wa Umma na changamoto zinazoyakabili maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo mfano, Bukombe.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na elimu. Elimu tunayohusika nayo ni ya Shule ya Msingi, Shule ya Sekondari, Vyuo vinavyosimamiwa na *NACTE,* Vyuo vingine na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, suala la umuhimu wa kuboresha elimu limeongelewa na baadhi ya Wabunge. Ninakubaliana na mengi yaliyosemwa, ingawa mimi nina pendekezo tofauti. Ninapendekeza kwamba, tunapaswa kuifanya elimu iwe kipaumbele namba moja. Pendekezo hili linatokana na ukweli kwamba, changamoto zinazotukabili hapa ni ngumu na utatuzi wake unahitaji dhamira ya dhati, juhudi ya dhati na uwekezaji mwingi na wa muda mrefu.

Baadhi ya changamoto zinazoikabili elimu katika Taifa letu ni hizi zifuatazo: Majengo: Madarasa, maabara, maktaba, nyumba za Walimu na ofisi za walimu; Zana: Vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia. Upungufu mkubwa wa zana na samani (madawati); Lugha ya kufundishia: kuanzia sekondari hadi Vyuo Vikuu lugha ya kufundishia ambayo ni Kiingereza inawakwaza Wanafunzi na hata Walimu; Maslahi duni ya Walimu: Walimu wanaofundisha katika Shule za Serikali wana maslahi duni;

Upungufu wa Walimu: kwenye ngazi zote za elimu kuna upungufu wa Walimu. Kwa ujumla, upungufu huu husababishwa na mazingira mabovu shuleni na maslahi duni katika Shule za Serikali; kukosekana kwa Mpango wa Chakula Shule za Msingi na Shule za Sekondari za Kutwa; uwiano baina ya Walimu na Wanafunzi: Uwiano sasa hivi ni Mwalimu mmoja kwa Wanafunzi 80 hadi 100. Lengo ni Mwalimu mmoja kwa Wanafunzi 30.

Mheshimiwa Spika, ili kuinusuru elimu, hatua zifuatazo zichukuliwe:-

- Elimu iwe kipaumbele namba moja. Hili halitakuwa jambo geni kwani miaka ya 1961 - 85 elimu ilikuwa kipaumbele namba moja. Aidha, katika nchi nyingi duniani, elimu ni kipaumbele namba moja; mfano, China, Cuba na kadhalika.

- Hatua hiyo itatuwezesha kuwekeza katika majengo, zana, kutatua tatizo la lugha ya kufundishia, kuboresha maslahi ya walimu, kutatua tatizo la upungufu wa walimu na mpango kabambe wa chakula shuleni.

-

Mheshimiwa Spika, licha ya kuinusuru elimu yetu, sababu nyingine za kuipa elimu kipaumbele namba moja ni: Elimu ni msingi wa kuendelezea sekta nyingine mfano, Kilimo, Afya, Sayansi, Teknolojia na kadhalika. Pia ni msingi imara wa ukuaji endelevu wa uchumi; Elimu ni Sekta inayosaidia kupunguza tofauti baina ya walionacho na wasionacho. Elimu ikiwa bora na watu wengi vijijini na mijini wakaipata, watapata ajira au watajiajiri, kwa hiyo, watakuwa wamejinusuru na tatizo la kukosa ajira; Elimu yetu ikiwa bora tutakuwa tumeweka msingi mzuri wa kukuza ubunifu na ugunduzi katika nyanja zote; Elimu bora itakuwa ni msingi imara wa ushirikishaji na Utawala Bora; na Elimu bora itaweka msingi imara wa kuondoa tofauti za kijamii za kijinsia.

Hatua zilizotajwa hapo juu ziende sambamba na mabadiliko yafuatayo: Katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari, elimu itolewe bure. Katika Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu Wanafunzi wapewe mikopo; Vyuo vya Ufundi vijengwe kila Wilaya, kama ilivyopangwa na Serikali; Vyuo vya Ualimu vijengwe kila Mkoa (kila Mkoa chuo kimoja); na Mitaala yote itazamwe upya na kupitiwa ili iendane na haja ya kuwa na wahitimu wanaoweza kukabiliana na changamoto ya ushindani katika Soko la Afrika Mashariki, Afrika na Ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza kuwa, hakuna nchi ambayo imeendelea bila kuifanya elimu kipaumbele namba moja. Bila elimu bora, maendeleo ya nchi husuasua. Tuchukue hatua bila kuchelewa, tusipofanya hivyo tutajuta baadaye.

Mheshimiwa Spika, tumechunguza maslahi ya Watumishi wa Umma, yaani mishahara, marupurupu na mafao ya uzeeni, tumegundua mambo yafuatayo: Tofauti kubwa baina ya maslahi (mishahara, marupurupu, mafao ya uzeeni) ya tabaka la juu la watumishi (Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na kadhalika) na tabaka la chini la watumishi; na maslahi duni ya watumishi wa tabaka la chini, maslahi yasiyotosha hata kwa mahitaji muhimu kama chakula, huduma za afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza mfumo wa maslahi uangaliwe upya na kuundwa upya ili kuhakikisha kima cha chini cha mshahara kinapandishwa kufikia kile kinachoweza kumfanya mtumishi mfano, Mwalimu, Nesi na wengine, waweze kumudu maisha na kusomesha watoto. Watumishi ambao hawalipwi mishahara (Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji/Vitongoji), walipwe mshahara.

Jambo lingine linahusu tofauti za malipo ya mafao yatolewayo na Mifuko ya Pensheni *(PPF, LAPF, NSSF* na *PSPF),* ilhali makato ya watumishi wote ni yale yale. Mifuko inayotoa malipo makubwa zaidi ni ile ya *PSPF* na *LAPF*. Ninapendekeza kuwa malipo ya mafao kwa Mifuko yote, yakokotolewe kwa namna moja ili kuondoa tofauti zilizopo ambazo zimelalamikiwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho linahusu Utaratibu wa Pensheni wa *SSSS,* ambao uliwahusu Wafanyakazi wa Vyuo Vikuu kabla ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika mwaka 1977. Kwa mujibu wa utaratibu huu, mtumishi anapostaafu, hulipwa malipo ya mkupuo mmoja tu ambayo siyo makubwa. Pensheni ya kila mwezi hawapati. Huu ni ubaguzi na dhuluma ya ajabu katika nchi huru. Jambo hili lirekebishwe mara moja ili wale wote ambao wamestaafu kwa utaratibu huu, waingizwe kwenye utaratibu wa kulipwa pensheni ya kila mwezi. Vyuo Vikuu vinavyohusika ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge wameongelea maeneo yenye maendeleo duni. Maeneo yaliyotajwa ni Rukwa, Tabora na Kigoma. Ninapenda kusema kuwa, hata Bukombe imo kwenye kundi hili la maeneo yaliyosahaulika kimaendeleo. Bukombe inazo changamoto zifuatazo: haina maji safi na salama, haina barabara nzuri za kuunganisha kijiji na kijiji na vijiji vingine havina barabara kabisa, haina umeme, haina majosho na malambo, huduma za afya ni duni, kwani mara nyingi dawa katika vituo vya afya/zahanati na hospitali ya wilaya hazipo, Shule za Msingi na Sekondari zinakabiliwa na changamoto za majengo yasiyotosha, upungufu wa zana (vitabu) na kadhalika. Aidha, asilimia kubwa sana ya Wananchi wa Bukombe hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ifuate ushauri ambao umetolewa hapa Bungeni kuwa, iandae Mpango Maalum wa kuyasaidia maeneo haya ili yapate maji safi na salama, umeme, barabara zinazopitika wakati wote zinazounganisha vijiji, majosho na malambo kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Bukombe imesahaulika kwa muda mrefu; Serikali yetu igeuzie jicho lake Bukombe ili Wana-Bukombe nao wafahamu kuwa wana Serikali inayowajali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, nami ningependa kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninawapongeza wawasilishaji wote, *especially,* Hotuba ya Kambi ya Upinzani, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Waziri Kivuli na ninampongeza sana kwa ushauri wake mzuri katika Hotuba hiyo.

Ningependa kuchangia katika suala la Halmashauri mbalimbali, mimi ninapendekeza Wakurugenzi au Wenyeviti wa Halmashauri, wawe wanachukuliwa hatua pale inapobainika Halmashauri zao hazifanyi vizuri hadi kufikia hatua ya kupata Hati Chafu, kwani inarudisha nyuma nia ya Serikari ya kutaka kusaidia Wananchi na pia kuwanyima haki yao ya msingi; mfano mzuri ni katika Mkoa wa Ruvuma, Halmashauri zote zina Hati Chafu isipokuwa Halmashauri moja tu ya Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kugusia michango mashuleni. Kumekuwa na michango mingi sana mashuleni hasa katika Shule za Msingi na hata kuondoa ile maana ya elimu bure katika elimu ya awali, kwani wanafunzi wamekuwa wakitozwa michango. Mfano mzuri ni mchango wa madawati; kila mtoto anatoa mchango huo na cha kushangaza hayo madawati hayajawahi kutosha na bado wanakaa wawili hadi watatu katika dawati moja. Je, Serikali haioni kama inaonesha kutokuaminika kwa Wananchi wake au fedha hizo huwa ni chakula cha watu fulani na kama siyo chakula basi iainishe inafanyia nini hiyo fedha zaidi ya kununua hayo madawati ili mzazi aelewe anachangia kitu gani na siyo kuzungukana kwa kisingizio cha madawati.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuongelea suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya hii imekuwa na mambo mengi ambayo ni ya kuwakandamiza baadhi ya Wafanyakazi; mfano, *Professional Staff* wote wanapaswa kutumia au kumiliki Pasi za Kidiplomasia, lakini kwa Watanzania imekuwa kama ndoto kwa muda wa miaka minne sasa na zinatolewa sababu za chinichini ambazo haziridhishi. Mfano, suala hilo lipo ngazi ya juu linashughulikiwa. Mimi hii ninaona ni kama kuwadhalilisha Watanzania wanaofanya kazi hapo kwani ni haki yao na makubaliano kati ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Headquarters Host Agreement),* yanaainisha hivyo. Ninaomba suala hili lifuatiliwe kwa ukaribu na kufahamu ugumu uko wapi.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni Wafanyakazi wa Serikali au Makampuni kuonewa pindi wawapo maofisini na katika utaratibu mzima wa kuhamishwa kikazi. Hapa kuna uonevu mwingi unafanyika kutokana na sababu mbalimbali, aidha, kimapenzi, ninamaanisha mfanyakazi anapokataa kushiriki mahusiano na bosi kwa kuwa bosi ana mamlaka, anatishia kumhamisha mfanyakazi sehemu ambayo haina miundombinu, yeye akijua anamkomesha kwa kutokubali ombi lake au hata kutompandisha cheo kwa muda mrefu au kutengenezewa sababu ya kufukuzwa kazi. Hii haijengi familia bora na inaendeleza zaidi ongezeko la UKIMWI. Mfano; benki, walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ya Utumishi, ifuatilie na ipende kuwasikiliza zaidi wafanyakazi kwani ndiyo waathirika wakubwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Kilimo Kwanza liangaliwe kwa upana zaidi kama linavyotangazwa, kwani kilimo ni pembejeo za kutosha na kufaa ili mkulima awe na uhakika wa kupata mazao mwisho wa msimu. Mfano, *power tiller* hazimkwamui mkulima bali zinampotezea muda mwingi shambani, kwani haina nguvu ya kutosha kama ambavyo trekta linafanya. Nimeongea na baadhi ya Wakulima wa Maswa wanasema, hata kilimo cha maksai ni afadhali zaidi. Pili, Serikali kama inaona ruzuku ya mbolea ni kero kutokana na baadhi ya Watendaji kujinufaisha wao, wauze kwa bei ya chini madukani ili kila Mwananchi ajiamulie kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaishauri Serikali yetu iandae Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wetu *(Diamond Jubilee),* kwa kishindo kwa sababu tumefanikiwa kujenga Taifa moja huru. Matatizo ya kiuchumi yapo, lakini tumehimili mengi kama vile vita, Taifa letu halikutetereka kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaiomba Serikali iigawe Wilaya ya Manyoni, ambayo ni kubwa sana, ina kilomita za mraba 28,000, asilimia 58 ya Mkoa wa Singida. Idadi ya watu imeongezeka kinyume na takwimu zinazooneshwa hivi sasa. Hii itasaidia Mkoa huo kupata mgao mzuri wa fedha za maendeleo na matumizi mengineyo (Keki ya Taifa).

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaishauri Serikali itatue tatizo la maslahi ya Madiwani, walipwe mshahara wa shilingi 2,000,000 kwa mwezi na waruhusiwe kukopa kwenye mabenki. Hapa Tanzania Udiwani ni ajira kwa kuwa Madiwani wetu ni maskini. Kuwaacha wajitokee bila malipo ni rahisi kurubuniwa na Watendaji wa Halmashauri kwa kulipwa malipo yasiyo rasmi na kuwaruhusu Watendaji hao kutafuna fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, nne, ninaishauri Serikali ijiandae kukabiliana na hali ya ukame uliojitokeza mwaka huu. Njaa itakuwa kubwa sana mwaka huu kwa sababu mvua hazikunyesha maeneo mengi. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kuwaruhusu wafugaji walishe na kunywesha mifugo yao kwenye maeneo ya mbuga za Hifadhi za Mhesi, Rungwa na Kizigo ili kunusuru mifugo hiyo isiteketee kwa kukosa malisho na maji, maeneo hayo ni Kata za Mgandu, Ipande, Kitaraka na Idodyandole. Hatua hii itasaidia wafugaji wasihame kwenda maeneo mengine ya nchi kama vile Kilombero.

Mheshimiwa Spika, tano, kwenye eneo la Utawala Bora, ninaishauri Serikali ichunguze kwa kina ni kwa nini kuna kesi nyingi zinazohusu ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora. Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imeonesha kuwa, asilimia 82 ya kesi zilizowafikia 2009/2010 zinaonesha ni kesi au malalamiko yanayohusiana na ukiukwaji wa Utawala Bora. Watendaji, Wilayani na Vijijini, wanawadhulumu Wananchi kwa mengi kwa sababu za unyonge na ujinga wao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu katika maeneo makuu matatu. Hata hivyo, kabla

sijaendelea, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba nzuri, inayojenga taswira ya Serikali jinsi ilivyodhamiria kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo. Ninaomba Serikali iimarishe usimamizi wa Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ninalotaka kulizungumzia ni tamanio la Ukanda wa Ziwa hususan Jiji la Mwanza kupata Chuo Kikuu cha Umma. Mwanza kumekuwa na Vyuo vya Diploma vya muda mrefu kama vile Ukiriguru na Butimba. Kwa nini Chuo cha Ualimu Butimba kisipandishwe hadhi sasa na kuwa Chuo Kikuu kama ilivyofanywa Chang'ombe au Mkwawa?

Tunajua mahitaji ya Wataalam wa Elimu ya Juu katika nchi yetu, lakini pia Vyuo Vikuu huwa ni chachu ya maendeleo katika eneo kutokana na biashara na uwekezaji unaoendana na uwepo wa chuo, walimu na wanafunzi. Idadi kubwa ya watu na uwepo wa miundombinu ya msingi, unahalalisha Mwanza kupewa Chuo Kikuu cha Umma. Tunahitaji maelezo kwa hili.

Pili, Tembo wamekuwa kero kubwa kwa vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Serengeti na Pori la Akiba la Kijereshi wakati Nyati ni tatizo kwa Hifadhi ya Msitu wa Sayoba. Kinachosikitisha zaidi ni uzito wa Watendaji wa Idara kuitikia kwenye matukio wanapoarifiwa kuwepo wanyama hao kwenye mashamba ya watu. Pia hata wale Wananchi waliofanyiwa tathmini tangu mwaka jana katika Kijiji cha Lukungu, bado hawajalipwa kifuta jasho. Kuna nini katika Idara ya Wanyamapori mbona malipo hayatoki?

Mwaka huu kuna njaa katika Ukanda wa ziwa Victoria, tunaomba watu waliolima mazao yao katika Vijiji vya Lukungu, Mwamalole, Lamadi, Mwakiloba, Muungano, Kijilishi, Mwagindi na Nyaluhanda, wafuatiliwe wapate kifuta jasho ili pesa hizo ziwasaidie kukabiliana na hali ya njaa.

Tatu, iwapo Tanzania tunataka tufanikiwe katika mipango yetu ya maendeleo, ni muhimu sana Halmashauri za Wilaya zisimamiwe kwa karibu utendaji kazi wake. Huku ndipo pesa nyingi ya Serikali hupotea kupitia Mikataba Mibovu ya Wakandarasi, ujenzi usiokidhi kiwango na malipo hewa. Iwapo eneo hili litasimamiwa vyema, pia Watendaji wakashirikishwa vyema Wananchi, Tanzania tunaweza kupiga kasi sana kimaendeleo. Halmashauri za Wilaya pia zimekosa ubunifu wa kuvutia uwekezaji na kupanua wigo wa mapato kwa Halmashauri na kwa Wananchi pia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kupongeza dhamira ya Serikali ya kukijenga na kukipanua Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kufikia kiwango cha Kimataifa. Ninaomba sasa taratibu za ujenzi ziende haraka ili Tanzania iweze kunufaika na biashara zitakazozalishwa kutokana na Uwanja huo. Sambamba na upanuzi wa kiwanja, ni vyema Jiji la Mwanza likatengeneza Mpango Mkakati wa kulifanya kitovu cha biashara kwa Ukanda wa Nchi za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Muungano umefikia miaka 47, lakini changamoto nyingi bado zingalipo katika Muungano. Mojawapo ya changamoto hizo ni mgawanyo wa misaada wa asilimia 4.5; ni muda mrefu changamoto hiyo haijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kuhusu changamoto hiyo na hizo nyingine ambazo ni muda mrefu hazijapatiwa ufumbuzi ni bora kila sehemu ya Muungano ifanye kwa kutegemea yale ambayo tutakubaliana katika kutekeleza hilo la mgawanyo wa fedha; inabidi Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ibadilishwe iwe Wizara ya Mambo ya Nje Ushirikiano wa Kimataifa ubakie kuwa si suala la Muungano ili Zanzibar iwe na ushirikiano na nchi za nje ili iweze kupata misaada na hata mikopo.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* ina wajibu wa kudhibiti bei ya mafuta kwa kuweka bei elekezi; ni jambo la kusikitisha kuwa wajibu huo umeshindikana na matokeo yake bei za mafuta katika Jiji la Dar es Salaam ni tofauti na baadhi ya mikoa iliyoko pembezoni. Je, *EWURA* wamechukua hatua gani kurekebisha tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza ni azma ya kukuza kilimo hapa nchini. Juu ya hivyo, nina wasiwasi mkubwa na Mpango huu kufanikiwa, kwani bado utekelezaji wa Mipango yetu huwa ni hadithi. Huwezi kuwa na kilimo bora na endelevu kama kilimo hicho si cha umwagiliaji. Bado ekari za umwagiliaji hapa nchini ni chache, kwa hiyo, mafanikio ya Kilimo Kwanza siyo rahisi kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mifugo, lakini uchangiaji wa mifugo katika uchumi wa Taifa ni mdogo. Hii inatokana na ufugaji usiyo bora. Wafugaji wana mifugo mingi, lakini tija inayopatikana hailingani na mifugo waliyonayo; ni vyema ukawekwa msisitizo wa ufugaji bora, uwepo mgawanyo wa ardhi baina ya wakulina na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, misitu ina umuhimu mkubwa kwa maisha ya binadamu. Juu ya umuhimu huo kwa binadamu, bado binadamu hao ndiyo wakataji wakubwa wa miti hiyo kupata nishati ya mkaa na hivyo misitu yetu itaendelea kukatwa kwa wingi mpaka pale Serikali itakapopata nishati mbadala ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, ardhi hapa nchini kwetu ni asilimia kumi tu ndiyo iliyopimwa. Ardhi iliyopimwa ndiyo yenye thamani zaidi kwa Wananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupima ardhi ili Wananchi waweze kufaidika na ardhi yao?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina matunda mengi, lakini ni jambo la kusikitisha; ni kweli huwa baadhi ya *juice* inayotumiwa hapa nchini inatoka Afrika ya Kusini. Hali hiyo imesababishwa na ukosefu wa viwanda. Kwa hiyo, ipo haja ya kuanzisha viwanda nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebahatika kuwa na Bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara, lakini bado huduma zinazopatikana kwenye Bandari hizo

hazitoshelezi; matokeo yake wahudumiwa wanazikimbia na kwenda Bandari za nchi jirani. Ipo haja Bandari hizo zipatiwe vifaa vinavyostahili na urasimu uliopo uondolewe.

Mheshimiwa Spika, zipo Shule nyingi za Sekondari za Kata ambazo zina upungufu mkubwa wa walimu, vifaa vya kufundishia na maabara. Matokeo yake inakuwa pale matokeo ya Kidato cha Nne yanapokuwa mabaya, ipo haja kufanyike marekebisho makubwa katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tuliomo humu ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuliotokana na Uchaguzi wa Mwezi wa Oktoba, 2010. Wabunge wa Majimbo, tumetokana na ushindi tulioupata baada ya kupigiwa kuwa na Wananchi husika wa Majimbo hayo.

Kilichodhihirisha katika Uchaguzi huo, upatikanaji wa wapiga kura kwa Wabunge baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, zilitumika Sheria mbili tofauti. Kwa Tanzania Bara, ilitumika Sheria ya Uchaguzi ya Tanzania na Tanzania Zanzibar ilitumika Sheria ya Uchaguzi ya Tanzania Zanzibar, ambapo Sheria hiyo inatumika kwa kuchagua Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, tofauti kubwa iliyopo katika Sheria hizo ni upatikanaji wa wapiga kura. Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar inataka ili mtu aandikishwe kuwa mpiga kura, lazima awe mkazi; na kwa kutumia kipengele hicho, wapo Wananchi wengi ambao walishiriki chaguzi za mwaka 1995, 2000 na 2005 hawakupiga kura Uchaguzi wa mwaka 2010. Sheria ya Uchaguzi ya Tanzania haina kipengele hicho.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwa vile Wabunge hawa wapo katika Bunge moja, walitakiwa wachaguliwe kwa sheria moja. Je, Serikali inaahidi nini kwa Uchaguzi wa mwaka 2015 katika kuondoa dosari hiyo?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii, nitoe mchango wangu kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge, kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ingawa inaweza kuonekana kwamba, hali ya uchumi imeendelea kuimarika na ukuaji wa Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 6.0 mwaka 2009 hadi asilimi 7.0 mwaka 2010, lakini hali halisi ya maisha ya Wananchi walio wengi, ambao wanaishi vijijjini na kutegemea kilimo, bado maisha yao ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, wazazi na walezi wengi bado wanashindwa hata kuchangia michango ya elimu na chakula kwa wanafunzi wao, wanaofaulu kujiunga na Kidato cha Kwanza. Katika familia nyingi, mlo umeendelea kuwa mmoja kwa siku tena hupatikana kwa tabu.

Mheshimiwa Spika, Azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza, ieleweshwe vizuri kwa Wananchi wote. Elimu ya Mpango wa Kilimo Kwanza itolewe kupitia vyombo vya habari hasa redioni kwani vijijini, Wananchi wengi husikiliza redio. Kimsingi, Mipango yote ya Maendeleo iwafikie Wananchi kwa kutumia *Media,* kwani *Media* ina nguvu sana na watu wengi zaidi wanaweza kupata elimu kwa wakati mmoja. Hii itaharakisha kupatikana kwa matokeo ya mipango hii kwa kubadili mitazamo *(mind set)* ya Wananchi ya kufikiri kila kitu watafanyiwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Kilimo Kwanza uangaliwe upya. Bei ya matrekta iangaliwe upya na ikiwezekana ipunguzwe, kwani Wananchi wengi hawawezi kumudu gharama ziko juu sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imejitahidi kuthibiti bei ya sukari ili isipande sana, lakini bado wafanyabiashara wengi hawajatekeleza kwa vitendo. Kuna haja ya Serikali kufuatilia kwa karibu uuzaji wa sukari ili Wananchi wasiendelee kuumia.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kimeendelea kuhamasisha na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje. Wawekezaji wengine wamekuwa na tabia ya kuwanyanyasa wafanyakazi wao. Mfano mmoja ni Kiwanda cha Jambo Plastic Ltd. kilichopo Mjini Dar es Salaam. Mwekezaji wa kiwanda, Bwana Suchak, ameajiri vibarua kwa zaidi ya miaka kumi, kwa kuwafanyisha kazi katika mazingira magumu na anawapa malipo ya kila siku badala ya mwezi. Hali ya usalama katika Kiwanda hicho haizingatiwi. Ninaiomba Serikali ifuatilie kwani pengine wapo pia wawekezaji wengine hapa nchini, ambao wana-*treat* wafanyakazi chini ya viwango vya haki za binadamu. Wananchi wasiendelee kunyanyasika katika nchi yao; Serikali iingilie kati.

Mheshimiwa Spika, ili Wananchi waweze kujikwamua kiuchumi, waeleweshwe kupitia vyombo vya habari na hasa redio ili wengi zaidi wafikiwe kuhusu ufugaji wa nyuki. Wizara husika itenge fungu la elimu kwa umma na ninaamini nyuki anaweza kufugika mahali popote na siyo lazima huko Tabora, Mpanda na kwingineko tu.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoambiwa kwamba, lita moja ni shilingi 8,000, basi shughuli hii ikieleweke na kupokelewa na wengi. Ninaamini inaweza kusaidia Wananchi kujikwamua kiuchumi na hivyo kubadili hali yao ya maisha. Kuna misitu katika maeneo mengi; Arusha, Kilimanjaro na miti michache michache katika maeneo mengine ya nchi yetu, ambayo pia inafaa kwa ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Spika, kinachohitajika ni elimu kwa Wananchi. Wanavijiji wahamasishwe ili wawe na mizinga angalau michache katika maeneo yao na hivyo, katika siku za baadaye wanaweza kujiendeleza na kujiondoa katika hali ya umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Hotuba aliyoiwasilisha Waziri Mkuu na kuiunga mkono. Hata hivyo, yapo baadhi ya mambo

ambayo yanahitjika kusimamiwa kwa karibu ili utekelezaji uweze kuwa wa ufanisi mkubwa. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa ndiyo Viongozi Wakuu katika ngazi ya mwanzo ya Uongozi wa Serikali, lakini walio wengi hawayaelewi vizuri majukumu yao, kutokana na kuchaguliwa na kutopatiwa mafunzo. Hivyo; ni muhimu sana kada hii ya uongozi ipewe umuhimu mkubwa wa mafunzo kwa sababu kero nyingi zinatokana na Wananchi wanaowaongoza katika maeneo yao; na hivyo hushindwa kuyakabili kutokana na kutozijua taratibu au baadhi ya sheria ndogondogo wanazotakiwa kuzitumia. Sambamba na hilo, baadhi ya Wenyeviti wa Mitaa/Vijiji wamekuwa vyanzo vya kero kwa kutumia nafasi zao vibaya kama vile utoaji wa vibali na uuzaji wa maeneo ya vijiji bila ushirikishi, kinyume na sheria na taratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo, ninashauri Wenyeviti/Serikali za Vijiji; ili tuweze kufaulu suala zima la Kilimo Kwanza, uwepo utaratibu wa kila Kiongozi wa Kijiji kuwa na shamba la mfano wa Kilimo Bora. Hii itasaidia Viongozi hawa wanapohimiza suala la Kilimo Bora, waweze kuelezea mifano waliyoifanya wao kwanza na Wananchi wengine watafuata. Aidha, lipo tatizo la Maafisa Ugani kutowajibika ipasavyo katika maeneo waliyopangiwa kutokana na kutokuwa na vitendea kazi kama vile usafiri wa kumwezesha kuyazungukia maeneo aliyopangiwa, hivyo kumfanya akate tamaa na yeye kuungana kuwa mwanakijiji. Ninaishauri Serikali iangalie namna ya kuwawezesha Watendaji hawa ili waweze kusimamia shughuli za kilimo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la Watendaji wa Halimashauri kukaa eneo moja kwa muda mrefu (miaka 10 - 20), bila uhamisho, jambo ambalo linasababisha kuzoeleka na Wananchi na kuwa chanzo cha kutumika vibaya na wale wasioitakia mema nchi yetu. Ninaishauri Serikali, Watumishi wawe wanahamishwa ili kuzinusuru Halmashauri. Kada zinazotakiwa kuhamishwa ni Wakurugenzi, Waweka Hazina, Maafisa Utumishi, Maafisa Mipango na Madaktari.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuchaguliwa kushika wadhifa wake huo na jinsi anavyotekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Mawaziri wake, pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa ngazi zote, wanao umuhimu mkubwa katika Taifa; na kwa maana hiyo, Viongozi wetu wa Vijiji, Vitongoji na Madiwani, ninaiomba Serikali iwatupie jicho la huruma kwa kuwafikiria angalau posho na mishahara kwa Madiwani wetu, kwani mti umadhubuti wake ni shina. Shina likiwa bovu, mti hauwezi kunawiri na hao Viongozi wa ngazi za chini ndiyo kimbilio letu, bila ya wao hatuwezi kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mirembe ina upungufu mkubwa wa Madaktari, ninaomba sana hiyo Hospitali tuiangalie kwa jicho la huruma kwa kuwapeleka wataalamu wa kutosha pale ili wagonjwa waweze kupatiwa huduma nzuri na za uhakika. Tusiwadharau wale wenzetu ambao Mwenyezi Mungu, amewapa mitihani ya maradhi yale, kwani wao ni binadamu kama sisi; tukumbuke kwamba, yeyote kati yetu anaweza wakati wowote kupata maradhi, hivyo tuwajali, tuwapende kwa kuwapatia madaktari wazuri na wa kutosha ili waweze kutibiwa na kupona haraka ili warudi kujiunga nasi katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mtoto iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, inasisitiza kwamba, haki za mtoto ni pamoja na kupewa huduma na katika huduma ni pamoja na matibabu. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusiana na watoto ambao wana matatizo kama ya kufanyiwa upasuaji kutokana na magonjwa aliyonayo na hudaiwa fedha nyingi ili aweze kufanyiwa upasuaji?

Je, hiyo ni haki ya motto na pengine wazazi wake hawana uwezo? Tunaona bora mtoto yule ateseke mpaka apoteze maisha kuliko kuokoa maisha yake kwa kujali fedha. Ninaomba haki za mtoto zilindwe kwa nguvu zote na tuwe na ufuatiliaji wa kina katika Hospitali zetu, kwani Watendaji wetu wengine siyo waadilifu hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba, Muungano wetu unakaribia umri wa miaka 50 sasa, bado unalalamikiwa kuwa na kero nyingi sana ambazo zimekuwa zikidharauliwa kadiri tunavyozisema. Tukumbuke kuwa, mdharau mwiba mguu huota tende. Inaonesha dhahiri kwamba, hata Mheshimiwa Raisi alipounda Wizara za Serikali, hakuona umuhimu wa kuweka Wizara ya Muungano, badala yake kaunda Idara tu ya Muungano na hiyo Idara Watendaji wake hakuna uwiano baina Zanzibar na Bara.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI ina majukumu mengi sana, ninadhani imefika wakati majukumu haya yapungue ili ufanisi uongezeke.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Maafa kiangaliwe upya ngazi ya Wilaya na Kata, kuna tatizo kubwa kwenye Kamati za Maafa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba misaada ya Maafa ya Mafuriko Kilombero ifuatiliwe kwa karibu, kwani kuna malalamiko mengi ya walioathirika na mafuriko hayo kutokana na misaada hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hali halisi ya njaa Jimboni, kwani ni hali ya kutisha pamoja na kupata chakula kutoka Ghala la Taifa. Tani 300 hazitoshi kabisa, ninaiomba Serikali ituongezee chakula haraka sana.

Pili, Wakulima wa Jimbo langu wana maeneo makubwa ya kulima, lakini kutokana na hali ya mabadiliko ya Tabia Nchi, mvua hazitoshi kabisa. Ninaiomba Serikali iweke mpango sasa wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika Kata ya Nyang'hwale, Kakora, Kharumwa, Bukwimba, Nyijondu, Nyugwa, Izunya, Kafita, Busorwa, Shabaka, Nyashiranga na Mwingiro ili kuinua kipato cha Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale.

Tatu, ninaiomba Serikali iwasaidie Wakulima wa Jimbo langu, kuwapimia mashamba yao na kuwapatia hatimiliki ili waweze kupata mikopo toka Benki na kupanua kilimo chao na kujenga nyumba bora.

Nne, Wafugaji wa Jimboni kwangu wameanza kukata tamaa na ufugaji kwa sababu Serikali imewasahau. Kwa kutowatafutia soko la ngozi, samli na ng'ombe. Pia ng'ombe wanateseka kwa kukosa maji, majosho na madawa. Ninaiomba Serikali iwatazame Wafugaji wa Jimbo la Nyang'hware kwa jicho la huruma.

Tano, Jimbo la Nyang'hwale lina matatizo makubwa ya maji safi na salama. Akina mama wanakwenda umbali mrefu kutafuta maji. Pia kuna shule za bweni, wanafunzi wanachukua muda mwingi kutafuta maji na kupoteza vipindi vingi. Ninaiomba Serikali ilitatue tatizo hili kwa haraka kuepusha Wananchi na maradhi yatokanayo na kunywa maji machafu na kuepusha kuvunjika kwa ndoa na kupata mimba ovyo kwa wasio waaminifu.

Sita, huduma za afya katika Jimbo langu siyo nzuri sana katika vituo vya afya na zahanati kutokana na upungufu wa madawa, vitendea kazi, Waganga, Wauguzi na kadhalika.

Saba, Elimu: Kuna matatizo mengi sana, nitasema machache kama upungufu wa walimu, nyumba za walimu, maabara, maktaba, madarasa, madawati na kushuka kwa nidhamu kwa wanafunzi. Ninaiomba Serikali ilitupie macho eneo hili ambalo nimelitaja ili kuleta tija kwenye elimu.

Nane, kero walinazo walimu ni nyingi sana, nitazitaja kwa uchache kama ugumu wa maisha walionao vijijini; huduma duni kama usafiri wa kufuatilia mishahara yao wilayani kwa gharama ya shilingi 30,000 hadi 50,000, hiyo ni nauli. Ninaiomba Serikali iwakopeshe usafiri wa pikipiki walimu hao na kukatwa kwenye mishahara yao kila mwezi.

Tisa, huduma ya afya kwa walimu kupitia Bima ya Afya. Walimu wa Jimboni kwangu wanadai kuwa hawaoni sababu ya kuwa wanachangia Mfuko wa Bima ya Afya wakati hawapati matibabu kupitia Mfuko huo. Walimu wa Jimbo la Nyang'hwale wamenituma kuwa hawataki tena kuchangia Mfuko kwa kukatwa mshahara. Pia

wanaomba kufutwa kwa Mfuko huo wa Bima ya Afya na kutolewa upya fomu za kujiunga kwa hiari.

Kumi, masilahi ya wafanyakazi wa migodini hususan Watanzania ni duni, pia kuna upendeleo mwingi; mfano, wafanyakazi toka nje wanalipwa kwa pesa za kigeni. Je, kwa nini na Watanzania wasilipwe kwa Dola? Ninaiomba Serikali iliangalie hili ili Wananchi wetu nao walipwe pesa za kigeni.

Kumi na moja, ninapenda kuishukuru Serikali kwa kuchukua hatua ya kupanua Kiwanja cha Ndege Mwanza. Hatua hiyo itafungua chachu ya maendeleo na kupanua wigo wa kupata watalii wengi, kwa hiyo, Mkoa wa Mwanza na Taifa zima, litapata mapato mengi. Ombi langu, Serikali ikamilishe ujenzi huo haraka.

Kumi na mbili, ninaishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza Mradi wa Umeme *(MCC),* kupeleka umeme katika Jimbo la Nyang'hwale. Upembuzi yakinifu umekwishafanyika. Ninaiomba Serikali ifanye haraka kufikisha umeme ili kuchochea maendeleo kutokana na Nishati hiyo na kuondoa dhana kwa Wananchi kusema kuwa Ahadi za Serikali ni hadaa tu.

Kumi na tatu, bei ya pamba inakatisha tamaa Wakulima wa Jimbo langu, ukizingatia pia bei ya pembejeo kuwa juu sana. Ninaiomba Serikali iliangalie suala la kupunguza bei za pembejeo na kupandisha bei ya pamba kulingana na soko la dunia ilyopo kwa msimu huo ili kuwapa moyo wakulima wa pamba kuendelea kulima zao hilo.

Kumi na nne, miundombinu ya barabara zifuatazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Mwanza kama barababra za kutoka Busini, Ngoma, Busolwa, Nyijundu, Kharumwa, Bukwimba, Nyang'horongo hadi Kahama. Kutoka Geita - Nyang'hware – Nyijundu – Kharumwa; kutoka Geita – Nyarugusu – Bukoli – Bugarama – Kahama; na kutoka Geita – Sengerema – Nyamazugo – Nyihunge – Nzela – Geita.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa vile wachangiaji wengi wamechambua kwa kina Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi ninapenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wote katika Ofisi yako, pamoja na Watendaji, kwa Hotuba iliyoandaliwa kwa kina, ila ninapendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ni kubwa sana, imebeba Wizara nyingi na kusababisha urasimu usio wa lazima. Kitendo cha kuhamishia Elimu ya Sekondari na Shule za Msingi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, kinasababisha utendaji uwe mgumu; shughuli hizi zirudi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Watendaji Wakuu; Makatibu Wakuu, Maafisa Tawala wa Mkoa na Wilaya pamoja na Watendaji wa Halmashauri *(DEDs)*, wanafanya maamuzi kisiasa; Watendaji wanaendeshwa na wanasiasa. Makatibu Wakuu wa Wizara ama wameacha kuishauri Serikali kitaaluma au wanatoa ushauri unaopendeza Mawaziri, wamekuwa waoga kwani wakitofautiana na mabwana wakubwa ama wanafukuzwa au wanahamishwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka kwamba, Serikali iliagiza nyumba za Serikali zilizoko katika maeneo ya Taasisi kama Hospitali na maeneo mengine nyeti kama Line Polisi na kadhalika zirudishwe. Maamuzi haya hayakutekelezwa, kwa mfano, katika Wilaya ya Mbulu, nyumba za Hospitali zilizoko katika eneo la ekari 250 ziliuzwa. Kitendo hiki kimekwamisha upanuzi wa Hospitali ya Wilaya pamoja na Chuo cha *MCH* kilichopo katika eneo hili. Chuo ambacho Mheshimiwa Raisi Jakaya Mrisho Kikwete alishauri ipanuliwe.

Mheshimiwa Spika, kilio cha Wananchi wa Jimbo la Mbulu ni maeneo ya ekari 250, zilizouzwa kwa watu wachache wasiozidi 16 zirudishwe; ni jambo la ajabu mtu mmoja kumiliki ekari hadi tano katikati ya mji na kuzuia kuendelezwa Taasisi ya Huduma ya Umma kama Hospitali na Chuo cha *MCH*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wananchi wa Jimbo la Mbulu wanaomba Mpango wa Serikali wa kujenga Shule tatu za Kidato cha Tano *(A Level)* katika Jimbo lao utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Watendaji wake wote, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Timu nzima ya Watendaji, kwa kuleta Bajeti hii nzuri. Pamoja na Hotuba nzuri, ninaomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kupangisha ardhi Wilayani Karagwe, Mkoani Kagera, kwa wafugaji mbalimbali. Ardhi hiyo iligawanywa katika *block*s. *Blocks* hizo baadhi yake wamepewa raia wa kigeni, wengine hawana mifugo bali hukodisha kwa biashara hasa kwa raia wa nchi jirani toka Rwanda na Uganda. Hali hii huwafaidisha raia wa nchi za kigeni tu wakati raia wa Tanzania wanabaki maskini. *Blocks* hizi zimewasonga na kuwanyima fursa za ufugaji mdogo mdogo Wananchi wa Kata ya Kihanga hasa Vijiji vya Kihanga, Katanda, Kibwera, Mushabaiguru na Mlamba. Kwa kuwa *blocks* zilizotolewa ni kubwa kuliko mahitaji; kwa nini Serikali isimege eneo hilo angalau nusu na kuwagawia Wananchi wa vijiji hivi? Kuna mgogoro ambao muda wowote utalipuka baina ya wafugaji na wakulima. Ninaomba Serikali iingilie kati haraka kabla hali haijawa mbaya.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba Kimisi lililoko Wilayani Karagwe, limeleta kero nyingi kwa Wananchi wa Kata za Rugu, Nyakasimbi, Bweranyange, Nyakakika na Ihembe. Kero hizo ni pamoja na wanayama waharibifu hasa Tembo kwa kula mazao ya Wanachi na kuua raia. Kero nyingine mbaya sana ni kwamba, eneo la Pori la Akiba la Kimisi limesonga Wananchi wa Kata nilizozitaja hapo juu. Eneo la Pori limeingia kwa kiasi kikubwa katika maeneno ya wafugaji na wakulima. Hali hii imeleta mtafaruku baina ya Wananchi na Wafanyakazi wa Pori, kwani mifugo ya raia inakosa malisho na mara iingiapo kwenye Pori hilo, mifugo hukamatwa na kutozwa faini zaidi ya shilingi milioni moja na kuendelea. Tunaomba Serikali ichukue hatua haraka kusogeza mipaka ya Pori hili angalau kwa kilomita kama thelathini kuingia ndani ili Wananchi wa Karagwe wa Kata nilizozitaja, wapate eneo la kufugia na kulima na hii ndiyo njia pekee ya kuwaletea maisha bora Watanzania waishio Karagwe. Serikali izingatie maombi haya kwa makini na haraka, kwani Wananchi hawa wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanachangishwa shilingi elfu tano, gharama za matibabu zinazohusisha madawa lakini jambo la kuudhi na kero ni kwamba, dawa hazitolewi kwa wagonjwa. Ajabu, tunaambiwa dawa zinaharibika *MSD,* Serikali iliangalie suala hili kwa umakini. Pongezi Hospitali ya Taifa ya Afya ya Muhimbili, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Madaktari wote ni wachapa kazi, wakarimu na wanajali sana. Pamoja na madaktari, pia watumishi wengi wanafanya kazi zao vizuri na kwa kujali wagonjwa wao. Ninawapongeza sana; hongera sana Muhimbili Hospital. Tatizo la Muhimbili ni upatikanaji wa madawa, madawa hayapatikani, yakipatikana ni kidogo sana. Wananchi wanaambiwa wakanunue dawa wakati hawana fedha na hata wakinunua hawarudishiwi fedha zao. Jambo linalosikitisha ni kwamba, dawa zinaharibika *MSD*. Ninaomba Serikali ihakikishe dawa zinapatikana muda wote katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, Zahanati za Vijiji zilizoanza miaka ya 2007 hadi 2010 hadi leo hii hazijakwisha wala kukamilika. Serikali ikamilishe Zahanati za Vijiji na zianze kutumika kwa kupewa madawa, Watumishi na vifaa vyote muhimu. Watumishi wa Zahanati ni muhimu sana, kwani zahanati bila watumishi ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mbegu za Miti kilichopo Morogoro, kipeleke mbegu Wilayani na ikiwezekana kila Kata. Serikali ifanye kila linalowezekana kuweka vitalu vya miti ya mbao, nguzo za umeme na kuni kila kijiji na iweke malengo kwa kila kijiji, kila kaya, ipande miti mingapi kila mwaka. Wizara ya TAMISEMI ni vizuri ikashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, waweke mkakati wa makusudi wa kupanda miti.

Mheshimiwa Spika, hali ya tabia nchi, inayojitokeza duniani na nchi yetu ikiwemo ni kutokana na kutopanda miti. Serikali iweke mkakati wa kupanda miti na siyo kulalamika tu kuhusu ukame. Sambamba na hilo, Wananchi wa Mkoa wa Kagera na hasa Wilaya ya Karagwe, wamepanda miti mingi aina ya mikaratusi, misizi na kadhalika. Miti hii tayari imekomaa, lakini Wananchi hawana soko la uhakika. Tunaiomba Serikali itutafutie soko la miti hii na hasa nguzo za umeme na mbao. Jambo hili likifanyika haraka

sana, litawakomboa Wananchi wa Jimbo la Karagwe na Wananchi wa Mkoa wa Kagera na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Nishati na Madini: Kuna ahadi za Rais Kikwete, Jimboni Karagwe, kuhusiana na umeme vijijini Karagwe. Mheshimiwa Rais aliahidi kupeleka umeme Vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi, Kyanyamisa hadi Ihembe. Tulielezwa kuwa mkandarasi atakabidhi Mradi huo Desemba, 2011. Hii ni habari njema, lakini dalili hazionekani. Tunaomba mkandarasi aanze kazi Krismasi itukute kwenye mwanga wa umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Bugene, Ihanda, Kamagambo, Nyakagoyagoye, Nyabiyonza hadi Nyakaiga sioni Bajeti yake. Ninaomba ahadi hii ya Rais itimizwe mwaka huu wa fedha. Umeme wa Kayanga, Ndama, Rukaka, Nyabwegira, Runyaga hadi Rwambaizi, nguzo zipo miaka zaidi ya mitano. Je, ni lini umeme utapelekwa?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda tena leo kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata fursa ya kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tangu nianze kutoa shukrani na pongezi zangu za wewe kupongeza kuchaguliwa kama mwanamke wa kwanza kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu, nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kujikita katika nidhamu ya matumizi ya fedha na matumizi ya madaraka waliyopewa watumishi waliopo katika ofisi husika na idara zake.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutofautiana kidogo na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa pale aliposema kuwa uchambuzi wa Benki ya Dunia *(IMF)* na baadhi ya waandishi wa vitabu kama vile Steve Redelet katika kitabu chake cha *Emerging Africa 2010* kuwa Tanzania ni nchi inayokua kwa kasi kiuchumi, mimi inanipa sana wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, hali ya umaskini wa Tanzania imeendelea sana kuwa kubwa hasa wale wanaoishi vijijini, sijui tathmini hii imetokana na tafiti zipi; hata Deni la Taifa limeendelea sana kukua sambamba na watoto wanaoishi katika mazingira magumu na pia hali ya watumishi kama vile walimu, askari, wauguzi wa ngazi ya chini yamezidi kuwa duni kimaisha na wanaishi maisha yasiyo ya kujiwekea faida, hii inathibitika kwa ushahidi ufuatao kila ifikapo mwisho wa mwezi wafanyakazi hawa wa kada ya chini utawakuta katika foleni ya kutoa fedha katika *ATM* za *NMB* ambapo ndipo mishahara yao huwekwa. Hii ni dalili ya kuwa wote uwaonao katika *ATM* wanatoa mishahara wakajinusuru na kulipa madeni na sio kuwekea faida, wapo wafanyakazi wa kada za chini waliojiingiza katika mikataba kandamizi kwa kukopa kwa watu binafsi wenye riba kubwa ili kuwasaida kuhisi na hawa wanakuwa na madeni yasiyokoma na mishahara yao ni kwa ajili ya kulipa madeni tu.

Mheshimiwa Spika, bado katika matumizi ya rasilimali watu hatujaweza kabisa kusimamia ipasavyo, na mfano halisi ni pale ambapo utakuta kuna baadhi ya wafungwa walioko Magerezani waliohukumiwa kufanyishwa kazi tofauti na taaluma zao kama vile utakuta fundi seremala anapangwa kupasua mawe wakati kuna upungufu mkubwa wa madawati katika shule zetu na misitu tunayo, utakuwa mwalimu aliyefungwa anachimba mitaro wakati tuna upungufu wa walimu mashuleni.

Mheshimiwa Spika, tukiweka utaratibu mzuri wa kuwalinda na kuwasimamia vizuri, tunaweza kuwatumia katika taaluma zao na muda wa kurudi gerezani ukifika basi warudi kutumikia kifungo kama ilivyo ada.

Mheshimiwa Spika, bado hatujaweza kabisa kusimamia fedha ziendazo katika Halmashauri zetu japo nia ya Serikali na Wizara ni njema, ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali bado inaonyesha kuna upungufu mkubwa sana wa utunzaji hesabu na ubadhirifu mkubwa kwa fedha za umma hasa katika Halmshauri za Wilaya na Miji.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa *money without control is nothing,* fedha za maendeleo bado kwa kiasi kikubwa zinaishia mifukoni mwa watu wasio waaminifu na wamekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa maendeleo yetu. Ningependa sana kusema kuwa kupata tu ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti haitoshi, ni vizuri sasa ripoti iendane na kesi mahakamani kuliko kuhadithiwa mamilioni yanapotea.

Mheshimiwa Spika, bado kuna shida kubwa sana kwenye shule za kata, imeanza kuonekana shule hizi ni za wapiga kura na wapigiwa kura watarajiwa wanasoma katika shule bora. Kuna changamoto nyingi sana katika shule za msingi na sekondari zikiwemo ukosefu wa vitabu, walimu, maabara na maktaba.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu letu sasa bila kujali chama wala eneo tunalotoka sisi kama Wabunge si jukumu letu kusifia shule za Kata, bali kuweka na kupanga mikakati itakayoboresha shule hizi na jukumu la kusifia liwe la wazazi wa watoto waliohitimu kutoka katika shule zetu hizi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya elimu imeongezeka kwa 12% kutoka shilingi milioni 2,045.4 hadi shilingi milioni 2930 ni ongezeko la kuridhisha ila kama hazitasimamia vema basi ujue ufaulu na ubora wa elimu hautaonekana.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia Serikali ilichukulie kwa uzito wa pekee kwa kuwa vijana wengi hawakufaulu mwaka 2010 na wapo mitaani si kwamba hawakuwa na uwezo bali ukosefu wa walimu, maabara na pia maktaba na vitabu.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuiomba Serikali kuwatafuta wanafunzi waliopo warudie japo kidato cha tatu na wafanye mitihani kama *private candidate,* kuliko kuwaaacha hawa ambao ni tegemeo kubwa kwa mustakabali wa Taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wakiachwa bila kusaidiwa wengi wao watajiingiza katika vitendo vya uhalifu na huo utakuwa mzigo mkubwa sana kwa Taifa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nitafarijika kama mapendekezo yangu na ya wenzangu yaliyo na nia bora ya kuendeleza nchi yetu yachukuliwe na yafanyiwe kazi ili Tanzania iwe mahali pazuri sana pa kuishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanza mradi wa Mchuchuma ambao utazalisha umeme *MW 600* na kuzalisha chuma ghafi. Umeme utasaida sana kupunguza mgao na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Lakini pia chuma ghafi kitasaidia sana kuanzisha viwanda vya kila aina na kukuza uchumi. Nashauri Serikali ijitahidi sana kutosafirisha chuma ghafi kabla ya kukidhi mahitaji ya ndani kwanza. Ni bora kusafirisha bidhaa zitokanazo na chuma ghafi maana unaongeza thamani na kupata fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kukamilisha Kanuni za Sheria ya *PPP*. Hii ni muhimu sana. Sasa Serikali inatakiwa kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ili waingie ubia na Serikali kwa miradi ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, umeme na kadhalika ili kuongeza kazi ya ukuaji uchumi.

Mheshimiwa Spika, *Vote 78,* imejitokeza dhana ya viongozi wa Mkoa kujipangia fedha nyingi sana kwenye *vote* hiyo na kupanga fedha kidogo sana za Wilaya ambako ndipo kuna miradi ya maendeleo. Kwa mfano, Mkoani Mbeya Katibu Tawala wa Mkoa kapangiwa zaidi ya bilioni wakati *DAS* Chunya kapangiwa shilingi milioni 238. Ukubwa wa Wilaya ya Chunya ni karibu nusu ya Mkoa wa Mbeya. Jambo hili linahitaji kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa Halmashauri, hasa walimu wapo wanaokaa mbali sana na Makao Mkuu ya Wilaya. Kwa Wilaya ya Chunya wapo wanaokaa na kufanya kazi kwenye umbali wa kilomita zaidi ya 200. Mwisho wa mwezi wanapaswa kufuata mishahara Makao Makuu ya Wilaya. Mishahara yao yote inaishia kwenye nauli na malazi. Naomba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia sehemu ya Muungano. Ni muda mrefu kumekuwa na manung'uniko kutoka pande zote mbili za Muungano kila upande umekuwa na madai kadhaa kuhusu suala la Muungano. Mara nyingi Serikali imekua ikiahidi kwamba inatafuta ufumbuzi juu ya suala hili, Tume mbalimbali zimeundwa na Serikali juu ya jambo hili lakini ukweli ni kwamba matokeo ya kuridhisha juu ya jambo hili bado halijaonekana. Sasa imefika wakati ambao Serikali ifanye juhudi za makusudi ili kuondoa kero hizi.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo yamekuwa ni kero kubwa ni:-

(a) Ugawaji wa mapato yatokanayo na Benki Kuu;
(b) Ugawaji wa misaada kutoka nje; na
(c) Ugawaji wa nafasi za ajira katika Idara za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu juu ya mgao wa mapato na faida yatokanayo na Benki Kuu. Ni vema sasa Serikali ifanye juhudi za makusudi juu ya jambo hili kwa kweli mpaka sasa mgao wa asilimia nne kwa Zanzibar kunaleta hisia kwamba Zanzibar inapunjwa hivyo Serikali iangalie upya juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugawaji wa misaada kutoka kwa wahisani kwa kweli ni vema jambo hili likawekwa vizuri juu ya ugawaji wa misaada hiyo ili pande zote mbili zikaeleweka ni vipi na kiasi gani kila upande unafaidika na misaada hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamekuwapo na manung'uniko hasa kutoka upande wa Zanzibar juu ya ajira katika Idara za Muungano zilizopo Zanzibar kwamba imebainika ajira nyingi katika Idara hizo zinaajiri vijana kutoka Tanzania Bara zaidi hata katika zile sehemu ambazo hazihitaji utaalamu maalum, mfano hata tarishi au mpika chai.

Mheshimiwa Spika, ni vema masuala madogo madogo kama haya ambayo yanaleta malalamiko kutoka kwa wananchi yakashughulikiwa haraka ili Serikali yetu sikivu iendelee kujijengea heshima zaidi na kuendeleza sifa yake ya usikivu na kuwajali wananchi wake.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, hali ya maji safi na salama kwa Mkoa wa Tabora ni mbaya sana na inaonekana mbali ya kilio cha muda mrefu cha Waheshimiwa Wabunge lakini bado Serikali haijafanikisha kupatikana kwa huduma hii muhimu kwa Mkoa wa Tabora.

Ninaishauri Serikali mpango wa maji safi na salama toka Ziwa Victoria unaoendelea kufika Shinyanga pia mradi huo Serikali ijiandae kufikisha huduma hiyo Tabora.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kubambikiza kesi bado linaendelea kuwatesa wananchi wasio na hatia na wengine kuonekana wanafungwa isivyo halali, ninaishauri Serikali kuangalia kero hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati mbalimbali ya Serikali kudhibiti matumizi ya fedha za umma lakini imebainika bado baadhi ya Wizara, Idara na Halmashauri zinatumia fedha za umma vibaya, kumejitokeza wizi, ubadhirifu na uzembe katika maeneo niliyoyataja. Ushauri wangu kwa Serikali ni kutembea katika maneno ya

Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliposema kuwa wizi, ubadhirifu na uzembe hautavumiliwa.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika huduma za jamii, bado inaendelea katika elimu kwa ujumla wake, katika afya kwa ujumla wake na hata askari barabarani *(traffic)* napo si salama, lakini mahakamani kumekuwa na kero hii zaidi.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa chakula au kilio cha njaa umekuwa ndio wimbo unaoendelea siku hadi siku huku Serikali haijajiandaa vizuri juu ya kutumia mito isiyokauka, mabonde yenye rutuba na mabwawa kuweza kukabiliana na upungufu wa chakula na kupambana na umaskini katika dhana nzima ya MKUKUTA hivyo ninashauri Serikali ikubali kuanza kuyatumia mito, maziwa na mabonde yenye rutuba katika kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi inaonekana hali ya mvua tulizozizoea zinapungua hivyo hali ya malisho ya wanyama yanaendelea kupungua hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa njia bora ya mifugo yetu kupata malisho ya uhakika. Hivyo naishauri Serikali kuongeza na kuandaa mashamba mapya ya malipo ya wanyama ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuharibiwa mazingira linaendelea likitekelezwa na wananchi mbalimbali hali ambayo ni hatari sana kwa mustakabali wa wananchi, miti inakatwa katika vyanzo vya maji, misitu inachomwa moto na uchimbaji fukwe za bahari. Hivyo ninashauri Serikali kuendelea kutoa elimu na kutoa adhabu kali kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Bajeti ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naishauri Serikali iangalie kwa makini suala la kuwawezesha Madiniwani wafanye kazi zao kwa ufanisi, wapatiwe namna ambayo watapatiwa/kukopeshwa vyombo vya usafiri na wawe na kipato ambacho kitawafanya watumie muda wao wote kwa ajili ya kusimamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Nzega na Jimbo la Bukene, kuna upungufu mkubwa wa watendaji wa vijiji, zaidi ya vijiji 40 havina watendaji. Hii inarudisha sana nyumba usimamizi wa programu za maendeleo vijijini. Kunapokuwa na jambo la maendeleo kijijini kwa mfano uandikishaji wa watoto kujiunga na shule ya msingi, jambo hili halifanyiki kwa ufanisi, kwa sababu hakuna mtendaji wa kulisimamia. Sababu kubwa kwa Wilaya ya Nzega ni kwamba sifa *(qualifications)* za watendaji wa vijiji na kata zipo juu sana kwa sasa. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, mara kadhaa imetangaza nafasi za watendaji wa vijiji lakini mara zote hawapatikani watu wenye ngazi ya *diploma* inayotakiwa. Naiomba Serikali itoe kibali maalum kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, iruhusu kuajiri vijana waliomaliza kidato cha sita wawe watendaji wa

vijiji na kisha Halmashauri yenyewe iwaendeleze wakiwa kazini hadi kufikia ngazi ya *diploma* ambazo zinatakiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu mkubwa wa madawati katika nchi yetu linaweza kupatiwa ufumbuzi kwa kuandaa mpango maalum wa kimkakati wa angalau mwaka mmoja wa kuondoa kabisa tatizo hilo kwa nchi nzima kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali nchi nzima. Wananchi, wazazi, taasisi na Serikali wote kwa pamoja tushirikiane kuchangia kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bahi ni miongoni mwa Wilaya zenye ukame mkubwa wa mvua na hivyo kusababisha kila mwaka Wilaya hii imekuwa ikipatiwa msaada wa chakula na Serikali. Lakini Wilaya hii ina fursa kadhaa za mito na maji yanayotiririka wakati wa masika ambayo kimsingi yangeweza kuhifadhiwa kwa njia ya mabwawa kwa shughuli za umwagiliaji. Hivyo naishauri Serikali iangalie kwa namna ya pekee fursa hizi zilizopo hasa mito na mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya hii kwa kufanya utafiti wa kina juu ya uwezekano wa kuanzisha mradi kabambe wa kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya hii hasa kwa kuziangalia upya skimu kumi za umwagiliaji zilizoko katika Wilaya hii ambazo ama hazijakamilika au zimechakaa sana. Naamini kama Serikali itaamua kusaidia sekta hii ya umwagiliaji katika Wilaya hii basi itakuwa fursa muhimu ya kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa chakula katika Wilaya na kuzalisha ziada.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bahi ni Wilaya mpya, inahitaji sana Serikali kuelekeza jicho lake katika kuwezesha mambo yafutayo:-

(a) Kuwezesha watumishi kuhamia Makao Makuu ya Wilaya toka Dodoma Mjini kwa kutoa fedha za ujenzi wa nyumba za watumishi, manunuzi za *furniture* za ofisi na mahitaji kadhaa ya watumishi.

(b) Kusaida juhudi za Halmashauri za kutatua tatizo kubwa la maji kwa kutoa fedha za kuleta maji umbali wa kilomita 40 toka Wilaya ya Manyoni ili kumaliza tatizo la uhaba wa maji katika mji wa Bahi ambao ndio Makao Makuu ya Wilaya.

(c) Kupewa fedha za kutosha ili kuanza kujenga miundombinu za ndani ya mji wa Bahi hasa barabara, maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu katika maeneo haya yafuatayo, maji, chakula, uwekezaji na ardhi.

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la maji, napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao unalenga kuwapatia maji wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na Wilaya zake. Mradi huu ambao kwa sasa unaitwa

*KASHUWASA* umewasaidia sana wananchi wa Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Kahama kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelewa Serikali imewasaidia wananchi wa Manispaa lakini kwa upande mwingine naona kama inawakomoa. Manispaa ya Shinyanga inayo mamlaka nyingine ya maji yaani *SHUWASA,* kuwepo na mamlaka mbili za maji, eneo moja ni kuumiza mtumiaji kwani sera ya maji safi na salama ikoje? Na ni kwa nini Shinyanga kuwepo na Mamlaka mbili za maji na isiwe moja?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwapunguzie mzigo wananchi wa Shinyanga kwa kubakiza mamlaka moja ya maji kama ni *SHUWASA* au *KASHUWASA*. Wananchi wanaumia kulipa ankara za maji hivyo Serikali inaonekana kama imewakomoa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hali ya chakula imeelezwa kuwa ni ya kuridhisha isipokuwa katika baadhi ya maeneo machache ya Wilaya 48 yaliyopata ukame ikiwemo Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu ameainisha maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa chakula na tayari tani 36,970 za mahindi zimeshapelekwa kwa walengwa. Nasikitika kusema Manispaa ya Shinyanga ina matatizo katika zoezi la ugawaji wa chakula, kwani Kata ambazo zinaongozwa na Diwani wa chama cha upinzani hapatiwi chakula cha kutosha. Hali hii inalenga kuleta taswira mbaya kwa wananchi ili Diwani aonekanae hasimamii vizuri matatizo ya wananchi ili 2015 CCM ipate cha kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu amegusia kuhusu hali ya kisiasa nchini ni nzuri na mpaka likaundwa Baraza la Vyama vya Siasa, hii inadhihirisha kuwa mfumo wa vyama vingi haukuota kama uyoga bali ni maamuzi ya kisheria ambayo yapo mpaka kwenye Katiba yetu. Leo hii kila raia ana haki ya kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa.

Mheshimiwa Spika, kujiunga na chama cha upinzani kwa wananchi imekuwa kama ni mateso kwani wananyimwa fursa nyingi kwa kusingizia kuwa wamechagua upinzani. Ninaiomba ngazi zinazohusika zizingatie kuwa vyama vingi vipo kisheria na vinatambulika Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ardhi. Ardhi ni rasilimali ya msingi katika uzalishaji kwa kuleta maendeleo na kujenga uchumi imara wa wananchi na Taifa. Naipongeza Serikali kwa kupima vijiji 11,242 na vijiji 7,043 kupatiwa hati za ardhi za vijiji. Mpango wa kushirikisha Halmashauri za miji na Wilaya kutumia vyanzo vyao vya mapato kupima mashamba na kutoa hatimiliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kuhusu utekelezaji wake, kuna vijiji ambavyo tayari wananchi wake wameshalipia gharama za upimaji vijiji lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri na ni halisi ni vijiji vitatu vilivyoko Manispaa ya Shinyanga. Ndembezi, Ngokolo na Kitangili kuna wananchi walilipishwa na Halmashauri kila mmoja kati ya shilingi 40,000 mpaka 85,000 kila mmoja ili apimiwe mashamba yao toka mwaka 2008 mpaka sasa hawajapewa *offer* wala *title.* Matokeo yake watu wachache wenye pesa wamekuwa wakija na *offer* wakidai ni wamiliki halali wa maeneo hayo na kufanya wanakijiji kubakia midomo wazi.

Mheshimiwa Spika, hili ni suala ambalo lisipopatiwa ufumbuzi wa kina na haraka damu itamwagika katika vijiji hivyo. Kwa nini Serikali inashindwa kuwapa haki zao hao wananchi ambao wote wamekulia humo na kuzaliwa hapo sasa waende wapi? Kwa nini Sheria ya Ardhi inapigwa chenga? Kwa nini wanathaminiwa watu walio na pesa na kwa kushirikiana na wafanyakazi wa ardhi na manispaa?

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho naomba nizungumzie kuhusu wawekezaji. Nina amini makampuni ya simu ni wawekezaji pia. Makampuni haya yamekuwa yakiweka minara yao kwenye vijiji na kuingia mikataba na wananchi wenye maeneo ambapo wanaweka minara bila kuwalipa chochote.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa vijiji wanakuwa wakishiriki katika kuhujumu haki za wananchi. Nina mfano ambao *Zantel* imeweka mnara kwenye shamba la mzee mmoja katika Wilaya ya Kishapu, Kata ya Maganzo na kuingia naye mkataba kisha kutokomea, leo hawajamlipa kitu na ni miaka mingi tangu waweke mnara wao.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iangalie haki za hawa wananchi wapatiwe fedha zao kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kazi nzuri unayofanya Bungeni kwa kupambana na changamoto zinazojitokeza. Serikali ya Awamu ya Nne inakabiliwa na changamoto nyingi kwa mfano ukosefu wa umeme wa kutosha kwa matumizi ya viwanda, maji safi na salama, walimu na vifaa vya kufundishia, huduma za afya na kadhalika. Lakini ili hali ya maisha ya Watanzania iwe bora ni lazima kilimo chetu kinachoajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania kiwe chenye tija. Lazima mkakati wa kilimo kwanza na sasa *SAGCOT* utekelezwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya bidhaa za kilimo, mazao ya korosho, pamba na kadhalika yanauzwa yakiwa ghafi lakini matunda mengi kama embe, mananasi, machungwa na kadhalika yanaoza wakati wa msimu. Ipo haja ya kuhakikisha kuwa ili kufanyika kwa mapinduzi ya kilimo ni lazima viwanda vijengwe kwa haraka kama ilivyoelekezwa katika Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, *TASAF* ni mfuko wa maendeleo unaolenga kuwasaidia wananchi kupitia miradi midogo midogo wanayoibua. Hata hivyo pamoja na nia nzuri ya mfuko huo bado kuna changamoto nyingi zinazohitaji kupatiwa maelezo. Kwanza uhaba

wa pesa za miradi kiasi kwamba miradi mingi sio endelevu kwa mfano unaweza kutengeneza barabara ya changarawe na kuweka kifusi lakini ukakosa pesa za kushindilia kifusi hivyo kwa muda mfupi barabara kuharibika.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine na masharti magumu yanayowekwa katika matumizi ya pesa za *TASAF* asilimia 50 ya pesa zinazotolewa lazima zitumike kwa kuajiri wafanyakazi hivyo pesa za kununulia vifaa zinakuwa chache. Tatizo lingine ni kuwa ili mradi ukubalike lazima asilimia 50 ya wanakijiji waukubali. Jambo hili ni gumu hivyo mara nyingi wahusika hulazimisha hali ionekane kuwa wanakijiji wamekubali mradi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, Sera ya *D by D* uamuzi wa kupeleka madaraka kwa wananchi ni nzuri. Matatizo yaliopo ni kuwa Wizara zinazoandaa sera hazina nafasi ya kufuatilia na kurekebisha matatizo yanayojitokeza. Serikali inapaswa kuangalia upya sera ya *D by D* ili uwajibikaji kwa upande wa watendaji uwe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, malengo ya MMEM na MMES ni mazuri na mafanikio yanatia moyo. Lakini lengo la elimu lazima lilenge katika kutoa wanafunzi wanaoweza kuitumia elimu yao kwa kujitegemea badala ya kusubiri ajira Serikalini. Ni lazima mitaala yetu ilenge katika kuwakomaza wanafunzi katika elimu ya sayansi ili tutakapojenga viwanda tuwe na wataalam wazuri watakaoweza kufanya kazi humo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tuliomo humu ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuliotokana na uchaguzi wa mwezi wa Oktoba 2010. Wabunge wa Majimbo tumetokana na ushindi tulioupata baada ya kupigiwa kura wa wananchi husika wa Majimbo hayo.

Mheshimiwa Spika, kilichodhihirika katika uchaguzi huo ni upatikanaji wa wapiga kura kwa Wabunge baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilitumika sheria mbili tofauti. Kwa Tanzania Bara ilitumika Sheria ya Uchaguzi ya Tanzania na Tanzania Zanzibar ilitumika Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo Sheria hiyo inatumika kwa kuchagua Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, tofauti kubwa iliyopo katika sheria hizo ni upatikanaji wa wapiga kura. Sheria ya Uchaguzi Zanzibar inataka mtu ili aandikishwe kuwa mpiga kura lazima awe mkazi na kwa kutumia kipengele hicho wapo wananchi wengi ambao walishiriki chaguzi za mwaka 1995, 2000 na 2005 hawakupiga kura kwa uchaguzi wa mwaka 2010. Sheria ya Uchaguzi ya Tanzania haina kipengele hicho.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwa vile Wabunge hawa wapo katika Bunge moja walitakiwa wachaguliwe kwa Sheria moja. Je, Serikali inaahidi nini kwa Uchaguzi wa mwaka 2015 katika kuondoa dosari hiyo?

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kayanza Mizengo

Peter Pinda, pamoja na ile ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbogwe na Wilaya mpya ya Mbogwe niipongeze Serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kusogeza huduma za kiutawala kuwa karibu zaidi na wananchi, hongera sana. Serikali ya Awamu ya Nne imeweka historia isiyofutika ya kuanzisha Wilaya mpya ya Mbogwe pamoja na Mkoa mpya wa Geita.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali sana kwa kuwajali wananchi wake kwa kuwapatia huduma mbalimbali za kijamii zikiwemo za ujenzi wa barabara za lami na zile za changarawe, huduma za afya, elimu, maji, umeme na huduma zingine za mawasiliano kupitia Mkongo wa Taifa na kupunguza gharama za mawasiliano kwa njia ya *TEHAMA*. Serikali imefanya mambo mengi ya msingi ikiwemo mpango wa elimu katika ngazi mbalimbali ikiwemo elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ili Wilaya yetu mpya ipige hatua kwa haraka zaidi katika nyanja mbalimbali niiombe Serikali ifanye mambo muhimu ya msingi yafutayo:-

(a) Kuipatia umeme kwa haraka Wilaya yetu kupitia ufadhili wa Benki ya Afrika *(African Development Bank)* katika mradi wa *electricity* pamoja na wakala wa usambazaji umeme vijijini *(Rural electrification Agency - REA)* tunaomba Serikali ifanye haraka ili kweli ratiba ya kuipatia umeme Wilaya hii ifikapo mapema mwaka kesho.

(b) Serikali ifanye kila linalowezekana kuzipandisha daraja barabara mbili ndani ya jimbo letu kuwa za Mkoa na zihudumiwe na Wakala wa Babaraba nchini *(TANROADS)*. Barabara hizo ni ile ya Masumbwe, Luganga, Nyasato, Mbogwe, Ilolangulu, Bugalagala hadi Lutembela, Nyekonga, Ipalamosa, Nyakatungulu, Butengo, Lumasa na ile ya Geita, Bukoli, Ikina, Wigo, Ivumwa, Nyitundu, Bwendamwizo, Iboya, Bwelwa, Nanda, Nyanholongo, Katome hadi Ushirombo Wilayani Bukombe.

(c) Wilaya haijawa na *high school,* tunaomba shule za Masumbwe na Mbogwe zote za sekondari zipanuliwe kuwa na vidato vya tano na sita.

(d) Tunaomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuharakisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Mbogwe ili kutoa fursa kwa vijana waweze kupatiwa taaluma ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe.

(e) Huduma ya maji safi na salama ni muhimu kwa matumizi mbalimbali ya maisha ya kila siku ya mwanadamu pamoja na mifugo. Upo pia umuhimu wa kupanua huduma ya mabwawa yatakayotumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji na unyweshaji wa mifugo pamoja na ufugaji wa samaki.

(f) Bei ya zao la pamba ni zao la biashara katika Wilaya yetu ya Mbogwe, tunaiomba Serikali iongeze juhudi za kuyasimamia kwa karibu makampuni ya ununuzi

wa pamba ili yaweze kutoa bei nzuri kwa wakulima na kudhibiti uchakachuaji wa mizani ya kupimia pamba ili wakulima wasipunjwe.

(g) Naiomba Serikali ione uwezekano wa kufungua soko la mahindi katika maeneo ya Jimbo la Mbogwe na Bukombe ili kuwasaidia wakulima wa mahindi na mpunga kuwawezesha wanunuzi wengi zaidi kufika maeneo haya hatimaye bei za mazao haya iweze kupanda kwa kufuata kanuni za kiuchumi za utashi na ugavi *(supply and demand).*

(h) Tunaipongeza Serikali kwa umakini wake wa kujua mahitaji ya wananchi wetu wanaokabiliwa na uhaba wa chakula uliosababishwa na ukame, kwa kutoa chakula cha msaada.

(i) Habari za utalii pia katika Hifadhi za Kigosi na Muyowosi ili kukuza pato la wananchi katika Wilaya yetu.

(j) Katika vipaumbele vya Serikali vya miundombinu, barabara, reli, madini, maji na afya kwa maana ya kuwa na zahanati kwa kila kijiji, vituo vya afya kwa kila kata.

(k) Tunaweza kuanza kujipanga kwa sasa kuwa na Mamlaka ya Utafiti wa Madini nchini kwa kutumia wataalam toka nchi zilizoendelea kwa makubaliano kama yanayofanya makampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu ya *GGM, Kahama Mine, Resolute* na Nyamongo.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi katika kijiji cha Ihelele ndiyo chanzo cha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama. Vile vile Serikali ina mpango wa kufikisha maji haya Nzega na Tabora. Niiombe Wizara ya Maji kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iharakishe kuvipatia vijiji vya Ihelele, Nyamhomango, Mkariku, Isesa na vingine ambavyo vinazunguka chanzo hiki cha maji vipatiwe maji. Kwa kweli haieleweki pale maji yanapotoka wanakijiji hawana maji kabisa kwa binadamu na mifugo yao.

Kwa umuhimu huo huo barabara inayotoka Mwanangwa kuelekea kwenye chanzo hiki cha maji itengenezwe kwa kiwango cha lami kwa sasa barabara hii inapaswa kupitishwa magari yasiyozidi tani 10 lakini magari yanayopeleka dawa na vifaa vingine kwenye chanzo hiki yanabeba uzito zaidi ya tani 10 na kusababisha barabara hii kuharibika mara kwa mara.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imeelezea mchakato mzima wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Hotuba yake pia imetoa maelezo ya hali ya kisiasa pamoja suala la mvurugano wa Uchaguzi wa

mwaka 2010 na kadhalika. Hali ya uchumi wa nchi pamoja na vipaumbele vya Serikali katika sekta za nishati, viwanda, maji na rasilimali watu vimeelezwa katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Ulanga Magharibi wameniomba niwasemee kero zao kubwa zinazowakabili, miundombinu hususan daraja la Mto Kilombero, huduma za benki, nishati ya umeme vijijini na kuwepo na Wilaya. Kero zote hizi Mheshimiwa Rais ameahidi kuzitatua/kuzimaliza katika kipindi chake hiki cha miaka mitano na ahadi hizi alizitoa katika kampeni zote 2010.

Mheshimiwa Spika, kero ya kivuko/daraja la Mto Kilombero sasa linaendelea kuwa sugu ukitilia maanani kuwa kivuko kilichopo/kinachotumika kimechoka/kimechakaa ambapo hutoa huduma chini ya kiwango chake na hivyo husababisha kusimamisha huduma zake mara kwa mara na kusababisha usumbufu kwa Wanajimbo la Ulanga, mfano mwezi Aprili, 2011 Wilaya ya Ulanga kwa muda wa siku tatu ilikuwa kisiwani ambapo ilikuwa hakufikiki toka sehemu zingine za Tanzania kutokana na kuharibika kwa kivuko hicho chakavu. Wananchi wa jimbo wanaomba hatua za dharura zifanyike kwa kufanya ukarabati mkubwa wa kivuko hicho wakati jitihada za muda mrefu zikifanywa kwa kuanza ujenzi wa daraja. Pia Serikali itoe tamko ni lini hasa daraja la Mto Kilombero litaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ulanga Magharibi ni mojawapo la wazalishaji wakubwa wa zao la mpunga nchini. Jimbo linazalisha karibu tani 200,000 za mpunga kwa mwaka na ni tegemeo kubwa la mchele katika masoko ya Morogoro na Dar es Salaam. Wakulima sasa wameshaanza kilimo cha biashara lakini wanaathirika na upungufu wa huduma za kibenki. Jimbo zima halina benki na mbadala wake huduma hizo zinapatikana Mahenge Makao Makuu ya Wilaya ya Ulanga ambapo ni mbali sana na jimbo. Kukosekana kwa benki nako kunaathiri huduma za jamii kama vile afya na elimu pale watumishi wanapotumia muda wa siku nne hadi tano kufuata mishahara benki Mahenge huku wakiacha zahanati/shule bila huduma. Wanajimbo wanaomba uangaliwe uwezekano wa kupatiwa huduma za benki ikiwezekana hata zile za *mobile* angalau kwa mwezi mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais kwa jimbo ni kuwa Wilaya kamili, kwa kiasi kikubwa kitatoa matumaini/ufumbuzi wa kero za benki na huduma zingine muhimu, kwani itakuwa kichocheo kikubwa kupelekwa huduma hizo Makao Makuu ya Wilaya kama zinavyoainishwa katika sera mbalimbali za huduma za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010. Nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa kuteuliwa na Rais na kuthibitishwa na idadi kubwa ya Wabunge kuwa Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa ushindi wa kishindo na kuchaguliwa

kwako kuwa Spika wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawapongeza Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote. Nawashukuru pia wananchi wote wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Naahidi kuwapatia utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo ya kilimo na hasa zana za kilimo (ukurasa wa 22); kilimo cha umwagiliaji (ukurasa wa 25) na mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Dodoma ni moja kati ya mikoa yenye ukame mkubwa Tanzania pamoja na bidii kubwa ya kazi ya wenyeji wa asili wa Mkoa huu, watu wetu wamekabiliwa sana na janga la njaa na umaskini usio na kikomo katika maisha yao. Ili kuwakwamua wananchi wetu na umaskini mkubwa walio nao, napendekeza haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, upatikanaji wa zana bora za kisasa za kilimo (ukurasa wa 22). Ingependeza kama Serikali katika kutoa mikopo ya matrekta, kwanza wangeangalia vijiji. Utaratibu mzuri ungeweza kufanyika kuhakikisha kuwa kila kijiji kinakopeshwa angalau trekta moja, bado wakalipa kama kijiji kidogo kidogo kutokana na mazao mbalimbali watakayopata, hasa yale ya biashara, mfano karanga, alizeti, ufuta na zabibu. Matrekta yataleta mapinduzi ya kilimo vijijini. Kabla mvua hazijanyesha, matrekta yatatifua udongo *(harrowing)* na baadaye mbegu zitapandwa vizuri kwa mistani *(sowing)* ikifuatiwa na palizi *(weeding)* na mwisho wananchi watapata mavuno mengi na safi hata pamoja na mvua kuwa kidogo. Tendo la matrekta kutifua udongo *(harrowing),* itasaida sana mvua kidogo kuzama ndani ya ardhi, na unyevu huo wa maji utasaidia mimea kukua kwa haraka na wananchi kupata mavuno mazuri.

Pili, kilimo cha umwagiliaji (ukurasa wa 22) pamoja na umuhimu wa matrekta, kilimo cha umwagiliaji nacho kitaleta mapinduzi makubwa sana ya kilimo katika miji au mikoa ya ukame ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Dodoma Mjini. Wilaya ya Dodoma Mjini ina utajiri mkubwa sana ya mabwawa na mito, lakini mabwawa na mito yote hii ni ya msimu *(seasonal dams and rivers),* mfano mabwawa ya Vikonje (Kata ya Mtumba, Bwawa la Nkulabi (Kata ya Mpunguzi), Bwawa la Mbabala (Kata ya Mbabala), Bwawa la Mbalawala (Kata ya Mbalawala), Bwawa la Makutupora (Kata ya Makutupora), Bwawa la Zuzu (Kata ya Zuzu) na Bwawa la Mkalama (Kata ya Mkalama). Kama mabwawa haya yatatolewa tope na kupanuliwa na kama mito mingi ya Dodoma *(seasonal rivers)* vitawekewa makinga maji, Dodoma itakuwa na maji mengi wakati wote, wakati wa masika na wakati wa kiangazi na hii itasaidia sana katika kilimo cha mboga mboga na nyanya, ili tuweze kukwamua wananchi wetu na umaskini mkubwa walio nao.

Tatu, mifugo na uvuvi (ukurasa wa 25). Mkoa wa Dodoma ni moja kati ya mikoa yenye ng'ombe wengi Tanzania, ng'ombe hawa wanahitaji majani, majosho na maji ya kunywa ya kutosha. Vijana wetu pia wamekwisha ona umuhimu wa kazi ya uvuvi na

faida zake. Wanavua samaki wengi katika Bwawa la kudumu la Hombolo lililopo katika Kata ya Hombolo na samaki hao karibu sasa wanaisha kwani wavuvi wanaelekea kuwa wengi kupita kiasi katika bwawa hilo. Kama mabwawa mengi yatapanuliwa katika Kata mbalimbali nilizozitaja na kisha makinga maji mengi pia yakawekwa katika mito yetu ya msimu, maji haya yatasaidia kilimo cha umwagiliaji na pia kunyweshea mifugo yetu ambayo hukonda na kufa kwa sababu ya kukosa maji, lakini pia mabwawa na mito yenye maji mengi yatakuza shughuli za uvuvi na kuwasaidia wenyeji wa Jimbo la Dodoma Mjini na Mkoa kwa ujumla kuwa na shughuli nyingi za kufanya za kiuchumi (kilimo, mifugo na uvuvi) mwaka mzima na kuwaondolea umaskini mkubwa unaowakabili leo hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa nafasi ya kuchangia moja kwa moja nawasilisha mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ni injini ya maendeleo ya Taifa. Ujumla wake ni muhimu katika kusukuma Bajeti yetu na Mpango wa Maendeleo kuanzia ule wa mwaka mmoja, miaka mitano mpaka lile lengo letu la mwaka 2025. Hiki ndicho chombo cha utekelezaji wa mipango na Bajeti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa mambo ambayo hatufanyi vizuri katika harakati za kufikia lengo letu. Ujenzi wa Taifa lenye watu wa uchumi wa kati *(MIC).* Jambo la kwanza ni uwajibikaji. Tunapaswa kujipanga upya kwa kuangalia majukumu wanayopewa watendaji wetu kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa mpaka Wizara. Tuwape majukumu tukizingatia malengo yetu sambamba na majukumu tuwape mamlaka. Hii ni nguvu ya kuhakikisha kuwa majukumu aliyopewa mtendaji yanatekelezwa, katika hali hiyo mtendaji atakiwe kuonyesha ufanisi kinyume chake awajibishwe. Nahimiza dhana ya *authority, responsibility and accountability.*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni ushirikishwaji wa umma katika maendeleo. Uzoefu katika ujenzi wa zahanati na sekondari za kata umedhihirisha fursa zilizomo katika nguvu ya wananchi. Wananchi wakishirikishwa vizuri wanaweza kuchangia bidhaa zinazopatikana katika maeneo (vionwa). Tuna mapungufu makubwa katika eneo hili, watendaji hawafanyi vizuri sana katika eneo hili. Hawafuatilii watu wote, hawatoi stakabadhi, hawahamasishi na hawatoi taarifa ya makusanyo na matumizi. Baya zaidi utendaji wa miradi hauonyeshi *value for money.*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni dhana ya uwekezaji. Uwezeshaji na uwekezaji umewekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Jukumu hili ni muhimu lakini juhudi na ubunifu unatakiwa ili wananchi waone mantiki ya dhana hii ambayo kimsingi ni nzuri.

Ushauri wangu ni kwa kuanzia na mazao ambayo tunafanya vizuri kama mahindi, ofisi husika itumie mahusiano yetu na nchi zilizotuzunguka ili kupata masoko huko.

Iwapo mpango maalum wa kufikia masoko hayo utafanyika kwa kupunguza watu wa kati, mwananchi (mkulima) atafaidika na kushawishika kuzalisha zaidi. Nchi za Japan, India na China kwa kutaja baadhi wote wametumia njia hiyo (MITI). Dhana hii inapata nguvu hasa kwa mazao ya chakula kwa kuzingatia ukweli kuwa kuanzia mwaka 1999 mpaka leo nchi zote zilizotuzunguka zimekuwa na mahitaji makubwa ya chakula.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ni utendaji wa pamoja *(team work).* Dhana hii inaendana na mfumo wa watendaji walio wengi wanapendelea kufanya kazi wakiwa ofisini na hawajali wananchi. Watendaji wengi wanapendelea mfumo wa kuhodhi ofisi, mimi ndiye fulani, mimi nimesema, hakuna wakupinga maamuzi yangu, hakuna *team work.* Bila kuingilia majukumu na mamlaka ya mtendaji, watendaji, viongozi na wananchi wanaposhirikiana utekelezaji wa majukumu yetu haya inakuwa rahisi. Tunayo hazina kubwa ya wahisani wengi, wengi wao wakiwa Watanzania wenzetu ambao wanapenda kushiriki kwenye maendeleo ya Vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa. Tatizo ni kuwa rasilimali hii inahitaji timu ya pamoja na kuwaalika. Lakini hata shughuli za kuhamasisha wananchi katika shughuli za maendeleo kauli na nguvu ya pamoja inahitajiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano ni mwitikio wa wito wa wananchi. Tunayo mapungufu katika kuitikia wito au maombi ya wananchi katika kukabili majukumu yao. Hii ni sehemu mojawapo ambayo tunahitaji kufanya marekebisho makubwa. Tuna tatizo la *customer service.* Wananchi wanajiuliza zaidi ya mara tatu kabla ya kuleta matakwa au shida zao katika ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika jambo la sita, ni kuimarisha sekta ya elimu upande wa walimu. Ipo haja ya kuiangalia kwa macho matatu sekta ndogo ya walimu. Vyuo vya Elimu viimarishwe kwa kupewa walimu mahiri, miundombinu na vifaa vya kufundishia. Baada ya hatua hiyo walimu wanafunzi watakaoteuliwa wawe wenye uwezo wa kuyamudu masomo ya ualimu na pia wawe na wito na taaluma hiyo. Tuamue sasa ualimu isiwe sekta ya walioshindwa kwa mtindo wa kuwasaili upya walimu na mafunzo ya mara kwa mara walimu wapewe leseni na mwalimu mwenye leseni ndiye aruhusiwe kufundisha. Tutakapokuwa tumejitosheleza kwa walimu wenye leseni hata wakifundisha shule binafsi wapewe sehemu ya mshahara wa Serikali.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali za nchi yetu. Aidha, napenda pia kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, kwa kuimudu vema Wizara yake. Ama kweli upele umepata mkunaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara Mkoani Mtwara mwaka 2009 akiwa Wilayani Tandahimba, Kijiji cha Malamba aliahidi kusaidia mradi wa maji wa Bwawa la Malamba na kufunga mabomba kutoka bwawani hadi kijijini. Jambo hili hadi sasa

halijatekelezwa. Ni vema sasa jambo hili likamalizwa. Aidha, Wilaya ya Newala na Tandahimba zina shida kubwa ya maji. Ilani ya CCM ya 2010 – 2015 imeweka wazi haja ya kufanya ukarabati wa mradi wa *Makonde Water Supply Authority*. Nashauri jambo hili lianze sasa na wananchi waone utekelezwaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri mpango wetu wa kila tarafa kuwa na shule ya kidato cha tano na sita uende sambamba na mabweni ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kuanzia sasa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote waliopata udahili wa Chuo/Vyuo Vikuu kupata mikopo bila kujali amepata kiwango gani cha ufaulu kwani wale walio wengi wenye *division three* wamesomea vijijini ambako vifaa na zana za kusomea ni vichache lakini pia wazazi wao ni wenye uwezo duni.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya nchi yetu ina tatizo kubwa la wataalam wa afya. Ni vema Serikali ikaona na kuanzisha mpango kamambe wa kuongeza wanafunzi wa eneo/kada za afya.

Mheshimiwa Spika, Tandahimba ipo kati ya Mtwara na Tandahimba. Ni wazalishaji wakubwa wa zao la muhogo kama chakula na korosho kama zao la biashara. Lakini tatizo kubwa ni mawasiliano (usafiri) hasa nyakati za masika. Barabara ni mbovu na inayogharmu sana kuikarabati kila baada ya msimu wa mvua. Ni vema basi mpango wa kufanya barabara hiyo kuwa ya lami uanze kwa kasi kama ilivyo kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015.

Mheshimiwa Spika, mwisho Ofisi ya Waziri Mkuu imalize malalamiko ya wananchi na Wabunge wa maeneo ya korosho kuhusu fedha za *export levy* kupelekwa moja kwa moja kwa Wilaya zinazolima korosho kama *Finance Act 2006* inavyoelekeza. Hali ya sasa ya Bodi ya Korosho kupelekewa fedha hizo licha tu ya kuwa na dalili ya kutowajibika, lakini kuna dalili za rushwa, Halmashauri zinapata hoja za ukaguzi na ucheleweshwaji wa pembejeo hizo kwa wakulima kwani mzunguko ni mrefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri inayoeleweka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia na kushauri kama ifuatavyo; kwanza naipongeza Serikali kwa kubuni mpango wa kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(SAGCOT)* ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo hasa kwa mazao ya chakula, matunda, mboga na kadhalika kwa kuwa mpango huu ni wa muda mrefu, nashauri iwekwe mipango itakayosimamiwa kimkakati. Kwa kuwa tunalenga kuongeza chakula nchini, kuondoa kabisa tabia ya kuombaomba chakula kutoka nje.

Ni muhimu sana pembejeo na hasa mbolea sasa ielekezwe kwenye Mikoa hiyo badala ya kuisambaza hata kwenye mikoa yenye ukame ambako hakuna mvua hata

kidogo. Kutakuwa na umuhimu wa kuwaelimisha viongozi na wananchi wa siasa na Serikali malengo mazuri ya Serikali. Nchi iamue kuwa na kuyatambua maeneo hayo yenye mvua za uhakika katika uzalishaji wa mahindi, mpunga na kadhalika kwa kuwa uzalishaji huo ni muhimu, tuanze haraka kuhamisisha ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza thamani ya mazao hayo katika kuweka *linkage* ya kilimo na viwanda. Hivyo basi ni matumaini yangu kuwa katika Mkoa wa Mbeya viwanda kama vya kusaga mahindi, kukoboa mpunga, kusindika maparachichi, kutengeneza juisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, barabara vijijini ziimarishwe ili mazao hayo yaweze kusafirishwa kwa urahisi na maafisa ugani waandaliwe kwa wingi ili wasambazwe katika vijiji vyote.

Pili, elimu ya msingi, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali ya kuipanga elimu ya msingi kuwa ni lazima kwa kila Mtanzania, bado kuna matatizo mengi yanayoikumba elimi hiyo. Uandikishaji wa lazima bado ni tatizo. Bado kuna watoto wengi hasa katika maeneo ya wafugaji hawaandikishwi kusoma. Nashauri, Serikali za vijiji ziwajibike kuona kuwa hakuna mtoto anayebaki nyumbani; la sivyo Taifa linarudi nyuma kushughulikia wananchi wasio na elimu.

Kuhusu ukosefu wa madawati, kwa kuwa upungufu wa madawati mashuleni, kuna haja ya wazazi kuhamasishwa kuchangia utengenezaji wa madawati. Si busara kuendelea kujenga madarasa na watoto wanakaa chini si sahihi.

Suala la elimu ya sekondari, elimu ya wasichana kwa kuwa bado kuna wimbi kubwa la wasichana kupata mimba wakiwa wadogo, utaratibu wa kutoa elimu ya afya ya familia uendelezwe kwa nguvu. Vilevile, ujenzi wa mabweni ya wasichana usimamiwe kikamilifu, lakini pia hata wananchi wenye fedha, ni muhimu wahamasishwe kujenga *hostels* karibu na shule za sekondari ili wanafunzi waweze kupangishwa na kulelewana vizuri na walimu wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na wanatakia heri utekelezaji mzuri.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na ninapenda kumtakia mema katika uadilifu wake na katika uwajibikaji kwani pamoja na mapungufu ya kibinadamu bado ameendelea kujenga rekodi ya uadilifu hivi ndivyo hata Mwalimu Nyerere alivyopata kuwa bora. Upatikane na mapungufu yoyote lakini sio uadilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza hoja ya kuitaka Serikali iangalie namna tunavyorudi nyuma katika kukabiliana na umaskini wa kipato kwani sekta zinazobeba watu wengi zinaanguka. Mwaka 2008 kilimo kilikuwa asilimia 4.6 lakini mwaka 2010 kimekuwa asilimia 4.2, sekta ya uvuvi mwaka 2008 ilikuwa asilimia 6 lakini mwaka 2010 sekta hii imekuwa kwa asilimia 1.5, sekta ya mifugo mwaka 2005 ilikuwa asilimia 4.4, lakini mwaka 2010 ilikuwa asilimia 3.4. Hiki ni kielelezo kuwa tumeshindwa

kukomboa kilimo. *REPOA* wamefanya utafiti kuwa tukikuza kilimo kwa asilimia 10 kwa miaka 10 mfululizo tutapunguza umaskini kwa asilimia 50, nashauri tuwekeze huko. Bado wavuvi wanatumia zana duni. Nashauri tuanzishe bodi ya mazao ya kilimo itakayosimamia uratibu wa mazao ya uvuvi, mifugo na mazao.

Nashauri tutumie vizuri Ziwa Tanganyika tuanzishe bodi itakayosimamia soko la mazao ya ziwa hili. Tuna *species 260* lakini tunavua *spicies 6* tu. Hali ya wavuvi Kigoma ni mbaya, bado wavuvi hawajapangwa waweze kuendesha majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Ukanda wa Kusini Jimbo la Kigoma, Jeshi la Polisi lihakikishe ulinzi badala ya wavuvi kujitolea kwa kuchangishana kulipa wanajeshi kusaidia ulinzi, wavuvi hawa wanapaswa kupewa haki ya usalama wanapokuwa wanavua ziwani.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha michikichi kifanyiwe mapinduzi. Nashauri tuanzishe bodi ya zao hili la michikichi ili tuendeshe kilimo bora cha michikichi kwa viwanda vya sabuni, mafuta ya kula, mafuta mazito ya kulainisha mitambo na kadhalika. Tunalo eneo kubwa la michikichi lakini bado kilimo ni cha ujima.

Kuhusu umeme, *vision 2025* inazungumza tujenge Taifa la tabaka la kati 2025, njia ya kubeba wote wafike huko ni kufanya mapinduzi ya kilimo na biashara za kati, ndogo na kukukuza ajira. Lakini mapinduzi hayo yanategemea umeme. Tukiboresha uwezo wa kuzalisha umeme japo *3000 – 5000 MW* zitachochea mapinduzi ya viwanda. Mapinduzi ya viwanda yataongeza ajira na kupanua sana soko la mazao ya kilimo. Umeme utachochea uvuvi, kilimo cha mazao na hata ufugaji. Umeme utatoa soko na kuongeza tija ya uvuvi, mifugo na mazao.

Mheshimiwa Spika, Kigoma katika Wilaya mpya ya Uvinza tumegundua *limestone,* utafiti uliofanyika umebaini kuna *reserve* ya kutosha kuzalisha tani milioni moja za saruji lakini inahitaji *24 MW* wakati Mkoa mzima wa Kigoma unazalisha *11MW*. Ni kwa mfumo mzima huu tunaweza kutafsiri ukuaji wa uchumi kuweza kutafsiri maendeleo ya uchumi *(economic growth to ecomonic development).* Naomba sana Wilaya mpya ya Uvinza tupate umeme kwa kuwa pia kuna kiwanda cha chumvi kilichofungwa kwa kukosa umeme na ni hapo hapo kuna *limestone* yenye kutengeneza chokaa na saruji. Kwa sasa wafanyabiashara wa kati wanatengeneza chokaa kwa teknolojia duni sana.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa matumizi. Ninashauri Serikali iongeze msukumo katika kusimamia maoni ya *CAG* na katika hili naomba Waziri Mkuu ahakikishe hesabu za vyama vya siasa zinakaguliwa kwa kuwa ruzuku ya chama ni kodi za walipa kodi ambazo ni sharti *CAG* akague hesabu za matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwazi katika Bajeti na malipo, bado mfumo wa Bajeti haupo wazi. Bajeti bado inatengenezwa kuhakikisha haieleweki vizuri, lakini pia nashauri malipo yote ya posho na mishahara kwa viongozi wote ziwe wazi kwa kuwa ni pesa za wananchi, ni kodi zao ambazo ni muhimu ieleweke, nchini Kenya posho na

mshahara wa kuanzia Rais mpaka Wabunge vipo wazi. Uwazi unaondoa utata. Uwazi unafuta manung'uniko yasiyo ya lazima, tuige hilo.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa chumvi Uvinza, huu mgodi ulibinafishwa tangu mwaka 1998 lakini mpaka leo wafanyakazi wa mgodi huu hawajapata mafao yao. Tangazo la *PSRC* wakati wa ubinafsishaji lilitangaza kulipa mkono wa kwaheri, leo ni zaidi ya miaka kumi wafanyakazi hawajalipwa hati hiyo. *CHC* ilieleza kuwa kwa makampuni ambayo hayakuwa yanapeleka michango kwenye Mifuko ya Hifadhi *CHC* ingefidia. Mpaka leo wafanyakazi wa mgodi huu hawajalipwa, walipewa pesa kidogo sana ambazo mgodi huu ulikuwa umelipa kwenye Mifuko ya Hifadhi. Ile fidia ya miaka ambayo mgodi haukuchangia wafanyakazi hawajalipwa.

Mwisho naomba Serikali iende kuchunguza wizi wa mitambo mikubwa ya mgodi wa chumvi uliokuwa ukizalisha chumvi kwa umeme. Leo kumefungwa, wameng'oa mitambo yote na wawekezaji hawa wanauza mitambo nje.

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama, hali ya Mkoa wa Kigoma ni mbaya kiusalama. Tuna mpaka mrefu sana na nchi za Congo, Burundi ambao wote uko wazi, huu ni Mkoa unaopakana na nchi ambazo hali yake kiusalama sio nzuri. Nasikitika kuona Bajeti ya Polisi Mkoa wa Kigoma imebaki kuwa ndogo sawa na mikoa ambayo haina hatari ya usalama kama Kigoma. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atazame hili kwani tumepata kuzungumza siku nyingi na aliahidi kutoa nafasi ya kutosha kuhakikisha tunapata polisi wengi zaidi, vifaa vingi zaidi, nyenzo za kazi za kipolisi za kutosha. Hii itafanyika kwa umaalumu wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Barabara, nasikitika kuona Mkoa wa Kigoma ndio umepata pesa kidogo za mfuko wa barabara kuliko Mkoa wowote Tanzania. Nimetazama katika jedwali Kigoma kuanzia mwaka 2005 – 2010 tumepata shilingi bilioni 8.7 tu mkoa ambao ni mkubwa na wenye barabara duni kabisa ndio huo unakua wa mwisho. Naomba Waziri Mkuu atazame vizuri jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya maji, pamoja na jimbo la Kigoma Kusini kuwa na vyanzo vya kutosha vya maji, bado maji ni tatizo sugu. Kata za Mteyo, Simbo, Sigunga, Kalya zinakabiliwa na tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Spika, naomba jimbo hili liangaliwe katika maji kwani nusu ya jimbo hakuna maji.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa nafasi hii adimu uliyonipa niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Rukwa kwa kupitia UWT kwa kura nyingi walizonipa na kuniwezesha kuwa Mbunge, ninawaahidi kuwa niko pamoja nao na sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mwenyezi Mungu kunijalia uhai, afya na nguvu ili niendelee kuwatumikia wananchi wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze watoto wangu Evelyne na Joyce ambao wameendelea kunivumilia na pia kuni-*support* kipindi chote ambacho nipo mbali nao nikiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuridhia uanzishwaji wa Mfuko wa Mahakama, mfuko ambao utaongeza uwezo wa kiutendaji na kuleta ufanisi katika Mahakama zetu nchini na hasa Mahakama za Mwanzo na za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania ni utaratibu kuwa kila Wilaya iwe na hakimu angalau wanne au watano kwa kila Mahakama ya Wilaya na pia kuwa kila Kata iwe na Mahakama ya Mwanzo yenye angalau Mahakimu watatu au wanne.

Mheshimiwa Spika, taratibu hizi zimekuwa hazifuatwi na taratibu hizi zimewekwa na Serikali ili kuwafikishia wananchi huduma za mahakama pale walipo, kutokuzingatiwa kwa taratibu hizi kumepelekea wananchi wengi hasa walio vijijini kutopata haki zao hasa za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa una Wilaya za Sumbawanga na Nkasi na hivi sasa Wilaya mpya ya Kalambo. Wilaya zote hizi katika Mkoa wa Rukwa una Kata 64 Mahakama ya Wilaya moja, Mahakimu wa Wilaya, lakini ina Mahakama za Mwanzo saba tu na Mahakimu nane tu, hii ina upungufu wa Mahakama ya Wilaya moja (Nkasi), Mahakimu wa Wilaya nne ina upungufu wa Mahakama za Mwanzo 53 na Mahakimu 56. Unaweza kuona ni jinsi gani wananchi wa Mkoa wa Rukwa wasivyopata haki zao za kisheria hasa wanapokuwa ni lazima wahudumiwe na mahakama.

Mheshimiwa Spika, Jedwali hapa chini linajieleza:-

A. Wilaya ya Sumbawanga: Idadi ya kata zilizopo 47, Mahakama ya Wilaya iliyopo 1, pungufu 0, Mahakimu wa Wilaya waliopo 4, pungufu 1, Mahakama za mwanzo zilizopo 5, pungufu 42, Mahakimu wa mahakama za mwanzo waliopo 10, pungufu 37.

B. Wilaya ya Nkasi – yenye Majimbo ya Nkasi Kaskazini na Nkasi kusini) : Idadi ya kata zilizopo 17, Mahakama ya Wilaya iliyopo 0, pungufu 1, Mahakimu wa Wilaya waliopo 0, pungufu 4, Mahakama za mwanzo zilizopo 2, pungufu 15, Mahakimu wa mahakama za mwanzo waliopo 2, pungufu 15.

C. Mkoa wa Rukwa - *Summary:* Idadi ya kata zilizopo 64, Mahakama ya Wilaya iliyopo 1, pungufu 1, Mahakimu wa Wilaya waliopo 4, pungufu 4, Mahakama za mwanzo zilizopo 7, pungufu 57, Mahakimu wa mahakama za mwanzo waliopo 12, pungufu 52.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo hapo juu Mkoa wa Rukwa unahitaji Mahakama ya Wilaya moja zaidi (Nkasi), Mahakimu wa Wilaya nne (Nkasi), Mahakama za Mwanzo 57 na Mahakimu wa Mahakama za mwanzo 52 ili wananchi wa Mkoa wa Rukwa wapate huduma za kisheria zinazotolewa na mahakama kwa sababu washtakiwa wengi wanaopata rufaa kutoka Mahakama za Mwanzo na pia walalamikaji hukata tamaa na kuachilia kesi zao *(surrender).* Hivyo ni muhimu mahitaji ya Mahakama na Mahakimu kwa ngazi za Wilaya za mwanzo yakazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, pia huwa ni usumbufu kwa hakimu wa Wilaya kutoka Sumbawanga kwenda kusikiliza kesi Nkasi na kurudi Sumbawanga kila anapohitajika na Mahakama za Mwanzo hazina mahabusu, hivyo kila baada ya kesi mahabusu hao hulazimika kupelekwa mahabusu ya Sumbawanga Manispaa kwa ajili ya matunzo ni usumbufu na *risk.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai yangu kuwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa wana haki ya kujua/kuelimishwa juu ya sheria mbalimbali zinazowazunguka kama vile Sheria ya Ndoa (hususan mirathi), Sheria ya Ardhi, Sheria ya Mikopo na Sheria nyinginezo.

Lakini pia waelimishwe kuhusu haki za binadamu, hii itawapelekea kuzifahamu sheria na hivyo kukwepa uvunjaji wa sheria, wananchi hawatafungwa jela hovyo hovyo kwa vile watayakwepa makosa yaliyo mengi, lakini pia hawatakubali kuonewa kwa vile watakuwa wamezijua haki zao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika sekta ya afya magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifo vya wajawazito kabla, wakati na baada ya kujifungua pia vifo vya watoto wachanga vimepungua lakini bado changamoto nyingi zimeendelea kujitokeza. Vifo vinavyotokana na uzazi vimepungua kutoka 578 kwa vizazi hai 100,000 mwaka 2004/2005 mpaka 454 kwa vizazi hai 100,000 mwaka 2009/2010. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 68 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2004/2005 mpaka 51 kwa vizazi hai 100 mwaka 2009/2010. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 112 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2004/2005 mpaka 81 katika vizazi hai 1000 mwaka 2009/2010. Asilimia ya watoto chini ya miaka mitano waliokuwa wamedumaa kwa matatizo mbalimbali ilishuka kutoka 38 mwaka 1999 mpaka 16.5 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, idadi ya vituo vya tiba *(health facilities)* vinavyotoa huduma ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto *(PMTCT)* viliongezeka kutoka vitano mwaka 2004 mpaka 3,626 mwaka 2009 Desemba hii ikiwa ni asilimia 78.6 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya ya uzazi nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyotajwa hapo juu yanatokana na juhudi za sekta ya afya na watumishi wote katika sekta ya kinga, tiba lakini pamoja na tafiti na

miradi mbalimbali ndani ya sekta ya afya ambayo imekuwa ikifanyika kwa kushirikiana na wafadhili lakini na wananchi pale walipokuwa wameshirikishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado zilikuwepo changamoto mbalimbali nyingi kwa mfano mdogo tu ni kiwango zaidi ya asilimia 50 ya wanawake walio katika umri 19 aidha, wana ujauzito au tayari wananyonyesha watoto hii huongeza tatizo au huwaweka katika hali tete (vulnerable) ya kupata matatizo au magonjwa yanayohusinana na Afya ya Uzazi.

Mheshimiwa Spika, taarifa niliyotoa hapo juu inatokana na taarifa iliyotolewa katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya ina upungufu mkubwa wa watumishi wa kada zote hasa wenye taaluma katika idara za kinga na tiba, tatizo hili limekuwa sugu wakati kila mwaka watumishi hawa huhitimu kutoka vyuo mbalimbali kwa viwango vya cheti, stashahada, stashahada ya juu na hata shahada mbalimbali kama madaktari, wauguzi, mafundi maabara, wafamasia, mionzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, imeonekana kuwa wahitimu hawa mara baada ya kuhitimu wachache huenda kufanya kazi katika maeneo waliyopangiwa lakini wengi hukimbilia nchi za nje au sekta binafsi wakifuata mafao mazuri.

Mheshimiwa Spika, natoa rai yangu kuwa Serikali ingeliangalia suala hili. Watumishi wapewe mishahara na posho stahili za kutosha ili kukimu maisha, watumishi wapewe motisha *(incentives)* mbalimbali ikiwa ni pamoja na usafiri, nyumba na mahali pa kazi pawe na mazingira rafiki, watumishi wapandishwe vyeo kila baada ya miaka mitatu kama taratibu zinavyosema siyo kufanya kazi kwa miaka nane hadi kumi bila kupandishwa cheo, pale *OPRAS* isipojulikana watumishi waelimishwe na wajaze, *OPRAS* zitathiminiwe na wanaostahili kupandishwa vyeo wafanyiwe hivyo, si kama ilivyo sasa, watumishi wanakufa moyo wa kufanya kazi na hali hiyo inawasukuma hata kuchukua rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Medical Stores Department (MSD),* nawapongeza na kuwapa pole kwa kazi kubwa ya kununua na kusambaza dawa na vifaa tiba kwa nchi nzima ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba Serikali iwapunguzie mzigo mkubwa huo *MSD* aidha, kwa kuongeza chombo kingine kitakachotoa huduma kama za *MSD* ili kuwarahisishia kazi *MSD* ambao wanaelekea kuelemewa na kazi hiyo ya kununua na kusambaza dawa na vifaa vya tiba kwa ajili ya hospitali zote za rufaa, za mikoa, za Wilaya, vituo vya afya na zahanati hapo hapo vituo vya tiba *(health facilitates)* za binafsi, vya dini, vya mashirika na kadhalika, vyote vinaitegemea *MSD* hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi dawa na vifaa tiba vinapoagizwa *MSD* tuseme unapoagiza *items* 100 za dawa/vifaa lakini utapewa *items* kama nane au kumi tu nyingine

zote huwa *out of stock (O/S)* na inaweza kurudia maagizo na tena mkapewa chache lakini nyingi huwa ni *o/s,* hii husababisha upungufu mkubwa wa dawa na vifaa tiba na kusababisha usumbufu kwa wagonjwa na hata vifo hasa pale ambapo mgonjwa anapokuwa amezidiwa na kukosa matibabu kwa vile dawa/vifaa havikupatikana kutoka *MSD.*

Mheshimiwa Spika, hali hii mara nyingi imepelekea wauguzi/madaktari kuwaelekeza wagonjwa kwenda kununua dawa/vifaa kwenye *pharmacy* za watu binafsi kwa walio na uwezo, lakini kwa makundi yaliyosamehewa kama vile watoto, wajawazito, wazee, wafungwa na wenye magonjwa sugu kama vile sukari, UKIMWI, shinikizo la damu na kadhalika wamekuwa hawapati dawa kwa bure kama sera na maelekezo ya Serikali yanavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, sheria na taratibu za manunuzi ya umma *(Procurement Act),* nayo kwa namna fulani imekuwa ikichangia katika kusababisha vifo kwa wagonjwa. Kama nilivyosema awali kuwa pale dawa na vifaa tiba vinapokuwa *O/S, MSD* inalazima hata dawa za *emergency* zinunuliwe kwenye maduka ya binafsi au kwa *tenderes* kwa kufuata taratibu za manunuzi ya umma, taratibu ambazo huchukua siku 28 hadi 30. Sasa mjamzito aliyekuja hospitali, *BP* imepanda sana na ana dalili zote za kifafa cha mimba au mtoto ameletwa hospitali na homa kali/degedege au mgonjwa aliyeletwa hospitali akiwa hana fahamu au mzazi *labour ward* aliyeanza ghafla kutokwa damu kwa wingi hao wote hukosa huduma/matibabu ya dharura hali ambayo husababisha vifo kwa vile *MSD* huwa haujatoa dawa, vitendanishi/vifaa na taratibu za manunuzi huwa hazikuruhusiwa dawa hizo zinunuliwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, ili basi kuboresha huduma za afya Serikali inayaangalia yote niliyozungumzia hapo juu na kuyarekebisha ili vifo viendelee kupungua kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, *MSD* mwanzo walikuwa na utaratibu wa *push system* pale ambapo walikuwa wanafungasha dawa na vifaa tiba kwa aina na kiasi walichoona kwa ajili ya vituo vya Afya, zahanati lakini pia hospitali za Wilaya, ikaonekana haikuwa nzuri kwa vile kwanza hawakujua mahitaji ya vituo hiyo, hivyo wakaanzisha utaratibu/mfumo wa *pull system* pale ambapo vituo vyenyewe vikahusika na kuagiza dawa na vifaa tiba vyao kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza pamoja na wazo zuri hilo la *pull system* lakini bado *MSD* katika *packing* yao imekuwa haizingatii maagizo kutoka vituo (hospitali, vituo vya afya na zahanati) wakati mwingi dawa wanazoagiza aidha, wanaletewa chache sana au nyingi kuliko mahitaji au hutolewa *item* ambayo haikuagizwa kabisa. Wakati mwingine dawa au vifaa huletwa kwa wingi sana kuliko mahitaji ukichunguza *expiry date* huwa ni wiki au mwezi mmoja unaofuatia.

Mheshimiwa Spika, *with MSD* ni adha kubwa sana na wapo hivyo kwa vile hawana mshindani, mara nyingine vifaa wanavyonunua huwa ni *sub standard* (chini ya viwango) mfano mdogo ni *blood pressure machine* ambayo unapoifungua kwenye kasha

huwa hatoi vipimo sahihi (inaweza kutoa kipimo kinachofanana kwa wagonjwa hata kumi waliofuatana kupima)  na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, ni rai yangu kupitia sekta ya afya na kurekebisha yote niliyozungumzia kwani kuzuia ni bora kuliko tiba yaani *prevention is better than cure* hii sekta inayohudumia wanadamu na siyo mifugo au mafaili.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele wanachopewa walimu na watumishi wa afya wangepewa hicho hicho *after all* hawajui hata kugoma na katika afya wauguzi wapewe kipaumbele cha mwanzo kwani ndio wanaokaa na mgonjwa saa 24. Yeye daktari akisha-*prescribe* huondoka na anaweza asimwone mgonjwa hata kwa siku tatu lakini muuguzi yupo na mgonjwa saa zote, mabadiliko mazuri au mabaya wa kwanza kuyaona ni muuguzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Marais Wastaafu wote akiwemo Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa jinsi ambavyo walikuwa makini katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa Maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee nazipeleka kwa Rais wa Serikali ya Tanzania wa Awamu ya Nne kipindi cha pili kwa kasi yake kubwa ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa vitendo kwani ahadi zake zote za awamu ya kwanza zimetekelezwa nina matumaini makubwa kuwa ahadi zake zote alizotoa kwenye kampeni ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 atazitekeleza ipasavyo zikiwemo ahadi za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa mtoto wa mkulima, Waziri Mkuu wa Serikali ya Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa uwezo wake mkubwa aliona katika kuwatumikia Watanzania na Watanzania wameridhika sana na utendaji wake wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Singida ambao wamenituma nimwambie wako bega kwa bega kamwe hawatamwangusha katika kudumisha amani na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ama kweli Ofisi ya Waziri Mkuu ina viongozi madhubuti sana wote kwa ujumla wao Mawaziri Mheshimiwa Kepteni George Huruma Mkuchika, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Ndugu Peniel Lyimo, Katibu Mkuu TAMISEMI Ndugu Hussein Katanga pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye kukidhi haja ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, inatia moyo sana Watanzania wanapoona kilimo bado kinapewa kipaumbele, Mkoa wa Singida unao wakazi wachapakazi pia ardhi ni nzuri, hivyo ninapenda kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhakikisha kila kata ina Afisa Kilimo na awe na usafiri, pili, wakulima kupata pembejeo kwa wakati kwa dhamana ya halmshauri, tatu, kila kijiji kiwe na mashamba ambayo wakulima wengine watajifunza hapo, nne, mazao yote yanayolimwa ya biashara kuwa na soko la kuaminika ili kuwatia moyo wakulima na tano, kuwe na maghala kila kata ya kutunzia chakula cha akiba.

Mheshimiwa Spika, posho za Madiwani, ni ukweli uliowazi kuwa Halmashauri zetu zinapelekewa fedha nyingi sana kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini cha kustaajabu Madiwani ambao ndio wanasimamia mabilioni haya wao hawana fedha. Hivi tunategemea nini kitatokea hapo, ni wazi matatizo yanaweza kuwakumba Madiwani ni kununuliwa na watendaji kwa bahasha ili kupitisha miradi iliyotekelezwa hata chini ya kiwango. Suala la rushwa kwa Madiwani linaweza kutokea kwani huwezi kumpa msichana ampe uji mtoto wakati yeye ana njaa.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Singida ni miaka mingi sasa tangu Serikali ilipoahidi kujenga Mahakama ya Rufaa Mkoani Singida lakini utekelezaji wake hadi leo ni wa kusua sua. Nimepitia Bajeti kwa makini sana ya mwaka 2011/2010 sijaona fedha iliyotengwa. Ninasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoani Singida, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone, Mkuu wa Mkoa wa Singida, kwa ubunifu wake wa kujenga hospitali hiyo Mkoani Singida na vilevile kuwa mstari wa mbele kutafuta vifaa vya hospitali hiyo. Huo ni uzalendo uliotukuka ukizingatia sio mzaliwa wa Singida. Niishukuru kipekee Serikali kwa kukubali kuunga mkono juhudi hizi kwa hatua za makusudi kwa kutenga shilingi bilioni mbili kwa miaka miwili mfululizo ikiwa ni pamoja na Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ombi, kulingana na ukubwa wa mradi huu ambao utakuwa na vitengo 37 na mpaka sasa tumemaliza vitengo viwili tu, ninaishauri Serikali kutuongezea kiwango cha fedha ili mradi uweze kupunguza siku za kukamilisha ujenzi huu ambao kwa mwendo wa shilingi bilioni mbili tutajenga kwa miaka zaidi ya thelathini. Ni bahati iliyoje viongozi wakuu wa nchi hii akiwemo Waziri Mkuu ameushuhudia kwa macho. Nitashukuru kupata majibu ya huruma.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* Singida, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Meneja wa Mkoa *SIDO* Singida kwa jinsi ambavyo anajitahidi kuwasaidia wajasiriamali hususan wanawake na yeye akiwa mwanamama mwenzetu amejitahidi sana kutoa semina na mikopo kwa wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi za meneja ninaomba aungwe mkono na Serikali kwa kuongezewa fedha ili aweze kuwasaidia wanawake wengi ambao wameamua kwa moyo moja kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya elimu na ukaguzi. Ninapenda kuishauri Serikali kuwa elimu inashuka kwa sababu nyingi sana ikiwa ni pamoja na elimu kuwa na ndani ya *OC* moja ambayo iko chini ya klasta, inasimamiwa na Mkuu wa Klasta ambaye ni Mhandisi wa Maji. Kuunganisha idara zote sio mbaya bali tunangalia idara kubwa kama Idara ya

Elimu na Afya hizi zingejitegemea kwa sababu ni kubwa sana. Ninapata wasiwasi kwani Mhandisi wa Maji wa Mkoa kuwa Mkuu wa Klasta inaweza kumpa shida kukumbuka idara zingine.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa taarifa kuwa walimu wawili walioajiriwa kwa mkataba baada ya kustaafu hadi leo wanadai fedha za miezi kumi na sita pamoja na Serikali kutoa majibu mazuri hapa Bungeni mara nne. Mpaka sasa walimu hawa wastaafu wamebaki sita tu wawili wamefariki, nitafarijika sana kupata majibu ya Waziri Mkuu ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wabunge Viti Maalum na Madiwani Viti Maalum kubaguliwa. Kwa faraja ya pekee ninapongeza uongozi wa Bunge chini ya Mheshimiwa Anne Makinda kwani Wabunge Viti Maalum hatujabaguliwa, haki zote ni sawa hata kugombea nafasi za uongozi. Ni vipi huko kwenye Halmashauri na Mikoani tunabaguliwa, vikao vingine tunazuiliwa na nafasi zingine za uongozi tunakatazwa kugombea. Naomba Serikali iondoe matabaka haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nchi ya Tanzania ni moja ya nchi za Afrika zenye misitu mikubwa (mfano Mufindi) nashauri Serikali ichukue hatua za dhati kabisa kumaliza tatizo la madawati kwa sababu hatuna sababu ya kuendelea na tatizo hili wakati Mungu ametupa nchi nzuri yenye miti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya matengenzo ya magari, takwimu zinaonyesha kwamba katika mwaka uliopita matengenezo ya magari yalikuwa asilimia 25 ya *Recurrent Expenditure* ya Ofisi ya Waziri Mkuu *(Vote).* Nashauri Serikali iweke mkakati mkubwa wa kupunguza matumizi hayo kwani ni makubwa mno.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia TAMISEMI, Mawaziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri mapendekezo na maombi kama ifuatavyo:-

Kwanza usimamizi wa matumizi ya fedha katika Halmashauri. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wamethibitisha kuwa hali ni mbaya sana na uthibiti unaizidi kushuka. Taarifa zinazopelekwa na Halmashauri kwenye Kamati ya Bunge hazifikishwi kwenye Kamati za Madiwani kabla ya kupelekwa na hivyo kubeba taarifa na nyaraka hewa zenye lengo la kuonesha matumizi ya fedha za miradi kwa kuonesha zimetumika zote, kwa nini tunaendelea kuziachia watendaji wa Halmashauri kukwepa Madiwani na kupeleka taarifa hewa kwenye Kamati za Bunge?

Pili, mamlaka anayopewa Mwenyekiti wa Halmashauri kuteua wajumbe wawili kwenye Kamati ya Fedha, kwa nini Mheshimiwa Mbunge ambaye ndiye kiongozi wa

jimbo na kata zote hapewi jukumu hilo badala yake anapewa Diwani wa Kata moja? Matokeo yake ni upendeleo na kuacha kuweka Madiwani wenye uwezo mzuri na sifa muhimu ili kusaidia Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wenye elimu ya Chuo Kikuu *(degree)* tangu mwaka 2000 hadi sasa hawapewi nafasi katika Kamati ya Fedha kwa kuwa wana uwezo mkubwa wa kuchagua na kutafsiri taarifa za fedha na hivyo kutoa mwanya wa kudhoofisha utendaji kwa kuficha hali halisi kwa manufaa ya waovu wachache. Tufanye marekebisho katika mfumo huu ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi nzuri ya kuwezesha kuboresha ufanisi.

Tatu, mapungufu ya mapokezi ya fedha za ahadi kutoka Serikali Kuu kwa mafungu ya *LGDG* 2010/2011. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI inaonyesha fedha za *LGDG* Aprili, 2011 ruzuku za maendeleo ya maji vijijini shilingi bilioni 63.2 hazitolewi kwa Wilaya ya Muheza *LGDG* ahadi ilikuwa shilingi 887,388,000/= lakini zimepokelewa shilingi 466,785,318/= na shilingi 420,602,682/= hazijatolewa.

Kutotolewa fedha hizo kumesababisha mradi ifuatayo kutotekeleza:-

(i) Ujenzi wa Kituo cha Afya Mhamba shilingi 61,078,000;
(ii) Ujenzi wa madarasa saba ya sekondari shilingi 21,500,000;
(iii) Ujenzi wa vyumba vitano vya walimu sekondari shilingi 35,000,000;
(iv) Ujenzi wa vyoo sekondari shilingi 12,600,000;
(v) Ununuzi madawati 148 sekondari shilingi 4,440,000;
(vi) Ujenzi madarasa mawili shule za msingi shilingi 18,000,000;
(vii) Ujenzi wa nyumba nne za walimu wa shule za msingi shilingi 52,000,000;
(viii) Ujenzi wa vyoo shule za msingi shilingi 16,800,000;
(ix) Ununuzi wa Madawati 104 kwa shule za msingi shilingi 5,200,000;
(x) Ukarabati mradi wa maji Misalai shilingi 24,000,000;
(xi) Ujenzi wa Kisima kirefu – Masuguru shilingi 20,000,000;
(xii) Ujenzi wa Kisima kirefu Kimara majengo shilingi 20,000,000;
(xiii) Ujenzi wa kisima kirefu Mtindiro shilingi 20,000,000; na
(xiv) Ruzuku ya Vijiji shilingi 109,984,682.
Jumla shilingi 420,602,682

Hali hii inadhoofisha maendeleo ya wananchi. Halmashauri imeandikia Hazina na TAMISEMI kwa barua Kumb.Na. HW/MUH/F.60/29/107 ya tarehe 13/6/2011, naomba mtusaidie kufuatilia fedha hizo. Taarifa ya Wizara TAMSESEMI ukurasa wa 23 pia inaonyesha tathmini ya fedha ambazo Halmashauri zitapata kama ifuatavyo:-

- Halmshauri 110 zitapa 100%
- Halmashauri 2 zitapata 80%
- Halmashauri 16 zitapata 50%
- Halmashauri 4 zitapata 25%

Kati ya jumla ya shilingi bilioni 423.67. Je, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ipo katika kundi gani na itapata kiasi gani?

Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Maji, hali ya maji katika Mji Mdogo wa Muheza ni mbaya sana licha ya ukweli kwamba chanzo cha mradi wa maji kinachopeleka maji katika Jiji la Tanga kinaanzia ndani ya Tarafa ya Amani katika Mto Zigi ndani ya Wilaya ya Muheza. Je, ni mkakati gani upo katika mradi huu kati ya Serikali ya Tanzania Benki ya dunia na Serikali ya Denmark kwa mwaka 2010/2011 hadi 2012/2015 ili kusaidia Mji Mdogo wa Muheza na kata zake kupata maji ya uhakika?

Kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Hali ya Hospitali Teule ya Muheza ni mbaya na inahitaji msaada. Hata jokofu la kuhifadhi maiti hakuna, sasa maiti zinapelekwa hospitali ya Bombo Tanga ambako ni zaidi ya kilomita 30. Fedha zilizopelekwa mwaka 2010 kununulia dawa na ukarabati zimetumiwa vibaya na watendaji ambao si wafanyakazi wa Halmashauri ila Kanisa! Tunaomba mtusaidie fedha kuweza kufufua hospitali ya zamani ya Ubwari ili iwe Kituo cha Afya kusaidia Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo wake kwa nchi na Watanzania kwa ujumla. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Pia nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na watendaji wote na wataalam wanaomsaidia kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambayo imejipanga vema kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu vipaumbele vilivyoainishwa ndiyo matakwa ya CCM ili kuwaondoshea kero za maisha Watanzania hasa maskini wanaoishi vijijini na mijini *(urban poor).*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwamba sekta binafsi ni kichocheo muhimu kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea kiuchumi kama Japan na zinazoinukia kiuchumi kama zile za Mashariki ya mbali mfano Malaysia, Singapore, Hongkong na kadhalika. Zimefanikiwa kukuza uchumi wa nchi zao kwa kupitia mchango wa uwekezaji uliofanywa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu itimize azma yake ya kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iweze kuwa mchangiaji mwenza katika kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ivutie mitaji ya kutosha ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Lakini napenda kuitahadharisha kwamba wakati ikivutia

wawekezaji, ni vema ikatathmini uamuzi wake wa kuwapatia wawekezaji wa nje *tax holiday* ya miaka kumi kama kivutio cha kuwekeza hapa nchini. Kama Taifa, lazima tufanye tathmini sahihi juu ya madhara ya kiuchumi na kijamii kwa sasa na kwa vizazi ijavyo.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini tukiachana na utaratibu mbovu wa kuwazungusha wawekezaji kwa sababu ambazo hazina msingi, kama ilivyoelezwa siku ya uzinduzi wa mpango wa miaka mitano pale Mtakatifu Gasper, kwamba tabia ya baadhi ya watendaji ya kuwatoa upepo yaani kuomba kitu kidogo wawekezaji ndiyo kitisho kwa mipango ya maendeleo hapa Tanzania. Tukiweza kuwadhibiti wenye tabia ya kuwaomba kitu kidogo wawekezaji na pia usumbufu usio wa lazima wa kuwekeza, itachangia kuvutia wawekezaji na kupanua uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nchi jirani ya Rwanda, wawekezaji wanatumia muda mfupi sana kupata kibali cha kuwekeza, hapa Tanzania hali haiko hivyo, pana usumbufu usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuwezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira, naipongeza sana Serikali yetu katika eneo hili. Hata hivyo naiomba Serikali iweke mazingira wezeshi ili mifuko mbalimbali iliyoundwa na itakayoanzishwa iwanufaishe wananchi wengi na kwa uwiano mzuri baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu iweze kufanikisha azma yake ya kukuza uchumi kwa kupitia sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na nyuki, naishauri Serikali kwamba utaratibu wa kuuza malighafi *(raw materials)* ya mazao yatokanayo na sekta hizi hauwezi kulinufaisha Taifa letu. Siku zote *our balance of trade* itaendelea kuwa na nakisi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile tunafahamu mapungufu yetu kwamba hatuna viwanda vya kusindika mazao yetu ili kuyaongezea thamani, nashauri juhudi za makusudi zifanywe ili kuvutia wawekezaji katika eneo hili. Nchi yetu inapaswa ianze kuuza *finished goods* pia naomba Serikali iwatoze kodi kubwa wenye viwanda, wafanyabiashara na matajiri wengine na maskini wapewe unafuu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda, ajira nyingi zitapatikana, masoko ya mazao mbalimbali yatakuwa ya uhakika na kodi zitakuwa za uhakika na hivyo mapato ya Serikali yataongezeka. Viwanda vitawapatia ari wakulima kwa vile watakuwa na masoko ya uhakika na bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie masuala ya ardhi, nyumba na makazi. Katika eneo hili, Serikali iangalie upya mipango ya matumizi bora ya ardhi. Naelewa na kila mmoja wetu anafahamu kwamba Watanzania ni maskini sana, lakini nchi yetu ni tajiri sana. Naishauri Serikali kwamba mamlaka zilizopewa dhamana ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ziwezeshwe vya kutosha ili ziweze kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, ardhi ya vijiji ipimwe na wananchi hati za kumiliki ardhi hiyo ili wazitumie kwa maendeleo yao. Pili, nyumba zenye bei nafuu zijengwe hasa katika maeneo ambayo hayafai kwa kilimo na tatu, Serikali ipige marufuku mtu binafsi kujenga nyumba yake binafsi ili kuondoa tatizo la wizi wa fedha za umma hii itasaidia kupunguza au kuomba kishawishi cha rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya utalii, nchi yetu ina vivutio vingi sana ambavyo kama vingetangazwa vizuri naamini Tanzania ingekuwa inatembelewa na watalii wengi sana kuliko nchi yoyote katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Nathubutu kusema kwamba taasisi iliyopewa dhamana ya kusimamia sekta hii imeshindwa kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, visiwa vya Zanzibar ni mojawapo ya maeneo yenye vivutio vingi vya kihistoria na fukwe nzuri za kupendeza na ni adimu kwa sasa kuziona katika maeneo mengine duniani vikitangazwa vizuri vitawawatia watalii wengi ambao wakifika Zanzibar watafika pia Tanzania Bara. Vilevile Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama, maeneo mbalimbali ya kihistoria mfano, mapango ya Amboni Tanga, Olduvai Gorge Arusha na Butiama, kwa kutaja baadhi ya maeneo tu ya nchi yetu, nashauri yatangazwe vizuri kupitia vyombo vikubwa vya habari ya Magharibi kama *CNN, BBC, VOA, DWTV, CCTV, Africa Journal* na kadhalika ingechangia vivutio vilivyopo kujulikana na watu wa Mataifa mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu ambavyo kwa sasa ni bidhaa adimu sana katika Mataifa mengine ya Afrika ni rasilimali muhimu ambayo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu ni kichocheo kimojawapo katika kushawishi makampuni makubwa yanayoongoza sekta ya utalii duniani.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi ya Kenya ambayo ndio nchi tunayoshindana nayo katika sekta hii inapokea watalii zaidi ya mara mbili ya wale wanaotembelea nchi yetu. Kenya imefanikiwa kwa sababu imeweka zaidi katika matangazo ya vivutio vyake kuliko tunavyofanya hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ingie katika makubaliano maalum na vyombo vya habari vikubwa vya magharibi kwa kulipia *Airtime* katika vyombo hivyo ili vivutio vyetu vitangazwe wakati wa *prime time* na hivyo kuweza kuonekana na watu wengi. Pia nchi yetu ishiriki kwenye maonesho makubwa ya utalii yanayoandaliwa na nchi kubwa za Marekani, Ujerumani, Italy, Ufaransa, Spain, Russia, Japan na kadhalika. Naamini tutaweza kuvitangaza vivutio vyetu kwa kushiriki katika maoneshao hayo.

Mheshimiswa Spika, sambamba na ushauri huu, nashauri pia kwamba miundombinu kama vile barabara, hoteli, viwanja vya ndege, umeme wa uhakika, ulinzi na usalama kwa watalii, viboreshwe na pia tuwe na Shirika letu la ndege la uhakika ambalo litawaleta watalii hapa nchini. Naomba pia uwepo ushirikiano wa karibu kati ya Bodi ya Utalii ya Tanzania Bara na Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nizungumzie kuhusu sekta ya madini kwamba pamoja na utajiri mkubwa tulionao katika sekta hii, bado rasilimali hii ambayo nchi yetu imepewa na Mwenyezi Mungu haijawasaidia wananchi wanyonge wa nchi hii ya Tanzania ambayo ni Kanani ya Afrika, wananchi bado wanaishi maisha dhalili na ya kinyonge kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali yetu ni sikivu na kwa vile iliazimia kufanya mapitio ya mikataba ambayo imeingia na makampuni ya nje, basi naiomba Serikali iwaambie watanzania ilichokibaini katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu na Taifa zima la Tanzania na Bunge lako Tukufu liambiwe kama mikataba tuliyoingia ina kasoro na hatua zilizochukuliwa kwa wahusika ambao wameiingiza nchi kwenye mikataba yenye viini macho isiyo na maslahi kwa nchi na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu lisikubali kukumbatia makampuni ambayo hayana nia safi na nchi yetu. Madini ni *non renewable resources,* Taifa letu litakuwa na kumbukumbu gani kama madini haya, hayachangii katika maendeleo ya nchi yetu? Naomba sote tuseme, basi kwa makampuni yanayopora rasilimali ya madini na utajiri wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona mchanga wenye madini mbalimbali unasafirishwa ng'ambo ya Tanznaia. Kama makampuni ya madini yameweza kujenga migodi mikubwa ya kisasa, nashauri pia yajenge viwanda vya ku-*extract* madini kutoka kwenye mchanga na hivyo kuyafanya makampuni hayo kuweza kulipa kodi stahiki kwa Serikali yetu na kuchangia maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kwamba kero ya mgao wa umeme inachangia kudumaza ukuaji wa uchumi nchini. Kadhia ya mgao wa umeme ni mojawapo ya kero inayoathiri ustawi wa uchumi wetu na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ninayo heshima kuleta mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba hii nzuri na Bajeti ni nzuri sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia naomba nikupe pole ya kazi kubwa ya uongozi Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mungu atakusaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala la wawekezaji. Wawekezaji ni watu muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Lakini pia bado kuna maeneo mengine wawekezaji wananyanyasa wananchi wa Tanzania. Kwa mfano, Kigamboni amekufa mwanamke katika mazingira ya utata sana katika hoteli ya kitalii. Wafanyakazi wanaofanyakazi katika sehemu za wawekezaji wengine wana roho za kikatili.

Mheshimiwa Spika, nakipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kupambana na wawekezaji wa aina hiyo. Kuna kesi nyingi zinazohusu wawekezaji na wananchi. Ushauri wangu naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kiupelelezi kutambua tabia za wageni wanaokuja kuwekeza nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika nimesema hivyo kwa sababu kuna wengine ni wanajeshi ambao maisha yao yalikuwa ni ya kijeshi hivyo anapokuja nchini kwetu anaongoza kijeshi ndio hapo anaanza kuteka mali za watu, kupiga watu na kufanya utapeli wa mali za watu.

Mheshimiwa Spika, si wawekezaji wote wako hivyo, ni baadhi tu. Lakini pia niipongeze Serikali kwa kukaribisha wawekezaji katika suala zima la umeme. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ajue kuwa umeme ni tatizo na pia unachangia sana kuanguka kwa pato la Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, niombe Mkoa wa Dar es Salaam uwekwe mpango wake mkakati kutokana na Mkoa wa Dar es Salaam hatuna mashamba kwa kilimo. Mashamba yetu ni biashara ndogo ndogo kama vile *saloon, viosk* vya kuuza maji baridi na *juice,* kuuza samaki wabichi, kuuza nyama, kuku na barafu. Biashara zote hizo ndogo ndogo zilizokuwa zinafanywa na Watanzania wenye uwezo mdogo wa kiuchumi zimekufa.

Mheshimiwa Spika, ukiacha biashara hizo ndogo ndogo kuna viwanda vingi Mkoani Dar es Salaam na majumba makubwa yanayofanya biashara kubwa ya kukusanya watu wengi sana kama vile *Mlimani City, Shoprite* pale Kamata, *Haidery Plaza, Benjamin Mkapa Tower, Dar es Salaam Airport* na majengo mengi ya Serikali na watu binafsi ambayo yanatumia *lift* na vitu vingi vya umeme na makampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri ni vyema tutafute mwekezaji kwa Mkoa huu. Kwa kutumia Gridi ya Taifa Mkoa huu utachangia sana kuminya umeme kwa mikoa mingine. Kama ikiwezekana kila Manispaa ya Mkoa wa Dar es Salaam kuweka jenereta ambalo litasambaza umeme katika manispaa husika za Temeke, Ilala na Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wapo na kama kuna uwezekano *TANESCO* ishuke katika Halmashauri tufanye majadiliano na viongozi na wananchi kwa ujumla kwani kila mtu amepewa kipaji chake na Mwenyezi Mungu na uwezo wake na pia hata wasio na elimu kubwa wana akili mbadala waje wachangie mawazo, nina imani tatizo litaenda na kuisha tu. Wananchi wanakata tamaa na hatuwapi nafasi na wao wapigane katika vita hii ya kupambana na tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa tuwaulize wananchi wanatakaje na wana ufumbuzi gani katika tatizo hili? Tunao Watanzania ndani na nje ya nchi lakini hawana uwezo wa kulikatia shauri. Niombe pia sheria ya umeme ya manunuzi irekebishwe kwa kusaidia kupunguza tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na tatizo la simu limeisha kabisa, tulikuwa na tatizo la usafiri Dar es Salaam tukaruhusu daladala na tatizo la maji kwa kuleta wachimbaji binafsi wa visima. Sasa wakati umefika katika sekta ya umeme kuweka masharti nafuu kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa sana kukuelezea kero ya barabara ya Kilwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi naishi Mbagala Rangi Tatu na nimekuwa Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Rangi Tatu mpaka naingia Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tegemeo la wananchi ni kuwasemea matatizo yanayowakabili. Nimejitahidi kuwasaidia walipwe fidia za nyumba zao walizobomolewa kupisha upanuzi wa barabara ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, kilichotekea katika kipindi kilichopita Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni alipata barua kutoka Ofisi yako kuwa limepatikana fungu la fedha la kuwalipa wananchi waliovunjiwa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara ya Kilwa. Baada ya barua hiyo tathmini ikafanywa na jopo la mainjinia toka *TANROADS* na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Wizara ya Miundombinu. Walichokisema ni kuwa hatutaweza kuwalipa fidia yote kwa wananchi bali tutatoa kifuta machozi tu kwa yale yaliyotokea. Wananchi waliridhika kwa kauli hiyo na wale wote waliohusika walitafutwa na kupigwa picha.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo malipo yalianza kutolewa kwa wale walioenda Mahakamani na wasioenda Mahakamani toka Kongowe mpaka Mzinga tu, kuanzia *St. Mary's* Mbagala mpaka Kurasini Bendere Tatu walilipwa baadhi ya wananchi walioenda Mahakamani na wengine wote hawajalipwa mpaka leo. Viongozi tunajitahidi, wananchi wamekuja mpaka huku Bungeni jibu ni kuwa wamejenga katika *road reserve* kwa hiyo hakuna malipo. Cha kushangaza miezi iliyopita Serikali ilitangaza kulipwa fidia ya barabara ya Ubungo Maziwa na *Davis Corner* mpaka *Jet.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa *Kilwa Road* hawaelewi. Wanaona Serikali yao haiwapendi kwa kuwa wapo Kusini (ni hisia zao tu). Mheshimiwa Waziri Mkuu kaka yangu, nihurumieni mimi ambaye naishi na kundi hili, hasira zao zote zinaishia kwangu. Sasa sijui tunafanyaje? Wananchi wanahangaika, mara wanataka kuandamana kwenda Ikulu, tunawatuliza. Sasa kundi lingine limeenda Mahakamani juzi juzi tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa maslahi ya chama changu na Taifa langu la Tanzania lenye upendo na amani.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaunga mkono asilimia mia. Pili hongera kwa Bajeti nzuri na tatu maombi tafadhali.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *SAGCOT* uingizwe pia na Lindi. Kuna mabonde ya shughuli za umwagiliaji na maeneo ya kilimo cha kawaida. Tuingizwe ndani ya mradi tafadhali.

Mheshimiwa Spika, suala la maji Lindi tufikiriwe, tuna miaka kadhaa hatuna maji Lindi Mjini, Nachingwea na Mchinga. Tunaomba tusaidiwe kwani Lindi tumezungukwa na bahari.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mjusi Dinosaur tupate maelezo, jitihada za kurudishwa kutoka Ujerumani vipi? Tunataka maelezo ya mjusi huyo alitoka Tendeguru/Mipingo/Lindi Vijijini. Ahsante sana.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ili mradi wa Liganga na Mchuchuma uweze kufanikiwa na ulete tija kwa wananchi wa kawaida ni lazima barabara ya kutoka Njombe – Ludewa hadi Manda ijengwe kwa kiwango cha lami. Hii itasaidia sana wakulima kupeleka mazao yao kule mgodini na pia itafanya biashara nyingine zishamiri.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Ofisi yako iboreshe maslahi ya Madiwani, walimu na askari polisi. Madiwani wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, ni lazima tuwasaidie.

Mheshimiwa Spika, zile pesa ambazo tunazipata kutoka kwenye ongezeko la bei ya mafuta ya taa, tuwarudishie wananchi wa kawaida kule vijijini. Fedha za mafuta ya taa zipelekwe au kwenye kilimo au kwenye barabara za vijijini au zipelekwe kwenye Mradi wa Umeme Vijijini *(REA).*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha kw akuunga mkono hoja ya hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

**MHE. NAMELOK E. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina mambo matatu ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, *MSD* kumekuwa na tatizo kubwa la kupelekwa madawa yaliyopitwa na wakati au yanayokaribia kupitwa na wakati katika Zahanati zetu za vijijini na hivyo kusababisha madhara kwa watumiaji au saa nyingine kupelekewa madawa wasiyohitaji. Nashauri *MSD* kuwa wepesi kukagua madawa yao kabla ya kuanza kusambaza au kabla hayajaingia nchini, waingizaji wa madawa wapewe masharti kwamba, dawa zote zinazoingizwa zilizokwisha muda wa matumizi ziwe mbali.

Mheshimiwa Spika, pili, kumekuwa na tatizo kubwa la ajali barabarani, hivyo kupelekea watu wengi kupoteza maisha na familia nyingi zimekuwa zikiteseka kutokana na kupoteza watu ambao ndo tegemeo lao, pia kusababisha ulemavu kwa wengine. Nashauri kila basi liwekwe *Traffic* mmoja na yanapokutana katikati *Traffic* hao wanaweza kubadilishana. Hii inaweza kuwa njia pekee ya madereva wetu kuogopa kwenda mwendokasi.

Mheshimiwa Spika, tatu, miaka ya zamani *SIDO* ilikuwa ina nguvu kubwa na ilikuwa inajulikana hadi vijijini. Japokuwa kwa sasa wamepanuka na kuendelea kuimarika, jambo la kusikitisha hawasikiki kabisa. Naishauri Serikali kuitangaza *SIDO* na kuwaongezea mtaji ili waweze kusaidia vikundi vidogovidogo na wajasiriamali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri. Mambo yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli uchumi unakua vizuri sana kwa asilimia saba, lakini ni kweli pia wananchi wetu hawaoni nafuu kwani maisha bado ni duni. Sasa naiomba Serikali itafsiri mafanikio hayo ili mwananchi wa kawaida aweze kuona (*appreciation*). Hii ni rahisi, kwa ufupi ni kusimamia rasilimani au fedha nyingi zinazoelekezwa Vijijini na Wilayani zisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuwa na mfumo mzuri wa kubaini kero na kuzitatua. Watendaji (wafanyakazi) baadhi husababisha kero kwa kutowahudumia vizuri wananchi na pia kutokutoa majibu ya kweli. Ni lazima Mipango yetu itekelezwe na kuwe na mpango wa ufuatiliaji kwa kila mwezi, robo mwaka, na kadhalika, wimbo wa Tanzania ni maskini uishe sasa. Nchi yenye rasilimali kama madini, ardhi nzuri na yenye rutuba, mbuga za wanyama, maji (bahari, mito, maziwa na mabwawa) bado ni maskini! Viko vitu tulivyonavyo na vichache tunavikosa kama teknolojia na mtaji. Lazima tuukatae umaskini kwa utajiri tulionao.

Mheshimiwa Spika, tunasherekea miaka 50 ya Uhuru. Naiomba Serikali pamoja na mambo mengine ifanye hili. Kubainisha maeneo yote ambayo hatukufanya vema na kuweka mikakati mipya ya utekelezaji. Katika kipindi hiki Serikali itakuwa imefanya makosa kadhaa, hivyo ni vema kukubali na kuomba radhi kama:-

- Kutaifisha mali za Mashirika ya Dini. Inafaa sasa mazungumzo yafanyike kwa nia ya kurudishwa.

- Bado yapo malalamiko kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tujiridhishe je, bado watu wanadai na kama ndivyo walipwe.

- Waliofungwa/rumande pengine kwa kuonewa, msamaha utolewe.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la kilimo. Pembejeo zipelekwe kwa wakati na wakulima wa kawaida wapate ruzuku, kama zao la pamba na mengine. Mikopo ya kilimo, Benki ya *TIB* masharti yake ni rafiki kwa wakulima. *TIB* wanahitaji Kampuni ambayo ni *Limited*. Mikopo hii haiwezi kuwasaidia wafanyakazi wanaotaka kulima au

wanafunzi wanaomaliza masomo yao. Kwa namba hii hatuwezi kuleta mapinduzi tunayotaka kwenye kilimo. Naamini mapinduzi kwenye kilimo yatatokana na kuwawezesha wafanyakazi (pamoja na wanasiasa) na wanafunzi wanaomaliza vyuo kama Chuo cha Sokoine.

Mheshimiwa Spika, nije katika ushirika. Hotuba ya Waziri Mkuu imezungumzia juu ya kuimarisha ushirika. Sisi Mbinga tuna uzoefu tofauti, Chama cha Ushirika Mbinga ambacho kipo chini ya Mfilisi kinadaiwa na wakulima zaidi ya Sh. 400,000,000. Chama cha Mbinga kimoja kimelipwa na Waziri Mkuu nashukuru. Hawa wengine watalipwa lini? Idara ya Ushirika ambayo ndiyo inapaswa kusimamia na kuendeleza ndio kwanza wanadidimiza Ushirika Mbinga kwa kuendelea kudai kwamba watalipwa kwa Sheria ya Mfilisi. Aliyeamua kuweka Mbinga chini ya Mfilisi ni Serikali, vyama vingine viliruhusiwa kuendelea. Mfilisi ni Serikali yenyewe, upo ushahidi wakati mali zilizokuwemo nyingi kuliko madeni. Usimamizi mbovu wa Mfilisi ambaye ni Serikali umefanya mali kupotea. Leo wananchi wa Mbinga wanaambiwa malipo ni kwa Sheria ya Mfilisi. Huku ni kuwaonea wananchi au haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri Mkuu aliangalie Jimbo hili, ulikwishaelekeza Wizara ya Kilimo ilipe lakini hawa wataalam wanayumbisha na kutoa taarifa zinazoyumbisha maamuzi. Rais pia aliahidi kwamba wananchi hawa watalipwa. Wananchi walisifu na kumwaga kura nyingi. Je, walidanganywa? Pamoja na ahadi hizo ni pamoja na barabara ya lami Nyoni– Maguu –Mkole na Mbinga – Litembo Hospitali. Naomba Serikali kutekeleza ahadi hizi.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu lishe. Nampongeza Waziri Mkuu kwa kuongelea jambo hili. Naomba Taasisi ya chakula na Lishe (*TFNC*) lipewe fedha za kutosha ili lifanye kazi yake vizuri kwani ndilo lenye dhamana juu ya masuala ya uanzishwaji wake Sheria No. 24 ya 1973. Halmashauri ziamriwe ziingize masuala ya lishe katika mipango yake na iajiri Maafisa Lishe kwa kushirikiana na *TENC*.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie maeneo mapya ya utawala. Tumeshukuru Mbinga tumepata Wilaya mpya, Kata, Tarafa na Vijiji. Lakini Jimbo la Mbinga Mashariki ni kubwa sana. Tarafa sita kati ya 34, Vijiji 165. Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kuanzisha Mamlaka kamili ya Mji. Tunaomba Wilaya yaani Tarafa ya Mbaji, Mkumbi upande mmoja na Mbinga Mjini, Kigonsera na Narawea Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwenye ngazi za Halmashauri, Wakurugenzi wanasafiri mno kwenye mikutano Dar es Salaam na Dodoma, safari hizi zipungue na posho za Madiwani ziongezwe.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Nimpongeze Waziri Mkuu kwa Hotuba yake iliyogusa karibu sekta zote. Aidha, napenda kutoa pongezi kubwa kwa Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa Hotuba yake nzuri iliyofanyiwa utafiti kwa kuibua hoja na kuzipatia ushauri. Natumaini Serikali itazitumia hoja hizo kwa faida ya Watanzania na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Manispaa ya Moshi Mjini chini ya uongozi wa CHADEMA kwa kushika namba moja kwa usafi. Naomba kuzungumzia kuhusu Jiji letu la Dar es Salaam ambalo ndio kioo cha nchi yetu. Nitazungumzia mambo matatu ambayo ni hali ya uchafu, msongamano wa magari na ujenzi holela katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwanza nizungumzie hali ya uchafu. Kwa kweli hali ya uchafu ni mbaya sana mfano, Morogoro *Road* pale pamekuwa ndio jalala la takataka, mfereji wa maji machafu ndio shimo la takataka. Watoto wanaokota *plastic* ndani ya mifereji hiyo. Hii inapelekea magonjwa ya milipuko kama *typhoid*, *cholera* yasiweze kwisha kabisa Dar es Salaam. Isitoshe hiyo mifereji iliyopo wazi ndio chanzo cha mazalia ya mbu ambalo siyo rahisi malaria kutokomea Dar es Salaam kama mazalia yatawaachwa wazi kwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu hata zile gari zinazozoa takataka ni mbovu, hazina vitendea kazi, badala ya kuzoa taka ndizo zinasambaza taka, hazina mifuniko na kadhalika. Ushauri wangu ni:-

(i) Mifereji yote ya maji machafu ifunikwe;

(ii) Magari yote ya kuzolea taka kwa sababu ni *tender* basi viwekwe vigezo lazima gari iwe ni maalum kwa kuzolea taka. Iwe imefunikwa na wale wafanyakazi/wahudumu wawe na vitendea kazi.

(iii) Sehemu zote zenye mazalia ya mbu zipuliziwe dawa.

Mheshimiwa Spika, pili, niongelee msongamano wa magari, Dar es Salaam tumeona wakati wa mvua msongamano ndio unakuwa mkubwa zaidi. Pamoja na Serikali kuleta mradi wa magari yaendayo kasi huu ni mpango mrefu. Kwa mpango mfupi zile barabara za pembezoni zingetengenezwa ili kuokoa msongamano ambao ni kero kubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tatu, nizungumzie kuhusu ujenzi holela. Ujenzi wa *Hotel* Dar es Salaam, je, katika Jiji letu kuna *master plan*? Kama ipo je, inatumika? Tumeona katika Jiji letu watu wengi wanajenga bila *plan* yoyote hata kwenye *open space*. Serikali imekuwa ikipinga watu kujenga kwenye *open space* lakini wamekuwa ni wa kwanza kuvunja sheria hiyo. Kwa mfano, Mwalimu Nyerere *foundation* wamepewa sehemu ambayo ni *open space Sokoine Road pale Sokoine Drive*. Pale palikuwa ni *parking space* na ni sehemu ya baadhi ya majengo ya Dar es Salaam kupanuliwa lakini Serikali wamewapa Nyerere *Foundation* kujenga pale. Je, hii siyo *contradiction*? Napenda nipate jibu la suala hili. Kwa nini msiwape kule Kigambonii Jiji jipya, wajenge huko hilo ghorofa lao? Je, ujenzi wa Bar katika makazi ya watu Sinza Makaburini nini hatima yake?

Mheshimiwa Spika, nichangie utunzaji wa mazingira Dar es Salaam. Kule Mikocheni kuna viwanda vingi sana kati ya viwanda hivyo kuna Kiwanda cha Shelly cha Madawa, *BIDCO* cha Mafuta na *MMI* cha chumvi. Viwanda vyote hivi vimekuwa vikielekeza maji machafu na yenye sumu kwenye mfereji wa Nyirenda. Je, Serikali inalijua hili? Kama hamlijui wawekezaji hawa wamekuwa na kiburi cha hali ya juu bila kujali afya za wananchi wanaoishi pale hawajali kabisa. Naomba Serikali iunde Tume kuchunguza ni kwa kiasi gani sumu ile inaweza kudhuru ubongo wa wananchi na ni kiasi gani kitakachotumia kuhudumia wananchi wale pamoja na mwekezaji huyo kuwapatia ajira na sio kuwanyanyasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira. Kuna wanafunzi zaidi ya 760,000 wanaomaliza vyuo na kati ya hao ni 40,000 tu ndio waliopo katika ajira na wengine waliosalia zaidi ya 720,000 watakuwa hawana ajira. Kuna baadhi ya ajira ambazo wastaafu huongezewa mikakati kama vile Watumishi wa Umma, Wakurugenzi wa Halmashauri, *DED* na *DAS*. Sizungumzii kazi za utaaluma kama Walimu, Madaktari na *Engineers*. Ni hizi kazi za utawala. Ni vigezo vipi vinavyotumika kuwaongezea muda wa mkataba? Je, siyo kuwalipa mishahara miwili wakati bado wanapokea *pension*? Je, waraka wa Utumishi wa Umma unasemaje kuhusu kujaziwa mkataba? Je, wanatakiwa warudi kwenye wadhifa ule ule?

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri, kama ni lazima waongezewe muda basi wawe washauri na kuwafundisha wanaomaliza vyuo na siyo kubaki katika wadhifa ule ule. Hii italinda ajira ya vyuo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia utalii. Ni Sheria ipi inayotumika kwa Ndege ya Kijeshi kutoka nchi nyingine kuingia Tanzania? Tumeona katika vyombo vya habari Ndege ya Kijeshi ya *Quarter* kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro. Je, ufisadi huu Serikali inatueleza nini? Haiingii akilini Ndege ya Jeshi ya nchi nyingine kuingia nchini na kutoka na nyara za Serikali halafu tukae kimya. Aliyetoa kibali cha ndege hiyo kutua ilieleza imekuja kufanya nini Tanzania. Naomba majibu sahihi.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULINJE:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zote chini yake na naiunga mkono. Napenda nishauri maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ibara ya 27 inazungumzia uwezeshaji wananchi kupitia *SACCOS*. Ni jambo zuri napongeza sana jitihada za Serikali kutilia mkazo jambo hilo. Angalizo langu ni kwamba wananchi wengi wanapohamasishwa kuanzisha *SACCOS* ili iwe ni njia ya kupitishia uwezeshaji; ihakikishe pia utaratibu wa kuziendesha *SACCOS* hizo kwa kuzingatia misingi na taratibu ya Ushirika zinazingatiwa. Baadhi ya *SACCOS* zimekuwa zinaundwa kwa ajili ya kupitishia fedha za uwezeshaji kwa kuwapatia wananchi mikopo tu bila wanachama wa *SACCOS* kupewa Elimu ya Ushiriki na utaratibu mzuri wa kuwafanya wanachama wa *SACCOS* waweze kujitegemea. Nashauri Idara ya Ushirika iimarishwe ili iweze kuzisaidia *SACCOS* hizi ili ziwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, pili, ibara ya 31, inazungumzia kuwawezesha wananchi kupitia Asasi zingine yakiwemo Mabenki, Taasisi za Fedha, Madhehebu ya Dini na kadhalika. Angalizo langu ni kwamba, Asasi hizi ziratibiwe vizuri na Serikali juu ya mienendo ya masharti wanayotoa kwa wananchi wanaokopeshwa na Mifuko hiyo. Baadhi ya masharti ya Mifuko hiyo hayawawezeshi wananchi kujitegemea, hasa urejeshi wa mikopo ambapo wanachama wengine hutakiwa kurejesha mikopo kila wiki, sharti hili haliwawezeshi wakopaji kujenga uwezo wakujitegemea.

- Baadhi ya Mifuko hulazimisha riba kubwa nalo hili haliwapi wananchi kujijengea uwezo wa kujitegemea.

- Baadhi ya mabenki yanayopitishia mikopo kupitia *SACCOS* huzuia *SACCOS* hizo kufuata utaratibu wa kujiendesha Kiushirika hasa suala la uchaguzi ndani ya *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, ibara ya 87, eneo la Chamwino katika Jimbo la Chilonwa ni moja ya maeneo muhimu ambako mpango kabambe wa ustawishaji Makao Makuu Dodoma umepitia. Napongeza sana hatua hii ya Serikali na wananchi wa Chamwino na Jimbo lote la Chilonwa kwa ujumla wanaukaribisha Mpango wa Ustawishaji Makao Makuu kwa mikopo miwili na sote tunaiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo mpango huo kabambe utayagusa washirikishwe kutokea hatua za awali kabisa kwa kueleweshwa juu ya mpango huo. Hali hiyo itaepusha migogoro hapo baadaye iwapo wananchi hawatashirikishwa mapema.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ardhi na wale wa Mipango Miji waelekezwe kuwahusisha wananchi kwa kuwapa taarifa juu ya maendeleo ya upimaji maeneo na upangaji wa miji.

Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo ya kiutendaji ibara ya 47, chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP*), nashukuru sana Serikali kwa kutoa fedha za kuendeleza kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji katika shamba la ZABIBU kwenye shamba la Chinangali II, Wilaya ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa umwagiliaji katika shamba la Zabibu la Chinangali II ni mfano mzuri katika kuwashirikisha wananchi kupitia Ushirika wa Akiba na Mkopo, *FUNE SACCOS* na *CHABUMA AMCOS*.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni mitazamo tofauti juu ya uendeshaji wa shamba lile. Najua kwamba shughuli pale ni Ushirika ambapo wananchi ndiyo wamiliki lakini baadhi ya watu wanafikiri kwa vile wanachama pale wamekopeshwa na *CRDB* kupitia *SACCOS* yao pamoja na kusaidiwa na fedha za *DADPS* wanawatenga wananchi wasishiriki katika

kuendesha shughuli za shamba la Zabibu, Chinangali kupitia taratibu za Ushirika. Hakuna uchaguzi wa ushirika pale kwa vile baadhi ya viongozi hawaoni umuhimu huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Aidha, naomba tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nitajikita katika maeneo kadhaa katika kuchangia Hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ili kupunguza malalamiko yanayojitokeza katika utoaji wa zabuni za Wilaya, Bodi za Zabuni za Wilaya ziwe na Madiwani angalau wawili kuliko ilivyo sasa hivi. Bodi za Zabuni za Wilaya zimesheheni wataalam wa ngazi mbalimbali na Wilaya ambao wanawajibika kwa Mkurugenzi. Naomba Serikali iweke *combination* nzuri kwa Bodi ya Zabuni ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pili, katika Mpango wa Miaka Mitano wa Serikali pamoja na Hotuba ya Waziri Mkuu, aidha, hata Hotuba ya Waziri wa Fedha hakuna mahali popote Kiwanda cha Nyama cha Mbalizi, Mbeya kinatajwa kwamba kitafufuliwa. Ikiwa hali ndio hiyo ni kwa nini wananchi wasipewe mashamba ya Ilota ili kuyalima kuliko yakae bure.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa kuwa tatizo la Watendaji wa vijiji na Kata la kutotoa Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Je, ni kwa nini Serikali haiwezi kutengeneza njia nzuri ya kudhibiti hali hiyo. Serikali iweke mfumo mzuri wa uwajibikaji kuanzia Vijiji, Kata na hata Wilaya.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Isyonje, Makete ni barabara muhimu kwa kukuza utalii Nyanda za Juu Kusini na maeneo mengine nchini. Naomba Serikali kuangalia kwa upya Bajeti ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu ujazo wa lumbesa katika bidhaa za aina mbalimbali. Lakini kwa Mkoa wa Mbeya hasa Wilayani kwangu ni lumbesa ya viazi. Kwa nini Serikali isitoe msimamo wa Kitaifa kuhusu ujazo huu mbaya na ambao unawaumiza sana wakulima. Mageti yamewekwa na ulinzi wa kutosha lakini lumbesa zinapitishwa kwenye mageti hayo hayo. Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kudhibiti?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote kwa kuandaa Hotuba nzuri yenye matumaini ya kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania. Naipongeza

Serikali kwa mafanikio iliyofikia katika sekta mbalimbali za maisha pamoja na kwamba changamoto bado ni nyingi. Baada ya pongezi hizi napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu katika Ofisi za Bunge hasa zilizopo ghorofani si rafiki kwa Wabunge wenye ulemavu waliopo sasa na wale watakaokuja miaka ijayo. Kwa msingi huo inakuwa vigumu au shida kutumia Komputa zilizoko maeneo hayo, hivyo kushindwa kupata taarifa mbalimbali kwa kutumia *internet* na kadhalika. Naomba Serikali ione uwezekano wa kurekebisha changamoto hii haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 11 na 23, maeneo hayo yameelezea kuanza kutekelezwa kwa Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini kwa Tanzania lakini cha kushangaza Mikoa iliyoko Kusini wala haiko kwenye Mpango huo kama Lindi, Mtwara na Ruvuma. Hivyo naomba ufafanuzi wa sababu ya kuachwa maeneo hayo kwa sasa. Au Mikoa husika itaingizwa kwenye mpango baadaye?

Ukurasa wa 13, nakubaliana na Serikali katika jitihada zake za uwekezaji kwa ajili ya kuongeza mitaji, teknolojia na ajira lakini ni muhimu kufuatilia suala la ajira kwa sababu hivi sasa kuna baadhi ya wawekezaji hasa wale wa kutoka nje wanakwepa kuajiri wazawa kwa visingizo chungu mbovu na kwa wanaajiri wazawa kumekuwa na dhuluma za mishahara, manyanyaso kwa vile wawekezaji hao hawafuati Sheria za Kazi za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukurusa wa 59, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kusogeza huduma za uratibu wa UKIMWI Mikoani, Wilayani na kwenye Halmashauri nchini. Ni jambo jema lakini ieleweke kwamba unyanyapaa bado ni changamoto. Bado wananchi wengi hawako tayari kupima kwa hiari ili kujua afya zao, wengine wanakatiza unywaji wa dawa pindi wanapoona afya zao kuimarika. Zaidi ile Sheria ya Kudhibiti ya 2007 inashawishi wananchi kutojitokeza kwa sababu imeweka adhabu kali, hivyo kuongeza woga wa kujitokeza waziwazi kwa waishio na Virusi vya UKIMWI. Kwa msingi huo uwezekano wa kupambana na kutojitokeza kupima na kuwa na uwezo wa kuambukiza wengine bila kufahamika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la huduma na matibabu kwa waishio na Virusi vya UKIMWI suala la lishe limekuwa ni tatizo. Ni lazima sasa kuandaa utaratibu wa jinsi ya kutoa lishe bora sambamba na huduma ya dawa bure.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia maeneo haya machache, naunga hoja mkono.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nizungumzie elimu. Napenda kuwashukuru wananchi kwa mwamko mkubwa kuhusu ujenzi wa shule za sekondari za Kata,

nawapongeza sana. Changamoto kubwa kwa Serikali ni kuhusu walimu, nyumba za walimu, maktaba, maabara, mabweni ya kulala wanafunzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kutatua matatizo sugu ya upungufu wa walimu ni kuongeza Vyuo vya Ualimu kwa daraja la cheti na stashahada. Tutumie fursa zote zinazopatikana (*PPP*) na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu inao mpango mkakati wa kuanzisha Chuo cha Ualimu AYALABE, Karatu kwa mafunzo ya Cheti na Stashahada.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isajili Chuo cha Ualimu AYALABE, Karatu na kukiendesha. Halmashauri imejenga miundombinu yote inayotakiwa na inaendelea kujenga.

Mheshimiwa Spika, pili, nizungumzie afya. Napenda kuwashukuru wananchi kwa kuitikia wito wa Serikali kuwa na Zahanati kila Kijiji na Vituo vya Afya kwa kila Kata na Hospitali. Nawapongeza sana Watanzania kwa utayari wao. Changamoto kubwa ni wataalam katika fani hiyo Wauguzi, Waganga na Wafamasia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na changamoto hizo Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa kuzingatia utaratibu wa (*PPP*) *Public Private Partnership* imeainisha Chuo cha Afya pale Karatu *Designated District Hospital* (*KDDH*), Chuo ambacho kwa kuanzia imekusudia kutoa *Diploma in Nursing and Diploma in Clinical Officers*. Tunaomba Serikali isajili Chuo hicho na kukiendesha. Hii itatusaidia sana katika tatizo la upungufu wa wataalam wa afya.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nizungumzie suala la barabara. Bonde la Eyasi, ni eneo zuri sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa mazao ya mpunga, vitunguu, mahindi na hata mbogamboga. Ili wakulima hawa waweze kunufaika na kilimo chao mambo makuu mawili yanatakiwa kushughulikia kwa haraka; moja, ni miundombinu ya maji, mifereji, miundombinu iliyopo sasa kaikidhi haja – imetengenezwa ilivyo sawasawa na mbili, ni barabara toka njiapanda hadi Mang'ola, Matala hadi Lalago, ni muhimu sana kujengwa kwa kiwango cha lami (na hii ilikuwa ahadi ya Raisi Jakaya Kikwete 2005). Naomba Serikali itimize ahadi hiyo ya Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uzinduzi wa barabara ya Makuyuni, Mto wa Mbu, Karatu hadi Geti la Ngorongoro, Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamini Mkapa aliahidi kujenga barabara katika viungo vya Mji wa Karatu kwa urefu wa kilomita mbili. Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Magufuli ni shahidi. Naomba Serikali itimize ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nne, niongelee kuhusu kilimo. Serikali iwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji maana tuna mabonde mazuri sana kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, pembejeo, utafiti yakinifu ufanywe kuhusu aina ya udongo na aina ya mbolea inayotakiwa, mbegu zinazotakiwa na kujua hali ya hewa kupeleka pembejeo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhakikisha soko la uhakika kwa bidhaa au mazao yanayozalishwa.

Mheshimiwa Spika, tano, nichangie kuhusu umeme vijijini. Nishati ya umeme ni ya muhimu sana kwa maendeleo ya jamii hasa wale walioko vijijini. Kwa umuhimu wote naomba Serikali ipeleke umeme Mang'ola, Mbulu, Endallah na kukamilisha mradi wa kupeleka umeme Endamararick. Hii itasaidia mafanikio makubwa kwa shule za Endallah, Florian, Awet na Zahanati katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sita, nizungumzie kuhusu ardhi. Ardhi ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Hivyo, naiomba Serikali iharakishe upimaji wa ardhi (mashamba) vijijini ili wananchi wamiliki ardhi na hiyo ardhi iwasaidie kama mitaji kwa maendeleo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie utaratibu wa wananchi kuuza ardhi ovyo na baadaye wao kubaki kuwa walinzi. Tabia hii imejitokeza sana katika jimbo langu la Karatu, wenyeji wanauza sana maeneo yao kwa wageni wawekezaji bila kujali kesho yao. Kuwe na sheria itakayombana yule anayeuza, asiuze ardhi kirahisi tu.

Mheshimiwa Spika, saba nisemee suala la utawala bora. Naomba Serikali iangalie *cause effect and not only the end result*.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri, yenye mwelekeo mwema unaolenga kutetea maendeleo ya wananchi wa nchi yetu. Ni imani ya wananchi kwamba baada ya uwasilishwaji wa Hotuba hiyo, Serikali itazingatia vya kutosha malengo yaliyoainishwa kuendana na utekelezaji ulio bora ili matumizi yaliyopangwa yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali zinazochukuliwa katika kuwapatia wananchi huduma bora, ikiwemo kuwapatia mafunzo watendaji wa kila Halmashauri kwa mantiki ya kutekeleza miradi itakayotumiwa fedha kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikajikita zaidi katika dhana ya ufuatiliaji na uwajibikaji vinginevyo Serikali ichukue hatua zinazofaa zaidi. Mara nyingi kumekuwa na matumizi mabaya ya fedha, kutokuwa na uzalendo katika kujali maslahi ya wananchi yanayoendelea kutolewa na Serikali. Watumishi wenye mwelekeo huo wanafahamika, wapo katika Taasisi zetu. Serikali itakaposimamia hali hiyo itasaidia kugundua udhoofishaji unaofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu afya. Pamoja na huduma za afya kuimarishwa katika harakati za kumletea mwananchi huduma bora, lakini yapo mapungufu katika hali za kiafya za watoto pamoja na mama wajawazito kwa kukosa lishe bora kama ilivyoelezwa katika Hotuba hiyo. Changamoto hiyo inasababishwa na ukosefu wa chakula cha kutosha katika maeneo ya baadhi ya vijiji kwa mama na mtoto kukosa maziwa ya kutosha, hii

inachangiwa na njaa inayowakumba wananchi hasa kule vijijini. Ushauri wangu ni kwa Serikali ielekeze nguvu zaidi kule vijijini ili kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la elimu. Serikali imejitahidi vya kutosha kuhakikisha kwamba, changamoto zimetatuliwa siku hadi siku ikiwemo upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari. Katika kutatua changamoto hiyo Serikali imekuwa ikiajiri walimu ili wanafunzi waweze kusoma kwa upana zaidi. Ushauri kwa Serikali, kwa vile kumekuwa na tabia ya walimu hasa wale wanaopangiwa kufundisha shule zilizoko vijijini, kuomba uhamisho mara kwa mara na kuziacha shule zikiwa hazina walimu. Serikali iweke mkakati wa kutokuhama kwa walimu, hadi atimize miaka 10 katika kituo alichopangiwa labda iwepo sababu maalum.

Mheshimiwa Spika, hali kama hiyo pia inawahusisha wahudumu wa afya. Ikumbukwe kwamba Watumishi wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa kanuni na taratibu za fedha za Serikali za Mitaa zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuainisha mipango mizuri katika sekta ya kilimo. Kama tunavyofahamu kwamba nchi yetu ni maskini na hadi sasa hatujaweza kukiepuka kilimo kimahitaji, pia mchango mkubwa katika pato la Taifa. Niiombe Serikali pamoja na mipango madhubuti iliyopangwa katika kuharakisha maendeleo ya kilimo nchini yamefikiwa. Lazima tujielekeze zaidi kumuimarisha mkulima kwa kumwezesha katika suala zima la mikopo kwa wakulima wakubwa na wadogo.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyotengwa kwa kupitia Benki ya Rasilimali yaani dirisha la mikopo bado ni ndogo haitoshi kutokana na suala la kilimo ukiliangalia kwa upana zaidi. Kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

- Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta njia itakayowezesha kuongezeka kwa fedha hiyo.

- Maeneo yaliyo na mito, maziwa yaimarishwe miundombinu ya umwagiliaji kwa kiwango kikubwa.

- Riba za mikopo ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi au Jeshi la Kujenga Taifa. Mara nyingi tumekuwa tukiona juhudi mbalimbali zinazofanywa na Jeshi hili wakiwemo askari wa aina zote, katika kulinda raia na kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinakuwepo nchini. Sisi ni binadamu lazima tuendelee kuthamini juhudi hizo lakini pia maslahi yao, tunalo jukumu la kuyatatua kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, muda mrefu sasa kumekuwepo na askari waliohamishwa pasipo kupewa posho yoyote na hatima ya fedha hizo hawafahamu, muda umekuwa mrefu na wanapojaribu kufuatilia huambiwa Makao Makuu fedha imeshatoka na vocha zinaonesha fedha imetumiwa.

Mheshimiwa Spika, hivi suala hili linachukuliwa hatua gani kama fedha imetoka wameichukua akina nani? Je, nini hatima ya malipo hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi. Serikali imetambua kwamba katika utekelezaji wa uwezeshwaji wananchi zilijitokeza changamoto mbalimbali kuhusiana na utekelezaji katika kipindi kilichopita. Ni vema katika kipindi hiki Serikali ikaandaa mikakati ya kuweza kuzikubali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Hotuba hii, pili nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie upande wa kilimo, uchumi wowote katika nchi unategemea kilimo. Lakini katika mtazamo wa sekta ya kilimo katika nchi yetu bado hatujawekeza vizuri, naomba Wizara husika ijikite katika kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha kusubiri msimu wa mvua kimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, nijikite katika sekta ya uwekezaji. Katika sekta hii ya uwekezaji na yenyewe bado hatujajipanga vizuri, wawekezaji ambao wanawekeza katika nchi yetu, wamekuwa wakijitajirisha kwa kuchukua madini yetu na kuondoka nayo. Naomba Serikali wapitie upya mikataba hiyo ili madini hayo yasipotee na tuweze kuyadhibiti ili tuweze kuingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa Hotuba nzuri. Napenda kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Mahakama za Mwanzo na Wazee wa Baraza wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Naiomba Serikali iboreshe mazingira ya kazi pamoja na maslahi ya wafanyakazi wa Mahakama. Naomba wazee wa Baraza wawekewe utaratibu wa kulipwa posho maalum kwa mwezi badala ya utaratibu wa sasa wa kulipwa shilingi 1,500/= kwa kesi mpaka inapokwisha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza suala la ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Jeshi la Polisi na Mahakama katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kupatikana kwa usafiri kwa Watumishi wa Mahakama za Mwanzo ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa Watumishi wa Mahakama wanapotaka kutoa maamuzi ya kesi mbalimbali na mwishowe kupanda gari moja (daladala) na watuhumiwa au ndugu wa watu waliohukumiwa.

Mheshimiwa Spika, vijana walio mitaani ambao wamemaliza kidato cha nne napendekeza wapelekwe katika Jeshi la Kujenga Taifa ili waweze kuongeza uzalendo, taaluma na ujuzi mbalimbali. Pia napendekeza Jeshi la JKT lipewe jukumu la Ujenzi wa barabara zetu ili kulinda fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tuweke utaratibu wa kuwalinda vijna wetu ambao wanakumbwa na janga kubwa la mabadiliko ya ulimwengu katika suala zima la utandawazi. Serikali isimamie ili kuzuia mmomonyoko wa maadili kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kwake kuwa Waziri Mkuu kwa kipindi kingine. Aidha, naomba pia nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Taifa letu, ni kitu ambacho kimetupa nguvu mpya akinamama, hongera sana. Napenda kuthibitisha kwamba wewe unaimudu kazi yako vizuri kabisa, kilichopo mbele yako ni changamoto tu hasa kutoka kwa Wapinzani, pole sana, kikubwa kwako ni kukaza buti tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nichangie sasa Hotuba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri Mkuu ni Hotuba ambayo inatia matumaini na pia inatupa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla. Kwa mtazamo wangu Hotuba imegusa katika sekta zote muhimu kama vile Elimu, Maji, Afya, Kilimo, Nishati na Barabara.

Mheshimiwa Spika, nianze na elimu. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kujenga shule za Sekondari kila Kata. Kwa sasa karibu watoto wote wanaofaulu wanapata nafasi ya kujiunga na Sekondari tena kwa gharama ndogo na wanakuwa karibu na nyumbani kwao. Naomba Serikali kwa sasa iweze kuongeza jitihada za ujenzi wa mabweni, inasikitisha sana unapowaona watoto tena wa kike wakiishi kwenye majumba ya watu au kwenye mageto. Maabara na walimu hasa walimu wa masomo ya Sayansi ni tatizo kubwa kwa shule za Kata.

Mheshimiwa Spika, pia niongelee suala la maji. Mkoa wa Geita na Mwanza upo kando ya Ziwa Victoria cha ajabu maji ya ziwa yamesambazwa Shinyanga lakini Mwanza na Geita hali ni mbaya sana, akinamama wanapata tabu sana na wanatumia muda mrefu na nguvu nyingi kwa kutafuta maji badala ya shughuli zao za ujenzi wa Taifa. Tunaomba mradi huo wa maji ya Ziwa Victoria uingizwe kwenye Vijiji vya Mikoa ya Geita na Mwanza. Aidha, tunaomba Serikali ijikite kwenye miradi ya uchimbaji wa visima virefu na vifupi kwani gharama yake ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaamua kila Kata kuwe na Kituo cha Afya na kila kijiji kiwe na Zahanati. Je nani anakwamisha azma ya Serikali?

Nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweke wazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, nichangie sasa katika suala la Kilimo Kwanza. Upande wa kilimo kuna suala la *power tiller*. Kuna taarifa za tofauti ya bei ya *power tiller*, kuna Mikoa mingine wanauziwa Sh. 8,000,000/= kwa kila *power tiller* na kuna baadhi ya Mikoa wanauziwa Sh. 1,000,000/=. Msingi wa tofauti kubwa hiyo ni nini?

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie barabara. Naipongeza Serikali sana kwa kuendelea na jitihada za kujenga barabara za lami na hasa barabara iliyofunguliwa na Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Kikwete ya kutoka Mwanza, Busisi, Geita, Katoro, Chato mpaka Bukoba. Imetukomboa sana wakazi wa maeneo haya. Hata hivyo, bado tunaiomba Serikali itengeneze barabara ya kutoka Busisi, Buyagu, Ngoma, Busolwa, Nyalubele mpaka Karamwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba nzuri. Pia nampongeza Waziri wa Nchi, TAMISEMI kwa Hotuba nzuri pia yenye kuonyesha utekelezaji wa kazi za Wizara hiyo kwa mwaka 2010/2011. Huko Majimboni tunapotoka tunaona wananchi wanaona jitihada za Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo. Maendeleo makubwa yanaonekana katika miradi ya *ASDP*. Kwa upande wa Jimbo la Pangani kwa upande wa Mpango wa "Kopa Ng'ombe lipa Ng'ombe" wafugaji wachache waliopo wamefaidika na hivi sasa kwa mwezi hupata si chini ya Shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika uvuvi. *MACEMP* imefanya kazi nzuri kwa kuwapatia wananchi elimu, nyezo na kadhalika. Mpango huu lazima uendelee ili matunda yake yawafikie wengi. Wavuvi wanahitaji pia masoko mazuri ya mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Ofisi za Wakuu wa Mikoa ndio wasimamizi Wakuu wa Utendaji katika Halmashauri. Ofisi hizi zina muundo ambao washauri wa Sekretarieti ni mmoja mmoja tu, hivyo kushindwa kusimamia na kutoa ushauri ipasavyo kwa Halmashauri. Muundo wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iangaliwe upya ili kukidhi majukumu na changamoto za utekelezaji na usimamizi wa Halmashauri. Kwa misingi hiyo hiyo Ofisi za Wakuu wa Wilaya ziangaliwe kimuundo maana nazo ziko karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia niende katika Halmashauri za Wilaya. Halmashauri za Wilaya ndizo zenye majukumu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo Wilayani. Kuna uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Naomba muundo wake utazamwe upya ili kukidhi majukumu mazito ya utekelezaji hasa wakati huu ambapo tutaanza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12 -2015/2016.

Mheshimiwa Spika, nichangie vile vile katika suala la *Dar Rapid Transit*. Mradi huu umesemewa sana kwamba, kuna kusuasua sana utekelezaji wake. Wananchi

wanataka kuona katika kipindi kifupi mabasi yanatembea. Ni vema kukawa na *Out of Court Settlement* ya kesi zilizopo Mahakamani ili kuharakisha utekelezaji wake. Kesi zinachukua muda mrefu. Kaeni na wananchi wenye malalamiko ili kuondoa kesi hizo Mahakamani ili mradi uanze. Mfano, ni kesi ya wakazi wa Gerezani ambapo itakuwa *Bus Terminal*.

Mheshimiwa Spika, mwisho niongelee umeme Vijijini. Tunashukuru kuvipatia umeme vijiji vya Kibinda na Mikunguni katika Jimbo langu. Ibara ya 61 ya Hotuba. Natumaini vijiji vingine vya Kigurusimba, Mkalamo, Kimang'a Choba katika Jimbo langu vitapatiwa Umeme. Serikali iongeze fedha kwa *REA* ili iweze kuwa na *coverage* kubwa nchi nzima. Sh. 435 Bilioni kwa *REA* hazitoshi. Wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuendeleza wanawake kiuchumi kwa kuwa ndio wengi katika umaskini na wakati huo huo ndio wengi katika idadi ya wananchi (Wwatanzania 51%). Je, Serikali ina mikakati gani kutoa fursa nyingi za kuwawezesha wanawake kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa Hotuba nzuri zenye matumaini makubwa kwa Taifa letu. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni aliwaahidi wananchi wa Mtwara Vijijini kuwa atawapatia gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Nanguruwe, Je ni lini ahadi hiyo itakamilishwa? Katika Wilaya ya Mtwara Vijijini inazo zahanati za Nitekela, Njengwa, Mgao, Chawi, Mnongodi, Mnyawi na Msanga Mkuu ambazo zipo mbali na vituo vya Afya na Hospitali ya Mkoa. Naomba Zahanati hizi zingesaidiwa Bajaji za kubebea wagonjwa. Mheshimiwa Rais pia aliahidi kusaidia Kituo cha Afya cha Nanguruwe kuwa Hospitali ya Wilaya, lakini kiasi cha fedha kinachotolewa ni kidogo mno, hivyo, kuashiria kuwa itachukua muda mrefu sana kituo hiki kuwa Hospitali ya Wilaya. Tunaomba Bajeti ya Wilaya kwa ajili ya Nanguruwe iongezwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia suala la Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa kukaa kituo kimoja zaidi ya miaka 20. Hii inarudisha ufanisi wa kazi kwani baadhi ya watendaji tangu waajiriwe kwa mara ya kwanza hawajawahi kuhamishwa na baadhi yao wanastaafia kwenye vituo hivyo hivyo. TAMISEMI wafanye ufuatiliaji wajue ni Watumishi gani wamekaa zaidi ya kituo kimoja kwa zaidi ya miaka 10 ili wawahamishie vituo vingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri Mkuu kwa Hotuba nzuri, pia nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2011/2012 kwa Geita ambayo ina Halmashauri tatu sasa yaani Geita, Nyang'hwale na Halmashauri ya Mji. Kiwango kilichowekwa kulingana na *ceiling* hakitoshi. Matokeo yake itaathiri utoaji wa huduma kwa jamii. Kwa kuliona tatizo hili la upungufu mkubwa wa kifedha Halmashauri imeleta maombi maalum yenye jumla ya Sh. 26,803,160,000 kwa barua yenye Kumb. Na. GDC/D.30/20/IV/90 ya tarehe 08/04/2011. Nami niungane na Halmashauri kuiomba Serikali nyongeza ya fedha hizo kwani fedha hizo zimepangwa kutumika katika sekta za Afya, Elimu na Utawala. Sekta hizi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kupitia nyongeza ya fedha hizi matumizi yake ni pamoja na ununuzi wa Magari matatu ya kubebea wagonjwa katika vituo vitatu vya Afya. Katika Jimbo la Busanda vituo vya Afya vya Katoro na Chikobe vinauhitaji mkubwa wa kuwa na magari. Katika Bajeti ya mwaka jana yaani 2010/2011, Serikali iliahidi kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya, Chikobe.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ikumbuke ahadi hii maana kituo hiki kiko mbali sana na Hospitali ya Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la walimu kumalizika. Kwa nyakati mbalimbali Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya kumaliza uhaba wa walimu wa shule za Sekondari. Mwaka 2009 Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Gaudensia Kabaka wakati akiwahutubia wanachuo wa Chuo cha Ualimu, Bunda (rejea gazeti la kulikoni la tarehe 3 Machi, 2009) alisema tatizo la upungufu wa Walimu ni la muda mfupi na kwamba muda si mrefu shule zote za sekondari zilizojengwa na wananchi zitakuwa na walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ahadi hii utekelezaji wake umefikia wapi? Hususan kwa Jimbo la Kawe, ambalo shule za wananchi zina upungufu mkubwa wa walimu. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aniambie kwa mwaka huu wa fedha utakaonzia 1 Julai, 2011, Serikali ina mpango wa kuajiri walimu wapya wangapi?

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kuhusu malipo ya madai ya Walimu. Serikali iliahidi kulipa madeni yote ya Walimu kutokana na kukamilika kwa mchakato mzima wa ulipaji madeni hayo. Kauli hii ilitolewa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi(aliyepita), Profesa Jumanne Maghembe wakati akiwasilisha Bungeni makadirio ya Bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itoe taarifa kwenye Bunge, mchakato huu umefikia wapi? Ni walimu wangapi wamelipwa malimbikizo husika? Kama malimbikizo

husika yamelipwa ni malipo yote au kuna wanaoidai Serikali bado? Pia kama wapo wanaodai, Serikali ina mkakati gani wa kulitatua hili? Je, katika Bajeti ya mwaka huu ni fungu kiasi gani lilitengwa kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya walimu nchi nzima na hususan Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Moja kati ya matatizo makubwa yanayozikumba Halmashauri zetu ni ubovu wa barabara za ndani ambazo ziko chini ya Manispaa husika. Katika maelezo ya kiutendaji ya Mheshimiwa George H. Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ametamka kwamba hadi kufikia Machi 2011, jumla ya kilometa 8,059 zilifanyiwa matengenezo mbalimbali kati ya kilometa 21,6036 zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Matengenezo ambayo ni pungufu ya 50% ya malengo. Nini chanzo cha kutotimizwa lengo husika? Je, kuna matarajio ya kukamilishwa kwa matengenezo husika kwa kipindi kilichobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Wabunge wengi, imegusia kwa kiasi kikubwa suala la *UDOM* lakini cha kusikitisha suala hili limekuwa likizungumzwa kisiasa zaidi na kama Ofisi yako isipochukua hatua, hali tete ya UDOM itaendelea kwa kipindi kirefu sana. Malalamiko makubwa yanayokihusu Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) ni kwa jinsi *management* inavyofanya kazi yake na hili haliwagusi wanafunzi pekee, linawagusa hata watumishi wa chuo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba wakati Waziri Mkuu alipotembelea Chuo cha UDOM kufuatia mgomo wa Walimu, aliambiwa kwa uwazi chanzo cha mgomo na vurugu mbalimbali zinazotokea katika chuo hicho. Kufuatia maelezo toka kwa wafanyakazi, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulitoa maagizo kwa chuo kufanya *decentralization* kwa kupeleka madaraka kwa *colleges* kutokana na ukweli kwamba kulikuwa na urasimu mkubwa sana pale maamuzi yalipokuwa yanafanyika kutoka ngazi ya Utawala.

Mheshimiwa Mwenyeketi, mapendekezo kama haya yalitolewa na Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kuzingatia kwamba Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) ni kikubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli yako uliwaahidi kushughulikia hili, mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Kumekuwa na malalamiko sana kuhusiana na jinsi chuo kinavyoendeshwa. Hakuna *security* ya kazi, watu wanafukuzwa ovyo wakipingana na wakubwa. Hata wale wafanyakazi ambao waliamua kuwa wawazi pale alipokitembelea chuo, ajira zao ziko kwenye hati hati. Chanzo cha migogoro husika kinajulikana. Kwa nini hamchukui hatua?

Mheshimiwa Mwenyeketi, nizungumzie udini katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Nchi yetu ina mjumuiko wa dini na makabila mbalimbali na hakika tumeweza kuvumiliana na kuheshimiana kwa kila mtu kuheshimu imani au kabila la mwenzake. Cha kusikitisha suala hili linapandikizwa kwa kasi kubwa sana na mbaya zaidi viongozi Wakuu wa Chuo wanahusika na ushahidi upo.

Mheshimiwa Mwenyeketi, naamini kabisa Waziri Mkuu analijua hili na ninamsihi kama halijui alifanyie utafiti wa kina. *Management* inashindwa kutekeleza wajibu wake, wanafunzi na walimu wa Kigoma, wanatoa visingizio vya ushiriki wa vyama fulani fulani na kibaya zaidi udini pia umekuwa ukitumiwa.

Mheshimiwa Mwenyeketi, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ayafuatilie haya masuala kwa ukaribu ili kulinda heshima yake kama kiongozi anayesimamia mambo aliyoyatolea maamuzi au maelekezo.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo. Napongeza mpango wa Serikali wa kuhakikisha yanakuwepo mapinduzi ya kilimo kwa kauli mbiu yake ya Kilimo Kwanza. Nchi yetu imebahatika kuwa na sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba, hali ya hewa nzuri kwa kilimo cha mazao mbalimbali na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya kuwa na kilimo chenye tija, nashauri Serikali ichague mazao machache ya chakula na mazao ya biashara. Mazao ya chakula, naishauri Serikali iweke mkazo kwenye kilimo cha mahindi, mpunga na alizeti hasa kwenye yale maeneo ya kilimo cha umwagiliaji kisha wakulima wajengewe uwezo kwa kuhakikisha wanapata elimu ya kilimo bora na cha kisasa, Serikali itoe ruzuku ya pembejeo na zana za kilimo ili maeneo haya yaweze kuzalisha chakula cha kutosha na ziada waweze kuuza nje ya nchi. Hii itasaidia Serikali kuachana na mpango uliopo sasa wa kuhifadhi chakula kwenye maghala kwa ajili ya kipindi cha njaa, ambapo tumeshuhudia kila mwaka wananchi wanakumbwa na baa la njaa.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu mazao ya biashara. Katika kilimo cha Pamba, Korosho, Kahawa na *Cocoa,* wakulima wajengewe uwezo ili waweze kuzalisha kwa wingi, kwa kupatiwa zana za kilimo na pembejeo za kutosha, mikopo ya riba nafuu kwa wakulima na uhakika wa soko la ndani na nje ya nchi. Kupitia soko la ndani Serikali ifufue viwanda vya ndani ya nchi ili hatimaye tuweze kuuza bidhaa nje ya nchi na hatimaye kuongeza thamani ya pesa yetu.

Mheshimiwa Spika, nije katika Sekta ya Uvuvi na Ufugaji wa Nyuki. Mazao ya samaki na asali yanahitaji Serikali kuweka nguvu kidogo kwa sababu ni maeneo ambayo yanahitaji kuvunwa na nchi kujiongezea pato kwa kipindi kifupi ikilinganishwa na maeneo mengine ya uzalishaji ambayo yanahitaji gharama kubwa za uwekezaji. Nashauri Serikali katika kuelekea utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa 2011 – 2016 iwe na mkakati maalum wa kuhakikisha tunajenga uwezo maeneo haya ya uvuvi wa samaki na ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie kuhus nishati. Tatizo la umeme limekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya nchi, bila kuwa na mkakati maalum wa kumaliza tatizo hili, naamini itakuwa vigumu kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuhakikisha uchumi wa nchi unakua hadi kufikia uchumi wa kati. Nashauri kama

ilivyofanyika katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, Serikali ilitafuta fedha na kufidia wakulima. Muda umefika kwa Serikali kuhakikisha inatoa kipaumbele kuhakikisha fedha zinapatikana kwa wakati ili miradi ya umeme itekelezeke ndani ya kipindi kilichowekwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam. Imekuwa kero kwa Jiji hilo hivi sasa kwa msongamano mkubwa wa magari, suala ambalo linarudisha nyuma uchumi wa nchi, kwani foleni hiyo huwacheleweshea wafanyakazi ambao ni nguvu kazi ya Taifa letu. Ushauri ni kwamba, mpango wa Serikali wa kutanua baadhi ya barabara, basi ifanye makusudi na itenge fedha za kuendeleza mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Bandari za Mtwara, Tanga na Dar es Saalam. Ujenzi huu napendekeza uendelee kwa kujengwa vizuri, ujenzi huo uanze mara moja baada ya kupitishwa kwa Bajeti hii. Vile vile nashauri katika utekelezaji wa miradi hii Serikali iwe *serious* na kwa yule atakayefanya uzembe au kukwamisha au ubadhirifu achukuliwe hatua za kinidhamu bila ya kuchelewa na baadaye taarifa tuletewe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nije katika usafiri wa reli. Nashauri kwamba iwapo mradi huu utatekelezwa kwa kipindi hicho ikiwa kwa pesa zetu au hata za mkopo, mradi huu utaleta tija ya kuongeza uchumi, maendeleo kwa jamii, pia utaweza kurejesha mkopo na kuingiza pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, niongelee pia suala la umeme. Inavyoonekana suala la umeme hapa Tanzania halitiliwi mkazo, kwani tumeambiwa kuwa tuna visima vingi vya umeme, lakini haviwatoshelezi wananchi. Hivyo, naishauri Serikali kusimamia ipasavyo suala la kueneza umeme nchini, hivyo shirika la *TANESCO* ni bora lisipewe kazi ya kusambaza umeme nchini kwani shirika hilo limeonesha halina uwezo wa kuifanya kazi hiyo na wananchi walio wengi wanalilalamikia.

Mheshimiwa Spika, vile vile niongelee kuhusu suala la Katiba. Watanzania wengi wamekuwa wakiisikia tu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kuiona au hata kusomewa hawajapata kusikia. Aidha, Taifa letu limo katika utaratibu wa kutaka kuunda Tume maalum ya kukusanya maoni kutoka kwa wananchi kwa madhumuni ya kutunga Katiba mpya. Nashauri kwamba kabla ya kukusanywa kwa maoni hayo, ni vema Serikali ikaweka utaratibu maalum wa kuwaelimisha wananchi wake kwa kuwasomea kipengele kimoja kimoja na waweze kuifahamu, na baadaye ndio kazi ya kukusanya maoni ifanyike. Vile vile nashauri kwamba suala la Katiba litolewe ufafanuzi kupitia shule, vyuo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho niongelee suala la Muungano. Kwanza natamka kwamba Muungano uendelee na usivunjwe, ila nashauri kero za Muungano zichukuliwe

hatua mara moja kwani kuchelewa kuchukuliwa hatua kwa kero hizo ndio maana kunaleta malalamiko kwa upande wa Zanzibar. Kuhusu hili, Serikali ilipe msukumo wa pekee na kama kuna watu ambao wanasitisha zoezi zima la kutatua kero za Muungano wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwezekana hata kusimamisha kazi. Nashauri hivyo kwa sababu wananchi wameshaanza kukata tamaa ya utatuzi wa kero za Muungano.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano) mingine ambayo hii inaonyesha ni jinsi gani wananchi wa Tanzania walivyo na imani naye katika kuliongoza Taifa letu hili. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda kwa Hotuba yake nzuri ambayo ameiwasilisha hapa Bungeni. Aidha, nakupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kufungua ukurasa mpya wa Historia ya nchi yetu kwa kuwa na Spika mwanamke. Nakupongeza sana na naamini kwamba unaweza. Sasa naomba niende kwenye mchango wa Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze na Hali ya Kisiasa. Napenda kuanza mchango wangu kwa kuliangalia suala la hali ya kisiasa nchini Tanzania. Ingawa Serikali ilikuwa na nia njema kabisa kufungua milango ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya siasa pamoja na kutoa uhuru mpana kwa vyombo vya habari katika kuripoti matokeo mbalimbali yanayotokea hapa nchini. Napatwa na wasiwasi kwamba iwapo Serikali yetu haitokuwa makini katika kuweka utaratibu maalum wa udhaifu wa matendo ya kila siku ya Vyama vya Siasa na kuweka ukomo wa namna ya utoaji wa taarifa kwa vyombo vyetu vya habari, basi Taifa letu lina uwezekano wa siku moja kuingia katika mgogoro mkubwa wa kisiasa kwa kuwa kuna baadhi ya Vyama vya Siasa vinajaribu kuchochea kwa makusudi hali ya uvunjifu wa amani ya nchi yetu na hasa kwa kuvitumia vyombo vya habari vilivyo tayari kutumika katika kuleta vurugu za kisiasa kwa kutumia mgongo wa hisia za hasira kutoka kwa wananchi dhidi ya Serikali yao iliyopo madarakani. Hivyo, naiomba Serikali kuweka utaratibu maalum wa udhibiti wa matendo ya Vyama vya Siasa pia kuviwekea mipaka ya utoaji wa habari vyombo vyetu vya habari usifikie hatua yenye kuashiria uvunjifu wa amani ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie katika uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira. Katika suala la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa kuwa sisi sote tunaelewa kwamba suala kubwa linaloitafuna nchi yetu hivi sasa ni suala la ukosefu wa ajira na hasa kwa vijana wetu wanaomaliza masomo yao, hivyo ningeiomba Serikali yetu sasa kupeleka fedha nyingi zaidi katika Taasisi zinazojishughulisha kwa karibu zaidi na kazi za kiuwezeshaji wananchi kwa kuwa kufanya hivyo kunaweza kuwafikia wananchi wengie zaidi na hasa wale wa vijijini na hivyo kupunguza mzigo mkubwa unaoikabili Serikali yetu, tatizo la ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, uhalisia wa suala hili unaweza kuonekana katika kuanzishwa Mfuko wa mabilioni ya Kikwete, aidha, uwepo wa Mfuko wa *TASAF*. Mifuko hii

imeweza kutoa picha nzuri ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na kusaidia sana tatizo la ukosefu wa ajira kwani mara baada ya kuanzishwa kwa Mifuko hii wananchi wameweza kwa asilimia kubwa kutumia fursa hii na hivyo kuinua hali zao za maisha kupitia fursa hii. Hivyo naiomba Serikali kuimarisha zaidi uwepo wa mifuko hii kwani inaonyesha uwezekano mkubwa wa ukombozi wa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kuhusu Muungano. Suala la Muungano wetu ni pana sana hivyo linahitaji uangalifu mkubwa katika kulizungumzia kwake. Hivi sasa inaonekana kuwa ni kama utaratibu uliozoeleka wa kila mtu kuzungumzia kero za Muungano. Nionavyo mimi ili suala la kero za Muungano liweze kupatiwa ufumbuzi wa kudumu, basi ni lazima kuwepo na utayari wa ile Kamati inayoshughulikia kero hizo wa kutoa taarifa za kila kero inayomaliza kufanyiwa kazi, basi iwe inachapishwa katika vyombo vya habari na hasa magazeti na redio ili wananchi waweze kuona ni juhudi gani zinazochukuliwa na Serikali yao katika kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchangia katika sekta ya madini, kwa vile Bunge letu Tukufu limepitisha Sheria mpya ya Madini katika mwezi wa Aprili, 2010. Sheria hii italeta mapinduzi makubwa katika eneo la uchimbaji wa madini, pia itasaidia sehemu kubwa katika kilio cha Watanzania ambacho wanasema mali yetu nyingi inachukuliwa na wageni bila ya sisi wenyewe kunufaika na mali hii, pia itasaidia kupandisha pato letu la Taifa, iwapo Kampuni za madini zitaweze kulipa mrahaba itakuwa vema kwa kuwasaidia wale wanaoishi karibu na sehemu za uchimbaji madini badala ya kuachiwa mashimo matupu na kupata tija.

Mheshimiwa Spika, pia itasaidia tatizo kubwa la wachimbaji wadogo wadogo na wakubwa la kugombania maeneo. Iwekwe sheria madhubuti ili kuwalinda wachimabji wadogo wadogo ambao wengi wao ni Watanzania ambao ndio wenye haki ili kupunguza matatizo na kuweka amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu Muungano. Vikao vinafanyika kati ya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Serikali ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ingefaa makubaliano yote yaliyotiwa sahihi katika mikutano inayofanyika kwa kupungua na kuyafanya mambo yawe mepesi katika Muungano wetu naomba yafanyike mambo yafutayo:-

- Zanzibar mapato yake mengi yanategemea biashara, sasa uwekwe mpangilio maalum katika sekta ya biashara, ili isaidie Zanzibar kukuza uchumi wake.

- *TBS* ni chombo muhimu kwa Tanzania yetu hii, ingekuwa bora ikafanyiwa Ofisi Zanzibar ili kusaidia udhibiti wa uingizaji wa vifaa vibovu na visio na umadhubuti unaotakiwa.

- Bodi ya biashara za nje, ijenge ushirikiano wa dhati kwa kufanya shughuli zake, pamoja na wafanyabiashara wa Zanzibar kwa vile hii ni Taasisi ya Tanzania katika biashara za nje.

- *BOT* ndio Benki Kuu kwa Tanzania, iweke mikakati maalum katika kuwasaidia wafanyabiashara wa Zanzibar katika kukuza uchumi wa Zanzibar pamoja na Tanzania kwa ujumla.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nilipewa nafasi ya kuchangia lakini muda haukunitosha. Naomba nitoe malalamiko yangu kuhusu wachimbaji wa madini ya shaba katika Kata ya Ibaga, kijiji cha Ilongo.

Mheshimiwa Spika, kwanza wachimbaji wadogo wapewe leseni za uchimbaji. Eneo hilo wamemilikishwa wao sio vinginevyo. Ili kuepuka migogoro itakayojitokeza baadaye.

Mheshimiwa Spika, gari la wagonjwa lirudi katika Kata ya Ibaga ili liweze kutoa huduma kwa wagonjwa Tarafa ya Kivume.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanajitahidi kujenga vituo vya afya lakini dawa hakuna. Tunaomba Serikali itoe tamko kuhusu Hospitali za Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, suala la ardhi, ili tuwalinde Wahadzabe wasinyang'anywe ardhi yao na makabila mengine. Mfano, Wasukuma, Wambulu na kadhalika, Serikali ihakikishe wanapewa hati ya kuwalinda, hati miliki. Hapa natoa mchango wangu wa mawazo, naomba walitekeleze.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri Mkuu kwa Hotuba na hali halisi ya nchi yetu. Nakwenda moja kwa moja kwenye uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira. Katika kutekeleza Ilani ya Chama Tawala, CCM tumeweza kuwahamasisha wananchi kuunda vikundi kwa ajili ya kuwezeshwa kwa mikopo na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwezeshe Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kuongeza Bajeti ili kutimiza azma ya Serikali ya Chama Tawala yaani Chama cha Mapinduzi kuondoa umaskini nchini. Maofisa Ushirika katika ngazi ya Wilaya ni kama wamekufa kwani Idara hii katika Halmashauri inadharauliwa sana kama haipo. Naiomba Serikali kupitia Wizara hiyo ya Ushirika na Masoko itoe fungu moja kwa moja kwenda katika Halmashauri za Wilaya, kwa kweli itasaidia sana katika kuelimisha wananchi na pia Semina kwa kuweza kuanzisha *SACCOS* katika kila Kata.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kuwawezesha wananchi kupitia *SACCOS* na vikundi vilivyoundwa, itungwe Sheria au kuunda moja ya Mashirika ya kufungua Benki nchini kuwakopesha *SACCOS* kwa riba nafuu ili iweze kuwakopesha wananchi kwa riba nafuu. Naamini kwa riba ya sasa hata kama atafanya biashara lakini hawezi kumudu kulipa deni.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa kampeni tuliyofanya na tuendelee kuwahamasisha wananchi kuunda vikundi ili tuweze kuondokana na umaskini na kuongeza ajira. Naomba Serikali iziombe Taasisi zote zinazotoa mikopo au zinazowezesha kufungua Ofisi zao kila Mkoa ili ziwe karibu na walengwa kuepuka gharama za ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, nashukru na naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu kaeleza kuwa hali ya kisiasa nchini ni ya kuridhisha. Vyama vya Siasa na wananchi wanaendelea kushiriki kwa uhuru katika shughuli za kisiasa. Naona hali ya kisiasa nchini sio shwari, Jeshi la Polisi linatumiwa kuzuia shughuli halali za Vyama vya Siasa na asasi nyingine. Tarehe 28/12/2010 Chama cha *CUF* kilizuiwa kufanya maandamano ya kuwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Rasimu ya Katiba mpya iliyoandaliwa na wadau mbalimbali kati ya 2006 na 2011. Tarehe 16 Aprili, Polisi Mkoa wa Dar es Salaam walizuia mkutano uliondaliwa na *Tanzania Centre for Democracy* (*TCD*) kufanyika *Karimjee Hall* kujadili Muswada wa mabadiliko ya Katiba. Mgeni Rasmi wa mkutano huo alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Jaji Joseph S. Warioba. Washiriki wa mkutano huo akiwemo Jaji Warioba walizuiwa kuingia *Karimjee Hall* kwa madai kuwa mkutano huo unaweza kuvunja amani. Mwenyekiti *TCD* alilazimika kumpigia simu *IGP* aingilie kati ili mkutano wa ndani wa *TCD* uruhusiwe kuendelea. Kwa bahati *IGP* alitumia busara na kuruhusu mkutano uendelee.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haina uwezo wa kusimamia Sheria ya Gharama za Uchaguzi, chama kinawasilisha taarifa hizo zimerejeshwa kwa maelekezo kuwa zifanyiwe uhakiki kwanza na Mkaguzi wa Mahesabu wa chama kabla hazijapelekwa kwa Msajili wa Vyama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameisifu sana Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuandaa na kusimamia uchaguzi Mkuu wa Uraisi, Ubunge na Udiwani nchini kwa mafanikio makubwa. Ukweli ni kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeshindwa kuandaa na kusimamia uchaguzi Mkuu kwa misingi ya uhuru na haki. Tume ya Uchaguzi imeonekana kuwa ni Tume ya uchakachuaji. Uchaguzi Mkuu wa 2010 uligubikwa na utata wa uchakachuaji wa matokeo na ushiriki mdogo wa wapiga kura walioandikishwa kutokana na matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa na mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi imedhihirika wazi kuwa Tume iliyopo haina sifa za kuweza kuaminika mbele ya macho ya Watanzania hasa ukizingatia kasoro, udanganyifu na mfumo wa uchakachuaji wa idadi ya wapiga kura waliojitokeza kwa 8,626,283 kati ya wapiga kura 20,137,303 waliodaiwa kujiandikisha hivyo kufanya idadi ya waliopiga kura

2010 kwa asilimia 42.8 tu ya wale waliojiandikisha. Hii ni tofauti kubwa sana ukilinganisha na waliojitokeza kupiga kura 1995 (76.7%), 2000 (84.4%) na 2005 (72.4%).

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wamepoteza kabisa imani kwa Tume ya Uchaguzi iliyopo inaweza kusimamia Uchaguzi ulio huru na wa haki. Tunahitaji Tume Huru ya Uchaguzi yenye uadilifu na uwezo wa kusimamia na kuendesha uchaguzi huru na wa haki ili kuepuka balaa na shari kubwa inayoweza kutokea kwa sababu ya usimamizi mbovu wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu kuimarisha Bunge. Ili kuimarisha Bunge katika jukumu lake la kusimamia Serikali Ofisi ya Bunge iwe na Taasisi huru ya Bajeti *Independent Parliamentary Budget Office* itakayokuwa inafanya uchambuzi huru wa masuala ya bajeti kulisaidia Bunge kutathmini Bajeti inayoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Vyuo Vikuu. Bodi ya Mikopo ni moja ya sababu inayosababisha umalaya kwa wanafunzi wa kike wa Vyuo Vikuu na ikiwa Taifa linajitahidi kupunguza maambukizo ya UKIMWI, kwa mtindo wa Bodi hii ni kuzidisha UKIMWI kutokana na wanafunzi kujiuza miili yao ili wasome. Naishauri Serikali, irejee mtindo wa zamani wa kuwepo *cafteria* na wapewe vyakula vizuri. Wanafunzi wasiende kula kwa mama ntilie. Waepushwe na mawazo ya wapi watapata chakula. Pia Serikali ifanye bidii haraka kujenga mabweni ya kutosha katika Vyuo Vikuu vyote ili kuepusha wanafunzi wa kike kupanga vyumba uraiani na kusababisha umalaya mkubwa katika Taasisi ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itilie maanani. Ahsante.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kutimiza ndoto yangu ya kuwa Mbunge katika Bunge lako hili Tukufu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake, ari, nia na moyo wake wa kizalendo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa na Mwenyezi Mungu neema nyingi sana za asilia, ambazo ni rasilimali muhimu na chachu ya maendeleo. Rasilimali hizo ni pamoja na watu, ardhi, misitu na wanyama pori, bahari, mito, maziwa, madini aina zote, hali ya hewa, jiografia ya nchi, utulivu, amani, mshikamano na upole na ukarimu wa watu wetu**.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na neema zote hizo nilizozieleza, kuna tatizo dogo linaloendelea kukua. Tatizo hili ni *lack of accountability*, *efficiency and selfishness*. Serikali isimamie kikamilifu matatizo hayo niliyoyataja. Iwapo itafanya hivyo bila ya kigugumizi, hofu, upendeleo wala uonevu kwa yeyote, uchumi wa nchi yetu utakua kwa asilimia 10 (*10% Economic Growth*) kwa mwaka katika muda wa miaka mitatu (*3 years*) tu ijayo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie upya mikataba ya madini ili nchi ipate gawio (*divided*) ya faida inayopatikana katika madini angalau asilimia 20. Pia naishauri Serikali itoze ada ya leseni za uvuvi wa bahari kuu dola 60,000 za Marekani kwa mwaka na Serikali ipate angalau asilimia 10 ya thamani ya samaki wanaovuliwa. Wavuvi wadogo wazalendo wawezeshwe ili wavue uvuvi wa kisasa ili kuunda ajira kwa watu wetu na Serikali ipate mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Rais Mheshimiwa Kikwete atuboreshee mshahara na posho zetu Wabunge ili tuchape kazi vizuri na tumsaidie kujenga nchi. Aachane na porojo za wasiojua wafanyacho wala watakacho.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikupata muda wa kutosha kuzungumzia matatizo mbalimbali au changamoto za maendeleo Kitaifa na kwa wananchi wa Ngara, naomba nichangie Hotuba hii kimaandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu sekta ya Elimu na Afya. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*FYDP*) pamoja na Bajeti ya Serikali, sekta hizo mbili hazikuwekwa katika vipaumbele. Najua rasilimali ni nyingi lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu bado sekta hizo mbili zina changamoto nyingi sana. Lugha iliyotumika katika Hotuba ya Waziri wa Fedha ni kwamba Serikali itaendelea kulinda mafanikio yaliyokwishapatikana katika Elimu na katika Afya. Katika Wilaya ya Ngara bado tuna tatizo la uhaba wa Walimu katika shule za sekondari na shule za msingi. Tuna uhaba mkubwa wa maabara na maktaba katika shule za sekondari ambazo ni 24 na shule za msingi 114. Hatuna vitabu vya kutosha vya kufundishia, vitabu ni vichache sana havikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, hatuna nyumba za walimu na mabweni (*Hostels*) kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Wakati wa MMEM I *capitation grant* ilikuwa Sh. 10,000/= kwa kila mtoto wa shule ya msingi, sasa hivi *capitation grant* huko Ngara ni Sh. 200/= kwa kila mtoto ndiyo maana shule hazina vitabu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afya utekelezaji wa mpango wa MMAM bado sana katika Wilaya ya Ngara. Ngara ina Kata 20, lakini tunavyo vituo vya Afya vinne, tu. Ngara ina Vijiji 72, lakini tuna Zahanati 43 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ulinzi na Usalama, Ngara ina matatizo ya Ulinzi na Usalama kwa sababu ya kupakana na nchi za Burundi na Rwanda. Bado kuna ujambazi ambao unaweza kudhibitiwa na Serikali. Ujambazi mwingi unatoka upande wa Burundi. Naiomba Serikali iendelee kuchangia katika vituo vya Polisi tunavyovijenga kama wananchi. Tatizo kubwa tulilonalo, sasa ni kuingiliwa na wahamiaji haramu kutoka nchi za Rwanda na Uganda. Ngara imefurika kwa ng’ombe kutoka nchi hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro mkubwa kati ya wahamiaji hao na wakulima wa Ngara, mgogoro wa ardhi. Jambo la kusikitisha ni lile la wahamiaji haramu kuwaua wakulima sita katika Kijiji cha Murubanga, Kata ya Murusagamba. Jambo hilo halikubaliki, hivyo naiomba Serikali iingilie kati na imalize migogoro ya Wilaya ya Ngara imeshindwa kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni usimamizi wa TAMISEMI wa Watendaji wa Halmashauri na hasa katika utekelezaji wa Miradi ya maendeleo na fedha wanazopewa kwa ajili ya maendeleo. Kuna uvujaji wa fedha za maendeleo na hasa kupitia wakandarasi mbalimbali. Tatizo hilo lipo Ngara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika Ngara na kujionea umaskini uliokithiri. *Per Capita Income per annum* kwa mwananchi wa Ngara ni Sh. 170,000/= wakati *Per Capital Income* Kitaifa ni zaidi ya Sh. 700,000 kwa mwaka. Ngara inahitaji mpango kama *SAGCOT* (*marshal plan*) upendeleo wa makusudi kuinua hali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kabanga *Nickel* ni wa pili duniani kwa ukubwa (*Deposits za Nickel*). Ni wa pili kwa ule wa Canada. Kabanga *Nickel* inahitaji umeme *megawatt* 30. Naiomba Serikali iwezeshe *TANESCO* ili iweze kutoa umeme huo. Kabanga *Nickel* inahitaji pia Reli kubebea *Nickel* itakapokuwa imechimbwa. Reli hiyo ni ile itakayojengwa kutoka Isaka kwenda Burundi na Rwanda kupitia Keza iliyoko Ngara. Kituo cha Keza ndicho kitakuwa *Junction*. Reli ya kutoka Keza kwenda Msongati Burundi ndiyo itapita Kabanga *Nickel*.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali ishughulikie mradi wa Rusumo *Falls,* mradi wa pamoja na nchi za Burundi na Rwanda ili Wilaya ya Ngara na Wilaya zingine za jirani zipate umeme wa *Grid*. Wananchi wa Ngara wanaulizia mradi huo utaanza na kukamilika lini. Wana hamu sana ya kupata umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali iheshimu ahadi za Rais alizozitoa wilayani Ngara wakati wa kampeni. Raisi aliahidi umeme Mji mdogo wa Rulenge na Miji Midogo ya Rusamo na Benaco. Pia Raisi aliahidi barabara ya lami kutoka Mnzani (Nyakahura) kupitia Keza, Rulenge hadi Murugarama.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2011/2012, pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika

kutusaidia sisi kama Wabunge, lakini pia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kiutendaji kwa Serikali na wananchi kwa ujumla bila kuchoka na bila woga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri niliyoainisha, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo machache kuwiana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla. Hotuba ya Waziri Mkuu imeonyesha jinsi uchaguzi mkuu ulivyoendeshwa na matokeo ya jumla katika Majimbo yote ya uchaguzi huku ikionyesha CCM iliongoza kwa kupata viti vingi zaidi. Pamoja na ushindi huu naiomba Serikali sikivu ya Chama Cha Mapinduzi ifanye kila liwezekanalo kuulinda ushindi huu na isiache watu wakaendelea kutukana na kukashifu matokeo yake, kupotosha umma hali inayopelekea wananchi wenye imani na Serikali yao wameanza kupata wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali iliyopo sasa suala la kilimo ni muhimu sana na kama Hotuba ilivyoainisha ni vema tukatilia mkazo zaidi katika dhana bora, napendekeza tuyatumie vizuri majeshi yetu ya Jeshi la Kujenga Taifa, Magereza, Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kuyapa teknolojia na pia tuwaongezee mtaji ili wafanye kilimo cha biashara na kupunguza pengo la chakula na pia hata kupunguza gharama za bei za vyakula ambazo zinaongezeka kutokana na uagizaji wa chakula nje ambapo biashara hii huendeshwa zaidi na Makampuni binafsi ambayo hayazingatii maslahi ya mlaji kwa maana ya mwananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba hii nimeona kuwa kuna mpango uliobuniwa na kuanzishwa ili kutoa msukumo wa kilimo na kuitekeleza vema dhana ya Kilimo Kwanza ambao unaitwa (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*). Mpango huu ni wa miaka ishirini (20) na kwa jina imeanisha kwamba ni mpango wa Kusini mwa Tanzania ila ni ajabu sana kuona mpango huu hauhusishi Mikoa ya Lindi, Ruvuma na Mtwara ambayo huwezi kuitaja Kusini ya Tanzania bila kuiweka. Naomba hili liangaliwe upya na mtupe nafasi nasi tuweze kushiriki na kunufaika na mpango huu kabambe.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uvuvi yamepewa kipaumbele ila napenda Serikali ichukue hatua zaidi kuimarisha Ulinzi Baharini kwa maana mpaka sasa hali ni mbaya na wananchi wanazuiwa kuvua baadhi ya maeneo huku wengine (wageni) wanavua na kuondoka na rasilimali hizi bila kuzingatia malipo au athari zozote ambazo zinajitokeza baadaye. Ni kheri wananchi wanaozuiwa kuvua basi wapewe mbinu mbadala ili kujiendesha katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji wa nyuki, nakubali ni njia bora sana katika kuimarisha uchumi ila tatizo kubwa ni elimu kwa wakulima. Lakini tatizo lingine kwa maeneo yetu ni migogoro isiyokwisha baina ya wananchi na viongozi kuhusu matumizi ya misitu ukizingatia kuwa, eneo letu limezungukwa na *Selou Game Reserve*.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ardhi katika nchi yetu ni kubwa sana na ipo haja sasa ya Serikali kuangalia upya namna ya kuboresha eneo hili kwa maana waathirika wakubwa ni wananchi ambao ni wa kipato cha chini. Naishauri Serikali iendelee

kuboresha Mabaraza ya Ardhi ambayo yamesaidia kupunguza migogoro, lakini yanazidiwa na wingi wa mashauri na upungufu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano, ipo haja sasa ya kuipitia hii sera ya kuyafanya Mashirika na Makampuni ya Simu yazingatie kutoa huduma bila kuangalia zaidi maslahi ya kibiashara kwa maana maeneo mengi hayana mawasiliano ambapo katika Jimbo la Kilwa Kaskazini maeneo kama vile Mitole, Mingumbi, Kandawale na Chumo yamesahaulika. Tuangalie pia uwezekano wa kuiwezesha Kampuni ya *TTCL* ili ijitanue zaidi na kuboresha huduma za mawasiliano ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mkakati wa kuunganisha maendeleo ya viwanda (*Intergrated Industial Development Strategy*) ili kuongeza thamani ya mazao mbalimbali nchini. Pamoja na mpango huu tuhakikishe tunapata namna bora zaidi ya kufufua viwanda vyetu bila kutegemea wawekezaji wa nje ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa mzigo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, hii pia inapelekea kelele nyingi kwa wasiofahamu maana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma zote kwa maana ya Afya, Elimu na Kilimo, ipo haja ya Serikali kutoa motisha kwa wale wanaofanya kazi maeneo ya vijijini kwa maana wapo katika mazingira magumu sana. Viwango vya mishahara havina tofauti na wanaoishi mijini hivyo inapelekea wengi kupenda kukimbilia mijini na wale walio vijijini kuhisi kuwa wanaonewa na wamepoteza thamani.

Mheshimiwa Spika, suala la maeneo mapya ya utawala limezua mjadala mkubwa sana katika eneo letu la Wilaya ya Kilwa kiasi cha wananchi kutokubaliana na hali ya kuwa na maeneo makubwa sana ambayo walitegemea kuwa katika mgawanyo huu mpya basi na eneo la Kilwa lingejumuishwa. Ikumbukwe kuwa pamoja na vigezo vinavyotumika sasa kwa maana ya idadi ya watu, tuangalie pia nini kinapelekea idadi hiyo kuwa kubwa katika maeneo mengine na mengine kuwa na idadi ndogo kama Kilwa? Huduma bora hakuna, ndio maana wananchi wanaamua kusogea mijini, ikumbukwe kuwa Kilwa ni mwendo wa masaa matano kwa njia ya barabara kufika Dar es Salaam. Hivyo, tuboreshe miundombinu na huduma ili wananchi wasikimbilie mijini. Lakini pia izingatie kuwa ukubwa wa eneo la Kilwa kama Wilaya ni sawa na Mkoa mzima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa utendaji wake mzuri pamoja na Hotuba yake nzuri yenye msukumo wa matumaini makubwa kwa Watanzania wote. Aidha, nimpongeze kwa

juhudi zake za kufanya ziara bila kuchoka akihimiza maendeleo pamoja na kusikiliza kero za wananchi. Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema pamoja na busara zaidi.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utendaji wao mzuri na kwa kutayarisha Hotuba nzuri. Ni matumaini yangu kwamba wataendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo yao ya majukumu. Nawapongeza sana Waheshimiwa Manaibu Waziri kwanza kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na mchango wao katika utayarishaji wa Hotuba ya Waziri Mkuu. Nawatakia Baraka za Mungu katika utendaji wao ili tuweze kupata maendeleo endelevu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza sana Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na watendaji wao wote kwa Hotuba nzuri kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015 kwa kiwango kinachoridhisha. Matokeo ya kazi hii nzuri yanaonekana kwa macho kama vile, mtandao wa barabara zinazounganisha Mikoa yote ya Tanzania. Naomba sasa tujipange vizuri kwa kuzitumia hizi barabara na madaraja yaliyojengwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, mengineyo ni kama ifuatavyo:-

- Huduma za maji zimeendelea kuboreshwa ingawaje bado tunazo changamoto kuhusu sekta hii.

- Huduma za jamii yaani Elimu na Afya zimeendelezwa kwa kiwango kikubwa. Changamoto iliyopo kwa sasa ni wahudumu pamoja na vitendea kazi. Naamini kwamba tumejipanga vizuri kuzishughulikia changamoto hizi.

- Kilimo Kwanza ni dhana yenye kudhihirisha dhamira ya Serikali kuboresha kilimo kama mhimili mkuu wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba maendeleo ya viwanda ni muhimu sana katika kujenga uchumi wenye nguvu na endelevu. Naomba suala hili mliangalie kwa makini sana hususan viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia maendeleo yaliyopatikana Kitaifa, napenda kuzungumzia matatizo yanayolikabili Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki. Kero kubwa ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni miundombinu, kuna barabara mbili za *TANROADS* ambazo hazipitiki wakati wa mvua. Naomba hizo barabara ziangaliwe vizuri

kwani zinagusa sana maendeleo na ustawi wa wananchi wa Wilaya ya Morogoro Vijijini. Barabara za vijijini ni matatizo makubwa. Vijiji vingi havina mawasiliano na Makao Makuu ya Kata na Wilaya nyakati za mvua. Vijiji hivyo ni Usungusa, Mkulasi, Seregete A na B, Lubumo, Visaraka na Tununguo na Tegetero. Naomba TAMISEMI ilitazame suala hili kwani wananchi wamekata tamaa kulima kwani hawawezi kusafirisha mazao yao kwenda sokoni.

Mheshimiwa Spika, pili ni kilimo, naomba kusema kwamba, matrekta ya *power tiller* hayatoshi kwani udongo wetu hauwezi kutifuliwa na matrekta haya madogo. Wananchi wanaomba wawezeshwe kupata mikopo ya matrekta makubwa ili waweze kuboresha kilimo kwani ardhi tunayo na nia ya kuzalisha ipo.

Mheshimiwa Spika, tatu ni maji, bado matatizo ya maji yapo na wanawake wanatembea mbali sana kutafuta maji. Wengine wanatembea zaidi ya kilomita 10-17 hususan katika maeneo ya Kata ya Mkurazi, Seregete A na B, Lubumo, Fulwe, Mhunga Mkola, Kikundi, Mkono wa Mara, Kalundwa na Matuli.

Mheshimiwa Spika, nne ni afya, bado Vijiji vingi na Kata bado hakuna Zahanati na Vituo vya Afya. Tatizo kubwa ni wahudumu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, tano ni elimu, bado kuna mapungufu ya walimu, vitendea kazi, madawati, maabara na vitabu. Naomba shule zetu za sekondari zipate Maktaba na *Hostels* ili tuweze kuboresha kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Spika, sita ni viwanda na masoko, Wilaya yangu ina viwanda viwili tu. Changamotto kubwa ni kushindwa kusindika matunda na viungo vinavyozalishwa katika Kata zetu. Kwa mfano, katika Kata za milimani kuna uzalishaji mkubwa wa matunda kama vile, ndizi, machungwa, mananasi na matunda mengine. Aidha, uzalishaji wa viungo kama mdarasini, karafuu na hiliki lakini wananchi hawavuni kwani soko ni la shida kutokana na ukosefu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, mengineyo ni ukosefu wa mtandao wa simu za mkononi hususan maeneo ya Tununguo, Mkulazi na maeneo ya Kiloka na Tegetero. Naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono Hotuba ya Waziri Mkuu na nimwombe Mungu abariki utekelezaji wake.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Kitengo cha Uwekezaji na Uwezeshaji kwenye Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji kuhusiana na mnyambulisho wa matumizi kwa Bajeti iliyopita ya mwaka 2010/2011 na maombi na maelekezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara ni mengi sana ilibidi yachambuliwe na kupangwa kwa sehemu mbili. Yapo yale yanayotutaka kupewa *priority* kutekelezwa kwanza katika Bajeti hii na mengine kutekelezwa hapo baadaye.

Kumekuwa na udhaifu wa kutofanya *monitoring and evaluation* ambayo itatoa *feedback* katika kila mradi wa uwekezaji au uwezeshaji ili kuwa na utekelezaji wa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya humwezesha mwananchi kama mfuko wa vijana, *NEDF*, mabilioni ya Kikwete havina lengo tarajiwa (*targets*) *to the targeted people* (walengwa) kitu hiki kinapelekea fedha kuishia mikononi mwa watu wachache na wasio na uhitaji huku tukiacha walengwa (maskini kutopata hizo fedha na kujikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu yanaonyesha kuwa wanapewa fedha watu wachache ila pesa nyingi kuliko lengo tarajiwa hasa hayo mabilioni ya Kikwete na Mfuko wa kuwawezesha wananchi, utaona mfano wanasema kukopesha ni Sh. 2,500,000 lakini utashangaa mikopo iliyotolewa inaonesha ni zaidi ya milioni 500 kwa mtu pamoja na kusema ni *revolving fund* lakini bado kuna tatizo la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia nyaraka hizi nimegundua kuwa kuna fedha zilitolewa na hazikutumika kwa mwaka wote wa fedha. Mfano *TIC* ilipangiwa Sh. 41,000,000 ambazo hawakuzitumia kwa mwaka 2010/2011, cha kushangaza mwaka 2011/2012, Wizara imeliomba Bunge liidhinishe Sh. 500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza mipango ya *TIC*. Sielewi sababu za ongezeko hili na ukizingatia milioni 41za mwaka jana hazikutumika na sasa wanadai Sh. 500,000,000?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi pia miradi hii iwe na desturi ya ku-*justify* matumizi na kuonesha *outcome* ya matumizi hayo. Mfano, imeelezwa kuwa kuna mwaka wa fedha uliopita *TIC* iliwakilisha Serikali katika Mikutano 120 ya Kimataifa lakini hamna maelezo ya nini Serikali ilinufaika na hiyo Mikutano au ni vipi wahusika wananufaika kwani ni dhahiri kwamba misafara ya kutembelea miradi hii huwa na watu wengi ambapo inapelekea kuwa na gharama zisizo za misingi. Hivyo, naishauri Serikali iwe ina-*justify* na idadi ya watu ipunguzwe, wawe wanakwenda wawakilishi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kufanikisha hayo yote inabidi Serikali iwe na mfumo wa *Results Oriented Budget* ambazo zitapima uwiano kati ya fedha zilizoidhinishwa na kutumiwa na matokeo au jumla iliyopatikana katika utekelezaji wa mipango husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa dimbwi la umaskini katika raia wa Tanzania inabidi kituo cha *TIC* kifanye yafuatayo:-

(a) Kuanisha maeneo ya kuwekeza katika viwanda hasa vijijini ili kuongeza ajira.

(b) Kutoa na kusambaza taarifa mpya kuhusu faida au motisha zilizopo kwa wawekezaji katika viwanda na kilimo.

(c) Kuandaa na kusaidia shughuli za kuinua uwekezaji katika kilimo na viwanda ndani na nje ya nchi ili kuongeza ajira kwa Watanzania.

(d) Kituo kiongeze juhudi za kutafuta, kukusanya, kuchanganua, kusambaza taarifa kuhusu nafasi za uwekezaji na njia za kupata mitaji ya kuwekeza na kuwashauri wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuainisha moja kati ya sababu zinazoweka kikwazo katika uwezeshaji na uwekezaji ni kutofikiria kwa makini ongezeko la watu ambapo sasa ongezeko la watu ni asilimia tatu kwa mwaka. Pia kuna kazi ndogo ya uwekezaji katika kuwawezesha wananchi kupata ajira za kuajiriwa na kujiajiri wenyewe na ili kufanikisha hili ni lazima uwezeshaji na uwekezaji, uanzie kwenye Halmashauri zenyewe kwa kuweka *District Economic Development Master Plan*.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri na naunga mkono hoja. Mbarali ipo miradi mingi iliyotengewa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza ni kauli mbiu muhimu kwa madhumuni ya kuleta changamoto ili kuboresha uchumi wa Taifa hili na hatimaye kutoa ajira kwa Watanzania walio wengi, lakini ili kuleta mafanikio ni lazima Serikali iweke mikakati maalum na pia isikwepe jukumu la kusimamia. Napendekeza ili kuleta tija Serikali iandae mashamba (*schemes*). Mashamba yanayoandaliwa yawekwe (*center*) vituo vya wataalam ambao watakaa katika vituo hivyo wakiwa na vitendea kazi mfano, matrekta na zana zake kwa ajili ya kusaidia wakulima (vijana). Katika hali hiyo walime kwa kukopeshwa, gharama zilipwe kipindi cha mavuno. Mikopo hii iwe kwa wale ambao watakuwa tayari kukopa kwa masharti yaliyowekwa. Hali hii itasaidia sana kuwapa ajira vijana na hata wataalam wa kilimo wanaohitimu Vyuo Vikuu wenye fani ya kilimo. Mbarali kuna ardhi ya kutosha kuanzisha miradi ya kilimo na kutoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, barabara ni kiungo muhimu sana kwa ajili ya kuleta maendeleo. Katika Wilaya ya Mbarali tuna matatizo ya barabara zinazokwenda vijijini na maeneo ya kilimo. Barabara ya Igawa-Ubaruku ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mchele kwenda sehemu mbalimbali za Tanzania. Kipindi kilichopita barabara hii ilileta mgogoro mkubwa kutokana na barabara hiyo kufungwa kwa muda kwa kukosa kiwango bora. Hasa ukizingatia kuwa barabara hii ni ya kiuchumi inasafirisha mchele kutoka kwenye viwanda kumi vya ukoboaji mpunga kikiwemo cha mwekezaji vilivyo Kata ya Ubaruku. Naomba barabara hii ikamilishwe kwa kiwango cha lami. *TANROAD* wameanza kuweka lami nyepesi kiasi cha kilomita saba bado kilomita kumi. Barabara ya Rujewa–Madibira kuwa kiwango cha lami ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, barabara za Uturo–Ukwavila, Rujewa–Kangaga kupitia Itipungi, Igunga–Utengule, Luhanga–Madundasi, Manienga–Ipwani, Luwango–Ibelege, Ilonga–Igalako, Mwatenga–Kilambo hizi ni barabara muhimu za kiuchumi zinazosafirisha mazao kutoka maeneo ya kilimo (mashambani). Tunaomba maeneo haya kwa vile yametengewa fedha zipewe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, huduma ya afya kwa wananchi wetu ni muhimu sana, Wilaya ya Mbarali wananchi wamejitahidi kujitolea kujenga Zahanati na Vituo vya Afya kama ifuatavyo:-

- Zahanati ya Mlungu, imekamilika lakini haijafunguliwa kwa kukosa wataalam. Kituo cha Afya cha Kata ya Mawindi kimekamilika lakini bado hakijaanza kufanya kazi kama Kituo cha Afya kwa kukosa Watumishi na gari la kubebea wagonjwa.

- Kijiji cha Igava kimejenga Zahanati bado kukamilika. Kijiji cha Kilambo, Kata ya Mwatenga imejengwa Zahanati bado haijafunguliwa kwa kukosa wataalam, Kituo cha Afya cha Utengule kilijengwa, kimekamilika japo kipo chini ya kiwango hakijafunguliwa kwa kukosa wataalam.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie wananchi hawa waweze kupata huduma hiyo muhimu. Fedha zitolewe ili tusiwakatishe tamaa wananchi.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo na kujenga misingi ya amani na utulivu katika Taifa, kwa bahati mbaya hali ni kinyume katika Kata ya Utengule. Halmashauri ya Wilaya ilitoa jumla ya Sh. 42,500,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matano. *WEO* wa Kata hii aliwaibia fedha wananchi Sh. 34,000,000, wananchi wanataka kuona fedha hizo zinarudishwa ili waweze kufanyia kazi iliyotakiwa ambayo ni ujenzi wa madarasa.

Mheshimiwa Spika, ipo kero katika kukamilisha ujenzi na kufunguliwa kwa Kituo cha Afya cha Utengule wananchi wanaomba kituo chao walichoshiriki kukijenga kifunguliwe.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbarali, wanakabiliwa na mgogoro wa mipaka kati yao na *TANAPA*, katika misingi ya utawala bora ushirikishwaji ni nyezo muhimu katika kutatua matatizo katika jamii. Awali iliamuliwa wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Ruaha, Usangu wahame likiwemo Bonde la Ihefu. Wananchi walikubali kuhama, makubaliano yalifikiwa katika kikao cha *RCC* kuwa mpaka wa Hifadhi ufuate makubaliano hayo. Ilikuwa tarehe 25/07/2006 baada ya zoezi la uhamisho, Serikali haikutimiza ahadi zake kwa wananchi, ikiwemo kujenga shule, miundombinu kwenye makazi yao mapya, na athari nyingi zilizojitokeza. Tarehe 18/02/2008 Baraza la Madiwani lilikaa kutafakari malalamiko ya wananchi waliohamishwa. Baada ya mjadala mrefu Baraza liliazimia kutoingiza Vijiji vingine kwenye Hifadhi ya Ruaha na Usangu *National Park*. Tarehe 09/06/2010 Wizara ya Maliasili na Utalii ilitoa agizo la kuhamisha vijiji vingine na eneo lao kuingizwa kwenye hifadhi, wananchi hawakushirikishwa, Madiwani hawakushirikishwa, *RCC* hakushirikishwa, ilitolewa kama agizo. Huu siyo misingi ya utawala bora. Maeneo yaliyopendekezwa kuhamishwa hayana vyanzo vya maji kama Wizara ya Maliasili inavyoripoti.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayopendekezwa yatamega eneo kubwa la kilimo na ufugaji. Wananchi waliohamishwa awamu ya kwanza wapo kwenye vijiji na vitongoji ambavyo vimeingizwa kwenye awamu ya pili, hivyo watahamishwa mara ya pili. Wananchi wa Wilaya ya Mbarali wanaomba zoezi hilo lisitishwe ili waendelee kushirikiana na Serikali yao katika kulinda hifadhi yetu mpya ya *Ruaha Usanga National Park*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbarali imekumbwa na misukosuko mingi katika mazoezi mengi ya Kitaifa, lilikuwepo zoezi la kuhamisha mifugo na zoezi la uhamisho wa vijiji awamu ya kwanza. Mazoezi yote haya yaliathiri sana wakazi wa Wilaya ya Mbarali. Tunaomba Serikali sasa iwaache wananchi watulie ili wafanye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kama mwakilishi wa wananchi napata ugumu sana kuwaongoza wananchi waliojaa hofu wakililia Serikali yao. Japo yapo makundi Wilayani Mbarali yanayofurahia hali ya kutokuwa na utulivu kwa maslahi binafsi, kutokana na harakati za uchaguzi, hivyo, wangependa kuona mambo hayaendi vizuri Mbarali.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi waliokuwa *NAFCO* Mbarali hawakulipwa mafao yao stahili. Hivyo, waliomba bila mafanikio. Walipeleka kesi Mahakamani kudai mafao yao. Uamuzi wa Mahakama uliwapa ushindi na kuagiza walipwe. Wamenituma niulize ni lini Serikali itawalipa malipo yao? Ahsante.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nichangie katika masuala yanayohusu Muungano. Muungano wetu umetimiza miaka 47 yenye maendeleo katika maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, lakini ipo haja Serikali kuwaelimisha vijana na watoto wetu umuhimu wa Muungano wetu ili uzidi kuimarika na udugu wetu wa damu uendelee kudumu kwa maslahi ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto (kero) zilizopo ni za muda mrefu, sasa ni muda muafaka kuzipatia ufumbuzi kero hizo ili wananchi waache kusumbuliwa ndani ya nchi yao hasa Bandarini Dar es Salaam kupitisha bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya uvuvi, Serikali iangalie sekta ya uvuvi kwa umuhimu mpana kwa sasa na kwa baadaye. Nchi yetu ina utajiri mkubwa sana hasa kwa mazao ya Baharini, hayahitaji mbolea wala utaalam. Wananchi wote wanaokaa ukanda wa Pwani wana utaalam wa Bahari na kuvua, mkakati umewekwa kwa kupatiwa vifaa vya kisasa ilikuweza kuvua maji ya kina kirefu bila ya kuathiri mazalia ya samaki na mazingira kwa ujumla. Pia viwepo Viwanda vya Kusindika Samaki na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Afya ni muhimu na kinga ni bora kuliko tiba. Nchi yetu kupitia Wizara ya Afya ina mpango gani wa kuelimisha jamii juu ya mabadiliko ya tabia nchi, milipuko ya maradhi ya Kansa, Kisukari, Presha, UKIMWI na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia mabilioni ya JK. Tunaipongeza Serikali kwa Mheshimiwa Rais kuanzisha Mfuko huu wa kuwapa nguvu wajasiriamali na *SACCOS*. Kuongeza mitaji yao kwa kukopa, lakini zoezi hili kwa mara ya kwanza usumbufu ulikuwa mkubwa, hivyo ni vyema kwa awamu hii tuhakikishe tunawafikia wale hasa wanaohusika, zisichukuliwe na wafanyabiashara wakubwa.

Mheshimiwa Spika, migomo na maandamano kwa Vyuo Vikuu. Uhuru usio na mipaka ni fujo na kila mtu uhuru alionao isiwe kero na bughudha kwa uhuru wa mwenziwe. Hivyo, Serikali ni lazima kuzuia au kupiga vita hali hiyo kwani mbali ya wanavyuo hao kutoshughulikia masomo pia huwalazimisha na wale wasiotaka kugoma na wakati mwingine hata kupigwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuchangia kwa maandishi Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza suala la Muungano wa Tanzania ni kitu kizuri sana kwani unaimarisha umoja wetu na kutuweka kama ndugu ili hali sote ni raia wa nchi moja. Muungano ni kama mwamvuli wa usalama wa nchi yetu na pia unatujengea heshima kubwa ndani na nje ya nchi yetu. Hivyo, ni kitu kizuri sana na ni vema uimarishwe. Uimarishaji wa Muungano wetu ni kuondoa kero na malalamiko yote ambayo inawezekana kabisa.

Mheshimiwa Spika, kero zenyewe ni kuweka usawa wa uwiano kwenye ajira zinazohusu Muungano mfano, Jeshi la Wananchi, Polisi, Uhamiaji na vyombo vihusianavyo na fedha. Aidha, nafasi za Mabalozi na Maafisa wake pia fursa za masomo ya nje. Mambo yote yanayolalamikiwa wala si makubwa na inawezekana kabisa kuyarekebisha na kuondoa lawama zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufisadi wa madawa ya kulevya. Madawa haya yamekuwa ni janga kwa Taifa letu kwa kupoteza nguvu kazi ya vijana wetu. Serikali imekuwa ikikemea sana madawa ya kulevya lakini bado hali inatisha. Hivyo, naishauri Serikali izidishe maradufu juu ya kuimarisha ulinzi katika sehemu nyeti za nchi kama Bandarini, Viwanja vya Ndege na mipakani.Naamini ikiwa ulinzi utaimarishwa ipasavyo janga hili litapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, ni suala zima la ufisadi juu ya rushwa. Rushwa imekuwa ikipewa majina tofauti ili kupotosha uhalisia wake huitwa chai, takrima, kitu kidogo na majina mbalimbali ili mradi watu waendelee kufanya ufisadi wao. Wananchi waelimishwe juu ya ubaya wa rushwa kuwa ni adui wa haki na watu wasikubali kununua haki zao.

Mheshimiwa Spika, uondoaji wa rushwa ni jambo moja gumu sana kwani ni jambo lenye maslahi miongoni mwa watoaji na wapokeaji, mwisho wa siku wananchi

walipa kodi ndio wanaolipa rushwa hii kupitia bidhaa wanazozitumia kwani mfanyabiashara akishatoleshwa rushwa hauzi bidhaa hizo mpaka ile rushwa aipigie mahesabu na kuiweka katika bidhaa ambazo wananchi ndio wanunuzi wa bidhaa hizo. Hivyo, hapa mtoaji na mpokeaji hawaathiriki na chochote ila ni kujipatia faida kwa jasho la wanachi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kupunguza urasimu mkubwa juu ya utekelezaji wa majukumu. Jambo moja kulipitisha kwa watendaji wengi ndio liishe, humu ndio mnamozaliwa rushwa.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la ajira za Jeshi na Polisi. Pamekuwa na malalamiko ya siku nyingi kutoka upande wa pili wa Muungano (Zanzibar) kwamba wanataka kujua mgao halisi wa nafasi hizi kwani msimu wa uajiri wa Idara hizi ni Wazanzibari wachache wanaopata nafasi hizi. Naishauri Serikali kwamba, nafasi zile ziwe kwa ajili ya Wazanzibari tu na zisigawiwe kwa vijana wa upande mwingine wa Muungano kwa mazingira ya kutatanisha.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni za Urais, Ubunge, Udiwani, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kilomita mbili za lami katika Mji wetu wa Babati Mjini, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Spika, Babati Mjini ilitoka katika Wilaya ya Babati ya zamani. Hospital ya mji, baada ya mgao haikupata chochote, hatuna gari la wagonjwa, hatuna gari la Daktari (*Town Medical Officer*) na hatuna gari la matumizi ya kawaida ya Hospitali.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Mji (*Town Director*) hana gari kabisa. Utendaji kazi unakuwa mgumu sana. Lini tutapewa magari kusaidia utekelezaji wa kazi ndani ya Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Babati Mjini, sehemu ya mipaka yake iko ndani ya maeneo ya mgogoro wa Kiru. Kitongoji kilichopo hapo, ni sehemu ya kijiji kilichoanzishwa na Serikali. Mwenyekiti wa Kijiji cha Imbichi yuko ndani kwa ghasia hizo, naye hahusiki. Lini Serikali itatatua na kumaliza mgomo huo?

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa Bajeti nzuri inayozingatia hali ya Watanzania. Pamoja na pongezi hizi, nina hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi umepangiwa fedha kidogo sana (Bilioni 22) ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya maendeleo yanayohitajika katika mkoa huo. Mkoa ni mkubwa sana na fedha hizi ni ndogo mno. Bajeti ijayo, Serikali iongeze fedha kwa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, mkoa umeleta pendekezo la kuanzisha Mkoa mwingine wa Nachingwea, utakaojumuisha Wilaya za Nachingwea, Tunduru na Nanyumbu. Jambo hili bado halijatolewa uamuzi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nachingwea ni kubwa sana *Square kilometer* 7,777, lina Kata 32 na Vijiji 126 na vitongoji 569. Nilikwishapendekeza kwako kuwa jimbo hili ligawanywe (yawe Majimbo mawili) lakini hoja hii bado haijapatiwa ufumbuzi na sababu imekuwa Wilaya haina watu wa kutosha. Yaani 196,000 ni watu wachache? Mbona Unguja na Pemba ina Wabunge ambao wana watu chini ya 10,000? Nao ni Wabunge sawa na wengine wote! Naomba Jimbo hili ligawanywe ili maendeleo yafike haraka.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini ni ahadi iliyotolewa na Mawaziri kadhaa wa Nishati, lakini mpaka sasa, hatujapata mradi wowote wa umeme vijijini. Naomba katika mwaka ujao wa fedha, tupatiwe umeme japo katika vijiji vichache.

Mheshimiwa Spika, Nachingwea kuna uhaba mkubwa wa Walimu hasa wa sekondari. Tunaomba tupewe mgawo mahsusi wa walimu hawa hasa wa Sayansi ili tuweze kufungua na sekondari zetu 12 ambazo zipo tayari, lakini tunashindwa kuzifungua.

Mheshimiwa Spika, Maji vijijini ni tatizo kubwa sana Nachingwea. Nashukuru kuwa mradi mkubwa wa maji ya Mbwinji unatekelezwa sasa. Lakini mradi huu ni wa kupeleka maji Nachingwea Mjini tu. Nashauri Ofisi yako au Wizara ya Maji ione jinsi ya kupata fedha ili tujenge Mabwawa Vijijini. Visima siyo *ideal* tu, ila Mabwawa ndiyo hasa yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na nakutakia utekelezaji mzuri wa Bajeti hii.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka 2011/2012. Katika hotuba yake amezingatia vipaumbele ambavyo vimewekwa ili kuinua uchumi wa Tanzania. Ili Tanzania iendelee kiuchumi, lazima ijikite kikamilifu katika maeneo ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, umeme ni muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi na maisha ya kawaida ya binadamu. Katika Jimbo la Mufindi Kusini, kuna tatizo kubwa la umeme katika Vijiji vya Mbalamaziwa, Malangali, Ihowanza, Ikangawami, Nyigo, Ipilimo, Nyololo, Kituo cha Afya na Kituo cha Watoto Yatima, Maduma, Kihanga, Mkalala, Ikwega, Ihomasa, Kilolo, Lwang'a Kitasangwa, Lugorofu, Rugema na Makunga.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuimarisha barabara katika Wilaya zetu katika Wilaya ya Mufindi. Jimbo la Mufindi Kusini kuna barabara ambayo inatoka Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango – Kiwanda cha Mgololo. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Imepita kwenye viwanda vikubwa kama vile Kiwanda cha Chai *(Uniliver Company Ltd)* na imeishia Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo. Pia wakulima binafsi wa chai na mazao mengine ya chakula wanakaa maeneo ambayo barabara hii imepita. Naiomba Serikali ijenge barabara hii kwa kiwango cha

lami kwa sababu magari yanayopita katika barabara hii ni makubwa, hivyo sasa hivi yanakwama kutokana na barabara kuwa mbovu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikarabati matenki ya maji ambayo yalijengwa kwa michango ya wananchi ambayo yapo kijiji cha Sawala, Kibao, Igowole, Nyololo na Nyigo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mufindi Kusini ni kubwa lenye Kata 15, Vijiji 77 na viwanda vitano, lakini halina Benki yoyote ile . Wananchi wanasafiri umbali wa kilometa zaidi ya 94, yaani kutoka Kiwanda cha Karatasi hadi Mafinga mjini. Hii ni hali ya hatari sana kwa wananchi wetu. Naiomba Serikali kupeleka huduma ya benki katika Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, daima tukumbuke maneno ya mwanazuoni maarufu Pilato, kwamba: "Binadamu kama hujagundua jambo lolote, uko tayari kufa kwa jambo hilo, hufai kuishi. Je, ni jambo gani uko tayari kulipigania hata ikilazimu kupoteza maisha yako? Je, uko tayari kulipigania hata ikilazimu kupoteza maisha yako? Je, uko tayari kujitolea kutaabika kwa ajili ya kizazi kijacho? Ukifanya mambo yaliyo na manufaa kwa jamii ya sasa na ya baadaye, hao ndio wanaoweza kuleta mabadiliko kwenye jamii au Taifa."

Mheshimiwa Spika, hivyo, tujenge mazingira ya wananchi kuelimishwa na kushirikishwa kikamilifu kwenye miradi ya maendeleo. Kuna ushirikishwaji mdogo wa uelewa finyu wa wananchi katika kuibua, kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu miradi ya maendeleo. Mradi wa kuchangiwa na mifuko mingi hiyo ndiyo inayosababisha ubadhirifu wa fedha. Kwa mfano, mradi wa maji Gehandu, Ming'enyi, Mirongori huchangiwa na mifuko ya *TASAF, Rural Water Supply Grant, Quick Win* na Ruzuku ya Maendeleo *(CDG).*

Mheshimiwa Spika, kazi iliyotakiwa kutekelezwa mwaka 2007/2008 ni ujenzi wa vioski vitano vya kuchotea maji na kuunganisha maji kwenye vioski vitano katika Kijiji cha Gehandu na Ming'enyi; na ujenzi wa viosk viwili vya kuchotea maji na kuunganisha maji kwenye vioski viwili katika Kijiji cha Mirongori.

| | | |
|---|---|---|
| Gehandu + Mingenyi | - TASAF | - 36,000,000 |
| | - Quick Win | - 57,490,000 |
| | - Mirongori | - 27,000,000 |
| | - CDG | - 30,000,000 |

Mheshimiwa Spika, matokeo yake, baada ya ujenzi huo, leo hii wananchi hawana maji kwa madai kuwa mabomba yameoza na kutitia chini ya ardhi. Ndio maana ninasema

kunahitajika sana kuwe na utaratibu wa kufuatilia miradi ya maendeleo *(value for money).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Madiwani ndio wasimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma, lakini kuna matatizo makubwa kwa Halmashauri nyingi kutumia fursa ya kutokuelewa Madiwani majukumu yao ndio wanatumia fedha hizo vibaya. Pia Wakurugenzi wengi kuwa miungu watu kwa kutoa maagizo bila kutembelea miradi katika Wilaya zima bali kupokea ripoti tu wanayopeleka watendaji bila ufuatiliaji. Mifuko ya barabara hutumika vibaya kwa kuwa Wizara haitembelei barabara zinazotengenezwa katika Halmashauri. Mfano, barabara za:-

(1) Basotu – Getanuwas kutengenezwa bila kuwekwa moram – Sh. 240,000,000.

(2) Gawal – Gawidu – kutengeneza bila *moram* na *culvate* zote hazina ubora Sh. 70,000,000/= + Sh. 84,000,000.

(3) Barabara za Mjini: Katesh – *Culvate* kutengenezwa kwa kuweka *wire mesh* badala ya nondo – Sh. 42,000,000 + Sh. 104,000,000.

(4) Endasak – Giting – Gawal – kutumia fedha nyingi barabara haina ubora kabisa na *culvate* na madaraja ni mabovu, kutolipwa vibarua – Sh. 35,700,000/= + Sh. 257,000,000 + Sh. 20,000,000.

(5) Basotn – Basodesh – kutengeneza daraja mpaka leo halikutengenezwa Sh. 29,000,000.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi hazina ubora pamoja na nyingine zinazosimamiwa na Halmashauri ya Hanang. Fedha zimeshatumia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ubadhirifu ni mkubwa, ni vyema sasa Serikali itafute utaratibu mwingine wa kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma kwa elimu inayotolewa kwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji wa Serikali yao, Watendaji kujua wajibu wao na kuwajibisha Watendaji wasiotekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, naomba marekebisho yafanyike katka kitabu cha Orodha ya majedwali yanayoambatana na hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 32. Mkoa wa Kagera – Halmashauri zote. Idadi ya waliofanya mitihadi na idadi ya waliofaulu, asilimia zilizotolewa siyo sahihi ukilinganisha na idadi yenyewe. Naomba marekebisho yafanyike.

| | **Walioanya mtihani** | **Waliofaulu** | (Jumla) |
|---|---|---|---|
| Biharamulo | 2878 | 2086 | – 140% |
| Bukoba (M) | 2502 | 1800 | – 140% |
| Bukoba (V) | 7529 | 3791 | – 98% |
| Chato | 6404 | 3939 | – 125% |
| Karagwe | 10430 | 5729 | – 100 |

Mheshimiwa Spika, hadi Ngara zote zisahihishwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata wasaa huu ambao ni adimu sana kupatikana. Nilikuwa kwenye orodha ya kuchangia kwa njia ya hotuba, lakini kwa bahati mbaya muda haukutosha na ukatushauri tuchangie kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mchango wangu katika nyanja za elimu, ulinzi na usalama, pamoja na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda niwapongeze vijana 20 waliofanya vizuri sana katika mitihani yao ya Kidato cha Sita iliyofanyika Februari, 2011. Aidha, nawapongeza wazazi wao pamoja na walimu wao licha ya mazingira magumu ya kazi wanayoifanya, lakini wamedhihirisha kuwa ni wavumilivu na wametoa matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, nilianza na suala la elimu ambalo hakuna ubishi wowote kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha na kutokuwa na elimu ni sawa na mali bila daftari. Nitazungumzia zaidi juu ya watoa elimu ambao ni walimu.

Mheshimiwa Spika, waraka wa Utumishi Na.C/AC.44/01/A/84 wa tarehe 1 Desemba, 2009 ni waraka ambao walimu wameuona na kuuita waraka kandamizi kwa sababu zifuatazo: kwanza, Mwalimu mwenye Diploma ya Ualimu aliye kazini, akiamua kwenda kusoma kwa maana ya *up-grading* katika taaluma yake hiyo ya ualimu, yaani atunukiwe shahada, basi Mwalimu huyo amalizapo masomo yake hutakiwa kuanzia na ngazi ya Mshahara ya *TGTS D* bila kujali umri ambao amelitumikia Taifa hili hata kama kabla hajakwenda masomoni alikuwa katika ngazi ya juu, mfano *TGTS E or F*. Mwalimu huyo hushushwa daraja na kuanzia ngazi ya *TGTS D* kwa maelezo kwamba kila mwenye Shahada ya Ualimu ni lazima aanzie na *TGTS D*.

Mheshimiwa Spika, huu ni uonevu wa kada hii na ni kuwavunja moyo walimu wasiweze kujiendeleza kielimu. Ninaishauri Serikali iangalie upya waraka huu urekebishwe ili walimu hawa waweze kutendewa haki na wathaminiwe kwani watu hawa wanategemeana sana katika maelezo ya watoto wetu ambao ndio Taifa la leo na kesho.

Mheshimiwa Spika, walimu hawa wanawajibika katika Wizara tatu, yaani Wizara ya Elimu, TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hali hii imefanya kuwa na mkanganyiko mkubwa, kwani wengi wao hawafahamu ni wapi hasa pa kufuatilia haki zao na wawajibike kwa nani hasa. Pia kumbukumbu zao nyingi zimepotea kiasi cha kupelekea wengi wao kukosa mafao yao ambayo ni stahili. Swali: Je, walimu hawa wako chini ya Wizara gani hasa?

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama wa raia na mali zao ni vitu muhimu sana kwa ustawi wa jamii yoyote ile. Hivi karibuni kumezuka wimbi la utekaji mabasi ya

abiria hususan katika Mkoa wa Kigoma. Tunaitaka Serikali ichukue hatua madhubuti na kudumu kwa Mkoa huu, kwa kuwa sasa abiria wanakuwa na wasiwasi mkubwa wawapo safarini. Pia kuna uwezekano mkubwa na tetesi pia zipo kwamba wengi wa majambazi hawa wanatokea nchi jirani za Burundi, Rwanda na *DRC*. Tunaitaka Serikali ifanye uchunguzi wa kina na ikithibitika kuwa majambazi hao wanatokea nchi hizo, basi hatua za kisheria zichukuliwe na hasa ikizingatiwa kuwa ni nchi ambazo ziko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na ikibidi hata hifadhi wasipewe katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ndiyo kioo cha uongozi wowote wa nchi. Kumekuwepo na ukiukwaji wa maamuzi au maagizo yanayotolewa na viongozi wa juu ambao utekelezaji wa maagizo ya viongozi hao hufanywa na Watendaji. Watendaji wamedhoofisha sana juhudi za Serikali za kuhudumia wananchi. Hali hii imefanya wananchi wengi kukosa imani na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka mamlaka husika kutowavumilia Watendaji wote wazembe wafukuzwe kazi na sio kuhamishwa, kwani nako watakwenda kuharibu. Aidha, Madiwani ni watu muhimu sana, ni kiungo kikubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo. Tunaitaka Serikali iangalie upya namna ya malipo yao ili Madiwani hawa waweze kupatiwa mishahara mizuri.

Mheshimiwa Spika. Nakushukuru sana.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana sasa hivi katika suala zima la nyumba zilizowekwa X na *Tanroads* wamekuwa hawajui hatima ya zoezi hili kwamba watabomolewa nyumba zao au watalipwa mafao ili waweze kujenga nyumba nyingine. Mimi nashauri kwamba Serikali itoe tamko kuhusu suala hili, lakini ifikirie sana namna ambavyo wenye nyumba hizi kwamba kama Serikali ina nia ya kubomoa nyumba hizi, basi iwalipe haraka au isitishe zoezi hili na kuacha kuendelea na zoezi la ujenzi kwani Serikali isifanye zoezi la kubomoa nyumba hizi pale ambapo kuna mradi tayari kuliko kubomoa nyumba zote bila kuwa na mradi.

Vile vile ni muhimu Serikali ikatambua barabara zote za Halmashauri kwa kilometa na kwa majina ili kuweza kukidhi masharti ya kupata fedha za kutosha kukarabati na kutengeneza barabara mpya pamoja na barabara za vijijini kitu ambacho kitarahisisha usafiri wa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na mpango wa kutenga fedha za kutoka kwenye kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Shinyanga ili tuweze kuondokana na matatizo ya njaa pale ambapo msimu wa mvua unakuwa siyo mzuri.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naanza na suala la vijana na ajira.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inazalisha vijana makundi mawili kwa kila mwaka ambayo hayana kazi (i) vijana 700,000 ambao wanaingia katika soko la ajira (ii) Vijana zaidi ya 700,000 ambao wanashindwa kuendelea na masomo yao ya Darasa la Saba na

wale wanaomaliza Darasa la Kumi, kundi lingine kubwa ambalo liko mitaani ni la wale ambao hawaendi shule, aidha hawasomi kabisa.

Mheshimiwa Spika, makundi yote hayo ni mzigo wetu (Serikali) na tuna wajibu wa kuwajibika juu ya makundi yote hayo.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa ambao ndio nguvu kazi ya Taifa, wanaishi maisha ya kubahatisha kiasi kwamba wanaonekana kama wamekata tamaa. Sisi Wabunge wa Bunge hili tunapambana na hoja za vijana hawa kila wakati juu ya mustakabali wao wa maisha yao ndani ya Taifa lao chini ya Serikali yao. Tuna kazi kubwa ya kujibu maswali na hoja za vijana hawa katika maeneo yote ambayo Wabunge tupo.

Mheshimiwa Spika, jambo linalosikitisha sana ni kwamba *ILO* ni Shirika la Kazi Duniani linalosaidia maendeleo ya vijana katika nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania. Lakini kana kwamba baadhi ya Watendaji wa Serikali hii hawaelewi kwamba Tanzania tuna tatizo hili la vijana wasio na kazi na kwamba fedha hizi zinakataliwa, inafanywa ni siri ya wachache ambao fedha hizi zinawafikia katika Wilaya, jambo linalopelekea fedha hizo mwisho wa siku kurejeshwa zilikotoka kwa kisingizio cha kukosekana kwa vijana wa kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni aibu kwa Tanzania na pia kwa utaratibu huu ni kuwafanyia ukatili vijana wetu na jambo linaloashiria kutojali kabisa vijana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zitakapoingia kwa mwaka huu wa fedha, naishauri Serikali kwamba Wabunge waarifiwe kwa lengo la wao kuweza kuwashajiisha vijana ili wajitokeze na waweze kufaidika na mfuko huu wenye lengo la kuwasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Taifa cha Utangazaji *TBC* chenye makao yake Mikocheni, pia kinalazimika kutumia fedha nyingi za wavuja jasho kwa kulipia kodi (pango) za majengo ambayo wamekodi kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Kama ingetumika busara ya kumalizia jengo la *TBC* lililopo Mikocheni, tungeweza kuokoa fedha nyingi za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, jengo hili lililowekewa jiwe la msingi na Rais wa wakati ule, Mheshimiwa Mzee Ali Hassan Mwinyi tangu tarehe 13 Aprili 1995. Inasikitisha kwamba hadi leo liko vilevile, katika sura ileile ya gofu. Ukweli ni jengo zuri na madhubuti sana na kama tutalimalizia, siyo tu kwamba tutaokoa fedha nyingi za umma, lakini pia tutaweza kuiongezea Serikali yetu majengo ambayo yatakuwa yanamilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii ndio athari ya kutokuwa na sera ya kitaifa ndani ya nchi yetu na inaonekana wazi kwamba kila Serikali inayokuja, inakuja na taratibu zake na hakuna mpango wa kuyaendeleza yale mazuri yaliyoanzishwa na Serikali iliyopita. Kwa mtindo huu ambao bado upo na unaendelezwa na Serikali iliyopo hivyo ndivyo ambavyo inatia shaka kwamba kama Serikali ijayo itaongozwa tena na Chama cha Mapinduzi

(CCM), hata ule mpango uitwao wa Taifa wa miaka mitano uliozinduliwa na Rais, basi unaweza usiendelezwe.

Mheshimiwa Spika, tangu alipomaliza muda wake wa Urais, Mzee Mwinyi, Marais waliofuata hakuna ambaye ameona haja ya kulimalizia jengo lile. Naiomba Serikali inayomalizia muda wake walimalizie jengo hili la umma na iwe ni mpango wa Serikali kufuatia bajeti itakayoanzia 1 Julai, 2011 ili *TBC* waweze kuhamishia ofisi zao ndogo kutoka ziliko hivi sasa na ziweze kuhamishiwa pale Mikocheni na kwamba pia itaokoa gharama za kuwasafirisha wafanyakazi pamoja na vifaa vyao kutoka Mikocheni hadi maeneo yaliyoko nje ya hapo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNAMERYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwa maandishi katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie katika mafungu machache, nianze na Kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo. Katika nchi yetu tumejaaliwa sana udongo wenye rutuba unaokubali mimea mingi. Nikiongelea Wilaya ya Mpanda, ina mbuga nyingi kama Kakese, Mnyagala na Mafunsi.

Mheshimiwa Spika, mbuga hizi huzalisha mpunga kwa wingi, lakini upatikanaji wa maji huwa ni shida hasa mvua zinapokuwa hazitoshi. Lakini mbuga hizi zimezungukwa na mto Katuma ambao huwa haukauki. Naishauri Serikali iwajengee wakulima hawa mifereji ya kupitisha maji katika mbuga hizi ili kufanikisha mavuno mengi kwa wakulima hawa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, utoaji wa ruzuku za mbolea na mbegu bora haziwafikii walengwa, wakulima wengi wanalalamika na hili.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye reli bado ni utata mtupu. Reli ndiyo njia iliyo rahisi kwa wananchi wenye kipato cha chini kwa kusafiri, pia usafirishaji mizigo, lakini usafiri huo hauridhishi kutokana na miundombinu mibovu kwa maana ya reli yenyewe watu wanasafiri kwa hofu kubwa kwani reli ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, mabehewa yaliyopo ni mabovu na chakavu, yaliyochoka na yamejaa kunguni na panya. Kwa hali hiyo, naiomba Serikali irudishe huduma iliyokuwepo zamani yenye heshima ikiwa ni pamoja na kurudisha mabehewa ya Daraja la Kwanza na daraja la pili ambayo kwa sasa hayapo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapotoa fedha kujenga barabara au daraja, inategemea wananchi wafaidike na matunda ya Serikali yao katika kuwakwamua katika huduma bora. Daraja la Nzaga lililopo umbali wa kilometa 26 kutoka Mpanda kwenda Urwila. Barabara hii inasimamiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* lakini daraja hili limekwishaharibika vibaya huku magari yakiendelea kupita tena makubwa. Naiomba

Serikali ikalichunguze daraja hilo kisha ichukue hatua ya kulitengeneza kabla halijasababisha madhara.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali inapotoa tenda, iwapatie wakandarasi wenye ujuzi wa kazi hiyo ili kupunguza gharama za Serikali kwa kujenga madaraja yanayoharibika kwa muda mfupi kama lilivyo hilo daraja la Nzaga ambalo limejengwa kuanzia tarehe 28 Desemba, 2006 na sasa tayari limebomoka na kutitia huku magari yakipita.

Mheshimiwa Spika, huduma ya maji safi na salama bado ni tatizo katika Wilaya ya Mpanda mjini na hata vijijini. Kata ya Nsemulwa sehemu ya mabehewani wananchi wana kilio cha maji safi na salama, Kata ya Mpanda Hoteli – Tambukareli pia Kazima ni sehemu hakuna kabisa visima na wananchi wanahangaika sana. Vijijini ndiyo kabisa. Kuna vijiji vingine wao wameona kama ndio sehemu ya maisha yao kuhangaika na maji mfano kijiji cha Iloba, Ikaka, Nkungwi na Chamalendi Tarafa ya Usevya. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iwajali sana wananchi wa vijijini hasa katika huduma ya maji safi na salama kwa ajili ya afya zao. Pia, kuepusha usumbufu wa kufuata huduma ya maji kwa mwendo mrefu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa hakuna anayemtakia mabaya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, na kama wapo, basi washindwe kwa jina la Yesu, kwani tuna matumaini naye, tunampenda, ni mwenzetu na wote ni watoto wa baba mmoja aliye Mbinguni. Pamoja na siasa, nashauri kwamba Wabunge tunahitaji kupendana, kuheshimiana na kuthaminiana ili tuweze kujenga amani ya kweli Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, gharama za maji zimekuwa mzigo mkubwa kwa mwananchi wa kawaida. Imebainika kwamba gharama hizi zimechangiwa sana na gharama kubwa za maji ambazo zinachangiwa sana na gharama za madawa ya kutibu maji. Madawa yanayotumika kutibu maji yamewekewa kodi tofauti na dawa za kawaida. Kodi kwa dawa za maji zimekuwa zikichochea kuongezeka kwa gharama ya lita moja ya maji hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa mlaji ambaye ni mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama hizi, napendekeza kuondolewa kwa kodi kwa dawa za maji ili kushusha gharama za maji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ni miaka 47 sasa toka Muungano wetu ulipoasisiwa na viongozi wetu ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais Abeid Amani Karume, na kumbukumbu yangu, kuna mambo walikubaliana yawe ya Muungano na mengine yasiwe ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kama sitakosea, ofisi yako ndiyo inashughulikia mambo hayo na hadi leo hii bado Wazanzibar wanalalamikia utekelezaji wake ambao unakwenda kwa kusuasua sana na vikao hivyo utekelezaji wake hautoi matunda kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ambayo imeasisi ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Tanzania, Muungano wa nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar na bado kuna kasoro za Muungano hazijamaliza kutatuliwa.

heshimiwa Spika, naomba kwanza kabisa zimalize kutatuliwa kero zote ili Tanzania itapojiunga na jumuiya hiyo, basi Zanzibar iingie nayo kama nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo la huduma za jamii. Tatizo kubwa la miradi ya maendeleo vijijini na mijini ni kuwa miradi hiyo huwa haiendelei hasa mradi wa maji wa *TASAF*, mradi huu ni wa kuchimba visima, lakini hauna ushughulikiwaji wa mgao wa maji kwa wananchi ambao wanapata taabu sana ya maji na visima vipo, lakini vimefungwa na hutolewa kwa nadra tu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba miradi yote ya maendeleo inayopelekwa mijini na vijijini ni lazima kuwepo na mwangalizi ambaye atatoa taarifa endapo tu kutatokea hujuma maana kumfungia mwananchi maji ni hujuma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti Ukimwi, kama ulivyosema, hivi sasa umeanza kuona dalili za kutia moyo na wananchi wamepata mwamko, na pia wananchi kiasi wanajitolea sasa bila uwoga kwenda kupima afya zao na kama mtu ameathirika huenda kujiunga na kuanza dozi.

Mheshimiwa Spika, nilisikia kuna dawa ambayo ni chanjo ambayo ukichanjwa hupati HIV. Je, kuna watu wangapi walipata chanjo hiyo na mpaka leo hii hatukuisikia kuletwa ila kuna dawa za *ARV* ambazo humzidishia mgonjwa matumaini ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi huona vituo vya huduma ya kutoa ushauri nasaha huwa vinashughulikiwa na watumishi ambao wao hawajaathirika na huwa wanafanya ubadhilifu wa kutoa vyakula kwa waathirika ambao vyakula vile ni kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba vituo vya huduma nasaha vishughulikiwe na wanaoishi na *HIV* wenyewe kwani wapo wenye elimu na wasomi kwani wanakuwa hawawanyanyapai wenzao maana na wao pia ni waathirika. Mara nyingi Sekta hii bajeti yake ni kubwa lakini haiwafikii walengwa ila wanafaidika wazima ambapo sio lengo la kufikia "Tanzania bila ya Ukimwi inawezekana."

Mheshimiwa Spika, tukitimiza wajibu wetu, yote haya yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea kuchangia hotuba hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo inatia moyo kwa nchi yetu na wananchi pamoja.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia hoja ya Muungano. Lazima ifahamike kwamba bila Zanzibar kukubali Muungano, basi kusingekuwa na Muungano. Vivyo hivyo bila Tanganyika kusingekuwa na Muungano ambao jina ni Tanzania. Tafsiri yake ni "Tanganyika na Zanzibar". Kwahiyo, ni lazima Zanzibar ijulikane ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, ipewe heshima zote za muhimu na kupata haki zote zinazostahili za Muungano. Kero za Muungano ziondolewe haraka isiwe hadithi tu za kila siku. Mimi binafsi sina hofu hata kidogo ya Muungano wetu, lakini najua wazi kuwa unapounga lazima na fundo au dhana sasa tutumie njia ya kuondoa fundo hilo au alama iliyopo kwa kuhakikisha yakuwa tunakwenda vizuri na Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba Muungano umeshafanya mengi Zanzibar. Ni wajibu wetu kupongeza jengo la *BOT* ambalo tayari limemalizika, Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Makamu wa Rais, Hospitali ya Jeshi la Ulinzi iliyopo Bububu na mengi tu. Lazima nipongeze.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za JK, zimeletwa kwa nia safi tu, lakini limepotoshwa na baadhi ya wahusika kwa kutoa mfuko huu kinyume na ulivyokusudiwa. Hao walengwa waliokusudiwa kwa hivi sasa kama mfuko huo utakuwepo lazima usimamiwe vizuri sana ili wananchi wawe na matumaini na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, nathubutu kusema kwamba mfuko wa JK wazanzibar wengi hawakufanikiwa kuupata.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wanajeshi wote na Jeshi la Polisi kwa kuhakikisha ulinzi upo. Lakini kwa upande wa Jeshi la Polisi lazima tuwapatie vitendea kazi vinavyoendana na wakati ili kuzidi kukabiliana na majambazi wavunja sheria na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu kutofaulu vizuri vijana wa kidato cha nne. Katika juhudi za Serikali kupunguza viashiria vya kuteremka kiwango cha elimu, ni pamoja na kujenga maabara.

Serikali ilikopa *World Bank* na kujenga maabara zaidi ya 400 lakini ni 108 tu ndiyo zilizopatiwa vifaa. Kwanini Serikali ikakopa fedha za ujenzi, bila kukopa kwa ajili ya vifaa? Serikali haioni kwamba itarudia makosa yale yale ya kujenga Shule za Kata bila waalimu, maabara, vitabu na madawati? Hali hii inadhihirisha isivyojipanga na kukosa mipangilio ya kukamilisha mahitaji yake?

Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya shule nyingi siyo ya kuridhisha. Yameanza kubomoka au kupasuka. Je, Serikali pamoja na tathmini ya kufeli watoto wengi, ina mpango gani wa kutathmini umadhubuti wa majengo hayo ya shule za Kata ili Serikali iweze kuchukua hatua za dharura kabla hayajaanguka hasa kwa vile hata fedha za matengenezo hazipo? Waziri Mkuu atayatolea kauli mambo haya mawili ya elimu katika kuhitimisha hoja yake?

Mheshimiwa Spika, suala la misamaha ya kodi ambayo imefikia wastani wa shilingi bilioni 900 sawa na wastani wa 2.5% ya *GDP* ambapo nchi jirani ni wastani wa 1% ya *GDP*. Tatizo la msingi ambalo Serikali haijalifanyia kazi ni kipimo cha kila dira ya msamaha. Juzi tulipitisha *Finance Bill – 2011/2012* na kusamehe kodi kwa kipindi cha miaka 10, kwa kuwa uwekezaji unatofautiana kwa ukubwa wa mradi, ukubwa wa mkopo na muda wa kulipa mkopo. Hivi ndiyo vingekuwa vigezo vya kutoa msamaha, lakini kwa wawekezaji wote wanapewa muda wa kusamehewa sana hata kama mwekezaji mmoja amewekeza *USD 250* na yule aliyeweka *USD* milioni moja au zaidi ya hapo. Nashauri Serikali katika utaratibu wa kupitia upya misamaha ya kodi ifanye uchambuzi pamoja na vigezo vingine, waangalie pia hayo niliyoeleza hapo juu. Aidha, naomba pia yaangaliwe makampuni ambayo yamemaliza muda wa miaka mitano ya *tax holiday* na hatimaye kuwekeza upya kwa njia ya kukarabati uchakavu wa mradi ulioanza.

Mheshimiwa Spika, suala la utoaji wa maamuzi na usimamizi wa utekelezaji wake limekuwa ni tatizo kubwa la kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali. Nashauri iundwe Kamati ya Bunge ya Kusimamia Ahadi za Serikali na kwa upande wa Serikali, lazima kuwe na *check list* ya anayetaka huduma fulani katika Serikali aelewe na muda wa kupatiwa huduma hiyo, ikieleza pia anayehusika na kutoa huduma hiyo ili pale mtaka huduma anapokwamishwa na urasimu, mhusika aweze kuchukuliwa hatua na itangazwe ili wengine wasirudie.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ijipange kwa kuwawezesha Watanzania. Ahadi nyingi na mipango mingi imepangwa, lakini bila kujenga kada ya kati ya wazawa, kwa mazingira ya ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Watanzania hawatapata fursa ya kuwa wamiliki wa raslimali zao. Kwa mfano, hivi sasa ni makampuni yasiyozidi 10 ya Watanzania yamewekeza katika nchi wanachama wakati makampuni yasiyopungua 250 ya Kenya yamewekeza Tanzania. Kampuni hizi siyo tu zinaleta wafanyakazi kutoka nchi zao kama *White Sand*, kati ya wafanyakazi 19 ni lazima wawili tu ndiyo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Serikali ipite vyuoni, waulize wanafunzi kwa njia ya kushirikiana, ni mradi gani wanataka kufanya baada ya masomo yao? Vijana hao katika kipindi cha masomo kwa vitendo ili wajijengee uwezo wa kuendesha mradi ambao wana nia ya kuutekeleza, Serikali iwapatie mtaji, vifaa na

nyenzo zote za kuwawezesha kutekeleza miradi yao. Kwa njia hii, tutajenga msingi mzuri wa kada ya kati ya Watanzania kumiliki na kuendesha raslimali zao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ikae na *LPF* ili kupata utaratibu wa kuwapatia mshahara au posho Madiwani na Viongozi wa Vitongoji, mpango ambao utawawezesha kulipwa kiinua mgongo baada ya muda wao wa uongozi bila Serikali kubeba mzigo mkubwa baada ya kumaliza miaka mitano ya uongozi wao. Kama Madiwani wakilipwa Sh.160,000/= na Viongozi wa Vitongoji Sh. 60,000/= baada ya uongozi wao, Madiwani watapata siyo chini ya shilingi milioni tano na Viongozi wa Vitongoji siyo chini ya shilingi milioni 1.5. Utaratibu huu pia unaweza kutumika kwa Wabunge ili Serikali isibebe mzigo wa kulipa mwisho wa uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, sekta hizi ni chachu ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira. Eneo la uvuvi lina samaki wasiopungua Mt.700,000 na mifugo isiyopungua milioni 13. Hivi sasa Vyuo vya Uvuvi na *VETA* vinafundisha Uvuvi na Ufugaji. Nashauri Serikali iende *Maladives* ikaombe wataalamu wa kuvua samaki kwa kutumia *Pole and Line* (Mishipi ya *Pole*) ambao sio tu wanapatikana samaki kwa wingi, bali pia uhifadhi wa mazingira na kulinda mazalia ya samaki ni mkubwa mno. Aidha, tukajifunze namna wanavyowawezesha wavuvi nao na sekta hiyo wageni hawapewi nafasi ya kuvua katika bahari yao.

Mheshimiwa Spika, nashauri tutunge sheria kuwa meli yoyote ya kigeni ambayo haina leseni, itaifishwe kama wanavyofanya wenzetu Afrika Kusini kwamba uvuvi ni kwa wazawa tu sisi tunashindwa nini?

Mheshimiwa Spika, mifugo ingeweza kutoa mchango mkubwa katika uchumi. Hivi sasa Watanzania wachache wanasafirisha nyama, mbuzi na kondoo katika nchi za Mashariki ya Kati *(Middle East)* mahitaji ni makubwa. Nashauri utaalamu unaotolewa *VETA* Dodoma, usambazwe katika VETA za Mikoa yenye mifugo mingi na wanafunzi wakimaliza hapo wafunguliwe mradi wao ili waweze kujiajiri. Hivi sasa wanapata ujuzi, lakini hawawezi kutumia ujuzi wao, kwani hakuna machinjio ya kuwatosha wao kupata ajira na hawapewi mtaji na vifaa vya kuanzisha mradi wao. Hili likisimamiwa na kwa kutumia Watanzania waliokwishaanza biashara, hii mifugo itachangia kwa kiwango cha juu katika pato la Taifa na kutoa ajira ya uhakika. Aidha, wafugaji watakuwa na uhakika wa soko la bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, madhara ya tabia nchi na wanafunzi wa mazingira, yamechangia sana upungufu wa maji na kupungukiwa uzalishaji. Nashauri Serikali itafute teknolojia ya kuvuna maji mengi yaliyoko hewani kama wanavyofanya Israeli ambao wamevumbua mashine inaitwa *Water Maker* ambayo kwa muda wa saa 12 unaweza kuvuna maji yasiyopungua lita 5000. Maji hayo ni safi kuliko hata ya Kilimanjaro. Niko tayari kuisaidia Serikali pindi ikihitaji taarifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kichocheo kikubwa cha uzalishaji wa bidhaa zozote ni uhifadhi na masoko ya bidhaa hizo hasa za kilimo, uvuvi na ufugaji. Ipo taaluma na teknolojia ya kuhifadhi mazao yasiharibike kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na

pia kupata soko nje ya nchi. Mheshimiwa Dr. Nagu tuliwahi kutembelea kiwanda kinachotengeneza mashine inayoitwa Aggrey ambayo hata maji yaliyomo ndani ya takataka au karatasi inayanyonya na kutumika. Pamoja na kwamba ninajitahidi sana kuwaelimisha taasisi mbalimbali kama SIDO, Kilimo na kadhalika, bado haijachukuliwa kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niipongeze kwa dhati hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na ile ya Waziri wa Tamisemi kwa jinsi zilivyojaa umahiri mkubwa. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kimekuwa kikifanya kazi nzuri ya kugawa chakula katika sehemu zinazokumbwa na ukame kwa utaratibu wa kugawa bure kwa wananchi wasiokuwa na uwezo kabisa na kwa wale wenye uwezo kidogo kuuziwa kwa bei nafuu. Naishauri Serikali itambue upande wa pili wa maeneo ya wakulima (wazalishaji) ambao lipo kundi la wale ambao hawana uwezo kabisa kiasi cha kushindwa kulipia kiasi cha pesa ili kukombolea pembejeo za ruzuku. Naishauri Serikali itambue uwepo wa kundi hili ili waweze kupewa bure pembejeo hizo au kuwe na utaratibu wa kuwakopesha na walipe pindi wanapovuna na lile kundi la pili wachangie kwa kutoa pesa.

Pia naiomba Serikali ikubaliane na hali halisi kwa Mikoa ambayo imekuwa na uhakika wa mvua na hivyo kuwa na uhakika wa kwamba pesa ya kutosha inaelekezwa kwenye hii Mikoa ili nchi iwe na uhakika wa kujitosheleza na chakula na kuuza ziada nje ili kuinua kipato na kuingizia Taifa pesa za kigeni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa na nia thabiti katika kuongeza ufanisi katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kwa kufanya mapitio ya sera na sheria zinazohusika ili huduma zote kwa wawekezaji zitolewe katika kituo kimoja *(One stop centre).* Ni nia njema sana ya Serikali. Naomba pamoja na hatua hizo, naishauri Serikali katika mpango wake wa kutoa vitambulisho vya Taifa *(National Identity Cards)* ihakikishe kwamba tunaitumia fursa hii ya kutoa vitambulisho kwa kuwa na *National data base* kwa taarifa zitakapochukuliwa *(particulars),* basi ziweze kusambazwa kwenye maeneo yote kwa maana ya taasisi zote za Serikali zinazopaswa kuwa na taarifa muhimu.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia sana kupunguza gharama kwani hali ilivyo kwa sasa mwananchi kila sehemu anayokwenda kupata huduma ataulizwa *particulars* zake kwa maana ya picha, tarehe ya kuzaliwa, wapi alizaliwa, wazazi wake wako wapi na lini alisoma.

Mheshimiwa Spika, tukitumia vizuri fursa hii ni kwamba *particulars* hizo zikipatikana zipelekwe vituo vya Polisi Makao Makuu kwa shughuli za usalama, kwa *TRA* itarahisisha ukusanyaji wa kodi ili kuhakikisha kwamba wote wanaopaswa kulipa

kodi wanalipa. Pia *particulars* hizo zifike ofisi za uhamiaji lengo ni kuwa na *One stop centre.*

Mheshimiwa Spika, haya yanawezekana na yamekuwa yakifanyika katika nchi nyingine kama vile Singapore, nasi tunaweza tukidhamiria.

Mheshimiwa Spika, hata zoezi lililoanzishwa na Serikali ya kuandikisha wale wote wanaotumia simu za mikononi halijaleta matunda yaliyotarajiwa, kwani watu bado wanadanganyana kutumia *line* za simu vibaya.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu Mikoa ya pembezoni ambayo inakosa fursa nyingi na hivyo kuendelea kubaki nyuma kimaendeleo, kwani watumishi wakipangwa kwenda kufanya kazi, hawaendi kuripoti kufanya kazi kwa visingizio mbalimbali. Kubwa kabisa likiwa ubovu wa miundombinu. Nashauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi ili kuhakikisha kwamba tunakwenda pamoja kwa kutokuendelea kuachana zaidi, kuelekeza na kusukuma maendeleo kwa Mikoa iliyo pembezoni mwa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, naamini hili litatekelezwa ili Mikoa yote ya pembezoni iwe ni sehemu salama ya kuishi kwa wananchi wetu na watumishi wafurahie kwenda kufanya kazi katika Mikoa iliyo pembezoni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, *CAG* alitoa taarifa yake kueleza kwamba hakupatiwa nyaraka za malipo ya shilingi bilioni 48 kwa makampuni yaliyofaidika na mpango wa 1.7 trilioni *Dh Stimulus package*. Nilipomwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hafahamu suala hili. Wabunge mara zote tumetaka ifanyike *Special Audit on Stimulus package*. Serikali mara zote imekuwa ikikiri kuwa *special audit* itafanyika na taarifa kutolewa kwa Wabunge lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Serikali itoe kauli juu ya jambo hili na kwamba ni lini *CAG* ataanza *Special Investigation Audit on Stimulus Package (1.7 trilion TShs).* Jambo hili limeandikwa sana kwenye vyombo vya habari na kusemwa sana Bungeni. Kwa hiyo, ni vyema sasa *audit* ifanyike na hatua muafaka zichukuliwe kwa watakaobainika kuiba fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kuchukua hatua ni dalili za kuficha maovu. Ni vyema Serikali iwe tayari wakati wote kuhubiri hoja hizi. Upotevu wa fedha za *Stimulus Package* hauwezi kukubalika kwani ni fedha ambazo Serikali ilikopa.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake ya kwanza ya *Extractive Industry Transparency Initiative (EITI)* ambayo sasa Tanzania ni *"Candidate country"* imeonekana kuwa shilingi bilioni 20 katika mwaka wa fedha 2008/2009 hazionekani upande wa Serikali, kwamba, fedha ambazo makampuni yamelipa zina tofauti ya ziada ya shilingi bilioni 20 kwa zile ambazo Serikali imesema imepokea. Mheshimiwa Rais

Jakaya M. Kikwete alipokuwa kwenye Mkutano wa EITI huko Paris, Ufaransa, aliahidi kuchukua hatua kwa kumtaka *CAG* afanye uchunguzi kuhusu tofauti hii kwa mwaka 2008/2009. Hatua hii ya Rais ni muafaka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba uchunguzi huu ufanyike kwa miaka nane ya nyuma (2009/2010, 2008/2009, 2007/2008, 2006/2007, 2005/2006, 2004/2005, 2003/2004, 2002/2003). Napendekeza hili kwa sababu kuna uwezekano mkubwa kuwa kuna tundu fedha za malipo kwa madini (*royalty* hasa) zinavuja. Mwaka mmoja tu (2008/2009) imegundulika shilingi bilioni 20 kupotea (au tofauti) ni jambo la kushtusha sana.

Mheshimiwa Spika, kwa makusudi kabisa tumeamua kupandisha ushuru wa mafuta ya taa ili kulinganisha bei ya mafuta ya taa na dizeli ili kudhibiti uchakachuaji wa mafuta. Naunga mkono suala hili. Hata hivyo, suala hili linahusu wananchi wa kawaida na tumeanza kuona malalamiko kwamba tutawaumiza wananchi vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa jambo hili linawagusa wananchi masikini. Hata hivyo gharama za uchakachuaji ni kubwa sana kwa uchumi wa nchi. Sisi kama viongozi, tuchukue hatua madhubuti ili kueneza umeme vijijini na kuwapunguzia wananchi adha. Kama nilivyopendekeza leo asubuhi nilipokuwa nauliza swali la nyongeza kwenye swali Na. 126 (27 Juni, 2011) kwa Waziri wa Nishati na Madini, ni vyema fedha zinazotokana na ushuru wa mafuta ya taa zielekezwe kwa wanaoumia na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa. Fedha yote inayokusanywa na *TRA* kutoka mafuta ya taa ipelekwe *REA* ili kueneza umeme vijijini. Jambo hili litasaidia sana kueleza wananchi juu ya maamuzi yetu kuhusu bei ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete alipokuja Kigoma, aliahidi Vituo vya Afya viwili, *Mahembe Ward* na *Mukigo Ward*. Hii haikuwa ahadi ya Kampuni, bali ahadi ya Urais kwani ilitolewa mwezi Juni, 2010. Halmashauri ya Wilaya Kigoma tayari iliwasilisha Serikalini miradi maalum. Ninapenda kujua kama miradi hii imepewa fedha kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa mfumo wetu wa utawala ubadilike. Tuachane na kada ya Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa na badala yake tuimarishe Kitaasisi kada ya *WEO's* na watendaji *(DED's)* na Wenyeviti wa Halmashauri. Kazi za kitendaji ni za Ma-*DC* wafanye Ma-*DED*. Kazi za kisiasa wafanye Wenyeviti wa *Council*/Manispaa. Uamuzi huu utasaidia sana kuimarisha utawala bora katika Serikali za Mitaa. Ninashauri Serikali ikubaliane na pendekezo hili ambalo siyo jipya.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu amesema Serikali itaongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa kuzalisha nishati ya umeme (ukurasa wa 37). Hatua hii ni nzuri na ninaomba itekelezwe kwenye mradi wa Malagarasi (Igamba III 41MW). Baada ya Mradi wa Mto Malagarasi (Igamba I 8MW) kuahirishwa kutokana na sababu za kimazingira *(MCC),* upembuzi yakinifu umefanyika kwenye maeneo mengine ya mto. Sasa imegundulika kuna umeme mwingi zaidi Igamba III, 41MW. Hata hivyo *MCC* hawawezi tena kutoa fedha za mradi huu maana ni mradi mpya.

Ninashauri sekta binafsi ipewe mradi huu kwa kupitia *PPP*. Mradi utangazwe ili kupata *Investors* wajenge *Hydroplant* ili Kigoma ipate umeme na kuingiza umeme huu kwenye gridi ya Taifa. Vilevile, Serikali inaweza kuuliza mifuko ya Pensheni ambayo imeonyesha *Interest* ya kushiriki kwenye kuzalisha umeme kama watapenda kuwekeza katika mradi huu. Kwa kutumia *PPP* ni fursa safi kabisa kumaliza mradi huu ambao utanufaisha Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi kwani 41MW zinatosha kabisa kuunganisha Mikoa hii.

Ninashauri kwamba ianzishwe *Special Purpose Vehicle (SPV) – Western Tanzania Electricity Co. Ltd (WTEC)* na ipewe *franchise* ya kuzalisha umeme, kusambaza na kuuza kwa eneo la Kigoma, Tabora na Katavi. *Special Purpose Vehicle (SPV)* iwe na *shareholders* kama *TANESCO, NSSF/PPF/PSPF/LAPF*. Eneo hili la Magharibi lipatiwe umeme kutoka kampuni hii na siyo *TANESCO*. Tuangalie wazo hili ili tuweze kutatua shida ya umeme Mikoa ya Magharibi.

Mheshimiwa Spika, RCC Mkoa wa Kigoma alipendekeza kuwa baada ya Wilaya ya Uvinza kuanzishwa Jimbo la Kigoma Kaskazini liitwe Kalinzi. Ninaomba *Government Notice* itoke ili jimbo hili liitwe jina linalopendekezwa na watu wa Kigoma. Vilevile naomba mara baada ya Halmashauri ya Wilaya Uvinza kuanzishwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iitwe Halmashauri ya Wilaya Gombe. Lengo ni kuhakikisha kuwa Hifadhi ya Gombe inatumika kama jina la Halmashauri ili kuitangaza kama ilivyo Katavi, Kilimanjaro, Manyara na kadhalika. Naomba katika *GN* mambo haya yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya POAC ilipitia hesabu za Shirika la Masoko Kariakoo. Kamati iligundua kuwa Shirika hili linaendeshwa bila kufuata sheria iliyoliunda. Naomba Waziri mwenye dhamana aunde upya Bodi ya Shirika la Masoko na kuunda upya shirika hili kwa mujibu wa mapendekezo ya CAG kufuatia ukaguzi maalum uliofanyika.

Nauli za shirika zilizopotea zirejeshwe haraka na Shirika liwezeshwe kujielimisha kisheria.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kujenga barabara Jimboni kwangu (Mwandija – Manyovu). Ninaomba sasa tujielekeze kwenye umeme vijijini. Tayari kijiji cha Mahembe kimepata umeme, naomba sasa vijiji vyote ambavyo vimepitiwa na barabara ya lami vipate umeme. Tayari nimepeleka maombi *TANESCO* na wamefanya tathmini. Ninaomba Waziri Mkuu asaidie kusukuma mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti nzuri na yenye kuonyesha wapi tumetoka na wapi tunakwenda. Ningependa kuchangia yafuatayo, lakini kabla ya yote kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Elimu kwa kujenga mashule katika kila Kata na hivyo kuongeza vijana wanaosoma shule na hivyo kuelimika. Hata hivyo, tunajua kuwa shule zetu hizi bado zina upungufu mkubwa wa vifaa, Walimu pamoja na maabara na majengo. Ili vijana hawa wapate elimu ya kutosha baada ya kumaliza na wasiwe mbumbumbu, waliomaliza shule tunahitaji kutilia mkazo sana katika elimu bora.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu kwa sehemu kubwa imekuwa elimu "isiyojitegemea." Nchi nyingi duniani Shule za Ufundi Stadi zinatiliwa mkazo sana. Siyo kila mmoja anaweza kwenda Chuo Kikuu. Ni muhimu kuhakikisha vyuo kama hivi vinatiliwa mkazo. Ndiyo maana suala la *Skills Development Levy* na mgawanyo wake unahitaji kuangaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya Taifa lazima vishughulikiwe kwa haraka. Vitambulisho vitaleta mabadiliko katika mambo mengi, kama kupata kodi zaidi, wananchi kupata mikopo na kadhalika. Tayari miaka mingi imepita na hivyo suala hili sasa lifike mwisho.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi hauwezi kuzungumzwa bila suala la idadi ya watu. Katika Kitabu cha Mipango cha cha mwaka 2011/2012 - 2015/2016 tunaelezwa kuwa ukuaji wa idadi ya watu hivi sasa ni 2.9% na inatarajiwa kuwa idadi ya watu itakua kwa 2.9% ifikapo mwaka 2015. Ili hili liweze kufanyika, suala la elimu ya Nyota ya Kijani, lazima lifufuliwe. Wananchi waelimishwe kwa kutumia viongozi mbalimbali wakiwemo Wabunge, Madiwani, Viongozi wa dini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia suala la matibabu kwa wazee. Suala hili lilikwenda sambamba tokea wakati tulipoamua kuchangia matibabu. Hivi sasa wazee wengi wanapata shida. Hata wale waliostaafu hawana uwezo. Dawa ni ghali sana na hata kumwona Daktari. Kuwe na utaratibu maalum kutokana na tatizo ambalo bado lipo la kuwapatia vitambulisho maalum vyenye picha ili wazee wahudumiwe. Wizara ya Afya inabidi itambue hivyo wakati wa kutuma dawa hospitalini. Hili ni tatizo na lazima Serikali ilione hivyo na kuona jinsi gani ya kulitatua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe kauli kuhusu fidia ya wananchi katika Jimbo la Ubungo. Wananchi hao wameandika barua za muda mrefu kwa Ofisi ya Wizara husika baada ya kutopata majibu toka Wizara za Kisekta. Maeneo hayo mahususi ni:-

- Fidia kwa wananchi na Kata ya Kwembe eneo la Mloganzila ambao wanapaswa kupitisha ujenzi wa Chuo cha Afya Muhimbili (MUHAS). Tathmini imefanyika mara kwa mara katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Wananchi hawa wana hati ya Kijiji na Dar es Salaam VC & O ya mwaka 1980;

- Fidia ya wananchi kuhusu mradi wa mabasi yaendeyo haraka *(DART);* fidia kwa mwananchi mmoja katika eneo la Kimara na pia fidia katika eneo la Shekilango. Pia, maombi maalum yaliyowasilishwa na *DART* Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya fidia ya wananchi wanaoishi eneo la Kituo cha Mabasi ya Ubungo kwa ajili ya upanuzi wa eneo la mradi; na

- Fidia kwa wananchi wa eneo la barabara ya Morogoro watakaoathirika na ujenzi wa *Flyover* na upanuzi wa barabara husika, kufuatia tamko la Waziri Mkuu kusitisha utekelezaji wa agizo la *TANROADS* na Waziri Magufuli ili kufanya tathmini ya athari, bado hakuna hatua kamili zimechukuliwa na Mkoa wala Wilaya kama Waziri Mkuu alivyoelekeza kutokana na viongozi husika kutokufika kwa wananchi. Wahanga hao wameandika barua kwa Mkoa na kwa Waziri Mkuu yenye maelezo na vielelezo vyote ikiwemo hati za ardhi (baadhi) hati za wakazi na utata uliopo wa kisheria kuhusu upana wa barabara na mgongano na Sheria ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu pia atoe kauli kuhusu maombi maalum yaliyowasilishwa na vyombo mbalimbali vya Mkoa wa Dar es Salaam iwapo ni kwa kiasi gani yamekubaliwa. Baadhi ya maombi hayo ni yafuatayo:-

- Maombi kwa ajili ya ununuzi wa mashine na uendelezaji wa dampo la jiji Kinyamwezi ili kukabiliana na ongezeko la uchafu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

- Maombi ya mradi wa *DART* ya kukarabati kwa dharura barabara za mchepuko *(Feeder/filter roads)* kwa ajili ya kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam wakati ujenzi wa barabara na Vituo vya Mabasi yaendayo haraka *(DART)* utakapoanza. Serikali izingatie kuwa barabara ya Morogoro itakapoanza kuvunjwa eneo la Ubungo mataa, foleni itaongezeka kwa kiasi kikubwa sana kama barabara za kuchuja magari mathalani *External* mpaka Kimara, Msewe mpaka Chuo kikuu, Mbezi mpaka Goba, Malamba mawili mpaka Kinyerezi ni muhimu zikapitika vizuri sana kama njia mbadala za kupunguza foleni.

- Maombi ya fedha za nyongeza toka *LAPF* kwa ajili ya kuhamisha mabomba ya maji Mbezi kuwezesha ujenzi wa kituo cha kuegesha malori eneo la Mbezi Luis kama ilivyotajwa katika maelezo ya kiutendaji ya Mheshimiwa Mkuchika Ofisi za Waziri Mkuu TAMISEMI Ukurasa 35.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya maendeleo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba zitengwe fedha za kuongezea nguvu za Manispaa baada ya Kinondoni kuhusu ujenzi wa njia baada ya barabara kuliwa na maji katika kingo ya Mto Gide eneo la Makuburi *External*. Suala hili limeshatolewa ahadi na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa miaka kadhaa nyuma. Nilimwandikia barua Waziri wa TAMISEMI, na nashukuru aliwakumbusha Manispaa ya Kinondoni. Manispaa imetenga shilingi milioni 10 kwenye mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Makuburi mpaka Makoka kwa kiwango cha changarawe. Hata hivyo, kiasi hicho hakitoshi kulipa

fidia kwa wananchi wanaopaswa nyumba zao kuvunjwa kupisha njia mbadala na pia gharama za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI itoe kanuni na mwongozo wa kufafanua majukumu ya uratibu ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ili kuepusha mgongano na Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la kuanzishwa kwa Wilaya ya Wanging'ombe Mkoa mpya wa Njombe. Awali ya yote, naipongeza sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa kuwa Wilaya hiyo ipo ndani ya jimbo hilo. Wilaya hii ina Tarafa tatu ambazo ni Wanging'ombe, Mdandu na Imelinyi ikiwa Tarafa ya Mdandu ipo katikati ya hizo Tarafa tatu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete akiwa Kata ya Igwachanya Tarafa ya Mdandu aliahidi kuwa suala la Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging'ombe wananchi wa Wilaya hiyo watapewa fursa ya kutoa mapendekezo ya mahali panapofaa kuwa Makao Makuu ya Wilaya hiyo. Mpaka hivi sasa bado mchakato wa kupata maoni ya wananchi haujaanza na nashauri utolewe utaratibu au waraka ili mjadala huo uanze kuanzia ngazi za Kata, Wilaya na mwisho Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa sana wa Watendaji wa Kata na Vijiji vingi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Nafasi nyingi ziko wazi na kumekuwepo na watu wanaokaimu nafasi hizo lakini hawalipwi mishahara. Hawa ndio walikuwa mstari wa mbele kuipinga CCM isichaguliwe na pia wengi wao walikuwa wanazuia wananchi kuchangia maendeleo ili Serikali ya Chama cha Mapinduzi ionekane dhaifu na kwa kweli kama hatua za haraka hazitachukuliwa mipango yote hii tunayopanga haitatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Kitengo cha Maafa. Namkushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maana wapiga kura wangu wa Kijiji cha Uhenga, Kata ya Saja walivyosaidiwa nyumba zao zilizoezuliwa na mvua na upepo mwezi Desemba, 2010. Halmashauri ya Wilaya Njombe itoe Sh. 3,900,000/= lakini Kitengo cha Maafa kilifidia Sh.2,900,000/= tu. Naomba fedha zilizobaki zitolewe ili Halmashauri isikwame kutekeleza miradi yake.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maamuzi ya haraka kuwapatia kibali walioomba kuingia katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ambayo yako Mchuchuma, Ngaka na Kiwira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuna uhakika na uwezo wa kifedha wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* ambalo limeomba kuendesha mgodi wa makaa ya mawe Kiwira, nashauri wapewe kazi au kibali cha kuendesha mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, walimu na watumishi wengine wa Wizara ya Elimu katika Mikoa na Hhalmashauri zetu wanakatishwa tamaa na hivyo kupunguza morali ya kazi zao

kiutendaji na matokeo yake ni kushuka kwa kiwango cha elimu kwa watoto wetu. Kwa mfano, Maafisa Elimu wa Mkoa sio Wakuu wa Idara na hao ndio wanaopendekeza Maafisa Elimu wa Wilaya kupanda vyeo na kuwa Wakuu wa Idara katika Halmashauri zao na kuwa na mishahara mikubwa kuliko *REO* na kuwazidi kwa kiwango cha zaidi ya Sh.800,000/=. Tendo hili sio la utawala bora.

Mheshimiwa Spika, walimu wako maeneo mengi, wanaishi bila waume au wake zao kwa kisingizio cha upungufu wa walimu na hivyo kila wakiomba uhamisho wanaambiwa watafute mtu wa kubadilishana. Jambo hili linaathiri utendaji na kiwango cha elimu kwa sababu walimu hawa huwa katika nafasi ya kupata magonjwa kama Ukimwi na hivyo Serikali kupoteza nguvukazi kwa walimu kufa kwa Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Makao Makuu ya Wilaya kwenda vijijini ni muhimu sana na siyo kuangalia barabara kuu kupitia katika Makao makuu ya Mkoa na kudhani Mkoa husika una barabara. Ni muhimu kuangalia barabara kwenda vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi ujenzi wa barabara ya Mpemba – Isongole kuunganisha na nchi ya Malawi. Ombi langu ni kwamba kwa kuwa wananchi walimsikia na kumshukuru Mheshimiwa Rais, naomba barabara hii ijengwe sasa.

Mheshimiwa Spika, linguine, kuna bonde la umwagiliaji la Sasenga Wilayani Ileje halijatengenezewa miundombinu yake kwa muda mrefu. Nashauri sasa bonde hili lipewe bajeti ya kutosha sasa.

Mheshimiwa Spika, pia Wilaya ya Ileje na baadhi ya maeneo katika Wilaya ya Mbeya vijijini, yanahitaji mbolea mapema mwezi wa Julai badala ya Desemba.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuzungumzia suala la afya. Hospitali ya Itumba Ileje haijakamilika kwa muda mrefu, watu wake wanakwenda nchini Malawi kufuata matibabu. Nashauri katika bajeti hii fedha itengwe kwa ajili ya Hospitali ya Itumba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu pamoja na Watendaji wake kwa kazi kubwa wanazozifanya na kuleta hotuba hii nzuri sana ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wa Viongozi Wakuu, yaani Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Muungano kukutana na kuzungumzia masuala ya kero za Muungano, kwani kwa nchi kama hii inayoendelea siyo busara kuzozana wenyewe kwa wenyewe. Ninaiomba Serikali zile kero zilizotatuliwa kwa kuwa Wabunge huhoji na kuuliza juu ya kero hizo, basi ni busara Waziri husika akalieleza Bunge juu ya maamuzi ya kero hizo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *MACEMP* kwa Zanzibar umefanikiwa sana kwani umeweza kuwanyanyua wavuvi wadogo, walima mwani kwa kuwapa maboti na nyavu za kuvulia na vifaa vya kulimia mwani. Mradi huu ni mzuri, ukiendelea, utawapunguzia umaskini wavuvi wengi wenye kipato cha chini kwani kuna wavuvi wengi hawana uwezo hata wa kununua nyavu. Ninaiomba Serikali itenge fungu maalum kwa ajili ya kuwapa mikopo wavuvi hawa kwani tunaweza kupunguza uvuvi haramu, kwa kuwa kila atakayepewa mkopo huo atapewa maelekezo ni vifaa gani vya uvuvi vinavyotakiwa na Serikali na masharti ya mikopo hiyo ni kununua vifaa vya kisasa ambavyo ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aiangalie Hospitali ya Kitete kwani iko katika hali mbaya hasa kwa upungufu wa majengo, dawa pamoja na vitanda katika wodi ya akina mama wanaojifungua. Hali ya maji safi pia ni tatizo kubwa katika hospitali yetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tabora hawana hospitali yake, lakini mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi milioni 100 tu. Hiki ni kiasi kidogo. Nashauri fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi mpya ya Halmashauri shilingi milioni 600 zihamishiwe katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwani kwa sasa ofisi iliyopo inatosha. Hospitali ya Wilaya ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tusaidiwe *TUWASA* waweze kulipwa fedha zao toka Wizara ya Ulinzi na Polisi ili tupate nguvu za kuweza kununua *pump* mbili. Hizi zitasaidia kuongeza uzalishaji wa maji katika Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, bei ya tumbaku siyo nzuri mwaka huu, tunaomba Serikali ijitahidi mwakani angalau bei iwe nzuri hasa ukizingatia wapinzani wanatumia kisingizio cha bei kushuka, eti fedha iliyotumika kununua sare za Chama cha Mapinduzi (CCM) zilitokana na kupunguzwa bei ya tumbaku. Utakumbuka Tabora ni miongoni mwa Mikoa iliyowezesha Chama cha Mapinduzi (CCM) kushinda Viti vyote vya Ubunge na Uenyekiti wa Halmashauri/Meya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika suala la reli, tunaomba karakana ya Tabora iangaliwe vizuri kwani hali yake kwa sasa ni mbaya na inavuja sana. Chuo cha Reli hakitumiki kikamilifu, tunaomba kiimarishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara nina imani hali inaridhisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwanja wa ndege, naipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 16, hizi zitasaidia ujenzi wa uwanja wetu.

Mheshimiwa Spika, nyumba za (Polisi) Askari wetu zinatisha sana, Tabora tumesahaulika sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mkoa wa Tabora umesahaulika sana kwa maendeleo, tunaomba mtukumbuke ili Mkoa wetu usije ukatekwa na wapinzani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu, kwa hotuba nzuri iliyosomwa na Waziri Mkuu katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba niweke wazi kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu nchi yetu inaadhimisha jubilee ya miaka 50 ya uhuru wetu tangu tulipoanza kujitegemea kama Taifa. Katika kipindi hiki tulishuhudia mataifa mengi ya Afrika yakisambaratika au kupigana wenyewe kwa wenyewe. Hata hivyo, Taifa letu limeendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani. Hili lisingewezekana ila tu ni kutokana na misingi imara ya amani na utulivu iliyowekwa na Waasisi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ili kuonyesha uimara wetu, tumepita katika mabadiliko mengi na mifumo mingi bila amani yetu kutetereka. Kwa mfano, tulianzisha Azimio la Arusha, tukaingia kwenye Azimio la Zanzibar, pamoja na hayo tulibadilisha mfumo wetu wa siasa na kupokea Mfumo wa Vyama Vingi na tuliingia katika Mfumo wa Biashara wa Soko, yote haya tuliyafanya kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, niliyoeleza, Taifa letu limepiga hatua kubwa sana ya maendeleo katika sekta mbalimbali kitaifa na kimataifa. Kwa kuwa ni vigumu katika muda niliokuwa nao kueleza kila kitu, inatosha tu nipongeze mikakati ya Serikali katika kukuza uchumi wa Taifa na kuinua maisha na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nijadili mambo kadhaa yaliyojitokeza katika hotuba ya Waziri Mkuu, nikiyahusisha na maendeleo, hali ya uchumi, matatizo na ustawi wa Jimbo la Rombo ambalo wananchi wake wamenipa heshima ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rombo, linategemea umeme kutoka katika gridi ya Taifa. Umeme unaokwenda Rombo unaanzia Kiyungi *(TPC)* kwenda Boma Ng'ombe na kisha Moshi - Himo, Marangu na hatimaye Rombo. Kutokana na urefu wa njia hii, ni wazi kwamba njia imezidiwa na hivyo Jimbo la Rombo lina matatizo ya kukatikakatika kwa umeme na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba upungufu wa nishati ya umeme unawaathiri wananchi kwa kupunguza uzalishaji na hata wakati mwingine kuathiri vifaa

vyao vinavyotumia umeme kutokana na makatizo ya ghafla na yasiyotabirika ya nishati hii. Wananchi wa Rombo wamenituma niiombe Serikali, na sasa natekeleza ombi lao kwa kuharakisha mradi ambao tumesikia kama tetesi kwamba utajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Japan ili kuutoa umeme moja kwa moja kutoka Kiyungi *(TPC)* kuelekea Rombo ili tuweze kupata umeme wa kutosha. Kama njia hiyo haitawezekana, ni ombi letu pia kwamba hekima na busara za Serikali zitawezesha kuleta utatuzi wa kero hii.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo tuliopitisha hapa Bungeni, kipaumbele cha maji kilijadiliwa kwa kina. Ni kwa sababu Serikali yetu inatambua kwamba maji ni raslimali yenye thamani kubwa kwa jamii yoyote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, Jimbo la Rombo limekuwa katika hali ya ukame wa mara kwa mara. Hali hii pamoja na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu, kumesababisha upungufu wa kutisha wa maji katika Jimbo la Rombo. Mito ya msimu tuliyokuwa tukitegemea pamoja na chemchemi ambazo zilikuwa zinaongeza upatikanaji wa maji zimekauka zote. Chanzo kikuu cha maji ni tenki kubwa la maji la Amboni lililojengwa kabla ya uhuru ambalo lilikuwa linapokea maji kutoka Marangu. Hivi sasa tenki hilo halipati ujazo wa kutosha na kusababisha mgao mkubwa wa maji usiowatosheleza wananchi hasa waishio ukanda wa chini.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi ambayo kama itatekelezwa, itatuletea nafuu au kuondoa kabisa tatizo hili. Kwanza kuna mradi wa ujenzi wa visima kumikatika ukanda wa chini ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Pili, Halmashauri na wananchi, wanashauri na kuiomba Serikali isaidie katika ujenzi wa malambo hasa ukanda wa chini ambayo yatatumika kwa ajili ya kuvunia maji ya mvua na yale yatokanayo na mito ya msimu kwa ajili ya matumizi majumbani na kwa kilimo cha umwagiliaji.

Kwa taarifa nilizonazo, wataalamu wa Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji walishafanya utafiti na kugundua kwamba yapo maeneo saba ambayo kama fedha zikipatikana malambo yakatengenezwa, tatizo la maji na njaa inayosababishwa na ukame litakuwa limetoweka.

Kwa sababu hiyo, naiomba sana Serikali katika bajeti ya mwaka huu ikubali kuidhinisha maombi ya fedha ambazo Halmashauri iliomba ili kuanzisha mchakato wa ujenzi wa malambo hayo. Fedha zilizoombwa kwa mujibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ni shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linaweza kutumika kutatulia matatizo yetu ya maji ni matumizi ya maji ya Ziwa Chala. Kwa kuwa alikwishatoa jibu la swali langu hapa Bungeni kwamba Serikali inafanya utafiti wa maji hayo, ni matumaini yangu kwamba utafiti huo utakwenda kwa kasi nzuri ili tuweze kujua hatma ya matumizi ya maji hayo.

Mheshimiwa Spika, kama mpango wa maendeleo wa miaka mitano unavyosisitiza, bado kilimo ni eneo linaloajiri Watanzania wengi. Hata hivyo, katika Jimbo langu, tunazo changamoto nyingi zinazotufanya tushindwe kupata faida na hivyo

kuinua maisha ya wananchi kupitia kilimo chetu. Wilaya ya Rombo ilitegemea sana zao la kahawa kama zao la biashara. Hata hivyo, gharama za uendeshaji, hali ya hewa, magonjwa mbalimbali ya kahawa, kuzeeka kwa mibuni na ukosekanaji wa Maafisa Ugani, kumewafanya wakulima kukata tamaa na kung'oa baadhi ya mibuni.

Wananchi wa jimbo la Rombo wanaiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka ruzuku katika pembejeo zinazohitajika kwa uzalishaji wa kahawa ili kupunguza gharama za uzalishaji na kufufua ari yao ya uzalishaji. Vile vile tunaiomba Wizara iweke mkazo na msukumo katika utafiti wa mbegu za mibuni zinazohimili magonjwa na hali ya hewa kwa sasa katika Jimbo la Rombo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa hali ya hewa katika Jimbo la Rombo haitabiriki. Kipindi kirefu sasa misimu ya mvua, yaani vuli na masika imekuwa ikichelewa sana au ikiwahi sana au kutopatikana kabisa na hivyo kuwafanya wakulima kushindwa kuweka mpangilio mzuri wa ratiba zao za kilimo. Hali hii ya ukame inasababisha mazao hususan nafaka kama mahindi na kadhalika kukauka mara tu yanapoanza kubeba.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rombo limezungukwa na mbuga za wanyama za Tsavo na Amboseli ambazo ziko nchi jirani ya Kenya. Kutokana na ukame, tembo wamekuwa wakivuka mpaka na kuingia katika mashamba ya wananchi upande wa Rombo katika ukanda wa nchi kwa makundi makubwa kutafuta maji na chakula. Katika siku za hivi karibuni, yameonekana makundi ya tembo zaidi ya 150 yakivuruga mashamba ya wananchi, kula mazao na kuhatarisha maisha ya watu. Serikali ilitoa ahadi ya kujenga Vituo vya Askari wa wanyamapori katika Vijiji vya Ngoyoni, Mahorosha na Kikelelwa. Hata hivyo, hadi sasa hakuna kituo hata kimoja kilichokamilika. Askari wanaotusaidia wana makao yao Arusha na mara nyingi wanapopigiwa simu gari yao inakuwa haina mafuta na kama wakifika, uharibifu mkubwa unakuwa umeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, zao pekee linalotegemewa sasa na wananchi wa Rombo ni migomba inayolimwa ukanda wa juu. Kutokana na hali hii, kwa miaka mitano mfululizo wananchi wa Rombo wamekuwa wakipewa chakula cha msaada na Serikali. Ndiyo maana tunaiomba Serikali kwa dhati na kwa unyenyekevu itujengee malambo hasa katika ukanda wa chini ili tuweze kuvuna maji yatakayotusaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa dhati kwa uamuzi wake wa kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa Shule za Kata. Hivi sasa katika Jimbo la Rombo, kila Kata imefanikiwa kuwa na Shule ya Sekondari na katika Kata nyingine, kuna zaidi ya Shule moja. Kwa jumla Jimbo la Rombo sasa lina Shule za Sekondari 48. Kati ya hizo, Shule 41 ni za Kata na saba zinamilikiwa na Mashirika ya Dini pamoja na Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi. Kati ya shule hizo, tano ni za Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, tunayo matatizo yanayofanana na yale ya wenzetu katika Majimbo mengine. Kwa mfano, tunao uhaba wa walimu. Shule nyingi hazina maabara na maktaba na pia nyingi bado ziko katika ujenzi wa madarasa na

matundu ya vyoo. Hali kadhalika, tuna uhaba mkubwa wa nyumba za walimu. Kutokana na uhaba wa ardhi shule tatu zimejengwa kwa mtindo wa ghorofa, nazo ni Shule ya Sekondari Shimbi, Shule ya Sekondari Makiidi na Shule ya Sekondari Bustani.

Mheshimiwa Spika, maombi yetu kwa Serikali ni haya yafuatayo:-

(1) Kupatiwa walimu wa kutosha;

(2) Kutusaidia katika mzigo mkubwa wa kumaliza ujenzi wa shule zetu hasa zile ambazo zinajengwa kwa mtindo wa ghorofa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo nakadhalika;

(3) Kutujengea Chuo cha Ufundi ili wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne na cha Sita ambao ni wengi sana waweze kuendelezwa na hivyo kupatiwa ujuzi wa kuweza kuwasaidia katika maisha; na

(4) Kwa kuwa watoto yatima wameongezeka, tunaiomba Serikali kuona uwezekano wa kuwafutia watoto hawa ada na michango mbalimbali.

Mheshimia Spika, katika Idara hii ya Elimu, yapo pia malalamiko makubwa miongoni mwa walimu. Wapo walimu wengi wanaofundisha katika Shule za Msingi ambao hawajapandishwa madaraja tangu mwaka 2005. Vilevile kuna walimu ambao wameajiriwa siku za hivi karibuni ambao hawajalipwa stahili zao za kusafirisha mizigo na hadi sasa hawajaingizwa katika utaratibu wa kawaida wa mishahara yao, yaani katika *payroll.* Tunaiomba Serikali kufuatilia na kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo tunakabiliana nalo ni mimba mashuleni. Katika baadhi ya shule, tatizo hili ni kubwa kutokana na wanafunzi kukaa umbali mrefu na shule na hivyo kulazimika kujitafutia sehemu za kulala ambazo siyo lazima. Mkakati ambao tunafikiri unaweza kuwasaidia watoto hawa ni kuwajengea hosteli katika maeneo maalum ambapo wanafunzi wa kike wa shule mbalimbali za jirani wanaweza wakakaa kwa pamoja chini ya uangalizi maalum. Ninaiomba sana Serikali itusaidie utaalamu pamoja na nyenzo ili kwa kushirikiana na wananchi tuweze kutatua tatizo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutujengea barabara katika kiwango cha lami kutoka Kilacha – Mwika na Marangu – Mkuu – Tarakea na Tarakea – Kamwanga ambayo inategemewa kukamilika mwaka huu. Haya ni maendeleo makubwa, kwani barabara hii itabadilisha hali ya kiuchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo ni kati ya Wilaya ambazo hazina Hospitali ya Serikali ya Wilaya. Hospitali inayotumiwa kama Hospitali ya Wilaya ni Hospitali ya Huruma ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi. Hospitali hii ni ndogo yenye uwezo wa kulaza wagonjwa wasiozidi 350. Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilitafakari kuanzisha ujenzi wa Hosptiali ya Wilaya katika Tarafa ya Mashati. Wazo hili bado lipo na tunaiomba Serikali katika bajeti yake ya mwaka ujao wa fedha pamoja na

mambo mengine iingize Wilaya ya Rombo katika mipango yake ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya.

Katika Idara hii ya Afya tatizo kubwa linalowakabili wananchi ni huduma kwa wazee, watoto chini ya miaka mitano na vifaa vya kujifungulia kwa akina mama wajawazito. Kama ilivyo sera ya Serikali, huduma kwa makundi haya inapaswa kutolewa bure, lakini hata hivyo bado utekelezaji wake umekuwa mgumu na hivyo kuyafanya makundi haya kuendelea kutaabika kutokana na gharama za matibabu. Tunaiomba Serikali ifikirie kutoa maagizo maalum ili hospitali zetu ziweze kutekeleza sera hii kikamilifu.

Vilevile huduma ya Bima inayotolewa, inalalamikiwa sana na wananchi, kwani mwamko wa kuingia kwenye Bima hiyo ni mkubwa, lakini wananchi hawapatiwi baadhi ya huduma na vile vile dawa hazipatikani.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo kama inavyojulikana ni Wilaya ya mpakani, kwa sababu hiyo upo mwingiliano wa watu kijamii hasa katika shughuli za biashara. Hali hii inavutia vitendo vingi vya uhalifu ingawaje katika miaka ya hivi karibuni vimepungua na ninachukua nafasi hii kuvipongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Jeshi letu la Polisi katika Wilaya ya Rombo linakabiliwa na matatizo makubwa yafuatayo:-

Askari Polisi katika Wilaya ya Rombo hawana makazi. Tangu Wilaya ilipoanzishwa mwaka 1972 hadi sasa miaka 39 hapajakuwa na mkakati wa kujenga nyumba za Polisi. Askari wetu wanaishi katika mabanda yaliyojengwa kwa mabanzi ambayo kwa kiasi kikubwa mengi yameliwa na mchwa pamoja na sungusungu. Hali hii kwa hakika inawanyima Askari ari na morali ya kufanya kazi zao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Askari wana malalamiko ya kutolipwa fedha za uhamisho kwa muda mrefu. Hata wanapofanya maombi ya kulipwa fedha hizo, hakuna hatua zinazochukuliwa na hivyo kubaki na utii wao wa kiaskari. Hili ni eneo lingine ambalo linawaondolea morali ya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya nzima, Askari hawana mahali ambapo wanaweza wakapumzika baada ya kazi ngumu hata wakafanya michezo au mazungumzo ya kubadilishana mawazo, yaani hawana bwalo ambalo lingeweza likawafanya wakafanya mambo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika miaka minne iliyopita Jeshi la Polisi katika Wilaya ya Rombo halijawahi kupata mgao wa mafuta ya magari yake. Wakati wa Uchaguzi Mkuu walipata mgao wa lita 400 tu za dizeli. Hali hii inalifanya Jeshi letu kuwa ombaomba. Wananchi wanatia shaka kwamba magari yaliyopo yanapata wapi mafuta na kujenga hisia kwamba yanaweza yakapatikana hata kwa wahalifu. Ndiyo maana wamenituma niiombe Serikali pamoja na kushughulikia matatizo mengine ya

Polisi Wilayani, Serikali itoe ruhusa maalum ya kutumia nusu ya tozo zinazotokana na makosa ya barabarani kwa ajili ya kununulia mafuta ya magari.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza lina matatizo yanayofanana na yale niliyoyataja kwa Jeshi la Polisi kuhusu Askari wake hapo juu. Hata hivyo, matatizo ya ziada ya Jeshi la Magereza katika Wilaya ya Rombo ni msongamano wa wafungwa unasababishwa na mambo matatu yafuatayo:-

Jambo la kwanza ni uhaba wa Mahakimu katika Wilaya ya Rombo unaosababisha mashauri mengi kuchukuwa muda mrefu kuamuliwa. Jambo la pili ni uhaba wa vyumba vya wafungwa na mahabusu na mwisho ni uchache wa Wapelelezi. Hali hii inatisha kwani nilipotembelea Gereza hili nilionana na wafungwa akina mama na watoto wao wachanga, mmoja akiwa mchanga wa wiki mbili mahabusu. Kilichonisikitisha zaidi ni kwamba mama mmoja anashikiliwa na mtoto wake mchanga kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa sababu mume wake anayetuhumiwa kwa mauaji anatafutwa na Polisi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo linaloikabi Idara ya Magereza ni ukosefu wa uzio wa kuzunguka eneo la Magereza.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya utawala bora kwa maoni yangu inatakiwa kupewa msisitizo mkubwa kitaifa. Baadhi ya watendaji ngazi za Vijiji, Kata na Halmashauri hawawajibiki. Fedha zinazopelekwa na Serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali na zile zinazochangwa na wananchi hazitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kilio kikubwa sana cha wananchi kwani katika kila kijiji, baadhi ya watendaji huwachangisha wananchi pesa za maendeleo kwa kutumia vitabu viwili vya risiti, kimoja chao na kingine cha Halmashauri. Vilevile vocha za pembejeo au chakula cha msaada kinapotolewa na Serikali, huwaorodhesha ndugu zao au Marehemu na vile vile hubadilisha majina yao kwa namna tofauti ili mradi wamenufaika na huduma hiyo iliyolengwa na Serikali kwa wananchi. Katika kufanya hivyo, Mikutano ya wananchi vijijini haiitishwi ili kupewa taarifa ya mapato na matumizi. Kama vile kuna mtandao, inashangaza katika ngazi ya Halmashauri, ufuatiliaji umekuwa duni sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuimarisha kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili fedha za miradi ya wananchi na zile zinazochangwa na wananchi zipate kusimamiwa na kukaguliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo ilianzishwa rasmi mwaka 1972 na ofisi zake zilianzia katika nyumba walimokuwa wakiishi masista wa Kanisa Katoliki. Kwa muda mrefu Mkuu wa Wilaya na ofisi zote za Serikali na Halmashauri zilikuwa katika jengo hilo ambalo vyumba vyake vilijengwa mahususi kwa ajili ya makazi tena ya Watawa. Hivi sasa tunaishukuru Serikali, kwani Mkuu wa Wilaya na baadhi ya Watendaji wa Serikali wamehamia katika jengo la Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo sasa ni jengo la ofisi ya Halmashauri. Hakika jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Rombo halionyeshi hata kidogo sura ya Wilaya

iliyodumu kwa miaka 39. Wananchi wa Rombo tunaiomba Serikali katika mipango yake ya baadaye au kwa vyovyote vile itakavyoona inafaa, kuanzisha mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Makao Makuu ya Wilaya ya Rombo bado yapo katika Kijiji cha Kelamfua katika Kata ya Kelamfua Mokala. Ili kuweza kuuendeleza mji wa Rombo, tunaiomba Serikali kuupandisha hadhi mji wetu ili uweze kuwa na mamlaka kamili ya mji ili tuweze kuharakisha maendeleo yetu. Kwa sababu baada ya barabara yetu kujengwa kwa kiwango cha lami, tuna matumaini makubwa kwamba mpaka kati yetu na Kenya utafunguka kupitia Rombo na hivyo tutawaalika wawekezaji wa ndani na nje kujenga mahoteli, maduka, nyumba za kulala wageni na kadhalika. Hatutaweza kufikia malengo haya kama bado tutaendelea na hali tuliyonayo. Ikumbukwe pia kwamba Mlima Kilimanjaro upo katika Wilaya ya Rombo na njia za kupanda mlima zilizopo Rombo ni fupi sana ila tu zinatakiwa kutangazwa na kuendelezwa. Tukipata Mamlaka ya Mji, haya yatawezekana na matokeo yake tutaongeza uchumi wa watu wetu na vijana wetu watapata ajira kupitia biashara mbalimbali zitakazofanyika na shughuli za utalii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho, natambua Serikali ina majukumu mengi. Hata hivyo natambua pia kwamba Serikali ni sikivu na inawapenda watu wake. Hivyo, sina mashaka yoyote na ninaamini kwa dhati kabisa Serikali yetu itasikia kilio chetu na itatufanyia lile inaloona linafaa kwani daima mzazi mzuri hawezi kuombwa mkate na mwanawe naye akampa jiwe au akaombwa samaki akampa mtoto nyoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayopaswa kuangalia masuala yote ya utawala, amani, utulivu, maendeleo na kadhalika. Lakini kinachosikitisha, ofisi hii imekuwa kubwa sana ikihusisha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inaratibu hospitali, Shule za Sekondari na Msingi, Halmashauri zote na kadhalika. Hali hii inafanya utekelezaji uwe mgumu sana. Ombi na ushauri wangu ni kuwa TAMISEMI ijitegemee na isiwe chini ya Waziri Mkuu ili ifanye kazi zake vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la uteuzi wa *DCs* na *RCs*, ni ukweli ulio wazi kuwa tunahitaji kiungo kati ya Serikali kuu – Mikoa na Wilaya hadi Vijiji. Uzoefu unaonyesha wazi kuwa viongozi wa kuteuliwa huwajibika zaidi kwa waliowateua na siyo vinginevyo. Hii ndiyo sababu Wabunge waliochaguliwa na wananchi wamekuwa wakiwajibika kwa wananchi na wananchi wanapokuwa na tatizo lolote huwafuata wao. Ninaishauri Serikali ifute mpango wa uteuzi wa watu hao na badala yake wachaguliwe kama wanavyofanya nchi kama za Marekani ambapo *Governors/*(*RC* hapa) huchaguliwa. Kwa kuwa Ma-*RC* ni wasaidizi wa Rais katika Mikoa na Rais si mteule, bali amechaguliwa, ni vyema na hawa *RCs* na *DCs* wachaguliwe pia ili wawajibike vilivyo kwa wananchi. Lakini pia uteuzi huu hauzingatii uelewa wa mazingira ya sehemu husika, iweje mtu aliyekulia katika maeneo ya uvuvi apelekwe Kilimanjaro au Arusha kusiko hata na bwawa?

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali iwapatie wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu mikopo yao kwa wakati ili kuondoa tatizo la migomo na maandamano. Maandamano yanapelekea vyuo kufungwa, hivyo kuongeza gharama zisizo na maana na kodi za wananchi. Ni vyema sasa pale inapobainika Serikali ndiyo chanzo cha migomo, basi watendaji wachukuliwe hatua. Pale wanafunzi wanapokuwa ni chanzo, wafukuzwe na kuchukuliwa hatua stahili. Ieleweke kuwa wanafunzi hawa sio watoto ni watu wazima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Watendaji wake kwa hotuba nzuri inayokidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilombero hasa wanawake naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kutuletea msaada mkubwa waathirika wa mafuriko Kilombero, chakula cha kutosha kama maharage, Mafuta ya kupikia na chumvi. Mpaka sasa chakula bado kipo ghalani kusaidia waathirika wa mafuriko.

Mheshimiwa Spika, pia tunashukuru kwa pesa taslimu kwa ajili ya ukarabati wa barabara na madaraja za Halmashauri, pesa ziko Benki. Nashukuru pia kwa ajili ya kutuletea Chuo Kikuu cha Madaktari Bingwa cha Kimataifa Ifakara. Mahali pale kuna Waganda, Wazambia, Wakenya na kadhalika. Hii ni faraja kwa wananchi wa Kilombero/Ulanga.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuipandisha hadhi Hospitali ya St. Francis Ifakara kuwa Hospitali ya Rufaa. Hospitali hii imekuwa ukombozi kwa wakazi wa Kilombero na Ulanga.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba Daraja la Mto Kilombero lijengwe mara moja, linaturudisha nyuma kimaendeleo. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwenye Ilani ya mwaka 2005/2010 na 2010/2015. Hivi karibuni Mawaziri wawili Mheshimiwa Selina Kombani na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda walikwama kwa sababu Pantoni ilikuwa mbovu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atuangalie kwa jicho la huruma atupe daraja la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuondolewa kwa wafugaji Wilaya Kilombero na Ulanga, kwa kweli tunanyanyasika sana kwa sababu ya mifugo. Kilombero ni ghala la Taifa, kwa hiyo, jambo hilo halitawezekana kwa sababu ya wafugaji. Kilombero na Ulanga limekuwa ni bonde la kunenepeshea mifugo. Wakulima wanashindwa kulima kwa sababu mazao yanaliwa na mifugo. Sasa hivi hatuna kilimo cha Dharura. Vyanzo vya maji vinakauka, leo hii hatuna samaki. Mabwawa, mito inakauka kwa sababu ya wingi wa mifugo. Rais mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi hata Mheshimiwa

Waziri Mkuu aliamuru mifugo iondolewe, lakini hadi leo kati ya Mto 79 – 39 imekauka. Mto Kilombero unapungua kina, samaki nao wamepungua. Ninaomba mtoe amri wafugaji waondoke, wanatupiga, wanazuia maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ripoti ya CAG kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2010 imeeleza bayana kwamba Halmashauri nyingi haziwezi kujiendesha kutokana na vyanzo vyake vya mapato kutokuainishwa na kuhitaji kuupitia upya na hivyo kupelekea Halmashauri hizo kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya shughuli za maendeleo, nashauri Ofisi ya TAMISEMI ichukue hatua za haraka za kuzifuatilia Halmashauri ambazo zimeainishwa na *CAG* katika suala hili na kuwawajibisha Watendaji ambao hawatumii nafasi zao vizuri katika kuainisha vyanzo vipya vya mapato mahali ambapo kuna fursa ya vyanzo hivyo. Mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Singida imeonyeshwa mapato yake kwa kuainisha vyanzo vipya kama vile minara ya simu iliyopo katika maeneo mengi ya vijijini, kupata hati miliki ya majengo na ardhi/maeneo inayomiliki ili kuweza kuyatumia kibiashara zaidi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Singida kwa mwaka ulioishia June 30, 2010 imetumia matumizi ya zaidi ya Sh. 3,268,853,161/= wakati mapato yake ya matumizi ya kawaida ni Sh. 14,084,463,839/= na yale ya kawaida ni Sh. 17,353,317,000/=. Napenda kufahamu hayo matumizi ya ziada yametoka katika fungu gani? Je, Watendaji wanachukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo la utendaji wa kifedha katika Halmashauri mbalimbali, *CAG* ameainisha pia mapungufu kadhaa mfano mfumo wa fedha usiokidhi mahitaji, udhaifu katika utekelezaji wa majukumu katika kitengo cha ukaguzi wa ndani, ukosefu wa mfumo wa udhibiti wa vihatarishi na ukosefu wa udhibiti wa mazingira ya kupashana habari. Masuala haya yasipotafutiwa ufumbuzi wa haraka, yatasababisha upotevu mkubwa wa fedha za Serikali katika Halmashauri zetu kwa kukosa udhibiti.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchangia shughuli za maendeleo kwa kuwashirikisha wananchi siyo jambo baya endapo linafanywa kwa kuwaelimisha wananchi dhana nzima ya *D by D* ili waweze kuelewa ni sehemu gani wao wanatakiwa kuchangia na nini Serikali au wafadhili wanachangia. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, elimu ya *D by D* haileweki kabisa kwa wananchi waishio vijijini. Suala hili limekuwa likifanywa na Watendaji wa Vijiji na Kata kwa kutumia nguvu nyingi wakiongozwa na Mgambo ili kuwalazimisha wananchi kutoa mchango hususan katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata. Kumekuwepo na udhalilishaji mkubwa kwa wananchi hasa wale ambao kwa hali halisi wamekuwa hawana uwezo wa kutoa michango hiyo kutokana na hali ya umasikini walionao. Wananchi wanapokuwa hawana pesa wamekuwa wakinyang’anywa kuku, mbuzi, ng’ombe na hata vyombo vya

nyumbani ambavyo ukilinganisha na thamani ya mchango wa Sh.15,000/= au Sh. 20,000/= haileti maana halisi ya *value for money*.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na udhalilishaji mkubwa unaofanywa na Mgambo hasa kwa akina mama wajawazito au wajane na wale waliokimbiwa na waume zao kwa kuogopa michango. Wanawake hawa wanapokosa michango, hukamatwa na kufungiwa kwenye Ofisi za Watendaji wa Vijiji au Kata na kupewa usumbufu mkubwa. Mfano, mwaka 2009, katika Halmashauri ya Wilaya Singida kuna wanawake wawili walijifungulia katika Ofisi za Watendaji wa Kata baada ya kukamatwa kwa nguvu na kufungiwa huko ili hali wakiwa wajawazito. Hii ni udhalilishaji wa haki za binadamu na siyo busara kumfunga mtu kwa kukosa mchango ambao siyo kodi ambayo ipo kisheria na siyo sera ya Chama fulani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekuwa hawasomewi mapato na matumizi ya michango yao na hata majengo yanayojengwa yamekuwa hayamaliziki mwaka hadi mwaka na hayakidhi viwango, lakini wananchi wamekuwa wakichanga bila kujua pesa zao zinafanya nini. Ili wananchi waweze kuchangia kwa uhuru, ningeomba TAMISEMI ifanye kazi ya ziada ya kuwachukulia hatua za kisheria Watendaji ambao hujinufaisha kwa michango ya wananchi na kutumia nguvu nyingi ikiwepo udhalilishaji kwa wananchi hususan wanawake. Hili nalisema kwa sababu Halmashauri ya Wilaya Singida haikutumia ruzuku ya jumla ya Sh. 449,890,483/= kati ya Sh. 2,361,453,406/= ambazo zilitolewa kama ruzuku ya shughuli za maendeleo hususan elimu, afya, maji, barabara na kilimo. Kwa kutokutumia ruzuku hiyo na Halmashauri kuendelea kulalamika na kupiga kelele kwamba wananchi hawachangii shughuli za maendeleo, hii maana yake nini? Kwanini Mkurugenzi wa Halmashauri hii asichukuliwe hatua za kisheria kwa uzembe aliousababisha kwa kuwakosesha wananchi maendeleo na badala yake kuwaamuru Watendaji wa chini kuwachangisha wananchi masikini? Inaashiria nini?

Mheshimiwa Spika, suala la elimu limeongelewa sana na wadau mbalimbali wakiwemo Wabunge. Kwa kweli bila elimu hatuwezi kufika popote. Kumekuwepo na tatizo la muundo wa utawala katika ngazi ya Mkoa, ambako katika kuunda Sekretarieti ya Mkoa, Idara ya Elimu ipo katika kundi moja na afya, ustawi wa jamii, michezo/utamaduni na vijana. Kwa mujibu wa shughuli za Klasta hii anayopewa raslimali au fedha ni Mkuu wa Klasta. Yeye ana mamlaka ya kupanga vipaumbele vyake hapa kwa namna yoyote kama Mkuu wa Klasta, anaamua kupanga anavyotaka na kuacha vipaumbele vya elimu kwa kuwa siyo vyake. Maana yake ni kuendelea kuididimiza elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili kwa kiasi kikubwa limepelekea ugumu kwa Idara ya Elimu hasa kwa Mkoa wa Singida kushindwa kutembelea Shule kwa kuwa haipewi vitendea kazi vya kutosha, na kwa maana hii itabidi Idara hii ipewe kwa hisani ya Mkuu wa Klasta. Kwa kuwa miaka minne iliyopita, TAMISEMI waliahidi elimu itakuwa ni Idara inayojitegemea na *REO* atakuwa ni Mkuu wa Klasta ya Elimu, vivyo hivyo kwa afya Mkoa na kadhalika. Lakini mpaka leo hii tumefika muda wa bajeti na TAMISEMI haijaeleza chochote kuhusu kutekeleza ahadi hii. Sasa Idara ya Elimu iendelee kutotembelea shule na kujionea matatizo yanayozikabili shule zetu? Ningeomba

TAMISEMI ifanye juhudi za ziada ili kutenganisha majukumu haya kwa mustakabali wa elimu ya Taifa letu na ufanisi wa Idara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa fedha na matumizi yake linategemea uimara wa Madiwani na uelewa wa masuala ya mahesabu na thamani ya vitu *(value for money).* Kwa kuwa Bunge lina Kamati za Kudumu za Bunge zikiwemo *"Oversight Committee"* ili kuona jinsi pesa za Serikali zinavyotumika, miongoni mwa Wajumbe kwenye Kamati za Fedha ni Wabunge wa Viti Maalum, lakini inapofika kwenye Halmashauri, Wabunge wa Viti Maalum wanazuiliwa kuingia kwenye Kamati ya Fedha, lakini Madiwani wa Viti Maalum wao wanaingia kwenye Kamati hii. Ili kuwa na *access* ya kudhibiti ubadhirifu wa fedha za Serikali, ningeshauri kanuni ziangaliwe upya ili Wabunge wa Viti Maalum nao waruhusiwe kuingia kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata wasaa huu ili kuchangia hoja hii kwa maandishi. Ni wazi na kweli kulingana na umuhimu wa shughuli nyingi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ndani ya nchi hii kumekuwa na mipango mingi, sera nyingi na maazimio mengi, lakini ufanisi na utekelezaji wake umekuwa wa chini kabisa au haupo na matokeo yake maazimio haya yanabaki kuwa historia na siyo mambo yaliyo na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na viongozi wengi sana ambao hawawajibiki ipasavyo. Hii imesababishwa na watu hawa kuwa karibu na Wakurugenzi na Wakurugenzi kuwaamini sana. Suala hili limepelekea Wakurugenzi hawa kutofuatilia kwa ukaribu hata kazi zao. Hawa Wakuu wa Idara wamekuwa ndio washauri wa Wakurugenzi kama wataalam katika vitengo vyao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, Halmashauri nyingi zimeingia kwenye migogoro mbalimbali na watumishi sababu ya watu hawa kuwa na fitina au chuki binafsi na baadhi ya watumishi na hii imepelekea kupunguza hata morali ya kazi. Wakuu hawa wa Idara wamekuwa hawawajibiki ipasavyo na matokeo yake ndiyo madai ya mapunjo ya mishahara ya watumishi, gharama za uhamisho n akadhalika. Aidha, baadhi ya watumishi wamenyimwa hata fursa ya kupata elimu au kujiendeleza wakiwa kazini na hata baadhi ya wanaopata fursa hizo wanafungiwa mishahara yao, na baadhi yao wamefuata taratibu, sheria na kanuni na leo hii wanapaswa kulipwa haki zao. Je, kwa hili Afisa huyu Serikali inamchukulia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya walimu wamepandishwa vyeo na mpaka wanastaafu hawajawahi kupata stahili zao za vyeo vipya walivyopewa na wanapoendelea kufuatilia, bado Wakuu hawa hawapo tayari kutoa maelezo yenye mshiko. Sasa Serikali iangalie wahusika hawa wanaosababisha hasara kwenye Halmashauri zetu ili

wawajibishwe ipasavyo, na hawa walionyimwa stahili zao, basi walipwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la huduma kwa wazee na walemavu limesahaulika kabisa. Kila mara suala hili limekuwa likizungumzwa bila mafanikio. Sasa Serikali ifanye utaratibu mahsusi wa kuwapatia watu hawa huduma muhimu za afya kama sehemu ya stahili zao kikatiba na kama binadamu walio hai.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ufuatiliaji na usimamizi wa mirathi. Katika Jimbo langu kuna watu wamehangaishwa sana na suala hili kwa kutokuwa na aidha uelewa bayana juu ya jambo hili au ukiritimba wa kutosaidiana na wajane kuwapa taarifa au nyaraka muhimu kwa ajili ya kufuatilia jambo hili. Inasikitisha kuona hata wengine ni watumishi katika Idara zetu za juu au wengine ni viongozi. Naiomba Serikali sasa kufanya maamuzi ya wazi aidha kwa kuwapatia elimu tosha wale wanaoshughulikia masuala haya ya mirathi au kupunguza mwenendo mzima wa ushughulikiaji wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, taratibu za Mahakama ziwe huru na wazi na pia sheria ziangaliwe upya hasa sheria ya kimila, sheria za kidini na Sheria za Mirathi ya Mahakama kama mhusika hakuwa muumini wa dini husika au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie masuala haya niliyoyaeleza kwa ukaribu sana kwani yanahusu nchi yetu nzima na siyo Jimbo la Biharamulo Magharibi tu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Viwanda kwa kuanzisha kiwanda cha kusindika ngozi na kutengeneza viatu *(SIDO)* hapa Dodoma. Hii itawaletea wafugaji faraja ya kuwa na uhakika wa mauzo ya mifugo yao pia kuwapa kasi zaidi ya ufugaji. Pia inatoa mafunzo ya bure. Hii ni kuonyesha wazi Ilani ya Chama chetu (CCM) kwa kuweza kuwahamasisha vijana kuweza kujiajiri wenyewe. Naiomba Wizara ifanye jitihada za makusudi za kuendeleza viwanda kama hivyo vienee Tanzania nzima ili kuwapa urahisi wafugaji wasisafirishe ngozi kutoka Mkoa hadi Mkoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Wizara na Serikali kwa jumla kuvifufua viwanda vyetu, pia kutafuta wafadhili waje wawekeze kwa kuweka viwanda vya matunda ili bidhaa kama *jam, juice* na achari na matunda ya makopo tusiagize toka nje. Pia itawasaidia wakulima wetu kupata soko la uhakika kwa sababu Tanzania tunalima matunda aina nyingi. Ajira pia zitaongezeka kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na ununuzi wa vifaa. Hilo ni jambo la msingi sana lakini bandarini hapo kuna vifaa kama matagi ya kisasa, lakini vifaa hivyo havifanyiwi ukarabati kwa wakati pia wakati wa kufanyiwa ukarabati huo hawashirikishwi kikamilifu wale wafanyakazi wanaovitumia kila siku vyombo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara wakati vinapoagizwa vyombo vipya wachaguliwe wafanyakazi wale watakaovifanyia kazi na wenye fani hiyo kwenda kupata mafunzo ya kutosha kujua kuviendesha vyombo hivyo kwa makini na kuepuka kufundishana wenyewe na kusababisha ajali kwa kutokuwa na ujuzi wa uhakika. Naomba wapatiwe mafunzo hayo hata kama nchi ya karibu kama Kenya kwa sababu kule kuna chelezo, pia vyombo kama hivyo viko muda mrefu na kuna wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata fursa hii ili niweze kutoa mawazo yangu katika hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee juu ya tofauti za kimaendeleo zilizopo baina ya Mikoa hapa nchini na jinsi Serikali inavyogawanya raslimali za maendeleo katika Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida ni Mkoa kati ya Mikoa ya mwisho kimaendeleo katika nchi yetu. Cha kusikitisha ni kwamba Serikali haionyeshi nia ya dhati ya kupunguza pengo la kimaendeleo katika Mikoa yetu. Katika mgawanyo wa bajeti ya maendeleo kwa Mikoa katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mkoa wa Singida ni wa pili kwa kupewa mgawo mdogo ikizidi Mkoa wa Lindi pekee. Ikiwa Mikoa ya Singida na Lindi ni ya mwisho kwa umasikini na ndiyo inayopewa fungu dogo zaidi la maendeleo, iko wapi nia ya Serikali ya kuikwamua Mikoa hii kimaendeleo?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa majedwali yaliyoambatanishwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkoa wa Singida pia umeendelea kutengewa fedha kidogo zaidi katika mfuko wa barabara katika miaka sita mfululizo kutoka mwaka 2005/2006. Kwa mtindo huu, Mkoa wa Singida unatarajiwa kujikwamua kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Singida inaendeshwa kwa matakwa ya Mkurugenzi na siyo kanuni za Halmashauri. Bajeti ya Wizara ya TAMISEMI katika mwaka huu wa fedha, inajumuisha jumla ya shilingi bilioni 29 ambazo hazikujadiliwa hata kipengele kimoja wakati wa kikao cha bajeti ya Halmashauri. Imekuwa ni kawaida kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hii kutokuwapatia Waheshimiwa Madiwani makabrasha yatakayojadiliwa katika vikao husika siku tano kabla ya kikao kama kanuni zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, Madiwani hukuta wameandaliwa makabrasha Mezani mwao asubuhi ya kikao husika na baada ya kikao hicho Madiwani hukatazwa kuondoka na makabrasha yao mara baada ya kikao. Hivi itawezekana vipi kufuatilia miradi mbalimbali iwapo hawabaki na kumbukumbu yoyote?

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilipitishwa kwa kupiga kura (kuwahoji) Waheshimiwa Madiwani bila hata kufungua ukurasa moja wa

kabrasha. Kama ilivyo desturi, Madiwani wengi ni wa Chama cha Mapinduzi, waliipitisha bajeti ya shilingi bilioni 29 bila hata kujali kilichomo ndani yake. Jambo hili tulilifikisha kwa Waziri wa TAMISEMI na *RAS* wa Singida kwa barua, lakini Serikali inayojifanya sikivu haikujali malalamiko hayo.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilipata Hati yenye Shaka. Lakini cha kushangaza, katika kikao cha Halmashauri, Mkurugenzi alilieleza Baraza kuwa Halmashauri yake ilikuwa imepata Hati Safi. Tulipowaeleza Waheshimiwa Madiwani juu ya ripoti ya *CAG*, Madiwani wa CCM waliamua kumwamini Mkurugenzi na siyo ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa TAMISEMI afuatilie kwa ukaribu jinsi ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Singida inaendeshwa ukizingatia kuwa Madiwani walio wengi ni wa elimu ya Darasa la Saba na hivyo kuathiri uwezo wao wa kujadili masuala ya msingi ikiwemo bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER L. M. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia angalau kwa maandishi kuhusu Bajeti ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, napenda kujielekeza zaidi kuhusiana na hali ya njaa kwa mwaka huu ambapo maeneo mengi ya nchi yetu hususan ukanda wa Ziwa Victoria kwenye Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mwanza ambapo hapajapatikana chakula cha kutosha. Nafahamu kuwa Shinyanga kuna maghala ya chakula, lakini maghala hayo yanategemea kuletewa nafaka kutoka maghala yaliyoko Kusini mwa nchi yetu pamoja na Dar es Salaam. Napenda kushauri kuwa Serikali ihakikishe chakula cha kutosha kinapelekwa kwenye maghala hayo ya Shinyanga mapema ili kiweze kuwafikia kwa urahisi wananchi pale kitakapotakiwa kugawiwa. Hata hivyo, kuna dalili ya wafanyabiashara wasio waaminifu wameanza kuvusha chakula kidogo kilichopatikana katika maeneo haya kukisafirisha kwenda nje kwenye nchi jirani ya Kenya kwa njia za panya. Tunaomba Serikali ifanye kila iwezalo kuidhibiti hali hiyo hadi hapo tutakapokuwa tumevuka kutoka kwenye janga hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu katika Sekta ya Uchukuzi ni ukosefu wa reli ya uhakika kutoka Dar es Salaam kwenda bara. Sina hakika kama kuna njama ya makusudi ya kuiua reli inafanywa na wafanyabiashara wa barabara ili isifanikiwe, lakini reli ndiyo njia muhimu ambayo inaweza kupunguza gharama katika kusafirisha bidhaa kwa Mikoa ya bara, lakini kwa jinsi inavyosuasua, kwa hakika inafanya watumiaji wa vifaa vya viwandani na kutoka nje waliyoko kanda ya Ziwa wawe na maisha ya ghali sana.

Mheshimiwa Spika, pia abiria wanaotegemea reli ni wale wanaoishi kwenye maeneo ambapo barabara hazifiki. Sasa wafanyeje? Hata hivyo, reli ya kati pia

inahitajika sana kwa biashara na uchumi wa nchi za ukanda wa Maziwa Makuu. Nasikitika kusema kuwa Tanzania tumeshindwa kabisa kuitumia vyema fursa hii tuliyopewa na Mungu.

Mheshimiwa Spika, sasa wananchi wamechoka kusikia mipango tu ya kwenye karatasi ambayo haitekelezwi kwa vitendo ya kuifufua na kuimarisha reli ya kati. Nahitaji maelezo ya kutosha kwanini reli ya kati haiamki?

Mheshimiwa Spika, Madiwani ndio wasaidizi wa karibu sana wa Wabunge. Hata hivyo posho wanazolipwa Madiwani wa Tanzania ni ndogo sana kiasi cha kufanya wasifanye kazi zao kwa ufanisi. Naomba Madiwani warekebishiwe sheria ili nao walipwe mishahara kama ilivyo kwa Wabunge. Madiwani kwa mazingira ya kazi zao, wanahitaji sasa vyombo vya usafiri ili kuwafikia wananchi ambao ufahamu wao na uelewa juu ya haki zao umeongezeka sana. Wananchi wanahitaji Madiwani wachacharikaji na wanaofuatilia shughuli za maendeleo na huduma za jamii kwa karibu. Bila usafiri na kuwaboreshea mishahara na posho, itakuwa vigumu kufanya kazi yao vema. Vinginevyo hata wale Madiwani wazuri watakuwa wanaachwa wakati wa uchaguzi kwa kushindwa kuwafikia wapiga kura wakati siyo kosa lao. Naomba sana suala hili la maslahi ya Madiwani liangaliwe upya ili Madiwani wetu waweze kuendana na mahitaji halisi ya jamii kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ili uchumi wa Tanzania uweze kukua na watu wengi waweze kuboresha maisha, ni muhimu sana Serikali ikajielekeza kwenye kuimarisha uchumi wa akina mama na vijana. Pesa inayotengwa na Serikali Kuu kupitia Mfuko wa Maendeleo na Vijana na kupitia Serikali za Mitaa, bado ndogo mno kuweza kuleta matokeo chanya katika jamii ya Watanzania milioni 40 sasa.

Mheshimiwa Spika, hata tatizo la ajira linalopigiwa kelele na Wabunge wengi lingeweza kupungua iwapo Serikali ingeendelea kuanzisha na kuimarisha makundi ya kujitegemea ya vijana na wanawake na kuyapa maarifa zaidi ya ujasiriamali na ubunifu. Ina maana makundi haya yangeweza kushiriki kiushindani ndani na nje ya nchi na hivyo kuongeza kasi ya uchumi. Taasisi kama vile *SIDO* na *VETA* ni za muhimu sana katika dhana hii ya kuwawezesha akina mama na vijana ambao ni zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wote. Hivi kwanini Serikali isiiangalie njia hii ya mkato ya kupunguza umasikini katika jamii?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nisisitize juu ya dhamira ya Serikali ya kuupatia mji wa Bariadi maji ya kutosha kutoka Ziwa Victoria. Mpango huu uko katika ahadi za Rais. Lakini umuhimu wa mpango huu ni kuwa utatoa huduma ya uhakika kwa wananchi wa Mkoa mpya wa Simiyu pamoja na vijiji vingi ambapo mradi huu utapitiwa. Pia tunaomba Halmashauri za Wilaya zisisitizwe kutenga fedha ya kutosha ili kujenga mabwawa kwa ajili ya binadamu na mifugo ili kupunguza kero kubwa iliyopo hususan katika Wilaya za Busega, Bariadi, Meatu na Maswa. Lakini pia fedha inayotengwa kwa kazi hiyo ya maji ni muhimu ikasimamiwa vema ili kuwe na kazi inayoendana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi hoja ya Waziri Mkuu kuhusu makadirio ya matumizi ya Ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ambayo ninaiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuzindua Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano Kati ya 2011/2012 hadi 2015/2016, Mpango ambao ni utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na takwimu kuonyesha kuwa uchumi wa nchi yetu unaendelea kukua, ukweli unabaki pale pale kwamba ukuaji huo bado hauonekani kuwanufaisha wananchi walio wengi hasa waishio vijijini (wakulima, wafugaji na wavuvi). Hii ni kutokana na ukweli kwamba Sekta ya Kilimo (kilimo, ufugaji na uvuvi) ambayo inategemewa na zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania waishio vijijini (kwa maana ya ajira na usalama wa chakula) sekta hiyo imekuwa ikikua kwa kasi ndogo sana ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu vijijini. Ukuaji huo mdogo umechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo ukame, kuyumba kwa bei ya mazao asilia katika Soko la Dunia na matumizi ya zana duni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sekta ya Kilimo ndiyo inabeba watu wengi, jitihada za kukuza uchumi lazima zilenge huko kwa kuleta mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi vijijini kwa kukifanya kilimo kiwe na tija. Sasa hivi sekta hii imegubikwa na utitiri wa kodi ambazo hazina mvuto kwa wawekezaji. Angalia *Towards a Tanzania Green Revolution: Policy Measures and strategies, summary of the Reports of the TNBC working Group, TNBC (2009).*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ikae kwa wadau katika sekta hii ili kodi hizo zijadiliwe kwa lengo la kuziondoa, *otherwise*, kauli mbiu ya Kilimo Kwanza itakuwa kuna maneno matamu yasiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mikopo kwa wakulima kupitia dirisha la kilimo pale *TIB* na Benki ya Maendeleo ya Kilimo inayotarajiwa kuanzishwa. Serikali itoe tamko ni lini Benki hiyo ya Maendeleo ya Kilimo itaanzishwa?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nina wasiwasi kama kweli ujio wa benki hiyo utajibu taswira inayomzunguka mkulima, mfugaji na mvuvi kwamba wakulima, wafugaji na wavuvi wanaokopesheka ni wachache. Masharti ya mikopo yasipolegezwa, wengi wao hawatakidhi masharti ya mikopo ya benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hati za ardhi za kimila bado hazijatambuliwa na mabenki mengi hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Pembejeo ambao bado umeendelea kudai *Certificate of Title* kama *Security* kwa wakulima wadogo wanaotafuta mikopo ya matrekta.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kilio cha wakazi wa mamlaka ya mji mdogo wa Bariadi cha maji safi na salama. Mji mdogo wa Bariadi na viunga vyake una idadi kubwa ya watu, idadi ambayo inaongezeka kwa kasi. Bwawa la Mto Bariadi limejaa tope *(Silitation)*. Chujio la maji linalojengwa pale Bariadi halitakuwa na maana kutokana na ukosefu wa maji. Ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo sugu la maji pale Bariadi na vijjji vinavyouzunguka mji huo ni kuyavuta maji kutoka Ziwa Victoria. Ziwa hilo lipo umbali wa kilometa 60 kutoka Bariadi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 aliwaahidi wananchi kuwa Serikali yake itaangalia uwezekano wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria na kuyaleta Bariadi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha Mkoa mpya wa Simiyu na Wilaya mpya ya Itilima na Budega. Taratibu za kukamilisha uanzishwaji wa maeneo hayo mapya ya utawala zikamilishwe haraka. Aidha, Serikali iajiri Watendaji wa Kata na Vijiji kwa maeneo mapya ya kiutawala yaliyoanzishwa. Sasa hivi maeneo mengi hayana Watendaji na wengi waliopo wanakaimu tu nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Naomba nijielekeze katika maeneo machache yafuatayo katika mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la viwanda na biashara napenda kusema kwamba ni budi tufufue viwanda vyote kwa vipaumbele kutegemea upatikanaji wa malighafi. Viwanda vya nguo ni muhimu sana kwa kuongeza thamani ya pamba yetu nau sindikaji wa matunda ni jambo la muhimu sana katika kuongeza thamani ya matunda yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uhaba wa umeme ni janga la kitaifa. Uchumi umeathirika sana kwa kipindi kirefu. Naomba Serikali ikemee kwa nguvu zote wale wanaopotosha umma kisiasa kwa mambo yanayoathiri uchumi wa nchi. Tatizo kubwa la umeme limeongezwa makali kutokana na mijadala iliyokuwa ya kisiasa kwa manufaa binafsi. Tungefuata ushauri wa *TANESCO* kununua jenereta za *Dowans* tungepunguza sana ukali wa tatizo lililopo leo. Juhudi za Serikali zilidhoofishwa na siasa potofu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, naomba Serikali ikubali kupandisha daraja barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya hadi Milingano – Mashewa. Barabara hii inahudumia Majimbo manne katika Mkoa wa Tanga. Majimbo hayo ni Mlalo, Lushoto, Bumbuli na Jimbo la Korogwe Vijijini. Kwa hadhi ya barabara hiyo, Mkoa uliomba ipandishwe daraja isimamiwe na *Tanroads* Mkoa wa Tanga. Naomba Serikali isimamie ombi hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. TAUHIDA C. G. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Rais wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa na wananchi kwa kura nyingi. Nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania. Napenda pia kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuteuliwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya vijana wote wa Tanzania, hususan Zanzibar, nashukuru kunipatia fursa hii ya kuchangia. Kwanza napenda kuipongeza hotuba ya Waziri Mkuu ambayo ni nzuri, iliyokamilika na inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imekuwa na mipango mizuri na mikakati mizuri inayojiwekea. Jitihada za Serikali yetu zimekuwa zikirudishwa nyuma na watendaji wachache wasioitakia mema Serikali yetu ya Tanzania, wapo kwa maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeazimia mambo mengi katika kutatua kero za wananchi, mfano, kero za maji, barabara, umeme na kadhalika. Napenda kuishukuru Serikali yetu kwa kujali wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa kabisa, fedha zinazotolewa na Serikali kupelekwa Halmashauri hazitumiki kama Serikali ilivyokusudia. Mara nyingi fedha zinatumika kwa masuala ya watu na siyo wananchi walio wengi. Watendaji husahau lengo la Serikali katika kupunguza na kuondosha kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu katka ukurasa wa 17 sehemu ya 18, Mfuko wa J.K hadi kufika tarehe 30 Desemba, 2010 imetolewa shilingi bilioni 47.14 kwa ajili ya mikopo kwa wajasiriamali. Serikali ichunguze kwa kina kwani fedha haziendi kwa walengwa bali wanaopatiwa ni wale wanaojulikana na Watendaji au wanaoweza kuhonga Watendaji hao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa chini wanashindwa kuamini kama mikopo hii imeazimwa kwa ajili yao. Watu wa vijijini wasiokuwa na uwezo siyo rahisi kupatiwa mikopo hii kwani hawajui imetoka wapi na vipi.

Mheshimiwa Spika, shughuli nzima za Serikali zinakosa usimamizi wa utekelezaji wa malengo ya Serikali vizuri kutokana na baadhi ya watendaji wabovu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Wizara ya TAMISEMI iisaidie Serikali katika sehemu muhimu ya kuajiri Watendaji wenye sifa za kutosha katika Halmashauri waliyokuwapo. Katika ngazi ya Mkurugenzi, Mhasibu, Injinia; Watendaji hawa hi muhimu katika kuendesha Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo ya kiutendaji kwa baadhi ya Watendaji wa Halmashauri. Kwa masikitiko, Watendaji hao hukuta wamehamishiwa Halmashauri nyingine na ugonjwa huo na matatizo hayo kuhamia huko. Huu siyo ufanisi mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe Serikali kupitia TAMISEMI haiwafumbii macho wasiowajibika na wasiojua majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yetu kupitia Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na yenye lengo la kuondosha kero za wananchi wake, na kuitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi iendelee kutawala.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu mia kwa mia.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Bajeti katika Serikali za Mitaa inajadiliwa na kupitishwa wakati Wabunge wako Bungeni?

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe tamko la kufuta tozo ya Sh. 200/= katika Mfuko wa *Cotton Development Trust Fund (CDTF)* na badala yake ibaki Sh. 15/= kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Hospitali ya *DDH* Bunda imekuwa ikitoa mchango mkubwa sana kwenye Sekta ya Afya. Lakini jitihada hizo zimekuwa zikikwama kwa baadhi ya changamoto zinazoikabili Hospitali hiyo. Moja ya changamoto hizo ni ukosefu wa madaktari na wauguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya *DDH* imekuwa ikipokea wanafunzi wengi wanaochukua taaluma ya udaktari, wanaokwenda kufanya mafunzo kwa vitendo, ambao wanatoa mchango mkubwa sana kwa kutoa huduma ya matibabu. Lakini pindi wanafunzi hao wanapomaliza mafunzo, huajiriwa sehemu nyingine. Kwa nini Serikali isiwapange Madaktari hao kwenye Hospitali hiyo pindi wanapowaajiri, ukizingatia tayari wameshazoea Hospital hiyo.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya *DDH* imepata msaada wa vifaa vya kisasa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi kutoka Marekani. Lakini cha kushangaza vifaa hivyo vimekaa zaidi ya miaka kumi havijatumika na wagonjwa wengi Mahututi husafirishwa kwenye Hospitali ya Bugando Mwanza kwa ajili ya kupelekwa kwenye chumba cha wagonjwa mahututi na wengine kufia njiani, huku *DDH* ina chumba cha wagonjwa mahututi na vifaa vya kisasa. Tatizo ni Madaktari na Wauguzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wauguzi na madaktari wa kutosha ili chumba hicho kiweze kufanya kazi na kuokoa maisha ya wakazi wa Bunda wanaofia njiani wakipelekwa Hospitali za Bugando. Hospitali ya *DDH* haina hata Daktari bingwa mmoja, hivyo wagonjwa wanaohitaji madaktari bingwa wengi hupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, je, mchakato wa Hospitali ya Manyamanyama kufanywa Hospitali ya Wilaya umeishia wapi? Tayari maombi yameshafika, na Hospitali hiyo

imekuwa ikitoa huduma hadi kwa wagonjwa wanaotoka kwenye Wilaya jirani, lakini mchakato wa kuifanya Hospitali ya Wilaya unasuasua mbali ya kuleta maombi zaidi ya miaka mitano, na ina vigezo vyote vya kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na kuhudumia wagonjwa wengi, tunaomba Hospitali hiyo iongezewe fungu la dawa za ziada, kwa kuwa imekuwa ikiishiwa madawa na vitendea kazi mapema kutokana na mgao mdogo wanaoupata ukilinganisha na huduma ya watu wengi wanayotoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa heshima na taadhima kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara zilizo chini ya ofisi hii kwa kuwasilisha bajeti makini kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda (Mb) kwa hotuba yake nzuri. Pia nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Waziri wa Nchi, Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu (Waziri wa Nchi, Uwezeshaji na Uwekezaji), Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika (Waziri wa Nchi, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa) kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea na hoja kuhusu hotuba hii, binafsi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ila kuna baadhi ya upungufu ambao ni muhimu urekebishwe ili kuleta ufanisi juu ya utekelezaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, binafsi kwa niaba ya wananchi wa Tarime, familia yangu hasa mke wangu Magreth Nyambari Nyangwine na watoto wangu Bhoke Nyambari Nyangwine na Bernard Nyambari Nyangwine. Nitaijadili hoja hii kwa kuangalia vipengele vya kilimo, ufugaji, maji, maafa, elimu, rushwa na kukosekana kwa haki, afya, vijana na ajira, miundombinu, uporaji wa rasilimali za Taifa letu, ubinafsi, chuki na tamaa, kukosekana kwa maadili katika Taifa letu, Muungano, viwanda, biashara na masoko, usafiri wa reli, bandari, anga na utalii.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo, bila shaka na ukweli uliodhahiri ni kwamba sekta ya kilimo ndio njia pekee ya kumkomboa Mtanzania wa kipato cha chini. Naipongeza Serikali kwa kulijua hilo. Katika nchi yetu, kilimo kinaongoza kwa kuwapatia watu binafsi shughuli halali ya kujikimu kimaisha, hivyo hatuna budi kukitilia mkazo. Serikali ihakikishe kuwa inawasaida wakulima hasa wa Jimbo la Tarime na maeneo mengine ya nchi kwa kuhakikisha kuwa inawapatia pembejeo, mbolea, dawa na mbegu za kisasa zinazoendana na mazingira ya eneo husika. Kwa mfano, katika Wilaya ya Tarime, mazao kama vile mahindi, mihogo, mtama, ulezi, maharage na ndizi ni muhimu yakatiliwa mkazo kwani yanatumika kama chakula na wakati huohuo yanatumika kama mazao muhimu ya biashara kwa kuyauza nchini Kenya. Mazao kama vile kahawa, tumbaku, chai na hata bangi ambayo hustawi kinyume cha sheria husaidia kwa kiasi kikubwa kuliingizia fedha eneo husika. Kitu cha msingi hapa ni kuangalia

namna ya kuwasaidia wakulima wa Tarime ili waweze kunufaika na kilimo cha mazao ya aina mbalimbali wanayolima.

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa katika Wilaya ya Tarime kuna msimu wa mvua mara mbili kwa mwaka. Kuna msimu mkubwa wa mwezi Februari hadi Mei. Huu ni msimu wa kupanda kila aina ya zao. Pia kuna msimu mdogo wa Oktoba hadi Novemba. Huu ni msimu mdogo lakini nao husaidia kustawisha mazao ya chakula na ya msimu kama vile mahindi, viazi mviringo, viazi vitamu, karanga, nyanya, vitunguu, mihogo, mtama n.k. Ili mkulima wa Tarime aweze kunufaika kwa kilimo, Serikali haina budi kupeleka vocha za pembejeo mara mbili kwa mwaka badala ya utaratibu wa sasa wa kupeleka mara moja tu kwa mwaka. Pia Serikali ihakikishe kuna soko la mazao yote yanayolimwa Tarime badala ya wakulima kupeleka mazao Kenya.

Mheshimiwa Spika, ufugaji, ifahamike wazi kuwa nchi yetu ya Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mifugo mingi katika Bara la Afrika. Inashikilia nafasi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi katika Afrika. Kinachonisikitisha sana ni kuona jinsi mfugaji anavyonyanyasika katika ardhi yake aliyompatia Mwenyezi Mungu. Mfugaji wa sasa wa Tanzania anakabiliwa na changamoto za kukosekana eneo la malisho, upungufu wa maji, upungufu wa majosho, mbung'o pamoja na kukosekana kwa uhakika wa soko la bidhaa yake.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Tarime ambayo ina jamii ya wakulima na wafugaji, Serikali imesahau kabisa wafugaji wa maeneo ya Komaswa, Manga, Kibasuka, Gibaso, Gong'ora, Masanga, Ketawasi, Msangucha pamoja na Kegonga. Naitaka Serikali ihakikishe kuwa inatenga eneo la hifadhi ya Serengeti kwa ajili ya wakulima wa Tarime. Pia Serikali ihakikishe kuwa inachimba malambo na mabwawa katika Kata zote 30 za Wilaya ya Tarime ili kuhakikisha kuwa kuna uhakika wa maji ya kunyweshea mifugo katika Wilaya ya Tarime. Pia Serikali isaidie kuweka Kiwanda cha Nyama mpakani mwa Tanzania na Kenya (eneo la Sirari) ili kuwahakikishia wafugaji uhakika wa soko, pia isaidie kuweka Kiwanda cha Maziwa Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Spika, suala la maji safi na salama ni muhimu sana kwa afya za wanadamu. Kwa bahati mbaya katika Wilaya ya Tarime suala hili limekuwa ni kama ndoto za mchana. Wakurya wa Tarime tangu enzi za mababu hadi leo hii hawajawahi kubahatika kupata maji safi na salama kwa afya zao. Inasikitisha na kushangaza sana Mheshimiwa Spika. Naitaka Serikali ihakikishe kuwa inachimba visima vya uhakika kwa kila kijiji katika Wilaya ya Tarime. Hebu tuache ahadi na porojo nyingi, tuwasaidie raia wa nchi hii kwa kuwapatia huduma bora ya maisha kwa kuwapatia vitu muhimu kama maji. Hii itawezekana kabisa kwa kuyakumbuka maeneo yaliyosahaulika kiuchumi katika nchi yetu kama vile Mkoa wa Mara, Rukwa, Lindi, Kigoma, Mtwara n.k. Tukiamua tunaweza sasa tuamue.

Mheshimiwa Spika, maafa, napendekeza kwa dhati kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kuwa inaweka Ofisi za Maafa katika maeneo ambayo yanapata athari za maafa moja kwa moja. Kwa mfano, katika Wilaya ya Tarime katika Kanda ya Ziwa ni Wilaya yenye maafa ya kila aina hususan vita vya ukoo, ujambazi, njaa na athari za kitamaduni.

Binafsi napendekeza Serikali ihakikishe kuwa inasaidia wananchi wa Tarime kwa kuwapelekea Ofisi ya Maafa Wilayani mwao. Ofisi hii itakuwa ni msaada mkubwa kwa waathirika wa maafa ya asili na yale yanayosababishwa na wanadamu katika Wilaya ya Tarime. Pia nasisitiza kupatiwa msaada wa chakula katika Kata za Komaswa, Manga, Kibasuka, Nyarokoba, Nyangoto, Kemambo pamoja na Kata ya Gorong'a. Msaada wa haraka wa chakula katika eneo hili la Tarime Magharibi utasaidia sana kuongeza nguvu kazi na hivyo kuleta ufanisi katika shughuli za uzalishaji mali katika Wilaya yetu ya Tarime. Naamini kwa dhati kuwa Serikali yetu ni sikivu na isikie kilio cha wakazi wa Tarime.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, katika nchi zinazoendelea na hata zile zilizokwishaendelea, ni la lazima katika kujileta maendeleo. Katika sekta hii ya elimu, napenda kwanza kukumbusha matokeo ya Kidato cha Nne ya mwaka 2010. Matokeo haya yanahitaji fikra mpya, mtazamo mpya pamoja na msimamo mpya. Eneo la kuanzia ili kufanikisha suala hili ni Walimu. Walimu wengi wanaonekana wamekata tamaa na wanatamani watoke kwenye Sekta ya Elimu na kukimbilia sekta nyingine kwa sababu wanavunjwa moyo na mazingira magumu ya kufanyia kazi hasa kukosekana kwa nyumba katika maeneo ya vijijini hususan katika Shule zetu za Kata. Pia mfumo wa malipo ya posho na maslahi yao bado ni duni. Napendekeza bajeti hii pamoja na mambo mengine katika sekta hii ya elimu itatue tatizo la mazingira magumu ya Walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kuwa Shule zetu za Kata zinapata umeme. Umeme utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapatia wanafunzi wetu nafasi nzuri ya kujisomea na hivyo kuongeza ufanisi katika masomo. Shule hizi zijengwe hosteli pamoja na mabweni, vitabu, vifaa vya maabara na vitu vingine vya kufundishia ni muhimu vifuatiliwe na kuhakikisha kuwa vinapatikana na vinatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali kupitia Wizara ya Elimu iangalie upya suala la Kamati ya kupitia vitabu vinavyofaa kutumika shuleni yaani *EMAC (Educational Materials Approval Committee).* Kamati hii iliundwa na Serikali kwa nia njema lakini kutokana na usaliti wa Watendaji na suala zima la rushwa, imeshindwa kutekeleza ipasavyo wajibu wake. Matokeo yake Watendaji wa Kamati wamebaki wakijinufaisha kwa rushwa na hatimaye wameabudu wachapaji wa vitabu toka nje ya nchi huku wakiwaacha wachapaji wazalendo wakitaabika kwa kukataa kupitisha vitabu vyao. Hiyo ndiyo hali halisi inayochangia kuporomoka kwa elimu katika nchi yetu. Ubinafsi, rushwa, tamaa pamoja na uzembe, ni vitu vinavyochangia kukosekana kwa vitabu mashuleni, tuzame zaidi kifikra.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa na kukosekana kwa haki. Kwa ruhusa yako, naomba kuliweka wazi jambo hili kuwa rushwa imekithiri katika nchi yetu kuanzia ngazi ya Balozi, Kitongoji, Kijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Rushwa inasababisha kukosekana kwa haki hasa kwa watu maskini wasio na chochote kwani bila kuwa na mali au utajiri wa kutoa rushwa, ni dhahiri kuwa uonevu hutendeka kwa yule asiyetoa rushwa. Hili halihitaji ushahidi, angalia *Traffic,* angalia Polisi, angalia Mahakama zetu, angalia Halmashauri zetu, n.k. Kila sehemu rushwa imekithiri na lengo

la rushwa hii ni kuhakikisha kuwa maskini hapati haki. Pia rushwa hurudisha nyuma maendeleo ya nchi. Watendaji wetu Serikalini ni wala rushwa. Kwanza, Watendaji wengi katika Wizara zetu wamejaa uroho, ubinafsi, tamaa na hata kukosekana kwa uzalendo. Hali hii isipokemewa, tutajenga Taifa la ajabu, chondechonde tujirekebishe!

Mheshimiwa Spika, suala la afya, naomba nitumie nafasi hii kuisihi Serikali ijitahidi sana kutatua matatizo ya msingi yanayoziandama hospitali zetu za Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya, pamoja na Zahanati tulizo nazo. Matatizo ya msingi ni ukosefu wa dawa, upungufu wa watumishi hususan Madaktari na Manesi, huduma za jamii kama vile ukosefu wa maji, umeme wa uhakika pamoja na posho za Madaktari/Manesi jambo hili husababisha huduma za afya kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo langu la Tarime, Hospitali ya Wilaya ya Tarime ina miundombinu mibovu kwani tangu ijengwe mwaka 1942 na Wakoloni hadi sasa hakuna chochote kilichobadilishwa. Hivyo tunahitaji ofisi ya utawala, uzio, majengo ya kutosha, watumishi angalau Madaktari 30 pamoja na Manesi 200 kwa ajili ya Vituo/Zahanati zetu, pamoja na *ambulance* za wangonjwa nne (4). Baadhi ya Zahanati zetu kama vile Komeswa na Mtana zipandishwe daraja/hadhi na kuwa Vituo vya Afya ili kuharakisha huduma za wananchi Wilayani Tarime. Vituo vya Afya kama vile Muriba, Nyarwana n.k. viboreshwe ili viweze kutoa huduma nzuri ya kuridhisha Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho katika Sekta hii ya Afya ni kuishauri Serikali ihakikishe kuwa inakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ya Kongwa. Hili jambo likifanikiwa ni matumaini ya wananchi wa Mkoa wa Mara kwamba watanufaika na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Chama ambacho muasisi wake anatoka Mkoa wa Mara. Hivyo basi Serikali ifanye hivyo kwa kumuenzi baba wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana lizingatiwe katika ngazi zote, msisitizo uwe elimu ya *VETA* (Ufundi) itolewe katika ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Elimu ya biashara itolewe kutoka ngazi ya *primary*, sekondari, *A level* hadi *Universities*. Hii itasaidia sana walengwa kujua maana ya ujasiriamali. Elimu ya ufundi pamoja na biashara (ujasiriamali) ndivyo vitu pekee vitakavyoweza kupunguza suala la ukosefu wa ajira hapa nchini. Halikadhalika vijana wetu wafundishwe umuhimu wa ujasiriamali na wafundishwe juu ya uzalendo badala ya kukaa kijiweni/vijiweni na kuilalamikia Serikali. Wafahamu wazi kuwa kazi ni uhuru au uhuru na kazi au kazi ni kipimo cha utu. Vijana wetu wajitahidi kufanya kazi kwa bidii huku wakizingatia maneno "Asiyefanya kazi na asile".

Mheshimiwa Spika, binafsi kama kijana, nina wasiwasi juu ya mustakabali wa nchi yetu pamoja na kizazi cha vijana. Nahisi kama tunajenga Taifa la walalamishi na wanung'unikaji. Hebu nitoe wito kwa Serikali kuwa iwaangalie kwa jicho kali wanasiasa uchwara na micharuko wanaowazuia vijana kuwajibika kujitafutia riziki halali na badala yake vijana wanakesha njiani na mabango ya kuikashifu Serikali, tubadilike.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iweke mazingira nafuu/mazuri yatakayomwezesha kijana wa leo aweze kujiajiri badala ya kijana wa leo kuiona nchi yake kama ni jumba la mateso. Kwa kufanya hivyo, msemo huu "Bora Kuzaliwa Mbwa Ulaya Kuliko Kuzaliwa Binadamu Tanzania" ambao ni wa vijana wa leo utafutika akilini mwao, tufikiri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la miundombinu, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuimarisha suala la miundombinu katika nchi yetu. Kazi nzuri zinazoendelea kufanyika za kuimarisha miundombinu hasa barabara za lami ni ushahidi tosha kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kuleta ufanisi katika ngazi ya Kitaifa hususan suala la usafirishaji. Kwa hakika barabara zinazoendelea kuwekewa lami ni nyingi mno. Barabara zinapunguza foleni hasa katika Jiji la Dar es Salaam, mfano barabara ya Kimara – Baruti – Msewe – Chuo Kikuu; Kigogo – Mabibo – Ubungo Maziwa; Tabata Dampo n.k. Kuna barabara nyingine kubwa zimepanuliwa na kufanyiwa marekebisho, mfano barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi zote, suala la miundombinu bora katika Wilaya ya Tarime bado ni kitendawili. Hakuna hata barabara ya lami katika Wilaya hii ukiachilia mbali ile barabara kuu ya Sirari – Makutano – Mwanza. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa barabara ya Nyamwaga inayoanzia Tarime – Mogabiri – Rozana - Kemakorere – Nyarero – Nyamwaga – Nyamongo – Mto Mara kuelekea Serengeti iwekewe lami. Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa Tarime. Pia *Security Road* ya Rorya – Susuri – Kibiterere – Sirari – Gwitiryo – Nyabisaga – Borega – Ganyange – Kimusi – Nyantira – Muriba – Kobori – Itingo – Nyamombara – Mangucha hadi Kegonga nayo iwekewe lami. Hizi zote ni barabara za Mkoa *(TANROAD)*. Pia kuna barabara kama vile Mangucha – Masanga – Masurura – Gibaso – hadi Mrito pamoja na ile itokayo Nyamwaga – Keisangura – Tagare hadi Muriba, nashauri ziwe chini ya *TANROAD* ili kuharakisha maendeleo ya Wilaya ya Tarime. Madaraja ya Kyoruba na Mto Mori yajengwe ili yasaidie kuleta maendeleo kwa wananchi wa Mara/Tarime.

Mheshimiwa Spika, suala la uporaji wa rasilimali zetu hususan madini ni kitu ambacho hakiwezi kuvumilika hata kidogo. Madini ndiyo yamefanikisha kujengwa kwa miji iliyoendelea kokote kule duniani. Inashangaza na kusikitisha kuwa Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa kuzalisha dhahabu lakini bado ni nchi maskini sana duniani. Suala hili lahitaji jicho la kiyakinifu katika kulishughulikia. Mikataba mibovu, kunyenyekea wawekezaji na umbumbumbu wa viongozi wetu ni vitu vinavyopelekea hali hii. Naishauri Serikali iangalie upya sekta hii ya madini ili iweze kulinufaisha Taifa letu. Hebu fikiria Nyamongo wananchi wanateseka kwa umaskini lakini kila siku rasilimali iliyo katika ardhi yao inaporwa na hakuna wanachofaidika nacho, tufumbuke macho.

Mheshimiwa Spika, ubinafsi, chuki, tamaa na usaliti ni vitu ambavyo vinarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Hali hii imesababisha baadhi ya sehemu zimebaki nyuma kwa maendeleo. Viongozi wetu hawalioni hilo. Baadhi ya viongozi wanajipitishia mipango ya maendeleo kwa kuangalia sehemu walizotoka badala ya kuweka Utaifa mbele. Ubinafsi, chuki, tamaa na usaliti ndiyo vitu vinavyosababisha kutokea matabaka

ya maskini na matajiri. Tabaka la matajiri limekuwa kikwazo cha maendeleo katika nchi yetu. Tofauti kati ya matajiri na maskini ni kubwa sana. Kama tunahitaji kujenga Tanzania yenye haki na usawa hatuna budi kupiga vita kwa nguvu zetu zote pengo lililopo baina ya matajiri na maskini. Viongozi wetu walijue wazi kuwa palipo na ubinafsi hakuna uzalendo, palipo na chuki hakuna upendo, palipo na tamaa kuna wizi halikadhalika palipo na usaliti maendeleo hayawezi kupatikana, usaliti hauwezi kuleta Utaifa hata siku, tufikiri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa maadili katika Taifa letu. Uko wapi uzalendo wetu? Iko wapi amani yetu? Upo wapi umoja na mshikamano wetu? Kila siku maandamano! Kila siku matusi kwenye vyombo vya habari! Kila siku migomo! Kila siku watani wangu wa chama kilichoshindwa wanatunga uongo! Wanawaita wafuasi wao kwa jina la Makamanda! Huu ni unafiki unaolifanya Taifa letu likose maadili. Maadili ndiyo yaliyotufanya tufike hapa tulipo. Siku hizi chuki, uongo, unafiki kwa baadhi ya wanasiasa hata Wahadhiri wa Vyuo Vikuu ndiyo wanavyohubiri nchini. Hali hii haiwezi kuvumilika hata kidogo. Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuyafumbia macho masuala haya yote ni kielelezo cha kutowajibika ipasavyo kwa wananchi wake. Naishauri Serikali ichukue hatua madhubuti dhidi ya matendo haya yote yanayochochea kuvuruga maadili ya Taifa letu. Hatuwezi kupandikiza chuki kwa kizazi kijacho kwa lengo la kujitafutia umaarufu na vyeo, tutafakari zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la Muungano, jambo ambalo hadi sasa tunajivunia katika nchi yetu ya Tanzania ni suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hii ni kumbukumbu ya kudumu ambayo tumeachiwa na Waasisi wa Taifa hili. Kinachonisikitisha na kunishangaza ni juu ya suala hili nyeti linavyochukuliwa na Wanasiasa machepele na micharuko kuhakikisha kuwa wanaingiza vijineno neno vinavyoashiria uvunjifu wa Muungano wetu. Tusikubali kuvurugwa kwa umoja wa Taifa letu kwa visingizio vya kero za Muungano. Kero hizo za Muungano zinajadilika na zitapatiwa suluhu ya kudumu lakini hata hivyo kero hizo zijadiliwe na Serikali za pande zote mbili na hatimaye suluhu yenye mantiki ipatikane. Chondechonde viongozi wetu wa Serikali tusiruhusu suala hili nyeti la Muungano kujadiliwa na kila Mwanasiasa, hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Wanasiasa wetu wenye uchu, tamaa na hasa wapenda madaraka hawataki kabisa kuuona Muungano wetu ukidumu, hao wasionewe haya. Wakatazwe hadharani pasipo uwoga wowote. Waitwe, waonywe na kukemewa, hata ikiwezekana waitwe Wahaini. Ifahamike wazi kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ukivunjika ni aibu kubwa kwa Watanzania katika nyuso za Mataifa mengine. Wito wangu ni kuwa Watanzania tuuenzi Muungano wetu kwa hali na mali kwa kuonyesha uzalendo wa hali ya juu sana wa kuipenda nchini yetu ya Tanzania. Watanzania tusikubali kuwapatia nafasi vibaraka wanaopinga umoja na mshikamano wa nchi yetu, Muungano kwanza mengine baadaye.

Mheshimiwa Spika, suala la viwanda, biashara na masoko, nchi yoyote ile haiwezi kuendelea pasipo kujali suala la mauzo ya bidhaa zinazozalishwa katika nchi husika. Aidha, fedha za kigeni haziwezi kupatikana pasipokuwa na bidhaa za kuuza nchi

za nje.  Hivyo, suala la viwanda, biashara na masoko ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa lolote lile. Uwiano wa viwanda, biashara na masoko ya kuuzia bidhaa zetu katika Afrika ya Mashariki na nchi za jirani kama vile Kenya, Uganda bado si nzuri. Hii ni kwa sababu sisi Watanzania tunaagiza kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na zile bidhaa tunazotuma (tunazouza) nje ya nchi.  Hali hii inapelekea fedha yetu kukosa thamani dhidi ya dola (US$) na hata shilingi ya Kenya (KSH).

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri katika Wilaya ya Tarime ambayo ina *Custom* ya Sirari, ina eneo zuri sana la kuanzisha ukanda wa viwanda.  Karibu barabara ipatayo km 8 -10 toka Tarime Mjini hadi Sirari eneo hili lote lafaa kuwa ukanda wa viwanda wa Sirari na kwa bahati nzuri kwenye ukanda huu kuna uwanja wa ndege wa Magena. Ni imani yangu kuwa tukianzisha viwanda vidogovidogo kama vile Kiwanda cha Chai, Kahawa, Juisi, Mvinyo na vinginevyo Wilaya ya Tarime itapiga hatua ya maendeleo na hivyo kuwezesha shughuli ya biashara na masoko kufanyika ndani ya Wilaya na hivyo kuweza kumwinua mkulima. Naishauri Serikali ingalie namna ya kuwasaidia Wakurya wa Tarime ili waweze kujikwamua kiuchumi, tukiamua tunaweza, sasa tuamue.

Mheshimiwa Spika, suala usafiri wa reli, bandari na anga, suala la usafiri na usafirishaji katika nchi yetu limechangia kwa kiasi kikubwa kurudisha nyuma maendeleo ya jamii ya Watanzania.  Kuhusu reli, tunashuhudia mikataba mibovu iliyopelekea baadhi ya reli zetu kukodishwa kwa kampuni ya *RITES* ya India ambayo haikuwa na uwezo hata kidogo. Sitaki kulizungumzia kwa undani suala hili kwani linatia kinyaa ila nataka kuishauri Serikali kuwa tubadilike, tutumie rasilimali tulizo nazo ili kuhakikisha kuwa tunaboresha huduma ya usafiri wa reli ambayo itakuwa ni mkombozi kwa mkulima na wafanyabiashara wa  nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, pamoja na mipango mizuri ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyo nayo ya kuipanua bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Musoma na hata Kigoma bado kuna tatizo la utendaji.  Haiingii akilini kuwa bandari ya Dar es Salaam haiwezi kutunza makontena na matokeo yake makontena hayo hutunza kwenye *warehouse* za Wahindi huku wafanyabiashara wakilipishwa pesa nyingi na Wahindi bila utaratibu maalum.  Huko ni kukosa akili za kufikiri.  Hebu tuishauri *TRA* na *TPA* waache kuwatania wafanyabiashara wa Tanzania. Naishauri Serikali itenge eneo maalum la bandari la nchi kavu la kuhifadhia makontena na hizo fedha ziingie Serikalini ili kukuza pato la Taifa badala ya kukuza pato la matapeli wachache wasioitakia nchi yetu mema.  Tufikiri kwa kutumia bongo za vichwa badala ya kufikiri kwa kutumia njaa za matumbo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu anga, kila wakati naililia *ATC*.  *ATC* imekufa! Imekufa kifo cha mende!  Kwa imani tuliyonayo na Serikali bado naamini itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa ndege za *ATC* zinafanya kazi.  Binafsi nakuwa huru na kuhisi raha nikifanya safari ndani kwa kutumia ndege za *ATC*.  *ATC* ni Taifa, *ATC* ni uzalendo.  Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kuwa *ATC* inafufuka. Walioiua *ATC* kwa tamaa zao wachukuliwe hatua, *ATC* kwanza ndipo mashirika mengine yafuate.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii ikitumiwa vizuri sana inaweza kuinua uchumi wa nchi hii na hata kila mtu akashangaa! Shirika la *TANAPA* liongezewe meno ya kutunga sheria kuhusu hifadhi zetu na kupewa uwezo wa kuzisimamia sheria hizo, naamini kwa dhati kuwa tunaweza kukusanya fedha nyingi za kigeni zinazotokana na utalii na hivyo hata kusaidia kuongeza thamani ya fedha (shillingi) yetu ya Tanzania. Matangazo na promosheni nyingi za utalii zenye kutangaza nchi na zaidizaidi zidhamirie kuwaleta watalii wengi hapa nchini. Naishauri Wizara husika itumie kila fursa ya halali iliyopo katika sekta hii ya utalii kuhakikisha kuwa tunatumia rasilimali za asili alizotupatia Mwenyezi Mungu kuliingizia pato la Taifa hili. Tuamue kuanzia sasa naamini tutaweza.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema mengi kuhusiana na hii Hotuba ya Waziri Mkuu huku nikiamini kuwa Waziri Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali. Hivyo haya niliyosema ndipo mahali pake. Naamini kwa dhati kuwa Waziri Mkuu wetu ni safi, anayejua matatizo yanayoiandama nchi yetu, ataweza kuishauri Serikali kwa karibu itekeleze yote niliyoyapendekeza kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu J.K. Nyerere alishawahi kuonya "Tanzania, Tanzania na tusipoisaidia, tumuombe Jalia, njia atumulikie, Tanzania ailinde, waovu wasiivamie. Nasi tunao wajibu wa kumsaidia, yote tusimwachie". Maneno haya ya hekima yanatukumbusha wajibu wa kila mtu katika kuilinda nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maoni niliyoyatoa nimeyatoa kwa nia nzuri ya kuilinda na kuitetea Tanzania. Mimi kama kijana wa Tanzania ninao wajibu wa kuitetea Tanzania hadi tone la mwisho la damu yangu. Namtaka Waziri Mkuu aiangalie Wilaya ya Tarime kwa jicho la huruma ili aisaidie ipate maendeleo kwani Wilaya ya Tarime ni sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA**: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kutokana na hotuba nzuri iliyosomwa ikijadili maendeleo mbalimbali katika nchi hii, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati itokayo Dar es Salaam – Mwanza na Dar es Salaam – Tabora – Kigoma iangaliwe kwa makini sana. Kuna wananchi wako mbali na barabara hivyo reli kwao ni mkombozi mkubwa. Reli hii husafirisha pia mizigo ambayo ni mikubwa kwa magari.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Nyamagana – Ilemela. Kupitia Bunge hili hili la 2005 – 2010 Manispaa ambazo zilipaswa kuanzishwa ni pamoja na Jiji la Mwanza kuwa na Manispaa mbili – Ilemela na Nyamagana. Tunashukuru sana na tunampongeza sana Waziri Mkuu kwa maamuzi hayo mazuri. Tunachongojea ni kuhalalishwa kama Lindi ilivyohalalishwa katika maandishi. Mwanza imekidhi vigezo vyote toka wadau, Baraza la Madiwani, Baraza la Ushauri la Mkoa *(RCC)* kwa kupitia vikao halali, kama ni

mihtasari halali ipo. Hivyo katika kuhitimisha, tunaomba muendelee kutupa matumaini katika hili.

Mheshimiwa Spika, baa la njaa limeikumba Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa. Napenda kuishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye utaratibu mzuri wa kuona ni Mikoa ipi ina njaa ili chakula kipelekwe mara moja. Mikoa yenye chakula inaeleweka mfano, Rukwa, Ruvuma n.k.

(ii) Serikali iwe na fungu (mfuko) maalum kwa ajili ya tahadhari ya njaa. Hii itasaidia wakati njaa ikitokea kwa ajili ya ununuzi wa chakula na kusafirisha chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba nichangie kidogo. Ninaanza na Mahakama; ama kweli Mahakimu walio wengi utendaji wao wa kazi hautoi haki kama sharti moja la kazi yao. Wao hutoa hukumu wakati mwingine kwa kuangalia hali ya mtu; mtu akionekana hohehahe, basi hukumu itakuwa kinyume na kesi ilivyo. Hii haipingiki ya kuwa anajaliwa mwenye kitu. Mara nyingi kesi za watu anaokuwa na wasiwasi nao juu ya rushwa, basi hiyo itachukua kipindi kirefu ili mhusika afikie kumtambua atakavyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Polisi nao wana matatizo hayo hayo. Mtu akienda kulalamika kama pengine katendewa uhalifu, jibu ni kwamba; sisi hatuna usafiri nenda kamkamate mlete, hapo ujue wanataka uwape fedha ya mafuta. Sasa hali kama hii itatufikisha wapi? Siyo hivyo tu, mtuhumiwa wakimwona kuwa ana uwezo, basi watafanya kila njia awape chochote na mlalamikaji aliye mlala hoi, kesi hiyo vinginevyo itaishia danadana hata kumtisha pia asifike mbali.

Mheshimiwa Spika, usalama barabarani pia ni tishio. Wao usalama wanaoutilia maanani ni kusimamisha magari yote yanayopita na kuyatafutia makosa na kutoza faini isiyo na risiti. Kama mabasi, wakisimamisha hawaangalii lolote na badala yake huwataka makondakta waende kule nyuma waliko ili wakatoe rushwa. Kama hakutakuwa na maafikiano na kondakta, basi hilo hapo halitoki hadi walitoe makosa ambayo itabidi alipe faini ya halali. Isitoshe basi, litatazamwa vibaya kila kukicha mpaka pale kondakta huyo atakaposhika adabu (kutimiza matakwa ya huyo askari), hali ambayo huwa ni kero kwa abiria.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, Hospitali zetu nazo ni hali kadhalika. Licha ya kuwa wahudumu ni wachache, lakini huduma nayo ni tabu. Ukifika pale pengine cheti/karatasi uwe nayo mwenyewe, huduma ya pale ni kuandikwa jina na tarehe. Daktari yeye ni kukuandikia dawa baada ya kujieleza ugonjwa wako, lakini dawa kanunue dukani kwa fulani. Kwa hali hii, Serikali iangalie haya kwa manufaa ya Umma.

Mheshimiwa Spika, nizungumze juu ya utawala bora. Kulingana na hali inayoonekana hapa Bungeni hususan hali ya malumbano kati ya hiki Chama cha

CHADEMA, ikumbukwe kila siku tunakuwa na wageni wa ndani na nje ya nchi, ni picha ya aina gani inayoonekana hapa? Ni kwamba uongozi unashindwa kuchukua hatua yoyote ya kuwaweka sawa walau kwenye Kamati ya Maadili? Maana kwa namna moja au nyingine hata wasikiaji na waonaji wa humu ndani (Wabunge) kwa wale wenye hekima na busara huona ni kero kubwa kiasi cha kukosa hamu ya kusikia maneno na majigambo na dharau ambazo zinaendelea hivi sasa, inatosha.

Mheshimiwa Spika, suala la ajali za barabarani, mara nyingi ajali hizi kwa namna moja au nyingine hauwa, ndugu zetu wa usalama barabarani wanachangia. Hawa watu kwa kiasi kikubwa inaonekana kazi yao kubwa ni kutoza kodi fulani katika magari kwani wao hujali pesa kuliko kazi iliyowapeleka pale. Mara nyingi nimeshuhudia jinsi wanavyokomalia kwa ukali na vitisho kwa Makondakta wa mabasi na hata kwa Madereva wa magari ya mizigo hata madogo. Ukiona gari linasimamishwa, kazi ni moja tu. Sasa kwa hali hii, hawawezi kuwakaba Madereva ili wasiendeshe vibaya magari. Mimi napenda kuishauri Serikali iweke Askari wa siri walau wachache tu ambao watawafuatilia hawa wahudumu wa usalama barabarani walau kwa muda mfupi kwa majaribio kwani ikionekana wanaitwa na uongozi wa nje ya idara yao na kuwaonya watapunguza kazi ya kutaka pesa zaidi na baadaye huenda wakajali kilichowapeleka pale.

Mheshimiwa Spika, nielekeze mazungumzo yangu sasa kwenye ustawi wa jamii. Pale Dar es Salaam kuna watoto wanaozungukazunguka barabarani wakiomba msaada kwenye magari, basi likisimama, wao huomba misaada kupitia madirisha hasa eneo la *Fire*. Wale watoto kuna hatari ya kupata ajali, wanalishikilia dirisha hali wamesimama kwenye tuta la katikati ya barabara ikitokea gari kuondoshwa hali yeye kashika dirisha si hatari? Watoto hawa walio wengi wazazi wao wapo jirani ya maeneo yale, hivyo, naiomba Serikali iwakamate watoto wale ili kuwapata wazazi wao na kuwapa karipio ili kukomesha hali hii kwa usalama wao.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwa kuzungumzia kwa ufasaha juu ya sekta ya afya. Kwa kweli sekta hii ina kero nyingi. Kwanza, nizungumzie juu ya ugonjwa wa malaria ambao ni tishio. Watu wengi hupoteza maisha kwa kukosa dawa. Hii hutokana na bei ya dawa kuwa juu na wananchi wa hali ya chini hushindwa kumudu. Serikali huwa inatoa dawa bure za magonjwa yasiyo ya wazi kama vile za mabusha, polio n.k badala ya kutoa dawa za malaria bure, ugonjwa ambao huwashambulia wananchi kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Bima ya Afya, mwanzo wa mpango, wananchi waliambiwa kuchangia shilingi 10,000 kwa mwaka tatizo hospitali zetu za Serikali hazitekelezi utaratibu ipasavyo. Pamoja na kwamba waliambiwa watatibiwa kwa pesa ile lakini mambo huwa kinyume. Dawa unalazimika kwenda kununua madukani kwa watu binafsi hata kwa ambao hawapokei vyeti vya Bima ya Afya. Sio hilo tu, mwanachama kama ni mtumishi wa Serikali mchango huu hutozwa kulingana na mshahara wake na hukatwa siku zote katika kipindi chote cha uhai wake katika utumishi. Jambo la kusikitisha ni kwamba pamoja na pesa zake hizo nyingi, magonjwa mengine inamlazimu kujitegemea. Kama vile macho yake kama atahitaji miwani, itabidi alipie/anunue, tatizo la meno, kama atang’oa na kuhitaji meno ya bandia ni lazima anunue.

Mheshimiwa Spika, hospitali nyingi vifaa havitoshi, katika hospitali za Wilaya na za Mkoa hakuna tofauti. Ukilinganisha na Zahanati ya mtu binafsi ni bora kabisa kuliko hizo kubwa za Serikali. Hospitali ya Mkomaindo ya Masasi ambayo ni ya Wilaya, huduma ni mbaya sana. Maji shida, wagonjwa hasa wazazi, maji huletwa hospitalini hapo kutoka nyumbani. Vitanda ni vichache kiasi wagonjwa wawili hulala kitanda kimoja kwa aliyezaa au wanaojitazamia, haijalishi ili mradi tu wapo wodini. Kwa hali hii ya ukosefu wa maji, hali ya hewa sio nzuri, harufu mbaya ni lazima iwepo. Pale hospitalini pana kisima ambacho kwa Halmashauri inayojali ingesaidia maji yakajazwa lakini kwa vile kuna baadhi ya vigogo wana maboza ambayo yanauza maji hilo halifanyiki. Je, isingekuwa vizuri kama maboza hayo yangekuwa yanapeleka maji pale? Naomba Serikali itolee maamuzi ya haraka kuokoa hali hii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Manaibu Waziri, Waziri TAMISEMI pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii, nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi mazuri ya bajeti hii, kuna mambo machache naomba niishauri Serikali. La kwanza ni kuhusu hizi shule za sekondari ambazo tumeanza kuziandaa kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita. Pamoja na kujenga shule hizi sijaona bajeti ya kuandaa mabweni katika shule hizi kwa sababu tutake tusitake ni lazima tujenge mabweni kwa sababu umbali wa wanakotoka hawa wanafunzi utakuwa ni mrefu hivyo hawataweza kwenda na kurudi. Naishauri Serikali sasa ilione hili na ianze kulifanyia kazi mapema kabla halijawa tatizo kubwa. Mfano Shule ya Sekondari Kutuli iliyopo Halmashauri ya Shinyanga tayari ina madarasa ya Kidato cha Tano, maabara iko kwenye lenta, jengo la utawala tayari lipo, sasa tunaomba msaada mkubwa kwenye mabweni katika shule hii.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni huduma za afya. Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inahudumia Halmashauri za Wilaya saba. Wilaya za Kishapu, Shinyanga Vijijini na Shinyanga Manispaa hazina hospitali za Wilaya hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa wagonjwa na huduma duni katika hospitali ya Mkoa. Naishauri Serikali iangalie suala hili kwa upana wake hasa kwa Wilaya ambazo zimeanza ujenzi huu, mfano Shinyanga vijijini wameanzisha ujenzi huu kwa nguvu za wananchi na fedha za Halmashauri na kuna nyumba ya mtumishi, jengo la *OPD* na misingi ya wodi iko tayari pamoja na nyumba nyingine mbili za watumishi misingi ipo tayari. Halmashauri imeshaomba ombi maalum na halijafanyiwa kazi. Naishauri Serikali ione nguvu na michango ya wananchi hawa iweze kuwasaidia, vinginevyo tunawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia, nina imani Serikali itasikia kilio change, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLA AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kufuta kodi za uzio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi kwa kutumia ndege za Tanzania, hili ni jambo zuri lakini kwa nini mambo yetu sio endelevu. Kwa mfano tulikuwa tukisafirisha minofu ya samaki Mwanza, kwa nini tulingoja mpaka kiwanja kikaharibika, lazima tujitahidi kutunza rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la *notification fee,* nakubaliana nalo, tutaongeza mapato lakini sikubaliani kuwa tutapunguza ajali za mara kwa mara. Kuwe na utaratibu maalum wa kukagua gari na Madereva. Ajali nyingi pia husababishwa na Madereva wanapoongea na simu huku wakiendesha gari, je, iko sheria ya kukataza au hakuna? Pia upakiaji wa abiria wengi kwenye magari na *Traffic* hawachukui hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa Wakaguzi ambao wanakula njama na walipa kodi na kugushi hati ya uhalali ya walipa kodi, hii adhabu naona ni ndogo iende sambamba na kufilisiwa mali yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upunguzwaji bei ya mafuta ya petroli na disel bado ni kidogo mno. Iko haja ya Serikali kuangalia upya kwani hii ni dhamira yetu kupunguza makali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la ajali barabarani, Serikali imeliona jambo hilo na itaendelea kutoa elimu ya matumizi ya barabara na kubadilisha leseni na kufanya *Operation* za mara kwa mara. Pamoja na kuona hayo, lakini kuna jambo halijaonekana nalo ni uzembe wa *Traffic*; kwa mfano, gari linaondoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, likiondoka hupakia abiria zaidi kuliko kiwango chake na gari hilo linapita vituo vingi na *Traffic* husimamisha magari haya na kuyakagua na kuthibitisha kuwa wamepakia watu zaidi, badala kumchukulia hatua yule dereva huwa wanachukua rushwa na kumwachia dereva aendelee na safari yake. Siku hizi kuna mtindo, madereva wanapoendesha magari huwa wanazungumza na simu; je, ipo sheria inayomkataza dereva kuendesha gari huku anazungumza na simu? Kama haipo, ninaomba ianzishwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati ya kuzuia dawa za kulevya zisiingie nchini, lakini vijana wanaotumia dawa za kulevya wanazidi kuongezeka kila siku. Nguvu ya Taifa letu ni vijana, lakini vijana wetu wanapotea kila siku, wakishaingia kwenye madawa ya kulevya huwa wanaharibika miili yao pamoja na akili. Tunasema tunazuia haya madawa yasiingie, lakini mimi ninasema bado madawa ya kulevya yanaingia kwa wingi sana; ninaishauri Serikali izidi kufuatilia na kujua ni nani anayaingiza haya madawa ya kulevya na yanapitia njia gani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha miundombinu katika Bandari lakini utendaji wa Wafanyakazi wa Bandari ni mbovu. Wananchi wanapata usumbufu mkubwa wanapofuatilia mizigo yao, huchukua hata wiki mbili au zaidi ili waweze kupata mizigo yao. Ninaiomba Serikali ilione hili na ilipatie ufumbuzi. Suala la kuwapa Sekta Binafsi ujenzi wa maeneo ya kuhifadhi mizigo nje ya Bandari, mimi sikubaliani nalo; ni bora

Serikali tenge haya maeneo na kuyajenga vizuri na Serikali ndiyo ikusanye hayo mapato kuliko kuipa Sekta Binafsi; hata jambo hili dogo tuipe sekta binafsi?

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha mimi kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi na wananchi wa Jimbo la Dimani tunaunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imejipanga vizuri kwenye maeneo mengi kama kilimo, elimu, maji, afya n.k Mimi ni mkazi wa Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara, katika sekta ya maji na mifugo, Wilaya ya Bunda hakuna mradi wa maji salama kwa wakazi wa mji huo, wanatumia maji ya visima na unapofika wakati wa kiangazi Wilaya hiyo inakuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama na ukiangalia sehemu hiyo ipo karibu sana na Ziwa umbali wa km 10 tu. Hivyo naiomba Serikali yetu iwaangalie kwa jicho la huruma wananchi wa Wilaya hiyo katika suala la maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufugaji, pia nalo linahitaji kuangaliwa kwa makini suala la ujenzi wa malambo kwani wafugaji wanatoka katika Kijiji cha Nyantari hadi Kinaro na mifugo yao kwa ajili ya kufuata maji pia wanatoka Itahiro mpaka Nyasana. Hivyo, naomba sana katika hitimisho nipate ufafanuzi juu ya suala hili la wananchi wa Wilaya ya Bunda linalohusu maji safi na salama na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, katika nchi yetu kuanzia Darasa la Saba hadi Chuo linaingiliana na kuwa la Muungano, hivyo ninaomba sana kuangaliwa kwa kupande wa kusahihisha na kutoa matokeo kwa mtazamo wangu binafsi kuna matatizo ya ndani sana, hasa kwa Kidato cha Tano kwenda cha Sita hadi Chuo.

Mheshimiwa Spika, suala la michezo, Zanzibar kwa upande wa mpira wa miguu kuna Chama cha Mpira wa Miguu, Z.F.A na Bara T.F.F lakini kwa nini Zanzibar yaani Z.F.A haifaidiki na faida yoyote kutoka *FIFA?* Jitihada za kujiunga *FIFA* zinakwamishwa na nini mpaka sasa hatujajiunga wakati Zanzibar hivi sasa ni mwanachama wa *SECAFA* na *CAF,* kwa nini tumeshindwa kujiunga na *FIFA?*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tayari nimechangia kwa mazungumzo Bungeni lakini kutokana na muda kuwa mchache sikuweza kuzungumzia mchango wote niliokuwa nimejiandaa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi haina huduma za maji zilizotosheleza hasa katika Mji wa Namanyere ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya. Huduma inayotolewa kutoka vyanzo mbalimbali ni kiasi cha asilimia 16 cha mahitaji ya wakazi wa Namanyere. Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni aliahidi kushughulikia changamoto hiyo na kuagiza mamlaka zinazohusika kuhakikisha kuwa walau kwa kupunguza tatizo, chanzo cha maji cha Mfili kiboreshwe ili kitoe maji mara mbili ya kiwango cha sasa. Kwa mshangao mkubwa mpaka sasa hakuna jitihada zinazoendelea kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais. Kwa ushauri wangu, Serikali ingeangalia kile

chanzo cha Zuma kilichopo Kate ambacho kilishafanyiwa upembuzi yakinifu na kuonekana kinaweza kufikisha maji Namanyere huku kikiwa kimehudumia njiani vijiji vipatavyo kumi vya Kate, Ntalamila, Nhenje, Ntemba, Kitosi, Chonga, Ifundwa, Msilihofu, Ntuchi na Isale. Chanzo kilichoko katika Milima ya Kate kinaweza kuwa suluhisho la muda mrefu kwa vile ni maji ya kutega.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho ya Madiwani, maslahi yao hayalingani kabisa na kazi wanazowajibika nazo katika kutekeleza wajibu wa kazi zao. Naiomba Serikali kuliona hilo na napendekeza kuwalipa Madiwani Sh.500,000/= kwa mwezi, Wenyeviti wa Vijiji walipwe Sh.120,000/= kwa mwezi vilevile Wenyeviti wa Vitongoji waongezewe kiasi cha posho yao ikiwezekana wapewe Sh.20,000 kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Taifa letu katika bajeti zetu tuwe na uwiano katika kuhakikisha maeneo ambayo wananchi wake wako katika umaskini mkubwa wanatengewe rasilimali za kutosha ili kuwavuta kimaendeleo, kupunguza kiwango cha umaskini kinachowakabili wananchi badala ya hali ya sasa ambayo maeneo yaliyokwishapiga hatua kubwa kimaendeleo yanapendelewa zaidi. Mfano, maji Namanyere ni tatizo kubwa kuliko ilivyo katika mji wowote, inashangaza hakuna mradi wowote ulioelekezwa kutoa suluhisho licha ya agizo la Mheshimiwa Rais na ahadi ya Waziri wa Maji alipotembelea Wilaya hii.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Ofisi hiyo kwa kazi kubwa wanazozifanya lakini pia kuleta hotuba hii nzuri sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuishukuru Idara ya Uratibu Maafa, kwa kazi ngumu na nzito wanayoifanya hapa nchini pamoja na kuwa na watu wachache/wataalam wa kuratibu maafa na pia ufinyu au uhaba wa fedha waliokuwa nao. Hata hivyo, Serikali sasa iangalie kwa umakini uendeshwaji au ufanyaji kazi wa Idara hii usionekane wa kisiasa au hawawajibiki ipasavyo kama wanavyosema Wapinzani.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ianzishe Kamisheni inayojitegemea kufanya kazi zake na kuanzishwa Mfuko wa Maafa kama ulivyotajwa ndani ya Sheria ya Maafa. Hii itawezesha kufanya kazi kwa umakini. Pia, iimarishe Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya na kuanzishwe Kamati hizo mpaka ngazi za Tarafa na vijiji na kuwezeshwa na Serikali Kuu na Halmashauri husika ili yanapotokea maafa au majanga yaanze kuratibiwa na kufanyiwa kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nachangia katika suala la Muungano, ili kuimarisha Muungano uwe wa kweli kama makubaliano au udumu, lazima sasa Serikali ya Muungano iishirikishe Serikali au wananchi wa Zanzibar kikamilifu katika maamuzi kwa vile Katiba ya Jamhuri ni nzuri lakini utekelezaji wake wa mambo ya Muungano haueleweki, iwapo Katiba ya Muungano itatekelezwa ipasavyo Zanzibar inaweza kujitegemea katika shughuli zake za kiuchumi ipasavyo na kunufaisha Wazanzibar na pia kutapunguza malalamiko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuamua kumaliza kukarabati magati sita kwa mwaka jana lakini nashauri kuangalia sasa ujenzi wa gati ndogo au vivuko kwa ajili ya wananchi wa kisiwa cha Songosongo na Pande, Kilwa Masoko kwani hali za maeneo hayo, sehemu za vivuko si nzuri na zinahatarisha wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nipongeze sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Manaibu Waziri na Watendaji kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaangaliwa na watu kama ndiyo mtetezi wao kwa shida zao na maendeleo yao. Sisi kama Wabunge wa CCM hatuna budi kuisaidia Serikali kuipa habari kutoka kwa wananchi hasa kwa mambo yanayowakera. Naomba nileta yafuatayo ili yaweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, madawati, wananchi wanaona hakuna dhamira ya dhati kutatua suala hilo kwa sababu fedha zinazohitajika sio nyingi sana na Serikali ingeweza kuwashirikisha wananchi kama inavyofanya siku nyingine. Naomba Serikali ichukue suala hili na kulifanyia kazi haraka ikiwezekana Serikali kama si kukamilisha basi iwe imetatua suala hili kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ya taa, Serikali ilitoa maelezo kuwa inapata gharama kubwa kwa ajili ya uharibifu mkubwa wa magari. Wananchi wanaona kuwa Serikali inajali maslahi ya wachache wenye magari kuliko kuongeza ukali wa maisha ya wananchi vijijini wanaotumia mafuta ya taa kwa kuonea na kupikia. Ongezeko ni kubwa mno, wakati petroli na dizeli bei zimepungua bei ya mafuta ya taa imeongezwa. Nashauri Serikali itafute ufumbuzi mbadala wa uchakachuaji wa *diesel*. Naomba nishauri kuwa na udhibiti kwa kutoruhusu wenye *petrol station* kuuza mafuta ya taa na mafuta ya taa yauzwe kwenye vituo maalum kama ilivyokuwa zamani. Hii itazuia uchakachuaji wa *diesel* lakini na mafuta ya taa yapewe bei yake halali ili isiathiri maisha ya wananchi wa kawaida. Suala la nyongeza ya bei ya mafuta ya taa tayari linazungumzwa kwenye vyombo vya habari na wananchi wameanza kulalamika.

Mheshmiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusu upimaji na ugawaji wa viwanja. Viwanja hivyo vinagawiwa vikiwa vimepimwa kwenye mashamba ya watu, wenye mashamba wanapewa fidia ndogo sana, wenye mashamba wanatakiwa kununua viwanja wanavyobakiziwa, viwanja hivyo Manispaa zinauza kwa bei ya Sh.6,000 – 10,000 kwa *square meter* moja na viwanja kuwa na ukubwa wa chini wa *square meter* 600 hivyo kiwanja cha bei ya chini ni shilingi 3.6 milioni – 6 milioni. Fedha hizo zinatakiwa kulipwa katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja. Wananchi wanahoji ni kwa nini Serikali iwanyang’anye mashamba yao na kulazimishwa wauze kwa bei ndogo na kuwaongezea umaskini kwani kwenye mashamba hayo waliweza kulima na kufuga ambapo sasa hawawezi lakini pia watoto wao ambao ndiyo kitu pekee ambacho wazazi

wangeweza kuwaachia wanageuka maskini kabisa. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati ili haki itendeke. Nashauri kama ifuatavyo, ardhi hii kama bidhaa yoyote yenye thamani ichukuliwe kama mtaji wa mwenye shamba. Ikiwa linatakiwa kugawiwa viwanja basi mwenye shamba awe mbia wa viwanja hivyo ili mauzo ya viwanja hivyo viinufaishe Serikali na mwenye shamba. Watoto wa mwenye shamba pia wagawiwe viwanja ili wasihangaike wanapokua.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uvamizi wa viwanja bila kufuata sheria. Uvamizi huu ni wa aina mbili, wafanyabiashara ambao wanavamia na kubomoa nyumba ndogo na kuvunja uzio. Wafanyakazi wa Manispaa na Ardhi wanahusika hata kubadili maandiko kwenye kompyuta. Mtandao huu ni mkubwa, lakini tatizo pia ni wafanyakazi waliokaa kwenye Manispaa muda mrefu na kujenga himaya. Wafanyakazi hawa ajira na kuwahamisha/kuwafukuza ni TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, pili, wananchi wahamiaji wanaoingia Jijini Dar es Salaam kila siku hasa wale waliotoka sehemu ambazo wanafahamu thamani ya ardhi (Kilimanjaro, Bukoba, Nyanda za Juu Kusini) wamekuwa wanavamia eneo lolote la wazi bila kujali ni la nani. Tayari hili limeleta mauaji. Tatizo ni ushiriki wa Watendaji wa Serikali za Mitaa lakini pia Serikali kutochukua hatua pale tu uvamizi unapotokea. Hii pia imeingia Mkoa wa Pwani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahishwa sana na mgao wa bajeti ya Waziri Mkuu, naomba iende kama ilivyoorodheshwa kwenye bajeti ila kuna matatizo ambayo yanajitokeza sana kwa Halmashauri, huwa bajeti yao wanacheleweshewa fedha zao na pia baadhi ya Watendaji kujiona Mungu Mtu, kutojali maslahi ya watumishi wa chini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo, shule kutokuwepo na Walimu wa kutosha na kumekuwepo na makusudi shule za vijijini kutokuwa na Walimu wa kutosha na wakija hawakai.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kero kwenye hospitali, dawa, hakuna.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la baadhi ya watu wa Wilaya kunyanyasa watu wa chini kila muda, kosa dogo yeye anawekwa mahabusi masaa 24 bila sababu yoyote. Pia kuingilia kazi za Wakurugenzi wetu bila sababu zozote na hawa Wakuu wa Wilaya kuwa ombaomba, naomba liangaliwe kwa sababu jicho la Rais ni Mkuu wa Mkoa na msaidizi wake ni Mkuu wa Wilaya sasa kama Mkuu wa Wilaya anakuwa msumbufu hatutafika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono bajeti ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na kuchaguliwa tena kwa mara ya pili kuendelea na wadhifa wa Waziri Mkuu. Nampongeza pia kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ya mwaka 2011/2012 ambayo inalenga kubadilisha maisha ya wananchi hasa wanaoishi Vijijini kwa kuboresha huduma muhimu za kijamii na uchumi kama miundombinu, afya, barabara, elimu, maji safi na salama, utawala bora, usawa katika kutoa huduma, kutoa msisitizo katika sera ya Kilimo Kwanza na mipango mingine mingi ya kuharakisha maendeleo kwa wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya Waziri Mkuu ya mwaka 2011/2012, kama itatekelezwa ilivyokusudiwa, nina imani kabisa itabadili maisha ya walio wengi ambao hali zao kimaisha na maendeleo ni duni na pia itapunguza umaskini. Bajeti hii inakusudia kuimarisha kilimo, kuwakomboa Watanzania wengi ambao uchumi wao unategemea kilimo. Pamoja na mipango mizuri ya kuendeleza Kilimo kama *(ASDP),* azma ya Kilimo Kwanza, mpango wa Ruzuku kwa wafugaji, uanzishwaji wa Dirisha la Kilimo katika Benki ya *TIB* na Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini (*SAGCOT*) na mengineyo, bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha utekelezaji wa Mipango hii inasimamiwa kikamilifu. Kwanza, kwa kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi walengwa na si kutumia makundi ya watu wachache, matajiri watakaodandia miradi hii, kuwarubuni wananchi wawauzie ardhi kwa bei nafuu au kwa huduma na kisha wasitekeleze malengo kwa faida ya walio wengi hii itadhoofisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma inaweza kuharakisha maendeleo. Kwa mfano, katika sekta ya miundombinu, Serikali inaweza kukaribisha wabia binafsi katika uendeshaji wa huduma na kupata faida bila kutumia gharama. Tuchukue uendeshaji wa huduma ya usafirishaji hasa kwa kutumia reli, Serikali inaweza kuingia mkataba wa ubia na wafanyabiashara binafsi wao wakanunua vichwa vya treni na mabehewa ya kusafirisha mizigo yao na wakalipia kutumia miundombinu ambayo itakuwa ni mali ya Serikali. Hapa Serikali itaondokana na jukumu la wafanyakazi na gharama nyingine zitakazobebwa na mbia wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Uwekezaji, napenda nichangie kwa kusema pamoja na kwamba wawekezaji wamevutiwa sana kuja kuwekeza katika nchi yetu na kwamba Serikali ina mipango ya kuhamasisha wananchi waweke vivutio vya kuongeza wawekezaji kwa kuangalia uwezekano wa kutoa tuzo kwa Wizara, Mikoa na Mitaa itakayovutia wawekezaji wengi, jambo jema lakini usimamizi unatakiwa uwepo maana wawekezaji wengine si waaminifu na wala si wazalendo. Napendekeza Sheria ya Uwekezaji iwekwe bayana kwa kumnufaisha mwananchi. Kwa mfano, sheria iboreshwe kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na wananchi wake kwamba mwekezaji yeyote wa nje ni lazima awe mbia na mwananchi na hasa katika masuala ya ardhi na madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda, viwanda ni nguzo kubwa ya kupima maendeleo ya nchi kwa kuondoa utegemezi na vikwazo katika mambo yanayohusu maendeleo. Nchi yenye viwanda ina maendeleo mengi kwani viwanda vinawezesha nchi kupata maendeleo ya haraka katika sekta ya kilimo, usafiri, TEKNOHAMA n.k. Kuna haja ya Serikali badala ya kuendelea kuagiza pembejeo na vipuri toka nchi za nje, kuwe na mkakati thabiti wa kufufua na kuongeza viwanda vyetu vikubwa kama *Kilimanjaro Machine Tools* na kukiongeza uwezo Kiwanda cha Nyumbu. Viwanda hivi nina imani vikipewa msukumo wa kutosha, vina wataalam wa kuweza kutengeneza pembejeo za kilimo kama matrekta na magari ya kubebea mizigo na mazao. Viwanda vingine vinaweza vikajengwa katika Mikoa mingine hata Kibaha Vijijini viwanda vya kusindika mboga, samaki na nyama vinaweza kujengwa vikaongeza pato la Taifa, kutoa ajira kwa vijana na hii itaharakisha maendeleo ya Jimbo la Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana biashara ya soko huria, kumekuwepo na wimbi la wafanyabiashara ambao wanajitajirisha kwa kutumia nguvu za wananchi kwa kuingiza nchini bidhaa feki zisizokuwa na kiwango. Bidhaa hizo zinachangia sana katika kuua viwanda vyetu vya hapa nchini ambavyo kwa kweli bidhaa zake ni imara kuliko zile feki zinazoagizwa kutoka nje. Bidhaa hizo feki zinapoingia hapa nchini huuzwa kwa bei nafuu hivyo kuwa rahisi kuwarubuni wananchi ambao wengi kipato chao ni duni, hivyo wanapoona kitu chenye bei ndogo wanadhani wamepata mkombozi lakini madhara yake ni makubwa kwani bidhaa feki kama vifaa vya umeme vyenye viwango duni vimewagharimu wananchi wengi walionunua kwa kuunguliwa nyumba.

Mheshimiwa Spika, siku hizi kuna viatu, nguo, mapochi ya kinamama, samani mbalimbali za ndani na maofisini, redio, luninga na vifaa vingi vya matumizi ya nyumbani ambavyo ni duni, vinatumika mara moja na kuharibika. Unakuta mtu kanunua kiatu, kavaa mara ya kwanza na siku hiyo kinamuadhiri kwa kuharibika na kutoka soli yake na hakitengenezeki tena, bidhaa hizi kwa kweli ni kama "*disposable*" na pia ni wizi wa waziwazi kwa wananchi. Hili nalo ni tatizo kwa wananchi, hivyo ni vyema Serikali ikaweka mikakati ya kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini kama samani za ndani, viatu vinavyotumia ngozi ya wanyama wetu, nguo zinazozalishwa katika viwanda vilivyoko nchini kwetu, vinatumia pamba yetu, hii itasaidia kuongeza ajira, kukuza uchumi wa wananchi na pia itaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la mipango Miji, ni la msingi na linaharakisha wepesi wa kuhakiki huduma za jamii kwa mfumo wa kisasa. Miji mingi ya hapa Tanzania haiko katika mipangilio inayovutia mandhari ya miji na pia inakuwa vigumu sana kwa watoa huduma kama za maji, umeme, huduma za posta, huduma za simu na kadhalika, kupanga huduma hizo kutokana na miji yetu kujengwa kiholela na hatma yake kutokuwa na mipangilio ya barabara zinazopitika kiurahisi, mitaa inayoeleweka na hata nafasi za wazi za huduma nyingine kama viwanja vya michezo na mazoezi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini bado halijajengeka sana. Serikali inaweza kufanya Jimbo lile kuwa mji wa mfano hapa Tanzania kwa maana ya kwamba Mji Mdogo wa Mlandizi unaweza kupimwa kwa kutenga na kuonyesha sehemu za makazi, sehemu za mashamba, sehemu za viwanda na hata sehemu za bandari kavu ya

kuegesha magari yote yanayoingizwa hapa nchini yawe ya *Transit* au ya kuuza hapahapa nchini kama ilivyo katika mji wa Sharjan kule Dubai. Kwa kufanya hivi, Serikali itasaidia kukuza maendeleo ya Mkoa wa Pwani na kuiweka katika ramani ya dunia.

Mheshimiwa Spika, mpangilio wa makazi katika Mji Mdogo wa Mlandizi kama utawekwa katika ramani kitaalam, inawezekana kujenga *'round about'* katika makutano ya barabara kubwa iendayo Morogoro/Mikoani na Ruvu JKT na ile iendayo Ruvu Makofia. Kufanya hivi, kutainua hadhi ya wakazi wa Mlandizi pia itavutia wawekezaji kujenga na kutoa huduma kama mabenki, viwanda na biashara mbalimbali kushamiri, majengo yataongezeka, hoteli za kulala wageni, maduka na mzunguko wa pesa utakuwepo kwani huduma mbalimbali zitaboreshwa. Yote haya yatavutia wataalam watakaopangwa kufanya kazi katika Jimbo la Kibaha Vijijini kuhamasika na kuongezeka kwani huduma zote muhimu na mandhari nzuri ya kufanyia kazi *"condusive working environment"* itakuwepo.

Mheshimiwa Spika, elimu ni ufunguo wa maisha, kwa sasa hivi hakuna kitu chochote kinachowavutia wataalam wanaopangiwa kufanya kazi katika Jimbo la Kibaha Vijijini kutokana na maendeleo duni. Serikali ijitahidi kuboresha shule na hasa zile Sekondari za Kata kwa kujenga maabara, mabweni kwa wanafunzi wa kike na wa kiume, vyoo vya kutosha na nyumba za Walimu zenye hadhi.

Mheshimiwa Spika, suala la maji safi na salama ni jambo linalowasumbua sana wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini. Maji ya Mto Ruvu ambao uko katika Jimbo lile yanatumiwa na watu wa Kibaha Mjini na sanasana watu wanaoishi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Wananchi wa Jimbo ambalo maji hayo yanatoka wamebaki kunywa maji ya visima vya kuchimba kienyeji vyenye kina kifupi hivyo kupata magonjwa ya mlipuko mara kwa mara, wakati wa ukame wananchi hawa wanalazimika kuchangia maji ya madimbwi na mifugo. Hii siyo sahihi kabisa. Naomba suala la maji lipewe kipaumbele kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wanapatiwa maji safi na salama toka Mto Ruvu. Hii itawapa moyo wa kutunza mazingira, kuhakikisha maji ya mto Ruvu yanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, umeme ni tatizo lingine kubwa linalozorotesha maendeleo ya uchumi wa Jimbo la Kibaha Vijijini. Kuna ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni ya Uchaguzi wa Urais, natumaini zitaheshimiwa na ahadi za kupatiwa umeme Kata ya Ruvu na ahadi nyingine zitatekelezwa ili kulinda heshima na kauli za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mtu ni afya, bajeti hii itambue na kuhakikisha kwamba hospitali na zahanati zetu zitakuwa na dawa na vifaa vya kutosha, wataalam wa maabara, Madaktari, Manesi na watoa huduma mbalimbali. Ni matumaini ya wananchi kwamba huduma hii itaboreshwa na zahanati na nyumba za watumishi zitajengwa kila Kata kama ilivyo kwa Shule za Sekondari za Kata. Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wanatarajia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kukipandisha daraja Kituo cha Afya cha Mlandizi kuwa Hospitali ya Wilaya itatekelezwa katika bajeti hii kwani kituo kile kinabeba majukumu mengi ya kuhudumia jamii kubwa kuliko malengo yake ya awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hotuba nzuri ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimalizie kwa kusema kwamba usimamizi wa utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika bajeti uwe thabiti, yasijirudie yale tuliyosikia Mheshimiwa Lyatonga Mrema akiyasema katika Halmashauri wakati Kamati yake ilipopitia kukagua matumizi ya mipango na maendeleo katika Halmashauri. Pili, niseme kwamba ari na uthubutu uliotumiwa kujenga Shule za Sekondari za Kata katika awamu iliyopita kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, utumiwe tena kwa nguvu kubwa awamu hii, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Vituo vya Afya kila Kata. Kama ujenzi wa Shule za Kata uliwezekana tena kwa kipindi kifupi basi ari ileile itumike katika kujenga Vituo vya Afya, masoko ya kisasa na Vituo vya Polisi ili kuweka ulinzi kila Kata.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba mambo yote mazuri yaliyotamkwa katika hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu yanawezekana kama Serikali itashirikisha wananchi katika kuwapa elimu na kupata mawazo ya pamoja katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kwa makini suala la Watendaji wa Halmashauri hasa Ma–*DT* ambao wanamiliki majengo makubwa ya ghorofa (hoteli) na majumba ya kupangisha yenye thamani kubwa, magari makubwa ya mizigo, pesa wanapata wapi? Wengine wanasema wamekopa kwenye mabenki zaidi ya shilingi 400 milioni kama Watendaji wanaweza kukopeshwa na Benki kiasi hicho? Sidhani kama kuna haja ya Watendaji hao kuendelea kutumikia Halmashauri kwa kuwa wana biashara zinazowapa kipato kikubwa kuliko makusanyo ya Halmashauri, ni vema wakaendelea na biashara zao kuliko kutumikia Halmashauri zinazowalipa mshahara mdogo kuliko vipato vyao kwenye biashara zao. Wengine biashara zao ziko kwenye majina ama ya ndugu zao au mke/watoto wao. Juhudi ziendelee kuwasimamisha/kuwaachisha kazi Watendaji watakaothibitika kama wameiba, ubadhirifu, uzembe n.k. kuliko kuendelea kuwahamishia kwenye Halmashauri nyingine. Chunguzeni mitandao ya wahalifu hawa kwenye Halmashauri ambao mitandao yao inasemekana inaanzia TAMISEMI. Kama tabia hii ipo ikomeshwe mara moja ili kuleta ufanisi kwenye utendaji wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR**: Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuchika na Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa, kwa hotuba nzuri iliyolenga Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwenye Ilani ukurasa wa 246 mpaka ukurasa wa 247, kuna masuala ya watu wenye ulemavu lakini kwenye hotuba hayakutajwa kabisa. Tukumbuke kundi hili ni kubwa na linaongezeka siku hadi siku, kuna ajali za barabarani, maradhi kama malaria, *malnutrition*, *meningitis* n.k.

Mheshimiwa Spika, watoto wenye ulemavu wanaiomba Serikali iwasaidie vifaa, wanasoma kwa taabu sana, wanaomba wapatiwe viwamba sikio kwa viziwi, *braille* kwa wasioona, *printer* kwa ajili ya kukuza maandishi, baiskeli *durable* kwa walemavu wa viungo, *sunscreen lotion* kwa wenye ulemavu wa ngozi. Wenzetu Kenya wana Baraza la Kitaifa la Walemavu kwa miaka mitatu sasa, vifaa vyote vinapelekwa pale na fedha zote zinapelekwa kwenye Baraza hilo la Walemavu. Pia Walimu wa elimu maalum ni wachache sana, hili lipewe kipaumbele inashusha sana elimu ya watoto wetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza uwezeshaji mikopo ipatikane ili waweze kujiajiri. *SIDO, VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi viboreshwe ili kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wasio na ajira. Walemavu ni Watanzania, wana haki ya kusaidiwa kikamilifu, ukali wa maisha ni mara mbili zaidi kwa wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake kwa kuwasilisha hotuba nzuri iliyosheheni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mkereketwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni muumini wa Serikali mbili. Ili kuhakikisha Muungano unapata nguvu zaidi, lazima baadhi ya kero ambazo ni rahisi kuondolewa ziondolewe haraka. Moja katika kero hizo ni bandari ya Dar es Salaam ambapo wafanyabiashara wa Zanzibar wananyanyaswa sana. Baadhi ya manyanyaso hayo ni kutozwa ushuru mara mbili. Wanaposhindwa kulipia mizigo yao huzuiliwa na baadaye kuibiwa ikiwa katika kizuizi. Wafanyakazi wa *TRA* waliopo ni wajeuri, mafedhuli kwa wafanyabiashara, wanapotaka kuonana na Afisa wa ngazi za juu wa *TRA* hawapewi nafasi, huambiwa yote waliyoambiwa ni sawa na hawana haja ya kuonana na Maafisa hao.

Mheshimiwa Spika, kero ya pili ni kodi kwa simu za mikononi zinazopigwa Zanzibar huwa hazipelekwi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mashirika ambayo hayalipi kodi kwa Serikali ya Zanzibar ni *TIGO, VODACOM* na *AIRTEL*. Shirika moja tu ndilo linalipa kodi kwa Serikali ya Zanzibar nalo ni *Zantel*. Hili pia linaweza kutatuliwa. Tafadhali Mheshimiwa Waziri chukua hatua za kulitatua.

Mheshimiwa Spika, kero ya tatu ni kuitumia ofisi ndogo ya Bunge iliyoko Zanzibar. Ingawa Kanuni inasema kuwa vikao vya Kamati vinaweza kufanyika katika ofisi ya Bunge la Zanzibar hadi leo hii hata Kamati moja haijawahi kufanyia vikao vyake katika ofisi hii. Ni jambo gani linalozuia? Mambo madogomadogo kama haya ndiyo yanayowafanya Wazanzibar kuona wanabaguliwa na hawapati manufaa katika Muungano.

Mheshimiwa Spika, nategemea kero hizi tatu zitapatiwa ufumbuzi katika hotuba hii ya majumuisho. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE**: Mheshimiwa Spika, tatizo la ardhi katika Jimbo la Mbozi Magharibi, kumekuwa na tatizo la Idara ya Ardhi Wilaya ya Mbozi kuchukua maeneo ya wananchi na kuyagawa kwa watu wengine bila kuwalipa fedha kwa kigezo kuwa ardhi ni mali ya Serikali. Miongoni mwa maeneo yaliyoathirika ni Tunduma (eneo la Chapwa na Mwaka) pamoja na Kata ya Chiwezi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, kwa kuwa ni moja ya nguzo za mawasiliano katika kuwaunganisha wananchi toka sehemu moja kwenda nyingine na hivyo kuwasaidia katika kuwaendeleza kijamii na kiuchumi lakini bado katika Jimbo la Mbozi Magharibi tatizo la barabara ni kubwa. Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikitenga fedha ndogo katika kukamilisha barabara hizo. Miongoni mwa barabara hizo ni barabara itokayo Ntungwa kupitia Chilulumo na Mkulwe kuelekea Kasambu. Hii ni barabara ambayo haipitiki kabisa wakati wa mvua. Hivyo Serikali tunaomba itenge fedha za kutosha ili nao waweze kuona umuhimu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vivuko na madaraja, maeneo mengi ya Jimbo la Mbozi Magharibi yanaunganishwa na mito na vijito vya msimu hivyo kukosekana kwa madaraja kunasababisha wananchi wengi kushindwa kufanya shughuli zao za kiuchumi wakati wa masika mvua zinapokuwa nyingi na pia watu wengi kufariki kutokana na kusombwa na maji mengi ya mtoni. Miongoni mwa maeneo yanayohitaji kivuko/madaraja ya kudumu ni Kijiji cha Yala cha Kata ya Chitete kwenda kijiji cha Kanyala, Kata ya Chilukemo, ambapo itapunguza urefu/umbali na hivyo kuwasaidia wananchi; pia toka kijiji cha Ivuna (Kata ya Ivuna) kuelekea vijiji vya Mkomba na Sante (Kata ya Ivuna).

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ujenzi wa madarasa, nyumba za Walimu, vyoo na maabara kwa Shule za Sekondari. Kwa kuwa katika orodha ya majedwali ya hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012, inaonyesha kuwa Wilaya ya Mbozi ina mahitaji makubwa ya madarasa, nyumba za Walimu vyoo na maabara, hivyo upungufu wake unahitaji Serikali ikamilishe mahitaji hayo kwa kuleta fedha za kutosha ili nasi kwa kushirikiana na wananchi tukamilishe idadi hiyo pungufu kabla ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, uchakachuaji katika pembejeo za kilimo hususan mbolea ya ruzuku kutokuwafikia walengwa kunahitaji majibu ya msingi yatakayowaridhisha wananchi, vinginevyo mpango wa Kilimo Kwanza utashindwa kwani huku kunawakatisha sana wakulima tamaa kwa kuwa pembejeo hazifiki kwa wahitaji.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya migongano kati ya Wakuu wa Wilaya na Wabunge Majimbo. Hili Mheshimiwa Waziri Mkuu usipochukua hatua litaleta mifarakano mikubwa kiutawala Majimboni na hivyo itapelekea kukwamisha maendeleo Majimboni. Hivyo basi Serikali inapaswa kutofautisha kwa kuainisha majukumu na mipaka ya kila kiongozi.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, imeeleza mengi na kwa ufanisi. Ninayo maoni machache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli, nimefurahi sana kuona sasa tumeona umuhimu wa kuipa reli uzito unaofaa. Reli ndio mkombozi na itakayosaidia uchumi wa nchi hii. Reli ndiyo itakayookoa barabara zetu kwani mizigo mizito inapaswa kusafirishwa kupitia njia ya reli na utengenezaji wake unachukua muda mfupi na haichakai haraka kinyume na barabara ambayo kila baada ya miaka miwili lazima ifanyiwe *re-surfacing.* Tuiboreshe reli yetu isaidie wakulima wanyonge na pale uwezo ukiwepo tufungue maeneo mengine ili reli ifike na isaidie uchukuzi wa mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni viwanja vya ndege. Kweli sasa tumeamua, uchumi utaboreka iwapo viwanja vyetu vitaboreshwa na mashirika mengine ya ndege yatapata nafasi ya kuwekeza nchini. Viwanja kama vya Kigoma, Tabora, Bukoba, Mwanza, Musoma viboreshwe na visivyo na lami viwekwe. Pia majengo ya kuongozea ndege na vifaa vipatikane na kuwepo na uzio ili kudhibiti usalama. Yote hayo yanawezekana iwapo Serikali itasaidia *TAA (Tanzania Airpot Authority)* iwe kwa fedha au kwa dhamana ya kukopa ili itimize ndoto yao hiyo.

Mheshimiwa Spika, *ATC* nayo ifufuliwe na *cost cutting measures* zifanywe, wafanyakazi wachunguzwe, watafutwe waadilifu hata toka sekta binafsi na walipwe vizuri ili wabaki katika shirika.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji wa baadhi ya Watendaji, wamejiingiza katika siasa na wengine hawawajibiki ipasavyo katika majukumu yao, uadilifu katika kazi sasa ni kitu cha nadra. Wachache wanaamua kujitajirisha. Kipato chao hakilingani na mali zao. Rushwa bado ni tatizo. Hupati huduma katika baadhi ya maeneo kama shati ni mikono mifupi. Rushwa Mahakamani (kwa baadhi ya Watendaji ni hatari). Polisi barabarani usiseme. Vita vya rushwa ni kwa watu wote na tusilegeze kamba. Serikali iendelee isiogope lawama. Mashirika kama *TBA/DAWASCO/TANESCO* wafanyakazi wake baadhi wanarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu, bado sekta za madini, utalii, uvuvi wa bahari kuu na misitu zinahitaji kufuatiliwa kwa karibu ili mapato yake yatusaidie katika uchumi wetu, ufuatiliaji wa kina juu ya mapato, mirahaba, *exemptions* na tozo mbalimbali, ili kuziba mwanya wa uvujaji wa mapato. Tunazo taarifa zisizo na uhakika kuwa ndege ndogo zinatua katika migodi na kuondoka na madini na hata kama utapiga picha haitoki. Je, hili ni kweli? Tufuatilie ukweli wake. Uharibifu wa mazingira katika migodi utafutiwe ufumbuzi hasa matumizi ya kemikali.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA**: Mheshimiwa Spika, shukrani kwa wapenda maendeleo wote waliopigia kura Chama cha Demokrasia na kuniwezesha kuingia katika Bunge hili Tukufu, nawashukuru.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniteua kuwa mmoja wa wabunge wa bunge hili tukufu. Namrudishia sifa na utukufu.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Katibu Mkuu, Dkt. Willibrod Slaa, kwa ujasiri mkubwa na uthubutu wa kugombea Urais na kuleta uhai na mafanikio makubwa sana katika Chama cha Chadema na siasa za upinzani.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru Kamanda Mkuu wetu, Mpiganaji asiyetetereka, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe (Mbunge), kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto. Mungu ambariki, namwahidi sitamwangusha kamwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani na pongezi hizi, naomba sasa nizungumzie masuala matatu au manne iwapo muda utaniruhusu. Kwanza kabisa, ni kuhusu bajeti ya watoto wa Tanzania. Matatizo yanayowakumba sasa ni kutokuwa na fungu la fedha linalowalenga watoto wa Tanzania na wala hawamo kwenye bajeti. Iwapo watoto wangewekewa fungu lao, matatizo ya malezi, matibabu, mikopo ya elimu, watoto wa mitaani n.k. yanayowahusu watoto yasingekuwepo kwa sababu kila mmoja angekimbilia kwa mzazi wake - Serikali na kupatiwa stahili yake. Napendekeza kuwa kwa kuwa suala hili ni la msingi sana, inafaa sasa kuwaanzishia mfuko wao kwa kuchangia asilimia 01%. kutoka kwenye kila uwekezaji na uvunaji wa kila madini, misitu na maliasili zote katika nchi hii kwani wenzetu hufanya hivyo na inawasaidia sana kuwapa amani wazazi wa watoto wa nchi zao.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchangia juu ya Serikali za Mitaa na mamlaka ya wananchi. Inavyoelekea ilivyo sasa ni kwamba wananchi huku chini tumewajengea tabia ya kutegemea kutoka juu. Inaelekea malezi yetu ni kuona tabia ya kuombaomba inakuwa utamaduni unaokomaa. Tabia hii ni mbaya, tuwawezeshe kutumia mazingira yao kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililopo hapa ni utamaduni wa uvivu wa kufikiri na kutoona yaliyo mbali na kupelekea katika mipango kila wakati tumekuwa tukipanga kwa ajili ya leo tu. Hii inajitokeza katika upungufu wa bajeti hii ya kutoona umuhimu wa kutoa elimu ya ukombozi wa fikra wa kiuchumi na hivi kupelekea watu kujitegemea badala ya kusubiria kuombaomba. Ni wakati sasa kwa Serikali inayojidai kuwa inasimamia maendeleo ya watu, iliangalie suala hili la ardhi ya madini. Mimi sioni kwa nini wawekezaji wanapopewa mikataba isiwawezeshe wananchi kuwa na hisia katika migodi hiyo badala ya kuwafukuza kwa kuwapa kiwango kidogo tu na kuwaacha solemba, tupunguze matatizo haya ya kujitakia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kutilia mkazo katika bajeti ya watu ni kuwatengea fungu la kutosha la elimu ya uraia. Serikali idhamirie kufanya mambo kwa vitendo, hii itasaidia sana uelewa wa wananchi kuhusu mambo mbalimbali hususan elimu ya kwa nini Vyama Vingi vilianzishwa nchini, badala ya kuwa tunapotosha wananchi kuhusu Vyama vya Upinzani, hii si sahihi. Ni muhimu watu waelewe kuwa Upinzani kazi yake kuu ni kuisimamia Serikali *(watchdog of the government in power),* Serikali sio kazi ya Chama kinachotawala kukichagulia mbinu za kufanikisha kazi yake hii.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Ushirika ndiyo madaraka ya watu na tunafahamu jinsi gani watu wakipewa nafasi ya kupanga, kuamua mambo yao na kusimamia mambo yao wanaweza, turudishe Vyama vya Ushirika kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuongeza msisitizo juu ya kutambua kazi muhimu za Madiwani, hivyo wawezeshwe kwa kupatiwa usafiri wa uhakika na badala ya posho wapewe mishahara inayolingana na kazi yao.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia Mkoa wangu naotoka wa Kilimanjaro, watu wamekuwa na mawazo potofu kuwa Mkoa huu uko mbele kimaendeleo kwa hiyo hatuhitaji tena maendeleo. Naomba nisikubaliane na mawazo hayo. Ni kweli babu na bibi zetu pamoja na wazazi wetu enzi hizo walijitolea fedha zao kupitia zao la kahawa ambalo kwa sasa liko kwenye hali mbaya pamoja na madhehebu ya dini ndiyo maana Kilimanjaro inaonekana ilivyo. Mkoa wa Kilimanjaro leo hii hatuna maji safi na salama, barabara zinazoingia vijijini ni mbaya sana, leo hii tuna njaa katika Mkoa wetu, mvua hazikunyesha za kutosha na hivyo kusababisha mazao kunyauka, kwa kifupi hali ya Mkoa wetu kwa sasa ni mbaya.

Hali ya biashara katika Mkoa wetu siyo nzuri ukizingatia viwanda vingi ambavyo vilikuwa vinaongeza uchumi wa Mkoa wetu vimefungwa na mpaka sasa hatujajua hatma ya viwanda hivyo, kibaya zaidi imechangia ukosefu wa ajira katika Mkoa wetu. Pia tunao upungufu wa Walimu na madawati katika Mkoa wetu, kweli shule zipo ila zina upungufu mwingi, hivyo basi ni wajibu wa Serikali kuhakikisha hayo yote niliyoyasema yanafanyiwa kazi katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro kwa sababu na sisi tunachangia zaidi ya asilimia 40 ya mapato yanayotokana na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie fedha za miradi zinazotumwa kwenye Halmashauri zetu ambazo hazifiki kwa wakati katika maeneo yetu, hii inatokana na bajeti yetu kuwa tegemezi na hii inachangia miradi mingi kutotekelezwa kwa wakati na kusababisha kero kwa wananchi wetu. Naomba niishauri Serikali fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitokane na fedha zetu za ndani zaidi na hizo za wahisani ndio zitumie kwa shughuli nyingine za uendeshaji pamoja na posho.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Maafa, kama nilivyosema mwanzo, Mkoa wetu unakabiliwa na njaa. Naomba nitoe tahadhari mapema kwa sababu kumekuwa na tabia ya kugawa vyakula na vitu vingine vinavyotolewa na Serikali kwa wananchi na kugaiwa kwa ubaguzi kufuatia itikadi za Vyama vyao. Tunaomba hili lisijitokeze maana njaa haichagui CCM, CHADEMA, *CUF, TLP* wala *NCCR,* njaa ni njaa tu. Hivyo tunaitaka Serikali ilisimamie na ihakikishe wananchi wake wote wanatendewa haki.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo niliyokusudia kuyasema leo, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa maoni yangu, ahsante.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU**: Mheshimiwa Spika, napenda nichangie hoja hii ya Waziri Mkuu, kwanza, kwa kuipongeza hotuba hiyo pamoja na Waziri Mkuu na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri iliyofanywa katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne hadi leo. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala la ongezeko la bei ya mafuta ya taa, japo imeshapita lakini ni muhimu kuangalia hali halisi ya wananchi wa vijiji ambako hakuna umeme na pia hali halisi ya maisha yao kuwa ya kipato cha chini sana. Kama tunataka kuhakikisha jamii haikati miti hovyo lazima kuwe na njia mbadala. Ni vema kwa kule ambako tunaona kwamba wananchi watapata shida sana ya nishati mbadala basi chondechonde, suala la bei ya mafuta ya taa liangaliwe kwa makini sana. Si tu kwa kuzuia uharibifu wa mazingira bali pia kuweza kuona (taa usiku) na kumpunguzia mama (mwanamke) mzigo wa kuhangaika kutafuta kuni wakati wa kupika.

Mheshimiwa Spika, ni vema pia tuangalie athari atakazopata mwanafunzi ambaye anaishi kwenye nyumba za kupanga jirani na shule anayosoma. Ni jinsi gani ataathirika kwa kununua mafuta ya taa kwa bei ya juu zaidi kitu ambao kitamsababishia kuingia katika vishawishi ambayo vinaweza kumrudisha nyuma kielimu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza na kuiunga mkono bajeti hii.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa jitihada zake za kuleta maendeleo kwa Watanzania katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kilimo bado ni mwajiri mkuu wa Watanzania kama kahawa inayolimwa sehemu kadhaa kama vile Bukoba, inaiingizia nchi fedha za kigeni. Tutilie mkazo kilimo cha kahawa. Utafiti uimarishwe, mbegu bora zitumike, madawa n.k. Cha msingi zaidi ni kuwahamasisha wakulima. Mkulima anapata pesa kidogo sana kwa kahawa na pesa hizi zinapotelea katika mlolongo wa ada na tozo na gharama zisizokuwa za lazima. Kwenye soko bei ya Kahawa ni nzuri, tupunguze mlolongo huu wa mirija inayonyonya bei ya mkulima. Kwa njia hii tutamwongezea mkulima hamasa ya kulima Kahawa na tutaboresha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, tuendelee kuhimiza kilimo cha wakulima wakubwa, hawa wawekeze. Tuvune sana na tuuze ziada nje tupate pesa za kigeni. Pia hii itaondoa baa la njaa na tutaneemeka. Pia kwa kilimo kikubwa, wataajiri watu wengi, kilimo kitaendelea kuwa na maana kubwa katika uchumi wetu.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii adimu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Nungwi kwa kuandika historia mpya tangu kuanza Mfumo wa Vyama Vingi kuchagua Mbunge wa Chama cha *CUF*. Naahidi kushirikiana na wananchi kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, sasa naingia katika kuchangia kwa kuzungumzia matatizo wanayoyapata wafanyabiashara wa Zanzibar. Wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoingia na mizigo bandari ya Zanzibar wanalipa ushuru kama sheria ilivyo lakini bidhaa hiyohiyo ikisafirishwa Bandari ya Dar es Salaam pia inatozwa kodi kwa mara ya pili. Kwa hiyo, huu ni usumbufu wa makusudi kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Spika, *TRA,* ni chombo kilichopewa mamlaka ya kukusanya mapato Tanzania nzima. *TRA* waliopo Zanzibar na waliopo Dar es Salaam wote wanakusanya mapato kwa Taifa la Tanzania, sasa inakuwaje mzigo ulioshuka bandari ya Zanzibar utozwe mara mbili? Inashangaza sana kwa chombo hiki cha *TRA* kwa sababu mizigo yote inayotoka nje ya nchi kwa kupitia mipaka ya Bara, kama Kenya, Uganda, Rwanda, Burudi na nchi mbalimbali unatozwa kodi mara moja tu na ilihali mamlaka inayotoza kodi ni *TRA* ambayo ipo Zanzibar na Dar es Salaam ipo mipaka ya Tanzania yote.

Kwa nini mizigo inayopitia mipakani ikishatolewa kodi mara moja tu inakwenda popote ndani ya Tanzania pasipo kubugudhiwa? Sote ni Watanzania ukiwa Zanzibar ukiwa Bukoba ukiwa Mkoa wowote na sheria inahitaji kufuatwa na wote. Kwa hiyo, kama *TRA* ni chombo kilichopo kisheria na kwa Watanzania basi haki itendeke kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia wavuvi wa Dago wanaotoka Zanzibar na kuvua Tanzania Bara na wao wanasumbuliwa na mamlaka husika. Wavuvi wa Dago wanapotoka Zanzibar wanatakiwa kukata leseni za ubaharia pamoja na leseni ya chombo kwa Afisa wa Uvuvi Wilaya husika. Pia hupatiwa karatasi maalum inayowaruhusu kwenda Dago. Jambo la kusikitisha pamoja na *document* zote walizonazo ambazo ni halali lakini wavuvi hawa wadogowadogo ambao ni Watanzania pia, wanavua Tanzania samaki wanauza Tanzania ambapo Serikali imekusudia kuboresha maisha ya kila Mtanzania kibali alichopewa na Afisa wa Uvuvi Zanzibar hakitambuliki Bara, huu ni usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia utamaduni wa asili wa Mtanzania ambao ni utamaduni wa urithi wa Tanzania ambao umepata heshima duniani kote. Utamaduni ambao nazungumzia ni upendo, huruma na kusaidiana. Vitu hivi vinatoweka kwa kasi sana na kama juhudi za makusudi hazitachukuliwa basi utamaduni huu utatoweka.

Mheshimiwa Spika, utamaduni huu uliruhusu watu kusaidiana katika majanga kama moto, ajali za barabarani na mambo mbalimbali. Popote unapotokea moto mfano nyumba kuungua watu wakishikamana kwa nguvu zao zote kuzima moto huo. Vitu vitakavyookolewa vyote vitakuwa salama pasipo kuibiwa wala kupotea chochote. Kwa kuwa sasa utamaduni huu unaondoka ikiungua nyumba moto, watu wengi wanaokwenda kwenye tukio hilo hawaendi kusaidia kuzima moto bali wengi wao wanaenda kuiba vitu vilivyookolewa, hapana upendo, huruma wala kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani, tulipokuwa na utamaduni huu ikitokea watu wote wanakimbilia kuwaokoa watu waliojeruhiwa pamoja na kutunza mali zao.

Wanahudumiwa vizuri pamoja na mali zao zote pasipo kupotea. Sasa ikitokea ajali ya gari barabarani wengi wao hawakimbilii kuokoa abiria na mali zao, wanakimbilia kuwaibia kila kitu walichonacho badala ya kuwasaidia. Utamaduni wa upendo, huruma na kusaidiana unaondoka.

Mheshimiwa Spika, kuondoka kwa utamaduni huu ndio kumepelekea watu kuwa kama wanyama, sasa imefikia watu kukatwa mikono, kuchunwa ngozi hata *Albino* kuuwawa, haya yote ni matunda machungu ya kuondoka utamaduni tulioirithi kwa wazazi wetu. Upendo, huruma na kusaidiana vimeondoka matokeo yake ni hayo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri walioko katika ofisi yake, Watendaji wote kuanzia Makatibu Wakuu, kwa hotuba nzuri na zenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo mambo kadhaa ya kuchangia ili tuweze kuboresha hasa katika utekelezaji na usimamiaji wa mipango yote iliyowekwa ili kukidhi haja na lengo au makusudi ya hotuba hii nzuri ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ili mipango yote itekelezeke vizuri na ifanikiwe, ni lazima Watendaji kwenye maeneo husika wawe na uzalendo wa kujivika jukumu kwa moyo wa dhati katika kutekeleza mipango yote iliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, nianze na Hazina, kumekuwa na mazoea ya Hazina kutotoa fedha tunazopitisha hapa Bungeni kwa wakati muafaka mbaya zaidi fedha hutolewa kidogokidogo na inakuwa ya kushangaza zaidi pale wanapoishia kutoa fedha nusu au hata nusu ya bajeti iliyoombwa haifiki, ajabu! Sasa hapo tuelewe nini kwamba fedha hakuna ama vipi kwa kuwa tunapopitisha hapa Bungeni waridhia kuwa wataweza kutoa fedha hizo iweje wasimalize zote? Hapa nitajibiwa kuwa ni fedha za wafadhili ndio huwa haziji zote, sio kweli, naomba tu Serikali ijibu kwa nini fedha hazitolewi zote? Hayo malengo yatatimiaje?

Mheshimiwa Spika, Halmashauri/Manispaa na kadhalika bado kuna mianya ya kutowajibika ipasavyo katika kuzitumia fedha za miradi ipasavyo. Naomba uwekwe utaratibu mpya wa kukagua *(Value for money),* Kamati ya *LAAC* haitoshi. Pia nashauri Wabunge wote wa Wilaya au Halmashauri husika wawe wanapatiwa orodha ya miradi iliyotengewa fedha kwenye maeneo yao na kiasi cha fedha kwa kila mradi; pia Madiwani wote wapewe kwa ufuatiliaji zaidi wenye Ilani yao (CCM (W)) Katibu, wapatiwe *copy* ili waweze kufuatilia wanapokuwa katika shughuli zao za kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama chao. Hiyo itasaida kuharakisha maendeleo katika maeneo husika. Maana ninahisi kwamba kuna baadhi ya Watendaji hukwamisha miradi isitekelezeke kwa maana ya kukikomoa Chama Tawala kionekane hakiwezi kuleta maendeleo ya wananchi, kitu ambacho ni dhambi kubwa sana mbele za Mungu.

Mheshimiwa Spika, *TRA,* ili mipango yote tuliyopanga ifanikiwe katika suala la utekelezaji, Serikali inahitaji fedha za kutosha na kwa wakati tena ni fedha toka

makusanyo ya kodi, lakini mimi naona bado *TRA* hawajaweza kukusanya fedha kiasi cha kutosha kutokana na idadi ya Watanzania waliopo. Inasemekana *TRA* wanakusanya kidogo sana ni kama watu milioni moja tu wanaolipa kodi, wengine wote hukwepa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara wakati akichangia hoja ya bajeti alikuwa akijibu swali la Mbunge, alitueleza kuwa si chini ya Watanzania milioni 20 wanaomiliki simu za mkono, je, hao nao si ni watu wazima hata tukitoa wanafunzi na wategemezi, hata tukisema watu milioni tano walipe *VAT,* ni kiasi gani cha fedha tutakuwa tumepata? Hapo bado kuna wafanyabiashara wakubwa, ukweli kuna ukwepaji mkubwa wa kulipa *VAT* na *TRA* sielewi wanakuwa wapi, mfano Kariakoo mtu anakwenda kununua kitu, anaambiwa je, nikupe bei ya *VAT* au ya kawaida bila risiti? Mtu ananunua bila risiti, *TRA* wako wapi? Mwisho wa mwaka mtu anakuwa amefanya biashara kwa kutokulipa *VAT* kwa kiwango kikubwa sana. Hivyo, *TRA* hebu wapanue wigo wa kukusanya fedha hasa kwenye maduka na wafanyabiashara wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupanua wigo wa kulipa kodi bado wamekuwa kwenye kona iliyojificha kwani *TRA* hawatajwi kwenye suala la rushwa, tunasikia tu kwenye maeneo mengine kama barabarani, hospitali, Mahakamani na kadhalika lakini *TRA* hawatajwi. Mimi kwa mtazamo wangu, naona pia kule kuna mianya ya rushwa kwa sababu ile hali tu ya *TRA* kuweka viwango vya kodi na yenyewe kukusanya, hiyo mimi inanipa shaka. Naomba niishauri Serikali kuwe na chombo kitakachompangia kiwango cha kukusanya na *TRA* ikusanye tu. Haiwezekani ijipangie na ikusanye yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu amenunua nyumba, *TRA* wanajadiliana na mhusika na kisha anaombwa kupunguza na *TRA* anamkadiria na kumlipisha, inakuja kweli? Kama sio mwanya wa rushwa hapo ni nini? Naomba kuwe na chombo cha kusimamia *TRA* na kumsaidia kuweka viwango au kukadiria ili kuongeza pato la Taifa. Taasisi au chombo kikishakadiria, *TRA* ni kukusanya tu hakuna longolongo wala kujadili tena.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 ilitungwa sheria ya kuzilinda hatimiliki na hakimiliki kupitia chombo cha kutetea kazi za sanaa *COSOTA.* Sheria hii kwa mtazamo wangu, haijawa na mafanikio makubwa kwa Wasanii na Taifa kutokana na sababu ya ukosefu wa maandalizi ya kutosha ya wadau na vyombo vya dola, mfano Polisi, Mamlaka ya Mapato *(TRA),* Mahakama, wasambazaji na kadhalika matokeo yake sheria ikaanzishwa bila utekelezaji. Pia Askari wakuu wa kulinda haki za wasanii ambao ni Watanzania hawana taarifa yoyote juu ya sheria hii na kama wanauelewa ni mdogo sana kwa wachache.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi pamoja na sheria kuwepo tena yenye viwango vya kimataifa, bado wasanii wa Tanzania wamekuwa ni vibarua wa matajiri wachache ambao ndio wasambazaji wa kazi za wasanii ambao wanaingia mikataba ambayo mimi naiona ni batili ya kulinda unyonyaji huo huku Serikali ikiwa haina hata taarifa na wala haitaki kujua taarifa zao, kwani hunyanyaswa bila mtetezi, nyimbo zao kunakiliwa na kutolewa *copy* ndani na nje ya nchi. Kweli inatia uchungu sana. Pamoja na hayo, nyimbo na kazi za sanaa, zimekuwa ni muhimu kwa sherehe zetu zote, harusi, msiba, dhifa mbalimbali,

mikutano ya hadhara, kuhamasisha pia redioni, TV, lakini bado wasanii wa Tanzania hawatambuliwi kama sehemu muhimu kwa uchumi na ajira Tanzania. Matokeo yake nchi yetu haifaidiki kabisa kutokana na fani hii.

Mheshimiwa Spika, sanaa ya mziki na filamu, ukizingatia kwamba Tanzania ndio asili ya wimbo uliouzwa mamilioni ya santuli duniani, wimbo wa malaika, ukizingatia vilevile ubunifu wa kisanii wa upigaji ngoma wa mzee wetu Mourise Nyunyusa ambao ulitingisha dunia na kuigwa na wasanii wengi walipotumbuiza Japan Osaka mwaka 1970, pia ukizingatia utunzi wa wimbo wa Asha wa Tabora Jazband wa wana Segere Matata wa miaka ya 1970, umeendelea kupigwa upya na Band mbalimbali za kimataifa akiwemo Lokasa ya Mbongo na ukizingatia kuwa utunzi wa Kitanzania wa wimbo wa Dezodezo uliotungwa na Ndala Kasheba uliimbwa na kupigwa upya Ufaransa na kuzua mgogoro mkubwa wa kisheria. Mifano hii yote inatosha kuelezea hazina kubwa ya ubunifu wa sanaa tuliyonayo Tanzania ambayo inaweza kuwa ni kipato kikubwa kwa wasanii wa Tanzania na kipato kwa Taifa pia kama ilivyo katika nchi nyingine zenye vipaji vya aina hiyo kama vile Brazil, Congo, Afrika Kusini na Marekani.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tulilonalo hapa Tanzania hatujajipanga kama Taifa kuwalinda Wasanii wetu dhidi ya Majangili wenye nguvu dhidi ya uharamia wa kazi za sanaa *(piracy)* ambayo imeshamiri ndani ya nchi na nje ya nchi yetu. Hakuna Taifa lililofaidika bila kuwekeza na pia kulinda hazina hiyo kwa nguvu ya dola. Ni lazima uwekeze ndipo upate.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu juu ya sanaa ya Tanzania ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, somo la hakimiliki na hatimiliki liwe sehemu maalum ya kozi zinazotolewa kwenye Vyuo vyote vya Polisi nchini pamoja na vyuo Vyote vya Biashara na Vyuo vya Kodi, kwani kwa njia hiyo tutapata kada mpya ya Watanzania wenye uelewa mpana wa masuala ya fani hii.

Pili, kipindi cha kubembelezana kimepita, Serikali izingatie sheria kwa kuwabana wasambazaji na wote wanaoingia mikataba feki na wasanii na wanao-*copy* kazi za wasanii kwa wizi *(piracy)* ili wasiendelee kuwanyonya wasanii.

Tatu, pia katika kuteua Bodi ya *COSATA* izingatiwe sifa za weledi wa wateuliwa, uelewa wa haki na hatimiliki na uadilifu (kwani anaweza akateuliwa Mkaguzi wa *CD*) hivyo akarubuni wajumbe wengine kutoweka mambo yatakayoziba mwanya wa yeye kuendeleza uharamia.

Nne, Tanzania bado hatuna Sera ya Sanaa, hivyo si rahisi kupiga hatua kwenda mbele bila sera ambayo ndio dira endelevu katika fani hiyo.

Tano, uongozi wa *COSOTA* uangaliwe upya ili kujiridhisha na utendaji kazi zao.

Sita, BASATA bado haina meno, kwani fungu au bajeti zao si za kufanyia kazi ya kumkomboa msanii, kama tumekusudia kweli, naomba iongezewe fedha.

Saba, ningeweza kusema *TRA* watoe *stiker* kwa kila kanda ya *CD* ili kuongeza pato la msanii na kulinda kazi ya msanii pia kuipatia Serikali mapato lakini nachelea kusema kwamba watazichakachua tu. Hebu Mawaziri wa Wizara husika wapate nafasi kwenda nchi za wenzetu, wakaone ni namna gani ambayo wameshatoka kwenye *stiker* na sasa wanatumia mitambo maalum (*electronics*) kuzuia wizi wa kazi za wasanii ili wailete hapa nchini.

Nane, mwisho kabisa, naomba ziwekwe taratibu au mpango mahsusi pamoja na *COSOTA*, BASATA kuwe na mpangilio mahsusi, usimamiwe na Wizara, kianzishwe Chama cha Wasanii wote wa nyanja za jukwaani Tanzania ambacho kitakuwa na sauti moja, kwani kwa sasa naona kuna utengano kidogo. Kitasaidia sana hata kutoa maamuzi na misimamo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kanuni zetu za Bunge, zinatubana Wabunge kuweza kutoa mawazo na mchango wetu kwa uhuru zaidi katika kuongea kwa kila aliyeomba na mimi ndiye niliyepitiwa na mstari wa kufunga kuongea, tafadhali naomba nipatiwe majibu yafuatayo:-

Kwanza, kwa nini Serikali ina kigugumizi katika kusimamia haki za wanawake wajane na watoto walioachwa na wazazi wao, katika kumaliza kesi zilizoko Mahakamani kwa kisingizio cha Dini na Mila?

Pili, je, kuna mikakati gani inayoenda sambamba kati ya kupunguza vifo vya wazazi wakati wa kujifungua na janga la Ukimwi? Kwani inaonekana Ukimwi unapewa kipaumbele kuliko vifo vya kinamama wajawazito na ndio maana Ukimwi fungu lake kubwa na ukawekwa kwa Waziri Mkuu kwenye maafa wakati ni wa kujitakia kuliko uzazi.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA**: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi zangu kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kwa hotuba nzuri aliyoitoa. Pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi nzuri sana kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya Awamu ya Nne, ilijiwekea malengo ambayo mengi yametekelezwa vizuri sana na inaendelea kuyatekeleza mengine. Kwa kazi nzuri hiyo, Serikali katika mpango wake wa usambazaji mbolea za ruzuku msimu uliopita na huu umeenda vizuri sana na kwa maeneo ya Mkoa wa Ruvuma tuliweza kuvuna mahindi mengi sana ya chakula na kwa mara ya kwanza Serikali ilinunua tani 50,000 kuhifadhi kwa ajili ya dhoruba ya njaa inapotokea. Kuna maeneo yameonyesha yana njaa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema humu Bungeni lakini sisi Ruvuma katika Hifadhi ya Taifa katika zile tani 50,000 ni tani 13,000 tu ndio zimehamishwa. Naiomba Serikali iongeze kasi ya kukichukua chakula kile na kukipeleka katika maeneo yaliyo na njaa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia mwaka huu Mkoa wetu wa Ruvuma umefanikiwa sana katika mazao ya chakula na biashara. Tunategemea kuvuna tani 120,000 na sasa ndio wakulima wanavuna. Nashauri tuhamishe mahindi yalipo katika hifadhi na tuweze kuingiza yanayovunwa sasa na pia kwa kuwa tuna maghala ya kutosha katika vijiji vyetu, tunaomba Taasisi ya Hifadhi ya Chakula wakanunue huko na kuyahifadhi kule kwa muda. Tunaomba idadi ya kuyanunua kwa tani iongezeke toka 50,000 ya mwaka jana angalau ifikie tani 80,000 mwaka huu. Mwisho, naomba Serikali itangeze bei ya kununulia mahindi mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA**: Mheshimiwa Spika, Shule za Sekondari za Kata, naishauri Serikali ifanye mpango maalum wa kupeleka Walimu, kujenga maabara, kupeleka vitabu na kuhakikisha kila darasa lina dawati bila kusahau Walimu walipwe stahili zao kwa wakati na wale Walimu wanaofanya kazi katika mazingara magumu wapewe motisha ambayo Serikali itaona inafaa bila kusahau kuwajengea nyumba Walimu hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Madiwani, kwa kuwa wengi wako chini kwa wananchi, inabidi Serikali iwajengee uwezo kwa kuwapa mafunzo ya uongozi, usimamizi wa fedha za umma na ufuatilaji wa miradi ya Halmashauri. Madiwani wapewe mishahara badala ya posho pekee yake ili wawezi kujikimu kimaisha na waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya pesa za umma kwenye Halmashauri zetu. Miradi mingi haitekelezwi kikamilifu na thamani ya fedha hailingani na hali halisi ya mradi uliokwishatekelezwa. Mifano iko mingi, cha msingi tusihamishe waliokosea hasa Wakurugenzi wa Halmashauri ila sheria iletwe Bungeni ili kipengele cha tozo kibadilishwe, Kamati ya Bunge ipewe meno itoe adhabu kwa wahusika moja kwa moja kama ilivyo nchini Uganda ambapo mtumishi akibainika na kosa hutiwa mikononi mwa Polisi kwa hatua za kisheria. Hii itasaidia kuwatia woga Watendaji wote wenye tabia za ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa Shule wafanye kazi ya kukagua shule zetu zote na waainishe kila tatizo lililoonekana ili Serikali isiache shule hata moja ili vigezo vya shule kukamilika visiwepo tena katika shule zetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kuwa na shule za *A-level* katika kila Kata hapo baadaye hii itasaidia wanafunzi kuona ipo haja ya kuendelea zaidi na Kidato cha Tano na Sita. Vivyohivyo ni muhimu Serikali yetu ijenge Vyuo vya Ufundi katika kila Wilaya lakini vile Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Serikali ishirikiane na Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili ziboreshe mitaala inayotakiwa ili vyuo hivyo viwasaidie watoto walioshindwa kuendelea na masomo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Viti Maalum hawaingii katika vikao vya Halmashauri vya Kamati za Fedha lakini hapa Bungeni Wabunge wote wanaingia katika

Kamati za Uchumi na Fedha. Serikali ibadilishe sheria inayomkataa Mbunge wa Viti Maalum kuingia katika Kamati za Fedha katika Halmashauri zetu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache yahusuyo hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita kwenye aya ya 17, ukurasa wa 10 wa Hotuba ya Waziri Mkuu ambaye ndiye kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Aya hii inazungumzia Bunge katika ujumla wake, aidha aya hii inataja mikutano ya Bunge iliyofanyika. Nitachangia maeneo mawili, maswali kwa Waziri Mkuu na uharaka kwa Katibu wa Bunge kurekebisha upotoshwaji. Kwenye hiyo Mikutano minne, moja ya shughuli za Bunge zilizofanyika ni maswali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, *framers* wa Kanuni za Bunge walipoingiza kipengele cha maswali kwa Waziri Mkuu pengine walikuwa na nia nzuri ya kuingiza kipengele hiki. Utaratibu huu nadhani wahusika hao "*framer*s" waliiga toka Bunge la Uingereza ambako kila siku ya Alhamisi Waziri Mkuu wa nchi hiyo huulizwa maswali.

Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wangu mdogo wa eneo hili, nchini Uingereza Waziri Mkuu ana *Executive Powers* na huulizwa maswali yahusuyo sera na si maswali yanayohusu Wizara. Hapa kwetu nielewavyo mimi Waziri Mkuu anayeulizwa maswali hana *Executive Powers,* mwenye *Executive Powers* ni Rais ambaye si Mbunge. Aidha, maswali yanayoulizwa si ya kisera hata kidogo ni maswali yanayohusu Wizara zinazohusika moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano kadhaa ya kuthibitisha hili ninalolisema, katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Saba, tarehe 14/04/2011, Mheshimiwa Murtaza Magungu, alimuuliza Waziri Mkuu swali lifuatalo, ninanukuu:-

*"Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ni kiungo muhimu sana katika kuleta maendeleo katika nchi yetu. Je, kwa nini barabara ya Ndundu – Somanga ambayo ndiyo itafungua uchumi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara inasuasua?"* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Nne, Kikao cha Tisa, tarehe 4/02/2010, Mheshimiwa F. Nkayamba pamoja na kuwa ilimchukua muda mrefu kutoa maelezo kabla hajauliza swali na hivyo kukatizwakatizwa na aliyekuwa amekalia Kiti (Naibu Spika Mheshimiwa Anne Makinda), naomba nimnukuu Mheshimiwa Naibu Spika alivyomueleza.

*"Nkayamba, hilo wala sio swali ni hotuba kubwa kabisa"*

Mheshimiwa Spika, swali lake lilikuwa:-

*"Ni lini barabara ya kuanzia Mwandinga mpaka Manyovu yenye kilo mita 60 itajengwa"?* Mwisho wa kununukuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha Nane, tarehe 22/04/201, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa aliuliza swali lifuatalo, naomba kunukuu.

*"Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi bilioni 22 na kuzikabidhi Benki ya Rasilimali ya Tanzania kwa ajili ya mikopo kwa wakulima lakini Benki hiyo sharti lao mojawapo ni kwamba mkulima hawezi kupata mkopo mpaka awe amechangia asilimia kumi ambayo kwa bei ya sasa ya trekta ni sawasawa na shilingi milioni kumi, wakati Benki ya kigeni ambayo iko "Rederal Bank of Middle East" inatoa asilimia tano ambayo ni sawasawa na shilingi milioni tano. Je, haoni sasa ni wakati muafaka kutoa nafuu zaidi kwa wakulima wetu kupitia hili dirisha la kilimo".*

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache tu inayoonyesha kuwa maswali anayoulizwa Waziri Mkuu wangeulizwa Mawaziri wahusika moja kwa moja wangepata majibu yenye kina. Katika hatua hii, ni maoni yangu kuwa dhamira ya "*Framers*" wa Kanuni hii imefutika au kwa Lugha ya Kiingereza imekuwa "*defeated*" na kwamba mimi sioni tena umuhimu wa Waziri Mkuu kuulizwa maswali.

Mheshimiwa Spika, nimesema dhamira imekuwa sio tu "*defeated*" lakini pia kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu kimetumiwa na baadhi ya Wabunge kumdhalilisha Waziri Mkuu au kukidhalilisha kiti cha Waziri Mkuu katika hili. Mifano ipo mingi lakini nitatoa mmoja ambao ulijitokeza katika Mkutano wa Pili, Kikao cha Tatu, tarehe 10/02/2011. Kwenye kikao hicho, Mheshimiwa Godbless S. Lema alinukuliwa akisema hivi, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 68(7), naomba kupata ufafanuzi kwamba Mbunge anaweza akachukua hatua gani kama anaona mtu mwenye nafasi kubwa katika nchi kama Waziri Mkuu analidanganya Taifa na kudanganya Bunge. Ahsante".* Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Spika katika hili alisema hivi, nanukuu:-

*"Mheshimiwa Mbunge, Bunge hili lazima liwe na adabu inayostahili. Kwa hiyo, kama tutafanya Bunge letu hili ikawa ni mahali, sasa unataka kusema Waziri Mkuu kwa ahadi aliyoweka ndani ya Bunge hili anadanganya?*

Mheshimiwa Spika, hapa ilionekana wazi kuwa muuliza swali Mheshimiwa Lema lililenga kumdhalilisha Waziri Mkuu na ndiyo ilivyotokea.

Mheshimiwa Spika, namalizia eneo hili kwa kusema kuwa najiandaa kuleta Hoja Binafsi ya kupendekeza kuondolewa kwa Kanuni ya Maswali kwa Waziri Mkuu. Wakati

najiandaa kufanya hivyo, nikuombe kwa yule atakayekuwa amekalia kiti kuyakataa maswali ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watu, vyombo vya habari, *NGO's* na kadhalika hupotosha mambo ama yanayohusu Spika ama Bunge kwa makusudi kabisa. Katika hatua kama hii, Ofisi ya Bunge kupitia kwa Katibu wa Bunge wawe wanajibu haraka kueleza hali halisi ili Bunge liwe katika uhalisia wake *(to put the House in order)* badala ya kukaa na kusubiri Spika ndiye aseme 'Hapana'. Utaratibu huo wa kukaa kimya sio mzuri kwa sababu, usipojibiwa itaonekana wazi kuwa uwongo au upotoshwaji huo kwa makusudi ni kweli.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kuna wageni wangu wengine, nikipata orodha nitawatambulisha, sijapata majina yao. Nitawatambulisha yakipatikana majina; si mnawaona huko juu, lakini nitawatambulisha baadaye. Kwa hiyo, tunaendelea, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, ninapenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha leo kuwa hapa mbele yako na kufanya tendo la kihistoria kwangu la kuwasilisha na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mkuu.

Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniamini na kunipa wadhifa na dhamana kubwa ya kushughulikia elimu nchini. Ahadi yangu kwake ni kufanya kazi kwa bidii na uwezo wangu wote. Ninakishukuru pia Chama changu cha Mapinduzi na Kamati ya Siasa Wilaya ya Ruangwa na Mkoa wa Lindi, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuniwezesha kupata ushindi mnono.

Ninaishukuru sana familia yangu, ikiongozwa na mke wangu, Mrs. Majaliwa na watoto wangu; Saad, Rehema Majaliwa na dada yao Furaha, kwa kuniunga mkono kwa dhati kwa shughuli zangu za kila siku. Nichuke fursa hii pia kukupongeza wewe, kwa kuteuliwa kwako kuwa Spika na kwa kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke Afrika Mashariki, akifuatia yule wa Uaganda; hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia nimpongeze Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Bunge hili kwa nguvu moja; ni kweli kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ana uwezo mkubwa, anayo busara ya kutosha, msikivu na mwenye uwezo wa kufanya maamuzi magumu; hongera pia. *(Makofi)*

Nimpongeze pia Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mckuchika, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais, kuwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI. Ninakiri anao uwezo mkubwa sana, hongera sana. Ninampongeza pia pacha wangu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri (TAMISEMI), kwa kipindi kingine. Ninatambua sana mchango wake kwangu. Mwisho, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, kwa ushindi mnono mlioupata kwenye Majimbo yenu; ninawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wafuatao, ambao wamechagia kuhusu Sekta ya Elimu, kwa maandishi na kwa kusema kama ifuatavyo: Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa January Makamba, Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa Michael Lekule Laizar, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Diana Chilolo Mkumbo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Mohamed Mahamoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum. Ningeweza kuwataja wote, lakini hawa wanatosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, ambazo zilijikita katika maeneo yafuatayo: Upungufu wa Walimu; upungufu wa miundombinu; mfumo wa ruzuku ya uendeshaji (*capitation grant);* vitabu na vifaa vya kufundishia; elimu kwa watoto wenye ulemavu; na malipo stahili ya Walimu na utoaji motisha.

Mheshimiwa Spika, hoja namba moja; upungufu wa Walimu. Serikali inatambua kuwa, uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini, unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Walimu ukilinganisha na idadi ya Wanafunzi waliopo shuleni. Kwa Elimu ya Msingi na Sekondari, mahitaji ya Walimu waliopo ni kama ambavyo inaonesha. Elimu ya msingi, tuna mahitaji ya Walimu 214,468, waliopo sasa ni 167,904 na tuna upungufu wa Walimu 46,564.

Kwa Elimu ya Sekondari mahitaji yetu Walimu 81,800, waliopo ni 44,573 na tuna upungufu wa Walimu 37,227. Upungufu wa Elimu ya Sekondari unajitokeza zaidi kwenye masomo ya sayansi, ambayo ni hisabati, kemia, baiolojia na fizikia.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012, wapo Walimu 13,737, kati ya hao; wanachuo 7,188 wanaosomea stashahada na 6,649 wa shahada wakiwemo Walimu wa masomo ya sayansi. Kwa upande wa Elimu ya Msingi, wapo wanachuo 11,196 waliohitimu mafunzo ya miaka miwili, ambao sasa wanatarajiwa kuajiliwa katika mwaka huu wa fedha na wataweza kuajiriwa kadiri watakavyofaulu masomo yao. Serikali ina mkakati wa kuendelea kudahili Wanafunzi ili kuongeza idadi ya Walimu wanaohitimu ili kupanga kufundisha katika shule zetu za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011/2012, jumla ya wanachuo 24,697 watadahiliwa kujiunga na masomo kwa ngazi ya stashahada na Daraja la Tatu A katika vyuo mbalimbali nchini. Vilevile vyuo binafsi vinavyotoa mafunzo ya ualimu, vimeelekezwa kudahili wanachuo wengi wenye sifa; na watakaofaulu, Serikali itawaajiri na kuwapanga katika Utumishi wa Umma. Matarajio yetu ni kuwa, katika miaka mitatu ijayo, suala la upungufu wa Walimu katika shule zetu linatarajiwa kufikia zaidi ya asilimia 85.

Mheshimiwa Spika, hoja namba mbili ni upungufu wa miundombinu. Changamoto nyingine ni upungufu wa miundombinu katika Shule zetu za Msingi na

Sekondari. Upungufu huu upo katika vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu, maabara, vyoo na madawati. Upungufu huu ni kama kama ifuatavyo: Mahitaji yetu vyumba vya madarasa ni 198,607 yaliyopo sasa ni 110,342 tuna upungufu wa vyumba vya madarasa 88,265; nyumba za Walimu mahitaji yetu ni 197,519, nyumba zilizopo ni 39,623, tuna upungufu wa nyumba 158,956; matundu ya vyoo, mahitaji yetu 381,241, yaliyopo ni 163,473 na tuna upungufu wa 218,011; na madawati, mahitaji halisi ni 3,359,691, madawati yaliyopo ni 2,028,518, tuna upungufu wa madawati 1,327,963.

Elimu ya Sekondari, vyumba vya madarasa mahitaji yetu ni vyumba 70,102, vilivyopo ni 45,645; tuna upungufu wa madarasa 24,457; tuna mahitaji ya nyumba za Walimu 61,904, nyumba zilizopo 20,187 na tuna upungufu wa nyumba 41,717; matundu ya vyoo, mahitaji yetu ni 76,097, yaliyopo ni 38,820 na tuna upungufu wa matundu ya vyoo 37,277; na maabara, mahitaji yetu ni 17,571, maabara zilizopo ni 7,680, tuna upungufu wa maabara 9,891.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), imepeleka shilingi bilioni 9.4 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa mwaka 2010/2011, kwa ajili ya ujenzi wa maabara, nyumba za Walimu na ukarabati wa shule mbalimbali, kwa lengo la kupunguza uhaba wa maabara na nyumba za Walimu katika Shule za Sekondari.

Kwa upande wa Elimu ya Msingi, jumla ya shilingi bilioni tano zimepelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kujenga nyumba za Walimu na kutengeneza madawati. Kupitia MMES, kwa mwaka 2011/2012, Serikali itajenga miundombinu muhimu ikiwemo nyumba, maabara, madarasa, maktaba na vyoo kwenye Shule za Sekondari za Kata 500. Lengo la Serikali ni kuzifanya shule hizi kuwa *functional,* kwa maana ya kuziwezesha kutoa Elimu ya Sekondari iliyo kamilifu na bora kwa manufaa ya Wanafunzi¸ Walimu, Wazazi na Jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwenye ngazi ya Elimu ya Msingi, Serikali itaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo Wazazi na Wananchi kwa ujumla, kushiriki katika kuongeza miundombinu muhimu katika shule hizo. Lengo ni kuwa na Shule za Msingi zenye miundombinu bora ili kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tatu ni mfumo wa fedha za uendeshaji shule, *Capitation Grant.* Serikali inazipatia Shule za Msingi na Sekondari, fedha za uendeshaji kwa ajili ya kuendesha shule kwa kununua vitabu, kufanya ukarabati, kununua vifaa vya kufundishia, utawala na kufanya mitihani ya ndani. Kwa upande wa Sekondari, fedha hizo hutumika kununulia vitabu vya kufundishia na kujifunzia, kununua vifaa vya maabara, vifaa vya kufundishia kama chaki, daftari, kalamu, vifaa vya michezo na kadhalika. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, umelenga kutoa shilingi 25 kwa kila Mwanafunzi kwa ruzuku ya uendeshaji kwa mwaka. Kwa mwaka 2010/2011, Serikali imetoa shilingi bilioni 41.2 kwa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shule za Msingi, lengo ni kutoa shilingi 10,000 kwa Mwanafunzi kwa mwaka. Dhamira ya Serikali ni kwamba, fedha za

uendeshaji wa Shule za Msingi zinafikia shilingi 10,000 kwa kila Mwanafunzi kwa mwaka kama ilivyokusudiwa. Mwito kwa Serikali ni kuwa, mamlaka za Serikali za Mitaa, zisimamie Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari, kutuma takwimu sahihi za idadi ya Wanafunzi ili kuhakikisha fedha zinazotolewa zinatumiwa kama ilivyokusudiwa na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hoja namba nne; vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali imekuwa inatoa fedha katika Shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kupitia Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari tangu Mipango hii ilipoanza kutekelezwa mwaka 2001/2002 na 2004/2005 sawia. Miaka iliyopita ununuzi wa vitabu katika Shule za Msingi haukufanyika vizuri. Serikali ilikuwa inapeleka fedha katika Halmashauri na baadaye fedha hizo kupelekwa shuleni, vitabu kwa kiasi kikubwa havikununuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua matatizo hayo, mwaka 2011/2012, Serikali imetenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kununua vitabu na vitabu hivyo vitanunuliwa na Serikali na kuvipeleka shuleni kupitia kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Lengo la Serikali ni kuona kwamba, ifikapo mwaka 2015, kila Mwanafunzi awe na kitabu chake yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha za *capitation* zinazotolewa kwa Shule za Sekondari**,** Serikali ilipata msaada wa vitabu 800,000 kutoka Serikali ya Watu wa Marekani kupitia Shirika la *USAID*, ambavyo viligawiwa katika shule mbalimbali za sekondari nchini kusaidia kupunguza upungufu wa vitabu vya sayansi na hisabati shuleni na hivyo kuimarisha ufundishaji na kujifunza. Ahadi ya Serikali ya Marekani ni kutoa msaada, vitabu milioni mbili tena katika Shule za Sekondari Nchini Tanzania, lengo ni kila Mwanafunzi kuwa na kitabu chake; hilo lengo litafikiwa.

Hoja namba tano; elimu kwa walemavu. Mfumo wa elimu nchini, umelenga kutoa elimu kwa walemavu. Mfumo wa elimu nchini, umelenga kutoa elimu kwa watoto wote hususan Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na inatolewa kwa makundi yote kadiri wanavyofaulu kujiunga katika hatua nyingine ya elimu wakiwemo walemavu pia. Takwimu zilizopo zinaonesha katika ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, wapo Wanafunzi Walemavu tena Wavulana kwa Wasichana, ambao wanapata elimu hiyo kama ifuatavyo:-

Elimu ya Awali, tuna jumla ya watoto walemavu 1,771, Elimu ya Msingi tuna jumla ya watoto walemavu 36,585, Sekondari kuna watoto 5,265 na kufanya jumla watoto 43,621, ambao wamegawanyika katika makundi ya wavulana na wasichana; wasichana 18,196 na wavulana 25,425.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inaangalia kwa makini suala la kuwapatia elimu watoto wenye ulemavu wa aina zote kadiri unavyojitokeza. Tatizo lipo kwa wazazi au walezi ambao huwaficha watoto wao majumbani, badala ya kuwapeleka shuleni ili wapate elimu kama watoto wengine. Vilevile Serikali imekuwa inahimiza na kusisitiza ujenzi wa miundombinu inayozingatia mahitaji ya kundi hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo; Serikali kwa kutambua umuhimu wa michezo shuleni, imerejesha michezo mashuleni kwa lengo ya kuibua vipaji miongoni mwa Wanafunzi katika nyanja mbalimbali kama vile riadha, mpira wa miguu, pete, kikapu, wavu, ngonjera, mashairi na nyimbo. Kwa upande wa michezo ya Wanafunzi wa Sekondari, Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISET)A, imerejeshwa miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Michezo na Taaluma za Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA), michezo hiyo imerejeshwa mwaka 2010 kwa kushirikisha wanamichezo kutoka mikoa 11, wakiwemo Wanafunzi wenye ulemavu ambao waliundiwa mkoa wao. Kwa mwaka 2011, michezo hiyo imejumuisha mikoa yote 21 ya Tanzania Bara na Wanafunzi Walemavu wameshiriki katika michezo hiyo kulingana na uwezo wao. Michezo ya UMITASHUMTA imefunguliwa tarehe 28 mwezi Juni mwaka huu katika Viwanja vya Michezo Shirika la Elimu Kibaha. Hivi sasa michezo hiyo inaendelea na itafungwa tarehe 7 Julai, mwaka huu wa 2011.

Hoja namba sita; stahili za Walimu. Serikali imekuwa inajali maslahi ya Walimu. Fedha zimekuwa zinatengwa katika bajeti za mamlaka ya Serikali za Mitaa kila mwaka kulipia stahili hilo kama likizo, uhamisho, masomo na posho ya kujikimu. Fedha za Serikali hutolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha, kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Fedha. Walimu wapya wanaoajiriwa hulipwa posho ya kuanza kazi, hurejeshewa nauli waliyotumia kwenda kwenye kituo cha kazi alichopangiwa na fedha za kusafirisha mizigo hadi kituo kipya cha kazi. Fedha hizo zinalipwa baada ya mwajiri kuhakiki uwepo wa mizigo hiyo usizidi uzito wa tani moja. Serikali itaendelea kulipa stahili hizo kwa watumishi, kwa kuzingatia miongozo ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la Walimu kuchelewa kulipwa mishahara baada ya kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa. Kwa Walimu walioripoti kwa muda mwafaka na kujaza fomu za kuthibitisha ajira na kuziwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, walilipwa mishahara yao baada ya kuingizwa kwenye kompyuta. Tatizo la kuchelewa kwa mishahara ni pale Walimu wanapochelewa kwenda kuripoti kwa wakati na wengine kutokuwa na nyaraka kama vyeti, kuthibitisha ufaulu wao wa masomo. Wengine huchelewa kujaza fomu hizo na zingine hujazwa visivyo; hivyo, hulazimika kujaza upya. Hali hii huchelewesha malipo ya mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, suala la motisha: Serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi, imejipanga vizuri katika kuona umuhimu wa motisha kwa Walimu, lakini siyo Walimu tu, pia Wanafunzi na Wazazi wao ambao hufanya kazi kubwa ya kuwaandaa watoto hawa kisaikolojia; kama leo mmeona hapa mbele yetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alivyotoa zawadi. Kwa kauli hii, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa pili, Mheshimiwa Mwanri, aweze kuchangia Hotuba yao.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba nichukue nafasi hii, kusema kwamba, mimi ninaunga mkono hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninasimama hapa, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa amenijalia nikaweza kupata nafasi hii na kuja Bungeni hapa. Kipekee, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Siha, ambao walinichagua mimi niweze kuwa Mbunge wao. Ninachoweza kusema kwa Wananchi wangu wa Siha ni kwamba, kama kazi inaua; mwaka huu itaniua. Nitafanya kazi kwa bidii sana, kuhakikisha kwamba, ninakidhi matarajio yao na matumaini yao. *(Makofi)*

Ninapenda nichukue nafasi hii pia kumshukuru mke wangu, Mama Grace Aggrey Mwanri, pamoja na watoto wangu. Ninajua kwamba, mke wangu ananiombea sana, wana maombi wananiombea sana. Kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana na ninajua ananisikiliza huko aliko. Mungu ambariki na ninawaombea watoto wangu pamoja na familia yangu yote, Mungu awabariki kwa sababu ninajua kwamba, kupitia nafasi hii wamekuwa wananikosa kwa muda mrefu. Ninapenda kumshukuru sana mke wangu kwa kunitia moyo. *(Makofi)*

Zaidi, ninaomba kuchukua nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Daktari; kwa heshima kubwa aliyonipatia ya kuwa msaidizi wake na kushirikiana na Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri ili tuweze kufanya kazi ya kulitumikia Taifa letu. Kipekee, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye amekuwa ni msaada mkubwa sana kwangu kwa maana kama Kiongozi wetu wa Wizara. Ametupa maelekezo mazuri na kila wakati amekuwa anatuonesha namna ya kufanya kazi yetu.

Ninapenda nichukue nafasi hii pia, kumshukuru Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Kiongozi wetu wa Wizara, ambaye tumekuwa tunashirikiana naye kwa karibu sana. Ninapenda kusema ninashukuru sana kwa maelekezo yake mazuri, ambayo amekuwa akiyatoa kwangu. Kipekee, nimshukuru ndugu yangu, Kassim Majaliwa, ambaye tunashirikiana kwa karibu sana. Sisi tunaitana pacha hapa, tunashirikiana, tunafanya kazi kwa pamoja. Ninapenda kusema kwamba, Ndugu Majaliwa, ninakushukuru sana kwa namna ambavyo tumekuwa tunashirikiana.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge wenzangu wote, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wananipa. Sina la kusema, ninachoweza kusema ni kwamba, nitashirikiana nanyi. Labda niseme tu kwamba, katika mazungumzo yote ambayo yamefanyika hapa, ninajua kwamba, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, atataja watu ambao wamezungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye atakayefanya kazi ile. Niseme nimejifunza nini kwanza ili niweze kusaidia, kwa sababu ninajua kwamba, mambo yaliyosemwa ni mengi. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atasema kwamba, kwa kweli mengi tutajibu kwa njia ya maandishi. Nimepata nafasi ya kukaa hapa,

nimesikiliza mazungumzo na kama Mbunge na kwa nafasi yangu kama Naibu Waziri, ni vizuri pia nikasema nimejifunza nini. Kuishi ni kujifunza na kujifunza ni kuishi vizuri zaidi. Cha kwanza, nimejifunza kwamba, linaposemwa jambo lolote ambalo kichwani mimi ninaona kama vile haliingii, yaani mtu anasema kitu unaona kama vile hakiingii kichwani kwangu.

Mheshimiwa Spika, wakati huu nimejifunza kwamba, ndiyo wakati wa kusikiliza sana. Ninaomba Wabunge wenzangu, akisimama mwenzetu hapa, sisi tuna *background* tofauti tofauti, mtu akisema jambo lolote ambalo unajisikia kwamba hulipendelei, mimi ninadhani wakati huo ndiyo wa kusikiliza sana. Haya ni maoni yangu binafsi mimi Aggrey Mwanri. Ukikaa hapa la pili ambalo nimejifunza ni kwamba, sina haja ya kuangalia ni nani anayezungumza; ninachotakiwa kufanya hapa ni kusema ni nini kinachozungumzwa. *(Makofi)*

Nani anayezungumza *background* yake na nini. Kwa maoni yangu, kwa namna tulivyokaa humu ndani na mchanganyiko wetu, haina maana sana. Kwa nini sisi sote tumekuja hapa ni Wabunge; haijalishi alifanya nini huko mpaka akafika hapa. Tukija hapa kwa maoni yangu kwa sababu ni wajibu wangu kama Mbunge na mimi kutoa maoni yangu kwamba, tufanye nini. Moja ya mambo makubwa ambayo tunatakiwa kufanya hapa ndani ni kunyanyua kiwango cha mjadala uliomo humu ndani. Kwa hiyo, likisemwa jambo jema, mimi siangalii nani amelisema, ninachoangalia ni nini kilichosemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimejifunza kwamba, kuna haja ya kuwa na uvumilivu, kila mmoja kumvumilia mwenzake. Sisi sote ni Watanzania, lakini kila mmoja hapa ana namna anavyojisikia. Leo kimefanyika kitu kikubwa hapa, tumewaona Wanafunzi wetu wamekuja hapa. Sisi tulikuwa tunasema kwamba, shule hizi ambazo zimeanzishwa zinaitwa *Voda Faster, Yebo Yebo* na nini, lakini leo tumepata ushahidi wa waziwazi hapa kwamba, shule hizi zimefanya kazi kubwa na leo ushuhuda umetoka hapa kwamba, kazi tuliyofanya, tulipoamua kwamba tusomeshe watoto wetu katika Shule za Kata, maoni yale na mawazo yale, yalikuwa ya busara na sasa tuendelee kufanya kazi zaidi ili kuhakikisha watoto wetu wanasoma. Nilitaka niseme haya kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumza humu ndani, wamezungumzia kuhusu tatizo la Watendaji wetu walioko katika Wilaya na katika Mikoa na katika Halmashauri zetu, kutokufanya kazi zao vizuri. Mawazo haya, Mheshimiwa Pindi Chana ameyazungumzia, Mheshimiwa Jenister Mhagama, ameyazungumzia na Wabunge wengine wengi sitaki kutaja majina, kwa sababu majina ni mengi sana, nikitumia nafasi hii kwa muda ulionipa hapa sitaweza kumaliza. Tunachozungumza katika Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa tunasema kwamba, kuna kitu kinachoitwa *D by D; D by D* maana yake *Decentralization by Devolution,* maana yake ni kwamba, usifanye maamuzi Dodoma na Dar es Salaam, fanya maamuzi haya katika ngazi ya mamlaka zile za Halmashauri za Wilaya kwa kupitia Mabaraza ya Madiwani, wale ndiyo wafanye maamuzi.

La pili, linalosemwa pale, wape nyenzo za kufanyia maamuzi, yaani watumishi, magari, vifaa na fedha. Kwetu sisi hapa tunachokifanya ni kupeleka ruzuku ya Serikali katika Halmashauri. Kilichozungumzwa humu ndani na ambacho kimepigiwa kelele sana hapa ni kwamba, tunapokwenda katika Miradi mbalimbali ambayo inafanyiwa kazi katika Halmashauri zetu, hatupati kitu kinachoitwa thamani halisi ya pesa zilizokwenda katika Halmashauri. Hakuna mtu yeyote atakayesimama hapa ateetee kwamba, hali haipo hivyo, kwa sababu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Fedha za Serikali imethibitisha kwamba, matumizi yetu siyo mazuri.

Mtu anakwambia nimejenga darasa, nimeweka kitasa pale cha *union* cha shilingi 28,000, ukienda kuangalia kitasa kile siyo cha *union* kimechukuliwa tu mtaani kikapachikwa pale. Sasa tunafanya nini? Ninataka nikuthibitishie, jana nimezungumza katika *TBC* nimeeleza; wale wote ambao wanahusika na matatizo haya ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani, tutawachukulia hatua. Tumeanza kuwachukulia hatua. Jana nilikwenda kwenye *extent* ya kuanza kutaja na Halmashauri ambazo wengine tumewavua madaraka na wengine tumeamua kuwafukuza kazi. Hivi tunavyozungumza hapa, ninataka nikuthibitishie, zipo kesi zingine zimekwenda Mahakamani. Jana Mwandishi wa Habari yule aliniambia kwamba, kuwavua madaraka tu inatosha. Nikamwambia hapa tunazungumzia habari ya Utawala Bora.

Tunachotaka kuwaomba Wabunge mtusaidie. Ninyi mko kwenye hizi Halmashauri, utaratibu ulioko pale katika Halmashauri unataka Baraza la Madiwani lihakikishe kwamba, linasimamia shughuli zote zinazoendeshwa katika Halmashauri pale. *That is the bottom line.* Hapa kinachozungumzwa ni kujenga mfumo, kama hatukujenga mfumo hapa hatutaweza. Mheshimiwa Mkuchika, atoke hapa aende Newala, aende Mwanza, tutoke tuzunguke, hatutaweza, lakini tukiweka mfumo hapa ambao ukicheki utauona unafanya kazi itatusaidia sana. Halmashauri nne; Halmashauri ya Rombo, Halmashauri ya Mwanga, Halmashauri ya Kishapu na Halmashauri ya Kilwa, zimepata Hati Chafu. Halmashauri zilizobakia nyingine Hati zake siyo za Kuridhisha na sisi tumeeleza hapa na Wabunge wote wamezungumza hapa.

Tunachokifanya ni nini? Cha kwanza, tumeamua kwamba, tutaimarisha Sekretarieti zetu za Mkoa; ndiyo hatua ya kwanza. Kwanza, ukikaa Dodoma, ukakaa Dar es Salaam, ukasema utafanya tu mwenyewe na wananisikia na Viongozi wetu. Nichukue nafasi hii, wakati nilipokuwa ninazungumza watu ambao ninawashukuru kwa namna walivyotusaidia, sikuwataja Wakuu wa Mikoa; wametupa msaada mkubwa, wameshirikiana na sisi. Ninapenda nisimame hapa kusema kwamba, tunawashukuru sana. Makatibu Tawala wa Mikoa wametusaidia sana. Wakuu wetu wa Wilaya wametusaidia sana. Hii nguvu iliyoko hapa ni nguvu kubwa ambayo tukiamua tunaweza. Kwa hiyo, tunataka tuimarishe Sekretarieti zetu, tuhakikishe zinafanya kazi na tunapata matokeo tunayotaka kuyapata.

Kwa upande wa Watendaji wetu wa Vijiji na Kata, tumesema kila mmoja asimame katika nafasi yake; Diwani simama katika nafasi yako; Mwenyekiti wa Kijiji asimame katika nafasi yake. Taarifa ya mapato na matumizi; anapoondoka Mwenyekiti

wa Kijiji anapokwenda kwenye *Ward Development Committee* aende pale akiwa amebeba Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kila kikao. Mwenyekiti wake ni Diwani, ambaye ni Mwakilishi wa Wananchi, akifika pale kwanza nipe Taarifa ya Mapato na Matumizi. Wanapofanya vikao hivi kule katika Halmashauri, tumewaambia mkiona vikao vinavyofanyika pale mara kwa mara ni vya dharura; ni hatari hujapata kuona; vikao vya dharura havina yatokanayo.

Kwa hiyo, mkiona vikao vya dharura vinakuwa vingi, maana yake ni kwamba, huna taarifa ya mapato na matumizi; ng'ang'anieni hapo. Tumefika mahali sasa hivi tumeamua kwamba, Mkaguzi wetu wa Ndani hatawajibika tena kwa Mkurugenzi Mtendaji. Mkaguzi wetu wa Ndani atawajibika kwa Mkaguzi wa Ndani wa Taifa na tutamwondoa katika ile Ofisi pale ili wasije waka-*collude*. Tutumie nafasi hiyo, kila baada ya miezi mitatu tunataka tupate taarifa ya mapato na matumizi kupitia Mkaguzi huyu. Madiwani walioko kule, Wabunge, daini hizo taarifa za mapato na matumizi. Tusikae tu tukasema hapa, hili jambo tunyanyuke sisi wote kwa sababu linatuhusu.

Wapo Wabunge wengi tu wamezungumzia kuhusu kuanzishwa kwa mamlaka mpya; Mheshimiwa Jesnista Mhagama, Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Paul Lwanji. Tumemsikia akisema hapa, ukitoa hayo maeneo mapya ya mamlaka maana yake nini? Maana yake ni kwamba, unasogeza karibu zaidi na Wananchi. Sasa tumesema kwamba tufuate taratibu. Vile vigezo huwa tunawasomea hapa kila siku. Wapo Wabunge ambao wamekuja hapa, ambao wanazungumzia maeneo haya lakini ukicheki na *District Consultative Committee* hawajapeleka pale. Wakitoka pale ni lazima waende kwenye Baraza la Madiwani, wakitoka pale ni lazima waende kwenye *Regional Consultative Committee,* maana Baraza la Mkoa ndilo ambalo Mwenyekiti ni Mkuu wa Mkoa. Kama hajapita kule kwetu yakaja hapa tutayarudisha mpaka kule, yatacheleweshwa. Kwa hiyo, ninataka niseme kwamba, Wabunge wote ambao wamezungumzia kuhusu maeneo mapya ya utawala, tutaangalia kwa vigezo tulivyoweka hapa.

Wapo wengine wanasema vigezo hivi vimekaa vipi mbona havikidhi; sasa kama tunazungumzia habari ya kubadilisha vigezo, tuzungumze; lakini ukija kuniambia mimi niteremke pale kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, nitakachoangalia ni vigezo. Ninajua Mheshimiwa Jenista Mhagama, amezungumza hapa, nimekwenda Madaba ninapafahamu, ninajua eneo analolizungumza, tumewaambia watuletee taarifa yao sisi tutapitia hapo. Wale wa Mamlaka ya Miji Midogo tulishasema, kwanza, kazi ile ni nyepesi wala haina urasimu mwingi; wapitie waangalie vizuri, lakini wapite katika hizo ngazi ambazo nimezizungumzia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, zimezungumziwa Hospitali za Mikoa, lakini ninataka niizungumzie Hospitali moja ya Mawenzi. Hospitali ya Mawenzi, Mheshimiwa Lucy Owenya, ameizungumzia hapa; ni kweli tumekwenda, tumetafuta, tumeuliza, kwa sababu alisema Mheshimiwa kwamba, jengo lile limevunjwa!

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kukanusha hapa ni kidogo tu kwamba, jengo lile siyo kwamba lilipigwa chini lote, lakini zile kuta zote zilikwenda kuangushwa

zikaanguka chini. Ulikwenda ukaguzi pale kutoka Wizara ya Afya, wakaenda kukagua pale, *Elerai Contractors* ndiyo waliokuwa wanafanya kazi ile.

Mheshimiwa Spika, ninataka nikwambie, tumewaagiza na *RAS* ananisikiliza pale alipo, tunataka tufuatilie kwa karibu. Hela zilizotumika siyo shilingi 400,000, hela zilizotumika pale ni shilingi milioni 220 na hela zinazofanya kazi ya ukarabati ule siyo shilingi 700,000,000 kama ilivyosemwa hapa. Vyovyote vile ambavyo inazungumzwa hapa ni kwamba, kuna hasara ambayo imetokea pale na *TBA* ndiyo walikuwa wakaguzi pale. Sasa tumemwambia *RAS* tukimaliza kazi hapa, tunataka twende Moshi pale Mawenzi, tujue *exactly* ni nini kilichotokea katika Hospitali ya Wilaya ya Mawenzi.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, kama ana taarifa zaidi, ninazo taarifa hapa ambazo nimeshindwa kuzipitia kwa sababu muda ni mdogo na kengele imeshagongwa hapa, tutakwenda kuangalia. Wale wengine wote wanaozungumzia habari ya kupandisha hadhi hospitali za mikoa; agizo la Serikali lilishatoka likaagiza kwamba, Hospitali zote za Mikoa zitakuwa Hospitali za Rufaa. Kwa hiyo, hakuna haja kuomba, hospitali yoyote pale ilipo ni Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninatamka kwamba, ninaunga mkono hoja iliyoletwa hapa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa mawaidha, uvumilivu na mwone ninyi Waheshimiwa, hakuna kumwangalia mtu sura na hii sura ya vyama katika majadiliano ya Bungeni, ipungue kwa kiwango kikubwa, kwa sababu tunazungumzia mambo ya watu wote. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, ninaomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Pili, leo Watanzania tunaadhimisha Siku ya Serikali za Mitaa, ambayo Kitaifa inafanyika Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa. Nitumie nafasi hii, kuwapelekea salamu wenzangu wote tuliomo katika Serikali za Mitaa na kupongezana katika kuadhimisha siku ya leo. Hatukuweza Timu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuunganika nao kule Sumbawanga, kwa sababu ya majukumu ambayo tunayatekeleza hapa. Nichukue pia nafasi kuwapongeza Makomredi, Nchi Rafiki, *Peoples' Republic of China,* ambao *Comred Mao Se Tum,* tarehe kama ya leo mwaka 1949, alitangaza Jamhuri ile; nchi ambayo ni rafiki na tumefaidika nayo kwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua nafasi hii na mimi niwapongeze Wanafunzi waliofanya mtihani vizuri, ambao wamepongezwa leo. Sisi katika TAMISEMI tunaendesha shule, lakini anayesimamia masuala ya Taaluma, Waziri wa

Elimu, ametoa ufafanuzi mzuri wa jinsi gani wale vijana wamefanya vizuri, wakiwemo vijana kutoka katika Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie fursa hii, niwashukuru Wabunge wote, waliochangia kwenye mjadala wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Serikali inaamini michango yao na itafanyia kazi ushauri mbalimbali walioutoa. Mjadala huu ulikuwa mrefu, watu wengi walihamasika kuchangia, sisi katika TAMISEMI tumepata faraja kwamba, karibu Wabunge wote mmezungumza, kutoa mawaidha ya nini tufanye katika TAMISEMI na sisi tumewasikia, tutakuwa tunatekeleza ushauri kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapoongea baadaye, atawataja Waheshimiwa Wabunge, waliochangia. Kwa hiyo, kwa kunusuru muda, niruhusu nizungumze kwa ujumla masuala yaliyojitokeza yanayohusiana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge, wameyazungumzia. Kutokana na muda nilionao kama ulivyosema, nitazungumzia baadhi ya maeneo kwa ujumla; maeneo ambayo nitayazungumzia ni Wabunge wa Viti Maalum kutoingia kwenye Kamati za Fedha, kuwajengea uwezo katika ngazi za msingi Viongozi wetu, ubovu wa barabara, matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri, ushuru wa mazao, migogoro ya ardhi na muda ukitosha tutaongezea mengine yakiwepo taratibu za ajira katika Halmashauri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ninalopenda kulizungumzia ni Wabunge wa Viti Maalum, kutoingia katika Kamati ya Fedha ya Halmashauri. Mbunge aliyechangia katika eneo hilo kama nilivyosema sitawataja, maana nikitaja mmoja nitawa-*offend* wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ninachotaka kusema ni ushiriki wa Wabunge katika Vikao vya Halmashauri, wakiwemo Wabunge wa Viti Maalum, hufanyika kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ambazo zinatawala katika uendeshaji wa vikao na shughuli za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kamati za Kudumu za Madiwani, huundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 288, pamoja na Kanuni za Kudumu za Halmashauri. Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizo, Diwani katika Halmashauri anapaswa kuwa Mjumbe walau katika Kamati moja, isipokuwa Kamati ya Fedha, ambayo huundwa na Wajumbe wafuatao: Mwenyekiti wa Halmashauri, Naibu Mwenyekiti, Mbunge wa Kuchaguliwa wa Jimbo, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu wa Halmashauri na Madiwani wawili watakaochaguliwa na Baraza la Madiwani. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuiangalia Sheria hii ili kuona uwezekano wa kuwashirikisha Madiwani wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi hapa ni kwamba, wakati Sheria inapitishwa, hatukuwa na Waheshimiwa Wabunge au Madiwani wa Viti Maalum. Sasa tumekuwanao baada ya hii Sheria kuwa imeshapita, ndiyo maana tunasema kuna umuhimu sisi katika TAMISEMI, tuliangalie suala hili kwa sababu Wabunge wengi sana wanakosa fursa,

hasa wa Viti Maalum, wanakosa fursa ya kutoa ushauri katika Halmashauri zao, kwa sababu hawakutajwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamechangia ni kuwajengea uwezo Viongozi wetu walioko katika ngazi za misingi, kwa maana ya Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji wa Mitaa na Vitongoji. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwenye maeneo haya wamesisitiza umuhimu wa kwamba, kama hatukuwa na uongozi bora ngazi za msingi, hatuwezi kupata maendeleo yanayotegemewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali chini ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, inayotekelezwa katika kipindi cha 2010/2011 hadi 2013/2014, imepanga kuelekeza nguvu zake katika kuwajengea uwezo Viongozi wetu wa ngazi za msingi wakiwemo Madiwani, Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Aidha, Serikali imepanga kuwahamasisha na kuwaelekeza Wananchi kushiriki katika kupanga na kutekeleza Miradi yao kwa lengo la kuwaondolea umaskini. Ujengaji wa uwezo kwa Viongozi hawa, utawaongezea ufanisi katika kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia wameongelea juu ya ubovu wa barabara vijijini na katika hili tunasema, Serikali inazipa kipaumbele barabara zilizoko maeneo ya vijijini zinazohudumiwa na Halmashauri. Kwa kutambua umuhimu huo, fedha za matengenezo ya barabara katika Halmashauri zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 84.5 mwaka 2010/2011 hadi shilingi bilioni 94.1 mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la 11.2% na sisi ahadi yetu ni kwamba, tutaendelea kuongeza fedha za kutengeneza barabara vijijini kulingana na uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wamezungumzia suala la matumizi mabaya ya fedha za umma zinazopelekwa kwenye Halmashauri na hivyo kusababisha Miradi mingi kutekelezwa chini ya viwango na hivyo kutokuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money).* Eneo hili limechangiwa na Wabunge wengi karibu 20.

Mheshimiwa Spika, hapa tunachosema ni kwamba, Serikali inakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, tatizo hili lipo. Hata hivyo, zipo juhudi za makusudi, ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali kupunguza kama siyo kukomesha kabisa tatizo hili. Ninataka kusema hapa kwamba, tathmini iliyofanywa na *Commonwealth Law Government Forum,* imeonesha kwamba, katika nchi 14 zilizopo Mashariki mwa Afrika mpaka *Horn* ya Afrika, Tanzania inaongoza kwa kuwawezesha kifedha Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, maana yake hapa ndiyo kusema fedha nyingi zinapelekwa kwenye Serikali za Mitaa, kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuhakikisha kwamba, usimamizi unakuwa madhubuti ili fedha ifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakubaliana na hoja hii ya Wabunge, lakini hata hivyo juhudi za makusudi ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali ili kupunguza kama siyo kukomesha tatizo hili ni kama zifuatazo: Kwanza, kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu, kulingana na taratibu za kiutumishi zilizopo; hii ikiwa ni pamoja na kuwafungulia hati za mashtaka na hati ya jinai kulingana na makosa. Mfano, hivi

karibuni Serikali imewachukulia hatua Watumishi wa Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo, Kishapu, Rorya na Rombo. Nami ninataka niahidi kama Waziri wa TAMISEMI, sitapata malalamiko, nikitosheka kwamba, Mkurugenzi fulani au mtumishi Fulani, ameshindwa kuwajibika, jawabu siyo kumhamisha maana unapomhamisha unahamisha tatizo lile kutoka mahali lilipo, kulipeleka mahali ambapo tatizo halikuwepo; tukimwona kwamba hatoshi, tutamtafutia kazi ambayo inamtosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni Serikali, imeifanyia marekebisho Sheria ya Fedha, Sura ya 348 ili kuruhusu kuwepo kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali na Naibu Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa lengo la kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uteuzi wa Viongozi hawa, utaimarisha usimamizi wa fedha za Serikali katika ngazi zote. Katika hili, Serikali imeamua wale watu wanaoitwa *DTs,* sasa hivi wapo chini ya Halmashauri. Hoja ya msingi hapa ni kwamba, huwezi ukawa wewe Halmashauri halafu unajikagua mwenyewe. Mkurugenzi akishaona kwamba, *DT,* yule Mkaguzi wa Ndani, anaomba usafiri aende akakague katika Mradi ambao hauridhishi, atakachofanya ni kumnyima mafuta na usafiri. Ndiyo maana Serikali imesema watu hawa sasa wasiwe chini ya Mkurugenzi, waende kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amechaguliwa na Naibu wao ili kuweza kuzikagua Halmashauri bila kutegemea kuomba posho wala mafuta kutoka Halmashauri. Serikali pia imetunga Kanuni hizi za Sheria ya Fedha ya Mitaa, Sura ya 290, kuwezesha tozo na adhabu, *surcharge,* kutolewa kwa wanaobainika kwenda kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kwamba, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, itatumia Mfumo wa *IFMs.* Tayari Serikali imeshanunua *computer* kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa mafunzo kwa Waweka Hazina wote na Wahasibu wawili wa kila Halmashauri, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba, Mfumo huu unatumika bila visingizio.

Tulikuwa tuna matatizo ya fedha, hatukuweza kuziwezesha Halmashauri zote, lakini Mheshimiwa Rais, aliagiza Hazina itoe fedha za kuwezesha Halmashauri zote kuingia katika Mfumo huu kwa mpigo. Fedha zile zimetolewa kwa Halmashauri, kwa hiyo, tunategemea tutakuwa tumeboresha usimamizi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe wito kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba, zinatumia Mfumo huu mara maandalizi yote yatakapokamilika. La mwisho, nimalizie kwa kusema kwamba, askari namba moja anayelinda fedha za Halmashauri ni Waheshimiwa Madiwani. Bahati nzuri, ndani ya Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge mpo.

Mimi ninaomba ile dhana ya kusema TAMISEMI, inayosimamia Halmashauri 133, inaweza ikawa inajua kinachoendelea kila siku katika Halmashauri, tafadhalini tusaidiane; sisi TAMISEMI tunaratibu, waliopewa kazi ya kusimamia fedha za Serikali kuona kwamba zinatumika vizuri ni Baraza la Madiwani na bahati nzuri kwa hekima ya Serikali yetu, Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani kule ndani. Tusaidieni kuhakikisha mambo katika Majimbo yenu yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la ushuru wa mazao, *produces,* limechangiwa na Waheshimiwa wengi. Ushuru wa mazao hutozwa mnunuzi wa mazao chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kwa Serikali za Mamlaka za Miji, Kifungu Namba 7, kwa Sheria ya Mamlaka za Wilaya, pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri zinazotungwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, pamoja na Sheria ndogo zinazotungwa chini yake. Ushuru huo haupaswi kuzidi 5% ya gharama za ununuzi. Serikali haijawahi kurekebisha Sheria hii; hivyo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaweza kuandaa Sheria Ndogo kulingana na Sheria hiyo ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nimeona nilizungumzie hili kuondoa mkanganyiko kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo zimekuwa hazina uhakika wa kiwango kinachopaswa kutozwa kwenye ushuru wa mazao. Ninataka niseme, hasa Halmashauri zetu za Vijijini, hiki ndiyo chanzo cha uhakika cha Halmashauri nyingi sana, wakikosa kukusanya fedha za kutosha katika kifungu hiki, hali ya Halmashauri zile inakuwa siyo nzuri. Kule kwetu Mtwara, tuna Halmashauri ya Tandahimba, *produces* mwaka huu wamekusanya *2.9 billion.* Kwa hiyo, unaona kwamba. inawapa uwezo Halmashauri ile kusimamia vizuri shughuli zinazohitaji fedha na nina uhakika katika maeneo mengi wanakolima kahawa, pamba, korosho na kadhalika, hali imeendelea kuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi inapaswa kuanza kushughulikiwa katika ngazi za msingi, yaani Mabaraza ya Vijiji na Kata. Changamoto iliyopo ni baadhi ya Wenyeviti na Wajumbe wake kuwa hawana ujuzi wa masuala ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Mji na Kata, yalianzishwa kupitia Waraka uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kwa Halmashauri zote hapa nchini. Kupitia Waraka huo, Halmashauri ziliagizwa kutenga Bajeti kwa ajili ya kutoa mafunzo ya majukumu ya Mabaraza haya ya Uendeshaji.

Kimsingi, Wajumbe wa Mabaraza na Wenyeviti, wanashughulika na malalamiko ya awali ya Wananchi na kutoa ushauri. Malalamiko ambayo hayawezi kutatuliwa katika ngazi hizi, hupelekwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, ambako malalamiko haya husikilizwa na kutoa ushauri unaojikita zaidi katika masuala ya kisheria. Serikali inaendelea kuziagiza Halmashauri kutenga Bajeti ya Uendeshaji na mafunzo kwa ajili ya Mabaraza haya pamoja na kufuatilia kupata Taarifa za Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Serikali inathamini michango ya Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia katika Hotuba hii. Tunaahidi kwamba, michango yao ile tutaifanyia kazi kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa kwa uchungu kabisa ni tatizo la uhaba wa Walimu katika Shule zetu za Sekondari hasa zile za Kata.

Ninataka kusema kwamba, Serikali tumejipanga kuwasambaza Walimu hawa kulingana na mahitaji; kule ambako kuna upungufu wa Walimu, wanapelekewa wengi zaidi; na kule ambapo hali ya Walimu ina unafuu kidogo, wanaambiwa wasimame kidogo wasubiri ili na wenzao wapate. Ndiyo maana kwa miaka miwili iliyopita mfululizo hakuna Walimu wa Sekondari waliopelekwa katika maeneo ya Miji, kwa sababu maeneo mengi ya Miji hali ya Walimu ni nafuu ukilinganisha na Vijijini.

Sisi TAMISEMI, tutaendelea kuhimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa na wao wakipata Walimu hawa, kuzingatia hili wakati wanapowatawanya katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa hapa linafanana na hilo, kuboresha Sekondari za Kata. Mimi leo nimefarijika sana, kuona kwamba, tumepata Wanafunzi saba, wamefanya Mtihani wa *Form Six* vizuri, Kidato cha Sita, waliosoma Sekondari za Kata.

Kwa hiyo, kama kuna mtu alikuwa na mashaka juu ya uwezo wa Sekondari za Kata, hawana maabara, hawana nyumba za Walimu za kutosha, tayari wameshaingia katika 20 Bora za nchi.

Mimi nina uhakika tukiboresha shule hizi, watafanya vizuri kama wanavyofanya shule nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira bora ya kufundishia ni mojawapo ya nyenzo muhimu zinazochangia kuinua kiwango cha ubora wa elimu na Serikali inatambua hivyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha Serikali inafanya nini kuboresha Sekondari za Kata, mwaka 2010/2011 zilitolewa shilingi bilioni 41 za *capitation,* yaani uendeshaji wa Shule za Ssekondari na asilimia 50 ilikuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na vifaa vya maabara. Shilingi bilioni 3.8 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu na *MMES* II. Serikali imetenga shilingi bilioni 4.3 kujenga nyumba za walimu. Aidha, shilingi bilioni tatu zilitolewa kujenga maabara 37 katika Sekondari za Kata. Walimu 9,226 wa Sekondari waliajiriwa na mwaka huu 2011/2012 katika bajeti yetu ambayo tutaomba Waheshimiwa mtupitishie, maabara 500 zitajengwa katika Sekondari za Kata.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba tukiyatekeleza haya, hali zetu za Sekondari za Kata zitazidi kuwa nzuri. Lakini nataka nichukue nafasi hii kuwaambia Watanzania wenzangu, sera ya Serikali ya CCM ni kuchanganya nguvu za Serikali na nguvu za wananchi. Sekondari tumeweza kuwa nazo moja kila Kata kwa sababu wananchi walijitolea wakashiriki kutoa michango na nguvu zao katika kujenga sekondari hizo. Mimi nataka niwapongeze Waheshimiwa Wabunge na wengine wa upinzani ambao wamekuwa na uchungu sana na michango ya wananchi. Naomba waendelee na uchungu watusaidie

kusimamia michango ya wananchi, ila wasitukataze kuchangisha maana tusipochangishana hatutafika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulinadi sera zetu hapa wakati wa uchaguzi, kuna chama kilisema wao kila kitu bure, CCM tukasema kila kitu bure hatuwezi, tutachanganya kile kilichoko kidogo kutoka Serikalini na wananchi na wachange. Lakini wananchi wakapiga kura wakasema hawa wanaosema tuchanganye nguvu za wananchi na Serikali, hawa ndio wenzetu, wakawapa kura. Sasa hiyo ndiyo sera iliyopo. Kwa hiyo, naomba sana tushirikiane katika hili na sisi katika TAMISEMI tutakuwa wakali sana, tutakuwa wakali kuhakikisha kwamba michango inayotolewa, inatolewa taarifa katika kikao kinachohusika. Kuna michango inawekwa na Serikali ya Kijiji, kuna michango inawekwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata, kuna michango inawekwa na Baraza la Madiwani, wananchi wanachanga, mradi unatekelezwa, lakini hakuna mrejesho wa kusema tulikusanya shilingi kadhaa, zimetumika kadhaa, kadhaa.

Kwa hiyo, nataka niungane na ndugu yangu Mheshimiwa Lissu, pale alipokuwa anachangia umuhimu wa kuhakikisha kwamba michango hii inakaguliwa, inatumika vizuri, ila niombe tu asitukataze kuchanga.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa hapa ni Sekretarieti za Mikoa kusimamia kwa makini Halmashauri zake. Nataka nieleze kwamba kwa mujibu wa sheria Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997, Ofisi za Wakuu wa Mikoa zina jukumu la kusimamia, kuratibu, kuwezesha na kuzishauri Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli zao za msingi. Ili kuziwezesha ofisi hizo kuweza kutekeleza majukumu yake, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, inazijengea na itaendelea kuzijengea uwezo Ofisi za Wakuu wa Mikoa ili waweze kutekeleza vizuri majukumu yao. Hapa nataka niseme kwamba Jumamosi iliyopita na Jumapili tulikuwa na kikao hapa cha Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Moja katika jambo tulilozungumza ni hili kwamba Mkuu wa Wilaya jukumu lake ni kuhakikisha fedha ya Serikali inayokwenda katika eneo lake anaifuatilia pia na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu TAMISEMI ipo Dodoma, lakini Mkuu wa Wilaya yuko kule sijui, Kishapu, yuko wapim Sumbawanga, yuko karibu na Halmashauri yake, nataka nitumie nafasi hii kuwaambia Wakurugenzi wote huko mliko, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa anapohoji shughuli za Halmashauri zinazokwenda, siyo kwamba anawaingilia, kwa mujibu wa sheria za nchi hii Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kila shughuli ya Serikali inayofanyika katika eneo lake inafanyika chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya.

Kwa hiyo, nashukuru Waheshimiwa Wabunge kutukumbusha hili. Wakuu wa Mikoa wapo wanasikia kwamba hela ikitumika vibaya kwenye Halmashauri kabla Waziri wa TAMISEMI hajaulizwa, ataulizwa DC, ataulizwa na mwenye Mkoa na Sekretarieti yake kwamba hivi wakati zinaliwa, ninyi si ndiyo mnazishauri Halmashauri? Mlikuwa wapi? Hili tumelizungumza, tumejipanga vizuri, nina uhakika tutaendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine limezungumzwa hapa, ni suala la makusanyo hafifu ya fedha katika mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ushauri wa Wabunge ni kuwa, apatikane mshauri mwelekezi ili aweze kubaini vyanzo vya mapato vya Halmashauri. Hapa tunataka kueleza kwamba jitihada za kubaini vyanzo vipya vya mapato vya Halmashauri zinaendelea na kwa kuanzia, Serikali imeajiri mshauri mwelekezi atakayeandaa mapendekezo ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutokana na mali zisizohamishika. Tunaanzia na mali zisizohamishika halafu tutaendelea na maeneo mengine ya mapato.

Mheshimiwa Spika, lingine hapa, limezungumzwa suala la kwamba Serikali za Mitaa zimenyimwa fursa ya kuajiri, na mimi nataka niseme kama Waziri wa TAMISEMI kwamba liko tatizo. Zamani tulikuwa na *Local Government Service Commission* ilikuwa inaajiri tu watumishi wa ngazi za juu, lakini wale wanaitwa *operational service,* walikuwa wanaajiriwa na Halmashauri yenyewe. Sasa tangu imeanza, nadhani Sekretarieti ya ajira karibu kila kitu wanafanya wao.

Mheshimiwa Spika, Ni gharama kubwa sana kwa watu kwenda *interview* Dar es Salaam, wengine wanaitwa *interview* hawawezi kwenda kwa sababu ya nauli. Sasa nataka niseme kwamba Serikali yetu, Serikali sikivu, *ALAT* imetoa rai kwa Waziri Mkuu, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, kwamba ifike mahali sasa pawepo na mgawanyo, ifahamike, aina zipi za watumishi wanaajiriwa na Sekretarieti ya Ajira na aina gani ya watumishi waajiriwe na Halmashauri yenyewe. Jambo hili linafanyiwa kazi, tupeni muda tutakapokuwa tayari tutatoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimeona kengele ya kwanza imegonga, nataka nirudie tu kusema kwamba sisi katika TAMISEMI tumejipanga ku-*deliver*, tumejipanga kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa ili wananchi waliotuchagua waone kwamba hawakufanya makosa. Sisi tutashirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote. Mimi nilisema hapa siku moja, Mbunge wa Tanzania ni Mbunge, umepitia mlango gani, siyo hoja, hoja ilikuwa kuingia humu ndani. Sasa tukishaingia humu ndani tushirikiane kujenga nchi yetu.

Nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Manaibu Mawaziri, ndugu yangu Mheshimiwa Mwanri. Zamani akiwa kivukoni ana jina la utani tulikuwa tunamwita *Suslov Party theoretician*. Namshukuru ndugu yangu Majaliwa ambaye anaposhughulika na mambo ya shule hana matatizo; namshurku Katibu Mkuu ndugu yangu Katanga, Manaibu wake Mwalimu Sajine, Maswi, Wakurugenzi wote wa TAMISEMI. Nawashukuru sana, maana bila ya ninyi wataalam kutushauri, mimi sikusomea mambo ya Serikali za Mitaa, nimesomea uanajeshi na ualimu, lakini hizi kazi nazifanya kwa sababu ninao washauri waliobobea ambao wana nia nzuri na nchi hii. Naomba tuendelee kushirikiana, tuijenge nchi yetu Tanzania paendelee kuwa mahali pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwezekaji na Uwezeshaji, ninao wageni wetu hapa, asubuhi hatukupenda kuchanganya mambo,

nafikiri wapo. Hapa kuna Ma-*miss Tourism Tanzania* na viongozi wao wa Taasisi wapo kwa ajili ya kufanya ziara hapa Bungeni. Lakini nimepata *resume* yao nzuri sana.

Sasa nikisoma, muda wangu utakwisha, naona niwataje ma-*miss* tu. Kuna Miss Sophia Dio, yeye ni Miss Tanzania 2011 mshindi wa Tano; Miss Utalii Dar es Salaam kumbe yeye ni Balozi wa Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Balozi wa Hifadhi ya Taifa ya Saadan na Miss Utalii wa Ndani 2011. Kuna Rosemary Kasiga, yeye ni Miss Utalii 2011 mshindi wa nne; Miss Utalii Mazingira 2011, halafu ni Balozi wa Hifadhi ya Taifa ya Saanane; kuna Miss Deis Mshumbuzi yeye ni Miss Utalii 2011 vipaji *talent*; Miss Utalii Kagera, Balozi wa Utalii wa kitamaduni Tanzania na Balozi wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na Balozi wa Uwindaji Haramu Tanzania. Sasa unaona haya mambo! Kuna miss Utalii Neema Isdory, huyu ni Miss Utalii Njombe. Mambo makubwa na Balozi wa Hifadhi ya Taifa ya Kitalu, Balozi wa Uvuvi haramu Tanzania. Huko kwetu tunavua! Hakuna kuvua. Kuna Miss Utalii Tabia Msuta, yeye ni Miss Utalii Tanzania 2011, Hifadhi za Bahari na Miss Utalii Vyuo Vikuu Kanda ya Kati na Balozi wa Hifadhi ya Taifa Tarangire.

Sasa na viongozi wao wana vyeo vikubwa sana, ningetaka kuvitaja lakini muda wangu hautoshi. Kwa hiyo, naomba niwakaribishe maana yake kuna Gideon Kipungahero naye ni Rais na ni Mwasisi wa Miss Utalii Tanzania. Ana sifa nyingine nyingine hapa muda haunitoshi; kuna Miss Vailet Kaberege yeye ni Mkurugenzi wa Fedha Uwezeshaji na Utawala; Miss Tanzania, Mkurugenzi wa Viovena company; halafu kuna Grace Kihongozi, Mkurugenzi Utawala na Nidhamu; kuna Idrisa Mziray, Mkurugenzi wa Uratibu na Itifaki; Johakim Mkwabi, Mkurugenzi wa Matukio; Daniel Mtanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais, huyo siyo Rais wa kwetu, huyu ni Rais wa hayo mambo ya utalii. Kuna Dimo Debwe, Mkurugenzi wa Picha na Filamu ya hiyo shughuli; kuna Emmanuel Masabo, Mkurugenzi wa Mipango ya huu Utaratibu Mzima.

Tunashukuru sana kuwepo kwenu. Kwa hiyo, nadhani mtakuwa na nafasi nyingi ya kuweza kutembelea huku.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi Uwekezaji pia ana wageni wake, hapa ni pamoja na Aafisa Elimu Hanang. Yuko Afisa Elimu Hanang na Wakuu wa Shule za Msingi kutoka Hanang na wanafunzi. Sidhani kama wamepata nafasi, wapo! Kama wapo, naomba wasimame. Ahsante sana, kumbe mpo. Kwa hiyo, wanafunzi na wapigakura wake, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, karibu utoe taarifa yako, muda ni ni nusu saa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kwa dhati kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge hasa eneo la uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi. Kabla sijafanya hivyo, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano

Mheshimiwa Jakaya Mrisho kwa kuja kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa awamu ya nne, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nakipongeza kwa dhati Chama changu cha Mapinduzi kwa kuendesha kampeni kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kunichagua kwa mara nyingine tena kuwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu kushughulikia masuala ya uwekezaji na uwezeshaji. Pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Billal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia nampongeza Mheshimiwa Kayaza Pinda kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne na namshukuru sana kwa maelekezo yake na uongozi wake katika ofisi yake. Napenda kwa moyo wa dhati kumpongeza Mheshimiwa Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar. Nawashukuru Mawaziri wenzangu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakinipa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge katika Afrika Mashariki. Hii imenipa faraja hasa nikizangatia nilikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto baada ya wewe kuongoza Wizara ile. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa zao. Aidha, napenda niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuingia katika Bunge hili bila kuwasahau Wenyeviti wetu wa Bunge. Nawashukuru kwa mshikamano Waheshimiwa Wabunge wote na ushirikiano wenu ambao pengine ni mchango mkubwa kwangu mimi kuendelea kuwa Waziri kwa muda ambao nimekuwa Waziri. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uwenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni akiwasaidiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa kwa mchango wao mzuri na wenye manufaa. Vilevile naomba nitambue mchango wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai kwa mchango wake pamoja na Msemaji Mkuu wa Wizara yangu, Wizara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Uwekezaji, Uwezeshaji na Maendeleo ya sekta binafsi.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Hanang, kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa miaka mitano kwa mara ya pili. Nawaahidi nitakuwa mchapa kazi, mtiifu na kuwapa ushirikiano ili tulete maendeleo katika Jimbo letu la Hanang. Bila ushirikiano wa karibu wa familia yangu, ikiongozwa na mume wangu mpenzi Prof. Joseph Nagu, kazi yangu ingekuwa ngumu sana, namshukuru sana. Nawashukuru pia wazazi wangu na majirani zangu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia hoja za Waheshimiwa Wabunge zinazohusiana na uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi, naomba

kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri waliyotoa. Hii inadhihirisha wazi kuwa Waheshimiwa Wabunge wanafahamu vyema umuhimu wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa na kupunguza umaskini na bila uwekezaji hakuna ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yake na nianze kwa maelezo ya jumla. Waheshimiwa Wabunge wanafahamu vyema kuwa ili kuhakikisha kuwa sekta binafsi inakuwa muhimili wa uchumi wa Taifa, Serikali ilifanya uamuzi wa kuingia kwenye mfumo wa soko huria mwanzoni wa miaka ya 1990. Ili kutekeleza azma hii, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imekuwa inafanya kazi kubwa ya kuandaa na kurekebisha sera, sheria na mifumo ya kitaasisi ili kukidhi matakwa ya soko huru. Changamoto kubwa ambayo inaendelea kujitokeza ni kuweka mazingira bora ya kuimarisha mazingira ya sekta binafsi na uwekezaji, pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii, kuwezesha ukuaji wa kasi na endelevu wa uchumi wa soko. Aidha, changamoto nyingine ni pamoja na kubadili mfumo uliozoeleka hususan urasimu na fikra potofu ambavyo vinakwaza ukuaji wa sekta binafsi. Kutokana na hali hii, ni vyema wote tukatilia mkazo mkubwa maendeleo ya sekta binafsi ili iweze kushika hatamu baada ya Serikali kuachia uzalishaji na biashara ili kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote Ulimwenguni, na uhuru wa kujitawala hautoshi bila kujitegemea kiuchumi. Ni uwekezaji peke yake ambao utaikomboa nchi hii kutokana na uchumi tegemezi. Uwekezaji unachangia kuongeza ajira, kuongeza uzalishaji na tija, kuongeza pato la Taifa, kuleta teknologia mpya katika Sekta mbalimbali hivyo kusaidia kuwawezesha wananchi na kupunguza umaskini. Kutokana na umuhimu huu, Serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa uwekezaji wa ndani na wa nje unakua kwa kasi sambamba na kuhakikisha kuwa wananchi walio wengi wananufaika na uwekezaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe takwimu chache, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita (2001 – 2010), jumla ya miradi 5,238 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 32 zimesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* na imesaidia kutoa ajira kwa Watanzania wapatao 756,689. Aidha, uwekezaji kutoka nje, *Foreign Direct Invesment-FDI* umekuwa ukipanda mwaka hadi mwaka kama ilivyoainishwa na *World Investment Report* inayotolewa kila mwaka na *UNCTAD*. Taarifa hiyo imeonyesha kwa mfano *FDI* ilikua kutoka Dola za Kimarekani milioni 520 mwaka 2005 wakati kwa mwaka 2008 ilikua Dola za Kimarekani 744 milioni. Hii inatokana na juhudi za Taifa letu katika kuwavutia wawekezaji. Mojawapo ya sababu zilizochangia kukua kwa *FDI* ni pamoja na misamaha ya kodi kwa vifaa vya mtaji, *Deemed Capital Goods* kwa baadhi ya sekta, mfano, mawasiliano ya simu, utalii na Ujenzi wa majengo makubwa. Napenda niseme kwamba kupitia *TIC* hakuna misamaha mingine inayotolewa bali ya *Deemed Capital Goods.*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uwekezaji kutoka nje au *Foreign Direct Investment Report* inayotolewa na *UNACTAD* inaonyesha kuwa kwa mwaka 2007, jumla ya mitaji yote ya duniani ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 1,833. Afrika ilipokea kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 53 ambazo ni sawa na asilimia tatu tu ya mitaji yote ya dunia. Bara

la Ulaya lilipokea Dola za Kimarekani bilioni 849, Amerika ya Kaskazini Dola za Kimarekani bilioni 341, Asia Dola za Kimarekani bilioni 320, Amerika ya Kusini Dola za Kimarekani bilioni 126 na Australia Dola za Kimarekani bilioni 22.

Katika mwaka huo huo wa 2007, Tanzania iliweza kupata Dola za Kimarekani milioni 600 tu kati ya Dola za Kimarekani bilioni 53 zilizokuja Afrika. Hii ni sawa na asilimia 1.1 tu ya mtaji wote uliokuja Afrika. Katika mitaji yote ya dunia, yaani bilioni 1,833, Tanzania tuliambulia asilimia 0.03 tu ya mitaji yote ya dunia. Hali hii inayoonyesha kuwa sote tunatakiwa kuongeza jitihada za kuvutia uwekezaji kutoka nje ili tuweze kupata *share* yetu stahiki kutoka mitaji ya dunia. Umuhimu wa mitaji kutoka nje unatokana na uwezo wetu mdogo wa kuweka akiba. Kiwango cha akiba ni asilimia 15.4 ya pato la Taifa kwa takwimu za mwaka 2008. Ukuaji huu bado ni mdogo sana ikilinganishwa na wastani wa dunia na nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaonyesha kwamba bado tuna changamoto kubwa ya kuvutia zaidi uwekezaji wa ndani na wa kutoka nje ya nchi ili tuweze kuongeza pato la Taifa, kupunguza umaskini na hatimaye kuwawezesha wananchi wa Tanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa tuliyonayo, ni kuona ni kwa jinsi gani ukuaji wa uchumi jumla na wa sekta mbalimbali unaweza kuchangia katika kupunguza umaskini kwa mwananchi wa kawaida. Tukijipanga vizuri, hili linawezekana. Ni vyema kila sekta ikahakikisha kuwa inatekeleza kikamilifu Sera ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuweka mipango sahihi ambayo inazingatia uwezeshaji wa wananchi katika ngazi zote. Nakubaliana na maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi wakati inatoa maoni kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/12 kwamba hili linawezekana tu pale ambapo raslimali za Taifa zitaelekezwa kwenye maeneo ambayo yanawagusa wananchi wengi katika shughuli zao za kila siku. Hivyo, jambo la msingi sana ni kuelekeza jitihada hizi katika sekta ambazo wananchi wengi wanategemea kama vile kilimo, mifugo na uvuvi bila kusahau maeneo makubwa ya Madani, mafuta na raslimali nyingine jambo ambalo Serikali inalizingatia sana.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi ni sehemu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025, ambapo kufikia wakati huo sehemu kubwa ya uchumi wa Tanzania unatarajiwa kumilikiwa na Watanzania wenyewe. Maendeleo hayo yanajumuisha Watanzania wote pamoja na kutoa nafasi kwa makundi yote kujiendeleza kikamilifu hasa kwa makundi yenye uwezo mdogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendelea kuwawezesha wananchi kwa kuweka mazingira wezeshaji ambayo ni pamoja na kukuza uchumi na kuweka mazingira bora ya uwekezaji. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwani Wizara itasaidia zaidi kuongeza kasi ya wananchi kuwezeshwa; kuboresha mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma nyingine za Serikali; upatikanaji wa mitaji; kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu; kuboresha miundombinu ya kiuchumi; kuendeleza sekta binafsi; kuboresha na kuimarisha masoko; kuimarisha ushirika na kuhakikisha ardhi inawasaidia wananchi. Aidha, ni lazima ieleweke kwamba uwezeshaji siyo kumnyang’anya

aliyenacho na kumpa asiyenacho, bali ni kumwezesha asiye nacho ili aweze kujikwamua kiuchumi na aweze kumkuta aliyenacho. Ni lazima kuwapa wananchi wote fursa sawa ili kujitegemea na Taifa letu lijitegemee.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zimeweka mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, mfano mzuri ni Afrika ya Kusini ambao wana sera ya kuwezesha wananchi ijulikanayo kama *Broad Based Black Economic Empowerment* ya mwaka 1994. Sera imeweka bayana kuwa uwezeshaji unalenga katika kuongeza idadi ya watu weusi wanaondesha, kumiliki na kudhibiti uchumi wa nchi yao na kupunguza tofauti ya kipato kati ya watu weusi na weupe. Aidha, kutokana na sera hiyo, vyombo mbalimbali vimeundwa na sisi tunajitahidi kupata mazuri kutoka katika sera hiyo vikiwemo Mfuko wa Uwezeshaji, Shirika la Kuendeleza Wajasiriamali wa kati *SEDA*, *Khula Enterprise*, *Industrial Development Corporation* ambalo huhudumia viwanda vikubwa, na *Development Bank of South Africa.*

Mheshimiwa Spika, Sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi imechukua yale yaliyo mazuri kutoka kwenye Mfumo wa uwezeshaji wa Afrika ya Kusini na kuyaboresha ili kukidhi mazingira yetu. Vile vile, kama ilivyo kwa Afrika ya Kusini, Sera ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi imeagiza kuanzishwa taasisi mbali mbali za kutekeleza sera hiyo kama vile Baraza la Taifa la Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wakala wa Dhamana za Mikopo, Wakala wa Kuendeleza Viwanda Vidogo, Taasisi ya kuendeleza ujasiriamali, Kituo cha uendelezaji masoko, Benki ya Maendeleo, Kilimo na Uanzishwaji wa Mifuko mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mifuko hii ni pamoja na Mfuko wa Wanawake *(Women Development Fund - WDF);* mfuko wa maendeleo ya vijana *(YDF);* mfuko wa udhamini wa mikopo kwa mauzo nje *(ECGS);* Mfuko wa Udhamini Mikopo kwa Miradi midogo na ya kati *(SME – CGS);* Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali *(NEDF);* Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(AGITF);* Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF);* Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania *(TASAF);* Mfuko wa Uwezeshaji Wajasiriamali Wadogo *(Small Entrepreneur Loan Facility - SELF);* Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira *(JK Fund)*; na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(Mwananchi Empowement Fund - MEF).* Lakini napenda niseme kwamba mifuko mingi chini ya Serikali, Wizara yangu itapenda kuona inafanya kazi ipasavyo. Ninapenda vilevile kukubali kwamba sekta binafsi na taasisi za kiraia pamoja na madhehebu ya dini hayako nyuma katika kuwawezesha Watanzani kujitegemea kiuchumi kwa kuwapa uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya mikopo ambayo imetolewa kupitia mifuko hii pekee ni shilingi bilioni 288.79. Hii inadhihirisha wazi kuwa Serikali imedhamiria kwa dhati kuwawezesha wananchi wake kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004 na Sheria Na. 16 ya mwaka 2004, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(National Economic Empowement Council)* ni chombo cha juu kitaifa kitakachosimamia, kufuatilia na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji

wananchi kiuchumi. Serikali inaweka utaratibu ili mifuko hii iwe chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama ilivyo kwa Zambia ambapo mifuko yote ipo chini ya *Citizen Empowerment Fund.* Hii inarahisisha kuratibu, kutathimini na itaondoa dhana ya mifuko kufanya shughuli zinazofanana *(duplication)* kwa mlengwa mmoja. Aidha Serikali, itaendelea na utoaji wa elimu ya Ujasiriamali ambapo Baraza la Taifa la Uwezeshaji kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu *(TIE)* inaandaa sera ya mitaala itakayotumika kufundisha ujasiriamali toka Shule za Awali hadi Chuo Kikuu kama ilivyo kwa nchi ya Malaysia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ujasiriamali yaliendelea kutolewa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwenye *SACCOs* zinazodhaminiwa mikopo na Mfuko wa Uwezeshaji kwenye Mikoa ya Mtwara, Manyara, Rukwa na Lindi.

Mheshimiwa Spika, ili kufaidi matunda ya kukua kwa uchumi, mwananchi mmoja mmoja ana jukumu la kufanya jitihada za kujikwamua kiuchumi kupitia mafunzo mbalimbali yakiwemo ya ujasiriamali, uwajibikaji na kufanya kazi kwa tija. Watanzania ni lazima tufanye kazi kwa bidii, Watanzania ni lazima tutegemee nguvu zetu tukiwezeshwa na kusaidiwa na Serikali yetu. Sambamba na hili, ni muhimu kubadilika kifkra potofu kuwa Serikali itafanya kila kitu ili kuinua uchumi wa Taifa. Ni vyema kujituma na kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa ili kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo napenda kusema kwamba kama alivyonipa Mheshimiwa Waziri wadhifa huu nitajihidi kuona raslimali za Tanzania zinawanufaisha Watanzania lakini vilevile lazima tuone umuhimu wa kukaribisha mitaji kutoka nje ili isaidiane na mitaji ambayo iko ndani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, sasa napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mliyotoa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa upande wa uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi. Naomba kukiri kuwa michango ya Waheshimiwa Wabunge itatusaidia sana katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na katika kuwezesha wananchi.

Mheshimiwa Spika, ilitolewa hoja kuwa Serikali itenge ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji kupitia Benki ya Ardhi *(Land Bank).* Hoja hii ilitolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo imewasilisha hoja kupitia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Devotha Likokola, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Ruvuma na ninapenda kumshukuru sana kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa umahiri mkubwa, na vilevile kwa kuongoza *VICOBA* kwenye Mkoa wa Ruvuma na kusaidia Mikoa mingine nayo ianzishe *VICOBA*. Ushauri wa Kamati umezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2010, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kilikuwa kimepokea jumla ya hekta 1,604,825 zilizotengwa na Mikoa yote ya Tanzania Bara isipokuwa Shinyanga, Pwani na Dodoma kwa ajili ya Benki ya Ardhi. Naomba Wakuu wa Mikoa hiyo mitatu wazingatie hilo. Kati ya hizo, hekta 567,308 sawa na asilimia 35 zimepimwa na hekta 1,037,517 sawa na asilimia 65 hazijapimwa. *TIC*

imesajili hekta 200,000 za *SUMA JKT* na hekta 267,000 za watu binafsi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja nyingine kuhusu Serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu faida na hasara ya misamaha ya Kodi inayotolewa kupitia *TIC*. Hoja hii ilitolewa na Msemaji wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Devotha M. Likokola kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Devotha Likokola kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuwasilisha maoni ya Kamati kwa ufasaha pamoja na juhudi zake za kuendeleza *VICOBA*. Ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Tathmini kama hii ilishafanyika mwanzoni mwa mwaka 2000 na ilionyesha kwamba kulikuwa na manufaa ya misamaha hii ya kodi na uwekezaji uliongezeka. Pamoja na mafanikio hayo, athari ilionekana wakati kodi hii ilipofutwa. Kwa mfano, mwaka 2009/2010 wakati ambao misamaha ya *Deemed Capital Goods* ilipoondolewa uwekezaji ulipungua kutoka miradi 427 (Julai – Desemba, 2008 hadi miradi 211 Julai - Desemba, 2009) ndiyo ambayo imesajiliwa. Kwa hiyo, mtaona kwamba miradi hii imeshuka kwa asilimia 50 baada ya kuondoa misamaha ya kodi kwa bidhaa za mtaji. Serikali itafanya utafiti wa kina kama Kamati ilivyotaka kuhusu faida na hasara ya misamaha ya kodi inayotolewa kupitia *TIC*.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa kuna dhana ya kuwategemea wawekezaji toka nje ya nchi ni potofu na tutegemee wawekezaji wa ndani Watanzania zaidi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere Mbunge wa Musoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji ni muhimu kama nilivyoeleza kwa kuwa hakuna nchi yoyote duniani inayoendelea bila kuvutia uwekezaji kutoka nje. Hii inatokana na ukweli kwamba uwekezaji kutoka nje pamoja na kuleta mitaji unatoa fursa ya kupata teknolojia, mbinu mpya za menejimenti na masoko.

Takwimu za miradi iliyosajiliwa na *TIC* zinaonyesha kwamba kati ya mwaka 2000 hadi 2010 wawekezaji wa ndani wanamiliki asilimia 48 ya miradi; wa nje asilimia 27 na makampuni ya ubia kati ya wawekezaji wa nje na wa ndani ni asilimia 25. Katika mwaka 2010 pekee, kituo kilisajili jumla ya miradi 509 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 5,066. Kati ya miradi hiyo, miradi 242 inamilikiwa na Watanzania, 160 inamilikiwa na wageni na 107 inamilikiwa kwa ubia wa Watanzania na wageni. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mwelekeo wa Taifa letu katika uwekezaji ni mzuri na tutaendelea kuona kwamba wananchi walio wengi zaidi wanashiriki katika uwekezaji. Taifa lazima lidhibiti uchumi wake na siyo kuwaachia wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kwamba uwezeshaji na uwekezaji uanzie kwenye Halmashauri kwa kuwa na *District Economic Development Master Plan*. Hoja

hii ilitolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai. Vijiji na Wilaya ndiyo chimbuko la uchumi wa Taifa letu na mipango yetu inaanzia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao umebainisha vipaumbele muhimu. Mikoa na Halmashauri zote zinatakiwa kutengeneza mipango ya utekelezaji kwa kuzingitia fursa na vipaumbele vilivyoanishwa katika Mpango huo na mimi binafsi nitatembelea Mikoa yote kuona hilo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa Serikali iwawezeshe wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uwekezaji hasa viwandani na migodini. Aidha, maslahi yaongezwe na unyanyasaji uondolewe kwa wafanyakazi wazalendo. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa George Simbachawene - Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Kulthum Mchuchuli - Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mariam Kisangi - Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitilia mkazo suala hili kupitia uwekezaji mkubwa kwa njia kuu nne ambazo ni:-

(i) Kama Sheria ya Uwekezaji inavyotaka, wawekezaji wanatakiwa kuajiri Watanzania katika nafasi zote isipokuwa pale tu ambapo utaalamu unaotakiwa na mwekezaji haupo nchini. Nami nitahakikisha vijana wetu wanapohitimu wanapata kazi katika miradi mbalimbali ya wageni. Hili linawezekana kama tutajielekeza huko.

(ii) Kituo cha Uwekezaji kimekuwa kikiendesha mpango maalum wa kuwaunganisha wafanyabiashara wadogo kuuza bidhaa zao kwa makampuni makubwa chini ya mpango wa *Business Linkages* ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali. Baraza la Uwezeshaji linajaribu kujiunga au kuji-*link* na wanafunzi wanaohitimu kwenye vyuo mbalimbali ili kuwawezesha kimitaji. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya ambaye kwa muda mrefu amekuwa akipigania vijana.

(iii) *TIC* imekuwa ikihamasisha wananchi kutumia raslimali hususan ardhi wanazomiliki kama sehemu ya kuvutia ubia na wawekezaji wakubwa. Wananchi wa Tanzania lazima wajue ardhi ni raslimali kuu na raslimali kubwa. Kwa hiyo, kila mmoja atumie ardhi yake kuweza kuingia ubia pale panapowezekana na kuitumia ardhi hiyo vizuri. Lakini kuna masharti ya kuandikisha hati miliki. Naomba mfanye hivyo, kama haiwezekani kwa sheria Na. 4 basi mfanye hivyo kwa sheria Na. 5 ya ardhi.

(iv) Serikali imekuwa ikihimiza makampuni makubwa yaongeze michango yao kwa jamii *(Corporate Social Responsibility*) lakini hata hivyo tunaangalia sheria mbalimbali za madini, mafuta na gesi ili Watanzania waweze kunufaika na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, njia zote hizi nilizotaja zinalenga kuongeza nafasi ya ushiriki wa wananchi katika shughuli za uwekezaji viwandani na migodini.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa Serikali iboreshe Sheria ya Uwekezaji ili ilenge kuwanufaisha wananchi kwa kuwa wawekezaji wengine siyo waaminifu na wala siyo wazalendo. Aidha, mwekezaji yeyote wa nje ni lazima awe mbia na wananchi hasa katika masuala ya ardhi na madini. Nampongeza Mheshimiwa Wiliam Ngeleja, leo asubuhi katukumbusha kwamba tusiwaone hawa wawekezaji kama wamekuja kupokonya mali yetu, lakini ni jitihada zetu ambazo zitatufanya na sisi tupate yale tunayotegemea kutoka kwa wawekezaji wakati wao wanatafuta faida kwa ajili ya mitaji wanayoleta na kwamba lazima tuwajenge matajiri wetu na kwamba ili tuwe na soko kubwa la watu wenye mapato ya kati. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa - Mbunge wa Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996, pamoja na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 zimebainisha umuhimu wa uwekezaji wa ndani na wa kutoka nje katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Serikali kwa kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* imekuwa ikihamasisha wawekezaji wa ndani na wa kutoka nje wawekeze katika fursa mbalimbali tulizokuwa nazo kama madini, viwanda, kilimo utalii na miundombinu ili kujenga uchumi wetu. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2005-2010), jumla ya miradi 3,881 imesajiliwa na *(TIC),* katika miradi hiyo, asilimia 51 ni ya wawekezaji wa ndani, asilimia 25 ni ya wawekezaji wa nje na asilimia 24 ni ya ubia. Serikali imeimarisha sekta mbalimbali ambazo mwekezaji kutoka nje anatakiwa awe na ubia toka ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sekta hizo ni Mawasiliano, Mabenki na Bima. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha sera, sheria na mazingira ya uwekezaji ili kuzidi kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Vilevile, Serikali imeboresha Sheria ya Madini na Sheria ya Utalii ili kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji katika sekta hizo. Juhudi hizi zitakuza uwekezaji na kuongeza pato la Taifa, kuongeza ajira na kuleta teknolojia mpya pia kujenga matajiri wetu. Naomba Watanzania wachukue jukumu hilo na hasa vijana wetu ambao ndiyo nguvukazi yetu na tegemeo la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kwamba Serikali iboreshe mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kupunguza gharama za kufanya biashara. Nilipokuwa nasoma kitabu cha Mwalimu Nyerere alipokuwa Afrika Kusini, alisema Afrika Kusini ina miundombinu mizuri ya kuweza kuvutia wawekezaji lakini Tanzania haina bahati kama Afrika Kusini, au Ulaya au Marekani. Namna pekee ya kuwavutia wawekezaji ni kuwa na namna yetu tofauti na wengine ili wawekezaji waje Tanzania, lakini wanapokuja na sisi tujue tunanufaika nao kwa namna gani.

Moja ya maeneo ambayo tunapaswa kuyaangalia ni kupunguza gharama za kufanya biashara Tanzania hasa urasimu ndani ya Serikali, rushwa na laghai mbalimbali. Wametokea Watanzania ambao wanashirikiana na wawekezaji kutoka nje wanawalaghai. Hii inaondoa sifa nzuri ya Watanzania. Naomba tusifanye hivyo, anafanya mmoja, lakini Tanzania yote inaonekana kwamba siyo nchi ya kuaminika.

Mheshimiwa Spika, namna pekee ya kuwavutia wawekezaji ni kuwa na namna yetu tofauti na wengine ili wawekezaji waje Tanzania, lakini wanapokuja na sisi tujue

tunanufaika nao kwa namna gani. Moja ya maeneo ambayo tunapaswa kuyaangalia ni kupunguza gharama za kufanya biashara Tanzania hasa urasimu ndani ya Serikali, rushwa na laghai mbalimbali. Wametokea Watanzania ambao wanashirikiana na wawekezaji kutoka nje na wanawalaghai. Hii inaondoa sifa nzuri ya Watanzania. Naomba tusifanye hivyo. Anafanya mmoja, lakini Tanzania yote inaonekana kwamba siyo nchi ya kuaminika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa Serikali iimarishe usimamizi wa utekelezaji wa sera na sheria ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuepusha migogoro kama iliyojitokeza**.** Hili ni eneo muhimu sana. Sekta binafsi inaogopa kwenye maeneo mengine. Inapokuwa na ubia na Serikali inakuwa haina uwoga huo ila jambo muhimu ni kuhakikisha kwamba *risks* zinagawanywa ipasavyo na manufaa yanagawanywa ipasavyo na tunafanya utafiti yakinifu wa kuona kwamba tunapata faida gani na sekta binafsi inapata faida gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi sana, lakini naona kwamba siyo vizuri kengele ya pili inikute, sehemu iliyobaki itajibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mfuko wa JK umesaidia sana wananchi wa hali ya chini kiuchumi hasa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, takwimu zipo, lakini kwa sababu watu wengi wamesema, tutafanya utafiti wa kina kuona kwamba ni akina nani wamepata, ni akina nani walio walengwa wamekosa ili wale waliolengwa hasa vijana na wanawake waweze kunufaika na mfuko huu kama Rais alivyotaka.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema tena kwamba uwekezaji ndiyo utakaoleta uhuru wa uhakika kwa sababu uhuru wa kujitawala hautoshi bila kujitegemea kiuchumi. Naomba kila Mtanzania mmoja mmoja, kwa pamoja na Serikali na wawekezaji kutoka nje waone kwamba hii ni sehemu nzuri ya uwekezaji, lakini tuhakikishe kwamba wale walio wengi wananufaika ili kudumisha amani na utulivu na hao ambao wanaandamana waache kuandamana.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakushukuru na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita msemaji wa mwisho mchana huu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge). *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nishiriki katika kuchangia, lakini kwa maana ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa mwaka 2011/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Isimani kwa kuwa na imani kubwa kwangu na kunipitisha bila kupingwa ili niwe

Mbunge wao kwa kipindi cha tatu. Ninawaahidi sitawaangusha na kule kwa sababu wengi wao ni wakulima wazuri wa mpunga, wana TV hivi sasa wanatazama.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kwa namna ya pekee kuwashukuru Waheshimiwa wafuatao: Mheshimiwa Mizengo Pinda - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezeshaji na Uwekezaji); Mheshimiwa Kpt. John Mkuchika - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI); na Manaibu Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa; Mheshimiwa Pindi H. Chana - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala na Wajumbe wa Kamati hii; Makatibu Wakuu wa Ofizi zote za Waziri Mkuu; Manaibu Katibu Wakuu; Wakuu wa Idara na Taasisi zote zilizopo chini ya Waziri Mkuu na Wakurugenzi na Watumishi wa ofisi hii, kwa ushirikiano mkubwa sana wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nimshukuru sana mke wangu anaitwa Jerumina Lukuvi na watoto wangu watatu, Norbert, Brown na Anificie, kwa huruma yao ya kunivumilia sana, maana mimi nimekuwa kama mkazi wa Dodoma sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba leo nimshukuru kwa dhati kabisa Mzee Ali Hassan Mwinyi - Rais wa Awamu ya Pili. Huyu ndiye aliyenianzishia mbio za kufanyakazi ndani ya Serikali, alinipa ukuu wa Wilaya mwaka 1994, namshukuru sana. Lakini pia namshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri mwaka 1995 – 2000, na mwaka 2000 – 2005 alinipandisha kuwa Waziri. Zaidi nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa na mnono alioupata kwa kishindo katika uchaguzi, lakini pia kwa kuniamini na kunipa Ukuu wa Mkoa wa Dodoma kwa miaka mitatu, na Dar es Salaam kwa mwaka mmoja na nusu na pia baadaye kunirejesha tena kwenye nafasi hii kwa kipindi kingine kuanzia mwaka jana. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ninawashukuru na kuwapongeza tena Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar, kwa ushindi mkubwa alioupata kule Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Bilali - Makamu wa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru hawa wote kwa sababu hawa ndiyo walionifanyia historia ya maisha yangu kwa miaka 16. Nchi hii kuna mama mmoja tu ambaye amewahi kuvunja rekodi ya kuwa na utumishi uliotukuka kwa nafasi zote za uteuzi za kisiasa, yaani Naibu Waziri, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Waziri. Huyu ni Zakia Hamdani Meghji, amewahi kuzunguka nafasi zote hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hapo na mimi nimevunja rekodi, nimefuata nyayo nimekuwa Naibu Waziri, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Waziri. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Zakiah Hamdani Meghji ingawa alikuwa mbali, nilikuwa namfuatia kama chuo changu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia, lakini nataka niseme kwamba inawezekana sitaweza kukidhi majibu yote ya hoja hii, lakini tunachoahidi sisi wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu tutachapisha hoja zote na majibu ili Waheshimiwa Wabunge wote waweze kusoma. Lakini pia hoja nyingi ambazo ziko humu ndani, kwa sababu Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mratibu wa shughuli zote za Serikali, baadhi ya hoja zake tumezipeleka kwa Mawaziri ambao watazijibu sambamba na zile hoja zilizotolewa kwenye Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge wakubali kwamba kama hawatasikia tuliyoyasema sisi wote tuliosema hapa leo asubuhi na pengine inawezekana hata kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, waamini tu kwamba majibu yote yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika shukrani zangu, naomba niwapongeze sana na kuwashukuru kwa kazi kubwa ya usimamizi wa utekelezaji wa ilani, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wote na Wakuu wa Mikoa Tanzania yote. Hawa ndiyo tunaweza kusema kama ingekuwa ni majembe ya kulima, basi haya ndiyo matrekta katika Kilimo Kwanza, lakini kwa maana ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo hoja zimetolewa nyingi lakini nianze tu na maswali matatu ambayo kuna Waheshimiwa Wabunge waliyauliza hapa. Mmoja anauliza kwamba, tukibanwa sana kwenye vyama vyetu tusipokubaliana na misimamo: Je, tutafukuzwa Ubunge? Hili swali nafikiri ni la kizushi, lakini limeulizwa. Mimi naamini kwamba wananchi ndiyo wametuchagua. Tumefika hapa kupitia milango ya Vyama, kwa hiyo, yeyote mwenye hofu ambaye anafikiri ana mnyororo amefungwa hakubaliani na maamuzi ya Chama chochote, ajiamini kwamba yeye ni Mbunge na amechaguliwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa vyovyote vile kama kuna hoja yoyote iko Mahakamani, atakwenda Mahakamani tu, Mahakama itamrudisha Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuna swali hapa: Je, vitabu vya ilani na ahadi za Rais mtatoa? Tutatoa maana maswali mengi sana yameulizwa hapa kuhusiana na utekelezaji wa ahadi za Rais. Tunaahidi tutawachapishia, tutaleta hivyo vitabu ili watu wote mjue ahadi zote zilizoahidiwa na Rais, maelekezo yake katika hotuba ya kwanza hapa Bungeni, lakini na mpango wetu wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tutawapeni wote kwa sababu wote lazima tukae katika msingi huo mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwingine anauliza hapa, hivi kwanini wale ambao hawakuunga mkono bajeti wapewe miradi? Nchi hii imekubali yenyewe mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, kwa hiyo, humu ndani tukibishana, tunabishana kwa mujibu wa Katiba. Wanaopinga hoja wanapinga kwa mujibu wa katiba, na sisi tunaounga mkono hoja, tunafanya hivyo kwa mujibu wa Katiba. Kwa sababu Serikali hii imechaguliwa na wananchi wote bila ubaguzi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itatekeleza kazi zake na itatekeleza Ilani ya Uchaguzi mahali popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ubaguzi wowote. *(Makofi)*

Hoja nyingine hapa imeulizwa na Mheshimiwa Pindi Chana - Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwamba vitabu vya bajeti viwasilishwe kwa

wakati. Hii ni hoja ya msingi. Nataka nikiri tu kwa niaba ya Serikali kwamba kwa kweli vitabu vya bajeti safari hii tumecheleweshа kidogo na ni kwa sababu za kiufundi. Nafikiri kipindi kijacho tutajitahidi viwahi mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja inayohusu Uchaguzi Mkuu imechangiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana, lakini pia imechangiwa na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni -Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Ezekia D. Wenje.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo imechangiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, inasema Serikali ihamasishe wapiga kura kujitokeza kwa wingi wakati wa kujiandikisha. Mimi nasema kwa ufupi ushauri umezingatiwa.

Hoja ya pili ilisema Serikali ihakikishe kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi inashirikiana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar katika kutoa elimu kwa wapiga kura. Hili nalo nasema ushauri umepokelewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe elimu kwa wagombea, wananchi pamoja na vyama vya siasa juu ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Hili ni la Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, lakini pia limechangiwa na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar. Nasema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu wazima ya Tanzania Bara na Zanzibar, itaendelea kuendesha mafunzo kwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine inayosema. Serikali ihakikishe kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inapata ofisi na maghala. Hii ni hoja iliyotoka kwenye Kamati. Serikali imeshatoa kiwanja kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya ujenzi wa maghala hayo. Mchoro wa majengo hayo umeshaandaliwa. Fedha zikipatikana wataanza kujenga maghala ya kisasa zaidi yenye hadhi ya kuhifadhi hizi nyaraka.

Lakini pia kuna hoja inayosema Serikali itoe maelezo kwa vyombo vya habari kunyimwa uhuru wakati wa uchaguzi wa mwaka 2010. Hii imetolewa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman A. Mbowe. Vyombo vya habari vina uhuru mkubwa na vimetekeleza kazi yake kwa uhuru mkubwa wa kuandika na kutangaza na viliendelea kuwa na uhuru huo wakati wote wa kampeni za uchaguzi. Pale ambapo chombo cha habari kinakiuka matakwa ya sheria, hukemewa na hatua huchukuliwa kwa mujibu wa Sheria. Serikali haitaacha na wala haitaweza kuacha vyombo vya habari kukiuka sheria pamoja na maadili ambayo vyombo vyenyewe vimekubaliana katika Baraza lao.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maelezo kuhusu upungufu uliojitokeza katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mbowe, ameuliza, Katika uchaguzi wa mwaka 2010 watu waliojitokeza kupiga kura wengi walipiga kura. Daftari la Kudumu la Wapigakura lilipelekwa mapema vituoni

na majina ya wapigakura yalibandikwa siku nane kabla ya uchaguzi ili watu wajue ni vituo gani wanatakiwa wapigie kura. Baadhi ya majina ya watu hao hayakuonekana na sababu ni kwamba watu kutokwenda kukagua Daftari la Kudumu la Wapigakura wakati lilipowekwa wazi ili wahakiki majina yao na hivyo kushindwa kutoa taarifa mapema kwa Tume iwapo majina yao yamekosekana ili yaweze kuingizwa.

Pili, baadhi ya wapigakura kutokuwa makini na wavumilivu wakati wanatafuta majina yao katika daftari na hivyo kuondoka vituoni bila kuona majina yao na kutokupiga kura licha ya majina yao kuwepo kwenye daftari.

Mheshimiwa Spika, kuna swali lingine limeulizwa na kutaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusu kujitokeza kwa tatizo la karatasi za kupigia kura na karatasi kufutika mara baada ya zoezi la kura kumalizika katika uchaguzi wa 2010. Aidha, Serikali ieleze ni shirika au kampuni gani ilitumika kuchapisha. Maswali haya yote yameulizwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Mbowe.

Mheshimiwa Spika, karatasi za kupigia kura zilichapishwa kwa ubora wa hali ya juu, haziwezi kufutika hata baada ya miaka kadhaa. Karatasi zilizodaiwa kufutika ni fomu za matokeo. Fomu hizo zilitengenezwa kwa namna ambayo ukijaza fomu ya mwanzo *(original)* nakala sita (6) zinajitengeneza zenyewe *(self copying forms).* Ili fomu hizo zitoe nakala zinazosomeka, mjazaji anapojaza fomu hiyo anatakiwa akandamize kalamu ipasavyo. Lakini kuna baadhi ya Watendaji hawakukandamiza kalamu zao ipasavyo na hivyo nakala zilizotengenezwa kutosomeka vizuri. Ila *original forms* zilizotumika kujumlisha matokeo zilisomeka vizuri. Katika uchaguzi wa mwaka 2015 elimu zaidi itatolewa kwa umma kuhusiana na ujazaji huo wa fomu husika.

Mheshimiwa Spika, kampuni iliyotumika kuchapisha karatasi za kura na fomu za matokeo ni kampuni iliyopo nchini Uingereza inayoitwa *Kalamazoo Secure Solution* ambayo ilipatikana baada ya kushinda zabuni iliyotangazwa kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Kampuni hii ina uwezo mkubwa na uzoefu wa takribani miaka 100 wa kuchapisha nyaraka nyeti. Ilichapisha karatasi za kura katika nchi mbalimbali zikiwemo Nigeria, Kenya na Malawi katika chaguzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifafanue ucheleweshaji wa kutangaza matokeo. Katika baadhi ya Majimbo, matokeo yalichelewa kutangazwa kwa sababu mbalimbali. Moja, ni ubishi uliokuwepo kwa baadhi ya wagombea au mawakala wakati wa zoezi la kuhesabu kura. Pili, baadhi ya wagombea au mawakala hutaka kura zihesabiwe na kujumlishwa upya hata pale ilipoonekana dhahiri wagombea husika wameshindwa. Tatu, kuzuka kwa vurugu zilizosababishwa na baadhi ya wafuasi mashabiki wa vyama vya siasa katika Vituo vya Kujumlishia kura, kulifanya baadhi ya watendaji kuwa na hofu na uwoga na hivyo kupunguza kasi ya ufanisi katika zoezi la kujumlisha kura. Hata hivyo, kwa ujumla, matokeo ya uchaguzi yalitolewa katika muda wa siku moja na siku nne.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo anasema Serikali ihakikishe kuwa inatekeleza ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais. Pongezi na ushauri vimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, kuna ushauri kwamba Tume ya Uchaguzi iwe ni chombo huru ili iweze kutenda haki kwa vyama vyote. Huu ni ushauri wa Mheshimiwa Ezekia Wenje - Mbunge wa Nyamagana. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 77 (7) na 74 (11) Tume ya Uchaguzi ni Idara huru inayofanya maamuzi yake bila kufuata amri ya mtu yeyote, Chama chochote au Serikali. Katika eneo hili, hizi ndiyo hoja zilizojitokeza. Lakini ziko hoja nyingine chache ambazo tutaziandikia.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya dawa za kulevya ambayo imeulizwa vilevile na Mheshimiwa Pindi Chana, lakini pia Mheshimiwa Amina Abdallah Amour na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar. Hawa ni baadhi ya waliojitokeza kuuliza maswali haya. Kwa ufupi katika eneo hili baada ya kuona hizi changamoto nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa tumeamua kama Serikali kwamba ile timu *(task force)* yetu ambayo inafanya kazi hii ije itoe semina hapa kwa Waheshimiwa Wabunge. Katika kipindi hiki cha Bunge, tutaomba nafasi na nitaomba Wabunge wote wahudhurie ili angalau tuwaonyeshe mambo yanayofanyika, watu wanaohusika tutawaonyeshe aina ya dawa tulizozikamata na mbinu mbalimbali zinazotumika na hao watu kutoka huko wanakozitoa mpaka kufika hapa na soko lao na waathirika wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshaagiza Tume ya Dawa za Kulevya na *task force* wajiandae vizuri maana sisi walituonesha juzi kwenye Semina Elekezi, waje hapa wawaonyeshe Waheshimiwa Wabunge jinsi vijana wetu wanavyoathirika na watu hao mnaowaita vigogo maana vigogo tafsiri yake mara nyingi huchukuliwa kwamba ni watu wa Serikali, lakini vigogo kwa tafsiri pana ni watu wenye uwezo, wanaojihusisha na shughuli hizi pamoja na wale ambao aliwasema Mheshimiwa Rais baadhi ya viongozi wa dini. Tutawaonesha moja kwa moja muwaone na shughuli wanazozifanya, walivyokamatwa ili Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi mshirikiane vizuri na Serikali lakini mkiwa mmearifiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii nataka kuwaomba wote waliotoa changamoto katika eneo hili wakubali kwamba ushauri wao tumeupokea, tunautekeleza, lakini zaidi ingawa hapa nimetaja, hata huyo kiongozi wa dini ambaye ni raia wa Nigeria ni Kiongozi wa Kanisa la *Lord's Chosen Charismatic Revival Church,* lililopo Kinondoni Biafra ambaye alikamatwa na jumla ya kilo 81 za *cocaine* maeneo ya Kunduchi Mtongani. Kanisa hilo lina matawi katika Mikoa ya Mwanza na Arusha, pia katika nchi za Kenya, Afrika Kusini na Uingereza. Kabla hatujatangaza taarifa hii, ukiwauliza waumini, maana ana waumini wengi sana kwa maelfu, mchungaji wenu yuko wapi? Wanasema amesafiri, kumbe tumemshika. Sasa angalau wanajua kwamba yuko wapi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge katika eneo hili tutakuja kuelezana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Bunge, Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa changamoto kwa Kamati, lakini Kiongozi wa Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Mbowe ametoa changamoto. Changamoto za Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwepo kwa bajeti ya kutosha, uendeshaji wa Mikutano ya

Bunge na kuhakikisha kuwa fedha zimepatikana kwa wakati, Serikali itatue tatizo finyu la maegesho. Hili la fedha tumejitahidi na bajeti nimeiona.

Mheshimiwa Spika, juu ya maegesho ya magari katika Ofisi za Wabunge Dar es Salaam, Serikali imepanga kujenga maegesho ya magari katika kiwanja kilichopo nyuma ya Ofisi ya Bunge, kiwanja hiki awali kilikuwa mali ya *International School of Tanganyika*, tutalifanya hilo, maana pale mahali ni pafinyu sana. Lakini pia Serikali iangalie uwezekano wa Wabunge kujiunga na Bima ya Afya, iundwe Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kusimamia vita dhidi ya rushwa *(Oversight Committee)*. Hili ni pendekezo la Mheshimiwa Mbowe. Haya yote mawili nitayafikisha kwa Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wetu Wabunge, mambo haya huwa tunayazungumza wenyewe na tunayaamulia wenyewe kupitia vikao vyetu vya Kamati ya Uongozi na mengine yanahusu Tume.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba Wabunge wa Kambi ya Upinzani wanakamatwa na Polisi bila ya kuzingatia sheria, haki, kinga na madaraka ya Bunge. Hilo lilisemwa na Mheshimiwa Mbowe. Nasema kama Serikali kwamba, hakuna ubaguzi unaofanywa wakati wa ukamataji wa Wabunge. Katika ukamataji, Polisi huongozwa na sheria na mazingira ya kesi husika. Wabunge wa Upinzani waliokamatwa na Polisi hawakuwa katika shughuli za Bunge. Maandamano au kufanya fujo sio shughuli za Bunge. Mheshimiwa Freeman Mbowe alikamatwa kwa amri ya Mahakama, na kisheria, Polisi hawana uwezo wa kuhoji amri ya Mahakama. Mbunge wa CCM anayedaiwa kupendelewa kwa kuombewa kibali cha Spika hakukutwa eneo la tukio, yeye ni mtuhumiwa tu na kimsingi lengo halikuwa kumkamata bali kumhoji kuhusiana na tuhuma za mauaji yaliyotokea Mwanza. Wakati huo yeye alikuwa Dodoma kwenye shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ameomba iundwe Kamati ya Bunge ya Kusimamia Utekelezaji wa Ahadi za Serikali. Hili nalo nitalipeleka kwa Mheshimiwa Spika ili tulijadili kwa utaratibu wetu, maana kwa utaratibu wa Bunge mimi sina mamlaka ya kuwaamria, ila kuna vyombo vinavyoundwa hapa ambavyo kwa kushirikiana nao, tunaweza tukakubaliana.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba Kamati ya Maadili ya Bunge iwachukulie hatua Wabunge ambao wanaonyesha utovu wa nidhamu Bungeni, kwani kumekuwepo na tabia ya Waheshimiwa Wabunge kutoheshimu Kiti jambo linaloijengea Bunge picha isiyo nzuri kwa wananchi. Mimi nadhani jambo hili Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wamekuwa wanalitolea maelezo kila mara.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la maafa ambalo limechangiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa Pindi Chana; Kiongozi wa Upinzani Bungeni; na Mheshimiwa Lekule Laizer - Mbunge wa Longido; Mheshimiwa Hussein Nassor Amour - Mbunge wa Nyang'wale; Mheshimiwa Regia Mtema - Mbunge wa Viti Maalum; Brig. Hassan Ngwilizi - Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Esther Midimu - Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rachel Masishanga - Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kaika Telele - Mbunge wa Ngorongoro; Mheshimiwa Mohamed Missanga - Mbunge wa Singida Magharibi; Mheshimiwa Ahmed Salum - Mbunge wa Solwa, Mheshimiwa Ritta Kabati - Mbunge wa

Viti Maalum Iringa; Mheshimiwa Maria Hewa - Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari Nyangwine - Mbunge wa Tarime na Alphaxard Lugola - Mbunge wa Mwibara.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, katika maeneo hayo, Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri mbalimbali wa namna ambavyo wanafikiri Kitengo hiki cha Maafa kiimarishwe. Lakini wengi sana hapa wameomba Serikali iangalie suala la njaa katika maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Freeman Mbowe amependekeza kwamba Serikali iweke mfumo wa awali wa kutahadharisha umma juu ya ujio wa majanga. Serikali inatumia Taasisi zake zilizopo katika kutoa tahadhari ya ujio wa majanga kama vile mamlaka ya hali ya hewa na timu maalum inayofuatilia hali ya chakula nchini. Aidha, Serikali inapitia upya Sera ya Sheria ya Maafa ili kukidhi mabadiliko ya teknolojia na mifumo mipya ya utoaji wa tahadhari wa majanga.

Kuna ushauri mwingine umetolewa hapa Serikali iendelee kusaidia Wilaya ya Longido kukabiliana na tatizo la njaa. Mheshimiwa Lekule Laizer - Mbunge wa Longido, mwezi Juni, 2011 Serikali imepeleka tani 3,209 za mahindi pamoja na Sh. 91,456,500 za kusafirishia. Lakini pia tumepeleka tathmini nyingine endapo kutahitajika mahitaji mengine Serikali ni yenu itaendelea kutekeleza. Mheshimiwa Hussein Nassor Amour alisema Serikali ipeleke msaada wa chakula haraka Nyang'wale. Katika tathmini mbili zilizofanyika mwezi Septemba 2010/2011 Wilaya ya Geita ilionekana inajitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, ipo tathmini ya kina ya hali ya chakula inayoendelea kufanyika katika Mikoa hiyo. Pindi itakapopatikana tatizo hilo tutalishughulikia mara moja.

Mheshimiwa Regia Mtema alisema Serikali ifuatilie kwa karibu misaada ya maafa ya mafuriko Kilombero, kwani kuna malalamiko mengi kwamba waathirika hawakunufaika. Kama nilivyojibu wakati ule Serikali imetoa misaada mbalimbali kusaidia wananchi walioathirika na mafuriko hayo kama ifuatavyo: Tumetoa tani 237 za mahindi, tani 30 za maharagwe, mafuta ya kupikia lita 18,000, kilo 1,400 za chumvi, kilo 23,000 za sukari na Sh. 340,000,000/= za kutengeneza barabara, lakini pia tumetoa Sh. 210,000,000/= za kutengeneza madaraja sita. Jukumu la kufuatilia na kuhakikisha kuwa misaada hiyo inafika kwa walengwa ni la Kamati ya Maafa zinazohusika. Kuna Kamati zimeundwa kwa mujibu wa Sheria na Sera, Kamati za Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Hassani Ngwilizi vile vile anaomba tupeleke chakula, mwezi Mei, 2011. Serikali ilitoa msaada wa tani 333 kwa ajili ya Wilaya ya Lushoto, lakini tunafanya tathmini hivi sasa tukiona tena mambo mabaya tutakuja tena. Mheshimiwa Esther Midumu na vile vile Viongozi wa Mikoa na Wilaya wamesema Serikali isimamie chakula cha misaada kisisafirishwe kwenda nchi jirani. Ni kweli Serikali sasa imetoa tangazo la kuzuia usafirishaji wa chakula kwenda nchi za nje hasa kwa sababu ya tishio hili la njaa. Lakini pia tunajipanga vizuri kuhakikisha kwamba kwa baadaye masoko yote ya chakula yawepo ndani ya nchi ili hata hao nchi jirani waje wanunue ndani ya nchi.

Kama Waziri wa Kilimo atakavyosema na ndiyo maana Serikali mwaka huu imeunda chombo maalum cha kununua mazao haya ambacho pengine kitatoa utaratibu

wa namna washiriki wengine watataka kununua mazao haya watashirikiana nacho, lengo ni kwamba mkulima wa Tanzania apate bei nzuri kulingana na jasho lake, lakini pia na nchi yenyewe ijitosheleze kwa chakula.

Mheshimiwa Kaika Telele - Mbunge wa Ngorongoro anasema Serikali isaidie kukabili balaa la njaa lililoikumba Wilaya ya Ngorongoro. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Serikali imetoa jumla ya tani 9,071 za msaada wa chakula katika Wilaya ya Ngorongoro. Lakini pia hivi sasa tunafanya tathmini nyingine, endapo tutaona kuna mahitaji Serikali haitasita kuleta msaada huu. Hali kadhalika Mheshimiwa Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi naye ameomba hivyo hivyo, lakini Serikali tayari imetoa msaada wa chakula cha njaa kwenye maeneo ya Wilaya za Manyoni tani 791, Iramba tani 473. Hata hivyo, tunafanya tathmini katika maeneo hayo ya Mheshimiwa Mbunge pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye alikuwa ameniambia maneno haya endapo kutaonekana kuna umuhimu Serikali haitasita kutoa msaada.

Mheshimiwa Ahmed Salum na Mheshimiwa Ritta Kabati, wote hawa wamezungumzia maeneo yao. Mheshimiwa Ahmed Salum ameomba chakula kwa nguvu zote kwa Jimbo la Solwa. Mheshimiwa Ritta Kabati ameomba chakula kwa ajili ya Jimbo la Iringa Mjini. Nataka kuwaahidi kwamba tunakuja kufanya tathmini na Serikali haitawaangusha. Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine naye ametoa ushauri, lakini mwisho ameeleza juu ya vijiji ambavyo vina matatizo. Nataka kusema tutafanya kama nilivyoeleza.

Mwisho, nataka kusema kwamba hivi sasa kwa eneo hili la maafa tunafanya tathmini, tunakuja huko. Wako Waheshimiwa Wabunge hapa ambao wameniona bila kuchangia, nao ni Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Lugola, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Ritta Kabati nimeshamtaja, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Esther Midumu, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Hussein Nassor - Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Mbunge wa Meatu, Mheshimiwa Freeman Mbowe naye ameongelea habari ya Hai. Tuko Mkoa wa Kilimanjaro sasa hivi tunafanya tathmini na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Arusha, Kilimamjaro, Manyara, Mara, Mwanza na Shinyanga tumetuma timu za wataalamu kwenda kufanya tathmini. Tupo hapa miezi mitatu, tuendelee kushauriana na sisi tutatimiza wajibu wetu.

Liko eneo la udhibiti wa matumizi ya fedha za mali ya umma ambazo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria aliliona katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Akasema kwamba gharama zile ni kubwa sana shilingi bilioni 16. Sisi tumefanya uchambuzi wa mchanganuo wa vifungu hivyo, unaonyesha kwamba gharama za ununuzi wa mafuta, Ofisi ya Waziri Mkuu tunayoizungumza hapa ni pamoja na TAMISEMI yote mpaka kwenye Halmashauri za Wilaya.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Mikoa na kila kitu, jumla uendeshaji wa mafuta, matengenezo na ununuzi wa magari ndiyo hizo shilingi bilioni 16 kwa Tanzania nzima, Serikali za Mitaa na Ofisi zote za Waziri Mkuu. Kwa hiyo, sisi tunafikiri kiwango hiki ni kidogo sana. Kwa sababu kama mnavyojua safari hii Serikali imejizuia sana ununuzi wa

magari mapya na kila anayenunua gari ndani ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania lazima apate kibali binafsi cha Waziri Mkuu. Kwa hiyo, haya tumepunguza sana. Ni gharama ndogo sana ukilinganisha na eneo pana ambalo linahudumiwa na fedha hizi.

Eneo la UKIMWI tumepata ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati - Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Fakharia Shomar, Mheshimiwa Margaret Agness Mkanga, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi na Msemaji Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Devota Likokola. Lakini pia tulipata ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta.

Mheshimiwa Spika, hawa wote wametoa ushauri mbalimbali kuhusiana na mambo yanayohusiana na mambo ya UKIMWI. Kwa kuwa tuna Kamati yetu hapa na sisi Wabunge wengi ni Wabunge wa *TAPAC* tulishatoa semina Dar es Salaam kwa Kamati hii, lakini tutajitahidi tena endapo mtapata nafasi tuje tuwajibu hayo kwa sababu wengi wa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati hii, tuje tuwajibu yote haya na shughuli gani inafanywa na *TACAIDS* na *coordination* yote ya masuala haya ya UKIMWI. Kwa hiyo, naahidi bila shaka inaweza kutekelezwa tukiwa hapa tu Mwenyekiti wa Kamati hii ya *TAPAC* anaweza aka-*organise* na sisi tuko tayari kushiriki katika kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna Mheshimiwa Salum Barwany amezungumzia ahadi za Rais. Nasema kama nilivyosema awali kwamba ahadi za Rais zitaendelea kutekelezwa. Nataka niwaambie tu wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna ahadi za Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambazo zitatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, ahadi za Rais vile vile zitatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na hii ndiyo bajeti ya kwanza ya miaka mitano. Msije mkafikiri basi hapa tumeshamaliza, kila jambo lazima litekelezwe.

Ninachoweza kuwaahidi ni kwamba ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais na ahadi zilizotolewa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi zitatekelezwa katika bajeti tano za kipindi hiki cha Ilani. Kwa ushauri wa Mheshimiwa Salum Barwany nataka kumwambia kwamba asiwe na wasiwasi, tunayo bajeti ya miaka mitano *inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda mambo haya yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya muundo wa Ofisi ya Waziri ili kupunguza urasimu na imependekezwa TAMISEMI iwe na Wizara inayojitegemea. Ushauri huu umetolewa na Mheshimiwa Edward Lowassa - Mbunge wa Monduli, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Mustapha Akunaay na Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 36 na 37. Mamlaka ya Kuunda Wizara na Idara ni ya Mheshimiwa Rais. Hapa uwezo wangu wa kujibu unaishia hapo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipunguze ukubwa wa Baraza la Mawaziri ambalo ni mzigo mkubwa kwa Serikali kwani lina Wajumbe 54. Mheshimiwa Lyimo kwa mujibu wa Katiba na vifungu hivyo nilivyovisema Mamlaka ya Uteuzi wa Viongozi Wakuu pamoja na wale wa Mikoani ni Mheshimiwa Rais na Mamlaka haya yanalenga kubadilisha vifungu vya Katiba jambo ambalo linahitaji mchakato mrefu. Lakini kwa

sasa kwa sababu mchakato wenyewe unaanza, basi pengine tusubiri maoni ya wananchi wanasemaje.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na zaidi, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nataka kuwahakikishia wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaifanya kama Serikali kwa dhati bila ubaguzi kama nilivyosema na tutaendeleza kazi hii kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya, kasi zaidi na nguvu zaidi. Mheshimiwa Zitto tuko pamoja, naona tunaelewana na Mheshimiwa Mbowe amenikumbusha hapa. Kwa hiyo, huo ndiyo msimamo, tutatekeleza kwa kasi zaidi na ari zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema katika utekelezaji wa jambo hili, Serikali imejipanga. Kama nilivyosema, kuna viongozi wenzetu wa Mikoa wanasaidia chini ya Waziri Mkuu. Lakini na sisi ndani ya Serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa. Sisi tunajua tuko kila mahali, tutasimamia jambo hili vizuri na nataka wananchi wapoe, wajue kwamba Serikali yao itatekeleza.

Mheshimiwa Spika, sisi ndani ya Serikali, maandamano yetu ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ndiyo maandamano yetu! Nataka niwaambie wananchi kila mtakapowaona Waheshimiwa Wabunge wenu wanakwenda kwenye maandamano, waacheni, sisi tutakuja kufanya hiyo kazi ya maendeleo huko kwenu, ndiyo kazi yetu sisi. Sisi tumechaguliwa kufanya maendeleo mahali pote, tutatekeleza kazi hii mpaka Mheshimiwa Mbowe atajisikia. *(Makofi)*

Nataka kusema kwamba miongoni mwa watu ambao wameomba chakula katika maeneo yao ni Mheshimiwa Lowassa, nilimwacha, lakini nae katika mchango wake amechangia sana jambo hili. Nawashukuru sana wananchi kwa uvumilivu wenu na kutusikiliza. Tunaomba kama Serikali, mwendelee kutuunga mkono. Sisi tuko pamoja.

Nawashukuru sana ndugu zangu wa Ismani kwa kuniunga mkono. Ila siku moja mliniangusha. Mmemwona Mbunge wa Kigoma amefika mpaka kwenye Jimbo langu kufanya maandamano halafu mmemwacha, hamkumpa hata gunia la mpunga. Siku nyingine watakapokuja kufanya maandamano kama barabara wanayoitaka haipitiki tengenezeni wapite kwa salama, halafu wakija wapeni na chakula, wapeni na mpunga. Mheshimiwa Zitto nimesikitika sana, nakuomba radhi umefika kwangu bila ya kupata chakula.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nakupongeza wewe kwa kazi nzuri kama *Chip Whip* mstaafu na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati, Tume kwa ushirikiano mkubwa ambao umetuwezesha kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoeleza asubuhi, hawa Mawaziri wanaomsaidia Waziri Mkuu wote wameweza kujaribu kueleza hoja katika maeneo yao.

Kwa hiyo, mchana nawaombeni Waheshimiwa Wabunge, vile vitabu mlivyopewa sijui Dar es Salaam au hapa viingie humu ndani na viko vitabu vitatu viingie humu ndani na ndiyo kazi inaanza humu ndani na maelekezo ya vile vitabu nitawaambia mchana. Maana nikiwaeleza bila vitabu sasa nitapoteza muda wangu bure. Mviweke humu ndani kuanzia sasa mpaka tutakapomaliza Bunge ndiyo itakuwa kazi ya vile vitabu na kama wewe uliacha wapi, nenda katafute viwepo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, sina mengine, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, pale asubuhi tulikuwa tumepata maelezo kwa Mawaziri wanaomsaidia, sasa ni zamu ya Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema hadi leo ninapohitimisha majadiliano ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kusimamia na kuongoza kwa umakini na uvumilivu mkubwa…

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona unafanya kazi ya bure, *Hansard* hai-*record* labda ungekaa kidogo.

Haya hata yasipoingia kwenye *Hansard* sio tatizo, kesho jioni saa moja na nusu, Wabunge wote wanakaribishwa kwenye tafrija kwenye Viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa na muziki utakuwepo, wa Twanga Pepeta na kwa kuwa nyie wengi ni vijana ndiyo wakati wenyewe huo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari.

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema hadi leo ninapohitimisha Majadiliano ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikushukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kusimamia na kuongoza kwa umakini na uvumilivu mkubwa mkubwa majadiliano ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru kwa njia ya kipekee Waheshimiwa Mawaziri kutoka Ofisi ya Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji); Mheshimiwa George Mkuchika – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mheshimiwa William Lukuvi – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge); Mheshimiwa Aggrey Mwanri – Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Mheshimiwa Kassimu Majaliwa - Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Elimu) kwa kuendelea kunishauri na kunisaidia katika kufanikisha majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Niwashukuru pia Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote na Watendaji kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia, kwa michango yao ya kina ambayo kwa kiasi kikubwa imewezesha Ofisi yangu kujua maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi na maeneo ambayo tumefanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 269 walichangia. Waheshimiwa Wabunge 126 walichangia kwa kuzungumza moja kwa moja hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 143 wamechangia kwa njia ya maandishi. Niruhusu niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala; Mheshimiwa Devota M. Likokola, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; Mheshimiwa Michael Laizer – Longido; Mheshimiwa Amos G. Makala – Mvomero; Mheshimiwa Edward N. Lowassa – Mondoli; Mheshimiwa Jenista J. Mhagama – Peramiho; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi – Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Augutino L. Mrema – Vunjo; Mheshimiwa Ismail A. Rage – Tabora Mjini; Mheshimiwa Ali Juma Haji – Chaani; Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa – Chwaka; Mheshimiwa Said Amour Arfi – Mpanda Mjini; Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe Ludewa; Mheshimiwa Abduljabir Marombwa – Kibiti na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad – Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine Mheshimiwa George B. Simbachawene –Kibakwe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga – Viti Maalum; Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha – Viti Maalum; Mheshimiwa Vicent J. Nyerere - Musoma Mjini; Mheshimiwa January Y. Makamba – Bumbuli; Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka – Simanjiro; Mheshimiwa Modestus D. Kilufi – Mbarali; Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi – Mlalo; Mheshimiwa Capt. John D. Komba – Mbinga Magharibi; Mheshimiwa Dkt. Hamis A. Kigwangala – Nzega; Mheshimiwa Desderius J. Mipata – Nkasi Kusini; Mheshimiwa Iganus A. Malocha – Kwela; Mheshimiwa Khalfan H. Aeshi – Sumbawanga Mjini; Mheshimiwa

Mohamed H. Mgimwa – Mfundi Kaskazini; Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi - Viti Maalum; Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele – Ngorongoro; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar - Viti Maalum na Mheshimiwa Subira Hamis Mgalu - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir – Matemwe; Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso – Mpanda Vijijini; Mheshimiwa Dkt. Kulikoyela Kahigi – Bukombe; Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Viti Maalum; Mheshimiwa Haji Khatib Kai – Micheweni; Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo – Magogoni; Mheshimiwa Susan A. Lyimo - Viti Maalum; Mheshimiwa Gosbert B. Blandes – Karagwe; Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli - Viti Maalum; Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali – Ziwani; Mheshimiwa Moza Abedi Saidy - Viti Maalum; Mheshimiwa Hamad Ali Hamad – Magogoni; Mheshimiwa Ali Abdallah - Tumbe; Mheshimiwa Lolensia J. Bukwimba – Busanda; Mheshimiwa Zainabu M. Vullu - Viti Maalum; Mheshimiwa Catherine V. Magige - Viti Maalum; Mheshimiwa Innocent E. Kologeris – Morogoro Kusini; Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge – Makete; Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya - Viti Maalum; Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa na Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo – Kilindi; Mheshimiwa Salum Barwany – Lindi Mjini; Mheshimiwa Moses J. Machali – Kasulu Mjini; Mheshimiwa Ezekiel D. Wenje –Nyamagana; Mheshimiwa Mohammed H. Missanga – Singida Magharibi; Mheshimiwa Riziki Omar Juma - Viti Maalum; Mheshimiwa Thuwayba Idrissa Muhamed - Viti Maalum; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed - Viti Maalum; Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga - Viti Maalum; Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu - Viti Maalum; Mheshimiwa Zarina S. Madabida - Viti Maalum; Mheshimiwa Riziki Said Lulida - Viti Maalum; Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah – Mafia; Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare - Viti Maalum; Mheshimiwa Mohamed Ibrahim Sanya – Mji Mkongwe; Mheshimiwa Haji Juma Sereweji – Mwanakwerekwe na Mheshimiwa John M. Shibuda – Maswa Magharibi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Salome D. Mwambu – Iramba Mashariki; Mheshimiwa Felister A. Bura - Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba – Buchosha; Mheshimiwa Jerome D. Mwanausi – Lulindi; Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir - Viti Maalum; Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya -Viti Maalum; Mheshimiwa Anastazia J. Wambura - Viti Maalum; Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati – Manyoni Mashariki; Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid – Rufiji; Mheshimiwa Seleman J. Zedi – Bukene; Mheshimiwa Juma S. Nkamia –Kondoa Kusini; Mheshimiwa Iddi M. Azzan – Kinondoni; Mheshimiwa Said Mussa Zubeir – Fuoni; Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi - Viti Maalum; Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke -Viti Maalum; Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba – Manyovu; Mheshimiwa Abdul R. Mteketa – Kilombero; Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu – Temeke; Mheshimiwa Lucy P. Owenya - Viti Maalum na Mheshimiwa Vicky P. Kamata - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Agnes E. Hokororo - Viti Maalum; Mheshimiwa Peter M. Msolla – Kilolo; Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusya – Rungwe Magharibi; Mheshimiwa Raya Ibrahim Hamis - Viti Maalum; Mheshimiwa Conchesta Lwamlaza -

Viti Maalum; Mheshimiwa Naomi M. Kaihula - Viti Maalum; Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa – Nanyumbu; Mheshimiwa Ahmed Ali Salum – Solwa; Mheshimiwa Susan L. Kiwanga - Viti Maalum; Mheshimiwa James D. Lembeli – Kahama; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto – Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Said J. Nkumba – Sikonge. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe – Serengeti; Mheshimiwa Silvestry Koka – Kibaha Mjini; Mheshimiwa Faith M. Mitambo – Liwale; Mheshimiwa Yussuf Abdallah Nassir –Korogwe Mjini; Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa – Iringa Mjini; Mheshimiwa Ally K. Mohamed – Nkasi Kaskazini; Mheshimiwa Rashid Ali Omar – Kojani; Mheshimiwa Luhaga J. Mpina – Kisesa; Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila - Viti Maalum; Mheshimiwa Ritta E. Kabati - Viti Maalum; Mheshimiwa Lucy T. Mayenga - Viti Maalum; Mheshimiwa John P. Lwanji – Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Hussein Nassor Amar - Nyang'wale; Mheshimiwa Aliko N. Kibona – Ileje; Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa – Naibu Waziri TAMISEMI; Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri – Naibu Waziri TAMISEMI; Mheshimiwa George Mkuchika – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI; Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji na mwisho ni Mheshimiwa William V. Lukuvi – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu –Sera, Uratibu na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa idhini yako niendelee kuwatambua Wabunge waliochangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Vicent J. Nyerere – Musoma Mjini; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa –Lupa; Mheshimiwa Khatib Said Haji – Konde; Mheshimiwa Rose K. Sukum - Viti Maalum; Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim – Mtambile; Mheshimiwa Hamad Ali Hamad – Magogoni; Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac - Viti Maalum; Mheshimiwa Amina N. Makilagi - Viti Maalum; Mheshimiwa Mwanamrisho T. Abama - Viti Maalum; Mheshimiwa Ali Hamis Seif – Mkoani; Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo - Viti Maalum; Mheshimiwa Mary P. Chatanda - Viti Maalum; Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo –Tandahimba; Mheshimiwa Seleman J. Zedi – Bukene; Mheshimiwa Omar A. Badwel – Bahi; Mheshimiwa Salim Hemed Khamis – Chambani; Mheshimiwa Rachel M. Robert - Viti Maalum; Mheshimiwa Agustino M. Masele – Mbogwe; Mheshimiwa Charles M. Kitwanga – Misungwi; Mheshimiwa Haji Juma Sereweji – Mwanakwerekwe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed – Wawi; Mheshimiwa Josephat S. Kandege – Kalambo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto – Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Hussein N. Amar – Nyanghw'ale; Mheshimiwa Clara D. Mwamtuka - Viti Maalum; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour - Viti Maalum; Mheshimiwa Riziki Omar Juma - Viti Maalum; Mheshimiwa Regia E. Mtema - Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Haji H. Mponda - Ulanga Magharibi; Mheshimiwa David M. Malole – Dodoma Mjini; Mheshimiwa Charles J. Mwijage – Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay – Mbulu; Mheshimiwa Zakia H. Meghji –Kuteuliwa; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye - Viti Maalum; Mheshimiwa David Z. Kafulila – Kigoma Kusini; Mheshimiwa

John J. Mnyika – Ubungo; Mheshimiwa Gerson H. Lwenge – Njombe Magharibi; Mheshimiwa Gosbert B. Blandes – Karagwe; Mheshimiwa Namelok E. Sokoine - Viti Maalum; Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila - Viti Maalum; Mheshimiwa Diana M. Chilolo - Viti Maalum na Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa –Kalenga. *(Makofi)*

Wengine Mheshimiwa Aliko N. Kibona – Ileje; Mheshimiwa Bahati Ali Abeid – Viti Maalum; Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo – Mbinga Mashariki; Mheshimiwa Lucy F. Owenya -Viti Maalum; Mheshimiwa Ismail A. Rage - Tabora Mjini; Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje –Chilonwa; Mheshimiwa Herbert J. Mntangi – Muheza; Mheshimiwa Magreth A. Mkanga – Viti Maalum; Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale – Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse – Karatu; Mheshimiwa Sylivester Masele Mabumba – Dole; Mheshimiwa Joseph R. Selasini – Rombo; Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi - Viti Maalum; Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah - Viti Maalum; Mheshimiwa Susan A. Lyimo - Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare - Viti Maalum na Mheshimiwa Ramadhan Haji Salehe – Bumbwini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Seleman Said Jafo – Kisarawe; Mheshimiwa Josephine T. Chagula - Viti Maalum; Mheshimiwa Salehe A. Pamba – Pangani; Mheshimiwa Margaret S. Sitta - Viti Maalum; Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda - Viti Maalum; Mheshimiwa Antony G. Mbassa – Biharamulo Magharibi; Mheshimiwa Amina A. Clement – Koani; Mheshimiwa Christina L. Mughwai - Viti Maalum; Mheshimiwa Ester L. Midimu - Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine – Tarime; Mheshimiwa Andrew J. Chenge – Bariadi Magharibi; Mheshimiwa Henry D. Shekifu – Lushoto; Mheshimiwa Hawa A. Ghasia – Mtwara Mjini; Mheshimiwa Lolensia M. Bukwimba –Busanda na Mheshimiwa Halima J. Mdee – Kawe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Sara M. Ali - Viti Maalum; Mheshimiwa Juma Sururu Juma – Bububu; Mheshimiwa Maria I. Hewa - Viti Maalum; Mheshimiwa Azza Hillal Hamad - Viti Maalum; Mheshimiwa Jadi Simai Jadi – Mkwajuni; Mheshimiwa Tauhida C. Galos Nyimbo - Viti Maalum; Mheshimiwa Philipa J. Mturano - Viti Maalum; Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee –Jang'ombe; Mheshimiwa Mariam R Kasembe – Masasi; Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir – Dimani; Mheshimiwa Desderius J. Mipata – Nkasi Kusini; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu – Kiembe Samaki, Mheshimiwa Zarina S. Madabida - Viti Maalum; Mheshimiwa Steven H. Ngonyani - Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Abuu H. Jumaa – Kibaha Vijijini; Mheshimiwa Ignas A. Malocha – Kwera; Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo –Liwale; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar - Viti Maalum na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye – Arumeru Magharibi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Gaudencia M. Kabaka - Viti Maalum; Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa – Amani; Mheshimiwa Salome D. Mwambu – Iramba Mashariki; Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer – Mikumi; Mheshimiwa Eng. Mohammed Habib Juma Mnyaa – Mkanyageni; Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis – Chonga; Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina – Ngara; Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan – Kinondoni; Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir - Viti Maalum; Mheshimiwa Suleiman

Nassib Omar – Mfenesini; Mheshimiwa David A. Silinde – Mbozi Magharibi; Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu – Kilwa Kaskazini; Mheshimiwa Dkt. Lucy S. Nkya – Morogoro Kusini Mashariki; Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari - Viti Maalum; Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla – Kilolo na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar - Viti Maalum. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Charles J. Mwijage – Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Subira H. Mgalu - Viti Maalum; Mheshimiwa Naomi M. Kaihula - Viti Maalum; Mheshimiwa Grase S. Kiwelu - Viti Maalum; Mheshimiwa Zainabu M. Vullu - Viti Maalum; Mheshimiwa Philipo A. Mulugo – Songwe; Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah – Tumbe; Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya – Viti Maalum; Mheshimiwa Esther N. Matiko - Viti Maalum; Mheshimiwa Modestus D. Kilufi – Mbarali, Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza – Bukoba Vijijini; Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa – Bagamoyo, Mheshimiwa Betty E. Machangu - Viti Maalum; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed – Ole; Mheshimiwa Asha M. Jecha - Viti Maalum; Mheshimiwa Abdallah Haji Ali – Kiwani; Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri - Babati Mjini; Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis –Nungwi; Mheshimiwa Martha M. Mlata - Viti Maalum; Mheshimiwa Mathias M. Chikawe – Nachingwea; Mheshimiwa Ritta E. Kabati - Viti Maalum; Mheshimiwa Salum K. Barwany –Lindi Mjini na Mheshimiwa Vita R. Kawawa – Namtumbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana majina mengine tumeyaruka, kwa hiyo, nitaomba basi kama nimefanya kosa hilo niletewe nitarekebisha hapa.

**SPIKA:** Tutaanza kuhesabu muda wako baada ya hapo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kukubali kuongeza siku za mjadala wa Bajeti ya Ofisi yangu ili kuruhusu Wachangiaji wengi zaidi kupata nafasi ya kutoa michango yao. Idadi ya Wachangiaji ni kubwa kuliko ilivyowahi kutokea miaka ya nyuma. Hii inaonyesha dhahiri jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnavyoweka umuhimu katika majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake. Wote tunawashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango na hoja ni nyingi. Mawaziri na Naibu Mawaziri wamejitahidi kujibu lakini bado zimebaki hoja nyingi. Hoja ambazo hatutaweza kuzijibu kutokana na muda, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa zitajibiwa na Wizara nyingine wakati wa kuwasilisha Hotuba za Bajeti zao na kama itashindikana kuzishughulikia zote bado tunaahidi kwamba tutatoa majibu kwa maandishi na kuziwasilisha kwenu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wabunge wote kwa jinsi mlivyochambua kwa kina utekelezaji wa shughuli za Serikali. Hii ni dalili kwamba Bunge hili lina Wabunge mahiri wanaojali maendeleo ya wananchi na Nchi yetu kwa ujumla. Mmefuatilia kwa karibu utendaji wa Serikali. Pamoja na kwamba ni takribani miezi nane tu tangu kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili, mmetumia nafasi

yenu kama Wabunge kudai ufafanuzi na kujiridhisha kuhusu ufanisi katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wote waliooneshа mafanikio ambayo tayari yamepatikana katika utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali. Vilevile, niwashukuru wale wote walioonesha miradi na shughuli ambazo Serikali haijatekeleza kwa ufanisi uliotarajiwa. Kwangu mimi, michango yote itatusaidia sana katika kufanya vizuri zaidi na kukabiliana na changamoto zinazowakabili wananchi. Aidha, michango hii mizuri imetusaidia kufahamu kwa kina kile ambacho wananchi wetu wanategemea kutoka kwa Viongozi wao na Serikali yao kwa ujumla. Kwa yeyote aliyefuatilia mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu atakubaliana na mimi kuwa nchi yetu imeendelea kuudhihirishia ulimwengu kuwa tuna demokrasia ya kweli na iliyokomaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaahidi wote waliotupongeza kwa kazi nzuri tuliyofanya, hatutabweteka na pongezi hizo bali zitakuwa chachu ya kutuwezesha kufanya vizuri zaidi. Kwa zile changamoto zilizotolewa, nawahakikishia tumezisikia na tutazifanyia kazi kwa nguvu zote, kwa uwezo wote na kutumia kila nyenzo tulizo nazo ili kupambana na changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi. Kubwa hapa tushirikiane maana ‘umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wametoa michango kuhusu namna ya kuboresha utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali tuliyojiwekea katika kuendeleza kilimo. Maeneo mengi yaliyoguswa yanahusu kuendeleza kilimo cha umwagiliaji; kuboresha mfumo wa utoaji wa pembejeo za kilimo; uwekezaji katika kilimo na kulinda ardhi ya kilimo hasa kwa wakulima wadogo; kuwaendeleza wafugaji, wavuvi na wafugaji wa nyuki; kuboresha miundombinu muhimu ya kuchochea ukuaji wa sekta ya kilimo ikiwemo barabara, reli, madaraja, vivuko, ujenzi wa masoko, kuboresha nishati na ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Serikali imedhamiria kwa dhati kuleta mapinduzi ya kweli katika kilimo. Tutaendeleza sekta ya kilimo kwa ujumla wake yaani sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na uendelezaji wa dekta ndogo ya nyuki. Serikali inatambua kuwa sekta hii ndiyo itakayotuwezesha kuondoa umaskini kwa haraka na kuongeza fursa nyingi za ajira. Serikali imeongeza bajeti ya kilimo kutoka Shilingi Bilioni 903.8 mwaka 2010/2011 hadi Shilingi Bilioni 926.2 mwaka 2010/2012. Kiwango hiki ni sawa na asilimia nane ya bajeti yote bila kujumuisha Deni la Taifa wala fedha zilizotengwa katika Wizara nyingine ambazo zinaimarisha sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, tumechukua pia hatua za kupunguza baadhi ya kodi kwenye kilimo ili kuvutia uwekezaji katika sekta ya kilimo. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itaimarisha miundombinu ya umwagiliaji ili wakulima wengi wawe na uhakika wa kupata chakula. Aidha, Serikali imejitahidi kuongeza Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo ili wananchi wengi waweze kunufaika. Tutaimarisha usimamisi wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)*.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wawe tayari kushirikiana na Serikali kusimamia Miradi ya *ASDP* katika Majimbo yao. Tunapeleka fedha nyingi katika Halmashauri chini ya Programu hii ambazo zinahitaji usimamizi makini sana. Pamoja na jitihada hizi, tunatambua kuwa zipo changamoto nyingi katika kilimo ambazo Serikali haina budi kuzishughulikia.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ya pembejeo za kilimo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa David M. Malole, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Philip G. Mturano, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Ibrahim Sanya.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameelezea kwa uchungu kuhusu upungufu wa usimamizi wa Vocha za Ruzuku za Pembejeo za Mbolea na Mbegu Bora. Serikali inatambua matatizo na changamoto zinazokabili mfumo huo. Ndiyo maana tayari Serikali imeanza kuchukua hatua kwa Mawakala, Watumishi na Wakulima waliobainika kufanya udanganyifu na kujinufaisha binafsi kinyume na utaratibu chini ya Mfumo huu wa Vocha. Vilevile, Serikali imeamua kufanya Ukaguzi Maalum wa Mfumo wa Usambazaji wa Pembejeo, Ukaguzi huo utafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na matokeo yake yatatumika kuboresha mfumo huo. Serikali itaimarisha kutoa elimu kwa mkulima ili aelewe umuhimu wa kutumia mbolea, mbegu bora asidanganywe na Mawakala wa Usambazaji wa Pembejeo.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba Serikali itajitahidi kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati ili wakulima waweze kuzinunua wakati wa mavuno. Serikali itapeleka mbolea kwenye Vituo vya Mazao ili wanapopata fedha wakati wa mavuno wazinunue. Natoa wito kwa wananchi na Halmashauri zote kuimarisha Vyama vya Ushirika vya Msingi na *SACCOS* ili Vyama hivyo vinunue pembejeo za wakulima badala ya Mawakala. Pamoja na hatua hizo, Serikali itatuma Timu ya Wataalam kwenda nchini Malawi ambapo Mfumo huo umefanikiwa ili kujifunza zaidi na kupata uzoefu wa kuboresha Mfumo wa Ruzuku ya Pembejeo kwa kutumia Vocha. Aidha, natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia ipasavyo usambazaji wa pembejeo za kilimo katika maeneo yao. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na viongozi hao kuwezesha wakulima wanaolengwa kupata pembejeo kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji katika kilimo, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Salum Hemed Hamis, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Magreth M. Mkanga na Mheshimiwa David Z. Kafulia.

Mheshimiwa Spika, nieleze kidogo kuhusu uwekezaji mkubwa katika kilimo. Azma ya Kilimo Kwanza ambayo imeanza kueleweka, ina lengo kubwa la kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima wakubwa na wadogo. Tumelenga pia kuikaribisha sekta binafsi kwenye kilimo kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao na kusaidia wakulima wadogo kiteknolojia na masoko ya mazao yao. Programu ya *SAGCOT* ambayo niliizungumzia kwa undani kwenye hotuba yangu ni moja ya mkakati mkubwa wa

kukuza na kuendeleza kilimo na kukifanya kweli kuwa Uti wa Mgongo wa Taifa letu. Ofisi yangu inaandaa semina kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge ya kufafanua zaidi kuhusu Programu hii ya *SAGCOT* na kupata maoni na ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza hoja kwamba Serikali isitoe ardhi kubwa kwa wageni kule Mpanda na maeneo mengine. Ardhi inayozungumziwa katika Wilaya ya Mpanda ni maeneo ya Mishamo na Katumba yaliyokuwa Makambi ya Wakimbizi. Maeneo haya kwa bahati nzuri yapo katika Majimbo ya Mpanda Vijijini na Jimbo langu la Katavi na siyo Jimbo la Mpanda Mjini. Baada ya mawasiliano ya kutosha na Wanavijiji na kupokea ushauri kutoka Mkoa wa Rukwa na sekta husika mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na Wawekezaji, Halmashauri wameingia makubaliano ya awali na Kampuni ya *Agrisol-Tanzania.* Kampuni ya *Agrisol – Tanzania*, ni Kampuni ya Ubia kati ya Watanzania na Marekani. Makubaliano hayo yanalenga kutumia ardhi ya Mishamo na Katumba kwa kilimo kikubwa cha mazao ya chakula hususan mahindi. Aidha, chini ya mradi huo, ufugaji wa kuku na ng’ombe utatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa ni kuongeza uzalishaji na kuimarisha usalama wa chakula nchini. Chini ya makubaliano hayo, wakulima wanaozunguka Vijiji 22; kati ya hivyo, Vijiji vitano vikiwa Mishamo na 17 vya Katumba vitanufaika na mpango wa kupata huduma za kitaalam ikiwa ni pamoja na huduma za ugani na masoko ya mazao yao kupitia mfumo wa “*outgrowers*”. Faida nyingine za mradi huo ni kuimarishwa kwa usafiri kutoka Mpanda hadi Mishamo na Katumba. Aidha, Halmashauri itafaidika na kodi na tozo mbalimbali zitakazolipwa na kampuni hiyo. Kwa kipindi cha muda mrefu, kuna mpango wa kuongeza thamani mahindi kwa kuzalisha nishati aina ya *“Ethanol”*. Ardhi itakayotumika itatolewa kwa utaratibu wa kisheria na kufuata makubaliano na jamii zinazozunguka.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2010, nilitembelea kazi za Kampuni ya *Agrisol* huko Lowa-Marekani. Hii ni Kampuni kubwa na inayozalisha mazao kwa wingi. Mahindi yanatoa *“Ethanol”*, chakula cha mifugo na Vitamin ‘A’ na kuzalisha ajira nyingi. Uwekezaji huu utaongeza ajira na kuleta uhai mpya Wilayani Mpanda na Mkoani Rukwa/Katavi kwa jumla. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Wananchi kwa ujumla kwamba, uwekezaji huu una nia njema na tahadhari zote muhimu zimechukuliwa kufaidisha Wanampanda na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jembe la mkono, napenda kuwahakikishia kwamba kilimo cha mashamba makubwa kwa kutumia zana za kisasa za kilimo, ni Mkombozi wa kweli wa kuondokana na umaskini. Mkitaka kujua nayoyasema, nawasihi Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuanza kutembelea mashamba mawili yanayotumia zana za kisasa ambayo ni *Kilombero Rice Plantations* kule Morogoro na *Kagera Sugar* kule Kagera. Kuona ni kuamini, nendeni mkajionee nini maana ya kilimo cha kisasa. Ni muhimu sisi sote tuthamini jitihada zinazochukuliwa na Serikali kwenye sekta ya kilimo. Tuthamini wawekezaji kwenye sekta ya kilimo na kila panapowezekana tuwasaidie badala ya kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba Tanzania inazo fursa nyingi katika kilimo (Mazao, Mifugo, Uvuvi na Ufugaji Nyuki). Tunazo hekta 44 milioni za ardhi inayofaa kwa kilimo inayotumika ni asilimia 24 tu; misitu hekta 35.3 milioni; eneo kubwa limefunikwa na maji kilomita za mraba 62,000; vyanzo vingi vya maji vinavyofaa kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya mifugo, kuna ng'ombe 19.2 milioni, mbuzi 13.7 na Kondoo 13.6 milioni. Mimi naamini Tanzania haitaendelea iwapo hakutakuwepo uwekezaji mkubwa kwenye kilimo ambacho ndiyo tegemeo la Watanzania zaidi ya asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, hoja ya fidia kwa wafugaji waliopoteza mifugo, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Edward Lowassa - Monduli, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka - Simanjiro, Mheshimiwa Kaika Telele - Ngorongoro na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer - Longindo. Kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Rais, alipokuwa akifunga Bunge la mwisho la bajeti mwaka jana alilizungumzia suala hilo na akaahidi kwamba Serikali itaangalia uwezekano wa kuwapa kifuta machozi wafugaji waliopoteza mifugo yote kutokana na ukame mkali katika Mkoa wa Arusha na hasa Wilaya ya Monduli na Longido. Lengo ni kuwawezesha wafugaji walioathirika sana kuendelea na maisha yao ya ufugaji kwa kuwapatia mifugo ya kuanzia, hata kama ni kidogo (*Seed Stock*).

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 8.7 kama fidia ya kupoteza mifugo. Utaratibu wa kulipa fidia hiyo umekamilika. Ni matarajio kwamba wahusika watapata Kifuta Machozi chao wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mbunge wa Mbarali, tarehe 28 Juni, 2011 nilikutana na Wawakilishi (12) wa Wananchi wa eneo la Mbarali wanaozunguka Hifadhi ya *TANAPA* wakiongozwa na Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mheshimiwa Modestus Kilufi. Madhumuni ya kukutana yalikuwa kuangalia njia bora ya kutekeleza agizo la Serikali lililowataka wananchi kuhama kutoka katika Bonde la Usangu ili kupisha shughuli za uhifadhi zinazofanywa na *TANAPA*. Agizo ambalo pia lilimega sehemu ya Vijiji ili kuviongeza katika Hifadhi ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, iko hoja pia kwamba Uongozi wa Mkoa umemega Vijiji hivyo vya Iyapa, Madundasi, Msanga na Magwalisi na kuviongeza katika eneo la hifadhi bila ya kuwahusisha wananchi wala Viongozi wa Vijiji hivyo. Ni kweli kwamba uamuzi wa Serikali kuwahamisha wananchi kutoka katika maeneo hayo ulilenga kuhifadhi maeneo ya vyanzo vya maji vinavyolisha Mto mkubwa wa Ruaha ambao ndio unaopeleka maji katika Bwawa la Mtera. Pamoja na kwamba wananchi wa Mbarali wangependa maeneo ya Vijiji yaliyoingizwa kwenye Hifadhi visiingizwe bila kuwashirikisha, bado upo umuhimu wa wananchi hawa kuhamishwa, kwani uwepo wao katika eneo hili bado utakuwa na athari kubwa kwenye mtiririko wa maji yanayoelekea katika Bwawa la Mtera, endapo itadhihirika wazi kwamba ni kweli maeneo wanayokalia sasa yana uhusiano wa moja kwa moja na Bonde linalotiririsha maji katika Bwawa la Mtera. Vilevile, iko ahadi ya Rais ambayo ni lazima tuizingatie alipoahidi kwamba,

kusingekuwa na ongezeko la Vijiji vingine wala Vitongoji katika eneo hili kumegwa kuingia katika eneo la *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, Serikali itaangalia upya uamuzi wake kuhusu Vijiji hivyo. Katika kutekeleza uamuzi huo, Serikali itahusisha Viongozi na Wananchi wa Vijiji ambavyo vinahusika. Vilevile, elimu zaidi itatolewa na kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi atakayenyang’anywa haki yake bila sababu za msingi. Nawaomba viongozi na wananchi wa Mbarali kushirikiana vizuri na Serikali katika kushughulikia tatizo hili. Kipindi hiki wakati Serikali inatazama hatua stahiki za kuchukua, tunawaomba viongozi wa Mkoa wawaache wananchi katika maeneo hayo bila kuwabugudhi hadi hapo uamuzi wa mwisho utakapokuwa umetolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu wahamiaji haramu – Kagera, Waheshimiwa Wabunge wafuatao wameongelea kwa hisia kali kuhusu hoja hii. Suala hili siyo lao pekee, bali la Taifa zima. Wabunge hao ni Mheshimiwa Gosbert Blandes - Karagwe, Mheshimiwa Assumpter Mshama - Nkenge, Mheshimiwa Elizabeth Batenga - Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera unapakana na nchi jirani za Burundi (Kusini Magharibi), Rwanda (Mashariki) na Uganda (Kaskazini). Wilaya za Ngara, Karagwe, Missenyi na Bukoba zinapakana na nchi hizo. Mkoa wa Kagera ndio Mkoa pekee ambao mpaka wake unapakana na nchi tatu, yaani Burundi, Rwanda na Uganda. Mpaka kati ya Mkoa wa Kagera na nchi hizo una urefu wa kilomita zipatazo 550**,** kuanzia Murusagamba, Wilayani Ngara hadi Rubafu, Wilayani Bukoba. Ni mpaka mrefu na kwa sehemu kubwa ni *”porous”*ama hauna ulinzi wa kutosha. Kwa hali hiyo, wahamiaji haramu huweza kujipenyeza na kuingia Mkoani kwa shughuli za ufugaji, ujangili, utekaji nyara, unyang’anyi, biashara za magendo na kadhalika. Katika Wilaya za Ngara, sehemu ndogo ya Karagwe na Wilaya za Missenyi na Bukoba**,** vipo Vijiji vya kudumu mpakani lakini sehemu kubwa iliyobaki ni Hifadhi za Taifa za Kimisi na mapori.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wahamiaji Mkoani ni la muda mrefu na hasa kutokana na machafuko na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi za Rwanda na Burundi. Kundi la kwanza la wakimbizi liliingia Mkoani Kagera katika Wilaya za Ngara na Karagwe katika miaka ya sabini (1970s). Kundi la pili la Wakimbizi kutoka nchi hizo kwa matatizo kama hayo liliingia Mkoani katika miaka ya tisini (1990s). Kufuatia makubaliano yaliyofanyika kati ya Serikali, Serikali za nchi za Rwanda, Burundi na *UNHCR*, Wakimbizi hao wote walirudishwa katika nchi zao. Sehemu kubwa ya Wakimbizi wa kundi la kwanza walipewa Uraia na kuishi katika Vijiji vya Wilaya za Karagwe na Ngara. Inasadikiwa kuwa Mkoa wa Kagera una Wakimbizi haramu wapatao 22,000, hususan katika Wilaya za Karagwe na Ngara. Mkoa umekuwa ukichukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo kama ifuatavyo:-

- Kuimarisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Vijiji na Kata ili zisaidie katika kukabiliana na tatizo hilo;

- Kuendelea kutoa elimu kuhusu uraia ili viongozi na wananchi wasaidie katika utambuzi;
- Kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo ya mpakani kwa kutumia Vyombo vya Dola;

- Kuimarisha Vituo vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Polisi vilivyoko mpakani kwa kuwapatia vitendea kazi na mahitaji mengine muhimu;

- Kuzuia Watendaji wa Vijiji na Kata kutoa *“Peasant Pass”* na kuagiza kazi hii ifanywe na uhamiaji;

- Kuhamasisha wakimbizi haramu kujitokeza na kuwa tayari kurudishwa makwao au kuhalalishiwa ukaaji wao. Zaidi ya wahamiaji haramu 2,000 walirudishwa makwao kwa utaratibu huu; na

- Kufanya operesheni za mara kwa mara katika mapori ya Hifadhi za Taifa Burigi, Biharamulo na Kimisi na kuwachukulia hatua za kisheria wakimbizi haramu wanaokutwa huko, ambao shughuli zao kubwa huwa ni ufugaji wa mifugo, ujangili na kadhalika. Kwa mwaka 2010 zaidi ya operesheni tatu za aina hiyo zimefanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kusaidiana na *UNHCR* kupitia mpango wa *”International Imigration Management Programme”*, Mkoa ulifanya yafuatayo katika Wilaya ya Karagwe:-

- Kuwapa uraia watoto wa wakimbizi wa kundi la kwanza ambao walisahaulika kupewa uraia;
- Kuwapa uraia wanawake walioolewa na Watanzania;
- Kuwapa vibali vya kuishi nchini wakaaji wa muda mrefu ambao hawajatimiza masharti ya uraia. Zoezi hili liliwahusu watu wapatao 4,345. Zoezi litaendelea katika Mkoa mzima kufuatana na upatikanaji wa fedha;
- Kufanya Mikutano ya Ujirani Mwema na viongozi wa nchi hizo ili kuwa pamoja kushughulikia matatizo mipakani;
- Kwa upande wa mpaka na Uganda kujitahidi kuzuia uingizaji wa mifugo kufuata malisho katika Vijiji vya Kakunyu, Bubale na Byeju vinavyopakana na Uganda;
- Kuendelea kutoa mafunzo ya Mgambo katika Vijiji vya mipakani katika jitihada za kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo; na
- Kupiga chapa mifugo yote iliyopo Wilayani Missenyi ili kuweza kuwa-*identify* kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zote hizo ambazo tumekuwa tukichukua, bado matatizo yameendelea kuwepo, Serikali itaendelea kufanya juhudi kubwa ili kuhakikisha kwamba tunadhibiti hali hiyo kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu mauaji ya raia yaliyotokea Wilayani Ngara, hoja ya Mheshimiwa Elizabeth Batenga – Viti Maalum). Mheshimiwa Elizabeth Batenga wakati

akichangia hoja ya Waziri Mkuu alilieleza Bunge tarehe 28 Juni 2011, kwamba watu waliouawa ni wapatao 16. Taarifa za Polisi zinaonesha kwamba waliouawa hasa walikuwa ni watu sita (6) tu.

Mheshimiwa Spika, mnamo usiku wa tarehe 30 Mei 2011, watu sita waliuawa katika Kijiji cha Mwingamba kilichoko Wilayani Ngara. Watu waliouawa ni raia wa Tanzania. Marehemu hao walikwenda kwa shughuli za kilimo katika eneo ambalo mwanzoni Serikali ya Kijiji ilikuwa imelitenga kwa ajili ya ufugaji lakini baadaye kuruhusu kilimo pia kufanyika katika eneo hilo. Hawa wananchi sita (6), walipofika huko waliwakuta vijana kama wanne hivi wakichunga mifugo katika eneo hilo. Purukushani zilianza na wale watu sita wakauawa kwa kukatwakatwa na mapanga. Polisi walipata taarifa hizo na kufika katika eneo la tukio. Hadi sasa Polisi wanamshikilia mwenye mifugo ambaye ni Mtanzania ili asaidie kupatikana kwa wachungaji raia wa Rwanda na Burundi wanaotuhumiwa kufanya mauaji hayo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna tatizo la uhamiaji haramu katika eneo hili katika Mkoa wa Kagera. Napenda kuwahakikishia Watanzania wote kwamba Serikali inafahamu tatizo hili na itachukua hatua za haraka sana mara tu baada ya shughuli za Bunge kumalizika ili tuweze kusimamia kikamilifu utoaji wa wale wote ambayo si raia wa Tanzania na kuhakikisha kwamba tatizo hili linapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji mapato na nidhamu ya matumizi ya Serikali, hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa wengi wakiwemo Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala, Mheshimiwa William Mgimwa - Kalenga, Mheshimiwa Masoud A. Salum - Mtambile, Mheshimiwa Vicent J. Nyerere – Musoma, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Maida H. Abdallah - Viti Maalum, Mheshimiwa Zitto Kabwe - Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mpanda Mjini, Mheshimiwa Lekule Laizer - Longindo, Mheshimiwa Charles Mwijage - Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar - Viti Maalum, Mheshimiwa Herbet J. Mntangi - Muheza, Mheshimiwa Joseph Selasini - Rombo, Mheshimiwa Moses Machali - Kasulu Mjini na Mheshimiwa Christowaja Mtinda - Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo pia limepata wachangiaji wengi ni kuhusu kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Awali, nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa kazi nzuri anayofanya ya ukaguzi wa mali na fedha za umma katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote za Umma. Ofisi hii imefanya kazi nzuri ya kutuonyesha maeneo yenye upungufu katika usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali. Kwa uzito huohuo, nazishukuru Kamati zote za Kisekta za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa zilizofanya kuisimamia Serikali katika eneo hili. Kipekee nazishukuru Kamati za Bunge zinazosimamia Hesabu za Serikali Kuu**,** Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa *(PAC, LAAC* na *POAC*) kwa ushauri wao muhimu kwenye taarifa walizoziwasilisha hapa Bungeni na hatimaye kutuletea Serikalini. Serikali imeanza kushughulikia ushauri wa *CAG* na Kamati za *PAC, LAAC* na *POAC*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara zote, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote wameelekezwa kutekeleza maelekezo yote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ameelekezwa kuwa anapogundua eneo lenye matumizi mabaya ya fedha za Umma apeleke majina ya wabadhirifu hao moja kwa moja kwenye Vyombo vya Dola badala ya kusubiri hadi taarifa yake iwasilishwe Bungeni. Tutaendelea kumsaidia ili aweze kutimiza wajibu huo inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa ufafanuzi kidogo kuhusu hoja zinazotolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ukaguzi unaofanywa na *CAG* una hatua mbili kwanza, wakati wa kuanza ukaguzi kwenye Taasisi husika (*Entry Conference*) na pili, wakati wa kufanya ukaguzi katika Taasisi husika *(Exit Conference)*.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Wizara na Taasisi zote zinazotakiwa kukaguliwa, Wahasibu wawe wameweka Hesabu zao vizuri ikiwemo kumbukumbu za Hesabu na Vitabu vya Fedha vyote na risiti zote za malipo pamoja na maelezo ya malipo yaliyofanyika wakati Mkaguzi wa Nje kutoka *CAG* anapopita na sio kuanza kuzitafuta wakati huo. Hatutakubali kuendelea kupokea visingizio vya kupeleka taarifa kwa *CAG* baada ya Ukaguzi. Mkaguzi huyu anachotaka ni kukuta hesabu zimekaa sawasawa na si vinginevyo. Serikali imewakumbusha Maafisa Wahasibu kuhifadhi kumbukumbu za Hesabu za malipo vizuri ili ziwepo tayari wakati wote na sio kuzitafuta wakati ukaguzi unafanyika. Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa umakini mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali ya Awamu ya Nne imejitahidi kwa kiwango kikubwa kupeleka rasilimali fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuziimarisha chini ya Mfumo wa Ugatuaji wa Madaraka kwenda katika Mamlaka hizo (*D by D*). Moja ya changamoto tunayokabiliana nayo ni udhaifu katika usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha nyingi zinazopelekwa kwenye Halmashauri. Aidha, ipo changamoto nyingine ya ukusanyaji mapato kidogo kwenye Halmashauri. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zisizoridhisha imeongezeka kutoka Hati moja (1) mwaka 2008/2009 hadi Hati nne (4) mwaka 2009/2010. Aidha, Idadi ya Hati zenye Mashaka imeongezeka kutoka Hati 55 mwaka 2008/2009 hadi Hati 65 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, hatua za makusudi lazima zichukuliwe ili kuweza kuongeza mapato ya Halmashauri kama njia mojawapo ya kutekeleza dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi. Lengo ni kutoa uhuru wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kujitegemea. Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza uwajibikaji na nidhamu katika ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za Umma kwenye Halmashauri. Aidha, itaimarisha ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo kwa karibu. Napenda kusisitiza kuwa Watendaji wa Halmashauri na Madiwani ni lazima

watembelee na kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha za Umma zilizotumika katika miradi hiyo (*Value for Money*).

Mheshimiwa Spika, Serikali itatoa mafunzo, kuajiri Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani wenye Ujuzi wa kutosha na kuimarisha Kitengo cha Wakaguzi wa Ndani katika Halmashauri. Kuanzia mwaka 2010/2011, Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani kilichopo kwenye Halmashauri kitakuwa huru na kinachojitegemea. Aidha, Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri watawajibika moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali badala ya kuwa chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, kuanzia mwaka ujao wa fedha, Halmashauri zote zitaanza kutumia Utaratibu wa Malipo kwa Mtandao (*Integrated Financial System Management*). Hivi sasa Wataalam watakaosimamia Mpango huo wanaendelea kupata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, katika mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea na juhudi zake za kudhibiti matumizi yake kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Hii ni pamoja na kusitisha ununuzi wa samani, ununuzi wa magari ya aina zote, kupunguza uendeshaji wa semina na warsha, gharama za maonesho na sherehe mbalimbali. Pamoja na kupunguza safari za ndani na nje na ukubwa wa misafara pia kudhibiti gharama za utengenezaji magari na ununuzi wa mafuta. Natoa wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni katika kukusanya mapato na kutumia fedha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ustawishaji Makao Makuu – Dodoma, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar.

Mheshimiwa Spika, tarehe 08 Juni 2011, Mheshimiwa Rais alikutana na Uongozi wa *CDA*, ili kupitia kwa pamoja Mawasilisho ya Mapitio ya Mpango Kabambe wa Mji wa Dodoma. Katika Kikao hicho, Rais alitoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusiana na Mapitio haya kama ifuatavyo:-

1. Eneo la Ofisi za Serikali lijulikane dhahiri na liwe na ukubwa wa kutosha. Alipendekeza Ofisi hizi ziwe karibu na Ikulu ya Rais ambayo ipo Chamwino. Aidha, alisisitiza uanzishwe Mji Mpya wa Serikali kuzunguka au karibu na eneo la Ikulu ya Chamwino.

2. Ili kufanikisha azma ya kuhamia Chamwino, mikakati ya kuanzisha Mji mpya sehemu hiyo uingizwe kwenye Mapitio ya Mpango.

3. Alisisitiza eneo la awali la Kikombo lililotengwa kama Mji wa Serikali liwekewe mipaka na kutunzwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za KiSerikali.

4. Katika mapitio hayo, *CDA* iliagizwa kutenga eneo la Viwanda ili hatimaye Mji wa Dodoma uwe ni kitovu cha viwanda. Alisisitiza kuwa hata kama eneo la viwanda likiwa kubwa zaidi ya eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma ni vyema kwani Mji wa Mtwara pamoja na kuwa pembezoni lina eneo la viwanda zaidi ya hekta 2,000 za viwanda. Alisema suala la uwepo wa Dodoma katikati ya nchi uangaliwe katika azma nzima ya kutenga maeneo ya viwanda ili eneo la Mji Mkuu liwe kitovu cha Viwanda (*Industrial Hub*) kama njia mojawapo ya kuongeza kasi ya maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii.

*5.* *CDA* itatenga maeneo makubwa kwa ajili ya malighafi ya Viwanda vya Kusindika (*Processing Industries*) kama vile *EPZ* yakiwemo Mashamba ya Zabibu na kadhalika. Pia malighafi kwa ajili ya viwanda vingine vya uzalishaji na uhifadhi wa bidhaa za viwandani (*Logistic Areas*) kama *"Bonded Warehouses*" yaangaliwe na kuwekwa katika Mapitio ya Mpango.

6. Maeneo ya huduma (*Service Centers*) yataongezwa na kuingizwa kwenye Mpango ili kuweza kuhudumia watu zaidi ya 50,000.

7. Mheshimiwa Rais aliagiza vivutio mbalimbali vya uhamiaji Dodoma vichanganuliwe na vizingatiwe na kuingizwa kwenye mapitio haya.

8. Mheshimiwa Rais pia alisisitiza kuwa maeneo yaliyopimwa na kukaliwa isivyo rasmi yaangaliwe upya katika michakato ya umilikishwaji baina ya wazawa wanaotambulika kisheria na wamiliki wapya.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 210 hadi 212 imeweka bayana uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma na ikaagiza Serikali kama ifuatavyo:-

"*Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010 – 2015) Chama cha Mapinduzi kitaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-*

*(a) Kuandaa Mpango thabiti wa kuhamia Dodoma hatua kwa hatua. Katika Mpango huo, Mpango Mji wa Dodoma (Master Plan) utazamwe upya ili kuhakikisha kuwa Majengo ya Serikali yanajengwa upya Chamwino kwa kuanzia na Majengo ya Ofisi na Makazi ya Rais (Ikulu).*

*(b) Kuihamasisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa hoteli za kisasa, viwanda, Hospitali n.k. katika maeneo ya Manispaa yaliyotengwa na yatakayoendelea kutengwa.*

*(c) Kutunga Sheria ya kutambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.*

(d) *Kuanzia sasa majengo mapya ya Wizara za Serikali yajengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam". Mwisho wa Kunukuu. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais na pia Ilani ya Uchaguzi, uamuzi wa kuhamia Dodoma hauna budi kutekelezwa. Kwa maneno mengine, hauna mjadala. Kwa maana hiyo, hata kama fedha zimetengwa kwa ajili ya kujenga ofisi za Serikali maeneo mengine zaidi ya Dodoma, nataka kuwahakikishia kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu itaanza kujenga ofisi yake hapa Dodoma na siyo Dar es Salaam.

Aidha, Wizara zote ambazo zimetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi, zianze kujenga Dodoma na tusibabaishane. Jambo muhimu ni kuvuta subira. Tutaendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kadri uwezo wa fedha utakavyoendelea kupatikana lakini kuhamia Dodoma ni lazima hakuna mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili limevuta hisia za Wabunge wengi na naomba niwatambue wale waliozungumza jambo hili mmoja ni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Ezekiel Wenje, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila na wengine ambao pengine nimesahau kuwataja.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza kuwa suala la posho kwa Watumishi wa Umma limekwishawekwa bayana katika Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano 2011/2012 hadi 2015/2016. Katika ukurasa wa 17 wa Mpango wa Taifa, nanukuu:-

*"Consolidation of most of fringe benefits such as housing, transport and allowances into salaries and wages will be one of the ways of creating an appropriate incentive structure. Sitting and Travelling Allowances currently create a perverse incentive structure and will need to be rationalised or consolidated".*

Mheshimiwa Spika, vilevile, suala hili Waziri wa Fedha amelieleza vizuri katika Hotuba yake wakati akiwasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012 (ukurasa 53). Mimi mwenyewe katika kipindi cha Maswali ya Waziri Mkuu nilijaribu kulielezea jambo hili kwa maelezo niliyoona wakati huo yanafaa.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara kwa Watumishi wa Serikali pamoja na malipo ya stahili mbalimbali za Viongozi na Watumishi wa Umma, yanatolewa kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni ambazo zimepitishwa na Bunge na Mamlaka za Ajira katika Utumishi wa Umma. Malipo hayo yanajumuisha posho mbalimbali. Kwa mfano, kwa mujibu wa Nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma wanastahili kupata malipo ya mshahara pamoja na stahili mbalimbali za posho zenye viwango tofauti kulingana na cheo cha mtumishi husika. Kwa sasa zipo aina za posho 18 katika kundi hili.

Mheshimiwa Spika, posho za Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge nao wanapata posho mbalimbali ambazo zimewekwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika hoja hasa ya upande wa Vyama vya Upinzani, wao wanataka Serikali ijielekeze katika Posho ya Vikao pekee, yaani *"Sitting Allowance"*. Mimi kwa maoni yangu na naamini ni maoni ya Serikali, naona kuwa suala hili ni muhimu litazamwe kwa upana wake wote na kwa msingi ulioelezwa chini ya Mpango wa Miaka Mitano yaani kuzungumzia posho zote tunazopata kwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Waraka wa Masharti ya Kazi za Mbunge, stahili za Waheshimiwa Wabunge ni zifuatazo:

(i) Mshahara wa Mbunge kwa sasa, *gross salary* ni Sh. 2,305,000/=, kodi ni Sh.588,000/=. Kwa hiyo, mshahara anaopata Mbunge ni Sh.1,717,000/= hapo sijazungumzia makato ya mkopo wa gari walilokopeshwa, wastani wake ni karibu shilingi 900,000. *(Makofi)*

(ii) Mbunge pia ana posho ya Ubunge, (*MP – Constituency Allowance*);

(iii) Posho ya Vikao vya Bunge na Kamati zake;

(iv) Posho ya Madaraka kwa Viongozi;

*(v)* *Entertainment Allowance* kwa baadhi Viongozi;

(vi) Posho ya Kujikimu ndani na nje ya Nchi;

(vii) Posho ya Mavazi anaposafiri nje ya Tanzania;

(viii) Posho ya Msaidizi wa Ofisi ya Mbunge;

(ix) Posho ya Usafiri wakati wa Vikao vya Kamati na Mikutano ya Bunge;

(x) Posho ya Mafuta (Lita 1,000) kwa mwezi; na

(xi) Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo (*Catalyst Consittuency Development Fund - CDCF*). Nao ni sehemu ya fedha ambazo zinamsaidia Mbunge katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili lipo ndani ya Mpango wa Maendeleo, Serikali italitafakari kwa undani na kuangalia posho zipi hazina tija na zipi zina tija na manufaa ya kuongeza ufanisi ili ikiwezekana zihuishwe na kujumuishwa ndani ya mishahara hii midogo ambayo sasa hivi Waheshimiwa Wabunge wanapata au vinginevyo kama itakavyoonekana inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itaangalia suala la kupunguza gharama za matumizi ya Serikali kwa ujumla wake ikijumuisha kupunguza matumizi yasiyo ya lazima katika Taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja ya maslahi ya Madiwani. Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa nguvu sana katika eneo hili wakiwemo Mheshimiwa Esther Lukago, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Mariam Ruben Kasembe, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Desderius Kipata, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Iddi Azan na wengine ambao sikuwataja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hoja hii lakini kwa bahati nzuri Serikali imekuwa na jambo hili katika kipindi chake chote na imekuwa ikirekebisha viwango hivi kadri fursa zilivyopatikana za uwezo wa kifedha. Serikali tutaendelea kuliangalia suala hili kwa makini kabisa. Kwa kuzingatia michango hiyo, Serikali imekuwa ikiboresha maslahi haya ya Madiwani na itaendelea kuyaboresha. Kwa hiyo, Serikali imepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kazi nzuri wanayofanya Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, itayafanyia kazi maoni hayo ili tuone namna bora ya kuyazingatia wakati wa kufanya Mapitio ya bajeti ya nusu mwaka. Kutokana na rai za Waheshimiwa Wabunge na nia nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali inakubali kuongeza posho hizo. Suala litakuwa ni wakati gani tuanze, kama tutaweza katikati ya mwaka ingawa naona kwa bajeti ilivyo inaweza ikawa ngumu, tunawaahidi mwakani kwa vyovyote vile jambo hili tutaliwekea uzito na tutaongeza posho.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imesikia na imelitizama suala la posho kwa Wenyeviti wa Vijiji. Kutokana na hali ya maisha ilivyo na ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu katika Serikali za Vijiji, Serikali imekubali vilevile kwamba sasa itakuwa inatoa posho kwa Wenyeviti lakini uanzaji wake huenda tukalazimika kuanza kwenye bajeti ijayo kwa kuwa bajeti ya mwaka huu imebana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwango vya posho tutaviangalia, tutashirikiana kupata maoni zaidi, yako mawazo ya shilingi 500,000 kwa Madiwani lakini tulikuwa tunafikiri kitakuwa kiwango kidogo lakini huenda tukaangukia kati ya shilingi 200,000 mpaka 300,000 kwa kadri uwezo utakavyoturuhusu. Yote tutaangalia kwa nia njema ili tuweze kuhakikisha kwamba Madiwani nao wanapata ahueni ya namna fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu bomoabomoa, suala hili limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wengi hasa pale wanapowekewa alama ya "X" kwenye nyumba zao kabla ya barabara yenyewe kujengwa bila kujali inajengwa wakati gani. Serikali itatafakari upya kuhusu mfumo mzuri wa utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, natoa wito kwa wananchi wote kuzingatia Sheria za Barabara na kuepuka kujenga kwenye hifadhi za barabara. Suala la ujenzi wa barabara linatawaliwa na Sheria iliyotungwa na Bunge hili Tukufu. Katika kutekeleza Sheria hiyo, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi. Serikali inao wajibu muda wote na kwa masuala yote unapopata malalamiko ya mara kwa mara basi kusikiliza vilio vya wananchi, kukaa chini, kutazama upya uamuzi wake na kuona ni namna gani bora zaidi inayofaa katika kutekeleza sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara zinachangia sana ukuaji wa uchumi, Serikali imeamua kuwa kwa zile barabara ambazo ziko kwenye mipango ya ujenzi, ujenzi wake uendelee. Kwa zile barabara ambazo haziko katika mpango wa ujenzi kwa hivi sasa, wananchi watapewa muda wa kutosha wa kuweza kuondoka katika maeneo hayo ili kupisha ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayotokana na ubomoaji yanatokana na kwanza, suala la fidia, pili ni alama zinazowekwa barabarani na tatu ni utaratibu mzima wa wakati gani mwananchi aondoke katika eneo hilo ili kupisha ujenzi wa barabara. Yote haya Serikali imeamua kwamba itayatazama kwa pamoja ili ujenzi wa barabara isije ikawa ni chanzo cha kuumiza wananchi na kuwatia katika majonzi yasiyokuwa ya lazima. Tutakapokuwa tunatazama zoezi hili, Serikali itaangalia pia maeneo ambayo nyumba zimeshajengwa na mazingira halisi ya jiografia yalivyo na kama hakuna uwezekano pengine wa kuweza kupitisha barabara katika maeneo hayo bila kusababisha athari kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mifano mizuri ni pale unapokuta barabara inapita katika maeneo ya miinuko na milima Lushoto, Njombe, Bukoba Mjini na maeneo mengine kama haya. Serikali hatuna budi kutazama ni namna gani nzuri zaidi isiyoleta kero kwa jamii ambayo inaweza ikaleta ufanisi katika utengenezaji wa barabara hiyo. Suala zima hili litaangaliwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Tararibu na kama hapana budi kufanya marekebisho katika sheria basi sheria hiyo itawasilishwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu utawala bora, eneo hili nalo pia limechangiwa na Wabunge wengi, Mheshimiwa A. Salim, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Antony Gervas Mbassa na Mheshimiwa Kangi Ndege Lugola.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, Kambi ya Upinzani imetoa maelezo kuhusu ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ambao umeendelea kukithiri nchini kwa kiasi kikubwa na kwamba TAKUKURU ina uwezo mdogo wa kuchunguza kesi na kufungua mashtaka. Niseme tu kwamba, nchi hii inaongozwa kwa utawala wa sheria. Kuna taasisi zimeundwa na zinafanya kazi yake kwa umakini mkubwa na wale wote wanaokiuka sheria wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa TAKUKURU, chombo hiki kinafanya kazi kubwa na katika mazingira magumu. Sote tunafahamu ilivyo vigumu kushugulikia

masuala ya rushwa kwa kuwa watoaji na wapokeaji wanatumia mbinu mbalimbali na wanafanya biashara hiyo katika hali ya uficho sana. Pamoja na changamoto zote hizo, katika kipindi cha mwaka 2008 hadi 2010 jumla ya malalamiko 17,752 yalipokelewa na siyo 14,426 kama yalivyotajwa na Mheshimiwa Mbowe na kati ya hayo, malalamiko yaliyohusu rushwa ni 2,682. Kati ya malalamiko hayo, TAKUKURU ilichunguza na kukamilisha majalada 2,973 kwa maana kwamba malalamiko yote yaliyohusu rushwa yalichunguzwa na mengine 291 ya miaka ya nyuma yalifanyiwa kazi pia. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2010, jumla ya kesi zilizoamuliwa na Mahakama zilikuwa 382 na kati ya hizo, Jamhuri ilishinda kesi 139 na washtakiwa walifungwa. Kesi zilizoshinda ni asilimia 36.4 na siyo asilimia 22.2 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ikahafamika pia kwamba, Sheria haibagui wala kuweka makundi ya walalahoi na vigogo kwenye rushwa na wala hakuna tofauti kati ya rushwa ndogo na rushwa kubwa, rushwa ni rushwa tu. Pengine kinachojitokeza ni kwamba rushwa ndogo ushahidi unaweza kupatikana kwa haraka wakati kesi kubwa wakati mwingine ushahidi wake huchukua muda mrefu na wakati mwingine huhitaji kuupata ushahidi nje ya nchi na hivyo kesi kuchukua muda mrefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu mauaji ya raia yanayofanywa na Vyombo vya Dola, kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, uhai wa mtu ni haki ya msingi ya raia wote. Kwa mujibu wa Ibara hiyo, kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria. Hakuna mtu anayeruhusiwa kuondoa uhai wa binadamu. Hivyo, kwa masharti ya Ibara hii, haki hii ya kuishi ni msingi mkubwa kwa Katiba ya nchi yetu inayofuata utawala wa sheria. Pale inapotokea uhai wa mtu umeondolewa, ni lazima taratibu za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, vifo hasa vile ambavyo vimetokea katika mazingira ya kutatanisha chini ya mikono ya Vyombo vya Dola, ni lazima vichunguzwe. Utaratibu wa kufanya uchunguzi wa vifo vya aina hii umeainishwa chini ya Sheria ya Uchunguzi wa Vifo, *(The Inquest Act)* Sura ya 24 ya Sheria zetu. Kifungu cha 3 cha Sheria hiyo, kinatamka mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Sheria kuanzisha Mahakama ya Kuchunguza Vifo hivyo *(Coroner's Court)* katika maeneo ya Serikali za Mitaa. Waziri atafanya hivyo kwa kushirikiana na Jaji Kiongozi na Waziri atatangaza uteuzi huo katika Gazeti la Serikali. Kazi hiyo pia inaweza kutekelezwa na Mahakimu wa Wilaya au Hakimu Mkazi katika maeneo ambayo Wachunguzi wa Vifo hawajateuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika madai yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, hususan wa kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu mauaji yanayodaiwa kufanywa na baadhi ya Vyombo vya Dola, ni vyema ikaeleweka kuwa, Serikali haina nia ya kupuuza shutuma hizi za mauaji ya raia wake. Katika kulishughulikia suala hili, suala la mauaji ya raia yanayodaiwa kufanywa na baadhi ya Vyombo vya Dola, Serikali imefikia uamuzi sasa wa kuvichunguza vifo hivyo kwa kupitia Sheria husika ya *Inquest* kwa kadri

itakavyowezekana. Inawezekana kwa muda mrefu utaratibu huo hauzingatiwi lakini kwa sasa, ni lazima tuufuate na ni lazima sasa tuutekeleze ili kutokana na maamuzi ya uchunguzi huo watu waweze kupelekwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi pale itakapobainika kwamba vifo hivyo au mauaji hayo hayakuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni muhimu tukatambua kuwa, kila kifo cha mtu kina tofauti zake pamoja na mazingira yake. Hivyo, kwa kuzingatia kilio cha wananchi ambao Serikali ina wajibu wa kuwalinda, vifo vyote ambavyo vimetokea kwa sababu ya matumizi ya nguvu au kifo cha raia kisicho cha kawaida kilichotokea akiwa chini ya uangalizi wa Vyombo vya Dola basi taratibu hizo nilizozieleza sasa lazima zizingatiwe. Serikali imeshaanza mipango ya awali ya kushughulikia tatizo hili kwa kupitia mamlaka husika. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atafafanua suala hili zaidi atakapokuwa anawasilisha Makadirio ya bajeti ya ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu maandamano, tafsiri ya Ibara ya 20(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani kuchanganyika, kushirikiana na wengine, ni dhahiri kwamba katika kukutana au kuchanganyika kunahusisha kufanya maandamano. Hata hivyo, kwa mujibu wa Sheria za Polisi, Kifungu cha 42, mtu au Chama cha Siasa sharti kuomba kibali kwa Mkuu wa Wilaya kabla ya kufanya maandamano au mikutano ya siasa. Kisheria, Polisi wamepewa mamlaka ya kuzuia maandamano na mikutano pale inapobidi na baada ya kujiridhisha kwamba lipo tishio la usalama. Ni vema wananchi wafahamu kuwa haiwezekani kuruhusu maandamano au mikutano iendelee huku kukiwa na taarifa za uvunjifu wa amani kwani itakuwa ni sawa na kuiweka rehani amani ya nchi yetu. Hata sheria za kawaida zinaruhusu taasisi au mtu kuchukua hatua za kupunguza madhara makubwa hata kama itabidi kusababisha madhara kidogo kwa mtu/watu wengine. Napenda kuwashauri rafiki zangu upande wa Upinzani na upande hata wa Chama Tawala, kuwa uchaguzi sasa umekwisha, sasa tuwahamasishe wananchi kufanyakazi na kujiletea maendeleo badala ya kuendekeza shughuli za maandamano na migomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kuwa hakuna ubaguzi uliofanywa wakati wa ukamataji wa Wabunge. Katika ukamataji, Polisi huongozwa na sheria na mazingira ya kesi husika. Wabunge wa Upinzani ni kweli walikamatwa lakini ilikuwa ni baada ya kufanya mañoso mbele ya Polisi na hawakuwa katika shughuli za Bunge. Maandamano au kufanya fujo sio shughuli ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Freeman Mbowe alikamatwa kwa amri ya Mahakama na kisheria Polisi hawana uwezo wa kuhoji amri za Mahakama. Mbunge wa CCM anayedaiwa kupendelewa kwa kuombewa kibali cha Spika hakukutwa eneo la tukio wala hakufanya kosa mbele ya Polisi, yeye ni mtuhumiwa tu na kimsingi lengo halikuwa kumkamata bali kumhoji kuhusiana na tuhuma za mauaji yaliyotokea Mwanza. Wakati huo yeye alikuwa Dodoma kwenye shughuli za Bunge. Aidha, ni maoni yetu kwamba kwa wale Waheshimiwa Wabunge ambao kesi zao zipo Mahakamani basi

wahakikishe wanafuata taratibu za Mahakama ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, hoja kuhusu amani na utulivu kwa ujumla. Wabunge wengi wamechangia hoja hii wakiwemo Mheshimiwa Masoud Abdala Salum, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rashid Ally Abdallah, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Nyambari Chacha, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu amani na utulivu kwa ujumla. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechagia hoja hii wakiwemo Waheshimiwa Masoud Abdala Salum, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Nyambari Chacha na Joseph Roman Selasini.

Mheshimiwa Spika, suala la amani na utulivu lilijadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakati wa mjadala huu. Huo ni udhihirisho kwamba wote tunahitaji amani, wote tunahitaji utulivu na wote tunahitaji kuishi kwa amani na kutekeleza kazi zetu za ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la amani na utulivu ni urithi ambao Waasisi wa Taifa hili walituachia. Tangu tupate uhuru, suala hili lilikuwa ni agenda muhimu sana ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ndani na nje ya nchi kila alipokuwa alisisitiza amani kwa nchi jirani, alisisitiza amani kwa nchi zote za Bara la Afrika na Duniani kote. Msisitizo wake mkubwa ulikuwa, utulivu, amani na maendeleo ya watu kwani alitambua kwenye amani kutakuwa na maendeleo ya watu na kwenye maendeleo ya watu kutakuwa na amani. Amani ni mazingira wezeshi ya kusaidia kila mmoja wetu kufanya shughuli zake za kijamii na kiuchumi. Ni dhahiri kwamba bila amani hatuwezi kuwa na maendeleo. Bila amani hatuwezi kuwa na uzalishaji na kwamba bila amani hatuwezi kuwa na uhuru wa Kikatiba wa kuishi. Kwa msingi huo, ni lazima tutumie urithi huu tulioachiwa na Baba wa Taifa kwa kulinda nchi yetu idumu katika amani na utulivu. Si busara kwa maoni yangu kuingiza mbegu za kuashiria uvunjifu wa amani katika kizazi cha sasa kutokana na kauli zetu, kutokana na vitendo vyetu. Vilevile, ni jukumu letu sote hasa tulioko hapa Bungeni kuendelea kuwakanya baadhi ya Viongozi wanaoanza kupanda mbegu mbaya kwa vijana na hasa wa Vyuo vya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu barabara kwenye hifadhi za Taifa. Tanzania inasifika Duniani kote kutokana na historia ndefu tuliyojijengea ya kulinda na kuhifadhi wanyamapori. Takribani asilimia 26 ya eneo lote la ardhi limetengwa kwa ajili ya Hifadhi za Wanyama. Kwa kutambua umuhimu wa Uhifadhi wa Wanyamapori kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo, Serikali imeamua kuwa barabara zote zinazopita ndani ya Hifadhi za Wanyamapori za Taifa hazitajengwa kwa kiwango cha lami bali zitajengwa kwa kiwango cha chagarawe. Barabara za kiwango cha lami zitakazojengwa zitaishia kwenye lango la kuingilia kwenye maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Taifa ili kurahisisha usafiri wa wananchi wanaoishi jirani au kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa. Serikali itaendelea kulinda, kuendeleza na kuhifadhi maeneo yote ya Hifadhi za Taifa kwa faida ya vizazi vya sasa na vijnavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko vilevile hoja juu ya maeneo mapya na imechangiwa na Wabunge wengi, naomba pengine kwa sababu ya muda nisiwataje. Mwaka jana Serikali ilitangaza nia ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala ya Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji. Pamoja na kuanzishwa maeneo hayo, bado maeneo mengine hayakuweza kugawanywa kwa kuwa maombi yalikuwa ni mengi na baadhi ya maeneo hayakuweza kukidhi vigezo. Katika mjadala wa hotuba yangu, Serikali imepokea maombi ya kuanzisha maeneo mapya ya Wilaya na Halmashauri katika Jimbo la Bumbuli, Manyoni, Rungwe na Katavi/Mpanda. Hoja za Waheshimiwa Wabunge walizozitoa tumezisikia na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itayafanyia kazi katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioupongeza uamuzi huu wa Serikali wa kuwasogezea maendeleo karibu na wananchi. Maeneo hayo yatakapotangazwa rasmi tutashirikiana na Wabunge katika kutekeleza rai zao kwa mfano, ujenzi wa viwanda na kwa wenye migodi kununua vyakula vilivyomo katika Mikoa hiyo na pia ujenzi wa miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwiano wa maendeleo nchini, kwa mujibu wa Takwimu za Taasisi ya Taifa ya Takwimu (*National Bureau of Statistics*) ya mwaka 2010, Mikoa Kumi (10) ambayo Pato la Mwananchi ni dogo ni kama ifuatavyo: (Mikoa hii imepangwa kwa mtiririko wa kuanzia nafasi ya 12 hadi 21. Kwa hiyo, ulio juu kabisa ni Mtwara ambao pato lake la wastani ni shilingi 700,436, Lindi 673,096, Mara 642,528, Pwani 572,466, Tabora 528,832, Shinyanga 510,023, Kigoma 499,428, Kagera 491,713, Dodoma 485,211, Singida ambao ndiyo Mkoa wa mwisho 483,922.

Mheshimiwa Spika, pato la wastani la Mtanzania kwa mwaka 2010 ni Shilingi 770,464. Kwa kuzingatia takwimu hizo, hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu umuhimu wa Serikali kuangalia Mikoa hii wakati wa kugawa rasilimali fedha kidogo tulizo nazo ni ya msingi kabisa. Hatua hiyo itawezesha Mikao hiyo kupanda na kuwa na uwiano mzuri wa kimaendeleo na Mikoa mingine. Vilevile, ni muhimu Serikali kutambua kuwa hata kwa ile Mikoa ambayo takwimu za pato la mwananchi ni kubwa kidogo bado kuna maeneo *(pockets)* ambayo yako nyuma kimaendeleo. Maeneo yote hayo yatahitaji kupewa kipaumbele katika ugawaji wa rasilimali za Taifa letu. Serikali imepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuhusu eneo hili na italifanyia kazi ili liweze kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi za Rais wakati wa kampeni, nalo hili limechagiwa na Wabunge wengi, lakini naomba tu niseme kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza suala la Serikali kuhakikisha kwamba inatekeleza kwa makini ahadi zote zilizo kwenye Ilani ya uchaguzi wa mwaka 2010. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itafanya hivyo na tumeshachapisha vitabu ambavyo tumeita ni Kamusi zinazohusu Ilani ya Uchaguzi, ahadi za Rais pamoja na hotuba aliyoitoa hapa Bungeni. Vitabu hivi vyote tutavitoa kwenu katika Bunge hili linaloendelea sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu walemavu wa ngozi. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa hasa kwa uchungu mkubwa ni pamoja na dada yangu Al-Shaymaa John Kwegyir pamoja Salum Khalfan Barwany. Ipo hoja kwamba hotuba ya Waziri Mkuu haikutaja chochote kuhusu Watu Wenye Ulemavu wakiwemo Walemavu wa Ngozi. Niwaombe radhi tu kwamba tulipitiwa lakini hii haina maana kwamba hatuwaweki maanani hata kidogo. *It was an oversight* na tuna–*apologyse* sana kwa jambo hilo. Napenda kuwahakikishia wananchi wote kwamba Serikali inathamini sana Watu wenye Ulemavu na inathamini mchango wao kwa Taifa. Mtakumbuka juhudi za Serikali katika kupambana na wimbi la mauaji ya Walemavu wa Ngozi nchini lililoibuka mwaka 2007. Matokeo ya juhudi hizo pamoja na za wananchi na wadau mbalimbali zimeweza kwa kweli kwa sehemu kubwa kutokomeza wauwaji hayo na sasa tunaona hali ya utulivu imerejea katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru Watanzania wote kwa kusaidia kumaliza mauaji ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi. Tumefanya kazi nzuri na tunaamini hali hii ya amani itadumishwa. Kwa kuthamini watu hawa, Serikali imekuwa pia ikiwashirikisha katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile michezo na niwakumbushe tu kwamba katika Mashindano ya Olimpiki ya Mwaka 2008 yaliyofanyika Uchina, Timu ya Watu wenye Ulemavu wa Viungo ndio pekee iliyotuletea sifa kwa kupata Medali na kuwashinda watu wazima ambao hawana ulemavu wowote. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana kwa heshima mliyotupatia. Serikali itaendelea na juhudi zake za kukabiliana na matatizo yanayowakabili Watu wenye Ulemavu na kuhakikisha kunakuwepo na takwimu za uhakika za Watu wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo pia na hoja kuhusu Muungano. Hoja imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, pengine niwataje, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Yahya Kassim, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa John Magalle Shibuda kwa kutaja wachache.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza hoja mbalimbali kuhusiana na Muungano lakini nataka niseme Muungano huu ni mzuri sana. Wananchi wa pande zote mbili wanaishi na kufanya kazi bila kuulizana wanapotokea. Inafurahisha sana unapowakuta Watanzania wa Zanzibar wakifanya biashara zao Rukwa, Mbeya, Simanjiro na kwingineko bila bugudha yoyote. Vivyohivyo, unawakuta Watanzania Bara wakifanya shughuli zao Micheweni, Kiembe Samaki na kwingineko bila bugudha yoyote.

Mheshimiwa Spika, nchi kubwa duniani zenye uchumi mkubwa zimeungana na zinaendelea kuongeza nchi nyingine ili kupanua Muungano. Tunao wajibu mkubwa wa kuona kwamba Muungano huu ni heshima kubwa na tutafute kila mbinu kuuendeleza kama yako matatizo tuyazungumze ili tuweze kuhakikisha kwamba Muungano unaendelea. Kama alivyowahi kusema Mwalimu Nyerere, hakuna atakayeendelea na kupewa sifa kwa kutengana, ni muhimu kuimarisha Muungano huu. Hizi chokochoko

ndogondogo zilizoanza kujitokeza, ni vyema tukazikemea zisiendelee badala yake tutatue matatizo ambayo ndiyo hasa yanataka kutufikisha huko tunakojitokeza kuelekea. Serikali imesisitiza sana umuhimu wa Viongozi wa pande zote mbili kutembeleana na kubadilishana mawazo. Tutaziendeleza hizo juhudi kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, Muungano wowote ule lazima ukumbane na changamoto na majaribu mengi kwa nyakati tofauti, wetu hauna tofauti na Muungano katika maeneo mengine. Kazi tuliyonayo ni kuendeleza juhudi za mshikamano na kutatua hizo changamoto ambazo sasa zinaendelea kukabili Muungano wetu. Tutaendeleza mikutano ambayo imekuwa ikifanyika chini ya usimamizi wa Makamu wa Rais ambayo inakutanisha viongozi wa pande zote mbili na naomba niendele kuwasii Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri kuendelea kutembeleana kwa lengo la kuimarisha na kujenga zaidi Muungano wetu na maelewano zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tukajikumbusha kidogo namna Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 184 nayo imeweka msisitizo mkubwa sana katika suala hili la Muungano, hivyo wote tunao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunausimamia vizuri, tunaulea kama yapo majadiliano, yazungumzwe kwa lengo la kuuboresha. Napenda kuwahakikishia wananchi wa pande zote mbili kwamba Serikali itayatekeleza haya yote kwa kadri itakavyowezekana. Zaidi ya yote, wananchi na viongozi watapata nafasi ya kutoa mawazo yao kuhusu masuala ya Muungano wakati wa mchakato wa maandalizi ya Katiba Mpya. Tutumie fursa hiyo katika kuboresha na kuimarisha Muungano wetu. Hakuna anayekataza hata kidogo kujadili muundo wa Muungano ili kuweza kupata muundo ambao mnafikiria kwamba ni mzuri zaidi, tunachowasihi, tusiuuwe Muungano.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Upinzani kuhusu ajira za upendeleo katika Utumishi wa Umma, kuna hoja iliyotolewa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba upande wa Serikali tuna upendeleo katika utoaji wa nafasi mbalimbali za Uongozi na kwa hiyo akataka tujirekebishe katika eneo hilo. Pia wako Wabunge wengi ambao nao kwa namna mbalimbali wameelekea kusema hivyohivyo. Nataka niliweke suala hili bayana kwamba Serikali ina utaratibu mzuri wa kuajiri Watumishi wa Umma. Kwa sasa kuna Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliyoanzishwa Kisheria ambayo hutangaza, kusaili na kuajiri watumishi kwa uwazi na ushindani. Wizara, Mikoa na Halmashauri zote huwasilisha nafasi zinazotakiwa kujazwa katika Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya kuajiri. Kwa upande wa nafasi za uteuzi, mamlaka ya uteuzi zimepewa mamlaka kupendekeza majina ya wale ambao wanaona wanaweza kujaza nafasi. Baada ya hapo, wanakuwa na mchakato mrefu wa kupata taarifa za utendaji, ili kuweza kuwa na watu waadilifu wanaoweza kufaa. Siyo suala la mtu mmoja kuweza kumteua rafiki au ndugu yake bila kupitia mchakato huo. Kwa upande wa Taasisi na Idara nazo vilevile zinafuata utaratibu huohuo ambao unatoa fursa kubwa kuweza kupata watendaji wazuri ambao wanaweza kusaidia katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaamini hata kwenye Vyama vya Siasa kuna taratibu zinazotumika kuchaguana kwenye kugombea Ubunge, kuteua Mawaziri, Mawaziri Kivuli na kadhalika. Mimi ni mmojawapo kati ya watu ambao sipendi kuamini kwamba bado

kuna mtu mwenye mawazo ya kwamba kuna Ukabila, Udini na Ujimbo kwenye kuteua viongozi wa nchi. Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima, nadhani tusirudi nyuma kwenye hisia hizo. Kwa maoni yangu, tudhamirie wote kusonga mbele, tujitahidi kuzingatia taratibu zilizowekwa ili kuweza kupata viongozi watakaoweza kutuongoza vizuri zaidi.

Mhehsimiwa Spika, iko hoja ambayo imechangiwa na Wabunge wengi kuhusu Serikali kufanya maamuzi magumu. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametupatia changamoto kuhusu hoja ya kutaka Serikali kufanya maamuzi na hasa maamuzi waliyoyaita magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kabisa tangu mwanzo kwamba Serikali ya Awamu ya Nne imekuwa ikifanya maamuzi thabiti na magumu lakini kwa busara na tahadhari kubwa ili kutenda haki na kwa kuzingatia uwezo wa Serikali ili kulinda maslahi ya wananchi na kudumisha amani. Katika kufanya maamuzi hayo, Serikali imekuwa makini kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa moja ya sifa za Kiongozi ni kuweza kufanya maamuzi. Tunayo historia ya Viongozi ambao tunawakumbuka kwa maamuzi yao kwa Taifa hili. Mfano mzuri tangu tupate uhuru nchi hii tunao Viongozi kama Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alisimama kidete na kufanya maamuzi magumu mengine kusema kweli yamepelekea hata Taifa letu kuweza kukosa fursa fulanifulani ambazo kama si kwa kujiingiza katika mambo hayo, pengine tungeweza kuwa katika hali nzuri zaidi. Mifano mizuri ni kazi kubwa aliyofanya ya kuamuua Tanzania kujitoa muhanga kuhakikisha nchi kama Angola, Afrika Kusini, Msumbiji, Namibia, Zimbabwe, kutaja chache zinapata uhuru kwa gharama yoyote ile bila kujali kwamba Tanzania katika kufanya hivyo vilevile ilipoteza fursa ya kuweza kufanya mambo yake hapa ndani. Awamu ya Pili hali kadhalika walifanya maamuzi magumu na wala haishangazi kwamba Mzee huyu walimwita Mzee Ruksa kwa kuwa alitoa uamuzi ambao ulikuwa si mwepesi sana katika mazingira tuliyokuwa nayo. Awamu ya Tatu hali kadhalika imefanya maamuzi makubwa mbalimbali ambayo leo ndiyo yametuwezesha kupata sifa nyingi kwa kuwa wakati huo hali ya uchumi haikuwa nzuri, lakini Rais Benjamin William Mkapa, Mstaafu, alichukua hatua thabiti kabisa kuhakikisha kwamba uchumi unarejea na kuwa thabiti. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Awamu ya Nne amechukua maamuzi magumu na mazito sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maamuzi magumu yaliyotolewa na Rais huyu wa Awamu ya Nne ni mengi lakini naomba niseme tu machache. Moja, ili kuimarisha utawala bora tumefanya uamuzi mgumu wa kuwafikisha Mahakamani waliokuwa Mawaziri wa Serikali zilizopita kutokana na tuhuma mbalimbali zinazowakabili za kutumia madaraka isivyo halali. Serikali ya Awamu ya Nne ndiyo iliamua kujenga Shule za Sekondari za Kata ambazo zimewezesha wanafunzi wengi kupata elimu ya sekondari. Leo tunashuhudia vijana wetu ishirini tukiwapongeza hapa, haya ni matunda ya maamuzi magumu lakini ambao leo yanaonekana kuwa na manufaa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweka historia ya kuamua kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho hakina mfano katika Bara la Afrika. Kwa wale ambao pengine hamjapata nafasi ya kwenda Hombolo, muende mkaone kazi nzuri inayofanywa pale Hombolo kujenga Chuo kwa ajili ya kuendeleza Serikali za Mitaa. Itawasaidieni kuweza kufahamu kwamba kwa kweli katika kufanya maamuzi, Rais na Serikali yake wamejitahidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imekamilisha miradi yote 27 ya barabara kuu zilizoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Hivi sasa unaweza kutoka Mtwara - Dar es Salaam - Dodoma bila matatizo hadi Mwanza kwa kupitia kwenye barabara za lami. Vilevile, tumeamua fedha zote za *MCC* tuzipeleke kujenga barabara za Mikoa iliyoko pembezoni. Tumeshuhudia ndani ya Bunge hili Waheshimiwa Wabunge, bila kujali itikadi za Vyama wakisifu maendeleo yaliyopatikana kule Kigoma. Tumesikia maendeleo yaliyopatikana kule Kilimanjaro. Tumesikia maendeleo yaliyopatikana kule Rukwa, na tumesikia maendeleo yaliyopatikana kule Mtwara. Tumesikia maendeleo yaliyopatikana maeneo mbalimbali nchini ambapo barabara za lami sasa zinakaribia kukamilika. Tutasimamia hili kikamilifu kabisa na nataka niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuko pamoja nanyi na tunazo fikra zinazofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukamilishaji wa miradi ya maji nchini. Tumefanya maamuzi mazito katika kuwalinda Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi lakini vilevile kuondoa mpasuko wa kisiasa Zanzibar, ilitulazimu tufanye uamuzi mgumu wa kuanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na leo wote tunaona matunda ya uwepo wa Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa. Tumefanya maamuzi ya kupanua na kushamiri kwa demokrasia nchini kwa kiwango kikubwa. Nadhani, hii ndilo linasababisha baadhi yetu sasa tunajisahau na kuanza kutumia maamuzi hayo visivyo. Tunahamasisha maandamano huku tukijisifu kwamba huo ndio uzalendo. Zaidi ya hayo, tumefanya maamuzi ya kuruhusu uhuru mkubwa wa Vyombo vya Habari, mtu anaandika anachotaka na uhuru wa kusema analotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumefanya uamuzi wa kuruhusu kuanzisha mchakato wa kupata Katiba Mpya. Hili nalo siyo jambo dogo hata kidogo, kubwa. Nimalizie kwa kusema ilikuwa ni awamu hiihii ambayo imelazimika kufanya uamuzi mgumu na mzito sana wa kuvunja Baraza la Mawaziri kufuatia kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa. Hili nalo jamani halikuwa jambo jepesi hata kidogo lakini ilitaka moyo na uamuzi ukafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, orodha ni ndefu na nisingependa kuwachosha katika kujaribu kueleza zaidi lakini nataka nisisize jambo moja kwamba maamuzi haya ni sehemu ya maisha ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake kwa dhana ya uwajibikaji wa pamoja *(collective responsibility)* kupitia Baraza la Mawaziri. Si sifa ya mtu yeyote mmoja mmoja hata kidogo. Ni sifa ya Serikali yote kwa kuwa tunafanya maamuzi haya kwa pamoja kwa lengo la kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika. Tunachohitaji zaidi hapa ni kuvumiliana, kuvuta subira, kwani mambo mema hayataki haraka. Tutaamua na tutayafanya.

Mheshimiwa Spika, mahusiano kati ya Waheshimiwa Wabunge na Watendaji wa Serikali. Mahusiano mema baina ya Viongozi na Watendaji katika ngazi zote za Serikali ni jambo muhimu mno linalosaidia kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala tuliokuwa nao hapa Bungeni, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametoa shutuma nzito kwa baadhi ya Watendaji wa Serikali. Tumefuatilia na kupata maelezo ya kina kutoka kwa wahusika. Jambo kubwa linalojitokeza ni kuwa kama Viongozi na Watendaji wangekuwa na mahusiano mema, mawasiliano kwa kupitia Vikao vilivyopo kwa mujibu wa Sheria mambo haya yasingetokea na yangemalizwa mapema huko huko kwenye Halmashauri na Mikoani. Napenda ieleweke kuwa tunapogombana Viongozi kwa Viongozi au Viongozi na Watendaji wanaoumia ni wananchi tunaowaongoza.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo wetu wa Uongozi tumeweka ngazi mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wanashirikishwa ili waweze kuwawakilisha wananchi ipasavyo. Aidha, Serikali imetoa fursa katika ngazi hizo, ili Wabunge wapate fursa ya kuwasilisha maoni ya wananchi. Kwa mfano, katika ngazi ya Wilaya, Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe hakukutoa picha nzuri sana. Nataka niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba sisi Wabunge tunazo fursa nyingi sana za kuwa sehemu ya maamuzi katika Wilaya zetu:-

(i) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati mbalimbali za Halmashauri ikiwemo Kamati ya Fedha na Uongozi;

(ii) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wilaya *(DCC);*

(iii) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Menejimenti na Uratibu wa Maafa (Wilaya);

(iv) Mbunge ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama chake katika Wilaya; na

(v) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati za Matukio mbalimbali yanayotokea ndani ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika Ngazi ya Mkoa; Wabunge ni Wajumbe wa Kamati zifuatazo:-

(i) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC);

(ii) Mbunge ni Mjumbe wa Bodi ya Barabara ya Mkoa (*Regional Road Board Committee*);

(iii) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Biashara ya Mkoa;

(iv) Mbunge ni Mjumbe wa Vikao vya Kamati na Sherehe mbalimbali; na

(v) Mbunge ni Mjumbe wa Kamati za Matukio makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa, tutumie fursa za Vikao na Kamati hizo kujadiliana kama kuna haja ya kusemana tusemane, tuwekane sawa , kwa manufaa ya Watanzania, kama hilo halitoshi Waziri Mkuu yupo. Kama mnaona Waziri Mkuu hamwezi kumfikia kwa urahisi Waziri mwenye dhamana kwa maana ya Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yupo. Nawaombeni sana yawasilisheni kwake na mimi nina hakika yatapata ufumbuzi. Ni imani yangu kwamba baada ya maelezo haya yale yaliyotokea katika maeneo hayo basi tutahakikisha kwamba sasa tunakokwenda hayatokei tena. Naomba niwasihi sana kwamba wakati mwingine katika Mabaraza ya Madiwani, Madiwani wamebanwa mno katika kutoa mawazo yao kwa uhuru mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana uamuzi wangu wa kutaka na wao wawe na dakika angalau 30 za kumhoji Mkurugenzi juu ya jambo lolote lile katika Halmashauri sasa liwekewe utaratibu ili na wao waweze kupata fursa ya kuhoji na wapewe majibu badala ya kutoka pale na kwenda kunung'unika pembeni. Nafahamu lipo tatizo la vikao mbalimbali katika baadhi ya maeneo Mikoani na Wilayani kutowiana na vikao vya Bunge. Tutajitahidi kulisimamia hili. Tumekuwa tukitoa maelekezo ya mara kwa mara lakini tutalisimamia vizuri zaidi ili vikao vya Bunge visigongane na vikao vya Mabaraza ili kuwawezesha Wabunge waweze kuwa washiriki wakamilifu kabisa katika mambo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wote tutumie vikao hivyo kutatua changamoto zote tulizonazo kwa kuwa naamini uwezo wa kufanya hivyo upo na tunao uwezo wa kufanya vizuri zaidi huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi siwezi kuzimaliza kujibu kwa leo. Hoja hizo zitajibiwa kama nilivyosema na baadhi ya Wizara za Kisekta lakini kwa wingi wake ukichanganya na zile ambazo zitajitokeza wakati huenda na wao wasizimalize zote. Naomba kuwaahidi tena kwamba tutajitahidi zote kuzichapisha na kuwaarifuni kwa maandishi ili muweze kujua Serikali ilichosema ni nini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niombe radhi kwamba nilisahau kutaja jina la Mbunge mwenzangu mmoja Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe. Naomba radhi kwa kusahau jina lako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Uombe kutoa hoja.

**WAZIRI MKUU:** Aaaa *sorry,* naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge katika mmoja ambaye jina lake pia mmelisahau ameniletea ki-*note* hapa ni Mheshimiwa Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Jimbo la Busega. Naye pia amechangia kwa maandishi. Ningependa kuwatambua wageni wawili walioingia sasa hivi. Kwanza kabisa yupo Mheshimiwa Mama Tunu Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na mwingine Mheshimiwa Abdulrahmani Kinana, Spika Mstaafu wa Bunge la Afrika Mashariki na wengine ambao sikuwaona tena karibuni, tunaendelea na kazi. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaingia hatua moja kubwa ambayo tungependa wote tuwe makini. Katika Kanuni zetu Kanuni ya 99 inasema: "Baada ya kumaliza kikao cha bajeti yaani hotuba ya bajeti tunakuwa na siku zisizopungua 50 kufikiria matumizi ya Wizara mbalimbali". Kwa hiyo tumeanza na Wizara ya Waziri Mkuu. Sasa katika kufanya kazi hii kuna mambo ambayo mtabidi mfanye. Kwa mujibu wa kifungu cha 101 pale mnaruhusiwa tukiingia kwenye kifungu kuuliza maswali, kupata ufafanuzi mambo ambayo yatatumia kama dakika tano, wewe unayepata nafasi ya kuuliza swali unaweza kujieleza, halafu kama utarudia baadaye ni dakika tatu.

Lakini ningependa Waheshimiwa Wabunge tuwe waangalifu, saa nyingine wanakujibu kabisa, lakini tena unauliza vile vile ulivyojibiwa, si kupoteza muda huko! Ningeomba upande wanaojibu nao wajaribu kujibu angalau kwa ukweli na ufasaha kusudi tuweze kupunguфu kujibu. Maana yake inakuwa kama ni lazima mpaka uulize tena swali la nyongeza si lazima. Kama umeridhika inabidi utulie kusudi utoe nafasi kwa watu wengine.

Kuna hatua nyingine ambayo tuna suala zima la kuondoa shilingi. Kwa mujibu wa kifungu cha 103(2), unaweza kuondoa shilingi. Sasa kuondoa shilingi wanasema mpaka uwe na jambo fulani mahususi. Kwa sababu kitendo cha kuondoa shilingi ni hoja. Lakini utapata dakika zile zile tano, kama kuna wenzio watakuunga mkono watapewa dakika tatu. Baada ya hapo watakujibu na wewe utakuwa na nafasi ya kujibu. Lakini kama ikionekana unang'ang'ania kukaa na shilingi hiyo tunapiga kura, tukipiga kura ukishinda na shilingi yako basi tutakuwa tumepitisha makadirio yakiwa yamepungua shilingi moja. Ukishindwa basi tunaendelea na vile ilivyo. Lakini ni jambo mahususi sio tu mnaondoa shilingi.

Sasa kama mtakavyoona hapa tuna saa moja. Ma-*book* niliwaambieni leteni matatu na yapo. Kwa hiyo Kitabu cha Pili ni matumizi ya kawaida. Katika matumizi ya kawaida tuna Fungu la 25. Sasa pale hakuna mshahara wa Waziri, ni Ofisi binafsi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, huwezi kusimama pale kwa ajili ya mshahara wa Waziri Mkuu. Mtakapotakiwa kusimama kwa ajili ya mshahara wa Waziri katika

matumizi ya kawaida ni Ofisi ya Waziri Mkuu, *Vote 37.* Kwa hiyo msije mkatoa mshahara katika Fungu 25 siyo penyewe.

Halafu tuna *Vote* nyingi katika matumizi hayo, ziko *vote* moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Kuna *vote* kama nane, halafu tutaingia kitabu cha tatu. Kitabu cha tatu ni matumizi ya kawaida ya Mikoa. Kwa sababu mikoa yenyewe iko mingi hatuwezi kuingia na yenyewe kifungu kimoja kimoja, tutakuwa tunakwenda Fungu la Mkoa, yaani tunataja mkoa fulani jumla yake. Kama umejiandaa utasimama utatuambia wapi unapotaka tu-*pay attention.*

Halafu tuna kitabu cha nne. Kitabu cha nne ni matumizi ya maendeleo. Sasa tukifika kitabu cha nne huwezi kuuliza swali ambalo halihusiani na kile kifungu. Huwezi kuuliza jumla jumla, kwa sababu ni maendeleo, ni kitu kilichopo ambacho tumepangiwa, ama unauliza hela, haitoshi au vinginevyo. Tutakuwa *very specific*. Huwezi kusimama tu kwamba, fungu fulani, lazima uingie kwenye kifungu mpaka na *sub-item.*

Sasa kwa haya yote inaonekana kwamba muda tulionao utakuwa una matatizo. Nina mamlaka ya kuongeza dakika thelathini baada ya saa za kawaida kwisha. Lakini pia ikibakia dakika 10 baada ya kuongeza zile dakika thelathini kama hatujafikia mwisho, jamani kuna kifungu cha *guillotine* maana yake tunaenda fungu moja hadi lingine bila hata kupewa mtu nafasi. Kwa hiyo, tutumie muda vizuri tuone tutafika wapi. Baada ya kusema hayo tunaingia kwenye kazi. Kama mkipenda muulize maswali kwa kifupi, siyo kuhutubia tena, tunaweza kwenda hatua ndefu zaidi. Tunaanza na kitabu cha pili. Katibu.

**VOTE 25 – PRIME MINISTER**

Kif. 1001 – *Administration and General*..Sh. 5,567,331,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi, ni *programme 10, Sub-Vote 1001,* sehemu ndogo ya 230100 *Routine Maintenance and Repair of Roads and Bridges.* Sasa nimeona pale pamekuwa panatengewa shilingi milioni mbili, sasa nikawa najiuliza hizi milioni zinaweza zikafanya kazi gani zilizotajwa kwamba ni *Routine Maintenance and Repair of Roads and Bridges.* Nilitaka kupata ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mmemwelewa? Anaweza kurudia kama hukumwelewa. *Microphone.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimepewa kama sehemu ya kumwezesha Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa msaada katika matengenezo madogo madogo kwa kadri anavyofanya ziara katika maeneo mbalimbali.

Samahani kidogo, samahani nilikuwa nimeangalia ni kifungu 230100. Ndani ya makazi katika maeneo ya makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Dodoma na Dar es

Salaam hizi zitatumika kama matengenezo ya mandhari na barabara mbalimbali zilizopo zinazopita ndani ya maeneo ya Waziri Mkuu endapo itahitajika. *(Makofi)*

Kule ndani huwa kuna vivuko vya maji machafu vile vile. Humu yameandikwa madaraja. *(Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ikubali kufanya masahihisho, kwa sababu shilingi milioni mbili sijui kama kwenye makazi ya Waziri Mkuu hakuna madaraja. Kwa hiyo, tufanye kwenye kifungu hicho.

**MWENYEKITI:** Hatuwezi kufanya sisi hapa, mradi maelezo mmepata. Baadaye kama *sub-vote* hizi zilikuwa zimeandikwa visivyo, basi watazifanyia marekebisho yanayostahili.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante *Vote 25*.

**MWENYEKITI:** Sasa naitwa Mwenyekiti jamani.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** *Sub-vote 1001* Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha utaratibu mzuri sana.

**MWENYEKITI:** Rudia tena sisi hatukupata hicho kitu.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** *Vote 25, sub-vote 1001* mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Tumekwambia hapo hakuna mshahara wa Waziri Mkuu.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Sawa, Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha utaratibu mzuri.

**MWENYEKITI:** Utaingia baadaye Mheshimiwa Pamba, kuna kifungu, *Vote 37* na tumekubaliana hivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**VOTE 27 – REGISTRAR OF POLITICAL PARTIES**

Kif. 1001– Admin. and General ...............Sh. 19,451,933,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**VOTE 37 – PRIME MINISTER'S OFFICE**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... .... .... Sh.

**MWENYEKITI:** Naomba mkae kwanza mpaka asome na hesabu aseme. Anataja kifungu, anasoma hesabu kabla sijawahoji ndiyo mnasimama. Tunaendelea.

**VOTE 37 – PRIME MINISTER'S OFFICE**

Kif. 1001 – *Admin. and General*................Sh. 3,890,971,700/=

**MWENYEKITI:** Sasa tunasimama. Haya mtalala humu humu basi. Naanza kuwataja Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Nkumba, Mheshimiwa Serukamba. Twende upande huu, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mnyaa. Twende hapa katikati Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Esther Bulaya nafikiri yupo. Hapo ndiyo mtihani wa Spika kuwajua watu. Mheshimiwa Kabati, Mheshimiwa Lwanji, tunakujua Mheshimiwa Lwanji.

Wengine ni Mheshimiwa Filikunjombe yuko mwenyewe peke yake. Tuje huku, Mheshimiwa Sakaya, wasiotajwa waendelee kusimama. Twende mpaka kule mwishoni kule. Mheshimiwa Dkt. Kebwe, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Mdee. Twende hapa Mheshimiwa Pamba tulikuona. Mheshimiwa Ntukamazima, Mheshimiwa Mwaiposa. Waheshimiwa tunarudi huku, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Zambi. Tunaendelea, Mheshimiwa Nchemba tunamwona. Tumalizie na hapa Mheshimiwa Salum. Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Kilufi. Mheshimiwa kule nyuma, Mheshimiwa Hewa, Mheshimiwa Kandege.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda nisimame katika hiyo *Sub Vote Number…*

**MWENYEKITI:** Tunajua mshahara tu, endelea.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza kwa sababu uchumi wa wananchi wa Dar-es-Salaam ni biashara zao na majengo yao yaliyoko katika Mkoa wao. Lakini katika hii bomoabomoa nimeona kuna mikoa mingine ambayo tayari wamepata athari kwa ng'ombe kufa na ukame, nao wameambiwa moja kwa moja kwamba watafidiwa. Je, hawa wananchi waliopata *stroke* katika barabara ya Kilwa, barabara ya Kigogo, barabara ya Ubungo Maziwa! Je, wao hawastahili kulipwa fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu halikunitosheleza. Lakini pia nimeona kwamba kuna maelezo kwamba kuna urekebishaji wa Sheria, je wale ambao wamelipwa, walilipwa kwa Sheria gani? Je, na hawa ambao hawajalipwa, hawatalipwa kwa sheria gani? Naomba ufafanuzi katika hilo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wakati mwingine mtakapokuwa mnauliza, unauliza swali moja tu. Sio *item* mbili, tatu.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Sera na Uratibu! Naibu Waziri wa Ujenzi, ndio wote Serikali nzima mnaweza kupata kujibu hapo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, chini ya Sheria yetu ya Bunge ya mwaka 2007, mtu yeyote ambaye barabara inamfuata anastahili kulipwa fidia, lakini yule mtu ambaye amejenga ndani ya hifadhi ya barabara, huyo hastahili kulipwa fidia. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge ajue, kama kuna mtu yeyote ambaye amefuatwa na barabara, anastahili kulipwa fidia. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza hapo hapo kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Zimetolewa hoja nyingi sana kuhusu matumizi ya Serikali. Aidha, Serikali kupitia Mawaziri mbalimbali imejibu na kipekee ikazungumzia Mpango wa Miaka Mitano, ukurasa wa 17 ambao ulizungumzia mipango mbalimbali itakayofanyika katika kubana matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo tulieleza katika Hotuba yetu ya msingi kwamba, zaidi ya 70% ya matumizi ya bajeti ya Serikali inaelekezwa kwenye matumizi. Na kwa sababu ni fungu kubwa mno na kwamba kama itafanyika hatua za makusudi na za haraka, Taifa linaweza kuokoa fedha nyingi sana ambazo zitasaidia katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imekiri kwamba ina nia njema katika hili, ni rai yangu kwamba, sasa Serikali ifanye mambo mawili na tuhakikishiwe na Serikali ili tuweze kukubali. Kwanza, ihakikishe katika muda ambao ni *specific* inaleta Sera ya Matumizi ya Umma na Matumizi ya Serikali. Kwa sababu, bila *Policy* inayo-*guide,* kila Taasisi ya Umma au ni Shirika la Umma au Wakala wa Serikali, wanajikuta wana uhuru wa kutekeleza mipango yao ya matumizi bila kuwa na *guideline* ambazo zinatokana na Sera ambayo ni lazima ifuatwe na Mashirika yote ya Umma… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tunaomba sasa unaingia kwenye kuchangia wakati hapa inatakiwa tuombe ufafanuzi.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni hoja yangu Serikali itoe tamko ni lini basi italeta mahususi Sera hiyo ya Matumizi ya Umma, iweze kuridhiwa na kujulikana kwamba ndio *blue print* ya kufuatwa na Taifa zima ili tuokoe fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na Sera hiyo ni ukweli usiopingika kwamba bado kuna matumizi mengine ambayo hayabanwi na Sheria, hayabanwi na Sera, hayabanwi na taratibu wala Kanuni za Uendeshaji wa Taasisi za Umma. Tumezungumza hapa kuna matumizi mengine ya Serikali ambayo sio ya lazima ambayo yanasababisha wizi wa kitaasisi ndani ya Taasisi za Umma na hapo Serikali ingeweza kukomesha upotevu huu kwa kutoa tamko kwamba kuanzia sasa vitu kama fulana, kofia, mabegi na vifaa vingine vinavyogawiwa bure kwa Viongozi, Wabunge na watu wengine katika

Semina na Makongamano mbalimbali ambavyo vinatumia mamilioni ya fedha za wananchi, tuvipige marufuku ili tujue tunaokoa hizi fedha ziende kwenye miradi mingine ya maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

**WAH. WABUNGE:** Aaaaah!

**MWENYEKITI:** *Item…*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inaruhusu mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tu ambalo ni la msingi sana ni kuhusu Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika hoja za msingi katika Hotuba yangu, nilizungumza kwamba tuna Makao Makuu ya Tume Dar-es-Salaam, ambayo inafanya kazi ya kuratibu maadili ya Viongozi wote wa umma, kuanzia ngazi ya chini kabisa kwa Madiwani mpaka Viongozi Wakuu wa Taifa. Ilikuwa rai yetu kwenye Kambi yetu ya Upinzani kwamba, ili kuwaondolea adha watumishi wetu katika ngazi za chini, basi Ofisi za Wakuu wa Mikoa katika mkakati ule ule wa kugatua madaraka kwenda katika ngazi za chini ziweze kuratibu masuala ya maadili ya Viongozi katika ngazi hizo za Wilaya na Kata.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kidogo kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Upinzani. Ni ngumu sana kusema muda maalum wa kuleta Sera, kwa sababu ingawa jambo lenyewe hili alilozungumza Mheshimiwa Mbowe, Kikanuni si mahali pake kwa sababu, hapa si mahali pa Sera ni mahali pa kutaka ufafanuzi juu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusema ni kwamba katika ule mpango naweza kusema mambo haya yote yanatekelezeka katika kipindi hiki cha miaka mitano kama mpango wenyewe ulivyoainisha, huo ndio muda muafaka ambao tumeuweka. Katika kutekeleza matumizi haya, yatakuja maelekezo maalum ndani ya Serikali yatakayoelekezwa na mpango ambayo yatazingatiwa na utumishi wote wa umma juu ya matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kipindi maalum ni hiki ambacho Bunge tumeipa Serikali katika kutekeleza jambo hili, miaka mitano. Tutakuwa tumekamilisha na kuweka hizo *guidelines* za matumizi ya umma kama anavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili pamoja na haya matumizi ambayo anasema hayabanwi na Sheria mbalimbali, ugawaji wa *T-shirt,* kofia na nini, haya ukinyumbua yako mengi sana. Mambo ambayo tunafikiri na hata kama Tume ingeweza kuweka nyongeza ya mambo ambayo watayatazama katika jambo zima la kupunguza gharama za matumizi ni pamoja na haya. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbowe, atupe

muda, haya ndio mambo hasa tunayotaka kwenda kuyaangalia, matumizi ambayo yanaweza yakapunguzwa katika kuendesha Serikali ni pamoja na haya. Lakini katika kipindi cha miaka mitano tutakuja na utaratibu maalum ambao utaelekeza aina ya magari yanayotakiwa na Serikali, uwiano wa matumizi, matumizi gani, posho na matumizi mengine katika gharama nzima za kubana matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumepokea hilo wazo jipya la kuwarahisishia kazi wenzetu wa Tume ya Maadili. Naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie jibu la Mheshimiwa Mbowe, kuhusu Tume ya Maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili mwaka 2005 ilifungua Ofisi katika Kanda sita za nchi hii na tunakusudia katika mwaka huu wa fedha tufungue Ofisi katika Kanda zingine tano, lakini nia ni kupeleka Ofisi hizi katika kila Mkoa wa nchi hii. Kwa hiyo, tunakwenda taratibu tutafika kila Mkoa na hatimaye nahisi tunaweza tukafika kila Wilaya kama tulivyofikisha TAKUKURU. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Waheshimiwa Mawaziri, la pili nimeridhika kuhusu maadili lakini hili la matumizi ya Serikali kujikita kwenye kipindi cha miaka mitano, panaonekana hapana dhamira ya kweli. Suala la matumizi ya Serikali ni suala ambalo ni *urgent* na ni suala ambalo tukidhamiria kweli kulifanya, tunaweza kulifanya katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ombi la Kambi ya Upinzani ni kwamba, Waziri atuhakikishie kwamba, inawezekana kuleta pendekezo hili katika muda wa mwaka mmoja ujao, hata kama sio bajeti hii, basi bajeti ya mwaka ujao? Lakini kutoa uhuru wa miaka mitano kwenye jambo hili ni hakika miaka mitano Serikali hii itakuwa inaondoka madarakani na haitakuwepo madarakani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongezea ufafanuzi. Kwanza si sahihi kusema kwamba hatuna Sheria yoyote inayo-*guide* matumizi katika Serikali ya sasa hivi, tunazo Sheria zinazo-*guide* matumizi ya Serikali, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Lakini kila mwaka kabla ya *planning* huwa Wizara ya Fedha inatoa *planning guideline* ambazo zinatumika katika kuandaa mipango yetu. kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, asipotoshe jamii kwamba Serikali iliyopo madarakani haina Sheria zinazo-*guide* matumizi. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia niliiomba Serikali yetu Tukufu itusaidie 800,000,000/= tulizoomba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika Wilaya ya Bahi, ambayo iliundwa mwaka 2004 na mpaka sasa hakuna nyumba za watumishi na Bahi ilikuwa Makao Makuu ya Tarafa, kwa hiyo hakuna

nyumba za kuweza kuishi watumishi 160 wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi. Lakini katika majibu ya Waziri Mkuu, sikusikia kuligusia hilo! Naomba Waziri Mkuu na Serikali ituangalie kwa jicho la huruma kwa sababu, wale watumishi wanatakiwa kuhamia tangu leo. Nauli ya kutoka Dodoma Mjini mpaka Bahi ni 2,000/= au 4,000/= kwenda na kurudi na kule hakuna nyumba za kuishi watumishi. Naomba ufafanuzi katika hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya mpya katika nchi hii ziko nyingi na hivi karibuni tunategemea nyingine zitaanza. Nimefika Bahi, tatizo analolieleza Mheshimiwa Mbunge, ni la msingi. Serikali inafanya mazungumzo na Shirika la Nyumba la Taifa ili waweze kujenga nyumba pale. Wale watumishi ambao sio *entitled,* ambao hawasubiri kujengewa nyumba na Serikali waweze kupata nyumba za kupanga.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo tu. Naomba kujua kwamba mazungumzo haya yameshakamilika au bado hata hayajaanza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwalimu wa lugha. Nilisema Serikali inafanya mazungumzo, kama unafanya mazungumzo maana yake umeanza.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nimezungumzia kwa hisia kali sana juu ya malalamiko makubwa sana ya wakulima wa tumbaku nchini. Kwamba, hivi sasa masoko yanaendelea lakini ratiba ambazo wakulima wanapangiwa sasa hivi, wamepangiwa ratiba ndefu mno! Kwamba kwa soko hadi soko, karibu mwezi mzima! Kwa hiyo, unaendelea kukaa na tumbaku yako, inapoteza uzito lakini vile vile inapoteza thamani na hii itakuwa hasara vile vile kwa wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niiombe Serikali labda inipe maelezo hapa, nilipochangia sikuona maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametujibu. Kama Serikali sasa iko tayari kuingilia kati kwa sababu malalamiko baadaye yanakuja kwenye Serikali, kuingilia kati kuona masoko haya yanarekebishwa ili yawe kama zamani ambayo yatakuwa yanakwenda angalau mara mbili labda kwa mwezi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nitoe maelezo yafuatayo. Ni kweli kwamba masoko ya tumbaku kwa mwaka huu yalianza polepole, lakini uongozi wa Mkoa wa Tabora uliitisha kikao cha wadau wote, wawakilishi wa wakulima, Vyama vya Ushirika kuanzia Vyama vya Msingi mpaka kwenye *Apex,* wawakilishi wa Serikali na wanunuzi pamoja na Bodi ya Tumbaku. Wameyazungumza matatizo mengi ambayo yanakumba msimu ikiwa ni pamoja na sababu ya bei ambayo ni ya chini kidogo mwaka huu ukilinganisha na ile ya mwaka jana, pamoja na wakulima wengi kuweka uchafu ndani ya tumbaku kama hatua ya ku-*compensate* uzito na kadhalika na kwamba wadau

wote walikubaliana namna ya kuendelea na soko na hivi sasa masoko yanaelekea kwenda vizuri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilitaka kupata maelezo ya Serikali. Nilikuwa nimependekeza tufanye mageuzi makubwa ambayo naamini yatakuwa ya kihistoria katika usimamizi mzima wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunabishana hapa kuhusu matumizi lakini nilisema njia bora zaidi ambayo wamefanya wengine ni ile namna ya ku-*account* fedha za Serikali. Serikali, leo tunatumia *Cash Budget,* katika mazingira ya kutumia *Cash Budget,* hutarajii mwisho wa mwaka kukuta madeni. Lakini leo, ukienda kila Idara ya Serikali yapo madeni ya mwaka jana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna bora ili tuweze kuyasimamia vizuri ni lazima turudi kwenye *Accrual basis* ambayo tutaomba kila Katibu Mkuu, nilikuwa nimependekeza, kila mwaka atoe *Financial Statement under IFRS,* ambayo maana yake ni nini? Ukitoa *under IFRS* maana yake una *disclosure* kubwa na kama *disclosure* ni kubwa unaweza sasa tuka-*track* matumizi. Kwa hiyo, *CAG* kila mwaka kila Wizara itatoa ripoti yake na kila Idara za Serikali halafu *CAG* atazipitia ni rahisi kuweza kuona matumizi ambayo ni ya lazima na yasiyo ya lazima katika mazingira hayo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema Australia na Newzland wamefanya na ndiyo sehemu bora pekee duniani, matumizi ya Serikali yametengenezwa vizuri sana na hii itazuia deni la Taifa kwa maana kwa ndani kupanda kila wakati. Ukienda leo Magereza wanadaiwa na vendors wengi sana, Polisi wanadaiwa, Jeshi wanadaiwa, Serikali, Wizara za Serikali zinadaiwa, wenye hoteli kule Dar es Salaam wote ukimuuliza kila mmoja anaidai Serikali. Lakini namna bora ya kuweza kuzuia haya matumizi na watu waweze kwenda kulingana na bajeti lazima twende kwenye hiyo fomu ya kutengeneza financial statement.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu moja na naomba Serikali wanielewe.

**MWENYEKITI:** Lakini usituutubie, wewe useme unachotaka Serikali ifanye.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dakika tano utanielewa tu, ninachotaka kusema hivi vitabu tunavyopitisha hapa Bungeni, tunapitisha fedha na matumizi ulitarajia mwisho wa mwaka tusione madeni, kwa sababu tumepitisha fedha hizi *unless* tuje, baada ya miezi tuje ku-review bajeti, lakini kama tumemaliza mwaka mzima maana yake tumepitisha vitabu hivi unatarajia uone kilichoombwa na Serikali ndicho kilichotoka na kama hakikutoka sababu ziwepo. Naomba maelezo ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao. Wazo la kuboresha matumizi au usimamizi wa matumizi ya Serikali ni moja katika mambo ambayo siku zote tunaona ya maana na tunayafuatilia. Wazo la Mheshimiwa Serukamba tutalifuatilia Australia na kwingineko na likionekana linafaa tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Si wamesema watafuatilia huko au umeamua kufanyaje sasa waende leo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka na Wabunge wawemo.

**MWENYEKITI:** Naomba tuwe *brief* maana yake sasa kama watafuatilia wewe fuatilia.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Ninachotaka kusema ni kwamba, nashukuru sana Serikali kwa kukubali, nataka kwenda mbali zaidi ambalo naona hakulisema, nimesema tunapitisha vitabu vya bajeti, tunapokuja kwenye utekelezaji mwisho wa bajeti Kamati zile za kisekta unakuta pesa kiasi fulani hazikuja lakini sisi tulipitisha hapa, maana yake ni nini, tunataka yule sasa ambaye anakusanya zile pesa kwa maana ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha aweze kutoa sababu ya kutoa *financial statement* tutajua sasa je, ni kweli hazikukusanywa.

Je, ni kweli wale waliotuahidi hawakuleta? Kwa nini sasa hazikwenda kwenye Wizara nyingine, hii ndiyo njia pekee tutakayoweza ku-*control otherwise* tutakuwa tunapitisha vitabu kila mwaka, mnamaliza baada ya mwaka mmoja, tunasema fedha hizi hazikuja na Waziri anatoa ripoti tunapitisha tunakwenda mbele.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kurudia kwamba wazo la Mheshimiwa Serukamba ni nzuri na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hiyo hiyo, katika mchango wangu nilizungumza suala zima la watu waliojitokeza kupiga kura katika uchaguzi wa 2010 na hali halisi ya mtiririko na Tume ya Uchaguzi, nategemea angalau nitapata jibu lakini sijapata jibu na picha halisi, nilitaka kujua kwamba hizi sababu yakini kwamba 1995 watu waliojitokeza kupiga kura asilimia 77; 2000 watu waliojitokeza asilimia 84.4; 2005 asilimia 72.4; lakini 2010 asilimia 42, kinachojionyesha hapo ni kwamba, watu hawaji kupiga kura sababu hasa ikiwa waliojiandikisha milioni 20, 137,303 halafu wapige kura watu milioni 8.6 hapa ndipo penye tatizo la msingi. Inawezekana watu wamekosa imani na Tume ya Uchaguzi na ndiyo moja katika sababu ya kuwafanya watu wasiende kupiga kura. Nataka maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo linaunganika hapo, bahati nzuri tuna mchakato huu wa Katiba Mpya na kama tunategemea kupata Tume Huru ya Uchaguzi baada ya kupata Katiba mpya, muda ule wa hiyo Tume Huru itakayotegemewa katika kupata Katiba mpya kama tutamaliza April, 2014 mpaka kufikia uchaguzi wa Oktoba, 2015 ni muda mdogo, ni dhahiri kwamba Tume inakuwa ni ile ile au sheria zitakuwa ni zile hata kama Tume itakuwa nyingine, sheria zitakuwa ni zilezile hata kama Tume itakuwa nyingine, bado tutakuwa na tatizo la uchaguzi huru na wa haki. Nilitaka maelezo pale na kwenye maelezo yangu nilipendekeza na napendekeza tena na nataka kauli ya Serikali, ikiwa je, hatuwezi mchakato wa kupata Tume Huru ya Uchaguzi na mchakato wa Katiba mpya ziende sambamba kupitia *TCD* pamoja na Serikali vishirikiane ili viende sambamba kama kuna sheria baadaye zibadilishwe ikifika 2015 tusiwe na matatizo tena, Watanzania tuiamini Tume yetu ya Uchaguzi itakayopatikana hapo, hivi sasa kuna matatizo, naomba tamko la Serikali. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa amekuwa anauliza swali hili kila mara na nampongeza kwa kufuatilia sana. Ni kweli tumekiri na taarifa zimeonyesha kwamba upigaji wa kura mwaka uliopita na takwimu zinaonyesha watu wachache sana walipiga kura. Ameshawahi kutoa sababu na tukaziunga mkono tukasema baadhi inawezekana ndizo hizo. Lakini jibu la msingi la sababu halisi zilizosababisha hatuna kwa sasa kwa sababu Tume yetu inaendelea, bado kufanya utafiti ili tujue ni sababu zipi hasa zilizosababisha watu kutokujitokeza kupiga kura. Tunaweza tukaorodhesha nyingi lakini naomba tusubiri utafiti unaofanywa halafu tutautangaza wazi kujua kitu gani kilichosababisha hasa mpaka watu wakakosa kwenda kupiga kura. *(Makofi)*

Lakini Tume huru ndiyo malengo ya Katiba hii, mapendekezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa katika kuunda Katiba Mpya ni kwamba lengo la juu kabisa ingewezekana Katiba hii iwe imekamilika ifikapo 2014. Kwa hiyo, hili ndilio lengo na pengine baada ya hapo ianze kutumika. Ni imani ya Serikali kwamba, uchaguzi ujao kama mambo yatakwenda vizuri utafanyika chini ya Katiba mpya na Tume mpya kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba. Kwa hiyo, naamini kwa sababu bado tunaendelea na humu ndani tutakuwa na mjadala wa hiyo sheria dhidi ya hadidu zake, naomba Mheshimiwa Mnyaa tusubiri muda utakapofika tujadili vizuri mapendekezo ya kuunda sheria ambayo itasimamia jambo hili. Nafikiri si wazo zuri kupeleka mambo mawili kwa mpigo. Naamini hii Katiba itatoa mwelekeo na maelekezo ya namna uchaguzi utakavyoendeshwa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tunajifunza na yaliyopita, kitendo cha ile Sheria ya Gharama za Uchaguzi halafu tukaingia uchaguzi, hapana muda na kitendo cha kutegemea kumaliza mchakato wa Katiba Mpya Aprili, 2014 pamoja na kwamba tutapata Tume mpya ya Uchaguzi muda ni mdogo, hoja hapa muda ni mdogo. Sasa hata kama ningeiomba Serikali kutafuta *mode* yoyote ya kutayarisha angalau haya mambo yaweze kwenda sambamba kabisa, hakuna tatizo. *We are provided,* tutashirikiana ndani ya Bunge hili hakuna tatizo, tunaweza kwenda sambamba ili hata tukishapata ile Katiba mpya ule hata kama tutakuwa na Tume mpya Huru ya Uchaguzi lakini muda ni mfupi ambapo matatizo yatajitokeza na tusome

kutokana na Sheria hii ya Gharama za Uchaguzi yaliyojitokeza baadaye na matatizo ambayo tumeyaona na ukakiri, tumefurahi kwamba angalau yote tumeyaona. Sasa na hili lisije likawa hivyo tena, tukaja tukajilaumu, tukarudi tena hapa ndiyo ombi langu na nafikiri Serikali itafakari vizuri hili suala lina mantiki muhimu sana. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka tu labda kurekebisha kwamba pengine watu hawakupiga kura kwa sababu hawana imani na Tume ni vigumu kuamini Tume hii imekuwepo mwaka 1985 na mwaka 2000. Hata mwaka 2005 ambapo watu walijitokeza wengi ilikuwa Tume hii hii. Kwa hiyo, haiwezekani ikawa watu hawaipendi Tume mwaka huu. Kwa suala la ku-*quote* Tume na matatizo yaliyotokea ndio sababu watu hawakwenda kupiga kura, nafikiri si sahihi, tufanye utafiti tugundue tatizo, tulitafutie dawa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa kuzungumza hapa Bungeni na wa maandishi nilipongeza juhudi za Mkoa wa Singida chini ya Dokta Kone, kwa kujenga Hospitali ya Rufaa na jinsi anavyojitahidi kutafuta vifaa, tayari kuna makontena yako Singida alishayaleta na juzi amekwenda Amerika yako mengine kwenye meli yanakuja, lakini hospitali jinsi inavyotengewa pesa kidogo, itajengwa kwa miaka 37. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaiona hospitali hiyo inavyojengwa na Waziri wa TAMISEMI, nikaomba Serikali ione basi juhudi za Mkuu wa Mkoa na wananchi wa Singida angalau tuongezewe hela ili hospitali hii iweze kujengwa angalau kwa miaka michache, wananchi wapunguze gharama za kwenda Muhimbili na *KCMC*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, yaani hapa hapa Ofisi ya Waziri Mkuu ni *juggle for trade,* kwa hiyo, mtaitwa tu, haisemi, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niupongeze uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Singida kwa jinsi ambavyo wamewasiliana na kupata wafadhili wanaosaidia kutoa vifaa vya hospitali na juzi tulimruhusu Mkuu wa Mkoa wa Singida kwenda huko na amerudi na vifaa. Sasa kuhusu fedha kidogo zinazotengwa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo, kwa bahati nzuri wiki mbili zilizopita nilikuwa kule, hospitali ile nimeitembelea, ni hospitali nzuri, nadhani katika hospitali ambazo nimeziona katika nchi hii zilizojengwa na Serikali inawezekana ile inaongoza na wale tumewapa kwa mwaka shilingi bilioni mbili. Kuna Mkoa mwingine wanataka kujenga Hospitali ya Rufaa wamepata shilingi milioni 500 tu. Kwa hiyo, nataka kusema kama ambavyo Waswahili wanasema, wema usizidi uwezo. Tungependa sana Singida tuwape fedha zaidi ya hizo, lakini ninachotaka kusema wanachotaka watu wa Singida ni huduma zianze, tatizo kubwa pale lilipo ni Madaktari, wanahitaji Madaktari Bingwa saba ili majengo yale yaanze kutumika. Hilo tunawasiliana na Wizara ya Afya, Madaktari hao wapatikane ili hospitali ile ianze kufanya kazi na tutaongeza fedha kila mwaka kulingana na uwezo wa Serikali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimechangia katika mchango wangu wa maandishi kuhusiana na changamoto ambazo

zinaikabili hospitali ya *DDH* iliyopo Wilaya ya Bunda. Hospitali ya *DDH*, mbali na matatizo yote yanayoikabili ili iweze kufanikisha kupata vifaa vya kisasa na kutenga chumba kizuri kwa ajili ya hususan wagonjwa mahututi. Lakini zaidi miaka kumi chumba hicho kimefungwa, hakifanyi kazi na kina vifaa vya kisasa lakini pia kuna baadhi ya wagonjwa ambao wanapoteza maisha wakiwa njiani kwa ajili tu ya kupelekwa hospitali ya Bugando, wakati wangeweza kuokoa maisha yao kwa kutumia chumba cha wagonjwa mahututi chenye vifaa vya kisasa kilichopo katika hospitali ya *DDH*, Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilivyokuwa kwenye ziara nilitembelea hospitali ile, kikubwa ni *staff*, hakuna wafanyakazi wa kutosha, hakuna Madaktari ndiyo sababu ya msingi iliyopelekea chumba kile kufungwa na vifaa vyake vya kisasa kutoka kwa Wamarekani. Lakini mbali ya hiyo, mbali na tatizo la maji ambalo wanakabiliwa wananchi wa Bunda, hospitali ya *DDH* ilifanikiwa kupata wafadhili ambao ni Wamarekani, wamewapa shilingi milioni sita kwa ajili ya mradi wa maji ambao unagharimu shilingi milioni 12. Tatizo hapa ni milioni sita tu, ninachohitaji ni *commitment* ya Serikali kati ya mambo hayo mawili.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mbunge kwa jitihada zake za ufuatiliaji wa hiyo hospitali. Lakini kwa kifupi tu hizo hospitali *DDH* ni hospitali ambazo zinamilikiwa kwa pande zote mbili, Serikali na Halmashauri, kupitia Halmashauri na wale wanaomiliki hizo hospitali. Kwa hiyo, tunachofanya Serikali kwa mkataba maalum ambao unasimamiwa na TAMISEMI, wao wanakubaliana na hospitali kwamba ni huduma zipi ambazo watapewa pale baada ya hapo Wizara ndiyo tunatimiza kwa mkataba ule. Kama wamekubaliana Madaktari wa aina gani na vifaa gani ambavyo vinatakiwa vipelekwe pale, ndiyo tunatimiza. Kwa hiyo hili suala tuliliona kwamba hospitali ile inahitaji kupelekewa wafanyakazi na ndani ya mpango huu tunapitisha mwezi wa Nane na mwezi wa Kumi tunategemea kupeleka Madaktari na Manesi ili angalau kuweza kukidhi mahitaji ya watumishi kwenye ile *DDH*.

**MWENYEKITI:** Naona inatosha si wamesema mwezi wa nane.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejibiwa upande mmoja bado katika shilingi milioni sita tu, za kukamilisha mradi wa maji katika hospitali ya *DDH*.

**MWENYEKITI:** Nilivyoelewa ni kwamba, kuna mkataba ambao wanakuwa nao hao watu na Serikali, sasa kama wajibu katika mkataba uko hivyo basi lingekuwa hivyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ninachokiongea nina uhakika nacho, Mheshimiwa Waziri amenijibu suala zima la *contract* inayohusiana na utaratibu wa kupeleka Madaktari lakini hili lingine ni suala la mradi wa maji ambao mbali na matatizo yote, wamejitahidi kupata milioni sita, naomba tu *commitment* ya Serikali hii kuhusu milioni sita nyingine wamalizie ule mradi tuna tatizo kubwa Bunda.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Waziri wa Afya, mahali kwenye hospitali teule ni nguvu za mwenye hospitali na Serikali. Sasa inategemeana mkataba wetu pale nani anashughulika na tatizo la maji, lakini kama ni suala la mchango wa Halmashauri, Baraza la Madiwani wa Bunda, wao tulipoambiwa fedha zenu mwaka huu *OC* matumizi ya kawaida ni haya, kama kweli tatizo ni hiyo milioni sita wao ndiyo walipaswa waseme hapa tatizo la kwanza maji, tutenge milioni sita tumalize tatizo la maji. Sasa leo bajeti imepita ya Wizara na Mikoa ukisema hapa Waziri unataka uwafurahishe hapa watu kwamba nitatoa shilingi milioni sita, wakati haimo kwenye bajeti nitakuwa sitaki kusema uwongo mbele ya Bunge hili. Kwa hiyo, sitaki kusema kwamba, *wasted opportunity*, lakini Baraza la Madiwani la Bunda lilikuwa na fursa ya kusema fedha za mwaka huu zikija kitu cha kwanza maji. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa maandishi nilipenda Serikali inifafanulie nini msimamo wake kuhusiana na suala la *operation* ya kuhamisha ambayo inafanyika *particularly* Mkoa wa Tabora na hasa Wilaya ya Urambo wa mara kwa mara kiasi kwamba mifugo ile inachukua kwenye maeneo ya vijiji ambavyo vimesajiliwa kisheria na tatizo hili linafahamika hapa Bungeni kuanzia mwaka 2008, lilikuwa limezungumziwa kwamba baada ya *task torce* kuundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu waligundua kwamba maeneo ya mifugo yanayochukuliwa ni maeneo ambayo hayajaainishwa, ni maeneo ambayo wananchi wako pale zaidi ya miaka 20, 25, hifadhi haijaainishwa vizuri na ile *task force* ilitoa taarifa kwetu kwamba inabidi Serikali iangalie jinsi gani ya kuweza kama ni kuhamisha basi uandaliwe utaratibu maalum ambao wale wananchi watahamishwa kwenda katika maeneo mengine lakini pia wawekewe miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Urambo imekuwa ni tatizo kwamba wananchi wanabughudhiwa kila siku, wanapigwa na niseme kwamba baadhi ya viongozi wa Wilaya wamewafanya wafugaji ni vitega uchumi vyao. Naomba Serikali iseme hapa Bungeni kwamba inatoa tamko gani kuhusiana na suala *particular* la Wilaya ya Urambo kuhusu mifugo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Sheria ya Hifadhi za Taifa hairuhusu mifugo kufugwa katika maeneo hayo. Lakini sasa hivi tuna Tume ya matumizi bora ya ardhi ambayo sasa hivi imeshapima vijiji 440 katika Mikoa 18 na Wilaya 38 na tumeshapima hekta milioni 2.3 ambapo maeneo hayo sasa hivi yameshatengwa kwa ajili ya wafugaji. Naomba kuishauri Halmashauri ya Urambo ihakikishe kwamba inajenga miundombinu ya mifugo katika maeneo ambayo wafugaji wanapelekwa, wakati Tume hii inaendelea na kazi yake katika Wilaya nyingi Tanzania maeneo hayo ambayo wafugaji wanahamishiwa basi miundombinu iweze kuwekwa. Lakini ni dhahiri kabisa kama nilivyosema awali kwamba maeneo ya hifadhi hayaruhusiwi kuwekewa mifugo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kujua wakati maeneo hayo hayajatengwa na miundombinu haijawekwa na wananchi wafugaji wanaendelea kubughudhiwa kila kukicha, wanapigwa, kunyanyaswa na mifugo yao inauawa. Nini Serikali inasema kuhusiana na wananchi sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba kila Halmashauri itenge maeneo ambayo inaweza kuweka wafugaji hawa ili waweze kukaa vizuri, lakini Halmashauri hiyo hiyo inahusika katika kuandaa miundombinu ya mifugo hususan malambo na mabwawa kwa ajili ya huduma za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi ninachosema ni kwamba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri ili iweze kutenga maeneo hayo kama Tume yetu hii ya kupima maeneo kwa ajili ya matumizi ya mifugo haijafika katika Wilaya ya Urambo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dr. Kebwe!

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niliiuliza Serikali *very specific,* kwamba Hospitali ya Rufaa, Musoma ambayo wananchi walianza kuhangaika kujenga tangu mwaka 1985, sera ya wakati ule ilikuwa hairuhusu Mikoa kuwa na Hospitali za Rufaa sasa hivi Sera ruhusa, sikusema kwamba tunaomba Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Yale majengo ambayo wananchi walishaanza kujenga mwaka 1985, napenda nifahamu hii shilingi milioni 100 ambayo imetengwa ni hela kidogo itafanya kazi gani?

Lakini sambamba na hilo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ambayo imeanza kujengwa, mwaka juzi Serikali ilitenga shilingi milioni 200, sasa hivi kuna jengo zuri linakaribia kumalizika chini ya msaada ya *ADB* katika mpango wa Mikoa mitatu ya Mtwara, Tabora na Mara juu ya kupunguza vifo vya akina Mama kutokana na uzazi. Sasa ile *Theatre* ikishakamilika halafu katika majengo mengine kuna msingi tu na haikutengwa hata senti tano, hivi ule utaratibu wa kuendeleza miradi ambayo tayari ilishaanza ukoje?

Katika sehemu ya pili niliuliza kuhusu barabara ambayo inapita Serengeti kilomita 452. Nashukuru maelezo ya Waziri Mkuu amesema kwamba barabara zile ambazo zitajengwa kupita katika maeneo ya hifadhi hapatajengwa lami. Lakini ningependa nifahamu barabara hii inajengwa au haijengwi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Kebwe nakuomba radhi sana, wewe umezungumzia habari ya Hospitali ya Rufaa, Hospitali ya Wilaya tena na hiyo barabara ya lami ni ya tatu, haiwezekani! Naomba Waziri ajibu!

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Afya!

**MHE. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Dr. Kebwe kwa jitihada zake za dhati kabisa za ufuatiliaji wa hospitali ya Mkoa. Lakini naomba nikiri kwamba, mojawapo ya vitu ambavyo tunavizungumzia mara kwa mara katika Wizara ni jitihada za watu wa Mkoa wa Mara kuanzisha ujenzi wa ile hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii tarehe 25/4/2011 alikwenda Musoma, Mara kuhudhuria siku ya Malaria Duniani na mojawapo ya kazi aliyoifanya ni kutembelea jengo lile na alipata nafasi ya kuongea na Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine wametoka na wazo licha ya mchango peke yake wa Serikali lakini vile vile tutaanza kampeni maalum au harambee kwa kushirikisha watu maarufu pamoja na *Miss Tanzania 2001*, mwanamuziki LadyJaydee angalau wao watupe changamoto tuwapate na wanamuziki wengine wa Marekani waje kuanzisha harambee ya hospitali na wadau wengine tuweze kuianzisha au kuendeleza ujenzi hatimaye Hospitali ikamilike na kufanya kazi, Hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ameniandikia barua kwa *agenda* hiyo hiyo na sasa hivi niko na wafanyakazi wenzangu tunaangalia namna gani nje ya bajeti ndogo ambayo tumeitenga kwa sababu Sungura mwenyewe kama tunavyofahamu ni mdogo lakini tutaweka mojawapo ya mbinu kama nilivyosema ni kuanzisha hiyo harambee angalau tuanze na kuendeleza ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Theatre* mara itakapokamilika Mheshimiwa Dr. Kebwe nakuhakikishia kwamba tutapeleka watumishi ili tuanze kuwahudumia akinamama na Watanzania wengine wenye Mkoa wa Mara.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo natumia kifungu cha 104(1) naongeza nusu saa.

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mbona sijakuita? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dr. Kebwe!

**MHE. DR. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni sawa! Lakini katika harambee ambayo inatarajiwa kwa ajili ya kusaidia kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Musoma. Matarajio na maombi ambayo yamepelekwa Serikalini zilikuwa ni shilingi bilioni 13, je, harambee hii kuna uwezekano wa kukamilisha malengo hayo? Pia katika hospitali ya Halmashauri ya Serengeti pale Mugumu eneo la Kibeo, hiyo *Theatre* ikikamilika na wataalam watakwenda, wataalam siyo tatizo kwani wapo. Tunachouliza ni hivi yale majengo mengine yataendelezwa vipi kwa sababu Serikali haijatenga hata senti tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi tu!

**MHE. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hospitali ni kwamba hatutajenga katika kipindi cha mwaka mmoja, tutakwenda awamu kwa awamu. Kama tutafanikiwa kupata kiasi chochote kwenye harambee hiyo huenda kisitoshe, bado tutaendelea na kuona ni namna gani tutaweza kupata hela za kuweza kumalizia ujenzi wa hospitali hiyo na hiyo tutaiongeza na kuiweka katika bajeti zijazo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Filikunjombe!

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Wakati nachangia kwa niaba ya wananchi wa Ludewa nilizungumzia soko la mahindi. Ununuzi wake pale Ludewa Mjini na Ludewa Vijijini ambayo kimsingi ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais toka mwaka 2008. Nalisema hili kwa sababu sijalisikia katika majibu yake, naomba kupata tamko rasmi na kauli thabiti wananchi wa Ludewa wanaomba ununuzi wa soko ufanyike Ludewa kama walivyomwomba Mheshimiwa Rais na kama alivyokubali ili kupunguza gharama za ununuzi na uchukuzi kwenda Mlangali pamoja na Shaurimoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimezungumzia Liganga pamoja na Mchuchuma. Leo hii Shirika letu la Umeme kwa majonzi makubwa kabisa linagawa giza kwa Watanzania wote badala ya kugawa umeme. Ukimsikiliza Waziri wa Nishati na Madini anakutajia miradi mingi, hazungumzii mradi wa Liganga na Mchuchuma wala hazungumzii umeme wa makaa ya mawe. Naomba kupata kauli thabiti ya Serikali kuhusu mgawo huu wa umeme na giza hili ambalo tunagawana sasa hivi, kwa nini tusitumie makaa ya mawe ya Mchuchuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye suala juu ya soko la Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge tulikutana naye jana na tukazungumzia suala hili la soko la Ludewa na nataka nirudie lile ambalo nilimueleza kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ni maagizo kwetu na kwamba Serikali itachukua hatua ya kuhakikisha kwamba soko hilo lililoahidiwa na Mheshimiwa Rais linajengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa ufafanuzi kuhusu swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe kuhusu hali ya umeme kama ifuatavyo:-

Napenda kutumia nafasi hii kuikumbusha Kamati yako na Watanzania kwa ujumla, kwamba miradi ya Mchuchuma na Liganga pamoja na ule wa Ngaka na Kiwira ambayo yote inatokana na makaa ya mawe. Yote ipo katika mipango yetu ndani ya miaka mtano ijayo. Kwa watakaokumbuka vizuri Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa ambao Bunge lako Tukufu limeupitisha ni mojawapo ya miradi iliyotajwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Liganga tunatarajia kuzalisha *megawatt 600* lakini ratiba ya utekelezaji na ukamilifu wa mradi huo ni mwaka 2015. Mradi wa Ngaka ambao ni megawatt *400* na wenyewe unatarajiwa kukamilika mwaka 2015, lakini mradi wa Kiwira *megawatt 200* tunatarajia kukamilisha mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Filikunjombe!

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa soko lipo, miundombinu ipo, kila kitu kipo tayari, wanachoomba wao ni kauli thabiti na dhamira ya Serikali kununua mahindi pale Ludewa kijijini. Mheshimiwa Waziri anasema atakuja kujenga soko, msije kujenga soko njooni tu mnunue mahindi. Hilo la kwanza.

La pili, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anasema Liganga watazalisha *megawatt 600*, Liganga kuna chuma wala hakuna makaa ya mawe, makaa ya mawe yako Mchuchuma. Kwa hiyo, kwa majibu haya naomba Mheshimiwa Waziri afike atembelee ile miradi ili kusudi anapotoa majibu humu Bungeni atoe majibu thabiti, asitoe majibu ambayo hayana upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri afike Ludewa akisema miaka mitano, hiyo miaka wamekuwa wakiisema kila siku, muda umekwenda sasa tumechoshwa na maneno, tunaomba mtoe kauli thabiti, hili giza mgawo wake utamalizika lini tutumie makaa ya mawe kutoka Mchuchuma? Tunaomba majibu thabiti.

**MWENYEKITI:** Tunaomba Waziri wa Nishati na Madini!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu adha na jinsi ambavyo Mheshimiwa Filikunjombe anaguswa, lakini tutaendelea kujenga nchi hii kwa kutoa taarifa sahihi. Utekelezaji wa miradi hii hauwezi kufanyika kwa namna ya kuelezea kwa kufurahisha umma, miradi hii itatekelezwa kwa taratibu zilizopo na kwa kuzingatia uzito wa miradi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si dhamira ya Serikali hata kidogo kuendelea kutaja miradi ambayo haitekelezeki na rejea yote ya vitabu ambavyo tunavyo tunaposema Mchuchuma-Liganga, Liganga-Mchuchuma tunamaanisha ni *integrated project* yaani ni mradi mmoja upande huzalisha makaa ya mawe lakini upande mwingine kuna chuma na

siku zote makabrasha yetu yanaelezea hivyo. Kwa hiyo, nimpe faraja Mheshimiwa Mbunge, rejea hiyo isimtie hofu kwamba pengine ni miradi miwili tofauti, hapana! Hata mwendelezaji ambaye amepatikana kwa ubia na Serikali kampuni ya *Sichuan Hongda Group* ya China ambayo sasa hivi taratibu zinakamilishwa kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa na tunaamini kwamba utekelezaji utakwenda vizuri. Mpango uliopo ni kutekeleza mradi huo kwa pamoja kama *integrated project. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Uwekezaji na Uwezeshaji!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongeze majibu ya nyongeza kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Liganga na Mchuchuma ni mradi mkubwa sana ambao utekelezaji wake unahitaji mtaji wa dola za Marekani bilioni 4.5 na kwa awamu ya kwanza kwa kuzingatia mahitaji ya umeme nchi hii, tutaanza na mradi wa Mchuchuma na kwa hiyo, ni mchakato hadi itakapofika mwaka 2015 tutakuwa tumepata umeme huu wa *megawatt* 600.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na subira na kwa sababu anausukuma nina hakika na Serikali nayo itahakikisha kwamba mradi unatiwa saini ili utekelezaji uanze mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pamba, ukishasimama mara mbili basi, nawe umesimama mara mbili.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajajibu mgawo wa umeme utakwisha lini!

**MWENYEKITI:** Ya Mahindi mwende mkapeleke magunia tu! Mheshimiwa Waziri wa Kilimo!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kituo cha kununulia mahindi, hilo nilishatoa maagizo kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa kwamba wafungue kituo cha kununua mahindi katika kijiji hicho ambacho Mheshimiwa Mbunge anapendekeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Pamba! Muwe *brief* jamani muwaonee huruma wenzenu wako wengi hapa na sijafika kokote.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali imeanzisha utaratibu mzuri wa kutengeneza barabara chini ya utaratibu wa *performance*

*best management and maintenance of rural roads* na ikamteua Mkandarasi wa *Lake Construction and Y&N* kwa barabara za Pangani Tanga na Muheza Pangani. Mwisho wa mwaka huu utekelezaji wa Mkandarasi huyu ni mbovu, barabara ya Pangani Tanga ni 38%. Barabara ya Muheza Pangani haikutekelezwa wala kutengenezwa kabisa na Mkandarasi amelipwa zaidi ya shilingi milioni 900. Sasa naomba melezo ya Serikali, Mhandisi Mshauri ameshauri *COWI Construction* kwamba Mkandarasi hana uwezo kabisa wa kuweza kuendelea na mradi huu chini ya *PMMR* na hivyo ameshauri kwamba *termination* ifanyike, mkataba ufutwe, atafutwe Mkandarasi mwingine, lakini wenzetu wa *TANROADS* wanaendelea kumrudisha Mkandarasi huyu kwenye *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate maelezo kutoka kwenye Serikali kwamba ni lini watakamilisha *termination* ya Mkandarasi huyu? Taarifa tulizonazo ni kwamba fedha zilizobaki ambazo Mkandarasi huyu hazijalipwa zinatosha kumalizia barabara ya Tanga-Pangani, zinatosha kumalizia barabara ya Muheza–Pangani. Ni lini Mkandarasi mpya atateuliwa ili kuweza kumaliza barabara hizi ambazo ni muhimu kwa wananchi wa Jimbo la Pangani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtolea maelezo Mheshimiwa Saleh Pamba, Mbunge wa Pangani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna mpango wa utengenezaji wa barabara unaoitwa *PMMR* ambao tumeufanya kwa majaribio katika Mikoa mitatu ambayo ni Mkoa wa Rukwa, Mwanza na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kwa nyakati tofauti kumekuwa na malalamiko kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, vilevile Bodi ya Barabara Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Tanga kwamba Mkandarasi aliyepewa mkataba wa kutunza na kuijenga barabara ya Pangani – Muheza – Amani ni *joint venture* ya *YN & Luck Contractors* kwamba kwa kweli hafai kabisa. *(Makofi)*

Baada ya kupata taarifa hiyo mimi nilikwenda Tanga kujionea mwenyewe na nimethibitisha kwamba kwa kweli Mkandarasi huyo si lolote, si chochote na nikatoa maagizo kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kuanzisha mchakato wa kuvunja huo mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari *TANROADS* walishafika Tanga na wakatoa siku 14 kwa Mkandarasi kujirekebisha ambapo nina uhakika hawezi kujirekebisha na hizo siku 14 zimeisha tarehe 28 mwezi uliopita. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nina uhakika sasa hivi mchakato wa kukatisha huu mkataba unaendelea na hatasikia tena kuhusu uchakachuaji katika mkataba huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Waheshimiwa mnarudia tena naomba mngefanya..., Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia suala la mapendekezo ya fedha ambayo imeongezeka katika ushuru wa mafuta ya taa kwenda kwenye *Rural Energy Agency* kwa ajili ya kufidia wananchi maskini ambao gharama zao za mafuta ya taa zimeongezeka kwa kusambaza umeme. Nchi yetu inaagiza takribani lita milioni 200 za mafuta ya taa kwa mwaka na kiwango cha ushuru ambacho kimeongezeka cha shilingi 123/= kama tukizielekeza *Rural Energy Agency* maana yake ni kwamba tutaweza kuwa na takribani shilingi bilioni 246 kwa ajili ya umeme vijijini na tutaweza kufikia malengo yetu ya kuwafikishia umeme 30% ya Watanzania. *(Makofi)*

Wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anajibu hoja hapa suala hili hakulijibu, nilikuwa naomba taarifa ya Serikali kuhusiana na pendekezo hili ambalo naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge wengi sana wanaliunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nilichangia kwa maandishi kuhusu suala la Shirika la Masoko Kariakoo ambapo toka mwaka 2000 Shirika hili halina bodi na kwa hivi sasa linaendeshwa kinyume cha sheria iliyoliunda, Sheria ya mwaka 1974 na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC)* ilipokutana na shirika hili na kuurudisha uongozi ule wa Shirika la Masoko Kariakoo, hatujapata *response* yoyote kutoka Serikalini na mpaka sasa Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI ambaye ni Waziri Mkuu hajaunda bodi ya shirika hili na yeye aliunda timu ya kwenda kufanya uchunguzi na ikagundulika mali nyingi sana za Shirika la Masoko Kariakoo zimeibwa, viwanja vyake vimechukuliwa, nyumba zimeuzwa kwa gharama nafuu na shirika hivi sasa liko hohe hahe, lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote ambayo Serikali imechukua. Nilikuwa naomba kauli ya Serikali juu ya Shirika la Masoko Kariakoo kuendeshwa bila kufuata sheria iliyoliunda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Je, nani atajibu habari ya mafuta? Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa ufafanuzi kuhusu suala la bakaa ya fedha ambayo itapatikana kwa kuongeza *excise duty* kwenye mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya kodi kwenye mafuta ya taa haikufanywa kwa ajili ya kupata *revenue,* lengo lake kubwa lilikuwa ni kuondoa tatizo la uchakachuaji. Fedha zile ziko Serikalini na tutazingatia mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge, iwapo tutayaona kwa pamoja yanasaidia tutayapa *merits*. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali analolizungumzia Mheshimiwa Kabwe Zitto, hili tatizo la kwamba uongozi uliopo pale umepita muda wake ni sahihi na ukiangalia katika majibu

ambayo tumeyatoa anachosema ni sahihi, na *thus why* walikwenda pale kama *POAC* na yeye kama Mwenyekiti walikataa kuzungumza na ile bodi pale kwa sababu kwa kweli kisheria haipaswi kuwepo. Tumelizungumzia jambo hili na tumekubaliana kwamba mchakato huu uanze na haya mengine yote anayoyazungumza sasa hutaweza kufanya jambo lolote mpaka uweze kupata ile bodi ambayo anaizungumzia. Kwa hiyo, tunakubaliana na yeye na sisi hili jambo tunalifahamu na tunalifanyiakazi. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Wananchi wa Ngara wameniomba nishikilie mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka nipate kauli inayotosheleza kuhusu masuala yafuatayo lakini wamenikataza nisilale ndani ya jengo hili kama Mbunge wa Manyoni Mashariki, Mheshimiwa John P. Lwanji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jamani hebu tutumie muda vizuri, kuongelea hayo mambo kunapoteza muda. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Kwanza ni utekelezaji wa ahadi ya Rais aliyoitoa wakati ametembelea Ngara wakati wa kampeni ya kuwapatia wananchi wa Ngara umeme wa jenereta katika miji midogo ya Rulenge, Benako na Rusumo. Pili, ni ahadi ya Rais ya kuwapatia barabara ya lami kutoka Munzani - Kenza – Rulenge mpaka Murugarama ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya kata mbalimbali lakini pia kwa nchi ya Burundi kupitisha mizigo yake kwa urahisi. Tatu ni utekelezaji wa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina ni mara mbili tu basi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mara mbili tu?

**MWENYEKITI:** Eeh!

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Basi ahadi hizo mbili za Rais, umeme na barabara.

**MWENYEKITI:** Basi ahsante. Haya anayehusika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. *(Kicheko/ Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kutoa ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ahadi ya Rais ilitolewa na mimi nilikuwepo, tunafahamu kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais zinatekelezwa ndani ya miaka mitano lakini ninataka nimpe faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya ya Ngara na Biharamulo ambazo zinahusisha pia Wilaya ya Chato pamoja na Wilaya ya Mpanda, zote sasa hivi tunaendelea na mchakato wa ununuzi wa majenereta wakati juhudi za kuiunganisha Mikoa ya Kagera, Kigoma pamoja na Rukwa kwenye Gridi ya Taifa

zinaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tuliongea nje ya Bunge hili ule utaratibu unaendelea na tutazidi kukupa taarifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira itakapokuja Bajeti ya Wizara ya Ujenzi atafurahi sana. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka tu nipate ufafanuzi wa ombi langu. Wakati nilipokuwa nachangia niliomba nipate ufafanuzi kuhusu ile shule ambayo ilikuwa Kipawa wakati wananchi wa Kipawa wanahamishiwa katika Jimbo la Ukonga, fedha zake zimetoka na mpaka sasa hivi hazijapatikana na kwa sababu tuna eneo la kujenga shule hiyo tunaomba Waziri Mkuu alitolee ufafanuzi ili tuweze kupata fedha hizo na kuanza kujenga shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la pili ni ombi langu ambalo nililiomba linalohusu wananchi zaidi ya 800 wanaoishi Bangulo ambao walipelekwa pale wakati wa *operation* ya vijiji kwa hiyo, nilimuomba Waziri Mkuu kwamba aangalie ni namna gani wananchi hao wanaweza kuendelea kubakia pale kwa sababu wametakiwa na Wizara ya Kilimo na Uvuvi waweze kuondoka pale, kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi wa hayo mambo mawili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujibia kuhusu suala la Shule ya Msingi Kipawa ambayo imelazimika kuhama kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametuthibitishia kwamba fedha za fidia zimetoka, ametuthibitishia kiwanja mahali ambapo…

**MWENYEKITI**: Kuna mtu hajazima mashine, zimeni *microphones* zenu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amethibitisha kwamba fedha za fidia zimetoka, mahali pa kuhamishia shule ile ya msingi kiwanja kipo, nataka nimuahidi kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, tutafuatilia kama fedha zimetoka kuhakikisha kwamba shule inajengwa mapema ili watoto wapate mahali pa kusoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu watu 800 inakuwaje? Eeh Mheshimiwa Waziri wa Mifugo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa kuhusu eneo la Bangulu ambalo ni sehemu ya Mnada wa Pugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili wananchi wamejenga kinyume cha sheria na wamejenga makazi ya kudumu, kwa hiyo, tuliwajulisha kwamba wanatakiwa kuhama na ni kweli wanatakiwa waondoke katika eneo hili kwa sababu wamevunja sheria ya matumizi ya ardhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda wa *guillotine* umefika, napenda tufanye maamuzi kwa sababu hii Wizara ni kubwa, tufanye maamuzi tuongeze muda kwa kutengua kifungu kingine. Kwa hiyo, Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, hoja.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kifungu cha 150(1) kutokana na mjadala huu kuhusisha Serikali nzima na jinsi inavyoendelea, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 104(2) ili kuongeza muda mwingine usiozidi saa moja na pia kutengua Kanuni ya 101 inayotaka uzungumzaji wa humu ndani uwe ni dakika tano ili kila mmoja apate nafasi ya kuzungumza dakika tatu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki! *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu mliojiandikisha pale mko 26 tukienda kwa dakika tano tunahitaji saa mbili na zaidi, kwa hiyo dakika tatu tunaweza kuchukua saa moja hii tunayoomba. Lakini wakati huo huo kumbukeni tuna Kitabu cha Maendeleo, mimi nisingependa kabisa tufanye *guillotine* katika eneo lile inakuwa ni kama vile tuna *bulldoze*, kwa hiyo ndiyo msingi wa hoja hii. Kwa hiyo, nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki utekelezwaji wa Hoja iliyotolewa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kuanzia sasa tutaongeza saa moja baada ya saa mbili na robo usiku na sasa tutakuwa tunachangia dakika tatu kwa hiyo, mji-*tune* uwe na swali moja ili uweze kujibiwa vizuri. *(Makofi)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, lakini baada ya saa moja hiyo tena kama hamjamaliza itakuwa ni *guillotine*. Haya tunaendelea na Mheshimiwa Martha Mlata. *(Kicheko)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi pia wakati nachangia kwa maandishi.

**MWENYEKITI:** Dakika tatu, wewe endelea tu.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo! Wakati nachangia kwa maandishi nilikuwa nimeomba kujua hatma ya kesi za mirathi kwa sababu hata juzi niliuliza hatma ya kesi za mirathi kwa sababu wanawake wamekuwa wakipata shida sana pale wanapokwenda Mahakamani na Serikali haikuweza kutoa majibu ya kuridhisha, lakini hata leo sikupata jibu lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashindwa kuelewa ni kwa nini jambo hili Serikali haitilii mkazo na ni jambo ambalo limekuwa ni kero kubwa, nikaomba basi hata pale mahakamani awekwe Mwanasheria kama ilivyo kwa kesi zile za mauaji ambazo huwa kunakuwa na Mwanasheria pale, awekwe Mwanasheria kwa ajili ya kuwatetea wale wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema kwamba inatumia Sheria ya India wakasema kwamba kuna ya Kiislam na ya mila lakini ninavyojua zile za Kimila zinaisha papo kwa papo, hata za Kiislam zinaisha vizuri, lakini zile ambazo zinakuwa zinakwenda mahakamani haziishi, zinakaa zaidi ya miaka hata mitano. Ninaomba ufafanuzi wanawake hawa wajane wanaolia na watoto wao Serikali mnasema nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki, maana juzi walikuendesha na bado wanaendelea. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka nifafanue suala hili muhimu alilouliza Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si jepesi kama anavyoliweka. Kama tulivyojibu katika swali la msingi siku ile, matatizo ya mirathi yanahusu vitu vingi sana; mahusiano, upana wa ukoo, ushahidi uliopo, maisha yaliyokuwapo baina ya mume na mke kabla mume hajafa, walitendeana nini? Je, kulikuwa na wosia ama hakuna? Halafu na mila na desturi.

Kwa hiyo, kuna yale ambayo yanakwisha upesi kwa sababu labda kuna wosia, kuna yale ambayo yanakwisha upesi kwa sababu wahusika waliishi maisha mazuri na walikubaliana, lakini kuna mengine yanakawia kwa sababu pande zote mbili ni wabishi. Sasa Serikali kwa mujibu wa Katiba yetu haiwezi kuingia katika eneo la Mahakama na kuweka utaratibu wa Kiserikali ndani ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaliona hili tatizo tutaendelea kushauriana na Mahakama ili tuweze kuona njia gani zitatusaidia kuweza kulipunguza. Wapo wenzetu wa Tume ya Kurekebisha Sheria wametoa mapendekezo fulani fulani, yote haya tunayafanyiakazi ili kuzidi kupunguza tatizo hili. Serikali inawahurumia sana wajane na watoto na ndiyo maana humu tunapitisha Sheria nyingi ambazo zinajaribu kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mambo ambayo hatuwezi Kikatiba tukayawekea utaratibu ndani ya muhimili mwingine, hayo yatakuwa ni kuvunja Katiba. Ninaomba tu Mheshimiwa Martha Mlata na mwenzie pia aliuliza Mheshimiwa Naomi Kaihula kwamba kama kuna matatizo maalum tuwe tunakaa pamoja maana yake wakati huu kwanza tunabanwa na wakati, tukae pamoja kama kuna tatizo mahususi tunaweza kusaidiana na Mahakama tatizo hilo mahususi linakwisha, vinginevyo hapa inakuwa kama mafumbo sasa kwamba, watu fulani wanapata taabu, tuletewe hapa tuwajue, hii ni Serikali sikivu, inajali watu wake tutachukua hatua haraka sana kwa kusaidiana na Mahakama kuondoa doa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ambao wana kesi zao Mahakamani kwa majibu haya hawatalala, kwa sababu ukisema kwamba kuna mambo ya mafumbo na kama kuna kesi mahususi, si kweli.

Mimi nimesimama kwa niaba ya wale wanawake wanaoteseka. Tunapofanya ziara kule mikoani na kwenye maeneo yetu ndiyo vilio tunavyovikuta. Mimi siwezi kuwaleta hapa, labda nipige mbiu ya  maandamano wafike wote kwa sababu siwezi kumjua mwanamke mmoja mmoja. Kwa hiyo, naomba Serikali iseme kama haiwezi kuingia Mahakamani je, si kuna sheria na kama haitoshi kwa nini isiletwe hapa tubadilishe ili kuwasaidia hawa wanawake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ningefikiri ungepokea yote mawili.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunazunguka hapo hapo, haitusaidii sana. *(Makofi)*

Kinachosemwa hapa ni kwamba mambo ya mirathi si jambo rahisi kama ambavyo tunajaribu kuliweka kwamba unaweza kutoa hata sasa hivi tukamwomba Waziri Mkuu akatoa tamko hapa kesho kesi zote za mirathi zikafunguka na mambo yakaisha. Mradi yako Mahakamani, yanadai ushahidi, yanadai mabishano kuhusu huyu anayesema anasimamia mirathi ni halisi na tunazo rufaa nyingi kuanzia Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, *Residents Magistrates*, Mahakama Kuu hadi Mahakama ya Rufaa na utaratibu huo unapokuwa hivyo hakuna namna ya Serikali kuingilia kati na kusema hili suala limechelewa sana basi muamue namna fulani.

Ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge, sisi sote tuna uchungu na Mtanzania yeyote anayeumia katika hali hii.  Ndiyo maana tunasema kama yapo matatizo mahsusi

na sio ya kijumla basi kwa kushirikiana na wenzetu mikoani kama vile Wakuu wa Mikoa yafikishwe Serikalini kama tatizo maalum inawezekana haki inapindishwa mathalani basi kama ni hivyo, Serikali ina wajibu pale wa kuliingilia kwa sababu tunaweza kuzungumza na wenzetu Mahakama ili mambo yaende na yatoe ahueni kwa wenzetu. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kupata ufafanuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege Songwe Mbeya umekuwa unajengwa takribani kwa miaka kumi sasa. Wakati huo Serikali imekuwa inazungumza kufungua Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya maendeleo ya mkoa wa Mbeya, lakini pia Nyanda za Juu Kusini na maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matamko mbalimbali ya Serikali kuanzia mwaka 2002 wakati uwanja huo unaanza kujengwa, mimi nimekuwa Mbunge nimekuta unajengwa, nimekuwa kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu katika Bunge la Tisa tumekwenda uwanjani pale karibu mara tatu tukaahidiwa kwamba ungeweza kwisha katika kipindi cha miaka mitatu haukwisha. Juzi Serikali limekuja na tamko hapa Bungeni kwamba uwanja huu utafunguliwa mwezi wa Desemba, 2011. Lakini bado kumekuwa na mabishano kati ya Serikali na mjenzi, mjenzi anasema nipeni muda mpaka mwezi Aprili, 2012 lakini Serikali inasema Desemba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tamko mahsusi la Serikali ni lini uwanja wa ndege Songwe Mbeya unafunguliwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kumthibitishia yale ambayo tumeyatamka Bungeni Desemba, 2011 uwanja utakamilika, Mheshimiwa Waziri alikuwa juzi kule na ameongea na mkandarasi na tumempa *ultimatum* Desemba uwanja ufunguliwe. Nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliomba tamko la Serikali kuhusiana na fidia ya wananchi wa Kata ya Kwembe ambao wanapaswa kuhamishwa kupisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Muhimbili majengo ya *MUHAS* suala ambalo linahusisha wananchi wa Mitaa ya Mloganzila, King’azi, Kisokwa pamoja na Kwembe takribani wananchi 2,300 na linahusisha eneo la takribani ekari 3,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kauli ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu jambo hili ni la muda mrefu kutoka mwaka 2004 na ilishafika kwenye meza ya Waziri Mkuu na mwezi Aprili, 2010 Waziri Mkuu akatoa maelekezo kwa Wizara zinazohusika, Wizara ya Ardhi ilikaa na wahusika mwezi Novemba, 2010 na ikaahidi pamoja na wale 1,919 waliolipwa fidia ya mimea watalipwa vile vile fidia ya ardhi, lakini mpaka sasa taratibu za fidia hazijakamilika. Ningeomba kauli ya Serikali wananchi hawa 1,919 taratibu zote za fidia na wale 402 na wale 8 zitakamilika lini?

Lakini la pili, kwenye mchango wangu wa maandishi niliomba vilevile kauli ya Serikali kuhusu mambo ambayo yanalikumba Taifa na hasa suala la mgao wa umeme. Pamoja na maelezo ya Waziri bado ningeomba kauli thabiti ya Serikali kwa sababu maelezo yote yaliyoelezwa ni ya mipango ya muda mrefu, lakini mgao uliopo sasa ni wa sasa, kwa hiyo, ningeomba kauli kuhusu hatua za dharura. Naelewa kwamba mgao uliopo hivi sasa umesababishwa vilevile na udhaifu wa kiutendaji wa kutoagiza mafuta kwa wakati na kufanya mitambo ya *IPTL* izalishe chini ya kiwango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa vilevile kwamba mgao wa sasa umesababishwa na udhaifu mwingine wa kiutendaji ambao ni vizuri Ofisi ya Waziri Mkuu ikaitolea kauli kwa sababu mwaka wa fedha uliopita Waziri Mkuu aliahidi Bungeni kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha kungekamilika ujenzi wa megawati 100 Ubungo na megawati 60 Mwanza, mradi ambao haujakamilika mpaka sasa, kwa hiyo, tungeomba kauli ya Serikali kuhusu hatua za dharura za kuondoa mgao kipindi cha sasa wakati ambapo suluhisho la kudumu linasubiriwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kutoa ufafanuzi wa madai ya wananchi wa Mloganzila juu ya maeneo tunakotaka kujenga Chuo cha *MUHAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Serikali tayari ilishalipa shilingi bilioni nane kufidia wananchi wa maeneo yale. Lakini kama tunavyotambua kwamba wananchi mara kwa mara wanakuja leo na kauli hii wamelipwa na wengine wanasema hatujalipwa na mpaka juzi tulikuwa tunafanya vikao kwamba bado wameleta tathmini kwamba wanadai Serikali shilingi bilioni tatu na tulichoamua sasa suala hili tumelipeleka kwa wataalamu wa ardhi waweze kutupa tathmini halisi, watuletee tuweze kuona namna gani ya kufanya kwa hiyo, liko linashughulikiwa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu swali lililoulizwa na Mheshimiwa John Mnyika, suala la mgao wa umeme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mwanzoni mwa mwaka huu tulitoa taarifa ya hali halisi ilivyokuwa inakwenda hasa baada ya kuona mvua zilizokuwa zinanyesha zisingeweza kulijaza bwawa letu la Mtera ambao ni bwawa mhimili. Tulisema mipango ya dharura itakayokuwepo pamoja na miradi iliyopo lazima tuwe na mitambo ya kukodi. Tulitoa taarifa hapa Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba tuliwaelekeza *TANESCO* wasimamie zoezi la kupata mitambo ya kukodi kutokana na *forecast* au maoteo ambayo walikuwa wameotea kwamba kwa kipindi kati ya mwanzoni mwa Juni mpaka mwezi Desemba tungekuwa na upungufu wa kiasi kati ya megawati 200 mpaka 264.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hilo tuliwapa Serikali ilikubali kusaidiana nao na ninapoongea hapa ni kwamba *TANESCO* wamekwishakamilisha zoezi la utaratibu wa

kupata mitambo ya kuzalisha megawati 212.5 kwamba mitambo ya *SYMBION* tayari inazalisha sasa hivi kiwango cha megawati 80, lakini lengo ni kufikia megawati 112.5.

Pia wamepata mkandarasi mwingine Kampuni ya *AGGRECO* ambayo tayari wameshatiliana nao mkataba saini ili kufikia mwezi Agosti iwe imeshaanza kuzalisha megawati 100. Tuna hakika tukishapata hizo megawati 212.5 pamoja na kupata mafuta ya kuendesha mitambo ya *IPTL* na niseme tu kwamba mgao ambao ulionekana umekuwa mkali sana wiki moja na nusu iliyopita ulisababishwa kweli upungufu wa mafuta. Lakini tunavyoongea hivi tayari Wizara ya Fedha ilishatoa pesa na mafuta yako Dar es Salaam tayari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, uongezaji wa uzalishaji wa umeme kutokana na mitambo ya *IPTL* toka ilivyokuwa megawati 10 itakapofikia 100 mitambo ya *SYMBION* pamoja na *AGGRECO* itatusaidia sana kutupunguzia adha ya mgao uliopo sasa. Lakini kuna mradi ambao Mheshimiwa Mnyika ameusema, mradi ambao tumesema utaendeshwa kwa gesi asili Dar es Salaam mradi huu sasa hivi baadhi ya mitambo yake imeshafika Dar es Salaam bandarini na inatarajiwa kwamba mwezi Desemba mtambo utakuwa umeshakamilika. Lakini nilisema tena kwamba na Mheshimiwa Mnyika ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Nishati na Madini tumesema kwamba ule mtambo wa Mwanza megawati 60 kwa taratibu zilizopo mchakato ulivyoendelea utakuwa tayari mwanzoni mwa mwaka 2012. Hizo ni hatua za dharura ambazo Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* imezichukua kukabiliana na hii hali ya mgao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaomba sana Watanzania, wako watu wanasema ni kwa nini sisi tumejielekeza katika umeme unaotegemea maji tu. Tunapotazama suala la mgao leo pia tuiangalie historia, Taifa letu sio kwa makusudi wala kwa bahati mbaya ilijielekeza kwenye miradi ya kuzalisha umeme kutokana na maji kama yalivyo Mataifa mengi duniani, lakini mabadiliko ya tabia nchi hivi karibuni yamekuwa ni changamoto dunia nzima ndiyo maana leo tunavyoongea rafiki zetu wa Japan wao kama sisi, sisi tukitegemea umeme unatokana na maji kwa asilimia 55 Wajapan walikuwa wamejielekeza kwenye umeme wa nyuklia na ni Taifa kubwa, lakini baada ya kupata hili tatizo la tetemeko la ardhi limeathiri uwezo wao wa kuzalisha umeme na sasa wana mgao wa miaka miwili. *(Makofi)*

Ninachosema hoja ya kusema kwa nini hatukutumia vyanzo vyetu vilivyopo ili kuwa na *generation mix* ni masuala ya kupanga na kuchagua. Leo Serikali imejielekeza katika kuwekeza kwenye eneo la nishati ikiwa ni kipaumbele cha kwanza katika mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano ijayo. Maana yake ni kwamba tumefikia mahali ambapo sasa miaka ijayo jambo la mgao wa umeme litakuwa historia. Nilitaka niliweke sawa, niwaombe Watanzania waelewe hatuko sisi peke yetu tunaoathirika kama Taifa, yapo Mataifa mengi ambayo yanaathirika kwa utaratibu wa kupanga na kujielekeza katika mojawapo ya vyanzo vya kuzalisha nishati ya umeme. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa jamani eeh tunaendelea, Mheshimiwa Mnyika utaongeza nini ndio hivyo hivyo tu. Nitawaita wote, mtaitwa naomba kila mtu avute subira.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Mpongeze, unapoteza muda tu. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Amefanya kazi nzuri sana. Pia nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia kwa maandishi na kama nimechangia kwa maandishi pamoja na mambo mengi ambayo nimeyachangia mojawapo kubwa linalosumbua katika Wilaya yangu Korogwe Vijijini ni njaa. Nina Kata pale zaidi ya kumi zimeingia njaa, naomba tu Serikali kwanza iangalie hilo, ili nipate chakula cha dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, baniani mbaya kiatu chake kizuri. Nimeona mambo mengi yamepangiwa Bajeti hapa, lakini waganga wa tiba asili na tiba mbadala sijaona Bajeti yao. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa tiba asilia zinapendwa tu iwapo Serikali imeshindwa kutibia watu, naomba waganga wa tiba asili, tiba mbadala pamoja na wakunga Serikali itamke leo kwamba nao wametengewa Bajeti gani ili na wao wawe na nguvu. Kwa sababu wanasaidia mambo mengi sana Tanzania.

**MWENYEKITI:** Haya tuanze na tiba ya asili. Jamani naomba muongee kwa kifupi Waheshimiwa Mawaziri tutawapigia kengele pia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mujibu wa Sheria namba 23 ya mwaka 2002 ambayo imeelekeza pamoja na kanuni zake namna gani tutaweza kusimamia shughuli hizi za tiba asili, kwa hiyo, hii ipo ndani ya Katiba yetu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge maelezo yake ya ndani ni kiasi gani ambacho tumekitenga tuonane hiyo tarehe 13 na 14 Julai, 2011 tutakapowasilisha Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umesema Katiba au Mpango wa miaka mitano?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Ipo kwenye Sheria.

**MWENYEKITI:** Sheria ipi?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Sheria Namba 23 ya mwaka 2002, Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katiba tulianza kufikiria haraka tukashindwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE);** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutakwenda kufanya tathmini na bahati nzuri

*RAS* wa Tanga yupo hapa, wataenda kufanya tathmini atatuletea hali halisi halafu tutashughulikia. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kwenye jimbo juzi nina Kata ya Kizara, Magoma, Kerenge, Mkumbara, Mazinde na Mkaramo, Mkomazi, Mombo, Mswaa mahindi hamna hata sasa hivi akienda kuchoma majani tathmini gani inatakiwa wakati wananchi wangu wanalala na njaa, naomba nipewe jibu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Na Mkuu wa Mkoa shahidi, haya naomba Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Sasa rafiki yangu Mheshimiwa Ngoyani anataka tumpe mahindi kiasi gani? Maana hata yeye sidhani anajua, maana anachotaka kufanya ni hicho hicho, tutakuletea mahindi lakini lazima tujue ni kiasi gani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji Lindi. Mkoa wa Lindi una matatizo ya maji katika Wilaya zake zote Wilaya za Lindi Mjini, Nachingwea, Ruangwa, Liwale na Mchinga. Pamoja na jitihada za Serikali za kuleta miradi ya *World Bank, GTZ,* Mbwinji na *JICA. Quick wins* kuvuna maji ya mvua lakini maji ni tatizo katika mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Lindi Mjini kulikuwa na vyanzo vya maji vya Mmongo, Mmbanja na Liwayawaya. Vyanzo hivi vilikuwa tu kwa ajili ya wakata mkonge, sasa hivi vyanzo vile havitoshi kwa wananchi wengi wa Mji wa Lindi. Serikali inatuahidi nini kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu kama ifuatavyo; kwa mji wa Lindi tuna mradi mkubwa sana ambao unaendelea sasa hivi na huko chini ya ufadhili wa *EU* ndani ya *SP Water facility*.

Kwa hiyo, nina uhakika kabisa baada ya muda si mrefu matatizo ya maji, tunaangalia kwa muda mrefu mpaka mwaka 2025. Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua pamoja na mradi ambao unaendelea wa Vijiji kumi kuhakikisha katika mkoa mzima wa Lindi tatizo la maji linashughulikiwa.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali imeandaa mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta ya kilimo nchini kuhakikisha kwamba imekuwa kwa kiasi kikubwa na kwa kuwa kipindi kilichopita wananchi walio wengi walikuwa wana hamu kubwa ya kupata mikopo ya kuendeleza kilimo na hawakubahatika na mikopo hiyo. Lakini sasa hivi Serikali ina mikakati ya kuanzisha Benki ya Wakulima, lakini mchakato bado haujakamilika.

Nilikuwa napenda kuishauri Serikali je, katika fedha ambazo zimepangwa kupitia dirisha la mikopo ya kuwapatia wakulima mikopo wale wakubwa na wadogo, Serikali inasemaje kuhusu suala la kuongeza fedha hizi shilingi bilioni mbili yaani kuziongeza zaidi ili kuwapatia mikopo zaidi wakulima wakubwa na wadogo kwa mantiki ya kuendeleza kilimo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mikopo hiyo iwahusishe na wale wavuvi pamoja na wafugaji na kuangalia utaratibu mzima wa kupunguza kiwango cha riba ambacho kimekuwa kwa kiwango kikubwa. Nilikuwa naiuliza Serikali inasemaje kwa hilo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Fedha ana-*wind up* Bajeti yake hapa alieleza kwamba Benki ya Kilimo iko kwenye mchakato na hatua nzuri ya kuanzishwa na katika taarifa ya Gavana wa Benki Kuu walikadiria muda kwamba ifikapo mwezi Novemba hii Benki itakuwa imefungua milango yake, aidha, Serikali imeweka fedha katika Bajeti hii kwenye lile dirisha la *TIB* la kilimo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kama anahitaji mkopo huo au wale ambao wanahitaji mkopo washauriane na *TIB* na mkopo huo nadhani utapatikana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala langu litahusiana na elimu ya juu na hususan suala la migomo hasa ukizingatia kwamba limekuwa likizungumzwa sana katika hii hotuba na hasa ikizingatiwa sana imekuwa ikienezwa kama *propaganda* kwamba kuna wanasiasa fulani wanaenda hususan kwenye Chuo cha *UDOM* kwa ajili ya kutaka kuwahamasisha wanafunzi kufanya migomo wakati ikijulikana wazi kwamba hata viongozi kadhaa wa CCM wanakwenda kwa shughuli hizi hizi za siasa. *(Makofi)*

Sasa mimi ninataka Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie kwa sababu moja kubwa. Baada ya migomo ya wafanyakazi, Waziri Mkuu alifanya ziara *UDOM* akakutana na wafanyakazi na wafanyakazi wakamuelezea Waziri Mkuu chanzo cha migomo ni nini. Moja ya chanzo ambacho aliambiwa na ambacho alikiri kwamba atakifanyia kazi ni cha kuweza kushusha mamlaka kwa *Colleges* hasa ukizingatia chuo ni kikubwa sana na wale viongozi pale juu hawawezi kuhudumia zile *colleges* tano *effectively,* matokeo yake kunakuwa na urasimu, maamuzi hayafanyiki kwa wakati na

hivyo mahitaji ya wanafunzi na mahitaji ya wafanyakazi hayafiki kwa wakati. Waziri Mkuu, uliahidi kushughulikia hilo.

Sasa mimi naomba unipe maelezo kwa sababu inasemekana hakuna *decentralization* yoyote iliyofanyika. Una kauli gani kuhusiana na hilo hasa ukizingatia wale wafanyakazi ambao walijaribu kuwa wazi baada ya kuona kiongozi wa Kitaifa amekuja sasa hivi wanatishiwa mustakabali wa ajira zao? Sasa naomba kauli ya Serikali kuhusiana na *UDOM. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni kuhusiana na madai ya walimu. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anaonesha kwamba madai yamelipwa mwisho mwaka 2008. Sasa nataka kujua hasa ukizingatia kwamba michango yetu imetaka kutuonesha kwamba tuna mapenzi sana na hawa watu wa daraja la chini, walimu, polisi na kadhalika. Katika mwaka huu wa fedha madeni ya walimu yamezingatiwa ama hayajazingatiwa kabisa ama hayapo kabisa kwa mantiki ya kwamba mlishawalipa yote. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kutoa ufafanuzi juu ya suala la Sheria ya Vyuo Vikuu lakini hasa Mheshimiwa Halima Mdee anasisitiza lile tamko la Waziri Mkuu namna ya kushusha madaraka kwenye zile *colleges*. Nadhani tamko likishatolewa haliwezi kufanyiwa kazi kwa wakati mmoja pale pale. Kunakuwa na utaratibu mwingi ambao ndani yake kuna sheria mbalimbali lazima zihusishwe. Kwa hiyo, kama kweli Waziri Mkuu alitamka basi tusubiri utaratibu unaendelea kufanyiwa kazi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** La pili, madai ya walimu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madeni ya walimu kama ambavyo tumeeleza kwenye majibu mbalimbali ya msingi ni kwamba Serikali ilifanya tathimini ya uhakiki wa madeni ya walimu wote nchini. Baada ya kufanya tathimini Serikali kufikia mwaka 2008 ilishalipa madeni yote yaliyohakikiwa na tukatoa maelekezo kwa Wakurugenzi kutozalisha madeni mengine kwa walimu na watumishi wengine na madeni yote yanayojitokeza sasa yanakuwa yamesharatibiwa na wakurugenzi kupitia fedha ambazo Serikali inatuma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kweli zoezi la ulipaji wa madeni kwenye maeneo ya masomo likizo, posho mbalimbali yanalipwa na Halmashauri zenyewe kutegemea na mipango ambayo Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri imeziweka kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mgongo kilichoko Tarafa ya Shelui kina huduma zaidi ya Kata tano na hakina umeme. Katika ahadi ya Rais pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Waziri wakati anajibu alitoa ahadi kwamba kitapatiwa umeme. Sasa naomba atoe tamko kwamba katika mwaka huu wa fedha ulioanza leo, je, kitapata umeme?

Lakini la pili, wananchi wa vijiji vya Ujungu, Msai na Mtoa pamoja na Kata nzima ya Mtoa kufika kwenye Kituo cha Afya cha Mgongo bado wanawabeba wajawazito kwenye vitanda punde mvua inaponyesha? Je, Serikali itakuwa tayari ijionee na kuchukua hatua ili kuokoa maisha ya akinamama hawa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali hili linalohusu huduma ya usafiri kwenye Kituo cha Afya pale akinamama wanapopata rufaa. Katika maelezo yetu, moja ya vitu ambavyo tunavilenga ni kuboresha mfumo wetu wa rufaa pamoja na usafiri. Ndiyo maana tume-*introduce* pikipiki za matairi matatu ambayo ni rahisi kwa bei na rahisi kwa uendeshaji wake ambapo tumetoa changamoto kwa Halmashauri zote, tumeanza na pikipiki 420 ambazo tutazisambaza na tayari baadhi ya Mikoa na Halmashauri zimeshaanza kupata.

Kwa hiyo, changamoto ambayo tumetoa kwa Halmashauri kwamba pole pole wawe wana Bajeti. Hizi pikipiki thamani yake ni dola 8,000 mpaka 9,000 kama watakuwa wanaweka kidogo kidogo ndani ya miaka mitano hadi sita watakuwa wameziwezesha karibu Kata zote kupata hizi pikipiki. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, la pili nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anisaidie.

**MWENYEKITI:** Naomba mjibu kwa kifupi kwa sababu kwenye hotuba zenu mtajibu tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mwigulu kuhusu umeme kwenye Kituo cha Mgongo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ombi la fedha kuhusu kufikisha umeme katika eneo hilo tayari tumeshaliwasilisha kwa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* na namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadri tutakavyopata fedha haraka na kwa kadri ambavyo Bunge lako litatuongezea uwezo wa kuwa na fedha zaidi ndivyo tutakavyotekeleza miradi hii mapema. *(Makofi)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia nilitaka kujua suluhu ya ujenzi wa daraja la Igumbilo katika Jimbo la Iringa Mjini. Kwa kuwa daraja hili uwezo wa kujengwa na Halmashauri ni mdogo na tayari kuna maafa yalishatokea na watoto watatu kupoteza maisha na upembuzi yakinifu ulionyesha kwamba daraja lile linahitaji kama bilioni 1.09 na nilikuwa nimeomba kwamba kama fedha hizi zitachukua muda mrefu sana ningepatiwa kivuko cha dharura kutoka kwa Waziri wa Ulinzi. Naomba ufafanuzi wananchi waelewe kwamba itakuwaje?

**MWENYEKITI:** Kutoka kwa Waziri wa Ulinzi? Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

Ombi hili limekuja, ni kweli lakini majibu yangu yalikuwa ni kwamba hizi *Bailey Bridge* zenyewe zinagharama zake na hivi sasa tunavyozungumza Jeshi lenyewe halina madaraja haya. Wanalo daraja moja tu ambalo si rahisi kulitoa kwa sababu ndiyo inapotokea dharura ya barabara kubwa watashindwa kabisa kuchukua hatua kwa maana hiyo ninachoomba Halmashauri ziangalie uwezekano wa kununua hizi *Bailey Bridge* halafu wataalam wa jeshi watatumika kuwasaidia kuzifunga, kwa sababu gharama zake ni nafuu ukilinganisha na madaraja ya kawaida. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipochangia jana sikuwa nimeunga hoja mkono, lakini baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu maeneo ya uanzishwaji wa Wilaya nimeridhika kwamba Manyoni maombi yake yanashughulikiwa na kwamba mwakani uamuzi utatolewa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja na sitalala hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naomba utupe muda kama umeshaunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba ufafanuzi mdogo tu. Kuna ahadi mbili sasa kwa sababu mwaka jana kabla hatujavunja Bunge niliahidiwa kuanzishwa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Itigi na ikawa *confirmed* tena mwaka huu wakati tumekuja hapa. Sasa nimepewa ahadi nyingine kwamba Wilaya ya Manyoni itagawanywa ili tupate Wilaya ya Itigi sasa hizi zinafuatana au vipi? Ninaomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nitoe maelezo kwa Mheshimiwa Lwanji kama ifuatavyo:-

Katika haya mawili jambo ambalo tutalishughulikia haraka sana ni uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo, lakini pia nataka nimhakikishie kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo inakuwepo ndani ya eneo la Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, watakapokuwa wamekidhi haja ya kuanzishwa kwa Mji Mdogo hauzuwii mchakato mwingine wa kuomba Wilaya kuendelea kushughulikiwa. Kwa hiyo, yote mawili haya yatakwenda pamoja. Lile litakalo kuwa la mwanzo kufuzu tutamjulisha. Nataka nimuahidi kwamba kwa sababu kalizungumza sana suala la maeneo haya Ofisini kwangu, tutapanga mapema iwezekanavyo kwenda ku-*figure* katika Jimbo lake tukakae nae tujue ni vigezo gani vinakidhi na vipi havikidhi na ikibidi tuzungumze na wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, kila mtu aulize swali moja kwa sababu tumebakiwa na dakika kumi tu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nilikuwa nimedhamiria kutangaza mgogoro na Serikali kuhusu barabara ya Sengerema – Nyamazugo –Nyehunge mpaka Zera Geita. Sikusikia kauli ya Serikali naomba tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimwombe Mheshimiwa Dkt. Tizeba kwamba suala la barabara yake ya Sengerema alisubirie mpaka litakapokuja kwenye Bajeti ya Wizara ya Ujenzi tutalijadili kwa kirefu zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimechangia humu Bungeni kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nikauliza Manispaa za Jiji la Mwanza baada ya kuona katika hotuba hiyo imo Lindi tu. Je, Mwanza baada ya Lindi ndiyo itafuata na ni lini? Naomba maelezo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mapendekezo ya kuanzisha mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara tulipendekeza tuwe na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, sio tulipendekeza; tulisema kwamba vikao vyote halali vya Mwanza kwa maana ya Halmashauri iliyopo sasa ilipendekeza tuwe na Halmashauri ya Jiji la Mwanza, tuwe na Manispaa ya Ilemela. Wakapeleka katika vikao vya *RCC,* Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mwanza ikakubali na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa akatoa *Government Notice* nia ya kuanzisha mamlaka hiyo, zikatolewa siku 60 za watu kutolea maoni.

Sasa Halmashauri zingine pingamizi zilizotolewa hazikuwa na uzito sana ndiyo maana mara moja imeagizwa kwamba zitaaza. Mwanza kilichotokea ni kwamba baadhi ya viongozi ambao wenyewe wameshiriki katika kupendekeza wameandika barua wakipinga. Sasa nataka nimuahidi Mheshimiwa Maria Hewa, sisi katika Wizara nia yetu Manispaa hii ianze pamoja na zile zingine. Tulikuwa tuna ngoja tumalize shughuli hii mkishatupatia hela tutapata na nauli ya kwenda Mwanza tukamalizane na wale na ikiwezekana Halmashauri ile ianze pamoja na zile zingine ambazo tulikusudia tuanze nazo pamoja. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi niliainisha tatizo la maji katika Wilaya ya Kisarawe na nimesema kwamba maji Kisarawe ni janga kubwa hivi sasa. Wananchi wa Tarafa ya Chole, Tarafa ya Mwanalumango na Mzenga hali ni mbaya sana kiasi kwamba wanafunzi na walimu hata suala zima la taaluma linashuka, uzalishaji unashuka maana hata watu kwenye shughuli za kilimo inashindikana. Sasa bahati mbaya sijasikia kauli ya Serikali kama tunahudumia katika suala la njaa katika maeneo mengine lakini Ofisi ya Waziri Mkuu inatamka vipi katika janga la maji kwenye Wilaya ya Kisarawe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe kuwa tulishazungumza tatizo la maji Kisarawe na tulikasimu kazi hiyo Mamlaka ya Maji Dar

es Salaam iweze kufanya tathmini na kuweza kuona namna gani tunaweza tukamaliza tatizo hilo kwa hiyo suala hilo tunalishughulikia. Lakini pamoja na mipango ambayo tunayo ya kutekeleza Mradi wa *WSDP* tuna hakika kabisa katika muda si mrefu tatizo la Kisarawe litakuwa limeshughulikiwa. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali kwa kukubali sasa kulipa Wenyeviti wa Vijiji posho pamoja na kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani.

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye swali muda haupo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mafupi mawili ni kwamba wakati nachangia nilipata wasiwasi mkubwa sana juu ya Serikali juu ya kuchonga barabara mpya za vijiji kwamba fedha zinazotolewa ni kwa ajili ya ukarabati tu. Hakuna fedha inayotengwa kwa ajili ya kujenga barabara mpya wakati vijiji vingi Tanzania hii havijapata barabara mpaka sasa. Sasa ni lini Serikali itaanza kutenga fedha za kutosha katika eneo hili?

La pili na la mwisho fupi kwamba nidhamu ya matumizi ya fedha yanaanzia kwenye Bajeti na kwa utaratibu uliozuka hivi sasa Bajeti za Halmashauri zinajadiliwa na kupitishwa wakati Wabunge tukiwa hapa Bungeni na Waziri Mkuu wakati anajibu alisema kwamba atahakikisha kwamba Wabunge katika Vikao vya Halmashauri tutakuwepo.

Lakini kauli hii imeendelea kutolewa kila siku lakini Bajeti zinaendelea kujadiliwa Wabunge tuko hapa na Wabunge kutukosesha haki yetu ya msingi ya wajibu wetu wa kusimamia fedha za umma. Sasa Waziri Mkuu atoe kauli nzito ya kuhakikisha hasa katika kipindi cha Bajeti kuhakikisha kwamba Wabunge tutakuwepo kusimamia fedha hizi za umma kwa nguvu zote. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, la pili hawajibu kwa sababu ametoa kauli nzito kabisa hapa. Wewe unataka kauli ya namna gani? Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, swali la kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba nitoe maelezo kwa swali la ndugu yangu Mpina maelezo kuwa Baraza la Madiwani ndilo linalopokea fedha za kutengeneza barabara. Baraza la Madiwani ndilo linajua barabara gani imeharibika, Baraza ndilo linaamua barabara gani itengenezwe na muundo wa Baraza la Madiwani Mheshimiwa Mpina yeye ni Mjumbe kwa sababu ni Mbunge anayewakilisha Jimbo la Uchaguzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba watumie fursa hizo za vikao kuamua barabara gani zaidi wanataka wazitengeneze mwanzo kuliko zingine. Lakini pia barabara hizi zina *grade* nyingi sana, kuna barabara inamilikiwa na Serikali ya kijiji, wanapata

kijiji na kijiji wanalima wanakutana katikati. Kuna barabara zinatengenezwa na Halmashauri ya Wilaya, kuna barabara za Mkoa na kuna barabara za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zile barabara zilizopo ndani ya Wilaya Mbunge awasiliane kuhamasisha wananchi kujitolea zile za kwao wenyewe lakini pia zile ambazo wanaona zinatengenezwa na Halmashauri ashiriki kushauriana na Madiwani kuamua barabara ipi waitengeneze kwa kuipa kipaumbele. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu mimi nilishauri sana ile hospitali yetu ya Wilaya Jimbo la Solwa ambayo inajengewa pale Salamagazi na vile vile iko kwenye ahadi ya Mheshimiwa Rais nikasema kwamba hizi hospitali za Wilaya katika nchi nzima ikiwemo Jimbo la Solwa gharama zake ni kubwa mno, nikaomba Serikali ione ni namna gani iweze kutusaidia hasa wale tulionesha nia nzuri ya ujenzi wa hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nipewe majibu na Serikali na sitapendezewa kupata majibu kwamba nipate fedha kutokana na wanamuziki hawa, naomba hela ya Serikali moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nyumba zilizowekewa alama ya X ni tatizo kubwa, mimi kutoka *Old Shinyanga* - Salamagazi, Solwa mpaka Salawe na kutokea Kata ya Tinde, Itwangi kwenda mpaka Kahama ni nyumba nyingi sana zimewekewa alama ya X kwa maana ya kwamba zinatakiwa zibomolewe na wamesimamishwa kabisa ujenzi mzima kwa maana kwamba pale ulipoishia kama ni renta hauendelezi tena, suala hili limekuwa kubwa na wananchi wenye nyumba hizi wamekuwa na wasiwasi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali inipe ufafanuzi au itoe tamko sasa hivi hapa kwamba pale ambapo mradi huu utapita basi wabomolewe na walipwe fidia zao. Lakini pale ambapo mradi haupiti basi Serikali itoe tamko kwamba ama walipwe wakajenge sehemu nyingine ama waendeleze ujenzi huo ili wananchi sasa waweze kupata ahueni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi siridhishwi kabisa na bomoa bomoa, kwa sababu sera yetu ya Serikali ni kupunguza umaskini na siyo kuongeza umaskini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la bomoa bomoa limejibiwa vizuri sana kwa maandishi na Waziri Mkuu naomba mjibu swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba tatizo kubwa lililokuwa katika hospitali ile ambalo amesaidia sana katika kujengwa kwa hospitali pale ilikuwa ni mahli pa kujenga hospitali, jambo ambalo lilishakwisha, sasa hela kwamba tunaweza tukatoa zote kwa ajili ya kujenga hospitali ikakamilika yote kama anavyoshauri Mbunge, haitawezekana kwa sababu hapa tunachozungumzia ni kwamba Halmashauri yenyewe inaangalia kipaumbele, kama inafikiri kwamba hitaji muhimu sasa ni hospitali

inawekwa sasa inaingia kama Bajeti *item* na tunaingiza katika lile eneo la kujenga hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachoweza kusema hapa ni kile kidogo kinachopatikana ndicho tunachopeleka kwa sababu hospitali hizi za Wilaya *almost* ni Wilaya zote mpya hazina hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa nne tulipigwa na tetemeko kubwa ndani ya Mji wetu wa Babati tetemeko ambalo liliharibu shule ya msingi Maisaka, shule ya msingi Oysterbay na shule ya sekondari ya Babati. Tumekaa tukaomba msaada ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu tukaleta makisio ya shilingi milioni 180, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wengine wanasoma nje na wengine wapo zaidi ya mia moja ndani ya darasa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huo msaada tuliioomba kama sehemu zingine zinazopata maafa watatusaidia lini kusudi tuweze kusimamisha hayo madarasa na wanafunzi waweze kuendelea na masomo ikizingatiwa kuwa hizo shule tumezijenga sisi wananchi na tuna mzigo bado wa kuendeleza shule zetu za Kata. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maombi ambayo tulipata kutoka Manyara mwezi wa sita ni ugonjwa wa tauni, waliomba shilingi milioni 62 tukawapa, na tulipata sehemu zingine, lakini nataka kumuomba tu Mheshimiwa Mbunge labda tutawasiliana na Mkuu wa Mkoa yupo hapa tupate haya maombi halafu tutaangalia uwezo wetu na namna ya kuyashughulikia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, mpeleke maombi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilisema kwamba idadi ya watu imeongezeka na ardhi haitoshi na vijiji vingi vimepakana na hifadhi. Hiki kilio ni cha nchi nzima, katika Wilaya za Kibondo na Kasulu wananchi wanaopakana na mipaka wanapata shida sana, hivi ninavyoongea wananchi wanafukuzwa mashambani wasilime, nilikuwa naomba nipewe ufafanuzi ni lini sheria italetwa haraka Bungeni ili mipaka iweze kusogezwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo analolisema Mbunge, ninavyofahamu mimi ni kwamba Mkuu wa Wilaya alikwenda katika lile eneo, kama sikosei ni eneo analolizungumzia na wana mawazo haya ya kusema kwamba tuone namna ya kuweza kupanua eneo lile. Kazi inayofanyika sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunawaondoa wale wananchi na wana vyakula, wamelima na Mkuu wa Wilaya anayekaimu pale ametoa agizo la kuwataka wavune wakimaliza wasiendelee tena pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la kwamba tunaweza kutamka hapa kwamba wanaruhusiwa ni jambo ambalo ni lazima tukae wote Maliasili na wale wadau wote wanaohusika ili tuweze kulifanyia maamuzi.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi niliainisha taabu ambayo ipo kwa wananchi hususani katika Jimbo la Kalambo ambalo katika operesheni ya vijiji miaka ya 1970 walipisha na wakaacha ardhi yao kusogea kwenye vijiji na kwa nia njema kwa Serikali walikuja kutwaa eneo hilo kwa ajili ya kuanzisha Ranchi ya Taifa ya Kalambo, sasa hivi Serikali imeamua kubinafsisha bila kuwahusisha wananchi wale na bahati nzuri wakati Ranchi ikiwa chini ya Serikali walikuwa wanaruhusiwa kulima, sasa hivi hawana eneo la kulima na wao wako tayari kufuata masharti yote ili ikiwezekana waweze kubinafsishiwa, walime wao badala ya mtu mwingine.

Je, Serikali ina kauli gani ili kuwahakikishia wananchi wa Kalambo pamoja na Nkansi wanapata eneo lililokuwa chini ya Ranchi ili waweze kulima kwa mwaka huu na kwa sababu tunaanza kulima kuanzia kiangazi?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mheshimiwa Kandege tulishaongea, tunamtafutia majibu ili kuangalia njia ya kuwasaidia wakulima hao kwa sababu wanazunguka Ranchi yetu ya Kalambo.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Njaa ni maafa, mafuriko ni maafa, mabomu ni maafa, kigezo kimoja tu cha kushughulikia maafa ni hatua za dharura, sasa kama mpaka leo mwenzangu wa Tanga wanasema kwamba Serikali itaenda ifanye tathmini huko ni kupoteza kigezo cha udharura, lakini Mwibara niliwalilia hapa kwamba kuna njaa kubwa sana na tayari sisi tulishawekwa kwenye kundi la njaa tukapewa chakula kwa mara ya kwanza, kwa hiyo sisi tulishafanyiwa tathmini tunachohitaji ni Serikali itoe kauli ni lini chakula hiki kitaenda maeneo ya Mwibara na Bunda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilizungumza hapa kwamba wakulima wananyonywa na mizani ambayo ni batili na haramu kwa sababu Bunge la Tisa liliharamisha mizani ya rula. Nataka kusikia kauli ya Serikali wakulima hawa mpaka sasa mazao yao yananunuliwa kwa mizani haramu. Ni lini kauli hii itatolewa hapa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekaa na wadau wa pamba Mwanza kujadiliana juu ya utaratibu mpya wa mizani ambayo inaweza ikatumika na mchakato wa kuwafundisha na kuwaandaa wananchi kwa ajili ya utayari wa matumizi hayo na tunategemea katika msimu huu unaoanza mizani hiyo mipya ambayo haitawahadaa wakulima itaanza kutumika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba tu Mbunge tuwasiliane zaidi na uongozi wa Mkoa wako hapa kama wanaweza kutusaidia kufanya tathmini ya haraka haraka maana yake hatuwezi tutatumia takwimu zile ambazo tulimpelekea chakula mara ya mwisho, kila mara hali inabadilika. Kwa hiyo, tutaendelea kuwasiliana kwa haraka sana kwa sababu uongozi wote upo na watendaji wote wapo. Tutapata taarifa kabla ya Bunge hili halijaisha tutakuwa tumetekeleza. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kupewa ufafanuzi ni kwa nini Mkoa wa Pwani hatukupangiwa pesa za MMAM kwa ajili ya ujenzi wa vtuo vya afya, zahanati, ukilinganisha na mikoa mingine, kwa mfano, Dodoma wamepangiwa shilingi milioni 964, Iringa shilingi milioni 965 na Mikoa mingine na kadhalika.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mbunge kwamba kwenye Bajeti yetu tumeweka pesa za MMAM nafikiri labda hujaiangalia vizuri lakini bado kuna nafasi tarehe 13 na 14 Julai, 2011 tutajadili zaidi kuhusu Bajeti yetu ya Wizara ya Afya na namna gani tumeelekeza mpango wa MMAM kwenye Mkoa wenu husika.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia Bajeti ya Waziri Mkuu nilielezea tatizo sugu la barabara ya Kalamazite - Ilemba na jinsi ambavyo Halmashauri haina uwezo wa kuitengeneza maana inahitaji fedha zaidi ya shilingi bilioni moja. Kwa bahati nzuri mwaka 2008, Waziri Mkuu wakati anaenda kukagua *scheme* ya Sakalilo alilazimika kuzunguka kilomita 150 badala ya barabara ya kilomita 24. Baada ya kuhutubia wananchi walimuomba apitie barabara ile maana ndiyo nao wanaipita, alilazimika kupitia ile barabara akaona uchungu wa ile barabara akaagiza Halmashauri ifanye mchanganuo na kuleta maombi maalum kwa TAMISEMI. Halmashauri ilifanya hivyo na mimi nimefuatilia mwenyewe nikaleta tena kumbukumbu nyingine kukumbushia na bado katika mazungumzo yangu nimeeleza tatizo la barabara hiyo lakini sijapata majibu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali inifafanulie kwamba wananchi waendelee kuteseka kufa mlimani kwa sababu ya jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hili suala nafikiri alishalileta hata katika kipindi cha maswali, tulimhakikishia kwamba barabara tatu alizozisema mbili tulishapokea maombi hayo kutoka kwenye bodi ya barabara ya Mkoa na imefika Wizara ya Ujenzi na sasa unafuata mchakato tu kumpelekea Waziri wa Ujenzi ashauriwe namna ya kuzipandisha daraja hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna barabara moja nafikiri ndiyo barabara ya Ilemba ambayo nilimwambia kwamba tufuate utaratibu kama inahitajika pia iwe moja ya barabara za Mkoa basi ipitie bodi ya barabara na Wizara ya U jenzi tutafikishiwa ili tufuate mchakato huo huo kuweza kuipitisha kuwa barabara ya Mkoa.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kusitisha zoezi hilo mpaka hapo tathmini itakapofanyika tena upya, maeneo ya Mlonga, Siriamboga, Magigiwe, Ivaranji, Igava, Igunda, Ikanutwa na Magwarisi…

**MWENYEKITI:** Naomba uende kwenye swali lako.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mwanawala, Mwanyungu, Mnazi na maeneo mengine…*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naomba uende kwenye swali Mheshimiwa tunapoteza muda.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa hata hivyo ndiyo hoja yenyewe, Iyala, Msanga na Madundasi ni maeneo ambayo vilevile yalikuwa yanaathirika na mgogoro huu wa mpaka, naomba Waziri itakapokuja hiyo tathmini basi ifike na maeneo hayo.

Katika swali langu la msingi nilimuomba Waziri wa Maliasili aweze kufika eneo ambalo lina mgogoro na Serikali ambayo ni kesi ili kusudi tukafanye mazungumzo ya nje ya Mahakama kwa vijiji vya Igawa, Igunda, Vikae na Ivaranje lakini mpaka sasa halijafanyika je, ni lini Waziri atafika kufanya hiyo shughuli kama alivyoahidi ndani ya Bunge hili Tukufu?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutamshauri Waziri wa Maliasili aende huko. *(Makofi)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika mchango wangu wa maandishi niliainisha tatizo la maji linalowapata wananchi wa Namanyere kwamba lingeweza kusuluhishwa vizuri na chanzo cha maji kutoka Milima ya Katezuma ambacho andiko lake limeshaandikwa vizuri na kuletwa Wizara inayohusika na kwamba katika kipindi cha kampeni Rais aliweza kutoa maagizo kwamba suala la maji Namanyere ni tatizo kubwa kwa sababu wananchi wa Namanyere wanapata kiasi cha asilimia 16 ya mahitaji yanayohitajika, mradi huu ungeweza kuwa ni suluhisho zuri kwa sababu utahusisha pia kuvipa vijiji zaidi ya kumi mpaka kufikisha Mjini Namanyere, je, katika maongezi yote haya na ufafanuzi uliotolewa na Wizara sijaona jambo hili likizungumziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suluhisho katika suala hili muhimu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Bajeti yetu ya Wizara ambayo tutaiwasilisha tarehe 11 na 12 suala hilo tutalizingatia.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika *guillotine*, nasikitika suala la mikoa tutapiga mmoja tu, Maendeleo hivyo hivyo pia. Tunaendelea.

**FUNGU 37 - OFISI YA WAZIRI MKUU**

Kifungu 1001 *Administration and General ……….*Shs.3,890,971,700
Kifungu 1002 *Finance and Accounts…………………*Shs.862,364,000

Kifungu 1003 *Policy and Planning…........…………….*Shs.2,971,006,300
Kifungu 1004 *Internal Audit Unit……………………….*Shs.258067,500
Kifungu 1005 *Information, Education and Comm…*Shs.230,218,200
Kifungu 1006 *Procurement Management Unit……*Shs.255,350,700
Kifungu 1007 *Legal Services Unit……….......……….*Shs.128,286,800
Kifungu 1008 *Mgt. Information Sytem Unit* .........Shs.8,725,484,900
Kifungu 2001 *Civl Affairs and Contingencies…*.......Shs.8,862,517,500
Kifungu 2002 *National Festivals…....…………….*Shs.9,665,999,000
Kifungu 3001 *Parliamentary and Political Affairs……*Shs. 683,446,700
Kifungu 4001 *Investment and Private Sector Dev.*Shs.7,391,243,200
Kifungu 5001 *Coordination of Gvt. Business.*............Shs.879,947,200
Kifungu 7001 *Government Printer…...…………….*Shs. 28,094,505,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 42 - MFUKO WA BUNGE**

Kifungu 1001 *Admnistration and General.*...........Shs.14,052,900,000
Kifungu 2001 *National Assembly…………………*Shs.77,798,694,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 56 - OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI**

Kifungu1001 *Administartion and General………….*Shs.8,453,143,813
Kifungu 1002 *Finance and Accounts………………*Shs. 547,113,978
Kifungu 1003 *Policy and Planning…………………*Shs.2,135,195,707
Kifungu 1004 *Mngt. Information Systems Division....*Shs.366,911,956
Kifungu 1005 *Legal Service Division……..…………*Shs. 397,967,607
Kifungu 1006 *Internal Audit Unit……...……………*Shs.312,799,442
Kifungu 1007 *Information, Edu. and Comm. Unit…*Shs.407,441,144
Kifungu 1008 *Procurement Mgt. Unit…*...........Shs.12,979,725,727
Kifungu 2001 *Regional Admnistration Division……*Shs. 2,151,218,490
Kifungu 2002 *Local Govt. Coordination Division…*Shs.14,906,178,596
Kifungu 2003 *Sector Coordination Division………*Shs.20,191,220,634
Kifungu 3001 *Organisation Dev. Division.*..........Shs.42,735,411,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 61 - TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

Kifungu 1001 *Administration and General…....…*Shs.1,771,283,000

Kifungu 1002 *Planning Monitoring and Ev. Division…*Shs.393,140,000
Kifungu 1003 *Finance and Accounts Unit…………*Shs.230,214,000
Kifungu 1004 *Internal Audit Unit……...................…*Shs.178,318,000
Kifungu 1005 *Legal Service Unit……..............………*Shs.493,327,000
Kifungu 1006 *Procurement Mgt. and Logistics Unit..*Shs.3,235,501,000
Kifungu 2001 *Election Management Division…………*Shs.218,233,000
Kifungu 2002 *Permanent National Voters Reg.*
*Syt. Div* ........................................................Shs.459,956,000
Kifungu 2003 *Voters Edu. and*
*Public Information Division.........................…*Shs.4,102,421,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 91 - TUME YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

Kifungu 1001 *Admnistration and General…………*Shs.1,294,358,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 92 - TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA**

Kifungu 1001 *Policy Planning and*
*National Response*…................................Shs. 188,261,000
Kifungu 1002 *Finance, Admin. and Resources*
*Mobilazation……......................................*Shs.2,521,705,000
Kifungu 1003 *Monitoring, Evaluation, Research and MIS………*Shs. 0
Kifungu 1004 *Advocacy, Information, Edu. and Comm*……......Shs. 0
Kifungu 1005 *District and Community Response.……..............*Shs. 0
Kifungu 1006 *Procurement Management Unit……….* Shs.54,000,000
Kifungu 1007 *Legal Unit.…………………........................*Shs.173,900,000
Kifungu 1009 *Internal Audit Unit.………..........................*Shs.50,000,000
Kifungu 1010 *Special Programs*……………..................Shs. 35,000,000
Kifungu 1011 *Information, Edu. and Comm. Unit.....*Shs. 3,082,866,000

**MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MIKOA**

**FUNGU 70 - ARUSHA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……...Shs.1,579,769,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts*……………...... Shs.195,476,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.…………………* ..........Shs.39,774,000

Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*…….. Shs.65,440,000
Kifungu 1005 *DAS-Arusha*……………………… .............Shs.224,213,000
Kifungu 1006 *DAS Ngorongoro*…………….. ……....... Shs.236,048,000
Kifungu 1007 *DAS Karatu*…………….………… ........Shs.133,529,000
Kifungu 1008 *DAS-Arumeru*……………..……….. ........Shs.291,058,000
Kifungu 1009 *DAS-Monduli* …………….…………. ..........Shs.199,993,000
Kifungu 1010 *DAS-Longido*…………..………….. ......Shs.3,198,872,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….……......Shs.228,864,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*……..Shs.167,269,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector Unit*….……….......Shs.190,324,000
Kifungu 2004 *Social Sector*…………………………..........Shs.260,973,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Service*……..............Shs.1,037,586,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*…….. ……………...Shs.3,643,341,000
Kifungu 8091 *Local Government*…………………......Shs. 109,290,195

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 71 - PWANI**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management.…*.........Shs.878,548,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts*……………….........Shs.176,046,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*……………………..........Shs.36,778,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.83,029,000
Kifungu 1005 *DAS-Kibaha* …………..................................Shs.225,557,000
Kifungu 1006 *DAS Mafia* ……..........................................Shs.212,345,000
Kifungu 1007 *DAS Kisarawe* …………..........................Shs.212,360,000
Kifungu 1008 *DAS-Bagamoyo*……….............................Shs.241,567,000
Kifungu 1009 *DAS-Rufiji.…….*..........................................Shs.249,173,000
Kifungu 1010 *DAS-Mkuranga*………..............................Shs.233,140,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….............Shs.267,857,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.198,167,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector Unit*……….............Shs.203,885,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………........................Shs.208,673,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Service*……..Shs.132,469,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...............................Shs.273,794,000
Kifungu 8091 *Local Government*…….....................Shs. 78,614,297,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 72 - DODOMA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……....Shs.1,012,271,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts*……………….......Shs.104,318,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………….............Shs.21,262,000

Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……...Shs.20,264,000
Kifungu 1005 *DAS-Kondoa* ……….............................Shs.228,419,000
Kifungu 1006 *DAS -Mpwapwa* ……..............................Shs.206,345,000
Kifungu 1007 *DAS -Kongwa* …………….........................Shs.162,827,000
Kifungu 1008 *DAS-Bahi*………..........................................Shs.204,415,000
Kifungu 1009 *DAS-Chamwino*……….............................Shs.198,767,000
Kifungu 1010 *DAS-Dodoma*…………...............................Shs.187,794,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…… ..............Shs.166,078,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…. Shs.147,758,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……….....................Shs.84,211,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………......................Shs.412,917,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Management Service*……....Shs.38,207,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.3,371,124,000
Kifungu 8091 *Local Government*………...................Shs. 97,646,795,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 73 - IRINGA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …….........Shs.698,390,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts*.……………..........Shs.105,181,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*…………………..........Shs.34,696,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.31,377,000
Kifungu 1005 *DAS-Iringa* ……….................................Shs.301,216,000
Kifungu 1006 *DAS -Njombe* ……....................................Shs.306,623,000
Kifungu 1007 *DAS -Mufindi* ……………........................Shs.247,545,000
Kifungu 1008 *DAS-Ludewa*.……….....................................Shs.316,072,000
Kifungu 1009 *DAS-Makete*.……….................................Shs.289,843,000
Kifungu 1010 *DAS-Kilolo*…………....................................Shs.268,225,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……..............Shs.278,681,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…. Shs.228,692,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ………. .................Shs.202,763,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………. .....................Shs.476,017,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*……................Shs.134,738,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……............................Shs.3,786,516,000
Kifungu 8091 *Local Government*……..................Shs. 122,660,608,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 74 - KIGOMA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …..........Shs.973,865,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Units*……………...Shs.98,000,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*…………………..........Shs.19,189,000

Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.46,000,000
Kifungu 1005 *DAS-Kigoma* ………..........................Shs.239,590,000
Kifungu 1006 *DAS -Kasulu*……......................................Shs.241,426,000
Kifungu 1007 *DAS -Kibondo* ………….......................Shs.212,934,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….............Shs.261,756,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…....Shs.231,594,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………...................Shs.221,711,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………....................Shs.334,515,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*……................Shs.106,705,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……..............................Shs.1,722,256,000
Kifungu 8091 *Local Government*…….....................Shs. 67,594,477,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 75 - KILIMANJARO**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……..........Shs.722,810,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.134,690,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*……………….............Shs.18,165,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……...Shs.81,861,000
Kifungu 1005 *DAS-Moshi* ………….................................Shs.136,465,000
Kifungu 1006 *DAS -Hai* ……..............................................Shs.190,749,000
Kifungu 1007 *DAS -Rombo* ………….............................Shs.182,084,000
Kifungu 1008 *DAS-Same*……….......................................Shs.214,485,000
Kifungu 1009 *DAS-Mwanga*……….................................Shs.171,875,000
Kifungu 1010 *DAS-Siha*………........................................Shs.119,194,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination.*…..............Shs.347,087,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.464,132,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………..................Shs.217,508,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………....................Shs.386,111,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*……...................Shs.125,518,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*.…..............................Shs.4,198,991,000
Kifungu 8091 *Local Government*……......................Shs. 130,310,969,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 76 - LINDI**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …............Shs.998,402,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………....Shs.70,995,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………..........Shs.38,481,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.51,247,000
Kifungu 1005 *DAS-Lindi* ………..................................Shs.260,107,000
Kifungu 1006 *DAS -Kilwa*.….........................................Shs.221,234,000

Kifungu 1007 *DAS -Liwale*……………..........................Shs.202,487,000
Kifungu 1008 *DAS-Nachingwea*……….........................Shs.222,214,000
Kifungu 1009 *DAS-Ruangwa*………...............................Shs.195,164,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination.*…….................Shs.220,167,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.191,491,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……….....................Shs.161,289,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………….........................Shs.339,874,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*…….................Shs.138,517,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital.*…...............................Shs.1,866,175,000
Kifungu 3002 *Prentive Srvices.*………...............................................Shs.0
Kifungu 8091 *Local Government*……........................Shs. 50,876,012,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 77 – MARA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ….........Shs.2,099,432,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………..Shs.208,368,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.*……………………............Shs.46,275,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……...Shs.72,832,000
Kifungu 1005 *DAS-Musoma* ……….............................Shs.229,154,000
Kifungu 1006 *DAS -Bunda*……...........................................Shs.203,721,000
Kifungu 1007 *DAS -Serengeti*…………..........................Shs.222,335,000
Kifungu 1008 *DAS-Tarime.*……........................................Shs.229,759,000
Kifungu 1009 *DAS-Rorya*……….......................................Shs.263,193,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……................Shs.299,104,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.206,167,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……......................Shs.176,339,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………........................Shs.316,645,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*…….................Shs.108,841,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.1,350,070,000
Kifungu 8091 *Local Government*……........................Shs. 90,757,295,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 78 - MBEYA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……...Shs.1,049,912,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………..Shs.99,504,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*…………………...........Shs.38,003,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……......Shs.31,148,000
Kifungu 1005 *DAS-Mbeya*………….................................Shs.234,592,000
Kifungu 1006 *DAS -Ileje*……...........................................Shs.212,367,000
Kifungu 1007 *DAS -Kyela*……………..............................Shs.193,570,000

Kifungu 1008 *DAS-Chunya*………......................................Shs.238,764,000
Kifungu 1009 *DAS-Mbozi*………..........................................Shs.228,151,000
Kifungu 1010 *DAS-Rungwe*……….....................................Shs.197,805,000
Kifungu1011 *DAS-Mbarali.………*…................................Shs.209,506,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……...............Shs.171,901,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…......Shs.211,797,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ………....................Shs.126,255,000
Kifungu 2004 *Social Sector.………………*.........................Shs.385,387,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……...Shs.76,660,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital.…..*..........................Shs.1,341,211,000
Kifungu 8091 *Local Government*……....................Shs. 158,424,884,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 79 - MOROGORO**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……........Shs.846,215,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.134,401,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*……………….............Shs.40,679,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.47,010,000
Kifungu 1005 *DAS-Morogoro*………..............................Shs.270,498,000
Kifungu 1006 *DAS -Kilosa*……............................................Shs.372,800,000
Kifungu 1007 *DAS -Kilombero.……………*.......................Shs.247,646,000
Kifungu 1008 *DAS-Ulanga*……….......................................Shs.276,890,000
Kifungu 1009 *DAS-Mvomero*……….................................Shs.237,225,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……................Shs.214,399,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.207,592,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……........................Shs.166,133,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………..........................Shs.348,055,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……...Shs.86,260,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……............................Shs.4,319,227,000
Kifungu 8091 *Local Government*……..................Shs. 119,537,916,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 80 - MTWARA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …........Shs.1,396,527,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.68,519,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*……………….............Shs.20,520,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit.……*....Shs.33,995,000
Kifungu 1005 *DAS-Mtwara*……….................................Shs.118,342,000
Kifungu 1006 *DAS -Newala*……........................................Shs.141,865,000

Kifungu 1007 *DAS -Masasi*……………...........................Shs.191,453,000
Kifungu 1008 *DAS-Tandahimba*……….........................Shs.161,739,000
Kifungu 1009 *DAS-Nanyumbu*………............................Shs.154,509,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……..................Shs.189,362,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.193,450,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ……….....................Shs.212,268,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………........................Shs.299,335,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……...Shs.82,825,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.2,068,304,000
Kifungu 3002. *Preventive Services*……...........................Shs.15,238,000
Kifungu 8091 *Local Government*…….......................Shs. 72,919,031,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 81 - MWANZA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …........Shs.1,195,564,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.123,370,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………….........Shs.53,421,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.61,988,000
Kifungu 1005 *DAS-Nyamagana*……….....................Shs.168,494,000
Kifungu 1006 *DAS -Sengerema*……...............................Shs.250,225,000
Kifungu 1007 *DAS -Geita*……………..............................Shs.258,366,000
Kifungu 1008 *DAS-Kwimba*……….................................Shs.239,882,000
Kifungu 1009 *DAS-Magu*……….........................................Shs.263,654,000
Kifungu1010 *DAS-Misungwi*………..................................Shs.237,359,000
Kifungu 1011 *DAS-Ilemela*…………...............................Shs.189,418,000
Kifungu 1012 *DAS-Ukerewe*……….................................Shs.242,148,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….............Shs.254,643,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…..Shs.168,530,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ….….....................Shs.169,881,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………….......................Shs.437,762,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Mgt. Services*……..................Shs.115,011,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.2,906,397,000
Kifungu 8091 *Local Government*……..................Shs. 168,318,202,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 82 - RUVUMA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …............Shs.912,118,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.116,484,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………….........Shs.51,576,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.265,929,000

Kifungu 1005 *DAS-Songea*………..............................Shs.265,929,000
Kifungu 1006 *DAS -Tunduru*……......................................Shs.297,803,000
Kifungu 1007 *DAS -Mbinga*……………............................Shs.290,587,000
Kifungu 1008 *DAS-Namtumbo*…….............................Shs.182,836,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….............Shs.185,246,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…. ...Shs.173,291,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………..................Shs.163,025,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………......................Shs.337,886,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……..Shs.81,987,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...............................Shs.3,617,579,000
Kifungu 8091 *Local Government*……......................Shs. 76,571,809,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 83 - SHINYANGA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……....Shs.1,372,014,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.147,886,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*……………….............Shs.34,094,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.48,369,000
Kifungu 1005 *DAS-Shinyanga*……….........................Shs.234,572,000
Kifungu 1006 *DAS -Maswa*……........................................Shs.227,240,000
Kifungu 1007 *DAS -Bariadi*……………...........................Shs.227,019,000
Kifungu 1008 *DAS-Kahama*……….................................Shs.239,434,000
Kifungu 1009 *DAS-Meatu*.………........................................Shs.332,700,000
Kifungu1010 *DAS-Bukombe*………................................Shs.188,491,000
Kifungu 1011 *DAS-Kishapu*…………...................................Shs.193,186,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……...............Shs.134,116,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…. Shs.180,407,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……......................Shs.140,226,000
Kifungu 2004 *Social Sector*…………….......................Shs.339,811,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Mgt. Services*……................Shs.113,291,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*…….................................Shs.907,851,000
Kifungu 8091 *Local Government*……......................Shs. 134,653,422,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 84 - SINGIDA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* …….Shs.1,275,397,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.51,715,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.*………………….............Shs.29357,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.45,923,000
Kifungu 1005 *DAS-Singida*…………..................................Shs.170,201,000

Kifungu 1006 *DAS -Manyoni*……......................................Shs.140,384,000
Kifungu 1007 *DAS -Iramba*…………..............................Shs.141,384,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….................Shs.227,912,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…......Shs.182,773,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………..................Shs.176,014,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………..........................Shs.335,314,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……...Shs.57,634,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.2,340,612,000
Kifungu 3002 *Preventive Services*……..........................Shs.32,937,000
Kifungu 8091 *Local Government*……....................Shs. 58,635,454,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 85 - TABORA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……..........Shs.813,373,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………. ...Shs.88,488,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.………………..*..........Shs.57,263,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……...Shs.63,449,000
Kifungu 1005 *DAS-Tabora*…………................................Shs.237,749,000
Kifungu 1006 *DAS -Nzega*……..........................................Shs.257,007,000
Kifungu 1007 *DAS -Sinkonge*…………..........................Shs.211,741,000
Kifungu1008 *DAS-Igunga*………......................................Shs.269,001,000
Kifungu 1009 *DAS-Urambo*…….......................................Shs.268,165,000
Kifungu 1010 *DAS-Uyui*………..........................................Shs.240,488,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…….................Shs.183,682,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…....Shs.141,855,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………..................Shs.129,400,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………........................Shs.272,359,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……. .Shs.92,239,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……...........................Shs.2,346,551,000
Kifungu 8091 *Local Government*……........................Shs. 85,807,150,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 86 - TANGA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……....Shs.1,727,278,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………..Shs.44,308,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.*……………….............Shs.34,139,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.39,089,000
Kifungu 1005 *DAS-Tanga*………......................................Shs.68,469,000
Kifungu 1006 *DAS -Kilindi*……............................................Shs.102,039,000
Kifungu 1007 *DAS -Korogwe*…………….............................Shs.93,935,000

Kifungu 1008 *DAS-Lushoto*………....................................Shs.100,642,000
Kifungu 1009 *DAS-Mkinga*………....................................Shs.86,990,000
Kifungu 1010 *DAS-Muheza*…………..................................Shs.81,313,000
Kifungu 1011 *DAS-Pangani*……………..............................Shs.72,581,000
Kifungu 1012 *DAS-Handeni*……………..............................Shs.91,489,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……............Shs.133,292,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…......Shs.198,160,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ……….....................Shs.186,517,000
Kifungu 2004 *Social Sector*…………………......................Shs.400,951,000
Kifungu 2005 *Local Govt.Management Services*……..Shs.72,335,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……............................Shs.3,642,926,000
Kifungu 8091 *Local Government*……......................Shs. 123,812,552,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 87 - KAGERA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……......Shs.1,001,773,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit.*……………...Shs.124,648,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………….........Shs.38,815,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.71,129,000
Kifungu 1005 *DAS-Bukoba*…………...............................Shs.244,624,000
Kifungu 1006 *DAS -Biharamulo*……..............................Shs.211,360,000
Kifungu 1007 *DAS -Chato*……………..............................Shs.196,437,000
Kifungu 1008 *DAS-Karagwe.*………...............................Shs.228,991,000
Kifungu 1009 *DAS-Misenyi*………....................................Shs.193,701,000
Kifungu 1010 *DAS-Muleba*…………...............................Shs.213,264,000
Kifungu 1011 *DAS-Ngara*……………..............................Shs.206,189,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination.*…...............Shs.199,435,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…...Shs.178,077,000
Kifungu 2003 *Infrastructure  Sector* ………..................Shs.186,395,000
Kifungu 2004 *Social Sector*……………….......................Shs.277,921,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Mgt. Services*……..............Shs.146,029,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……..............................Shs.2,178,390,000
Kifungu 3002 *Preventive Services*……..........................Shs. 38,585,000
Kifungu 8091 *Local Government*……...................Shs. 110,815,435,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 88 - DAR ES SALAAM**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……......Shs.1,222,565,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………...Shs.54,278,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit.*…………………..........Shs.26,879,000

Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.40,917,000
Kifungu 1005 *DAS- Ilala*…………........................................Shs.219,107,000
Kifungu 1006 *DAS - Kinondoni*…….................................Shs.234,157,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……............Shs.170,822,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*…......Shs.161,801,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ………..................Shs.175,579,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………......................Shs.404,651,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Management Services*……..Shs.72,166,000
Kifungu 8091 *Local Government.*…….................Shs. 210,823,971,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 89 - RUKWA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Management* ……....Shs.1,017,414,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………....Shs.185,946,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*………………...........Shs.55,809,000
Kifungu 1004 *Procurement Management Unit*……....Shs.52,746,000
Kifungu 1005 *DAS-Sumbawanga*……………………........Shs.370,978,000
Kifungu 1006 *DAS -Nkasi*……………………….............Shs.304,220,000
Kifungu 1007 *DAS -Mpanda*………………………..........Shs.363,154,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*…………......Shs.184,559,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*……..Shs.274,367,000
Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* …………………....Shs.157,920,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………. ………….....Shs.376,473,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Mgt. Services*……..............Shs.141,960,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*…………………….....Shs.2,264,097,000
Kifungu 8091 *Local Government*…….………………Shs. 2,264,097,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 95 - MANYARA**

Kifungu 1001 *Admn. and HR Mgt.*………….............Shs.956,528,000
Kifungu 1002 *Finance and Accounts Unit*……………Shs.201,278,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*…………………........Shs.32,590,000
Kifungu 1004 *Procurement Mgt. Unit.*………...............Shs.51,879,000
Kifungu 1005 *DAS- Babati* ……………………………......Shs.213,198,000
Kifungu 1006 *DAS - Hanang*…………………… ……....Shs.219,734,000
Kifungu 1007 *DAS - Kiteto*…………… ………….........Shs.259,303,000
Kifungu 1008 *DAS - Mbulu*…….........……………………Shs.227,781,000
Kifungu 1006 *DAS - Simanjiro*……………………….......Shs.250,246,000
Kifungu 2001 *Planning and Coordination*……………....Shs.217,997,000
Kifungu 2002 *Economic and Productive Sector*……..Shs.205,668,000

Kifungu 2003 *Infrastructure Sector* ……………….........Shs.142,776,000
Kifungu 2004 *Social Sector*………………………….......Shs.358,079,000
Kifungu 2005 *Local Govt. Mgt. Services*……...............Shs.123,192,000
Kifungu 3001 *Regional Hospital*……..………………........Shs.360,258,000
Kifungu 8091 *Local Government*………………….. Shs. 70,576,916,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 27 - MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*……………....Shs.69,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 37 - OFISI YA WAZIRI MKUU**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*…………Shs.4,000,000,000
Kifungu 1003 *Policy and Planning*………………........Shs.14,035,189,340
Kifungu 1005 *Information, Educ and Comm.*……………............Shs.0
Kifungu 1008 *Mgt. and Information System Unit*……….............Shs. 0
Kifungu 2001 *Civil Affairs and Contingencies*…………Shs.729,135,000
Kifungu 2002 *National Festival*……………….................Shs.100,000,000
Kifungu 3001 *Parliamentary and Political Affairs*……….......…Shs.0
Kifungu 4001 *Investment and*
*Private Sector Dev.*…..............................................Shs.58,995,363,060
Kifungu 5001 *Coordination of Gvt. Business*…….Shs.30,663,655,600
Kifungu 7001 *Government Printer*…………….........Shs. 881,133,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 42 - MFUKO WA BUNGE**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*……………..................Shs.0
Kifungu 2001 *National Assembly*…………….........Shs. 3,000,000,000

*((Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 56 - OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*…………Shs.1,000,000,000
Kifungu 1003 *Policy and Planning*……..........………Shs.2,500,000,000
Kifungu 1004 *Mgt. Information Sytem Div.*…….......Shs.460,000,000
Kifungu 1005 *Legal Services Division*……………............................Shs.0
Kifungu 2002 *Local Gvt. Coordination Div.*……...Shs.20,620,255,600
Kifungu 2003 *Sector Coordination Div.*……………Shs.43,280,516,400
Kifungu 3001 *Organisation Dev. Division*…..............Shs.1,331,981,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 91 - TUME YA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA**

Kifungu 1001 *Admnistration and General*…………Shs.1,309,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 92 - TUME YA KUDHIBITI UKIMWI**

Kifungu 1001 *Policy, Planning and National Response.*…...................Shs.1,764,388,508
Kifungu 1002 *Finance, Admn. and Resource Mobilization*…......……Shs.6,119,892,573
Kifungu 1003 *Monitoring, Evaluation, Research and MIS*……..........................….Shs.1,978,889,216
Kifungu 1004 *Advocacy, Information, Education and Comm*...........…………Shs.2,289,300,000
Kifungu 1005 *District and Community Response*……......…Shs.4,092,135,369
Kifungu 1006 *Procurement Mgt. Unit*……………….….Shs.185,250,000
Kifungu 1007 *Legal Unit*……………………………………Shs.482,200,000
Kifungu 1008 *Mgt. Information Systems*…...........….Shs.1,276,515,000
Kifungu 1009 *Internal Audit Unit*………....……………..Shs.576,578,000
Kifungu 1010 *Special Programs*…………………………Shs.419,897,000
Kifungu 1011 *Information, Edu. and Comm. Unit*….Shs.1,408,438,334

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 70 – MKOA WA ARUSHA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt*.................Shs. 783,584,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………….. Shs 20,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*….. Shs. 46,175,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* …………..............Shs. 63,590,000
Kifungu 2004- *Social Sector*…………..............................Shs. 30,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* …………...................Shs. 935,318,000
Kifungu 8091- *Local Government* ………............Shs. 41,287,661,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 71- MKOA WA PWANI**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*...Shs. 50,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………Shs. 66,143,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……Shs. 51,428,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*...……....………..Shs. 678,488,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………Shs. 211,363,000/=
Kifungu 8091- *Local Government*………………….Shs. 21,323,327,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 72 - MKOA WA DODOMA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt*.…………..Shs2,123,891,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……..Shs. 57,964,000
Kifungu 2004- *Social Sector*………………….............Shs. 290,238,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………......Shs. 800, 000,000
Kifungu 3002- *Preventive Services*……………………………........Shs. 0
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs. 43,573,034,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 73 - MKOA WA IRINGA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..Shs. 526,027,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………..Shs. 65,946,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* ……Shs.56,638,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………..Shs. 78,488,000
Kifungu 2004- *Social Sector* …………......……………..Shs. 227,273,000
Kifungu 2005- *Regional Hospital* ……………......……….Shs.73,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………..Shs. 34,223,049,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 74 - MKOA WA KIGOMA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ............Shs. 1,264,569,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination.*……………..Shs. 64,783,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector.*…….Shs. 6,000,000
Kifungu 2004- *Social Sector.*……………………………........Shs. 30,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ………...............………Shs.446,485,000
Kifungu 3002 *Preventive Services.*…..............……………………….Shs. 0
Kifungu 8091- *Local Government.*…………………Shs.42,068,169,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 75 - MKOA WA KILIMANJARO**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management* ..Shs.400,210,000
Kifungu 1005- *DAS-Moshi* ……………………….............Shs.5,000,000
Kifungu 1006- *DAS-Hai* ……………………….................Shs.5,000,000
Kifungu 1007- *DAS-Rombo* ……………………………....Shs.5,000,000
Kifungu 1008- *DAS-Same*……………………..................Shs.5,000,000
Kifungu 1006- *DAS-Mwanga*……………………...............Shs.5,000,000
Kifungu 1006- *DAS-Siha*…………………..........................Shs.5,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……....……Shs. 30,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….Shs. 51,852,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* ……………………..Shs. 67,783,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ……….......…………………Shs. 30,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*……………………Shs. 1,714,448,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs.27,935,581,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 76 - MKOA WA LINDI**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..Shs.145,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………Shs. 42,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……Shs. 68,864,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* …………………….Shs.536,247,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ………………………..Shs.595,455,000
Kifungu 3002- *Preventive Services*……………………….Shs. 30,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs. 19,258,884,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 77 - MKOA WA MARA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*....Shs. 20,000,000
Kifungu 1005- *DAS-Musoma*..............................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1006 – *DAS- Bunda*...............................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1007 – *DAS- Serengeti* ...........................................Shs.5,000,000
Kifungu 1008- *DAS- Tarime*...............................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1009- *DAS- Rorya*…………………….........……Shs. 5,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….Shs. 60,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* ……Shs.70,675,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*…………………..Shs. 977,493,000
Kifungu 2004- *Social Sector*……………………......……Shs. 64,683,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….Shs.346,452,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………..Shs. 33,141,750,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 78 - MKOA WA MBEYA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..Shs. 376,610,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………..Shs. 5,450,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* …….Shs. 57,731,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* …………….……..Shs.78,488,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ……………………………Shs. 257,273,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……………………….Shs. 622,454,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….Shs.51,227,039,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 79 - MKOA WA MOROGORO**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ...........Shs. 1,138,174,000
Kifungu 1005- *DAS- Morogoro* ........................................Shs. 10,000,000
Kifungu 1006- *DAS- Kilosa*....................................................Shs.5,000,000
Kifungu 1007- *DAS- Kilombero*..........................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1008- *DAS- Ulanga*................................................Shs.5,000,000
Kifungu 1009- *DAS- Mvomero*………………...…………Shs. 5,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………Shs.29,713,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….Shs. 56,019,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* …………………..Shs. 78,488,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ……….......………………Shs.195,455,000

Kifungu 3001- *Regional Hospital*………..…………….Shs.  430,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*……………….Shs.  30,056,825,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 80 - MKOA WA MTWARA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ..............…Shs. 713,450,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….Shs.  10,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*………Shs.56,372,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*…......………………Shs.64,783,000
Kifungu 2004- *Social Sector*……………..............……….Shs.30,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*………………………Shs.  695,455,000
Kifungu 8091- *Local Government*……..………….Shs. 35,272,517,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 81 - MKOA WA MWANZA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.*……………..Shs. 60,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….Shs.  39,260,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….Shs. 51,638,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*………………….Shs. 1,119,488,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ……………………………..Shs. 211,363,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*……………………….................Shs.0
Kifungu 8091- *Local Government*…………….....…Shs.62,158,933,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 82 - MKOA WA RUVUMA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ...........…Shs. 670,933,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………………….Shs.  0
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* ……Shs.  66,151,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………Shs. 20,000,000
Kifungu 2004- *Social Sector*……………....……………Shs. 274,328,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* …...………………….Shs.  230,000,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs, 25,890,529,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 83 - MKOA WA SHINYANGA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*...Shs. 55,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……..…….Shs. 36,000,000
Kifungu 2002 - *Economic and Productive Sector*……Shs. 59,687,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*…....……………..Shs. 711,446,000
Kifungu 2004- *Social Sector*………………………….Shs. 227,273,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*…………………………Shs. 68,500,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………..Shs. 48,442,990,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 84 - MKOA WA SINGIDA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* …...…….Shs.195,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………..Shs. 13,436,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……Shs. 45,834,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*…...……………….Shs. 64,783,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*…………….......….Shs.2,163,636,000
Kifungu 8091- *Local Government*………………….Shs.21,001,799,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 85 - MKOA WA TABORA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* …………Shs. 1,042,733,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………Shs. 38,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….Shs. 45,427,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………...…….Shs. 78,488,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ………….................…………………..Shs. 0
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ……...……………….Shs. 289,888,000
Kifungu 8091- *Local Government* ……….......……Shs.32,540,435,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 86 - MKOA WA TANGA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ............…Shs. 396,936,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*…………….Shs. 66,173,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*…….Shs.88,606,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ………………….......…….Shs.. 78,488,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*……………...………..Shs. 743,182,000
Kifungu 3002- *Preventive Services*…………………......…....…….Shs. 0
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs. 46,565,141,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 87 - MKOA WA KAGERA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.* ............... Shs.1,142,301,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………Shs. 30,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* …….Shs. 54,076,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*………………..….Shs. 328,488,000
Kifungu 2004 - *Social Sector* ………………….……….Shs. 227,273,000
Kifungu2005-*Local Gvt. Management Services*………Shs.6,000,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital* ....……………………Shs. 80,000,000
Kifungu 3002- *Preventive Services*……………...............……….Shs. 0
Kifungu 8091- *Local Government*……………..…..Shs. 43,785,107,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 88 - MKOA WA DAR ES SALAAM**

Kifungu 1001- *Administration and HR Mgt.*…………. Shs.455,000,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*……………..Shs. 69,626,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* …….Shs. 40,566,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* ………....…………Shs.48,693,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ………………..........……..Shs. 147,727,000
Kifungu 8091- *Local Government*……………….Shs. 29,853,992,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 89 - MKOA WA RUKWA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..Shs. 902,140,000
Kifungu 2001- *Planning and Coordination*………………Shs. 30,000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector* ……Shs. 51,317,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector*……………………Shs. 64,783,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*…………....……...…Shs. 179,545,000
Kifungu 3002- *Preventive Services*.....................…………………Shs. 0
Kifungu 8091- *Local Government*…………………..Shs.27,969,707,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 95 - MKOA WA MANYARA**

Kifungu 1001- *Administration and HR Management*..Shs. 312,791,000
Kifungu 1005- *DAS – Babati* ..............................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1006- *DAS –Hanang* ................................................Shs.5,000,000
Kifungu 1007- *DAS –Kiteto*..............................................Shs. 30,000,000
Kifungu 1008- *DAS –Mbulu*................................................Shs. 5,000,000
Kifungu 1009- *DAS –Simanjiro*..........................................Shs.20, 000,000
Kifungu 2002- *Economic and Productive Sector*……Shs. 46,813,000
Kifungu 2003- *Infrastructure Sector* ……………………Shs.   64,783,000
Kifungu 2004- *Social Sector* ………………......………Shs.  225,455,000
Kifungu 3001- *Regional Hospital*………………………Shs. 1,832,796,000
Kifungu 8091- *Local Government*…………………Shs.24, 576,243,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi baada ya kujadili Taarifa ya Mapato na Matumizi na mwelekeo wa kazi za Serikali, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko…

**SPIKA:** Siyo Kifungu ni Mafungu kwa Mafungu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mafungu kwa Mafungu…

**SPIKA:** Ndiyo. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mafungu kwa Mafungu bila mabadiliko, hivyo basi naomba sasa Bunge lako liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yalipitishw ana Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Mawaziri wake wanaomsaidia pia na Mawaziri wote waliofanya kazi, nafikiri Mawaziri wamefanya kazi, kwa sababu wameweza kujibu maswali ambayo hayakuwa katika maeneo yao. Lakini ndiyo mnatakiwa kuwa hivyo wakati wote mjue maeneo yenu vizuri. *(Makofi)*

Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa kazi tuliyoifanya, tutaangalia utaratibu mzuri zaidi wa kupitisha vifungu hivi kwa sababu kwa mtindo huu tutajikuta tunakuwa na *guillotine* kila siku na jambo hili halipendezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine maswali mengine mliyouliza hapa yalikuwepo kwenye maswali ya kawaida lakini bado watu mnaendelea kuuliza. Itabidi tukae kwa sababu naona huu utaratibu utakuwa na matatizo sana. Tutakuwa tunapitisha namna hii kila kifungu siyo vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewatangazia kwamba kesho saa moja na nusu usiku tutakuwa na tafrija itakayokuwa imeandaliwa na *Tanzania Distilleries Limited (TDL)* katika viwanja vyetu vya Bunge. Mje kuchangamka pale na bendi ya Twanga Pepeta itakuwepo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kufanya kazi kwa wiki nzima vizuri, muangalie ratiba yetu ni Wizara gani zinafuata wiki ijayo ili mjiandae. Waliozungumza kwa mara ya pili hawatapewa nafasi, ndivyo tutakavyofanya. Tunaanza na Wizara moja moja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 3.15 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 4 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*